
Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

# HISTORIA KUU YA AFRIKA •

Juzuu Lililofupishwa

# VII Afrika chini ya Utawala wa Wakoloni 1880 - 1935

MHARIRI A. ADU BOAHEN



TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

Historia Kuu ya Afrika · VII

# Afrika chini ya Utawala wa Wakoloni 1880 - 1935

MHARIRI A. ADU BOAHEN

Toleo Lililofupishwa

TUKI . CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM . UNESCO

Jina la Asili: **GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL VII**

© UNESCO 2000
ISBN 9976 911 24 6

*Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.*
*Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.*
*Toleo la Tafsiri ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.*

Historia Kuu ya Afrika · VII

# Afrika chini ya Utawala wa Wakoloni 1880 - 1935

## Toleo Lililofupishwa

UNESCO Historia Kuu ya Afrika

**Juzuu I** *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*
Mhariri **J. Ki-Zerbo**

**Juzuu II** *Staarabu za Kale za Afrika*
Mhariri **G. Mokhtar**

**Juzuu III** *Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja*
Mhariri **I. Hrbek**

**Juzuu IV** *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita*
Mhariri **J. Ki-Zerbo na D.T. Niane**

**Juzuu V** *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane*
Mhariri **B.A. Ogot**

**Juzuu VI** *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi miaka ya 1880*
Mhariri **J.F. Ade Ajayi**

**Juzuu VII** *Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935*
Mhariri **A. Adu Boahen**

## Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

**Juzuu VIII** *Afrika Kuanzia 1935*
Mhariri **A.A. Mazrui**
Mhariri Msaidizi **C. Wondji**

Toleo lililofupishwa la
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO

**Limechapishwa na:**

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110
Dar es Salaam, Tanzania

Pamoja na:
UNESCO Publishing
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris

Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.

# *YALIYOMO*


| | | |
|---|---|---|
| | *Dibaji* ................................................ | vii |
| | *Wasifu wa Mradi* ........................................ | xii |
| | *Maelezo ya Wendo* ....................................... | xv |
| | *Wanakamati* ............................................. | xvi |
| | *Wasifu wa Waandishi* .................................... | xviii |
| *1* | *Afrika na changamoto ya ukoloni* | *1* |
| 2 | *Kugawanywa na kutamalakiwa kwa Afrika* ............ | *11* |
| 3 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika dhidi ya kugawanywa na kutamalakiwa* | *28* |
| 4 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika: Kaskazini-Mashariki mwa Afrika* ............ | *38* |
| 5 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika: Afrika Kaskazini na Sahara* ............ | *54* |
| 6 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika: Afrika Magharibi 1880-1914* ............ | |
| 7 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika: Afrika Mashariki 1880 – 1914* ............ | *85* |
| 8 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika: Afrika ya Kati 1880 – 1914* ............ | *97* |
| 9 | *Juhudi na ukinzani wa Waafrika: Afrika ya Kusini* ... | *112* |
| *10* | *Malagasi kuanzia 1880 – 1936* ............ | *129* |
| *11* | *Liberia na Ethiopia 1880 – 1914* ............ | *143* |
| *12* | *Vita vya kwanza vya Dunia na matokeo yake* ............ | *158* |
| *13* | *Mbinu na taasisi ya utawala wa kizungu* ............ | *171* |
| *14* | *Uchumi wa Kikoloni* ............ | *182* |

| | | |
|---|---|---|
| 15 | *Uchumi wa Kikoloni: Kanda zilizokuwa chini ya Wafaransa, Wabelgiji na Wareno* | 192 |
| 16 | *Uchumi wa Kikoloni: Kanda zilizokuwa chini wa Waingereza* | 204 |
| 17 | *Uchumi wa Kikoloni: Afrika Kaskazini* | 219 |
| 18 | *Matokeo ya kijamii ya utawala wa kikoloni* | 236 |
| 19 | *Athari kubwa za kijamii: miundo mipya ya jamii* | 245 |
| 20 | *Dini katika Afrika enzi ya ukoloni* | 255 |
| 21 | *Sanaa katika Afrika wakati wa utawala wa kikoloni* | 268 |
| 22 | *Siasa na utaifa wa Kiafrika: 1919 – 1935* | 281 |
| 23 | *Siasa na utawala Kaskazini-Mashariki mwa Afrika 1919 - 1935* | 291 |
| 24 | *Siasa na utaifa Maghreb na Sahara, 1919 - 1935* | 304 |
| 25 | *Siasa na utaifa Afrika ya Magharibi, 1919 – 1935* | 316 |
| 26 | *Siasa na utaifa Afrika ya Mashariki, 1919 – 1935* | 327 |
| 27 | *Siasa na utaifa katika sehemu za Kati na Kusini mwa Afrika 1919 – 1935* | 339 |
| 28 | *Ethiopia na Liberia, 1914 – 1935* | 355 |
| 29 | *Afrika na Ulimwengu mpya* | 369 |
| 30 | *Ukoloni katika Afrika: Taathira na umuhimu wake* | 384 |

*Bibliografia*
*Faharasa*

# *Dibaji*

**AMADOU - MAHTAR M'BOW**
*Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)*

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayounganisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezewa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya bidhaa, imani, desturi ua mawazo baina ya

jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokeazaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika,* ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi

1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa)* kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha sehemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia;* kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihausa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kiteknolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine mufumu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika,* na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepukana na inadi katika utafiti wa masuala mufumu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha

mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini aambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii.Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayowezesha kueleweka kwa vipengele fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*[1] yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika

*Historia Kuu* inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika.* Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika

---

[1] Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu:
*Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuvuka Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukoloni Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika weusi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyama vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.*

harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

*Historia* hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa elimu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginepo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na vipengele vinavyoelezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango walioutoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.

# *Wasifu wa Mradi*

*B.A. OGOT*[1]

*Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)*

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

(a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.

(b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya sehemu zote za bara ambazo mara nyingi hutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.

(c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.

[1] Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wapya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

(d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahsusi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vote vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huthibitisha muswada wa mwisho. Inapoona kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hafanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaoonekana mrefu na mgumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika.* Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imeikataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa

asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.

Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusisitiza umuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano miongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maelewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.

# *Maelezo kuhusu Wendo*

Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na 'kabla ya enzi ya Ukristo' na '-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

(i) 2300 KS = - 350

(ii) 2900 KK = - 2900
1800 WK = + 1800

(iii) Karne ya tano KK = Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo
Karne ya tatu WK = Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.

# *Wanakamati wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika*

*Tarehe zilizotajwa zinawakilisha tarehe za wanachama.*

Profesa J.F.Ade Ajayi
(Nigeria), tangu 1971
Mhariri Juzuu VI

Prof. F.A. Albuquerque Mourão
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. Adu Boahen
(Ghana), tangu 1971
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama
(Niger), 1971-8 (alijiuzulu 1978);
alifariki 1982

Dakta (Bibi) Mutumba M. Bull
(Zambia), tangu 1971

Hayati Profesa D. Chanaiwa
(Zimbabwe), tangu 1975;
alifariki 1993

Profesa P.D. Curtin
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa H. Djait
(Tunisia), tangu 1975

Hayati H.E.M. El Fasi
(Morocco), tangu 1971; alifariki 1991
Mhariri Juzuu III

Profesa J.D. Fage
(Uingereza), 1971- 81 (alijiuzulu)

Hayati Profesa J.L. Franco
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dakta V.L. Grottanelli
(Italia), tangu 1971

Hayati Profesa E. Haberland
(Ujerumani Magharibi), tangu 1971; alifariki 1992

Dakta Aklilu Habte
(Ethiopia), tangu 1971

Hayati H.E.A. Hampâté Bâ
(Mali), 1971 - 8; (alijiuzulu); alifariki 1991

Dakta I.S. El-Hareir
(Libya), tangu 1978

Profesa M. Difuila
(Angola), tangu 1978

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop
(Senegal),1971- 86; alifariki 1986

Hayati AbbéAlexis Kagame
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki

Profesa I.N. Kimambo
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo
(Burkina Faso), tangu 1971
Mhariri Juzuu I na IV

Bw. D. Laya
(Niger), tangu 1979

Dakta A. Letnev
(Urusi), tangu 1971

Dakta G. Mokhtar
(Misri), tangu 1971
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa
(Uganda), tangu 1975

Profesa L.D. Ngcongco
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane
(Senegal), tangu 1971
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),
tangu 1975

Profesa Bethwell A. Ogot
(Kenya), tangu 1971
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary
(Madagascar), tangu 1971

Hayati Dakta I. Hrbek
(Czechoslovakia), tangu 1971; alifariki 1993
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Dakta (Bibi) A. Jones

Hayati Profesa W. Rodney
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dakta E. Williams
(Trinidad na Tobago), 1976-8;
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui
(Kenya)
Mhariri Juzuu VIII,
Siyo Mwanakamati

Profesa C. Wondji (Côte d'Ivoire)
Mhariri Msaidizi Juzuu VIII
Siyo Mwanakamati

*Ukatibu wa Kamati ya*
*Kimataifa ya Kisayansi*
A. Gatera
Kitengo cha Taaluma za Utamaduni na Sera
1, rue Miollis
75015 Paris

# Wasifu wa Waandishi waliochangia kwenye Juzuu Kuu

**Toleo lililofupishwa lilitarishwa kutoka kwenye matini za toleo kuu lililoandikwa na waandishi wafuatao**

| | |
|---|---|
| SURA YA 1 | A. Adu Boahen (Ghana); mtaalamu wa historia ya ukoloni wa Afrika Magharibi, mwandishi wa machapisho na makala mengi kuhusu historia ya Afrika; Profesa na Mudiri wa Idara ya Historia; Chuo Kikuu cha Ghana. |
| SURA YA 2 | G. N. Uzoigwe (Nigeria); mtaalamu wa historia ya Afrika Mashariki, hususan historia ya ufalme wa zamani wa Bunyoro nchini Uganda, mwandishi wa vitabu na makala kadhaa kuhusu historia ya Afrika; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Michigan, Ann Arbor. |
| SURA YA 3 | T. O. Ranger (Uingereza); mtaalamu wa ukinzani wa Kiafrika na harakati za kizalendo, mwandishi na mhariri wa vitabu na makala mengi katika uwanja huu; Profesa wa zamani wa Historia wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na UCLA; Profesa wa Historia ya Sasa, Chuo Kikuu cha Manchester. |
| SURA YA 4 | H. A. Ibrahim (Sudan); mtaalamu wa historia ya karne ya kumi na tisa na ishirini ya Misri na Sudan; amechapisha vitabu kadha Mhadhiri wa Historia, Chuo Kikuu cha Khartoum. |
| | I. Abbas (Sudan); mtaalamu wa historia ya karne ya kumi na tisa ya Sudan na historia ya Afrika Mashariki; mwandishi wa vitabu na makala katika nyanja hizi; Mudiri wa zamani wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Khartoum, amefariki. |
| SURA YA 5 | A. Laroui (Moroko); mtaalamu wa historia ya Maghrib, mwandishi wa vitabu na makala kuhusu historia ya karne ya kumi na tisa ya Afrika Kaskazini; Profesa wa Historia ya kisasa na wakati huu katika Chuo Kikuu cha Rabat, Moroko. |
| SURA YA 6 | M. Gueye (Senegal); mtaalamu wa historia ya karne ya kumi na tisa na ya ishirini ya Afrika Magharibi; mwandishi wa vitabu kadha kuhusu biashara ya watumwa na ukoloni wa Ufaransa; Mhadhiri wa Historia katika Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Dakar, Senegal. |
| | A. Adu Boahen. |
| SURA YA 7 | H. A. Mwanzi (Kenya); mtaalamu wa historia ya Afrika Mashariki, mwandishi wa vitabu kadha na makala, hususan kuhusu Wakipsigi wa Kenya; Mhadhiri Mwandamizi katika Historia, Chuo Kikuu cha Nairobi. |
| SURA YA 8 | A. Issacman (Marekani); mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa vitabu na makala mbalimbali; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Minnesota. |
| | J. Vansina (Ubelgiji); mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa vitabu na makala mengi kuhusu historia ya Afrika ya kabla ya ukoloni; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison. |
| SURA YA 9 | D. Chanaiwa (Zimbabwe); mtaalamu wa historia ya karne ya kumi na nane na kumi na tisa ya Kusini mwa Afrika; Profesa wa zamani wa Historia, Chuo Kikuu cha Califonia State; Northridge; Mkurugenzi, Idara ya Uajiri na Maendeleo ya Uajiri, Harare. |
| SURA YA 10 | M. Esoavelomandroso (Madagascar); mtaalamu wa historia ya karne ya kumi na nane na kumi na tisa ya Madagascar; Profesa wa Historia, Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Antananarivo. |

| | |
|---|---|
| SURA YA 11 | M. B. Akpan (Nigeria); mtaalamu wa historia ya uchumi ya Afrika Magharibi; mwandishi wa vitabu na makala kadha kuhusu historia ya Afrika Magharibi. Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Calabar, Nigeria.<br>A.B. Jones (Liberia); mwanahistoria na mtaalamu wa Afrika Magharibi ya karne ya kumi na tisa; Balozi wa zamani na Mwakilishi wa kudumu wa Liberia katika Umoja wa Mataifa.<br>R. Pankhurst (Uingereza); mtaalamu wa historia ya Ethiopia; mwandishi wa vitabu na makala mengi kuhusu historia ya Ethiopia, Mkurugenzi wa zamani wa Taasisi ya Taaluma za Ethiopia, Chuo Kikuu cha Ethiopia. |
| SURA YA 12 | M. Crowder (Uingereza); mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi; mwandishi wa vitabu na makala mengi kuhusu historia ya Afrika Magharibi; alishika cheo cha Profesa katika Vyuo Vikuu mbalimbali; mhariri wa *History Today*; hivi sasa ni Profesa Mgeni katika Chuo Kikuu cha Botswana. |
| SURA YA 13 | E. F. Betts (Marekani); mtaalamu katika ukoloni wa Wazungu wa karne ya kumi na tisa na ishirini; mwandishi wa vitabu na makala kadha kuhusu historia ya Afrika; Profesa wa Historia katika Chuo Kikuu cha Kentucky.<br>I. Asiwaju (Nigeria); mtaalamu katika historia ya Afrika Magharibi; mwandishi wa vitabu na makala mbalimbali kuhusu eneo hili; Profesa wa Historia katika Chuo Kikuu cha Lagos. |
| SURA YA 14 | W. Rodney (Guyana); mtaalamu katika historia ya Uchumi ya Afrika Magharibi; mwandishi wa vitabu na makala kadha kuhusu biashara ya watumwa ya Afrika Magharibi; Profesa wa zamani wa Historia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Tanzania na cha West Indies; sasa ni marehemu, |
| SURA YA 15 | C. Coquery-Vidrovitch (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya jamii na uchumi ya Afrika, amechapisha vitabu na makala kadha kuhusu somo hilo; hivi sasa ni Profesa wa Historia Chuo cha Paris VII. |
| SURA YA 16 | M. H. Y. Kaniki (Tanzania); mtaalamu wa historia ya uchumi wa Afrika Magharibi, amechapisha vitabu na makala kadha, zamani alikuwa Profesa Mshiriki wa Historia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; hivi sasa ni Profesa wa Historia Chuo Kikuu cha Zambia, Lusaka. |
| SURA YA 17 | A. Kassab (Tunisia); mtaalamu katika jiografia ya uchumi; amechapisha makala kadha yanayohusiana na uwanda huo; Mhariri Mkuu wa "La revue Tunisienne de Geographie".<br>A. Abdussalam (Libya); mtaalamu katika historia ya uchumi ya Libya; mwandishi wa vitabu kadha katika somo hilo; Profesa Msaidizi wa Uchumi, Chuo Kikuu cha Garyounis, Benghazi, Libya. |
| SURA YA 18 | J. C. Cadwell (Australia); mtaalamu wa demografia; mwandishi wa vitabu kadha kuhusu idadi ya watu katika Afrika ya Tropiki; Profesa wa Demografia na Mkuu wa Idara ya Demografia, Taasisi ya Uchunguzi wa Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Taifa cha Australian. |
| SURA YA 19 | A. E. Afigbo (Nigeria); mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa vitabu na makala ya kisayansi kadha kuhusu historia ya Nigeria; Mkurugenzi wa zamani wa Taasisi ya Taaluma za Kiafrika; Chuo Kikuu cha Nigeria (Nsukka). |
| SURA YA 20 | K. Asare Opoku (Ghana); mtaalamu wa dini za Kiafrika, mwandishi wa vitabu na makala kadha kuhusu vipengee anuwai vya dini za Kiafrika; Mchunguzi Mwandamizi katika Dini na Maadili, Taasisi ya Taaluma za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Ghana. |
| SURA YA 21 | W. Soyinka (Nigeria); mtaalamu wa tamthiliya, fasihi na falsafa ya Kiafrika; mwandishi wa vitabu vingi katika uwanja huo; Profesa wa zamani wa Chuo Kikuu cha Legon, Ghana na hivi sasa ni Profesa wa Tamthiliya katika Chuo Kikuu cha Ife. |
| SURA YA 22 | B. O. Oloruntimehin (Nigeria); mtaalamu katika Afrika Magharibi ya Kifaransa ya zamani tangu karne ya kumi na tisa; alichapisha vitabu na makala yanayohusu uwanja huo; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Ife. |
| SURA YA 23 | H. A. Ibrahim |

SURA YA 24 J. Berque (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya jamii ya Uislamu wa siku hizi; mwandishi wa vitabu kadha kuhusu historia ya Misri na Magharibi; Profesa wa zamani wa College de France.

SURA YA 25 A. Adu Boahen

SURA YA 26 E. S. Atieno-Odhiambo (Kenya); mtaalamu wa historia ya Siasa ya Afrika Mashariki; mwandishi wa vitabu na makala kadha kuhusu maendeleo ya uzalendo katika Afrika ya Mashariki na ya Kati; Mhadhiri Mwandamizi wa Historia, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

SURA YA 27 A. B. Davidson (Urusi); mtaalamu katika historia ya Afrika; amechapisha vitabu kadha kuhusu Afrika; Profesa katika Taasisi ya Historia Kuu, Akademia ya Sayansi ya Urusi, Moscow.

R. Pelessier (Ufaransa); mtaalamu wa harakati za ukinzani katika historia ya Afrika ya karne ya kumi na tisa na ishirini; mwandishi wa vitabu na makala kadha; Mtafiti.

A. Issacman.

SURA YA 28 M. B. Akpan, A. B. Jones na R. Pankhurst.

SURA YA 29 R. D. Ralston (Marekani); mtaalamu wa historia ya Afrika ya karne ya kumi na tisa na ishirini; mwandishi wa makala kadha kuhusu mahusiano kati ya Afrika na Ulimwengu mpya; Profesa Msaidizi wa Historia, Idara ya Taaluma za Kiafro-Amerika; Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison.

F. A. Atburquerque Mourão (Brazil); mtaalamu katika historia ya Afrika; mwandishi wa vitabu na makala kadha kuhusu historia ya Wabrazili-Waafrika; Profesa wa Historia na Mkurugenzi wa Kitivo cha Taaluma za Kiafrika (Centro de Estudos Africanos) katika Chuo Kikuu cha São Paulo, Brazil.

SURA YA 30 A. Adu Boahen.

Mhariri Msaidizi Y. Kwarteng (Ghana); mtaalamu katika uandishi wa habari wa mawasiliano; tasnifu yake ya M.A. inahusu, "Maendeleo ya Uandishihabari katika Afrika ya Magharibi kuanzia mwaka 1957

# 1

# Afrika na Changamoto ya Ukoloni

Katika historia ya Afrika hapajawahi kutokea mabadiliko mengi na ya haraka kama yalivyojiri kati ya miaka ya 1880 na 1935. Hivi karibuni hadi mwaka 1880, maeneo machache tu ya Afrika yalikuwa yakitawaliwa moja kwa moja na Wazungu na kuwa watawala wa Kiafrika na viongozi wa ukoo waliudhibiti uhuru na umamlaka wao (angalia mchoro 1.1). Lakini kufikia mwaka 1914 bara zima la Afrika, isipokuwa Ethiopia na Liberia, lilikwisha gawanywa na kutamalakiwa na nguvu za kibeberu za Ufaransa, Uingereza, Udachi, Ureno, Ubelgiji na Italia; na kwa hakika ukoloni ulikwishashamiri. Kwa hiyo, kwa maneno mengine, katika kipindi cha 1880 hadi 1935, Afrika ilikabiliwa na changamoto kubwa, ambayo ilikuwa changamoto ya ukoloni.


## *Hali ya Afrika ya Kujiandaa:*

Je, mwelekeo wa Waafrika wenyewe kuhusu ukoloni uliokuwa unastawishwa na ambao ulileta mabadiliko makubwa katika aina ya uhusiano uliokuwepo kati yao na Wazungu katika kipindi kilichotangulia cha miaka mia tatu ulikuwaje? Jibu lake ni dhahiri: mamlaka mengi sana na viongozi wa Kiafrika walipinga katakata mabadiliko hayo na walipania kibwebwe kudumisha hali yao ya zamani na, juu ya yote, kuhifadhi umamlaka na uhuru wao. Jibu hili linaweza kuthibitishwa kwa maneno ya viongozi wa Kiafrika wenyewe wa wakati huo.

Katika mwaka 1891 wakati Waingereza walipotaka kumpa himaya Prempeh I wa Waasante katika Gold Coast, yeye alijibu ya kuwa:

> Pendekezo la kuwa Asante kama ilivyo hivi sasa ipate himaya ya Malkia Mtukufu na Malkia wa India ni jambo la kuzingatiwa kwa makini sana, na ambalo ninafurahi kusema tumefikia natija ya kuwa ufalme wangu wa Asante kamwe hautakubali kufuata sera hiyo. Asante lazima ibaki kama ilivyo na ilivyokuwa tangu zamani na pape hapo idumishe urafiki na watu weupe wote.

Katika 1895, Wabogo, Moro Naha au Mfalme wa Wamosi (katika Burkina Faso ya sasa) alimwambia Kepteni wa Kifaransa Destenava:




**1.1** Afrika kabla ya kugawanywa ikionyesha kiasi cha eneo la utamalaki hadi mwaka 1880.

> Ninajua kwamba watu weupe wanataka kuniua miye ili watamalaki nchi yangu, na bado wewe unadai kuwa watanisaidia kuendesha vizuri nchi yangu. Lakini siwahitaji. Ninatambua nini cha muhimu kwangu na ninachotaka; nina wafanyabiashara wangu mwenyewe: pia, ushukuru bahati yako sikuamrisha kichwa chako kikatwe. Nenda zako; na zaidi ya yote, usije tena.

Wakati Wataliani waliposhambulia Ethiopia baada ya kuachwa wafanye hivyo na Uingereza na Ufaransa, Mfalme Menelik, katika tangazo la kuondoa majeshi yake mnamo Septemba 1895 alisema hivi:

> Maadui wametujia kudamiri nchi yetu na kubadili dini yetu... Maadui zetu wameanza mashauri yao kwa kuvamia na kujiingiza katika nchi kama fuko, kwa msaada wa Mungu sitawaachia nchi yangu... Leo, nyinyi wenye nguvu, nipeni nguvu zenu, na nyinyi msio na nguvu, nisaidieni kwa sala.

Hisia kama hizo pia zilielezwa na Lat Dior Damel wa Cayon (katika Senegal ya sasa) katika 1883 na Mfalme Machemba wa Wayao katika bara la sasa la Tanzania katika 1890, na Hendrik Witthoi, Mfalme mmojawapo wa South-West Africa (Namibia).

Hayo ni maneno hasa ya watu waliokabili changamoto ya kikoloni na yanabainisha uthabiti wa dhamira yao ya kuwapinga Wazungu na kulinda uhuru, dini na desturi zao za jadi za maisha yao.

Kauli hizo zote zinadhihirisha kuwa watawala hao walijiamini katika kujiandaa kwao kuwakabili wavamizi wa kizungu. Na kujiamini huko kulikuwa na sababu zake. Mosi, waliamini kuwa uchawi wao, wahenga wao na miungu au Mungu wao atawasaidia. Wengi wao punde tu kabla ya uvamizi wenyewe kufanyika walishughulika na sala au matambiko au mitishamba na nyimbo za kidini. Kama itakavyodhihirika katika sura nyingi zitakazofuata, dini ndiyo ilikuwa mojawapo ya silaha zilizotumika dhidi ya ukoloni. Aidha, watawala wengi wa Kiafrika waliweza kujenga himaya zenye ukubwa mbalimbali katika miongo miwili tu iliyopita, na wengine bado walikuwa katika kupanua au kuhuisha falme zao. Wengi wao walikwishaweza kuhami uhuru wao kwa msaada wa watu wao wakitumia silaha za kijadi na maarifa. Baadhi yao kama Wasamari Ture wa Himaya ya Mande katika Afrika Magharibi na Menelik wa Ethiopia waliwahi hata kufanya majeshi yao yawe ya kisasa. Kutokana na hayo yote, watawala wa Kiafrika hawakuona sababu kwa nini wasiweze kulinda uhuru wao wakati huo. Vile vile, baadhi yao walidhani wangeweza kuwaepuka wavamizi kwa njia ya diplomasia.

Aidha, kutokana na baadhi ya kauli zilizotangulia ni dhahiri kuwa watawala wengi wa Kiafrika walikaribisha mabadiliko mapya yaliyokuwa yanatokea "*asteaste*" tangu mwongo wa tatu wa karne ya kumi na tisa kwani mabadiliko hayo mpaka wakati huo hayakuwa yanahatarisha uhuru wao. Kwa mfano katika Afrika Magharibi, kutokana na amali za Wamisionari, Chuo cha Fourah Bay kilikwishaasisiwa tangu

1826 na shule za msingi na shule moja ya sekondari pia katika Gold Coast na Nigeria zilikwisha anzishwa kwenye miaka ya 1820. Ama kwa hakika, wito wa kuanzisha Chuo Kikuu katika Afrika Magharibi ulikwishatolewa na mtetezi wa Uafrika – wote aliyezaliwa Carribean, Edward Wilmot Blyden. Tangu mwaka 1887, baadhi ya Waafrika tajiri walikwishaanza kuwapeleka watoto wao Ulaya kusoma zaidi na kwa mafunzo ya kitaalamu na baadhi yao walikwisha rejea nyumbani wakiwa wamefuzu kuwa madaktari na mawakili.

Fauka ya yote, baada ya kubatilishwa kwa biashara katili ya watumwa, waafrika walikwishaweza kubadilisha mfumo wao wa uchumi na kuingia katika mfumo wa uchumi wa bizanje wa mazao ya biashara – mafuta ya mchikichi huko Nigeria, karanga huko Senegal na Gambia. Yote hayo yalitokea kabla ya mwaka 1880 na kakao ndiyo kwanza ilikuwa imerejeshwa tena katika Gold Coast na *Tetteh Quashie* kutoka *Fernando Po* katika 1879. Hayo yote yalijiri pasi ya kuwa na Utawala wa moja kwa moja wa Wazungu, isipokuwa hapa na pale kwenye sehemu za mwambao. Ama kwa hakika, kikundi kidogo cha Waafrika Magharibi ambao walikwishafaidika kutokana na mtindo wa elimu ya Kizungu ilipofikia 1880 kilikuwa kimeshastawi vizuri mno. Walikuwa wamekwishashika nafasi chache serikalini; kwenye sehemu za mwambao, baadhi yao walikuwa wanaendesha biashara zao za kuagiza na kusafirisha mali na walikuwa wanahodhi ugawaji wa mali kutoka nchi za nje. Ni katika Afrika Mashariki tu ndiko taathira za wazungu bado zilikuwa kidogo ingawa baada ya safari za kihistoria za Livingstone na Stanley na propaganda zilizofuata safari hizo za jamii za wamisionari muda si muda kukaanzishwa makanisa, shule na barabara na reli pia.

Kwa hiyo, Waafika waliohusika hawakuona haja ya kufanya mabadiliko ya msingi katika mahusiano yao ya karne nyingi na Ulaya, na waliamini kuwa iwapo Wazungu walitaka kulazimisha mabadiliko ya aina yoyote na kujipenyeza katika bara, wangeweza kuwazuia kama walivyoweza kufanya kwa miaka mia mbili au mia tatu iliyopita. Ndiyo maana kauli zilizokaririwa hapo juu zinaonyesha kuwa Waafrika walau walijiamini, kama si kudiriki kuonyesha ukaidi.

Lakini jambo ambalo Waafrika walikuwa hawajang'amua bado mpaka 1880, ni kuwa kutokana na kuenea kwa mapinduzi ya kitasnia katika Ulaya, na maendeleo yaliyotokea ya kiteknolojia yakiwakilishwa na meli za Stima, reli na telegrafu na, fauka ya yote, bundaki za kwanza – bunduki ya Maxim – Wazungu, ambao walikuwa wanajitayarisha kuwakabili, walikuwa na malengo mapya ya kisiasa, haja za kiuchumi na teknolojia iliyoendelea. Hii ina maana kuwa hawakujua kuwa enzi ya zamani ya biashara huru na udhibiti usio rasmi wa kisiasa ilikwishapitwa na, chembilecho Basil Davidson, "enzi ya ubeberu mpya na mashindano ya uhodhi wa kibepari" na kwa hiyo basi wazungu hawakutaka biashara tu bali pia walitaka udhibiti wa moja kwa moja wa kisiasa. Pili, viongozi wa Kiafrika hawakaelewa kuwa bunduki walizokuwa wakitumia mpaka wakati huo na ambazo walikuwa wamezirundika, bunduki za mrao za mitutu (Wafaransa walikamata bunduki za mrao 21365 kutoka kwa Wabaule wa Ivory Coast baada ya kuzima uasi wao wa 1911) zilikwisha kuwa kongwe kabisa na zisingeweza

kupambana na zile za Wazungu, bunduki za "Kupakiwa risasi sehemu ya nyuma" ambazo zilikuwa na uwezo wa mara kumi wa kupiga na kasi ya mara sita na bunduki za maxim za kisasa kabisa. Mshairi wa Kiingereza, Hilaire Belloo, alitoa muhtasari mzuri wa hali ilivyo aliposema:

> *Whatever happens we have got The Maxim-gun and they have not* (Litakalokuwa na liwe siye tunayo Bunduki la Maxim wao hawana).

Hapo ndipo watawala wa Kiafrika walipoghafilika na mara nyingi matokeo yakawa ya kuhuzunisha. Kama itakavyodhihirika hapo baadaye, machifu wote waliokwisha tajwa, isipokuwa mmoja tu, walishindwa na kupoteza uhuru wao. Aidha, Lat Dior aliuliwa, Prempeh, Behanzin na Cetshwayo wa Wazulu walihamishwa nchi na Lobengula wa Wandebele alikufa alipokuwa anakimbia. Kama itakavyodhihirika katika sura mojawapo ya baadaye, ni Menelik tu peke yake aliyewashinda wavamizi wa Kitaliani na kwa kufanya hivyo akaweza kunusuru uhuru na umamlaka wake.

## *Muundo wa Juzuu hili:*

Kwa hiyo, kuna ushahidi kuwa, mahusiano kati ya Waafrika na Wazungu yalibadilika kimapinduzi na Afrika ilikabiliwa na changamoto ngumu ya kikoloni kati ya miaka 1880 na 1935. Kwa hiyo, ni asili ya changamoto hii ya pekee, changamoto ya ukoloni? Au kwa maneno mengine, vipi na kwa nini mahusiano ya karne tatu kati ya Afrika na Ulaya yaliweza kubadilika kimsingi kiasi hicho na hatua gani za kisiasa, kiuchumi, kisaikolojia na kiitikadi zilichukuliwa kuimarisha mfumo huo? Waafrika walikuwa wamejiandaa kiasi gani kuikabili na waliikabili changamoto hiyo kwa jinsi gani na walifanikiwa kiasi gani? Ni mabadiliko mapya yapi yalikubaliwa na yapi yalikataliwa? Mambo yapi yalidhamiriwa? Ni unasibishaji upi na marekebisho yapi yalifanyika? Hayo yote yalileta athari gani kwa Afrika, kwa watu wake, na kwa miundo na asasi zake za kisiasa, kijamii na kiuchumi? Mwishoni, nini umuhimu wa ukoloni kwa Afrika na historia yake? Hayo ni maswali ambayo juzuu hili litajaribu kuyajibu.

Kwa madhumuni ya kujibu masuala hayo, na kueleza juhudi na majibu ya Waafrika kwa changamoto ya ukoloni, juzuu hili limegawanywa katika sehemu tatu kuu, isipokuwa sura mbili za mwanzo. Kila sehemu inatanguliwa na sura (3, 13, 22) ambamo maudhui ya sehemu hii inapitiwa kwa jumla na kuonyesha mkabala wa kilimwengu (kijumla), na sura zinazofuata zinashughulikiwa kikanda. Sehemu ya utangulizi ambamo ndani yake mna sura hii na sura inayofuata inajadili mikabala na kujiandaa kwa Waafrika katika kipindi kilichotangulia badiliko hilo muhimu katika uhusiano wake baina ya Wazungu na Waafrika, na sababu za ugawanaji, utamalaki na ulowezi wa Afrika na dola za kibeberu za Kizungu.

Sehemu ya pili inashughulikia maudhui ambayo hadi miaka ya 1960 yalikuwa ama yamewasilishwa vibaya au yalipuuzwa kabisa na fikra za kikoloni za uandikaji wa

historia ya Afrika, yaani, juhudi na majibu ya Waafrika kukabiliana na utamalaki na ulowezi wa Afrika. Wanahistoria waliokuza fikra za kikoloni k.v. H.H. Johnston, Sir Alan Burns na hivi karibuni, Margery Perham, Lewis Gaun na H. Peter Duignan, waliona kuwa kwa hakika Waafrika walikaribisha utawala wa kikoloni kwani licha ya kuwakomboa Waafrika kutokana na ghasia za kutokuwa na sheria za vita vya wenyewe kwa wenyewe, vilevile uliwaletea manufaa halisi. Hivyo ,Margery Perham alisema:

> Mbari nyingi zilikubali kwa haraka utawala wa Kizungu kama ni sehemu ya mfumo usopingika, mfumo ambao ulileta faida nyingi, na juu ya yote amani, na vitu vipya vya kusisimua, reli na mabarabara, taa, baiskeli, plau, vyakula vipya na mazao mapya, na yote yale yaliyoweza kupatikana na kufaidika nayo mijini na vijijini. Ama kwa upande wa tabaka zilizotawala, za kijadi au zilizoundwa, utawala huo ulizidisha nguvu zao na kulinda hadhi pamoja na kuleta aina mpya za utajiri na nguvu. Miaka mingi baada ya utamalaki, ingawa bado kulikuwepo mfadhaiko, uasi ulikuwa mdogo, na *haielekei* kuwa kulikuwepo hizaya ya kutawaliwa.

Mawazo hayo pia yanajitokeza katika matumizi ya istilahi za Kiulaya kama vile 'Pacification' (usuluhisho), *Pax Britannica na Pax Gallica* zilizotumika kwa kejeli kuelezea utamalaki na ukaliaji wa Afrika kati ya 1890 na 1914.

Ni katika kusahihisha fasiri hii potofu ya shule ya mawazo ya kikoloni, kusawazisha ukweli na kuonyesha taswira ya Kiafrika ndipo tumeweka Sura saba za kuelezea mada hii ya juhudi na majibu ya Waafrika.

Katika sura hizi itadhihirika kuwa ile fikra ya kuwa Waafrika waliwapokea maaskari wavamizi kwa furaha na waliukubali haraka utawala wa kikoloni haina ushahidi wowote. Ama kwa hakika, majibu ya Waafrika kuhusu suala hili yalikuwa kinyume na fikra hiyo. Kuna ushahidi wa kutosha wa kuonyesha kuwa Waafrika walikuwa na hiari mbili tu, ama kuusabilia uhuru na umamlaka wao, au kuulinda kwa kila njia. Ni muhimu kufahamu kuwa wengi wao, kama itakavyodhihirika vyema katika juzuu hili, bila kujali miundo ya kisiasa na ya kijamii-kiuchumi ya mataifa yao walipokabiliwa na kila hatari, waliamua kulinda umamlaka na uhuru wao. John D. Hagreaves ameuliza suala lifuatalo la kusisimua:

> Kutokana na aina ya mielekeo ya wavamizi wa Kizungu, hiari kadha zilikuwa mbele ya watawala wa Kiafrika. Miongoni mwa faida za muda mfupi zingepatikana kutokana na mikataba na au kushirikiana na Wazungu hazikuwa tu uwezo wa kujipatia silaha na bidhaa za matumizi, lakini fursa za kupata marafiki wenye nguvu katika migogoro ya ndani na nje. Kwa nini basi mataifa mengi ya Kiafrika yalizikataa fursa hizo, na kuchagua kupigana vita na Wazungu?

Suala hilo linaweza kuwa la kubabaisha kwa yule anayetazama suala hili kwa jicho la Wazungu. Kwa Mwafrika suala halikuwa faida za muda mfupi au za muda mrefu, bali lilikuwa suala la msingi, la ardhi yake na umamlaka wake. Na kwa sababu hii ndiyo

mataifa yote ya Kiafrika yaliyokuwa na Serikali Kuu au yasiyokuwa yenye Serikali Kuu, mwanzoni au baadaye yalichagua kudumisha au kulinda au kujaribu kukomboa umamlaka wao. Hao hawakufanya mapatano, na kwa hakika viogozi wengi wa mataifa hayo walihiari kufa vitani, kukimbilia kwingineko au kuhama nchi kuliko kusalimisha umamlaka wao bila ya mapambano.

Hivyo, wengi kati ya watawala wa Kiafrika walichagua kulinda umamlaka na uhuru wao. Walitofautiana tu katika mikataba na mbinu walizotumia kufikia lengo hili kuu. Kama madondoo yaliyotangulia yanavyoonyesha Watawala wengi wa Kiafrika walichagua mkakati wa mapambano ama kwa kutumia diplomasia au silaha za kijeshi au yote miwili. Kama itakavyoonekana hapo baadaye, Samori Toure na Kabarega wa Bunyoro walitumia silaha zote mbili, lakini Prempeh I na Mwanga wa Buganda walitumia diplomasia peke yake. Wengine kama vile Tofa wa Porto Nono (katika Benin ya sasa) walichagua mkakati wa unafiki au wa kusaidiana, sio wa ushirikiano.

Suala hili la mkakati linahitaji kudokezwa hapa maana huko nyuma limekuwa likieleweka vibaya sana na limesababisha fikra za kuwa watawala wa Kiafrika walikuwa washiriki wa ukoloni na vitendo vyao vimekuwa vikichukuliwa kama ni ushirikiano na wakoloni. Tunapinga matumizi ya neno hili ushirikiano siyo tu kwa sababu si neno sahihi bali pia kwa sababu linadhalilisha na kuonesha mkabala wa Kizungu. Kama tulivyokwishaona hapo awali, suala la msingi lililojitokeza kati ya miaka ya 1880 na ya 1900 linalowahusu watawala wa Kiafrika, lilikuwa la umamlaka, na katika suala hilo ni dhahiri kuwa hakuna aliyekuwa tayari kupatana na wavamizi. Watawala wa Kiafrika ambao wanaitwa washiriki kwa makosa ni wale ambao waliona kuwa njia ya kulinda umamlaka wao au hata ya kuunyakua umamlaka wao ambao pengine ulikuwa umetwaliwa na dola nyingine ya Kiafrika kabla ya ujio wa wazungu, haikuwa ile ya kufanya ushirikiano, bali ilikuwa ile ya kusaidiana na wavamizi wa Kizungu.

Hata hivyo, juu ya mikakati yoyote ile iwayo iliyofuatwa na Waafrika, watawala wote – isipokuwa wa Liberia na Ethiopia – yote ilishindwa, kwa sababu zitakazoelezwa baadaye, kutunza umamlaka wao. Kufikia mwanzoni mwa Vita Vikuu vya Kwanza ambayo ndiyo tarehe ya kukomea katika sehemu ya kwanza ya juzuu hili, Afrika ilikwishatawaliwa na wakoloni. Vipi na kwa nini Waliberia na Waethiopia waliweza kunusurika na uvamizi huo wa ukoloni vimezungumziwa katika sura II.

Kwa hiyo ni kitu gani ambacho madola hayo ya kikoloni yaliyafanyia makoloni yao katika nyanja za siasa, jamii na uchumi baada ya kipindi cha kupumua cha Vita Kuu vya Kwanza? Swali hilo ndilo linalojibiwa katika sehemu ya pili ya juzuu hili. Hapa, kwa vile vyombo mbalimbali vya uendeshaji wa makoloni na itikadi zinazozitawala vimeelezwa vizuri – katika maandishi mengi yaliyopo yanayozungumzia ukoloni katika Afrika, basi sura moja tu inashughulikia mada hii. Badala yake macho yameangazwa zaidi kwenye *jiha* za kiuchumi na kijamii za mfumo wa kikoloni, na taathira zake kwa Afrika ili kupata utaurari unaotakiwa. Katika sura hizi itadhihirika kuwa kipindi cha baada ya Vita Vikuu vya Kwanza hadi 1935,

ambacho kimewasifiwa na baadhi ya wanahistoria wa hivi karibuni kuwa ndicho cha kilele cha ukoloni, kulijengwa muundombinu wa barabara na reli na kuleta mabadiliko fulani ya kijamii kama vile uanzishaji wa shule za msingi na za sekondari. Lakini, watawala wa kikoloni walikuwa na nia moja kuu, nayo, ilikuwa ya kunyonya kikatili raslimali za Afrika kwa manufaa tu ya dola za kikoloni na kampuni zao za kibiashara, migodi na za kifedha katika nchi mama. Sura moja katika sehemu hii ambayo hasa inafaa itupiwe jicho ni ile inayozungumzia *jiha* za kidemografia za utawala wa kikoloni. Hii ni mada ambayo kwa kawaida haionekani katika mitalaa iliyopo inayohusu ukoloni katika Afrika.

Kulikuwa na juhudi na majibu yapi ya Kiafrika katika kukabiliana na uimarishaji huu wa ukoloni na unyonyaji wa bara lao? Hili ni swali linalojibiwa katika sehemu ya tatu ya juzuu hili. Suala hili linazungumziwa sana kufuatana na falsafa inayotawala kazi hii, yaani, ya kuangalia masimulizi kwa jicho la Mwafrika na kukuza juhudi na majibu ya Kiafrika. Kwa hakika, mwelekeo wa Mwafrika katika kipindi hiki haukuwa wa kutojali, wa ukimya au wa ukubalifu. Iwapo kipindi hiki kimeonyeshwa kuwa kilikuwa cha kilele cha ukoloni, basi nacho pia ni enzi ya kilele cha mkakati wa ukinzani katika Afrika. Kama itakavyoonyeshwa kote kuwili katika mapitio ya jumla na katika mapitio yatakayofuata ya kikanda, Waafrika walitumia mbinu na hatua kadhaa – kwa hakika hatua na mbinu anuwai ziliundwa za kupinga ukoloni.

Inafaa isisitizwe kuwa isipokuwa kwa viongozi wa Afrika Kaskazini wakati huo shabaha haikuwa kuupindua mfumo wa kikoloni bali shabaha ilikuwa kuufanya mfumo huo uwe na maondokeo na kuishi nao. Shabaha kuu ilikuwa ya kuufanya ukoloni upunguze ukandamizaji wake, uheshimu utu na unufaishe Waafrika na Wazungu. Viongozi wa Kiafrika walitaka kurekebisha hasa hatua na kashifa za ushokoa, kodi kubwa za mapato, kilimo cha kulazimishwa, ukengeusho wa ardhi, sheria za vipande, bei ndogo za mazao ya kilimo na bei kubwa za bidhaa zinazoagizwa nje, ubaguzi wa rangi na ubaguzi kwa ujumla na kuongeza suhula za kijamii ambazo wakati huo zilikuwa hazitoshi, kama vile mahospitali, maji ya bomba na shule.

Inapaswa kusisitizwa kuwa hisia za malalamiko hayo dhidi ya mfumo wa ukoloni zilitokea miongoni mwa tabaka zote za jamii, wasomi na wasiosoma, wakazi wa mjini na wa vijijini, na zilileta dhamira ya aina moja kati yao ya kuwa walikuwa Waafrika na watu weusi kinyume na wakandamizaji wao ambao walikuwa watawala wa kikoloni na watu weupe. Ni katika kipindi hiki ndimo uzalendo wa kisiasa wa Waafrika ulipoimarishwa na ambao ulianza punde tu baada ya ukamilishwaji wa mfumo wa kikoloni katika miaka ya 1910. Uwadhihishaji wa hisia hii na uongozi wa harakati ya upinzani, ambao katika kipindi cha hadi miaka 1910 ulikuwa wajibu wa mamlaka za jadi na ulikuwa katika mazingira ya miundo ya kisiasa ya kipindi cha kabla ya ukoloni, sasa ulikuwa mikononi mwa kikundi kipya cha wasomi au watu wa tabaka ya kati. Jambo la kushangaza ni kuwa viongozi hao wapya walikuwa matokeo ya mfumo huohuo wa ukoloni ulioundwa na kudumishwa shuleni na katika asasi za kitawala, migodi, za kifedha na za kibiashara zilizotokana na mfumo huo. Ni

mkusanyiko huo wa uongozi wa amali za kizalendo na za kupinga ukoloni uliokuwa katika uwezo wa Waafrika wasomi ambao aghalabu waliishi katika miji ndio ulisababisha uzalendo wa Kiafrika wa kipindi cha vita viwili uchukuliwe kwa makosa kuwa ulikuwa wa tabaka hilo peke yake na kubainishwa kuwa kimsingi ulikuwa katika jumla ya harakati za kimji.

Vikundi na jumuiya nyingi ziliundwa kwa ajili ya kudhihirisha maulikio hayo ya kizalendo. Kama itakavyodhihirika katika sura zilizomo katika sehemu hii, mikakati na mbinu zilizoundwa katika kipindi hicho za kuelezea maulikio hayo vilevile zilitofautiana. Kama walivyoeleza B.O Oloruentimehin na E.S. Atieno – Odhiambo (sura ya 22 na ya 26 hapo baadaye), vikundi hivyo vilikuwa pamoja na jumuiya za vijana, jumuiya za kimbari, jumuiya za wanafunzi wa zamani, vyama vya siasa, aina ya harakati za kisiasa za kimataifa, za ndani na nje ya bara, Muungano wa Jumuiya za Wafanyakazi, biashara, vilabu vya wasomi, vilabu vya watumishi wa serikali, jumuiya za kurekebisha mambo na madhehebu na harakati mbalimbali za kidini. Baadhi yake yalikwishaundwa katika kipindi kabla ya Vita Kuu vya Kwanza. Lakini hapana shaka kuwa hizo zilizagaa katika kipindi kinachozungumziwa kama sura hizo zinavyoonyesha.

Silaha au mbinu zilizotumika wakati wa kipindi cha ukoloni, kinyume na zile za kipindi cha kabla ya Vita Kuu vya Kwanza ambamo nasi na machafuko vilitokea sana, zilikuwa za aridha na Ujumbe wa kuzungumza na Serikali za nchi mama na Serikali za nchini, migomo, misuso, na fauka ya yote, magazeti yote na mikutano ya kimataifa. Miaka ya kati ya Vita viwili ilikuwa kilele cha uandishi wa habari katika Afrika kwa jumla na hasa Afrika Magharibi. Papohapo mikutano yote ya Kiafrika wote pia ilikuwa njia mojawàpo ya harakati ya kupinga ukoloni. Mikutano hiyo ilidhamiriwa izipe sura ya kimataifa harakati za wuzalendo na wapinga ukoloni katika Afrika. Mikutano hiyo ilitarajia kuzifanya dola za nchi mama ziyazingatie matukio yaliyokuwa katika makoloni yao. Ndiyo maana mikutano ya Uafrika wote iliyoandaliwa na Mwamerika mweusi Dkt. W.E.B. Dubois, ilifanyika huko Paris, London, Brussels na hata Lisbon. Mada hii inazungumziwa kwa urefu zaidi katika sura ya 29 ambayo inahusika na mawasiliano kati ya watu weusi wa Afrika na watu weusi wa "diaspora" waliotawanyika huko Marekani katika kipindi chote kinachozungumziwa.

Hata hivyo, ingawa kulikuwapo jumuiya mbalimbali na mchangamano wa mbinu, hadi kufikia miaka ya 1930, mfumo wa ukoloni haukuwa umeathirika sana isipokuwa Misri tu. Katika 1935, wakati majeshi ya kibeberu ya kifashisti ya Italia ilivyotawaliwa na Mussolini ilitwaa na kutamalaki Ethiopia, mojawapo ya nguzo mbili zilizobakia za matumizi na alama kuu ya uhuisho na unyakuaji tena wa umamlaka wa Afrika katika siku za baadaye, ilionekana kana kwamba bara la Afrika lilikwishajaaliwa lifungwe minyororo ya ukoloni maisha. Lakini hayakwenda hivyo. Mnepo wa watu wa Afrika, utamalaki wa Ethiopia yenyewe, kuongezeka kwa uzalendo na hisia za kupinga ukoloni baada ya Vita Kuu vya Pili, ukiungana pamoja na vyama

vipya vya siasa vilivyotokeza na uongozi mpya wa kimapinduzi ambamo haukuamania kwenye maondokeo bali kwenye ung'aaji wa ukoloni – vipengee vyote hivyo, kama vile Juzuu la VII la kazi hii litakavyoonyesha, vilikusanyika kusababisha utokomezaji wa ukoloni barani Afrika kwa kasi ileile na katika muda wa kipindi cha miaka ishirini ambayo kilichukua kuisitawisha. Lakini, kati ya 1880 na 1935, ukoloni ulikuwa umeshajenga mizizi barani Afrika. Ni athari zipi ambazo ukoloni uliacha barani Afrika? Hilo ndilo swali linalojibiwa katika sura ya mwisho ya juzuu hili.

# 2

# Maelezo Mafupi Kuhusu Kugawanywa na Kutamalakiwa kwa Afrika na Wazungu

## *Utangulizi: Kipindi cha Vita na Mabadiliko ya Kimapinduzi*

Kipindi kilichofuata mwaka 1880 kilikuwa kipindi cha mabadiliko ya kihistoria yaliyo muhimu sana kwa wakati wa leo. Katika kipindi hicho, Afrika, bara lenye eneo la kilometa za mraba zaidi ya 28 milioni, iligawanywa na kutamalakiwa kikamilifu na mataifa ya Ulaya yaliyokuwa yameendelea kiviwanda. Jambo la kushangaza zaidi ni jinsi walivyoshirikiana kwa kasi na kwa urahisi- katika mtazamo wa Wazungu – katika kulitekeleza jambo hili. Kitu kama hicho kilikuwa hakijawahi kutokea. Ni kitu gani kilicho sababisha jambo hili? Yaani kwa nini Afrika iligawanywa kisiasa na taratibu ikakaliwa na Wazungu katika kipindi hicho? Na kwa nini Waafrika hawakuweza kuwazuia maadui wao hao?

## *Kugawanywa kwa Afrika na Ubeberu Mpya: Uhakiki*

Nadharia mbalimbali kuhusu tukio hili muhimu katika historia ya Afrika zimewahi kupendekezwa. Nadharia hizi zaweza kugawanywa katika mafungu manne nayo ni Nadharia ya kiuchumi, ya kisaikolojia ya kidiplomasia na ile ya hali halisi ya uwezo wa Waafrika.

### Nadharia ya Kiuchumi

Umaarufu wa nadharia hii umekwishabadilika na wakati kama mitindo ibadilikavyo. Kabla ukomunisti haujatishia mfumo wa kibepari huko Ulaya magharibi, hakuna mtu aliyejishughulisha sana na kuchunguza kwa makini misingi ya kiuchumi ya ueneaji wa ubepari. Mizizi ya nadharia hii imejikita katika tukio la mwaka 1900 wakati Wajerumani waliofuata siasa ya Demokrasia ya Jamii walipoweka mada ya Waltpolitiki (Siasa ya kiulimwengu – yaani sera ya upanukaji wa kibeberu katika masafa mapana ya kiulimwengu) katika ajenda ya mkutano mkuu wa mwaka wa chama chao, uliofanyika huko Mainz. Ni katika mkutano huo, ambapo Rosa Luxemburg alifafanua ya kuwa ubeberu ndiyo hatua ya mwisho ya ubepari. Ni katika mkutano huo huo pia ambapo George Ledebour alionyesha kuwa kiini cha Weltpolitik ni "kusababisha mainuko ya ubepari kuendeleza mfumo wa unyang'anyi ambao ungepeleka ubepari wa Marekani na Ulaya duniani kote". Lakini John Atkinson Hobson (1858 – 1940) ndiye aliyetoa maelezo ya kinaganaga zaidi, na

yanayozingatiwa hadi leo, kuhusu nadharia hiyo. Yeye alisema kuwa uzalishaji mali kwa wingi sana, ziada ya mitaji na matumizi pungufu katika mataifa yanayotegemea viwanda viliyafanya mataifa hayo kuweka sehemu kubwa zaidi na zaidi ya raslimali zao za uchumi nje ya maeneo yaliyokuwa chini ya mamlaka yao kisiasa, na kwa kufanya hivyo kuchochea ari ya upanuzi wa kisiasa wa kuteka na kukalia nchi nyingine.

Lenin akiyazingatia mawazo ya kiini ya mjadala huo wa Wanademokrasia ya Jamii wa Ujerumani pamoja na mawazo ya Hobson alisisitiza kuwa ubeberu mpya ulijidhihirisha katika mpito wa ubepari kutoka katika mfumo wa kutohodhi mali "ambao ulikuwa wa mashindano huria kwenda kwenye hodhi ya kibepari hadi kwenye mitaji ya fedha" ambao "unahusiana na kupamba moto kwa mapambano ya kuigawanya dunia". Kama vile ushindani wa kibepari ulivyotegemea uuzaji nje wa bidhaa vivyo hivyo hodhi ya kibepari ilijikita katika uuzaji nje wa rasilmali iliyotokana na faida kubwa zilizokusanywa na benki na viwanda. Maendeleo haya ndiyo Lenin aliyoyaita 'kiwango cha juu kabisa cha Ubepari'. Akifuatilia na kuyapinga mawazo ya Hobson, Lenin aliamini kuwa Ubepari ungejiangamiza wenyewe kwa vile ungechochea vita kati ya mabepari na mataifa yaliyonyonywa; vita ambavyo kwavyo ubepari ungeshindwa kwa vyovyote vile. Kwa hiyo basi matokeo ya ubeberu ni vita, kitu ambacho kitasababisha kufa kwa haraka kwa ubepari. Propaganda hii kali imekubaliwa na wafuasi Wasomi wa Marx, wananchi wa "Dunia ya Tatu" na wanamapinduzi wengi kama jambo la msingi. Wakiungana kwa mawazo na wasomi wanamapinduzi wa Kimagharibi wanauonyesha Ubeberu na ukoloni kama matokeo ya unyonyaji katili wa kiuchumi.

Ijapokuwa Hobson na Lenin hawakuwa wakiifikiria Afrika wakati wa malumbano yao, inaonekana wazi kuwa uchambuzi wao una uhusiano fulani wa kimsingi na ugawanywaji wa Afrika. Baadaye jeshi kubwa la wasomi wasiomfuata Marx kwa njia moja au nyingine wameibomoa nadharia ya Marx ya Ubeberu wa kiuchumi na jinsi inavyohusiana na Afrika. Hata hivyo kwa sasa inaonekana wazi, baada ya uchunguzi thabiti zaidi wa Historia ya Afrika ya kipindi hiki kuwa ubeberu kwa asili yake ulileta na sababu za kiuchumi.

## Nadharia za Kisaikolojia

Nadharia hizi zaweza kuelezwa kama misakumo isiyotokana na watu na ambayo ilileta upanuzi wa kibeberu, nazo zaweza kuainishwa kama Udarwini wa kijamii, Ukristo wa kiinjilisti na jamii kurudia mila na desturi za mababu. *Udarwini wa Kijamii*: Mwezi Novemba mwaka 1859 Charles Darwin alichapisha kitabu chake kiitwacho *The Origin of Species by Means of Natural Selection or the Preservation of Favoured Races in the Struggle for Life* (Asili ya Spishi kwa Njia ya Uteuzi wa Asili au Mahifadhio ya Kabila zilizopendelewa katika Mapambano ya kuishi). Kitabu hicho kilionekana kutoa msaada wa msimamo wa kisayansi kwa imani ya kuwa mataifa ya wazungu ni ya

kiwango cha juu zaidi; mada ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara katika namna mbalimbali zisizo dhahiri katika maandishi ya kizungu tangu karne ya 17. Kwa hiyo Wafuasi wa baadaye wa Darwin walifurahi mno kuweza kuthibitisha sababu zao za kushindwa na kukaliwa kwa "mataifa – tawaliwa" au "mataifa duni" na "mataifa bora" "kama tokeo lisiloepukika la" "uteuzi wa kiasilia" ambao kwao mwenye nguvu humtawala mnyonge katika mapambano ya maisha ya kiuchumi. Kwa hiyo walihubiri kuwa wenye nguvu ndiwo wenye haki. Hivyo kwao mgawanyo wa Afrika ulionekana kama jambo la asili ambalo lisingeepukika. Hata hivyo, ukweli ni kwamba Udarwini wa kijamii, kama ulivyohusishwa na Afrika, ulikuwa njia ya kutetea tukio baada ya tukio kufanyika, kuliko kuwa sababu ya tukio lenyewe.

**Ukristo wa Kiinjili*

Nadharia nyingine iliyojitokeza kuelezeaMgawanyo wa Afrika ilikuwa Ukristo wa Kiinjili. Imepata kuelezwa kuwa mgawanyo wa Afrika, kwa kiasi kikubwa ulitokana na "umisionari mpana zaidi" na msukumo wa huruma ambao ulitokana na ari ya kuwaendeleza Waafrika katika utamaduni wa Kimagharibi. Ama kwa hakika imepata kudaiwa kuwa Wamisionari wenyewe ndio hasa waliotayarisha majilio ya ukoloni katika Afrika ya Mashariki na ya Kati na pia katika Malagasi. Ijapokuwa ni kweli kuwa Wamisionari hawakupinga kutawaliwa kwa Afrika, na ijapokuwa inaeleweka kuwa katika sehemu nyingine waliendeleza utawala wa wageni, hata hivyo Umisionari hauwezi kuingizwa kwenye nadharia pana ya Ubeberu kwa vile ulikuwa na mashiko finyu.

## *Marudi ya Jamii katika Itikadi ya JadiMarudi ya Jamii katika Itikadi ya Jadi*

Joseph Schumpeter ndiye mtu wa kwanza kuelezea ubeberu mpya katika mawanda ya kijamii. Kwake yeye, ubeberu haukutokana na sababu za kiuchumi ila ulitokana na matamanio ya binadamu kumtawala binadamu mweuzie kwa sababu tu za ubwana zinazotokana na kiu ya asili ya nguvu na utawala. Anaendelea kutetea mawazo yake kuwa ubepari wenyewe kwa dhati yake hauhimili ubeberu na hauna madhara makubwa. Nadharia hii kwa kweli, hairidhishi hata kidogo.

Kutokana na maoni yaliyokwisha tolewa inaonekana kwamba ingawa nadharia za kisikolojia zina ukweli wa namna fulani kuhusu kugawanywa kwa bara hili hazielezei kwa kuridhisha sababu za kugawanywa kwake katika kipindi kulimotokea. Hata hivyo zinagusia kwanini kuliwezekana na hata kuaminika kuwa ilikuwa lazima kutokee kwa namna na wakati huo.

Nadharia za Kidiplomasia

Hizi ni nadharia zilizokitwa kwenye siasa tupu na ndizo ambazo zinapendelewa sana katika kuelezea mgawanyo. Lakini kwa namna fulani pia, nadharia hizi zinaegemeza kwa uthabiti zile nadharia za kisaikolojia. Hizo zaweza kugawanywa katika mafungu matatu, yaani *Sifa ya Kitaifa, Urari wa nguvu na mkakati wa kiulimwengu*

*Sifa ya Kitaifa:*

Mtetezi mkuu wa nadharia hii ni Carlton Hayes. Katika aya mojawapo ya kujua katika maandishi yake anasema:

> Ufaransa ilitafuta kufidia ng'ambo kile ilichopoteza Ulaya. Uingereza ilipotengwa na Ulaya ilipanua na kuitukuza himaya yake. Urusi iliposimamishwa katika maeneo ya Balkani iligeukia tena Asia. Vivyo hivyo mataifa ya Ujerumani na Italia yalitaka kuonyesha ulimwengu kuwa sifa walizozipata kwa mabavu huko Ulaya zilikuwa na haki ya kuziimarisha kwa unyonyaji wa kibeberu kwingineko".

Haya anahitimisha basi kuwa "ubeberu mpya kimsingi ulikuwa suala la kitaifa" na siyo suwala la kiuchumi na kwamba mabeberu wapya walikuwa wakitafuta sifa ya kitaifa.

*Urari wa nguvu:*
F.H. Hinsley kwa upande mwingine anasisitiza kuwa matamanio ya Ulaya kuwa na amani na umoja nyumbani kwao ndiyo hasa yaliyoleta mgawanyo. Aonavyo yeye, tarehe muhimu itakayokumbukwa kuashiria kipindi cha mwelekeo wa nje ya Ulaya, yaani kipindi cha Ubeberu, ilikuwa mwaka 1878. Kuanzia mwaka huo, katika mkutano wa Berlin mashindano ya Urusi na Uingereza huko Balkani na katika Himaya ya Uturuki yaliyaingiza mataifa ya Ulaya katika nusura ya vita. Wanasiasa mashuhuri wa Ulaya waliweza kukwepa msukosuko huu wa siasa za kimamlaka na kujirudi. Kuanzia wakati huo mpaka katika msukosuko wa Bosnia mnamo mwaka 1908 siasa za kimamlaka ziliondoshwa Ulaya na kupelekwa Afrika na Asia. Maslahi yao katika Afrika yalipotishia kuharibu amani Ulaya mataifa ya Ulaya hayakuwa na la kufanya bali kuigawanya Afrika ili kulinda urari wa kidiplomasia uliokwishakuwepo kuanzia miaka ya 1880.

*Mikakati ya Kiulimwengu:*
Kuna na wengine wanaoshikilia ya kuwa matamanio ya wazungu kwa Afrika na ambayo yalileta mnyang'anyiro yalisababishwa na mkakati wa kiulimwengu na siyo uchumi. Watetezi wa nadharia hii, Ronald Robinson na John Gallagher, ambao wanasisitiza umuhimu wa Afrika katika mawasiliano ya Uingereza na India, wanafikiri kwamba mgawanyo ulitoka kwa sababu vyama vichanga vya kuanzisha

utaifa huko Afrika vilitishia matakwa ya mataifa ya Ulaya *kimkakati.* "Mapambano" haya ya "kimaendeleo na ya kimawazo" yaliwalazimisha wanasiasa maarufu wa Ulaya, ambao hadi wakati huo walikuwa wametosheka kuishikilia Afrika kwa mbali, kuigawa na kuitamalaki. Kwa hiyo waonavyo wao, Afrika ilikaliwa siyo kwa sababu ilikuwa na chochote cha kutoa kwa watu wa Ulaya, kwani ilikuwa hohe hahe kiuchumi, bali kwa vile ilitishia matakwa ya mataifa ya Ulaya penginepo.

Ijapokuwa nyingi ya nadharia hizi za kidiplomasia zinashawishi kukubaliana nazo, hazipingi zile za kiuchumi na za kisaikolojia na kwa kweli zinakamilishana. Kwa mfano, Hayes alifanya uchunguzi na kuandika kwa kinaganaga juu ya vita vya mapato ya kodi vilivyotokea katika mataifa ya Ulaya wakati huo muhimu wa mgawanyo. Anakubali mwenyewe ya kuwa "kwa kweli kilichoanzisha msukumo wa kiuchumi" kuingia "Bara la Giza" na "visiwa vya Pasifiki" "vilivyounguzwa kwa jua", siyo uzalishaji wa ziada wa bidhaa za viwanda bali ukosekanaji wa *malighafi* na kwa hiyo ili knzuia nchi nyingi ulimwengu zisihodhiwe na Ufaransa, Ujerumani, Italia wala dola nyingine kuu, Uingereza iliamua kujinyakulia kwa nguvu sehemu kubwa ya ulimwenguni na kuiingiza katika himaya yake ya biashara huru. Kwa maneno mengine ufanyaji Biashara Mpya, baada ya kuanzishwsa, ulileta mashindano ya kibeberu. Ajabu ni kwamba katika kurasa zinazofuata Hayes anazikanusha sababu za kiuchumi za Ubeberu mpya! Kwa kweli wasomi wengi hawaridhiki na nadharia ya mkakati wa kiulimwengu lakini kwa wanahistoria wasio wataalamu wa mambo ya Afrika na kwa wasomi wa kawaida, nadharia hii inavutia sana. Hata hivyo tunaelewa fika kuwa *nadharia* hiyo ni *nzuri* mno na yenye mashaka mno kuweza kukubaliwa. Imejaribiwa katika sehemu za Afrika ya Magharibi ya Kati, ya Kusini na ya Mashariki na kuonekana kuwa na upungufu. Pia imeonyeshwa kuwa kuwapo kwa Waingereza huko Misri na Afrika ya Kaskazini hakukuhusiana kamwe na mkakati wake wa Ubeberu wake huko India.

## Nadharia ya Maelezo ya Kiafrika

Kuna maelezo mengine pia yanayoanza kupata mashiko hasa baada ya machapisho ya Dike na ya Hopkins ya hivi karibuni. Maelezo hayo yanaangalia matukio ya mgawanyo katika mtazamo wa Kiafrika. Hapa inafaa kuyakariri maoni ya Hopkins:

> "Kwa upande mmoja inawezekana kukubali kuwa kulikuwa na maeneo ambamo mabadiliko kutoka katika biashara ya utumwa yalifanyika vizuri, kipato kikaendelea kuwapo na tofauti za ndani za kisiasa zikapata kuzuiliwa. Kwa maeneo kama haya mgawanyo unawseza kuelezwa kwa kusisitiza matukio kutoka nje kama vile mahitajio ya kibiashara na mashindano ya Waingereza na Wafaransa. Kwa upande mwingine inawezekana kabisa kuyapata maeneo ambamo watawala wa jadi walichukua mielekeo ya kipingamaendeleo, kipato kikatafutwa kwa nguvu na mapambano ya ndani kisiasa yakawa mengi. Kwa maeneo kama haya, Ubeberu uliweza kuingia kwa sababu za udhaifu wa ndani wa mipaka ya Afrika. Hata hivyo, hatutaweza kuzitupilia mbali sababu za matukio ya nje ya Afrika".

Mtetezi mkuu wa dhana hizi wa hivi karibuni ni G.N. Uzoigwe ambaye anakubaliana na maoni mengi ya wafuasi wa shule hii ya mawazo. Yeye anakubaliana nao kwa kuelezea Mgawanyo kama tukio lililosababishwa na mambo ya ndani ya Afrika na Ulaya na kwa hiyo kwake yeye nadharia ya mwelekeo wa Kiafrika ni nyongeza ya nadharia za Kizungu ambazo zimeshajadiliwa. Kwake yeye, Mgawanyo na kutamalakiwa kwa Afrika vimetokana na kugugunwa kwa Afrika na Mataifa ya Ulaya, ambako kulianza siku nyingi kabla ya karne ya 19. Uzoigwe anakubali kuwa msukumo wa kiuchumi ulisababisha mguguno huo, ulibadilika katika miaka 25 ya mwisho ya karne ya 19, badiliko ambalo lilisababishwa na kuinukia kwa biashara halali badala ya biashara ya utumwa, ambako pia kulileta kupungua kwa biashara ya kuuza na kununua bidhaa za nje katika kipindi hicho. Mabadiliko hayo ya kiuchumi katika Afrika na upinzani wa Waafrika dhidi ya maongezeko ya athari za wazungu vilisababisha kutamalakiwa kwa nguvu za kijeshi. Inaelekea kuwa nadharia hii ya “Maelezo ya Kiafrika” inaelezea mgawanyo vizuri zaidi ikizingatia ukweli na uhalisia wa kihistoria kuliko nadharia zote za “Maelezo ya Kizungu”.

Mwanzo wa Mnyang’anyiro

Hadi kufikia robo ya tatu ya karne ya 19 nchi za Ufaransa, Uingereza, Ureno na Ujerumani zilikuwa zimefanya biashara na kuanzisha mahusiano na maeneo mengi ya Afrika. Ijapokuwa hivyo, kisiasa nchi hizo hazikuwa zimeimiliki Afrika kwa kiwango chochote kikubwa. Ujerumani na hasa Uingereza zilikuwa na uwezo wa kuiathiri Afrika kwa kiwango zilivyotaka na hakuna kiongozi mwenye busara ambaye angetaka kukaribisha matatizo yasiyotazamiwa wakati ambapo angeweza kupata faida zile zile kutoka nchi hiyo bila kuitawala rasmi.

Lakini mwelekeo huu ulianza kubadilika baada ya matukio matatu makuu yaliyojitokeza kati ya 1876 na 1880. Tukio la kwanza lilikuwa ni yale matamanio makubwa ambayo Duke wa Brabant, aliyetawazwa kama mfalme wa Ubelgiji kikatiba (Leopold I) 1865, aliyokuwa nayo katika Afrika. Matamanio yake haya yalidhihirishwa na Mkutano Mkuu wa kijiografia wa Brussells, aliouitisha mnamo mwaka 1876, na ambao kutokana nao chama cha kimataifa cha Afrika kilianzishwa na kumwajiri H.M. Stanley mwaka 1879 kuivumbua Congo kwa niaba ya chama hicho.

Tukio la pili lilikuwa mfululizo wa shughuli za Ureno kuanzia 1876 na kuendelea. Wareno walikasirishwa walipojua kuwa walikaribishwa katika mkutano huo kama kijalizo tu na hivyo Ureno ikaamua kufanya safari nyingi nyingi na kutuma wavumbuzi kuanzia mwaka huo. Hata ilipofikia 1880 walikwishashika maeneo mengi ya Afrika kwa ajili ya manufaa yao Kufuatana na maomi ya Wareno na ya Mfale Leopold, mnyang’anyiro ulikwishaanza tangu 1876.

Tukio la tatu na la mwishao ambalo lilisababisha mgawanyo kuendelea kwa kasi, lilikuwa ni mwelekeo wa kupanuka ulioshamiri katika sera ya kikoloni ya Ufaransa kati ya 1879 na 1880.Mwelekeo huu unaweza kuonekana wazi mosi, katika

kushiriki kwao kuitawala Misri pamoja na Uingereza mnamo 1879; pili, katika mwanzo wa kuelekea mashariki wakiwa Sudani ya Magharibi mnamo 1876: tatu, walipomtuma Savorgnan wa Brazza kwenda Congo na kuandikiana mikataba kati yake na Chifu Makoko wa Bateke, na mwisho walipofufua ukoloni wao huko Tunisia na Malagasi.

Matukio haya ya nchi hizo kubwa kati ya 1876 na 1880 yalionyesha wazi kuwa zilikuwa zimeamua kupanua ukoloni na kuitawala Afrika. Jambo hili lilizifanya nchi za Uingereza na Ujerumani zitupilie mbali mtindo wao wa kuishikilia nchi kwa mbali, wakachukua mfumo rasmi ulioziwezesha kuyatawala maeneo ya kusini, Mashariki na Magharibi mwa Afrika kuanzia mwisho wa 1883 na kuendelea.

Inadhihirishwa na maelezo yaliyotangulia kuwa kilichosababisha mnyang'anyiro sio kukaliwa kwa Misri na Uingereza mnamo 1882, kama wanavyodahili Robinson na Gallagher, bali ni yale matukio ya 1876 hadi 1880 katika maeneo mbalimbali ya Afrika.

## Mkutano wa Berlin 1884 – 1885

Wazo la kuwa na mkutano wa kimataifa wa kukubaliana juu ya ugomvi wa mipaka ya maeneo ya nchi uliotokana na shughuli za wazungu huko Kongo, lililetwa na Ureno kwa kuhofia kufukuzwa Afrika. Wazo hilo lilifuatiliwa baadaye na Bismarck ambaye baada ya kushauriana na himaya nyingine za Ulaya alishawishiwa kulileta katika majadiliano. Mkutano ulifanywa huko Berlin kati ya tarehe 15 Novemba 1884 na 26 Februari 1885. Habari zilipotoka kutangaza kufanyika kwa mkutano huo, zilizidisha harakati za mnyang'anyiro.

Ilivyokuja kudhihirika ni kwamba hapo awali haikuwa nia ya mkutano huo kuigawa Afrika, lakini baadaye uliishilia kufanya hivyo; mkutano ukapitisha maazimio yaliyoruhusu utumiaji huru wa mito ya Niger, Benue na vijito vyake; na kuweka "sheria za kufuatwa siku za usoni kuhusu ukaliaji wa nchi za pwani ya Afrika". Kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha sheria ya Berlin, ambayo ilitiwa saini na wahudhuriaji wa mkutano huo, "Nchi yoyote ya Ulaya iliyomiliki nchi katika pwani ya Afrika au iliyotwaa eneo na kulimiliki, ilitakiwa itoe taarifa kwa nchi zilizotia saini mkataba huo ili madai hayo yathibitishwe". Hii ndiyo kanuni ya *"Maeneo yaliyomilikiwa"*. Kifungu cha 35 kilisema kuwa mtawala wa eneo lolote hilo la pwani alitakiwa pia aonyeshe bayana kuwa alikuwa na 'kulinda haki za uhuru wa biashara na wa usafiri kufuatana na masharti yaliyokubaliwa". Hii ndiyo kanuni ya *"Utwaaji nchi kikamilifu"* ambayo iliufanya ushindani wa kutamalaki Afrika uwe shughuli mbaya mno. Ingefaa isisitizwe hapa ya kuwa mkutano huu haukuanza mgawanyo wa Afrika, bali uliweka sheria chache za kusimamia jambo lililokwishaanza zamani.

## *Uandikianaji wa Mikataba 1885 – 1902*

Kabla ya sheria ya Berlin, Nchi za Ulaya zilikuwa zimejitwalia "maeneo ya kumiliki" huko Afrika kwa njia mbalimbali kama vile kwa kuzikalia, kuzivumbua, kwa kuanzisha vituo vya biashara, kwa kuweka vituo vya wamisionari, kwa kukalia maeneo muhimu na kwa kuandikiana mikataba na watawala wa Kiafrika. Baada ya mkutano wa Berlin, kumiliki nchi kwa njia ya mikataba ikawa ndiyo njia muhimu kuliko zote ya kuhalalisha mgawanyo uliokwishafanywa kwenye ramani karatasini. Mikataba hiyo ilikuwa ya aina mbili, ile iliyotiwa saini baina ya Waafrika na Wazungu, na ile ya makubaliano ya nchi mbili za Kizungu. Mikataba baina ya Waafrika na Wazungu nayo ilikuwa ya aina mbili. Kwanza kulikuwako na mikataba ya biashara ya utumwa na ya bidhaa ambayo ilisababisha misuguano iliyovuta uingiliaji kisiasa wa nchi za kizungu katika mambo ya Waafrika. Pili, kulikuwa na *mikataba ya kisiasa* ambayo kwayo ilidaiwa kwamba eti watawala wa Kiafrika waliachia Wazungu mamlaka yao ya kutawala ili wapate ulinzi kutoka kwa mataifa ya Ulaya au waliacha kuandikiana mikataba na nchi nyingine za Kizungu. Kielelezo bora cha mikataba ya namna hiyo ni ile iliyofanywa kati ya Kampuni ya *"Imperial British East Africa Company"* (Himaya ya Uingereza ya Afrika ya Mashariki) na Kabaka Mwanga wa Buganda mnamo Desemba 1890 na tena mnamo Machi 1892.

Mikataba ya Mgawanyo kati ya nchi za Ulaya:

Wakati Mikataba kati ya Waafrika na Wazungu iliweka wazi maeneo ambayo yangekaliwa na wazungu mikataba baina ya Wazungu kwa Wazungu ilihitimisha mgawanyo wa Afrika uliokwishafanywa kwenye ramani hadi kufikia mwisho wa karne. Kwa mfano, mkataba wa mipaka uliotiwa saini baina ya Wajerumani na Waingereza mnamo Novemba mosi 1886 una umuhimu wa kipekee. Mkataba huo uliiweka Zanzibar na maeneo yaliyotawaliwa na Sultani chini ya Mamlaka ya Uingereza na kuthibitisha mamlaka ya kisiasa ya Ujerumani juu ya Afrika ya Mashariki, hivyo ukaondoa hodhi ya Uingereza katika eneo hilo.

Mikataba ya 1890 na 1893 baina ya Uingereza na Ujerumani na ule wa 1891 kati ya Italia na Uingereza, kwa pamoja ililitambua eneo la Upper Nile kama eneo lililokuwa chini ya utawala wa Waingereza. Huko Kusini ya Afrika, mikataba ya 1886 kati ya Ufaransa na Ureno, mwaka 1886 kati ya Ureno na Ujerumani, na 1891 kati ya Uingereza na Ureno iliitambua himaya ya Ureno huko Angola na Msumbiji na kuiachia Uingereza maeneo ya Afrika ya kati. Mkataba wa 1894 wa Eneo Huru la Kongo ya Waingereza uliliwekea mipaka eneo hilo. Huko Afrika ya Magharibi mipango inayokumbukwa zaidi ni Makubaliano ya Say-Baruwa (ya 1890) na Mkataba wa Niger (wa 1898) ambayo ilimalizia mgawanyo wa eneo hilo baina ya Uingereza na Ufaransa. Mwishowe Mkataba wa Uingereza na Ufaransa wa 21 Machi 1899 ulihitimisha suala la Misri na papo hapo mkataba wa Amani ya Vereeniging (wa 1902)

uliomaliza vita baina ya Waingereza na Makaburu ulithibitisha, (ijapokuwa kwa muda tu), utawala wa Waingereza huko Afrika ya kusini.

## *Kutamalaki kwa Kijeshi 1885-1902*

Mgawanyo wa Afrika katika ramani ulifuatiwa na kutamalaki kwa kijeshi kufuatana na kanuni ya *utwaaji nchi kikamilifu*. Haijulikani kwa nini hasa, lakini Wafaransa ndio walioutumia zaidi mfumo huu wa kutamalaki kwa kutumia majeshi. Wakianzia Upper Niger na kuelekea Lower Niger, Wafaransa walimshinda kwa urahisi Damel wa Cayor, Lat Dior, ambaye alipigana hadi kufa kwake katika 1886; mwaka wa 1887 walimpiga na kumshinda Mamadou Lamine katika vita vya Touba-Kouta, na kwa hivyo wakauangamiza utawala wa Soninke aliouanzisha huko Senegambia. Wafaransa walifanikiwa kuyavunja mapingamizi maarufu ya Mwinyi Samori Ture walipomkamata mnamo mwaka 1898 na kumpeleka kifungoni huko Gabon mwaka 1900. Mafanikio mengine yalikuwa yale ya Koundi (1889), Segu (1890) na Youri (1891) ambayo kwayo Meja Louis Archinard aliuangamiza utawala wa Segu-Tukulor ambapo katika vita vya Kusseri katika mwaka 1900, Utawala wa Rabih ulivunjwa kabisa, hata ukasababisha kutamalakiwa kwa Chad. Wafaransa wakatamalaki Pwani ya Ivory Coast, na eneo ambalo lilijulikana kama French Guinea ambako walianzisha makoloni mnamo mwaka wa 1893. Kati ya 1890 na 1894 Ufalme wa Dahomey ulishindwa na kutamalakiwa. Hadi kufikia mwisho wa karne ya 19 Wafaransa walishakamilisha ushindi wao huko Gabon, wakajiimarisha huko Afrika ya Kaskazini na kutamalaki Malagasi baada ya kuwapeleka Malkia Ranavalona III na Waziri Mkuu Rainiariwony kizuizini huko Algeria.

Ubeberu wa Kiingereza nao ulikuwa mkubwa na wa umwagaji damu. Waafrika nao waliamua kupinga kwa nguvu zao zote na kwa muda mrefu, kama itakavyodhihirishwa katika sura zitakazofuata. Waingereza wakiitumia Gold Coast (siku hizi Ghana) waliwazuia kabisa Wafaransa kueneza utawala wao huko Niger na katika nchi ya Asante. Msafara wa Kivita wa mwisho wa Kumasi (1900) ulifuatiliwa na utekwaji wa Asante katika mwaka 1901 na Mfalme Nana Prempeh akapelekwa kizuizini huko Shelisheli. Maeneo ya Kaskazini ya Asante nayo yalitekwa mwaka wa 1901 baada ya kukaliwa kwa kipindi kati ya mwaka 1896 hadi 1898. Kutoka katika koloni lake la Lagos, Uingereza iliweza kushambulia na kutamalaki Nigeria. Kufikia mwaka wa 1893, eneo la nchi ya Wayoruba lilikwishatangazwa kuwa nchi lindwa na nchi ya Itsekiri nayo ilichukuliwa mnamo 1894. Kwa kutumia visingizio mbalimbali nchi za Brass na Benin zilitamalakiwa kufikia mwisho wa karne ya 19. Hivyo kufikia mwaka 1900 nguvu ya mamlaka ya Uingereza kusini mwa Nigeria karibu ilikwisha shamiri. Hata hivyo kukaliwa halisi kwa nchi ya Igbo na maeneo mengine ya bara ya mashariki hakukuwezekana hadi miongo miwili ya kwanza ya karne ya 20. Huko kaskazini, Waingereza waliweza kujipatia ushindi kutoka Nupe ambapo mnamo mwaka wa 1895, Kampuni ya Kifalme ya George Goldie iliweza kutawala eneo hilo

kutoka Lokoja hadi pwani. Iloria ilitawaliwa mwaka wa 1897 na kuanzishwa kwa Jeshi la Mpaka wa Afrika ya Magharibi mnamo 1898 kulimwezesha Lugard kuushinda Usultani wa Sokoto mwaka 1902.

Huko Afrika ya Kaskazini, Uingereza ambayo ilikuwa tayari inaikalia Misri, ilingoja hadi mwaka wa 1896 wakati ambapo amri ya kutamalaki tena Sudan kijeshi ilithibitishwa. Ushindi ulipatikana mwaka wa vita vya kishenzi na vya umwagaji damu usiokuwa wa lazima. Zaidi ya Wasudani 20,000, pamoja na Kiongozi wao, Khalifa Abdallah, walikufa katika vita hivyo.

Kufuatia kutangazwa rasmi kwa Zanzibar kama nchi-lindwa ya Uingereza mnamo 1894 na sehemu nyingine za Uganda zilitamalakiwa mnamo 1899, mwaka ambao mfalme Kabarega na Mfalme Mwanga walikamatwa na kupelekwa kizuizini huko Shelisheli. Lakini huko Kenya mambo hayakuwa rahisi hivyo kwani iliwachukua Waingereza miaka kumi kabla hawajaimarisha utawala wao kwa Wanandi.

Huko Afrika ya Kati na ya Kusini Cecil Khodes British South Africa Company (BSA) (Kampui ya Kiingereza ya Afrika ya Kusini (KKAK) iliyomilikiwa na Cecil Rhodes) iliamua kuikalia nchi ya Wamashona bila ruhusa ya Lobengula. Katika mwaka wa 1893 mfalme alilazimika kuukimbia mji wao mkuu; akafariki mwaka 1894 kama mkimbizi huko maporini. Hata hivyo, ufalme wake haukushindwa kabisa hadi mwaka 1896 – 7 wakati maasi ya Wamashona na Wandebele yalipozimwa na kutokea umwagaji damu mkubwa. Ushindi wa Waingereza huko Nothern Rhodesia (sasa Zambia) haukuwa na matata sana nao ulipatikana mwaka 1901.

Nchi nyingine za Kizungu nazo ziliuona utwaaji nchi kikamilifu kuwa jambo gumu. Kwa mfano, Wajerumani waliweza kuuimarisha utawala wao huko Afrika ya Kusini-Magharibi kufikia mwisho wa karne ya 19 kwa kuwa kwa zaidi ya karne moja uadui baina ya Wanama na Waherero uliwazuia kujiunga pamoja dhidi ya ukoloni. Katika nchi ya Togo, Wajerumani waliungana na falme ndogondogo za Kotokoli na Chakosi kuharakisha kuushinda ukinzani wa Wakonkomba (mnamo 1897 – 8) na Wakabre (mwaka 1890). Huko Cameroon, Meja Hans Dominik, kamanda wa kijerumani, alipata matatizo makubwa huko kaskazini lakini kufikia 1902 alikwishaweza kuwashinda Wafula na kuteka miji yao. Vita vya Wadachi kutamalaki German East Afrika (Africa Mashariki) ndivyo vilivyokuwa virefu kuliko vyote katika historia ya utwaaji nchi kikamilifu. Hivi vilidumu kuanzia 1888 hadi 1907.

Ureno nayo ilianza utwaaji wa maeneo ya Afrika kwa vita mnamo 1880 lakini haikukamilisha utwaaji huo hadi karne ya ishirini. Ijapokuwa walikuwa maskini Wareno walijiona sana na ijapokuwa kazi hii ilikuwa ngumu waliweza hata hivyo kuimarisha utawala wao huko Msumbiji, Angola, na Guinea (sasa Guinea & Bisau). Dola Huru ya Kongo nayo ilipatwa na matatizo makubwa kabla ya kufanikiwa kujiimarisha kijeshi katika maeneo yake yenyewe.

Italia ndiyo iliyofanya vibaya zaidi katika vita vyake vya utwaaji nchi kikamilifu katika Afrika. Mnamo mwaka 1883 Italia iliikalia Eritrea. Himaya ya Omani ilipogawanywa 1886, Italia ilijipatia pia sehemu ya Somalia. Lakini jaribio lao

la kuikalia Ethiopia liliishia katika kushindwa kwao kwa aibu na fedheha katika mapigano ya Adowa (ya 1896). Hata hivyo Italia iliweza kushikilia sehemu za Eritrea na Somalia. Huko Afrika ya Kaskazini, Italia haikufanikiwa chochote hadi 1911 ilipoweza kuyakalia maeneo ya pwani ya Sirenaika na Tripolitania (sasa Jamhuri ya Kisoshalisti ya Waarabu wa Libya), Morocco iliweza kuuhifadhi uhuru wake hadi Wahispania na Wafaransa walipoukomesha mnamo mwaka wa 1912. Hadi kufikia 1912 ni Ethiopia na Liberia tu zilizobakia huru, ijapokuwa kwa jina tu.

## *Kwa nini Mataifa ya Kizungu yaliweza Kuitamalaki Afrika?**Kwa nini Mataifa ya Kizungu yaliweza Kuitamalaki Afrika?*

Mataifa ya Kizungu yaliweza kuitamalaki Afrika kwa urahisi mno kwa sababu kwa vyovyote vile bahati ilikuwa upande wao. Kwanza kabisa, kufikia mwaka wa 1880, Wazungu walikwishajua mambo mengi sana juu ya Afrika kwa sababu walikwishajulishwa mambo hayo na wavumbuzi na Wamisionari. Waliijua Pwani na bara ya Afrika, mandhari yake, jiografia yake – milima na mabonde, uchumi wake, mali yake, walijua udhaifu wa dola za Kiafrika na jamii zake, kuliko Waafrika walivyoijua Ulaya.


Pili, kutokana na mabadiliko ya kimapinduzi katika teknolojia ya tiba na madawa, hasa hasa kutokana na kugunduliwa kwa njia ya kuzuia malaria kwa kutumia kwinini, Wazungu hawakuiogopa tena Afrika kama walivyokuwa wakiihofia kabla ya kipindi cha kati ya karne ya 19.

Tatu, kutokana na kukosekana kwa urari wa biashara kati ya Afrika na Ulaya kufikia miaka ya 1870 na hata kwa baadaye, pamoja na hatua Ulaya ilizopiga katika mapinduzi ya viwanda, Wazungu walikuwa na mali na fedha nyingi za kutumia kuliko Waafrika. Hivyo wakati ambapo Wazungu waliweza kutumia mamilioni ya fedha kwa kupigana ng'ambo, Dola za Kiafrika hazikuweza hata kujilinda na shambulio lililojulikana awali.

Nne, kufuatana na mawazo ya J. Holland Rose, wakati katika Ulaya kipindi cha 1877 – 8, baada ya vita vya Warusi na Waturuki, kilikuwa "kipindi cha msawazisho wa kisiasa, kilichoruhusu amani na utulivu" katika Afrika kipindi hicho hicho kilikuwa cha mashindano, ukinzani na makabiliano ya ndani na nje ya dola – Wamande wakigombana na Watukulor, Waasante na Wafante, Waganda na Wanyoro n.k. Hivyo basi, wakati Ulaya ilikuwa na nafasi ya kushughulikia nia yao ya kupata ushindi wa kijeshi katika shughuli zao za kibeberu bila ya kuwa na matatizo nyumbani, dola za Kiafrika zilikuwa zimegawanyika katika mahitajio yao. Tena basi siyo kwamba Ulaya ilifaidi kutokana na amani nyumbani tu, bali nchi za kizungu zilizojishughulisha na ugawaji wa bara hili zilionyesha mshikamano thabiti ambao kwanza uliwaondoshea vita baina yao na pili uliwazuia watawala wa Kiafrika na jamii zao kuwaingilia kwa hadaa. Hivyo basi tawala za Kiafrika zilishindwa kwa sababu hazikuonyesha mshikamano, umoja wala ushirikiano.

Silaha zilizotumiwa na Waafrika na wapinzani wao wa kizungu wakati wa vita kati ya 1880 na 1935.

**2.1** Vita vya Asante vya 1896 (Ghana): mashoka na visu vya kutupa



**2.2** Wapiganaji wa Kavirondo (Kenya): wakishika mikuki na ngao







**2.3**

Oba (Mfalme) wa Kiyomba (Nigeria) wa karne ya kumi na tisa akiwa na maamiri-jeshi wake walioshika bunduki kongwe za aina ya 'Dane'

**2.4**

Askari wa King's African Rifles wakiwa na bunduki ya 'Maxim'





**2.5** *Bunduki ya 'Gatling'*

**2.6** *Ndege zilizotumika katika vita vya kikoloni vya 1920*




Sababu ya mwisho na ambayo ni wazi ilikuwa muhimu zaidi ilikuwa kwamba Ulaya ilikuwa na maendeleo ya hali ya juu sana ya mbinu na zana za kivita na za kiufundi kuishinda Afrika. Wakati ambapo Ulaya ilikuwa inatumia majeshi yaliyoiva sawasawa kinidhamu, nchi chache mno za Kiafrika zilikuwa na jeshi kamili na nchi chache zaidi zilikuwa na majeshi ya kulipwa. Dola nyingi za Kiafrika wakati huo zilikusanya watu wakati tu wa tukio fulani kwa ajili ya ulinzi au kupigana. Zaidi ya hayo, kama inavyodaiwa na Isaaeman na Vansina, Wazungu waliweza pia kuwategemea askari wa kulipwa wa Kiafrika, jambo ambalo liliwafanya wawe na askari wengi zaidi. Tena la maana zaidi ni kuwa fuatana na Mkataba wa Brussells wa 1890, nchi za kibeberu zilikubaliana zisiwauzie Waafrika zana za Vita. Hii ilimaanisha kuwa majeshi mengi ya Kiafrika yalikuwa na zana za jadi kama vile pinde, mishale, mikuki n.k. au walikuwa na bunduki za mitindo ya zamani kabisa zisizokuwa na risasi, nyingi ya hizo zikiwa aina ya magobori. Tena nchi za Kiafrika hazikuwa hata na mizinga wala majeshi ya majini. Majeshi ya Kizungu yalikuwa na mizinga ya kisasa kabisa na bunduki kama "rifle" na zile za aina ya Galting na Maxim. Pia walitumia mizinga ya manowari za jeshi la majini. Laroui anatueleza ya kuwa katika vita vya mwishomwisho, hata magari na eropleni yalitumika, (taz. picha 2.6).

Kutokana na mafao ya kiuchumi, kisiasa na zaidi ya yote yale ya kijeshi na ya kiteknolojia waliyokuwa nayo wazungu ukilinganisha na wenzao Waafrika, kwa kweli mashindano hayakuwa sawa hata kidogo na haishangazi kamwe kuona kwamba Wazungu waliwashinda Waafrika kwa urahisi mno. Kwa kweli kwa Wazungu, kipindi cha vita hivi hakingeweza kuwa bora zaidi kwao na kwa Waafrika kilikuwa kibaya mno pia.

## Ramani ya Afrika baada ya Mgawanyo na kukaliwa

Ramani mpya ya tawala za Afrika iliyochorwa baada ya miaka kumi hivi ya utengaji mipaka na kukaliwa kijeshi ilikuwa tofauti sana na ile ya 1879 (taz. Mchoro 2.1). Nchi za Ulaya ziliigawa bara la Afrika katika sehemu arobaini za tawala. Baadhi ya wasomi hawaikubali mipaka mipya wakidai kuwa imefikiwa bila mpango na bila kutilia maanani mataifa ya Afrika kabla ya majilio ya Wazungu. Wengine, kama vile Joseph Anene na Saadia Touval wanaiona mipaka hiyo mipya kuwa nafuu ya ile ya 1879.

Kuna ukweli katika maoni ya makundi yote mawili. Asilimia 30 ya urefu wote wa mipaka, imechorwa kama mistari iliyonyooka, nayo mara nyingi hupita kati ya makundi ya lugha moja au jamii moja. Kwa upande mwingine mipaka iliyosalia inafuata mipaka ya asili, kwa hiyo haiwezi kufikiriwa eti ni ya ovyo au isiyofaa kama vile wapinzani wao wangependa tuamini. Na kwa kweli, katika kipindi hicho, tawala za Kiafrika zilizokuwa zinainukia wakati huo, kutokana na mapambano kama yale ya Oyo-Dahomey, au vita vya jihadi vya Fulani au mapambano ya Mfecane ya Afrika ya kusini – zote hizo hazikuwa na mipaka thabiti na kwa hivyo hakuna shaka ya kuwa




**2.7** Afrika Kwenye 1914

mgawanyo uliimarisha mipaka hiyo. Kwa hiyo inaweza kukubaliwa ya kuwa ijapokuwa ramani ya Afrika ya 1914 (taz. Mchoro 2.7) inakanganya ukiilinganisha na ile ya 1879, ukweli ni kuwa uchoraji wake ulikuwa bora sana kwani ulisaidiwa na maendeleo yaliyotokana na taaluma ya Kartografia, yaani uchoraji ramani.

Hadi kafikia 1902, Afrika ilikwishatamalakiwa; nayo shughuli yenyewe ilikuwa mbaya na ya umwagaji damu. Uwezo wa Bunduki ya Maxim katika kuteketeza adui na maendeleo ya hali ya juu ya teknolojia ya Kizungu iliwatia unyonge Wafaransa. Hata hivyo, ijapokuwa Ulaya iliishinda Afrika kwa urahisi, kukaliwa na kutawaliwa kwake na wazungu hakukuwa rahisi. Sura, zifuatazo zitaonyesha haya.

# 3

# Juhudi na Ukinzani wa Waafrika Dhidi ya Kugawanywa na Kutamalakiwa

Utaratibu wa Wazungu kutamalaki na kumiliki Afrika ya tropiki kati ya mwaka 1880 na 1900 usingeweza kuepukwa kwa namna yeyote ile lakini ungeweza pia kupingwa sana. Haungeweza kuzuiwa kwa sababu kama ilivyoelezwa hapo awali kwa mara ya kwanza, Wazungu walisaidiwa kwa kisasi kikubwa na silaha, na kwa mara ya kwanza, gari la moshi, simu na meli viliwawezesha kutatua tatizo la mawasiliano na Afrika na baina ya Afrika na Ulaya. Uliweza kupingwa kwa sababu ya ukubwa wa Afrika; kwa sababu ya nguvu ya watu wake; na kwa kuwa Ulaya haikuwatoa watu wengi wala kutumia teknolojia nyingi. Hata hivyo hatimaye "ilikuwa lazima Wazungu washinde" na baada ya kushinda kwao walirekebisha mambo yaliyowaletea matatizo. Vitabu viliandikwa juu ya jambo lililoitwa "usuluhishi", ikatolewa picha kuwa Waafrika wengi walikubali kwa shukrani kile kilichoitwa "Pax Colonica"; na vitendo vya ukinzani wa Kiafrika vikapuuzwa. Lakini ushindi wa Wazungu haumaanishi kwamba ukinzani wa Kiafrika ulikuwa siyo muhimu kwa wakati huo au hauhitaji kuchunguzwa sasa. Na kwa hakika katika miaka ishirini iliyopita, suala hili limechunguzwa sana.

Sehemu kubwa ya uchunguzi wa miongo miwili iliyopita ilikuwa yenye uchunguzi makini, wenye kina, wakitaalamu na ambao haukukwepa utata na ukinzani mwingi. Sehemu ya uchunguzi umekitwa au umetumiwa kuelezea dhana tatu zilizochukuliwa kuwa sahihi na ambazo bado kimsingi ni za kweli ingawa kila moja imebadilishwa na utafiti na mchanganuo wa hivi karibuni. Imedahiliwa kwamba suala la akinzani wa Kiafrika ni muhimu kwa sababu limethibitisha kwamba Waafrika hawakukubali kwa hiari kugawanywa na kutekwa na Wazungu. Pili, imedahiliwa kwamba ukinzani huo haukuwa wa kukata tamaa wala wa kipumbavu, lakini mara nyingi ulikuwa ukiongozwa na itikadi za busara na za mabadiliko. Tatu, imedahiliwa kwamba ukinzani huo haukuwa wa bure; kwamba ulikuwa na matokeo ya maana kwa wakati huo na bado yana manufaa hadi leo kwa kiasi fulani. Hoja hizo tatu zinastahili kurejewa tena hapa pamoja na mabadiliko yaliyopendekezwa kwao.

## *Ujumla wa Ukinzani*

Katika mwaka 1965, mwanahistoria wa Kirusi, A.B. Davidson aliwataka wanazuoni kukanusha maoni ya kizungu ya tangu zamani kwamba Waafrika walichukua "ujio wa

wakoloni kama bahati njema; kama ukombozi kutoka katika vita vya kidugu, kutoka kwenye udhalimu wa mbari za jirani, kutoka kwenye magonjwa ya kuambukiza na njaa zisizokwisha" na kwamba watu ambao hawakuwapinga walisifiwa kama "wapenda amani" na hao ambao waliwapinga, walichukuliwa kama "wenyekiu-ya-damu". Davidson alionyesha kuwa "walinzi" wa utawala wa kikoloni walikataa kuchukulia maasi kama "jambo" la kawaida. Waliyaelezea maasi hayo kama majibu ya "kishenzi na yasiyo ya tafakuri, au kama ghasia za wachache wenye "kiu-ya-damu" na zaidi "walikataa maelezo sahihi ya pekee ya kwamba maasi yalikuwa vita vya haki vya ukombozi na kwamba sababu hiyo ndiyo ilifanya waungwe mkono na idadi kubwa sana ya Waafrika".

Mwisho Davidson alisisitiza kwamba "maasi mengi bado hayajulikani, mara nyingi hatuna maelezo ya yakini kuhusu maasi hayo ambayo yanachukuliwa kama jambo lililokwishathibitishwa!

Tangu Davidson alipoandika kazi ya kufafanua ukinzani imeendelea kwa haraka. Wanahistoria wameanza kuainisha maasi kwa usahihi zaidi, wakitofautisha "uharamia wa kijamii" na "maasi ya wakulima wadogo", na vita vya askari wa msituni na mapigano ya majeshi. Mara nyingi, mambo yaliyofasiriwa na wakoloni kama maasi yameonekana kuwa yalilazimishwa kwa watu kutokana na ujinga na woga wa Wazungu. Katika sehemu nyingi zaidi ukinzani mkubwa na wenye maana umefanywa kufahamika kwa uwazi kabisa kwa mara ya kwanza. Uchunguzi wa kina juu ya maasi mengi muhimu sasa unapatikana na katika baadhi yake, majadiliano makali kuhusu njia bora ya kuyaeleza na kuyafasiri maasi hayo yamekuwa yakifanyika. Kutokana na hayo yote, ni dhahiri kabisa kwamba Davidson alikuwa na haki kwa kufikiri kwamba ukinzani ulikuwa "jambo la kawaida".

Ni dhahiri pia kwamba majaribio ya zamani ya kutofautisha jamii za Kiafrika ambazo kiasili hupenda vita na zile ambazo kiasili hupenda amani si ya muhimu. Uchunguzi umeonyesha kwamba hazikuwepo nchi ambazo eti zilipendelea vita, zenye kupenda kushambulia na kuteka nchi nyingine na zile ambazo eti zilipendelea amani, zile zenye kupenda biashara na kilimo kwani karibu nchi zote zilikuwa na maslahi na imani zao ambazo zilikuwa tayari kuzilinda kwa ukinzani wa silaha kama ilihitajika. Wazo kwamba serikali za Kiafrika za kiwango cha juu tu ndizo zilikinzana na ukoloni ambapo zile za jamii za kiwango cha chini hazikuweza kuutumia wala kukinzana na utawala wa kikoloni pia limekanushwa vilivyo. Yule Marks katika kazi yake juu ya ukinzani wa Kikhoisan huko Afrika Kusini ameonyesha kwamba watu waliogawanyika wanao uwezo wa kupambana na vita vigumu dhidi ya wazungu sawa na wale ambao hawakugawanyika. John Thornton hivi karibuni amelinganisha uwezo wa ukinzani wa jamii zenye dola na ule wa jamii zisizo na dola na kufikia hitimisho kuwa ule wa jamii zisizo na dola ni mkubwa zaidi.

Kwa kifupi, kwa kweli kila aina ya jamii ya Kiafrika ilikuwa na ukinzani na kulikuweko na ukinzani karibu katika kila mahali palipokuwa na wazungu. Tunaweza sasa kukubali kuwa huu ni ukweli ambao hauhitaji maelezo zaidi. Tunachohitaji

kufanya sasa ni kutoka kwenye maainisho kuelekea kwenye fasiri, kutoka katika kuonyesha tu ukinzani uliokuwepo na kufanya tathmini na kueleza viwango vya nguvu zake.

## *Itikadi ya Ukinzani*

Watetezi wa Ukoloni walisisitiza kwamba ukinzani wa silaha ulikuwa sio wa busara na ulikuwa mbaya mno. Walidai kwamba mara nyingi ulitokana na "ushirikina" na kwamba watu ambao walikuwa tayari kuupokea utawala wa kikoloni walirogwa na "waganga wachawi". Wahakiki wa Kizungu wengi wa ukoloni waungao mkono ukinzani wa Waafrika hata hivyo walikubali pia kwamba Waafrika hawakuwa na mambo mengi katika fikra zao za "kijadi" ambayo yaliwasaidia kupata jibu la kufaa kuhusu mashambulio juu ya hali ya maisha yao. Itikadi za maasi zilikuwa zikifikiriwa kama "uchawi wa kukata tamaa", ambayo ilikuwa haina budi kushindwa na ambayo haikuwa imeelekeza mawazo katika wakati ujao. Katika mtazamo huu ukinzani, japo uwe wa kishujaa namna gani ulikuwa na mwisho mbaya sana.

Katika miongo miwili iliyopita au zaidi wanahistoria wa ukinzani wametoa changamoto juu ya fasihi hii. Wamefanya hivyo kwa njia mbili: kwa kuonyesha kwamba ukinzani wa Kiafrika ulikuwa na itikadi yake ya msingi na kwa "kugeuza" itikadi za kidini.

Itikadi kuu ya kilimwengu ambayo imependekezwa ni ile dhana ya "umamlaka". Jacob Ajayi ameandika kwamba

> kipengele muhimu kabisa cha athari ya Kizungu ilikuwa ni kupotewa kwa umamlaka ......... Mara tu watu wanapopoteza umamlaka wao na kukubaliwa na utamaduni. mwingine wanapoteza walau sehemu ndogo ya kujiamini na kujiheshimu kwao, wanapoteza haki ya kujielekeza, uhuru wao wa kuchagua wabadili nini katika utamaduni wao wenyewe au nini waige au watupilie mbali yatokayo katika utamaduni mwingine!

Jambo kama hilo linatiliwa nguvu zaidi na Walter Rodney:

> Anaposema "ushindi wa kipindi kifupi cha ukoloni unatokana hasa na ukweli kwamba Afrika ilipoteza mamlaka. Mamlaka ya kutenda kwa uhuru ni dhamana katika kushiriki ipasavyo na *kwa uaminifu* katika historia. Kutawaliwa ni kuondolewa katika historia ..... kwa ghafla dola za Kiafrika zilipoteza mamlaka yao, uhuru wao na maana yao".

Ni dhahiri kwamba wazo la umamlaka lilijenga itikadi ya ukinzani. Hata hivyo hatuna budi kufanya marekebisho fulani ya maelezo. Watawala siku zote hawakuwa wako wazi wazi kabisa "walinzi wa umamlaka wa watu" Katika karne ya 19 huko magharibi, mashariki na kusini —dola mpya zilikuwa zimejitokeza. Dola za namna hiyo mara nyingi zilipinga kuongezeka moja kwa moja mamlaka ya kizungu lakini ukinzani wao

ulikuwa umekabiliwa na chuki ya wengi wa raia wao. Ndivyo zilivyokuwa dola za Samori Ture, Shehu Ahmadu na "dola ndogo" za bonde la Zambezi.

Dola kama hizi zinaweza kulinganishwa na Serikali thabiti za siku nyingi ambazo watawala wamefikilia "uhalali". Lakini hapo napo ingekuwa kupiga chuku kudhani jamaa zote za zamani zilizokuwa zikitawala zilifurahia imani na kuungwa mkono na watu wengi. Makundi tawala kati ya baadhi ya watu thabiti wa siku nyingi yalitendeza mamlaka yao kwa njia isiyo ya kanuni na matokeo yake yakawa kwamba hayakuweza kutegemea kuungwa mkono na watu wengi katika kupambana na wazungu. Hii inaeleza kwa kiasi fulani sababu ya uhafifu wa ukinzani huko Rhodesia ya Kaskazini ambako machifu wa Kibemba walipambana na kile Henry Meebelo alichokiita "machukio ya watawaliwa dhidi ya tabaka lililotawala" na ambako ukoo bora wa nchi ya Barotse (Barotseland) iliogopa machafuko ya watumwa pindi wangejaribu kupinga kupanua kwa athari ya Waingereza.

Hata pale ambapo serikali thabiti za siku nyingi zilikuwa zimejiimarisha kiuongozi pamoja na uhalali wa kutambuliwa na zilikuwa na uwezo wa kuhamasisha wingi wa watu wake katika ukinzani, wanahistoria wa siku hizi wameelekea kushutumu namna finyu ya maneno matupu ya kijadi ya dhana yao ya umamlaka. Wanahistoria hao wameweka mkazo juu ya umuhimu wa ule ukinzani ambao dhana ya umamlaka ilifafanuliwa upya. Ndiyo maana Allen Isaacman anadahili kwamba kinyume na ukinzani uliotangulia ambao ulifanywa kwa madhumuni ya kurejesha tena uhuru wa serikali za kale au uhuru wa kundi fulani la watu walio na mnasaba machafuko ya mwaka 1917 katika bonde la Zambezi "yalilenga kukomboa watu wote wa Zambezi kutoka katika udhalimu wa kikoloni", yakiwahamasisha hasa wakulima wadogo wadhulumiwa wa kila mbari. Mageuko haya ya shabaha yalionyesha "kiwango kipya cha zinduko la kisiasa ambapo kwa mara ya kwanza Mreno alitambuliwa kama mnyanyasaji wa watu wote".

## *Jukumu la Dhana za Kidin*

Wakati huo huo wanahistoria wamekuwa wakitazama tena jukumu la dhana za kidini katika ukinzani wa Waafrika. Hayo waliyoyagundua hayafanani hata kidogo ama na "waganga wachawi" washupavu walioelezwa katika ripoti za wakoloni au na "uchawi wa kukata tumaini". Kwanza wamegundua kwamba mafunzo na ishara za kidini mara nyingi zilihusiana moja kwa moja na suala la umamlaka na uhalali. Watawala walihalalishwa kwa njia za kufanya tambiko na mtawala fulani na watu wake walipokusudia kulinda umamlaka wao wakiegemea sana kwenye dhana na ishara za kidini. Mara nyingi matatizo ya uhalali wa aina hii ndiyo yaliyosababisha'kuzuka kwa vyama vikubwa vilivyojaribu kufafanua tena umamlaka. Vyama vya aina hii karibu vyote vilikuwa na bahati ya kuongozwa na viongozi wa kiroho waliokuwa wakieneza habari ya umoja ulio mpana zaidi. Wakati mwingine aina hii ya maendeleo ilitokea katika muktadha wa Uislam, pengine ilitokea kwa sababu ya athari ya mawazo ya

Kikristo, na mara nyingi sana ilitokea katika muktadha wa dini ya Kiafrika. Hii ilitokea huko Rhodesia ya Kusini ambako maasi ya mwaka 1896 yalihamasishwa na kuratibiwa na viongozi wa kidini. Isaacman anadahili kwamba maasi ya mwaka 1917 katika bonde la Zambezi yalichochewa na mafunzo ya mjumbe wa kiroho, Mbuya, ambaye hakudai kurejeshwa kwa nchi yake mwenyewe Barue bali badala yake alihubiri juu ya injili ya udugu na kunyanyaswa kwa Waafrika wote.

Mafundisho ya kinabii ambayo yalikuwa chanzo cha baadhi ya ukinzani mkubwa taratibu yanaanza kupembuliwa kwenye taarifa potofu za wapinzani wake.

Taarifa ya Gilbert Gwassa juu ya maendeleo na tabia ya itikadi ya MajiMaji ya Kinjikitile ni mfano mzuri wa aina hii ya upembuzi. Muundo mpya mwingine umefanywa na Mongameli Mabena juu ya mafunzo ya nabii na mzalendo mkuu wa Kixhosa, Makana ambamo ameonyesha kwamba hayakuwa "fungu la dhana za kidini zisizopatana na zisizofungamana", bali yalikuwa "ruwaza ilijengwa kwa ustadi wa vipengee vya Kikhosani, Kixhosa na vya Kikristo" vilivyofungamanishwa pamoja kwa kutumia ubunifu wa hali ya juu. Kwa namna nyingine mafunzo ya Makana yalikuwa tafsiri ya Kiafrika ya itikadi ya Kikristo ya Kiprotestanti kuhusu umamlaka. Alihimiza umoja wa uxhosa wote na imani katika ulimwengu wao wa maadili. Dali'dephu, Mhenga wa Waxhosa angewafukuza wazungu wote, wafu wa Kixhosa wangefufuka; na enzi mpya ingeanza.

Kwa hiyo ujumbe wa kinabii wa aina hii haukuwa upuuzi mtupu bali ulikuwa jaribio makini la kutaka kupanua na kufafanua tena dhana ya umungu na uhusiano wake katika taratibu za maadili mema na ulisababisha mabadiliko makubwa katika mawazo ya ndani ya Kixhosa na uhusiano na pia kuweka "msingi wa itikadi ya ukinzani". Peter Rigby amedai hivi karibuni kwamba unabii wa Kiafrika haukuwa tu matokeo ya nguvu za nje za ufisadi katika kipindi cha ukoloni au ya kuvunjwa kwa dini za Kiafrika lakini zaidi ya kujaribu kuzifanya dini za Kiafrika zilingane na mazingira. Kutokana na wao hili la mifumo ya kidini ya Kiafrika ambayo mara kwa mara iliweza kuanzisha uongozi wa kinabii kutokana na mivutano na uwezo wao na kutokana na viongozi wa kinabii kuweza kuunda sanisi mpya ambazo wakati huo huo ziliimarisha za zamani na pia kuacha zile mpya ziendelee, tumetoka mbali kuanzia kwenye dhana ya itikadi za kinabii za upinzani kama "uchawi wa kukata tamaa".

Pamoja na kwamba kazi hii yote imekuwa na thamani, mkazo juu ya itikadi ya kidini katika ukinzani umeshambuliwa katika pande mbili. Kwa upande mmoja, baadhi ya wanazuoni wanadai kwamba jukumu la dini katika ukinzani limetiliwa mno nguvu; kwa upande mwingine baadhi ya wanazuoni wanadai kwamba jakumu la ukinzani katika dini limetiliwa chumvi.

Kwa mauzili hayo waandishi wa kikoloni walizungumzia juu ya kiongozi wa kike wa maasi ya Giriama katika mrima wa pwani ya Kenya kama "mchawi"; wanahistoria wa hivi karibuni wamemfasiri kama "nabii". Lakini Cynthia Brantley Smith, katika taarifa yake ya kuvutia na kamilifu ya Giriama ameonyesha kwamba hakuwa namna yoyote ya kiongozi wa kidini bali alikuwa mwanamke wa kuheshimika

na mwenye nguvu. Hii ni hali mojawapo inayoonyesha kuwa fasiri ya maneno ya kikoloni kama vile "mganga" au "mchawi" hayatoshi kurekebisha upotofu wa taarifa rasmi. Imependekezwa na wachunguzi wawili wa historia ya Ndembela na Shona, David Beach na Julian Cobbina kwamba hiyo ni kweli pia kuhusu taarifa ya Ranger mwenyewe ya maasi ya mwaka 1896 ya Rhodesia ya Kusini na kwamba wajumbe wa kiroho walikuwa na athari ndogo kuliko alivyoeleza na kwamba pengine makasisi wa Nwari hawakushiriki kabisa katika maasi.

Haya yote ni muhimu katika suala la kiini cha ukinzani dhidi ya vyama vya kinabii. Nabii anajitokeza katika mwitikio kwa wananchi juu ya haya ya kuwepo kwa mabadiliko makubwa lakini si lazima hii itokane na tishio la kutoka nje. Nabii anaweza kutokezea kwa sababu ya hali ya wasiwasi mwingi kutokana na mivutano iliyomo katika nchi au mabadiliko makubwa au hata kwa sababu ya hamu ya jumla ya kutaka kuzidisha mwendo wa hatua za mabadiliko na kuchukua mielekeo mipya. Ndiyo maana mara nyingi kiongozi wa kinabii anaelekeza mafunzo yake katika upande wa maadili ya jamii za Kiafrika – wakati mwingine akiongoza chama cha ukinzani dhidi ya umamlaka wa ndani, wakati mwingine "akipinga" zaidi maumbile ya asili ya kibinadamu. Inadhihirisha wazi katika kazi zinazofanyika sana juu ya idadi kubwa ya viongozi wa kinabii katika Afrika ya karne ya 19 kwamba wengi wao hawakujishughulisha na ukinzani dhidi ya weupe au hata kupambana moja kwa moja na weupe.

Hata viongozi hawa wa kinabii ambao kimsingi walijihusisha na kufafanua mahusiano ya watu wao na Wazungu hawakuwa kamwe na shauri moja katika kupendekeza kuukataa au kuukinza ukoloni. Kama anavyosema Mabona, unabii wa Xhosa ulizaa itikadi ya ukinzani na itikadi ya kuyakubali baadhi ya mambo mageni kwa njia dhibitifu. Nabii wa ukinzani alikuwa Makana, nabii wa 'ukubalifu wa mambo mageni kwa njia dhibitifu' alikuwa Ntsikana.

Ingawa hapana tukio jingine linalotuonyesha kwa wazi majadiliano ya kinabii baina ya Makana na Ntsikana, uwezekano wa mapambano ya kinabii ya namna hiyo unajidhihirisha hata katika maeneo ya ukinzani thabiti, kama katika maeneo ambamo MajiMaji ilijitokeza au maeneo ya Shona ya Rhodesia (sasa Zimbabwe). Baada ya kushindwa kwa MajiMaji, jumla ya ishara na madai kuhusu nguvu ya kiroho ambayo Kinjikitile aliitumia vilitumiwa na mfululizo wa manabii ambao walihusika na utakaso wa ndani mwa jamii za Kiafrika, na ambao waliongoza kile kilichoitwa "vyama vya kufutilia mbali uchawi".

Kuhusu Shona Elleck Mashingaidze ameandika makala ya kuvutia sana juu ya mfuatano wa ushauri wa kinabii uliotolewa kwa watu wa Shona wa eneo la bonde la Mazoe, Wajumbe wa kinabii wenye wasilishi wote wenye athari kubwa zaidi kwanza waliwashauri watu kusikiliza kwa uangalifu mafundisho ya wamisionari; halafu waliwashauri kushiriki katika maasi na kuwafukuza weupe; na baadaye waliwashauri tena kuwapeleka watoto wao katika shule za misioni ili kupata kile walichokiita "hekima" ya kizungu. Mashingaidze halichukulii jambo hili kama mfuatano wa

mikanganyiko au usaliti bali kama ukumbusho kwamba bado kulikuwa na nafasi ya kukubali au kukataa baadhi ya tabia za utaratibu mpya kwa kutumia dini ya kijadi. Ama kwa hakika Profesa B.A. Ogot amewapinga wale wanaofasiri harakati za kinabii za Kenya kimsingi kuwa harakati zenye kupinga ukoloni. Anaandika juu ya mmoja wa nabii wa aina hii, Simeo Ondeto, kwamba kwa kweli alikuwa "“mwanamapinduzi"”lakini mapinduzi yake yalihusiana zaidi na mazingira ya maadili kuliko mazingira ya kisiasa na yalikusudiwa kutoka katika fikra za mtu binafsi. Ogot amewahi kusema kwamba asili ya vyama vya kinabii ni kwamba “vinageuza nguvu za kiroho na za kijamii na kujenga jumuiya mpya zenye kuweza kukabiliana na changamoto za ulimwengu wa leo”. Ndiyo kusema itikadi kuu za kinabii za ukinzani zinatokea kama sehemu ya jaribio kubwa katika kufafanua tena msingi wa maadili ya jamii.

## *Matokeo na Uhusiano wa Ukinzani wa Kiafrika*

Hadi kufikia miaka ishirini iliyopita, ilikuwa ikikubalika kwa jumla kwamba ukinzani haukuwa na faida yoyote. Tangu wakati huo kumekuwa na madai makali kwamba ukinzani ulikuwa na mtazamo wa siku za baadaye. Maadamu ukinzani ulihusika na umamlaka uanaweza kuchukuliwa kuwa ulikuwa unatazamia kupatikana tena kwa umamlaka na ushindi wa utaifa wa Kiafrika; maadamu yalikuwa na itikadi za kinabii unaweza kusemwa kuwa ulitoa mchango katika jumuiya mpya za dhana. Baadhi yake zikawa na matokeo ya kuendeleza hali ya watu ambao waliasi. Ukinzani mwingine ulileta uongozi mwingine dhidi ya ule wa machifu uliotambuliwa rasmi. Ranger amedai kwamba ukinzani ulihusiana na hali ya utaifa ya umma kwa kuwa ulitokana na vyama vya umma; kwa njia ya mwendeleo wa hali na ishara ambazo zilikuwepo katikati ya vyama vingine vya umma katika kipindi cha kati; na mwisho kwa sababu hamasa dhahiri ambayo vyama vya utaifa vilipata kutokana na kumbukumbu za wakati uliopita wa kishujaa.

Sababu hizi zimeendelezwa na waandishi wengine na uhusiano wa leo wa ukinzani umekuwa kanuni thabiti ya wananadharia wa utaifa na wa vita vya msituni. Ndiyo basi Walter Rodney mwishoni mwa uchunguzi wake wa ukinzani wa Ovimbudu dhidi ya Mreno; alisema:

> Wapigania uhuru wa Angola wenyewe wanathibitisha uhusiano baina ya vita vyao vya ukombozi wa taifa na ukinzani uliotangulia na kwamba (kwa mamlaka yao) inasemekana watu wengi wanakumbuka kichanya nia ya matukio kama vita vya Bailundu. Wasomi wasiotalii mambo hawana sababu ya kulikana jambo hili.

Wasomi wawe wataliimambo au la wakanushe uhuriano uliofikiriwa kuwepo baina ya ukinzani na vita vya uhuru vya baadaye. Makanusho ya aina hii yametoka pande zote mbili, “kulia”, na “kushoto”. Akiandika akiwa amemili ‘kulia’, Henri

Brunschwig amekanusha kuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja tokea ukinzani hadi vyama vya utaifa. Wakiandika wakiwa wamemili "kushoto" baadhi ya wanahistoria wengine kama vile Steinhart wamekanusha uhusiano uliofikiriwa kuwepo baina ya ukinzani na utaifa kwa misingi kwamba hiyo ni njia ya kisomi kuwaruhusu wachache wanaotawala, ama ambao mara nyingi hawajali wengine, katika dola mpya kudai uhalali wa mapinduzi.

Kazi ya hivi karibuni zaidi na ambayo ni ndefu zaidi kuhusu ukinzani-kitabu cha Isaacman juu ya maasi ya Kiafrika katika bonde la Zambezi – inajaribu kushughulikia kwa namna isiyo dhahiri, maoni ya Brunsechwig na Steinhart.

Isaacman anashughulika na Brunschwig kwa kuweka mkazo wake siyo juu ya "ufinyu" wa mawazo ya maasi ya Kimbari bali juu ya fasiri mpya ya umamlaka ambao anadai kuwa umejitokeza katika maasi ya mwaka 1917. Anashughulika na Steinhart kwa kulinganisha aina hii ya ukinzani uliokuzwa siyo na utaifa wa watu bora bali na chama cha ukombozi wa kimapinduzi FRELIMO.

## *Mgawo wa nyakati za Fasili ya kiuchumi*

Zaidi ya fasili za kisiasa na za kidini za ukinzani kulikuwepo pia na fasili ya kiuchumi. Labda fasili mpya ya kimapinduzi zaidi ni ile ya Samir Amin. Amin anadai kwamba ukinzani wa Afrika Magharibi wa kikweli kweli dhidi ya Ulaya ulitokea mwishoni mwa karne ya 17 na 18 katika kipindi cha biashara ya watumwa ya Antlantiki iliyoendeshwa na Wazungu na kwamba Uislamu ulitoa itikadi ya ukinzani. Anaukataa ukinzani wa kipindi cha Mnyang'anyiro wenyewe na kuueneza kama vitendo visivyo na mashiko vya tabaka linalotawala ambalo tayari lilikwishafikia masikilizano. Kwa maoni ya Amin kilichokuwa hasa hatarini katika mapambano kati ya Afrika na Ulaya siyo utawala rasmi wa kisiasa bali majaribio ya Ulaya katika kuutumia uchunguzi wa Afrika. Ukinzani halisi wa Kiafrika ulielezwa dhidi ya hila za kiuchumi za aina hiyo.

Wakati Amin anatoa hoja ya kwamba ukinzani halisi ulitokea kabla ya Mnyang'anyiro, wanahistoria wengine wakitumia mtazamo wa kiuchumi wanaonekana kudai kwamba ukinzani halisi na muhimu dhidi ya utawala wa kikoloni ulitokea tu katika karne ya 20. Bila shaka kulikuweko na ukinzani mwingi wa kiuchumi katika kipindi cha Mnyang'anyiro. Hasa Wazungu walivunja mapatano yao ya zamani na wafanyabiashara wa Kiafrika na wachuuzi na wakatumia nguvu katika kuimarisha uhodhi wa biashara. Matokeo yakawa ukinzani mkali kwa upande wa wafanyabiashara wa Kiafrika iwe uliongozwa na Chifu Nana wa Itsekiri katika delta ya Niger (Nigeria) au na machifu wa Kiafrika na wa Kiswahili ambao waliongoza biashara ya watumwa kaskazini mwa Msumbiji, au na mfanyabiashara mkuu, Rumaliza ambaye alipigana na Wabelgiji na Wajerumani katika Afrika Mashariki.

Immnuel Wallerstein amevichukulia vita hivi vya wafanyabiashara kama mojawapo ya matukio thabiti ya ukoloni wa mwanzo. Ametoa hoja kwamba kuanzia mwaka 1879, ushirikiano wa zamani kati ya Afrika na wafanyabiashara wa Kizungu

ulianza kuvurugika na kufikia mwaka 1900 kutokana na kusambikwa kwa utawala wa kikoloni kuweko kwake kukawa kumekoma; na kwamba athari ya mara moja ya utawala wa kikoloni ukawa juu ya wafanyabiashara wa Kiafrika ... hadi kufikia mwishoni mwa Vita vya Kwanza mfifio mkali wa umuhimu wa Mwafrika, na ule wa tabaka la Kiarabu lifanyalo biashara ukawa umedhihiri.

Lakini kwa jumla wanahistoria wa siku za karibuni hawakuunga mkono ukinzani wa wafanya iashara. Hopkins anatutahadharisha tusichukulie kwamba wafanyabiashara wa delta ya Niger kama kina Nana Olomu walikuwa waasisi wa utaifa au wawakilishi wa manung'uniko ya watu wengi. Ameonyesha kwamba maono yao ya haki ya kijamii hayakuhusika na ukombozi wa watumwa (wao) wenyewe. Nancy Hafkin anasisitiza kwamba maslahi waliyopigania machifu wakinzani wa Msumbiji ya Kaskazini yaliwahusu wao binafsi tu na wala siyo umma. Anahitimisha kuwa "ukinzani wao haukuwa wa kimaendeleo hata kidogo wala haukuungwa mkono na umma".

Uwezo wa wafanya biashara wakuu wa ukinzani kama ule wa watawala wa nchi ndogo ulidhoofishwa na chuki na manung'uniko waliyokuwa wamejenga kwa Waafrika. Kampuni ya *British Imperial East Africa Company* (Kampuni ya Afrika Mashariki ya Kifalme ya Uingereza) ilipotaka kuvunja nguvu ya wafanyabiashara wa Kiarabu, wa Kiswahili na wa Kiafrika, ikaanzisha njia mpya ya biashara katika bara kutoka Malindi "ambayo ilitegemea maboma yaliyojengwa na jumuiya za watumwa waliowatoroka mabwana zao wa Kiarabu katika mashamba ya pwani". Wamiliki biashara wakuu wa mrima wa Lagos walipata tabu kuweka ukinzani thabiti dhidi ya majilio ya Mwingereza kwa sababu ya kutumikisha kwao watu kazi kwa nguvu; watu ambao zaidi walikuwa watumwa na mahadimu. Hali ya biashara ya kimataifa, ambayo ilileteleza kuinakia kwa wafanyabiashara wa Kiafrika wenye uwezo mkubwa pia ilihakikisha kwamba mafanikio yao yangepatikana basi kungekuwa na chuki nyingi ya ndani na mvutano.

Zilikuwepo tofauti kuhusu hali hii ya mvutano kati ya wafanyabiashara wenye uwezo mkubwa na watu wa kawaida kwa jumla. Ndiyo maana katika ufalme wa Bailundu huko Angola ambako kila mtu alishughulika na biashara na kwa hiyo nchi ikastawi tangu mwaka 1870 hadi kushuka kwa bei ya mpira katika miaka ya 1899 – 1902 na kuingia kwa wafanya biashara weupe, mvutano wa namna hiyo haukuweko. Katika maoni ya uchunguzi wa hivi karibuni juu ya vita vya Bailundi vya mwaka 1901, chuki juu ya uchokozi wa biashara ya Wazungu ulihusika sana na maasi makubwa ya watu wote ambayo yalizuka dhidi ya Mreno.

Lakini kwa jumla wanahistoria wa ukinzani wanaotalii jambo hili kwa msingi wa kiuchumi wanahusisha migomo ya watu wengi siyo na chuki juu ya mashambulizi ya Wazungu dhidi ya biashara, bali na kuzidi kuelewa polepole zaidi kwa watu wa Kiafrika kwamba weupe walikuwa na nia thabiti ya kupata watumishi rahisi. Mwanzoni, Waafrika wengi waliweza kuwakaribisha Wazungu kama walinzi dhidi ya machifu wadhalimu au wafanyabiashara wa Kiswahili wenye tamaa, au mabwana wa

watumwa. Lakini punde tu waligundua kwamba masharti ya Wazungu kwao yalikuwa mabaya vivyo hivyo, kama siyo zaidi, Mwanzoni Mabwana wengi wa Kiafrika wa watumwa, machifu na wafanyabiashara waliwaogopa na kuwachukia wazungu lakini wengi wao baadaye waligundua kwamba maslahi ya watawala weusi na wazungu mara nyingi yalilingana. Kwa hali hiyo mageuzo makubwa ya mfumo wa ukinzani yakajitokeza.

Sawa kama Mnyang'anyiro wa kwanza kuhusu nchi na umamlaka vilivyopingwa, vivyo hivyo ndivyo ulivyokuwa Mnyang'anyiro wa huu wa pili uliohusu wafanyakazi. Ulipingwa na kukinzwa kwa silaha na msaada mwingi uliotolewa kwa machafuko makuu ya mwanzoni mwa karne ya ishirini ambayo yalijitahidi kufafanua tena umamlaka uliotokana na watu waliochukia kazi ya kulazimishwa. Ulipingwa pia na utoro na migomo, na kukataa kufanya kazi mashimoni, na ghasia mbalimbali. Katika kazi za wanazuoni kama vile Charles Von Onselen, mwelekeo mpya kuhusu utafiti juu ya ukinzani umezuka – siyo tena mwelekeo wa "ukinzani wa Zambia" au "ukinzani wa Bemba" bali mwelekeo wa ukinzani katika mfumo mzima wa mawasiliano baina ya nchi na nchi katika makoloni kuhusu kimia cha Uhamaji wa Wafanyakazi.

## *Hitimisho*

Ni dhahiri basi kwamba historiografia ya ukinzani ni jambo la kusisimua na lenye kuzua majadiliano. Hata hivyo mabadiliko na mielekeo mipya inaongezeka zaidi kuliko inavyokanusha maswali matatu ya msingi yanayojadiliwa. "Kawaida" na "ujumla" wa ukinzani vinajitokeza bado dhahiri zaidi wakati ukinzani wa mwanzoni usio dhahiri dhidi ya uchokozi wa kiuchumi wa Wazungu unapojumuishwa katika orodha yetu ya ukinzani wa silaha na katika machafuko katika kipindi cha Mnya'anyiro. Uvumbuzi wa msingi wa Kiitikadi wa ukinzani unapewa sifa mpya ambapo matokeo ya kwanza ya "utambuzi" kwa upande wa wafanyakazi au wakulima wadogo kuhusu wazo la umamlaka na katika kutafuta mfumo mpya wa maadili vinapojumuishwa. Na uvumbuzi wa mahusiano kati ya ukinzani na hali ya sasa ya Afrika unapewa mkazo mpya kutokana na wazo la ukinzani wa kiuchumi.

# 4


## *Juhudi na Ukinzani wa Waafrika: Kaskazini mwa Afrika*

Hakuna mahali katika Afrika ambako juhudi na ukinzani wa Waafrika dhidi ya kugawanywa na kutawaliwa kwa bara hili na Wazungu vilikokuwa na nguvu na vilikochukua muda mrefu zaidi kama ilivyokuwa katika dola ambazo leo zajulikana kama Misri, Sudan na Somalia, Kaskazini – Mashariki mwa Afrika. Mapambano hayo yalianza mwaka 1881 yalipotokea maasi ya kijeshi katika Misri na yakaendelea katika baadhi ya sehemu za eneo hilo hadi kwenye miaka ya 1920 hivi. Hapakuwahi kutokea katika historia ya Afrika ambapo watu walipigana vita kali katika kulinda uhuru wao, himaya yao, na zaidi ya yote utamaduni wao na dini yao kama walivyofanya watu wa eneo hili. Katika sura hii tutajaribu kutalii jitihada na mapambano haya tukianza na Misri, kisha Sudan na hatimaye Somalia.

### *Misri*

Mnamo Februari, 1881 jeshi la Misri, kwa mara ya kwanza kabisa katika historia ya sasa ya Misri, lilijitoma katika siasa kwa kuanzisha mapinduzi dhidi ya ubeberu na Khedive Tawfik chini ya uongozi wa Kanali Ahmad Urabi. Sababu za mapinduzi haya ni changamano na zilikuwa na athari kubwa. Hapana shaka sababu ya kwanza ilikuwa ni matumizi mabaya ya fedha yaliyofanywa na Khedive Ismail (1863 – 1879) na mrithi wake Khedive Tawfik (1879 – 1892). Hadi kufikia mwaka 1880 mikopo Mikubwa ambayo Khedive Ismail alipata kutoka Ulaya ilikwishaifanya Misri ikaribie kuwa mufilisi. Wakati nusu ya mapato ya Misri yalikuwa yakitengwa kulipia madeni ya mikopo hii. Wamisri walitozwa kodi kubwa sana na wale *fallahin* (ambao ndiyo walikuwa wengi) ambao walishindwa kuzilipa kodi hizo walipigwa bila huruma. Hali hii ngumu ya uchumi na yakudhalilishwa kwa watu vilileta chuki na ukinzani mkubwa dhidi ya Khedive Tawfik na serikali yake iliyojaa maovu na rushwa.

Sababu nyingine iliyoleta chuki ni kule kutawaliwa kabisa kwa Misri na mataifa ya Ulaya yenye nguvu na Wageni wakazi. Mataifa hayo yenye nguvu ambayo yalikuwa yameipa Misri mikopo ya fedha yalimiliki serikali na fedha za nchi na baadaye ikawa karibu haiwezekani kabisa kwa serikali yoyote ya Misri kuanzisha mabadiliko yoyote ya kiutawala au kiuchumi bila kibali cha pamoja cha mataifa kumi na manne ya Kizungu. Wakati Wamisri walipokuwa wakihangaika na taabu zote hizi wageni walioishi katika nchi hiyo walikuwa wakijitajirisha, mara nyingi kwa njia zisizo halali kwa gharama ya umma. Walikuwa hata hawafungwi na sheria za nchi; walikuwa na mahakama zao wenyewe. Hapana shaka kwamba hamu ya kutaka




**4.1** *Siasa na Uzalendo katika Afrika Kaskazini-Mashariki*

kukomesha hali hii ya kudhalilishwa na kunyanyaswa na watu wageni ilikuwa ndiyo sababu kubwa ya mlipuko wa mapinduzi ya Kiurabi.

Sababu ya tatu ilikuwa ni kuenea kwa mawazo ya siasa ya kiungwana kati ya Wamisri kutokana na kuenea kwa elimu na maendeleo ya uandishi wa habari kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Hii ilisababisha kuanzishwa na kuendelezwa kwa chama cha kikatiba katika Misri kuanzia miaka ya 1860, hasa kati ya Wamisri waliosoma Magharibi na ambao walipinga utawala wa Mzungu na siasa ya Khedive ya kujitwalia madaraka peke yake. Wakiongozwa na Muhammad Sharif Pasha wazalendo hawa wa chama cha kikatiba walipigania kuanzishwa kisheria kwa katiba ya kiungwana na kuanzishwa kwa serikali ya wawakilishi.

Jambo muhimu kabisa lililotokea mara tu baada ya mlipuko huo wa mapinduzi lilikuwa ni kutoridhika na kuvunjika moyo kwa jeshi la Wamisri. Maaskari walipata mishahara midogo sana, piasta 20 kwa mwezi, na maafisa wa jeshi wa Kimisri hawakuruhusiwa kupata vyeo vya juu. Vyeo vya juu vyote vilichukuliwa na maofisa wa kijeshi wageni, wa Kituruki – Kiserkasi (Turco-Circassian) ambao waliwadharau na kuwatendea vibaya Wamisri waliokuwa chini yao. Ni kutokana na haja ya kukomesha hali hii ya kudhalilishwa na kujaribu kuleta hali ya uauanchi katika nchi yao ndipo jeshi la Misri lilipoanzisha mapinduzi, mapema katika Februari, 1881, dhidi ya ukoloni wa Kizungu na Khedive Tawfik.

Kiongozi wa mapinduzi hayo, Kanali Ahmad Urabi (1839 – 1911) alikuwa mtu mwenye haiba kubwa na mwenye asili ya *Kifallah* (picha 4.1). Ingawa Urabi alikuwa mtu wa hali ya kawaida na hakuwa na busara nyingi lakini alikuwa mtu jasiri na msemaji hodari. Sifa hizi za uongozi baadaye zilimfanya Urabi kuwa kiongozi pekee wa mapinduzi, na alihusika sana na kuanzishwa kwa *Al-Hizb al-Watani* (Chama cha Wazalendo). Wanachama wake walikuwa mchanganyiko wa watu wenye asili ya *Ki-fallah* na baadhi ya Wamisri maarufu ambao waliungana pamoja katika kutoridhika na kwao na utawala dhalimu wa Tawfik.

Katika hatua zake za mwanzo mapinduzi hayo yalipata mafanikio makubwa. Uthman Rifki, Waziri wa vita wa Kiserkasi aliyekuwa maarufu sana na ambaye ndiye aliyekuwa mchochezi mkuu wa sera ya ubaguzi katika jeshi alifukuzwa kazi na nafasi yake ikachukuliwa na mshairi maarufu na mwanasiasa wa kimapinduzi Mahmud Sami al-Barudi. Baadaye baraza kamili la mawaziri wa Ki-Urabi liliundwa na Ahmad Urabi mwenyewe akiwa Waziri wa Vita. Tawfik aliingiwa na hofu kiasi kwamba aliamuru paundwe Bunge la wananchi na tarehe 7 Februari, 1882 akaidhinisha katiba ambayo kwa kiasi kikubwa ilizingatia haja za wageni. Lakini wakati akiruhusu mabadiliko haya kufanyika Khedive alikuwa akila njama na mataifa ya Kizungu na Wageni wengine ili wayazime mapinduzi hayo. Katika kujaribu kutoa udhuru wa mataifa ya nje kujiingiza katika mapambano haya, baadhi ya wanahistoria wa (historia ya ) Misri hudai kwamba wafuasi wa Khedive na Waingereza waliandaa mauaji ya Alexandria ya tarehe 12 Juni, 1882: ambako wageni wengi waliuawa na mali nyingi ikaharibiwa. Mashtaka haya yawe ni yakini au la si jambo la muhimu hapa lakini hakika ya mambo



4.2 *Kanali Ahmad 'Urabi' ('Arabi Pasha') (1839 – 1911)*

ni kwamba Khedive aliwakaribisha Waingereza kuingilia kati nao kwa hamu kubwa na haraka walikubali na kuupiga mizinga mji wa Alexandria tarehe 11 Julai 1882. Jeshi na wananchi wa Misri wakaungana kupigana vita dhidi ya wavamizi hawa lakini walishindwa kwa kuwa hawakuwa na silaha bora kama wapinzani wao. Wamisri wapatao karibu elfu mbili waliuawa katika vita hivi.

Baada ya kushindwa huku Urabi akatangaza vita vya *Jihadi* dhidi ya Waingereza: matangazo ya vita hivi yaligawanywa kwa wananchi wa Misri. Katika mwezi Agosti, 1882 vita vilitokea mara kadha huko Kafr al-Dawar mahali ambako jeshi la Misri lilikuwa limerudi nyuma katika vita vya mwanzo. Umma wa Misri pasi na kusita ukalipelekea jeshi lao misaada ya kifedha na maelfu ya vijana wakajitolea kwenda vitani. Hata hivyo mambo hayakukiendea vizuri chama hicho cha ukinzani. 'Urabi asingeweza kumudu zaidi ya askari 16,000 waliopata mafunzo; na hata idadi hii ndogo ilitawanywa katika sehemu za Kafr al-Dawr, Dimyat (Damietta) na eneo la Mfereji wa Suez. Isitoshe basi, jeshi la Misri halikuwa limepata mafunzo ya kutosha, hawakuwa na zana na silaha za kisasa, wala hawakuwa na njia madhubuti za usafiri. Hivyo halikuwa jambo la kushangaza kuona kwamba tarehe 13 Septemba, 1882 Jeshi la Kisiasa la Waingereza, lenye askari 20,000, chini ya uongozi wa Sir Carnet Wolseley, liliwashinda Wamisri na kuteka nchi yao. Waingereza wakaitawala nchi hii kwa muda wa miaka sabini na miwili.

Kushindwa kwa mapinduzi ya Kiurabi katika kuiondoa Misri katika athari za Ulaya na kukomesha utawala wa Kituruki usiokuwa na haki kunaweza kuelezeka kwa urahisi. Ingawa mapinduzi haya yaliungwa mkono na Wamisri wengi lakini hayakupata muda wa kutosha wa kuyahamasisha. Aidha baada ya muda mfupi palitokea mgawanyiko katika muungano wa wazalendo hao uliosababishwa na mgongano baina ya chama cha Wanajeshi na chama cha wanakatiba. Wakati kundi la pili kimsingi lilipinga kujiingiza kwa jeshi katika siasa kundi la kwanza liliamini kuwa kumiliki kwao serikali kungekuwa ndio njia bora ya kuyalinda mapinduzi. Zaidi ya hayo mapinduzi yaliathirika vibaya kutokana na hila za ndani zilizofanywa na Khedive na Maserkasi waliomuunga mkono na ambao waliyasaliti mapinduzi na kuwasaidia Waingereza kutawala.

Urabi mwenyewe alifanya makosa kadhaa. Kukataa kwake kumwondoa Khedive katika ufalme mwanzoni mwa mapinduzi eti kwa sababu hii ingekaribisha uvamizi kutoka nchi za nje na kuleta fujo nchini kulimpa Tawafik nafasi nzuri ya kufanya hila zake na kula njama dhidi ya mapinduzi. Kosa jingine kubwa alilofanya Urabi ni kule kukataa kwake ushauri wake wa kivita juu ya kuafunga mfereji wa Suezi. Alikataa ushauri huo kwa matumaini kwamba Ufaransa isingeweza kuiruhusu Uingereza kuutumia mfereji huo kuishambulia Misri; matumaini ambayo kwa hakika hayakuwa na msingi. Lakini zaidi ya yote ni kwamba hatimaye mapinduzi ya Kiurabi yalishindwa na nguvu za Kiingereza za kivita na kiteknolojia.

Jitihada za Wamisri na Ukinzani dhidi ya Kutamalaki kwa Waingereza 1882 – 1914

Kushindwa kwa mapinduzi ya Kiurabi katika vita kuliwavunja moyo wananchi na kukaleta hali ya kukata tamaa na kuwafanya watu wayatazame mambo kwa makini zaidi. Kwa hiyo hapakuwepo na ukinzani wowote wenye athari katika mwongo wa kwanza wa kutawaliwa na Waingereza, tangu 1882 hadi 1892. Huko Misri kwenyewe watu muhimu waliotoa mawazo ya kutetea utaifa wao katika mwongo huu walikuwa ni wale wananchi wakimbizi. Ni kuanzia mwaka 1893 ambapo ukinzani ndani ya Misri ulianza. Ukinzani huu ulianzishwa na Khedive mpya aliyejulikana kama Abbas Hilmi (Abbas wa II, 1892 – 1914). Khedive huyu kijana na mpenda makuu aliwashawishi watu kuanzisha chama cha wananchi ambacho kilidai kuondolewa kwa Mwingereza mara moja. Hatua moja muhimu kabisa aliyoichukua ni kule kutoa msaada wa kifedha uliokiwezesha chama kuchapisha habari na kuimarisha shughuli zake. Haukupita muda mrefu Khedive huyu akawa tishio kubwa kwa ntawala dhalimu wa Cromer, ambao ulidumu tangu 1883 hadi 1907. Hatimaye huyu Khedive akafaulu kumlazimisha Waziri Mkuu huyu wa Misri aliyekuwa akiunga mkono utawala wa Mwingereza ajiuzulu mnamo tarehe 15 Januari, 1893. Ingawa baada ya tukio hilo Hilmi hakuweza kufanya mambo yake waziwazi kutokana na nguvu za Mwingereza alizokabiliana nazo pamoja na ghilba, bado aliendelea kuwashawishi watu waliokuwa tayari kuendeleza mapambano dhidi ya kutawaliwa na Mwingereza. Hawa walikuwa kundi la vijana wasomi ambao waliyaelewa vema mawazo ya mapinduzi ya Wafaransa na ambao walikuwa na nadharia za kisasa za kijamii na kisiasa.

Wapinzani wakubwa wa utawala wa Mwingereza kwa wakati huo walikuwa wafuatao: kwanza alikuwa Mustafa Kamil, kiogozi mwenye haiba kubwa, shupavu na msemaji aliyeongoza chama chake cha *Nationalist Party*. Mwanzoni Kamil alifanya juu chini kuhakikisha kuwa anaungwa mkono na Wazungu katika kutafuta uhuru wa Misri. Kwa kutumia fedha nyingi alizopata kutoka kwa Khedive, Kamil alitembelea miji ya Ulaya katika kipindi cha 1895 – 1898 ambako alihutubia mikutano, akahojiwa na waandishi wa habari na akaandika makala na vijuzuu mbalimbali. Shughuli hizi zilileta mvuto mkubwa huko Ulaya lakini zilishindwa kutoa mshawasha juu ya uhuru wa Misri. Ufaransa yenyewe ikiwa na makoloni yake Afrika Kaskazini isingeweza kushawishika na mawazo ya Kamil ya watu kujitawala wenyewe. Na kwa vyovyote vile, kama tukio la Fashoda la mwaka 1898 lilivyoonyesha, Ufaransa haikuwa tayari kupigana na Uingereza kwa ajili ya Misri.

Kazi ya haraka kabisa iliyokuwa ikiwakabili vijana wazalendo ilikuwa ni kuonyesha kwamba madai ya Cromer kuwa Wamisri hawakuwa na uwezo wa kujitawala wenyewe kwa kufuata misingi ya ustaarabu yalikuwa ni madai ya kibaguzi na ya kupendelea kuwashawishi Wamisri wenyewe kuwa wao walikuwa ni taifa kamili lililokuwa na uwezo na lililostahili kujitawala lenyewe: na kuendeleza elimu ya taifa ili kuimarisha hisia za kizalendo miongoni mwa watu. Kamil aliamua kuelekeza juhudi

zake zote katika kazi hii kuanzia mwaka 1898. Kazi yake katika Misri; hadi kufikia mwaka 1906 ilikuwa ni ya kutoa hotuba na makala katika magazeti ya wakati huo, hasa katika *al-Liwa (*Bendera), ambalo yeye mwenyewe alilianzisha katika mwaka 1900. Kazi za Kamil za kisiasa zilianza kutoa matunda kwani alifanikiwa kuongoza mgomo wa wanafunzi wa sheria mnamo mwaka 1906.

Tukio la Dinshaway la Mei 1906 liliipa msukumo mkubwa kampeni ya Kamil katika Misri. Kwa ufupi takio lilitokea hivi; kundi la maofisa wa Kiingereza lilikuja katika kijiji cha Dinshaway kuwinda njiwa. Lakini wanakijiji walikasirishwa sana na kitendo hiki cha Waingereza kuwauwa njiwa ambao ndio walikuwa chakula chao. Hapo kukatokea vita na mmojawao wa hao maofisa akaumizwa vibaya sana. Serikali ya Waingereza ikachukulia jambo hili kwa pupa na kuwapa wanakijiji hao adhabu kali sana. Watu wanne walinyongwa hadharani na wakazi wote wa kijiji cha Dinshaway wakalazimishwa kuhudhuria tukio hilo la kunyongwa kwa wenzao. Ni dhahiri kwamba tukio hilo liliamsha upya kabisa umoja wa kitaifa kati ya wananchi wa Misri na kuwafanya wachukie sana kutawaliwa na Waingereza. Kwa mara ya kwanza tangu 1882 Waingereza wakaanza kutambua dhahiri kwamba maisha yao katika Misri yalikuwa hatarini. Ni kutokana na hofu hii Waingereza walipoamua kuifikiria upya sera yao ya ukandamizaji na kutamka wazi kuwa walikuwa tayari kuitayarisha nchi hiyo kujitawala yenyewe. Cromer akastaafu katika mwaka 1907 na akarithiwa na Eldon Gorst. Kustaafu kwa Cromer kulikuwa ushindi mkubwa kwa Kamilo na chama chake cha Nationalist Party. Chama ambacho kuanzishwa kwake sasa kulitangazwa hadharani mwaka huo wa 1907.

Baada ya kifo kisichotazamiwa cha Kamil katika Februari 1908 Muhamad Farid alichukua nafasi yake kama rais wa chama cha *Nationalist Party.* Farid aliendelea kuandika na kuhutubia mikutano ya hadhara akidai kuondolewa kwa majeshi ya Waingereza. Shughuli zake hizi za kudai uhuru ziliingharimu kifungo cha miezi sita katika mwaka 1911. Baada ya kifungo hicho aliamua kuishi kama ukimbizi.

Hata hivyo hadi kufikia mwaka 1907, baadhi ya Wasomi wa Kimisri walikwishaona kuwa haingewezekana kumwondoa Mwingereza Misri kwa njia ya mapinduzi. Aidha walihisi kwamba kulikuwa na dalili hasa za mabadiliko katika sera ya Mwingereza baada ya mkasa wa Dinshaway. Kwa hali kama hiyo hawakuona ubaya wowote kushirikiana na Waingereza waliokuwa Misri ili kuweza kupata kutoka kwao kile ambacho kingeweza kupatikana hadi hapo uhuru kamili wa nchi yao ungepatikana. Kundi hili lilianzisha chama kipya cha siasa kilichojulikana kama *Umma Party* (Chama cha Watu). Chama hiki kilianzishwa mwezi Oktoba, 1907, Kikiongozwa na Ahmad Lufti al-Sayyid mwandishi wa habari maarufu na mwanaelimu. Chama hiki kiliwahimiza Wamisri kuyapa mtazamo mpya mapokeo yao ya dini ya Kiislamu kwa kuingiza mawazo na taasisi za Kiingereza ambazo zilikuwa muhimu kwa maendeleo yao. Zaidi ya yote chama kilisisitiza umuhimu wa elimu kama njia muhimu ya kuwapa mafunzo watu wenye uwezo wa uongozi na kama njia ya kupatia uhuru wa nchi yao. Lakini chama hiki cha Umma hakikuwa maarufu sana kati

ya Wamisri walioamania utaifa kwa sababu jitihada zao za kushirikiana na Waingereza na mawazo yao ya kutoaminia sana dini viliwatenga Wamisri wengi ambao toka kuzaliwa kwao walikuwa wamekwisha lelewa kwa kuyaaminia sana mapokeo ya kiislamu.

Kwa hiyo harakati za utaifa wa Kimisri kabla ya Vita Kuu hazikuwa na umoja na zilimilikiwa zaidi na watu wa tabaka bora ambao hawakuweza kuwashawishi watu wengi wa kawaida. Matokeo yake ni kwamba harakati hizi zilikuwa dhaifu mno kuweza kupata jambo lolote muhimu toka kwa Mwingereza. Ilibidi wangoje hadi mwaka 1919 kabla hawajajitokeza wazi wazi kuiza kutawaliwa na Mwingereza.

## *Sudan*

### Mapinduzi ya Ki-Mahdi

Kuanzia 1821, Sudan ilikuwa imetawaliwa na Serikali ya Kituruki ya Misri. Kwa hiyo mnamo mwaka 1880 wananchi wa Sudan kama walivyokuwa wenzi wao wa Misri, nao walikuwa wakipinga vita ya kujikomboa kutokana na utawala dhalimu. Bendera ya jihadi iliyoinuliwa na Urabi katika Misri na ukinzania wa Kiislamu dhidi ya utawala wa kigeni vilisikika sana katika harakati za mapinduzi ya kivita chini ya uongozi wa Muhamad al-Madhi huko Sudan. Harakati hizo zilizojulikana kama *Madhiyya* kimsingi zilikuwa ni za vita vya jihadi: kwa hivyo ziliungwa mkono na waislamu wote. Lengo lake kuu, kama lilivyoelezwa tena na tena katika nyaraka za mahdi na matangazo yake, lilikuwa ni kurejesha tena imani ya kale ya uislamu isiyokuwa na upotofu, nyongeza au ubatili wa aina yoyote, na kuitangaza imani hiyo ulimwenguni pote kwa kutumia nguvu iwapo ilibidi. Mbali na dini kulikuwa na sababu nyingine zilizosababisha mapinduzi hayo, zaidi hasa zikitokana na utawala mwovu wa Kituruki – Kimisri. Ghasia zilizoandamana na kutamalaki Sudani katika mwaka 1820 – I zilikuwa zimejenga hamu kubwa ya kulipiza kisasi. Kwa upande mwingine kodi kubwa zilizotozwa kwa nguvu na Waturuki zilisababisha manung'uniko makubwa nchini kote. Majaribio ya serikali kuzima biashara ya utumwa yalizidi kuwatenga zaidi watu wa Sudan Kaskazini kwani walikuwa wameguswa kwenye kitovu cha utajiri wao na kiini cha uchumi wao wa nyumbani na wa kilimo cha nchi.

Kiongozi wa mapinduzi ya Kimahdi, Muhamad Ahmad Ibn 'Abdallah, alikuwa mcha Mungu ambaye alimwamania Nabii Muhamad. Mapambano ya kwanza ya kivita baina ya Mahdi na serikali ya Kiingereza – Kimisri yalikuwa kuanzia mwaka 1881 hadi 1885. Mwanzoni serikali ilikuwa imempuuza Mahdi na kumwona kama *darwish* (maskini ajitafutiaye riziki) tu. Hii inathibitishwa na msafara dhaifu na usio na mpango uliopelekwa kumshughulikia katika kisiwa cha Aba. Kukatokea mapigano madogo ambamo *Ansar* (wafuasi wa Mahdi) walipata ushindi kirahisi na utawala wa serikali ukabaki katika mkanganyiko.



4.3 *Muhammad Ahmad Ibn 'Abdallah', Mahdi (1844 – 1885)*

Baada ya mapigano haya Mahdi akaamua kuhama Aba na kwenda Djabal Kadir katika milima ya Nuba. Mbali na kuwa sawa na ilivyokuwa wakati wa mtume umuhimu mkubwa wa Hidjra (Hijira) ulikuwa ni kuhamisha harakati za mapinduzi toka maeneo ya kando ya mito kwenda Magharibi ya Sudan: tukio lililokuwa na athari kubwa sana kwenye mapinduzi hayo. Kuanzia wakati huo na kuendelea watu wa magharibi wakawa ndio viongozi wakuu wa mapinduzi na makamanda wa vita wakati watu walioishi kando kando ya mito pole pole walianza kutoweka katika mstari wa mbele.

Tukio jingine la muhimu katika historia ya mapinduzi ya Kimahdi lilikuwa ni vile vita vya Shaykan vilivyotokea tarehe 5 Novemba 1883. Akiwa amedhamiria kumvunjilia mbali Mahdi. Khedive Tawfik na serikali yake walitayarisha msafara uliokuwa na mabaki ya askari wa Urabi na uliokuwa chini ya amri ya afisa wa Kiingereza, Hicks Pasha. *Ansar* wakawaangamiza kabisa maadui wao katika msitu wa Shaykan, karibu na al-Obeld. Ushindi huu ulikuwa kichocheo kikubwa kwa Mahdi na mapinduzi yake. Wasudani wengi walijiunga na mapinduzi hayo na wajumbe kutoka baadhi ya nchi za Kiislamu walikuja kumpa Mahdi pongezi kwa ushindi wake dhidi ya 'makafiri'. Jambo jingine lililotokana na vita lilikuwa ni kuanguka kabisa kwa utawala wa Kituruki-Kimisri katika Sudani magharibi na kuanzishwa kwa utawala wa Kimahdi katika majimbo ya Kordofan, Darfur na Bahr al-Ghazal.

Sera ya Uingereza kuhusu suala la Sudan ikawa na mabadiliko makubwa baada ya vita ya Shaykani. Wakati huko nyuma serikali ya Uingereza ilishikilia hoja kwamba suala la Sudan lilikuwa likiihusu Misri pekee baada ya tukio la Shaykan serikali hiyo ilihisi kwamba maslahi ya ubeberu wao yaliihitajia Misri kuondoka katika Sudan. Hivyo serikali ya Uingereza ikaiamuru serikali ya Misri kuondoka Sudan na ikamchagua general Charles Gordon kutekeleza amri hiyo. Wakati huo huo Mahdi alisonga mbele kuelekea Khartoum na kumtia General Gordon katika hali ngumu sana. Baada ya kuuzingira mji wa Khartoum kwa muda mrefu majeshi ya Mahdi yakaushambulia na kumwua Gordon tarehe 26 Januari, 1885. Na hapo wakawa wameukomesha utawala mwovu na dhalimu wa Kituruki – Kimisri katika Sudan.

Katika miaka minne ya mwanzo (1881 – 5), Mahdiyya ilibadilika kutoka katika harakati za Mgomo wa kidini na kuwa dola yenyewe nguvu za kivita ambayo ilitawala Sudan kwa muda wa miaka kumi na minne. Taasisi zake za kitawala, fedha na mahakama na sheria zake vilikitwa kwenye misingi ya Kurani na Sunna.

Mahusiano baina ya dola ya Kimahdi na ulimwengu mwingine yalitawaliwa na *jihadi*. Mahdi na Khalifa wake, 'Abdullah ibn al-Sayyid Muhammad, walikwishaandika barua za maonyo (indharat) – karibu yakiwa ni masharti ya mwisho (ultimatums) – kwa baadhi ya viongozi wa ulimwengu, kama vile Khadiva wa Misri, Mfalme wa Uturuki na Mfalme wa Ethiopia, kuikubali tume ya Mahdi au sivyo wakumbane na *jihadi* mara moja.

Ingawa Mahdi hakuishi kwa muda mrefu kueneza ujumbe wake – kwani alifariki Juni, 1885 – lakini *jihadi* ilikuwa ndiyo sera ya mrithi wake, Khalifa 'Abdullah, kwa nchi za nje. Pamoja na matatizo makubwa ya kiutawala na kiuchumi aliyokabiliana nayo, Khalifa Abdullah bado aliweza kuendeleza *jihadi* katika mikabala miwili: dhidi ya Misri na Ethiopia. Chini ya uongozi wa Abdu al-Rahman al-Nudjumi, majeshi ya Kimahdi yaliishambulia Misri lakini yalishindwa katika vita vya Tushki mnamo mwaka 1889. Kusonga mbele kwa wana-Mahdi katika upande wa mashariki pia kulikabiliwa na ukinzani mkubwa; *Ansar* wakapoteza Tokar katika mwaka 1891 na Kassala katika mwaka wa 1894. Kung'ang'ania kwa Khalifa kuwa Mfalme wa Ethiopia akubali na kuamini Umahdi na Uislamu kulimkatisha tamaa Mfalme wa Ethiopia na kuzifikisha jitihada zake za kutaka kuungana na Sudan dhidi ya ubeberu wa Ulaya. Kushindwa kwa jitihada hizo kulileta mgongano na mapambano ya kivita ya muda mrefu baina ya hizi nchi mbili za Kiafrika; mapambano ambayo yalizidhoofisha sana na kuzifanya zishindwe na ubeberu wa Ulaya kwa urahisi.

Hadi kufikia Machi, 1896 maslahi ya ubeberu wa Kiingereza yalikwishahitajia kushambuliwa kwa Sudan. Jeshi la Kiingereza – Kimisri chini ya uongozi wa General Kitchezer, likaundwa kwa ajili hiyo. Katika awamu ya kwanza ya mashambulizi hayo – Machi mpaka Septemba – maadui walishikilia jimbo lote la Dongola bila kupata ukinzani mkubwa kutoka kwa wananchi wa Sudan. Hii ilisababishwa na mambo mawili. Kwanza maadui walikuwa na teknolojia ya hali ya juu zaidi kuliko wenyeji na pili, walimshitukiza Khalifa.

Kitchener alipokuwa akisonga kusini, Khalifa akaamuru watu wake wajiimarishe vizuri tayari kwa vita. Wakiwa chini ya uongozi wa Emir Mahmud *Ansar* walijaribu kuwarudisha nyuma maadui katika vita ya Atbara, tarehe 8 Aprili, 1898. Wasudani elfu tatu waliuawa na zaidi ya elfu nne wakajeruhiwa. Mahmud mwenyewe alikamatwa na kufungwa katika gereza la Rosetta, huko Misri, ambako alifia katika mwaka 1906. Khalifa mwenyewe alikutana na maadui katika eneo la makao yake, Omdurman, ambako Wasudani walipigana kwa ujasiri mkubwa sana katika vita vya Karari vilivyopiganwa tarehe 2 Septemba, 1898. Kwa mara nyingine tena walishindwa na silaha za maadui ambazo zilikuwa madhubuti zaidi. Karibu Wasudani 11,000 waliuawa na kiasi kama 16,000 walijeruhiwa. Kuanzia wakati huo Khalifa akakimbilia mashariki ya Kordofan ambako aliendelea kuwa kikwazo kwa utawala mpya kwa mwaka wote mzima. Hata hivyo baadaye alishindwa katika vita vilivyopiganwa Umm Diwaykrat tarehe 24 Novemba, 1899. Baada ya vita Khalifa alikutwa amekufa kwenye zulia la ngozi ya kondoo alilokuwa akiswalia – majenerali wengine wote wa Kimahdi ama waliuliwa au walifungwa jela. Huu ukawa ndiyo mwanguko wa dola ya Kimahdi, ingawa Mahdiyya kama dini na mtazamo wa kisiasa haikufa.

## Maasi ya Kimahdi

Ingawa utawala wa kikoloni wa Uingereza ulipiga marufuku madhehebu ya kimahdi sehemu kubwa ya jamii ya Kisudani iliendelea kuwa waumini wa madhehebu hayo kisirisiri. Wengi wao walionyesha kimya kimya kukataa kwao kutawaliwa na Waingereza kwa kuendelea kusoma *ratib* (kitabu cha Mahdi cha Swala) na kufanya tambiko nyingine za Kimahdi. Lakini kundi dogo la waumini wakubwa wa Kimahdi mara kwa mara walijaribu kuunganisha kwa nguvu utawala wa 'hafiri'. Kwa hakika kati ya mwaka 1900 na 1914 ilikuwa vigumu kupita mwaka mzima bila ya kuwepo na maasi ya Kimahdi kaskazini mwa Sudan. Maasi kama hayo yalitokea mnamo mwezi Februari, 1900; katika mwaka 1902 – 3; na katika mwaka 1904. Lakini maasi muhimu kuliko yote ni yale yaliyoongozwa na Mwana-Mahdi Abd al-Kadir Muhammad Imam, anayefahamika zaidi kama Wad Habuba. Maasi hayo yalitokea mnamo mwaka 1908. Yeye alihubiri Umahdi katika Djazira; na akiwa katika kambi yake katika kijiji cha Tukur, karibu na Kamlin, alitamka wazi kuwa alikuwa akiipinga serikali. Jeshi la serikali lilipelekwa kupigana naye lilishindwa vibaya sana. Wad Habuba akaamua kuendelea na vita; na mnamo mwezi Mei akawashambulia ghafula maadui katika kijiji cha Katfia. Wana Mahdi walipigana kwa ushujaa lakini ngome ya maasi yao ilivunjwa. Hata hivyo Wad Habuba, akiwa katika kutoroka kama alivyofanya Mahdi, alikwishahama pale, labda katika jitihada za kukimbilia Omdurman. Lakini alikamatwa njiani na akanyongwa hadharani, tarehe 17 mwezi Mei. Wafuasi wake wengi walihukumiwa vifo na wengine kifungo cha muda mrefu.

Ingawa hayakuwa yameratibiwa vizuri na hayakuwa na wafuasi wengi lakini maasi haya ya kimasihi yalileta namna fulani ya mwendeleo katika kipindi cha dola ya Kimahdi na Kuthibitisha kwamba Umahdi ulikuwa hai bado na kwamba ulikuwa nguvu muhimu ya kidini na kisiasa katika Sudan. Tena basi, maasi haya yalidhihirisha kuwa nia ya kuupinga utawala wa kikoloni ilikuwa bado imara katika mioyo ya Wasudani wengi wa Kaskazini.

## Shughuli za Upinzani katika milima ya Nuba na Sudani Kusini

Watu wa Milima ya Nuba na Sudan kusini nao halikadhalika walipinga vikali mgawanyo na utawala wa Wazungu. Ijapokuwa majeshi ya kikoloni yalifanya ukatili mkubwa lakini bado jamii mbalimbali za Kinuba zilijishughulisha sana katika kuupinga utawala wa Mwingereza. Wakati Ahmad al-Numan Mek wa Kitra, alipotangaza wazi chuki yake juu ya Mwingereza wananchi wa Talodi nao walianzisha maasi katika mwaka 1906: maasi ambayo yalisababisha kuuliwa kwa maofisa kadhaa wa kiserikali na maaskari. Maasi makubwa zaidi yalikuwa yale ya *mek* Faki Ali wa vilima vya Misri. Ali aliyatia wasiwasi majeshi ya serikali kwa muda wa miaka miwili lakini alikamatwa katika mwaka 1916 na akafungwa huko wadi Haifa.

Katika eneo la kusini upinzani uliongozwa na kuendelezwa kwa muda mrefu na Wanueri walioishi katika nchi inayounganisha mto Sobati na White Nile. Chini ya utawala wa nyuma Wanuer walizoea kuongoza mambo yao wenyewe kwani tawala hizo hazikuwa na usimamizi mkali juu yao. Lakini sasa Wanueri walikataa kuitambua nguvu ya serikali mpya na wakazidi kuonyesha chuki juu yake. Viongozi wao wawili Degkur na Diu ndio waliokuwa mstari wa mbele kabisa katika suala hili. Ingawa viongozi hawa maarufu walifariki (Dengkur 1906, Diu 1907) harakati za Kinueri hazikufa na katika mwaka 1914 kiongozi mwingine wa Kinueri, Dowl Diu, alimshambulia mjumbe wa serikali. Ingawa kulikuwa na hatua kadhaa za adhabu kali upinzani wa Wanueri uliendelea kupata mashiko mpaka ulipotokezea kuwa maasi maarufu ya Wanueri ya mwaka 1927.

Waazande, chini ya Uongozi wa Chifu wao, Yambio, pia walikuwa wamedhamiria kabisa kuyazuia majeshi yoyote ya kigeni yasiingie nchini mwao. Walikabiliwa na hatari ya uvamizi wa Wabelgiji na serikali ya Wakondomini. Yaelekea Yambio aliogopa zaidi uvamizi wa Wabelgiji kuliko ule wa Waingereza. Kwa hivyo akaonelea kwamba ilikuwa bora kuondoa tofauti baina yake na Waingereza kwa kufanya urafiki nao ili aweze kupata msaada wa kuishughulikia hatari dhahiri ya Wabelgiji iliyokuwa ikimkabili. Akawakaribisha Waingereza kuanzisha kituo cha kufanyia biashara katika ufalme wake. Mwaliko huo ulifanywa kwa imani kwamba Waingereza wasingeweza kuja na kwamba kama wangekuja angeweza kupigana nao.

Lakini Waingereza waliukubali mwaliko huo na mnamo mwezi Januari, 1903 kundi la askari liliondoka Wau kuelekea nchi ya Yambio. Wakati wakiwa safarini hawa wakashambuliwa na Wazalendo, wakakimbilia Rumbek. Mnamo mwezi Januari, 1904 serikali ya Khartoum ikatuma kundi jingine la askari. Hili nalo lilishambuliwa na Waazande na likalazimika kurudi nyuma na kukimbilia Tonj.

Wakati Wabelgiji wakijitayarisha kuivamia nchi ya Yambio, Yambio naye alitayarisha jeshi la Waazande 10,000 ambalo kwalo alithubutu kukishambulia kituo cha Wabelgiji kilichokuwa Mayawa. Kwa ujasiri mkubwa Waazande wakawapa taabu maadui lakini hawakuweza kuzihimili bunduki zao kwa kutumia mikuki tu. Vita hivi vilidhoofisha sana mioyo na nguvu za kivita za Waazande. Akiwa na jeshi lililodhoofika sana Yambio alilazimika kukumbana na jeshi la uvumbuzi la serikali mnamo mwezi Januari 1905. Mwishoni alishindwa akakamatwa na kufungwa jela. Hakuchukua muda mrefu akafariki tarehe 10 Februari, 1905. Hata hivyo watu wake waliendeleza mapambano. Katika mwaka 1908 baadhi ya askari wa Yambio walijaribu kuchochea maasi na wakati huohuo wengine walipigana na Waingereza katika vita vya Kwanza vya Dunia.

## *Nchi ya Somali*

Majibu ya Wasomali dhidi ya mgawanyo 1884 - 97

Kuanzia katikati ya karne ya kumi na tisa nchi ya Somalia kwa haraka ilianza kuwa uwanja wa mashindano ya ukoloni wa Wazungu kati ya Italia, Uingereza na Ufaransa. Kutokana na kuwa na maslahi katika India na sehemu nyingine za Asia, Uingereza na Ufaransa zilikwishajiimarisha katika pwani ya Somalia mapema kwenye miaka ya 1880. Nchi hizi mbili zilifuatiwa na Italia na kila moja ikaingiza athari zake bara. Katika mwaka 1885 Wafaransa walitangaza kwamba eneo la Somalia walilokuwa wakiwasiliana nalo litakuwa chini ya ulinzi wao. Mnamo mwaka 1887 Waingereza nao wakafanya hivyo hivyo; Waitalia nao wakatangaza kuwa miji ya Brava, Merca, Mogadishu, Warsheikh na baadaye Obbia na Somalia ya Midjurteyn kaskazini ilikuwa chini ya ulinzi wao. Ethiopia pia ilikuwa imepanuka hadi kufikia Somali, ikachukua maeneo ya kuishi watu na ikaweza kuanzisha utawala katika majimbo ya Haud na Ogaden. Mgawanyo wa Somalia ulimalizika rasmi katika mwaka 1897.

Masultani na machifu wa Kisomali hawakuuachia kwa hiari utawala wao; na kwa hakika wao walikuwa viongozi wa baadhi ya ukinzani na maasi mengi ya wananchi dhidi ya ubeberu wa Wazungu katika kipindi cha mgawanyo. Wakiwa wanajna ushindani uliokuwepo kati ya mataifa ya Kizungu katika upanuzi wa makoloni, machifu wa Kisomali walijaribu kuwashindanisha kwa kufanya makubaliano na ama huyu au yule. Kwa mfano machifu wa Kisomali walifanya mikataba mingi na Waingereza. Lakini hatimaye mikataba hii ilishindwa kufikia lengo lake kwani mataifa haya ya Kizungu yalipatana katika ugomvi wa kibeberu kwa amani.

Mbali na jitihada hizo za kidiplomasia baadhi ya koo ya Kisomali ziliamua kupigana vita ili kutetea utawala wao. Waingereza wakatuma makundi manne ya safari ya maaskari: katika mwaka 1886 na 1890 wakapambana na Isa, katika mwaka 1893 wakapambana na Habar Gerhajis na mwaka 1895 wakapambana na Habar Awal. Waitalia pia walipoteza watu wengi. Katika mwaka 1887 kundi la Waitalia liliuawa katika Harar na katika mwaka 1896 kundi la Waitalia kumi na wanne liliuawa na Wabimal. Mapambano ya mara kwa mara baina ya majeshi ya Waethiopia na koo za Kisomali yaliwafanya Wasomali wasiweze kujenga makazi ya kudumu katika Ogaden; wala hawakuweza kupanua utawala wao kuvuka vituo vya kijeshi vilivyosambaa katika eneo hilo.

Vita vya Uhuru wa Somalia 1897 – 1914

Mapambano ya Wasomali dhidi ya wakoloni yalifikia kilele chake Sayyid Muhammad Abdille Hassan alipotangaza *jihadi* dhidi ya ubeberu wa kizungu. Sayyid Muhammad Abdille Hassan alizaliwa mwaka 1864 na baada ya kusoma katika vituo vikuu vya

Kiislamu katika Mashariki ya Afrika, Harar na Mogadishu, na labda sehemu za athari kubwa ya Umahidi huko Kordofan aliamua kwenda kuhiji huko Maka katika mwaka 1895. Alikaa Arabuni Maka alisomeshwa na Shaykh Muhammad Salih na akaamua kujiunga na madhehebu yake, yaani Salihiyya. Yawezekana muda mrefu aliokaa huko ng'ambo na safari mbalimbali za Kiislamu vilimfanya Sayyid huyu kupata mawazo ya kuhuishwa kwa Uislamu, mawazo ambayo yalikuwa viongozi wengine wa kidini naye pia alikuwa ameathiriwa sana na maongozi ya Mahdi. Aliporudi nyumbani alikaa kwa muda Berbera ambako aliwahubiri wananchi wenzake warejee kwenye njia ya kuuamania kikamilifu Uislamu na kuukataa ukoloni wa Kikristo na elimu ya magharibi.

Kwa kutumia haiba yake kubwa na uongozi wake madhubuti, na hasa kwa kutumia mashairi mengi aliyotunga mwenyewe na ambayo mengi yake bado ni maarufu nchini kote Somalia mpaka hivi leo, al-Sayyid aliweza kabisa kuwaunganisha, kuwatia hamu na kuwavuta katika Uislamu wananchi wenzake wengi. Hawa wakawa walinzi wakubwa wa Uislamu na wakaunda jeshi lililokadiriwa kuwa la askari 12,000.

Al-Sayyid alianzisha *jihadi* yake huko Berbera ambako kati ya mwaka 1895 na 1897 alijaribu kuwahamasisha watu wapinge mabeberu. Lakini kitendo chake cha kwanza cha mapinduzi kilikwa utekaji wa Burao katikati ya Usomali ya Waingereza mnamo mwezi Agosti, 1899. Waingereza walisumbuliwa sana na tukio hili kiasi kwamba kati ya mwaka 1900 na mwaka 1904 walituma misafara minne ya askari kuyafukuza mashambulizi ya Al-Sayyid. Ingawa Waingereza walisaidiwa na Waitalia katika Vita hivi uhodari wa kipekee wa kivita aliokuwa nao al-Sayyid na kufanikiwa kwake katika kuitumia misafara na mbinu mbalimbali za vita ya msituni viliwapa ushindi kadhaa askari wake. Mojawapo ya ushindi huu ni ule uliotokea *Gamburu Hill* ambako maofisa tisa wa Kiingereza waliuawa katika mwezi Aprili, 1903.

Hata hivyo, hadi kufikia 1904 jeshi la Sayyid lilikuwa limekwisha dhoofishwa sana. Kwa hiyo alirudi nyuma akaenda katika eneo la Midjurteya, lililokuwa chini ya ulinzi wa Waitalia, ambako tarehe 5 Machi 1905 alitia saini mkataba wa Illing na Waitalia na akatoa masharti yake. Hadi kufikia mwaka 1908 al-Sayyid alikwishatayarisha majeshi yake kuanzisha upya mapambano ambayo yaliwalazimisha Waingereza kuondoka bara, mwezi Novemba, 1909, na kuelekeza nguvu zao pwani. Lakini al-Sayyid alitishia kuishambulia miji ya pwani pia. Mnamo mwezi Agosti, 1913 alipata ushindi mkubwa alipowashambulia vikali askari wa ngamia waliokuwa wameanzishwa punde tu. Baa hili liliwalazimisha Waingereza kuendelea kupigana na al-Sayyid mpaka alipofariki mwezi Novemba, 1920. Ingawa *jihadi* hii ya Wasomali hatimaye ilishindwa kuuondoa utawala wa kigeni katika nchi yao lakini ilijenga hisia na moyo wa uzalendo miongoni mwa watu. Wasomali wakajiona kuwa kitu kimoja kinachopigana dhidi ya maingiliano ya wageni. Aidha mapambano ya Sayyid Muhammad yalilifanya taifa la Kisomali lizindukane na kuwa na uzalendo ambao usingeweza kufutwa na ambao uliwatia mori watu na vizazi vya baadaye.

## *Hitimisho*

Pengine hakuna sehemu katika Afrika ambako kutamalaki na kutawala kwa Wazungu kulipingwa kwa nguvu zaidi katika kipindi cha 1880 – 1914 kama ilivyokuwa katika sehemu ya kaskazini – mashariki ya bara hili. Hii inathibitishwa na maelfu ya Wamisri, Wasudani na Wasomali waliopoteza maisha yao katika vita mbalimbali vilivyopiganwa baina yao na majeshi ya Wazungu. Nguvu ya ukinzani huu inatokana na ukweli kwamba mbali na hisia za kizalendo zilizoichochea kulikuwa na hisia nyingine yenye nguvu kubwa zaidi, yaani imani ya kidini. Watu wa Misri, Sudan na Somalia hawakuwa tu wakipigana kulinda miili yao bali pia kuilinda dini. Waislamu wa sehemu hizi, kama walivyo waumini wa Kiislamu wengine kwingineko, walikuwa na hadhari juu ya ghasia za kijamii na za kidini ambazo zingeweza kuletwa na majilio ya wageni katika nchi za Kiislamu. Pia ilikuwa kinyume cha Uislamu kwa jamii ya Kiislamu kutawaliwa Kikristo. Kwa hiyo vyama vya kimapinduzi vya Urabi, Mahdi, na Sayyid Muhammad shurti vitazamwe katika muktadha wa vyama vya kuujenga upya Uislamu ambavyo vilisambaa na kuathiri vikubwa ulimwengu wa Kiislamu katika karne za kumi na nane na kumi na tisa.

# 5 Juhudi na Ukinzani wa Waafrika: Afrika Kaskazini na Sahara


Utamalaki na ukaliaji wa dola za Afrika Kaskazini za Moroko, Algeria, Tunisia na Tripoli (Libya) uliofanywa na wazungu ulifanyika katika nyakati tofauti tafouti. Ingawa Algeria ilitamalakiwa na Wafaransa mapema mwaka 1830 na eneo lizungukalo Melilla huko Moroko likatamalakiwa na Wahispania mnamo mwaka 1860, ni hadi mwaka 1881 ndipo Tunisia ilipotamalakiwa na ufaransa hali Libya na Moroko hazikutamalakiwa na Italia na Ufaransa hadi kati ya 1911 na 1934. Hata hivyo, kulingana na juhudi na matendo ya Waafrika, matukio haya yote yalikuwa sawa katika kipindi chote kizma. Yote yalitokea kama luteka la kiplomasia, lakini zaidi kama ukinzani wenye kutumia silaha kulinda umamlaka na uhuru wao.

## *Tunisia*

Katika Tunisia, mara tu baada ya Wafaransa kutamalaki nchi hiyo na kumlazimisha Beya kutia sahihi mkataba wa kulindwa na wafaransa mnamo Mei 12 1881, wakazi wa Sahel na wale wa makao makuu ya kidini ya Karyawan, waliasi. Wafaransa walilazimika kufanya mashambulio mengine ambayo yalipingwa vikali katika maeneo ya milimani ya kaskazini-magharibi, katikati na kusini. Ilibidi miji ya Safakas na Kabis ipigwe mabomu na vikosi vya majini hali maji na Kayrwan ulistahimili mazingiwa ya muda mrefu katika kipupwe cha mwaka 1881. Lakini baada ya ukinzani wote huu kushindwa, sehemu za kusini mwa Tunisia karibu na Tripolitania hazikuwa na usalama kwa muda mrefu.

## *Moroko*

Katika Moroko, serikali ya nchi hiyo kwa karne nyingi ilikuwa akiwapiga Wahispania ambao walikuwa wamekwishajiimarisha *Ceuta* na Melilla. Nchi hii kila mara iliwakataza wakazi wake kutojihusisha na Wahispania hao, na ni kwa haja ya kutaka kuvunja vikwazo hivi ndipo Uhispania ilianzisha vita vya 1859 - 1860 ambavyo vilikuwa vya uharibifu mkubwa kwa Moroko. Nchi hii ililazimishwa kulipia faini kwa kukubali upanuzi wa sehemu ya mji wa Melilla iliyozungusha ngome na kuiacha sehemu katika pwani ya Atlantiki kama kimbilio kwa wavuvi kutoka Visiwa vya Canary. Kutokana na kuchakuliwa kwa Ghuba ya *Rió De Oro* ambavyo ilani ya kukaliwa kwakwe ilitolewa kwa watia saini wa Mkataba wa Berlin mnamo Desemba 26, 1884, Uhispania, hadi mwishoni mwa karne hiyo, ilikuwa na ngome tatu katika




5.1 *Kanda Kuu za Magharibi na Sahara*

pwani ya Afrika Kaskazini, Katika mwaka 1880 na mwaka 1881 Mkutano wa Madrid kuhusu ulinzi wa watu katika Moroko ulipokutana kwenye vikao viwili, Makhezen ilifanya jaribio la mwisho la kupata uhuru na umamlaka wake juu ya nchi yenye mipaka ya wazi inayokubalika kimataifa. Ingawa liliungwa mkono na Waingereza jaribio hili lilishindwa kutokana na muungano wa kichoyo wa Wafaransa, Wahispania na Waitalia. Ufaransa ikaleta katika majadiliano tatizo la Tuwat, lakini kwa kuungwa mkono na Waingereza, Sultani wa Moroko alikataa madai ya Wafaransa na wakati huohuo akaimarisha kuwepo kwake kiutawala na kisiasa katika Tuwat.

Hata hivyo, mnamo Desemba 1899, kwa kutumia kisingizio cha uvumbuzi wa kisayansi, kikosi imara cha Kifaransa kilipelekwa In Salah na kuwataka wakazi wa mji huo kusalimu amri mara moja. Chifu aliyeteuliwa na Sultani wa Moroko akisaidiwa na askari wa Makhzen na masherifu wa In-Salah walipinga vikali uvumizi huo. Baada ya vita vikali kama vile vya In Ghar mnamo Desemba 1899, ambapo matokeo yalikuwa dhahiri kutokana na kutolingana kwa sehemu zilizohusika, kanda nzima ya maoasisi ilitekwa; mapigano ya mwisho yalitokea Talmini mnamo Machi 1901. Uingereza na Ujerumani zilimshauri sultani kijana Abd al-Azizi kukubali matokeo, naye akafanya hivyo: bila hiari akatia sahihi mkataba Aprili 20, 1902. Hat hivyo kama fidia kuwa makubaliano haya, alijaribu bila kufaulu, kutaka iwekwe mipaka ya wazi kusini na mashariki kati ya Moroko na sehemu zilizomilikiwa na Ufaransa kwa kuwa Wafaransa walipendelea utata uliowapa mwanya wa kuendeleza utamalaki wao.

Kutekwa kwa Tuwat kulikuwa mojawapo ya sababu za kuporomoka kwa mamlaka ya Sultani; hali ambayo ilizidi kudidimia hadi mwaka 1911. Makhezen alijua kuwa Ufaransa ilipanga kuizingira Moroko ili iitenge na kuitawala; alijua pia kwamba Uingereza ilikuwa haipingi tena hila za Ufaransa. Mabadiliko aliyoyafanya nyumbani ili kuimarisha jeshi na utawala hayakuwa na matokeo yaliyotazamiwa. Haikutegema kitu chochote kingine kutoka Ujerumani zaidi ya msaada wa kidiplomasia; na kwa kweli Ujerumani ilitetea uhuru wa Moroko hadi mwaka 1911 ilipotia sahihi makubaliano na Ufaransa kuruhusu nchi hii kufanya chochote Moroko na yenyewe kufidia huko Afrika ya Ikweta.

Baada ya mwaka 1905 Ufaransa ikaamua knzidisha kasi ya kuhimiza mambo na kukalia *bilad al-siba.* Haya yalikuwa maeneo maskini ya jangwa na yenye wakazi wachache ambayo kutokana na hali hiyo ya umaskini sultani aliacha yatawaliwe na machifu, lakini bila kufuta haki zake na mamlaka. Mara kwa mara aliarifiwa juu ya hila za kikoloni, iwapo kulitokea tishio dhahiri alituma mwakilishi wake kuongoza ukinzani. Hatua kama hii ndiyo ilichukuliwa katika eneo la Kenedza na katika Shiakit.

Kutokana na kukataa kwake siku zote kuwekeana mpaka na Moroko zaidi ya Figuig, Ufaransa ilifuata sera ya kumega nchi polepole. Yakielekea juu kwenye bonde la Sumra, majeshi ya Kifaransa yaliikalia nchi kati ya Wadi Gir na Wadi Zusfana kwa kisingizio cha kukomesha fujo na hali ya kukosekana kwa usalama na kuruhusu biashara ya mpakani kupanuka. Serikali ya Ufaransa pia ilitoa pendekezo kwa *Makhzen* kuwa wagawane mapato ya forodha, na hili lilikubaliwa mnamo Machi 1910.

Kusini zaidi, Ufaransa ilikuwa imelazimisha ulinzi wake juu ya maemir wa Trarza na Brakna. Na mnamo mwaka 1905 bigwa na mambo ya *marabout* kutoka Algeria, Xavier Coppolam, alianzisha sera ya "mpango wa amani", iliyofanyika kwa kuwasiliana moja kwa moja na machifu na viongozi wa dini kwa nia ya kuwashawishi kujumuishwa katika athari za Kifaransa. Katika kufanya hivi alijikuta akipigana na mpinzani mkubwa Shaykh Ma'Aynayn ambaye kwa zaidi ya miaka thelathini alijionyesha kama mwakilishi wa sultani wa Moroko. Taarifa ilipelekwa kwa Mulaya Abd-Aziz naye akamtuma mjomba wake Mulay Idris ambaye aliandaa vikosi vya ukinzani. Wakati huohuo kambi za Coppolani huko Tidjikdja lilishambuliwa mnamo Aprili 1905 na mtume wa "mpenyo kwa amani" akauawa. Ikitumia mizozo ya ndani nchini Moroko, Ufaransa ilitaka Mulay Idris arejeshwe; na hii ilifanyika Januari 1937; hata hivyo ukinzani uliendelea. Kikosi cha askari chenye nguvu kilichoongozwa na Kanali Gouraud kilikwenda kupigana sehemu za Kaskazini; kilishambuliwa na kurudishwa nynma vibaya sana huko al-Moyrian mnamo Juni 16 1908, lakini baadaye kikafaulu kuingia Atar mnamo Januari 9, 1909. Shykn Ma al-Aynayn na wafuasi wake walirudi nyuma hadi Sakiyat al-Hamra ambako waliendelea kuwahangaisha Wafaransa na Wahispania hadi 1933.

Katika kipindi hicho, Uhispania nayo ilifuata mfano wa Ufaransa. Ufaransa ilipokalia Shiukit, Uhispania iliondoka katika makazi yake kwenye ghuba ya Rio de Ora na mamo mwaka 1906 ikaandaa kikosi cha Sahara cha Uingiliaji kati ambacho kilipenya kilometa 30 ndani ya nchi. Huko kaskazini Wahispania walingoja hadi Wafaransa walipoingia Wadja mnamo 1907 kabla ya kuandaa kikosi cha wanajeshi 45,000 ambacho mnamo Septemba kilitoka kwenda kuteka Rif. Kama jibu kwa shambulio hili wenyeji wa sehemu hiyo wakiwa wamehamasishwa na wito wa jihadi uliotolewa na Shaykn Ameziya, walianzisha ukinzani mkali ulioshindwa mnamo mwaka 1926.

Katika maeneo ya Atlas na Sahara kulikuwa na ukinzani mkabwa zaidi. Hadi 1931 sehemu kubwa ya maeneo haya ilikuwa nje ya udhibiti wa kikoloni. Lakini, katika mwaka huo; mabadiliko yalitokea katika sera ya kikoloni ya Ufaransa. Kutokana na kukerwa kwao na kujiimarisha kwa Wajerumani, Waziri wa Vita wa Ufaransa, Massimy, aliutenga mwaka 1935 kuwa mwaka wa mwisho wa kutamalaki nchi. Majeshi katika Afrika yalipewa vifaa vilivyohitajika na mipango ilifanywa kuratibu shughuli za pamoja baina ya Ufaransa na Wahispania; kuanzishwa kwa Jamhuri ya Madrid kulirahisisha uratibishaji huu. Hivyo katika majira ya mchepuo kikosi kiliandaliwa kwenda katika moja ya "vituo vya uhalifu".

Hata hivyo ushindi wa mwisho haukupatikana kwa urahisi. Atlas ya kati ilididimizwa katika mashambulio mawili mnamo 1931 na 1932; kutoka Julai 12 hadi Septemba 16 16 ya mwaka huo wa nyuma mapigano makali ya Tezikazaut yalitokea. Jeshi la Ufaransa liliwazingira watu wa familia 3000 ambao walikuwa wameanza kurudi nyuma kabla ya kusonga mbele kwa ukoloni tangu 1922. Mapigano haya yaliendelea toka Agosti 22 hadi Septemba 11. Ukinzani mkali ulioongozwa na Al-

Wakila Amhouch na ndugu zake haukuweza kuvunjwa kwa upigaji mabomu wala vikwazo. Ilibidi vibanda visafishwe kwa makombora. Mapigano yalipokwisha, Wamoroko 500 walikuwa wameuawa. Mnamo 1933 ilifika zamu ya Djabal Saghuru, ambapo mapigano ya Bu Ghafir (Februari 13 hadi Machi 25) nayo yalikuwa makali sana. Mnamo mwaka 1934 Wapiganaji wa mwisho upande wa ukinzani walizingirwa katika Ati-Atlas na baada ya hapo Wafaransa waliingia Tinduf mnamo mwezi Machi. Wahispania waliteka Sidi Ifni wiki moja baadaye mnamo mwezi Aprili 6 1934.

## Libya

Lakini pengine hapana sehemu nyingine ambako mapambano baina ya Waafrika na Wazungu yalikuwa ya muda mrefu, makali na ya kikatili kama yalivyokuwa Libya. Mnamo Oktoba 1915, Italia ghafla iliivamia Libya chini ya utawala wa Waturuki na kuteka miji ya Tripoli, Benghazi, Homs na Tubruk. Hata hivyo Waitalia walipotoka nje ya mipaka ya mji, walikutana ukinzani mkali. Mfululizo wa mapigano ulitokea nje ya miji kama vile: al-Hani mnamo Oktoba 23, 1911 nje ya Tripoli. Waitalia walishindwa vibaya na wakaanza kuwatesa wakazi wa mji wa Tripoli. Nje ya Benghazi, Waitalia walipigana mapigano makubwa matatu huko Djuliana, al-Kuwayfiya, na al-Hawwari mnamo Novemba 28, 1911. Walishindwa na kulazimishwa kurudi nyuma hadi Benghazi. Huko al-Khumas Waitalia na majeshi ya Waturuki na Waarabu walipigana kwa nguvu zao zote kudhibiti kituo muhimu cha al-Markib kuanzia Oktoba 23, 1911 kabla ya Waitalia kufaulu kuwaondoa mnamo Mei 2, 1912. Huko Derna, kikosi kidogo cha Kituruki kilirudi nyuma hadi kwenye milima iliyokabiliya mji na kikisaidiwa na mwenyeji, kilipigana na Waitalia. Ukinzani huko Derna uliimarishwa na kundi la maafisa wa Kituruki lililofika hapo likiongozwa na Anwar Pasha (Enver) na Mustafa Kamala (aliyejulikana baadaye kama Ataturk). Akisaidiwa na Ahmad al- Sharif kiongozi wa kidini wa Sanusiyya, Anwar na kundi lake (Picha 5.1) waliwahamasisha Waarabu wa bara na wakafaulu kuunda jeshi la kutisha.

Anwar aliongoza jeshi hili katika mapigano mawili dhidi ya Waitalia huko al-Karkaf na Sidi 'Abdallah mnamo Oktoba 8, 1912 na Machi 3, 1912. Huko Tubruk Waarabu walikutana na Waitalia katika mapambano makubwa mawili huko al-Nadura mnamo Machi, 3, 1912 na al-Mudawwar mnamo Julai, 17, 1912 ambapo Amiri jeshi wa Kiitalia, Jenerali Salsa aliuawa. Ni vigumu kuyaelezea mapigano yote yaliyofanywa dhidi ya Waitalia huko Libya katika historia talii; hata hivyo, inatosha kusema kwamba ndani na kuzunguka kila jiji, mji na mabonde kulikuwa na mapambano dhidi ya waitalia. Ukinzani huu mkali ndio ulifanya Waitalia washike miji zaidi kidogo tu ya ile mitano katika miezi sita ya kwanza ya vita.

Kufikia mwishoni mwa 1911, Waitalia wengi walikuwa wameanza kuonyesha dalili za kukata tamaa kuhusu kipindi cha vita huko Libya. Ili kuibana Uturuki kuondoka Libya, serikali ya Italia ilishambulia Visiwa vya Dodecanese na Dardanelles. Kitendo hiki kipya cha Italia katikati ya Uturuki kilitishia amani ya dunia na kufufua



**5.2** *'Umar al-Mukhatar (b.c. 1862), kiongozi wa ukinzani wa Wasanusi dhidi ya ukoloni wa Kitaliani hadi alipouliwa mwaka 1931.*

*The Eastern Question* (Suala la Mashariki), suala ambalo hakuna utawala wa kizungu uliotaka lizuke kwa sababu ya utatanifu wake. Kwa hiyo tawala kuu za Kizungu zilizibana Uturuki na Italia kuafikiana kwa amani na zilifaulu kuishawishi, kama sio kuilazimisha, Uturuki kutia sahihi Mkataba wa Lausanne na Italia mnamo Oktaoba 18, 1912. Kulingana ua mkataba huu, Uturuki iliwapa uhuru wananchi wa Libya ili kujiondoa katika lawama za Dunia ya Kiislamu na kwa upande wake, Italia iliahidi kuondoa majeshi yake kutoka maeneo ya Bahari ya Uturuki.

Jibu la Walibya kuhusu mkataba wa amani ambao haukuwashirikisha halikuwa moja. Baadhi walitaka kufanya mazungumzo na Waitalia hali wengine walitaka kupigana hadi mwisho. Watu wa Cyrenaica chini ya kiongozi wao wa kidini Ahmad al-Sharif walikuwa upande wa wale waliotaka mazungumzo ya amani.

Wakitumia fursa ya kuondoka kwa Waturuki toka Libya, Waitalia walishambulia majeshi ya Ahmad al-Sharif kusini mwa Derna lakini wakashindwa vibaya kwenye mapigano ya Tawn al-Djumia mnamo Mei 16, 1913, Mapigano haya yalikuwa muhimu sana kwa sababu ndiyo yalikuwa pambano kubwa la mwanzo kati ya Waarabu na Waitalia baada ya kuondoka kwa Waturuki. Akikariri amri iliyotolewa na Sultani wa Uturuki iliyotoa uhuru kwa Walibya, Ahmad al-Sharif alitangaza kuundwa kwa serikali iliyojulikana kama "al-Hukuma, al-Sanusiyya", serikali ya Sanusi. Hivyo mnamo siku kabla ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, Walibya walikuwa wamefaulu kuwapinga Waitalia na walikuwa wakidhibiti maeneo makubwa ya nchi yao.

Hata hivyo, baada ya vita Waitalia walianzisha tena mashambulio yao huko Libya na kuvamia maeneo kadhaa kwa ajili ya "reconquisita" mnamo 1922. Jeshi kubwa likiongozwa na Jenerali Graziani lilielekea Gharyan, mji mkuu wa Tripolitania ambao ulitekwa Novemba 7, 1922. Jeshi jingine lilishambulia Misurata na kuuchukua mnamo Februari 20, 1923. Kamati Kuu ya Jamhuri ya Muungano iliyoundwa mnamo Januari 1922 ikawa imegawanywa na migogoro miongoni mwa wajumbe wake na vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya Misurata na Warfallah kwa upande mmoja, na ugomvi kati ya Waarabu na Waberiberi wa Milima ya Magharibi kwa upande mwingine, haikuweza kuandaa kikosi cha kutosha kuwazuia Waitalia. Matokeo yake, kamati kuu ilivunjika na wajumbe wake kuikimbia nchi hadi Misri, Sudan na Tunisia. Kuvuruga mambo zaidi, mnamo Desemba 21, 1922 Amir Idris al-Sanusi, kiongozi wa kidini wa muungano na Amiri-jeshi Mkuu aliamua mwenyewe kukimbilia Misri. Kuondoka kwake ghafla kusikoelezeka, snala ambalo bado linajadiliwa na wanahistoria, kuliwakatisha watu tamaa kabisa na kufanya sehemu kubwa ya wapiganaji kuondoka nchini au kujisalimisha kwa Waitalia. Hata hivyo, kabla ya kuondoka, al-Sanusi alimteua ndugu yake al-Rida kama naibu wake na 'Umar al-Mukhtar kama Amirijeshi wa Vikosi vya Taifa katika *Green Mountains*, ambaye chini ya uongozi wake na kwa sababu ya ubingwa wake wa vita vya msituni alioendeleza akaweza kuendeleza ukinzani hadi 1937. Aligawanya majeshi yake katika kombania tatu kubwa (adwar) na kuweka kambi katika sehemu za milima kusini mwa al-Mardj

huko Djardas. Mifululizo ya mashambulio dhidi yake katika majira ya kiangazi ya mwaka 1923 yote ilizuiliwa. Jeshi jingine lililopelekwa kushambulia kambi yake mwezi Machi lilishindwa na kufukuzwa.

Tripolitania ndiyo iliyotekwa kwanza. Kufikia Juni 1924, ardhi yote inayofaa kwa kilimo ilikuwa imekaliwa. Lakini kwa kuwa walijua udhaifu wao wa kutodhibiti jangwa, Waitalia walianza kampeni ya kudhibiti jangwa na hatimaye Fazzan. Mpango huu haukufaulu sana japokuwa zilitumiwa ndege kutupa mabomu na pia hewa ya sumu. Misafara kadhaa ya mashambulizi ya Waitalia ilizuiliwa. Hadi mwaka 1928 Walibya walilizuia jeshi kuu la Waitalia huko Faghrift kusini mwa Surt. Lakini kufikia mwisho wa 1929 na mwanzoni mwa 1930, Fazzan hatimaye ilikaliwa na ukinzani wa Walibya magharibi na kusini ukaporomoka.

Wakati huohuo, ukinzani katika Cyrenaica uliendelea na kufaulu kuwashinda vibaya Waitalia. Mafashisti waliposhindwa kukandamiza mapinduzi ya Umar al-Mukhsar huko Cyrenaica kwa mashambulizi ya kijeshi, waligeukia hatua ambazo zilikuwa hazijawahi kutokea katika historia ya vita vya kikoloni barani Afrika. Awali kabisa walijenga ua wa seng'enge wenye urefu wa kilomita 300 katika mpaka wa Tripoli na Misri kuzuia msaada wowote kutoka Misri. Pili, kutokana na kuendelea kwao kuimarishwa, walikalia maoasis ya Djalo, Djaghabub na Kufra ili kuwazingira na kuwatenga wapiganaji katika Cyrenaica. Hatimaye, waliwahamisha wakazi wote wa vijijini wa Cyrenaica hadi katika jangwa la Sirt ambapo waliwaweka kwenye makambi ya wafungwa yaliyojengewa ua. Hatua hii ilinuiwa kuzuia majeshi ya al-Mukhtar yasipate msaada wowote kutoka kwa wenyeji. Magereza mangine ya watu wengi wa makambi ya wafungwa yalianzishwa huko al-Makrun, Suluk, al-Aghyla na al-Barayka. Hali katika makambi haya zilikuwa mbaya mno hata kufanya iaminike kwamba zaidi ya watu laki moja walikufa humo kwa njaa na magonjwa, achilia mbali mifugo yao ambayo ilichukuliwa kwa nguvu. Katika kambi la gereza la huko al-Baryka peke yake kulikuwa na watu 80, 000 ambao miongoni mwao 30, 000 yasemekana walikufa kati ya 1930 na 1932 kwa mujibu wa takwimu za Waitalia wenyewe.

Hata pamoja na hatua hizi kali, uasi uliendelea. Zikaanza kutumiwa mbinu za kuvamia na kukimbia. Waitalia walikubali tena kufanya mazungumzo na al-Mukhtar. Mfululizo wa mikutano ilifanyika kati ya pande hizo mbili. Miongoni mwa mikutano hiyo ni ile iliyofanyika karibu na al-Mardj muamo Julai 19, 1929 na kuhudhuriwa na Gavana na Badoglio. Katika mkutano huu Waitalia walikubali kumhonga al-Mukhtar ambaye alikataa hongo hiyo na kusisitiza ukombozi wa nchi yake. Baadaye al-Mukhtar alipogundua kuwa Waitalia walikuwa wakijaribu kutumia sera ya "wagawanye uwatawale" miongoni mwa wafuasi wake, alivunja mazungumzo na Waitalia na kuanzisha tena mbinu za vita vya misituni zilizojumuisha mapigano madogo-madogo, uvamizi, mavizio, na mashambulizi ya ghafla nchini kote. Hat hivyo mnamo Septemba 1931, al-Mukhtar alitekwa na kupelekwa Benghazi. Baadaye alihukumiwa kijeshi na kunyongwa mbele ya maelfu ya Walibya katika mji wa Suluk septemba 16, 1931.

Baada ya kutekwa al-Mukhtar, wafuasi wake walimchagua Yusuf Abu Rahil,

naibu wake, kama Amiri jeshi. Aliendeleza mapambano kwa miezi sita na baadaye akaamua kuacha na kwenda Misri. Aliuawa alipojaribu kuvuka mpaka wa Libya na Misri. Mnamo Januari 24, 1932 *Badoglio* alitangaza kutekwa na kakaliwa kwa Libya na huu ukawa mwisho wa mojawapo ya ukinzani wa muda nırefu sana dhidi ya ubeberu wa Kizungu.

## *Kushindwa kwa juhudi na Ukinzani wa Waafrika*

Hata pamoja na makusudio makubwa ya watu wa Maghreb kudumisha mamlaka yao na namna yao ya maisha, na hata pamoja na ukinzani kuwa wa muda mrefu, eneo lote la Maghreb liliingia mikononi mwa mabeberu, wa Kifaransa, Kihispania na Kiitalia kufikia mwaka 1935. Swali la mwisho la kuchunguzwa ni kwa nini watu wa Maghıeb walishindwa.

Kinyume na kile kilichoweza kufikiriwa mambo kama idadi ya watu, hali za nchi na za uchumi ndiyo mambo ambayo mara nyingi yalikinzana na maslahi ya wapinzani wa Afrika kaskazini.

Tunajua sasa kwamba idadi ya watu wa Afrika kaskazini ilifanyiwa makadirio ya juu mno katika karne ya kumi na tisa. Watu waliokuwa wa umri wa kutosha kubeba silaha walikuwa wachache na pia walipatikana tu kwa nıuda mfupi kwa sababu walihitajika katika shughuli za kilimo na ufugaji; na hii iliziachia nafasi juhudi za adui. Tidikelt ulitekwa na kikosi cha watu 1000 hali ulikuwa na wakazi wasiozidi 20, 000. Huko Tit mnamo Mei 7, 1902, Twarik wa Wahaggar waliposhindwa, uwiano ulikuwa wa watu 300 kwa 130; lakini hii ndiyo idadi kubwa waliyoweza kukusanya, na kifo cha watu 93 kilikuwa pigo kubwa mno kwao. Maeneo ya nyanda za juu, ambayo yalifikiriwa kuwa na watu wengi zaidi, yalikuwa na hali nzuri kidogo, katika kila pambano lililofaulu washambuliaji walisaidiwa na idadi yao. Watu wa Rif walishambuliwa na askari 300, 000 wa Kifaransa (bila kuhesabu Wahispania) - yaani idadi inayolingana na ile ya watu wote wa Moroko ya kaskazini. Katika kilele cha ukinzani katika atlas ya Kati jumla ya Watu 10,000 wakiwamo wanawake na watoto walikabiliana na jeshi la watu 80, 000. Katika Djabal Saghru askari 7,000 walishambuliwa na watu 34,000 wenye silaha zilizotengenezwa nyakati hizo. Ni jambo la kukiri kwamba si wanajeshi wote wa kikoloni walikuwa wapiganaji, lakini ni kweli kwamba kwa kutazama tu idadi, majeshi ya kikoloni yaliyojiandaa kwenda kuwashambulia "wenyeji kwa vitisho na kuwakatisha tamaa" yalikuwa na watu wengi zaidi.

Mara nyingi hufikiriwa kwamba wapiganaji wenyeji hufaidika na mbinu za miondoko na ujuzi wa mazingira; lakini mbinu hizi zilizidi kupungua umuhimu vita vilivyozidi kuendelea. Ujasiri ulionyeshwa huko Tidjikdja mnamo Juni 1905, ambako Xavier Copplani aliuawa na ambao ulicheleweshа kutekwa kwa Adrar hadi 1909; mapigano ya Kasiba tangu Juni 8 hadi 10, 1913 ambako Wafaransa 100 walikuawa na 140 kujeruhiwa; wa mapigano makali zaidi huko al-Hari mnamo Novemba 13, 1914

walipouawa 510 na 176 kujeruriwa; mapigano ya Anwal tangu julai 22 hadi 26, 1921 ambapo waliuawa Wahispania 15,000, na 700 kuchukuliwa mateka na pia kupoteza bunduki 20, 000 za aina ya *rifle*, 400 za aina ya *machinegun* na 150 ya aina ya 'fieldgun'; ushujaa wote huu wa matumizi ya ajabu ya silaha (ukionyesha ujuzi wa kushangaza wa mazingira na ulioathiriwa na miondoko na ukatili katika mapigano) ulikomesha ushindi wa wakoloni kwa miaka michache lakini haukusaidia katika kurudisha nchi iliyotekwa. Si wakazi wa jangwa wala wale wa nyanda za juu waliweza kuacha shughuli zao za kilimo na ufugaji; na hii iliwaruhusu wavamizi kuwaingiza katika vita halisi vya kiuchumi. Wakati wa mapambano ya Adrar mnamo 1909 askari wa Kifaransa walikalia maoasis katika kipindi cha kuvuna tende na kungojea watu walazimishwe na njaa kuja na kusalimu amri (ingawa si kwa muda mrefu). Katika maeneo ambako uhamaji wa mifugo kufuatana na majira, ulifanyika, walifunga sehemu za malisho ya majira ya baridi na kutegemea baridi na njaa kuwalazimisha wenyeji kukubaliana na masharti yao. Mapigano yalipoanza vikwazo kamili viliwekwa, kama ilivyokuwa dhidi kya Zayyan mnamo 1917 - 8 na dhidi ya watu wa Rif mnamo 1925 - 6. Mnamo 1928 - 9, Waitalia, kama ilivyokwisha onyeshwa juu, waliwahamishia kaskazini watu wa Cyrenaic na kuwakusanya katika kambi za seng'enge zenye miiba. Mojawapo ya matokeo ya njaa hii ya mzazano, ambayo ilidhuru zaidi mifugo kuliko watu, ilikuwa ni kufanya watu wengi wajitolee kujiunga na jeshi la kikoloni kila baada ya mapigano.

Baada ya muda, ile rasimali kubwa waliyokuwa nayo wapiganaji wakinzani, yaani miondoko wakati wa mapigano nayo ilizidi kutokuwa na hakika. Tangu 1901 na kuendelea majeshi ya Kifaransa yalianza kutumia ngamia wa mbio vizuri sana hata kufanya kutekwa kwa Sahara kuelezwe kuwa kulitokana na wendesha ngamia wa Sha'amba. Njia ya reli pia ilijengwa kabla ya utekaji karibu katika sehemu zote; ilifika Ayn Sifra mnamo 1887, Bishar mnamo 1905 na Ziz mnamo 1930. Mnamo 1915 motokaa zilijaribiwa kwa mara ya kwanza na malori ya Epinat yaliendeshwa katika barabara za Altas kwa matarajio ya mapigano ya 1931 - 3. Mwisho, ndege zilitumiwa tangu 1920 na kuendelea, kwa upigaji wa picha toka angani kwa ajili ya maandalizi ya mapigano na kwa kuwakatisha tamaa wenyeji wakati wa mapigano.

Hii hutufikisha kwenye tatizo la silaha ambazo kwa kuwa zilikuwa hazitengenezwi mahali hapo ilibidi zipatikane toka kwa adui. Ufaransa kila mara ililifanya suala la kimataifa magendo ya silaha kwenda Maghreb, ikizishitaki Ujerumani na Uturuki kuwa wauzaji wa silaha hizo na Uhispania na hata Uingereza kwa kuruhusu upitishaji wa silaha katika Pwani za Rif na katika pwani ya Atlantiki kwa ajili ya Moroko na kupitia maoasis ya Libya kwa ajili ya Tunisia na Shara ya Kati. Ni kweli kwamba upitishaji huu wa silaha ulifanyika siku zote; hata hivyo ukweli upo pia kwamba Wafaransa wenyewe walikuwa hawajawahi kushika silaha za Ujerumani huko Atlas ya Kati au Anti-Atlas. Kila koo moja kubwa ilipolazimishwa kujisalimisha, ilipeleka bunduki zake kwa majirani waliokuwa huru bado, na ni mwishoni mwa mapigano hapo Machi 1934 ndipo Ufaransa ilipogundua idadi kubwa kabisa ya silaha

yenye kufikia 25,000. Tukumbuke kwamba silaha hizi mara nyingi hazikuwa na kazi kwa kuwa zilikosa zana kama risasi na baruti, na zaidi ya yote haikujulikana ni kwa kiasi gani zilifaa dhidi ya ndege, mizinga ya masafa marefu na deraya ambazo majeshi ya uvamizi yalikuwa nayo baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Hii ndiyo iliyowafanya majemadari wa Kifaransa kusema kwamba mapigano ya 1931 - 4 ndiyo yalikuwa luteka zenye adui hai.

# 6

# *Juhudi na Ukinzani wa Waafrika: Afrika Magharibi 1880 - 1914*

Kama inavyodhirihika katika sura ya pili katika kipindi cha 1880 - 1914 Afrika ya Magharibi, yote isipokuwa Liberia, ilitawaliwa na wakoloni. Jambo hili, ambalo kwa kweli lina maana kwamba Waafrika walipoteza Uhuru wao na nchi yao, lilitokea kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilidumu kuanzia 1880 hadi miaka ya mwanzo ya 1900, na ya pili kuanzia miaka ya mwanzo ya 1890 hadi mwanzo wa Vita Vikuu vya Kwanza mnamo 1914. Kila moja ya awamu hizi ilishuhudia shughuli tofauti za Wazungu ambazo zilileta juhudi na ukinzani kwa upande wa Waafrika.


Katika awamu ya kwanza Wazungu walitumia ama diplomasia au uvamizi wa kijeshi au vyote viwili. Huu ndio wakati mikataba ya kila aina ilipofanywa karibu katika eneo lote la Afrika ya Magharibi, mikataba ambayo mara nyingi ilifuatiwa na uvamizi wa kijeshi, kutamalaki na kukaliwa na majeshi ya aina na namna mbalimbali. Kwa kweli haijawahi kutokea katika historia ya Afrika nchi kuvamiwa kijeshi na kukumbana na vita dhidi ya dola na jamii zake kama ilivyotokea katika kipindi hicho (taz. mchoro 6.1.1).

Katika awamu hii ya kwanza, karibu Waafrika wote walikuwa na lengo moja, nalo lilikuwa kuutetea uhuru wao na mila na desturi zao. Lakini njia zilizotumiwa zilikuwa tofauti. Waafrika walikuwa na mambo matatu ya kuchagua: ama kupigana, au kufungamana na maadui kirafiki au kukubali na kuridhika na kutawaliwa.

Mkakati wa kupigana ulijumuisha vita bayana, mazingira, vita vya msituni, uchomaji moto wa makonde pamoja na diplomasia. Kama itakavyodhihirika hapa chini njia zote tatu zilitumika.

## *Kutamalaki na Ukinzani huko Afrika ya Magharibi ya Wafaransa, 1880 - 1900*

Inadhihirika wazi kutokana na ushahidi uliopo ya kuwa kuanzia 1880 na kuendelea Wafaransa walianzisha sera ya kulikalia eneo lote la Afrika Magharibi, kuanzia Senegal hadi mto Niger na Chad na kuyaunganisha maeneo haya na vituo vyao vya pwani ya Guinea huko Ivory Coast na Dahomey. Utekelezaji wa sera hiyo ulikabidhiwa kwa maofisa wa Jeshi lao la maji. Katika kukalia Afrika ya Magharibi, Wafaransa walitumia njia ya kutamalaki kwa kijeshi badala ya makubaliano ya





**6.1** *Uingiaji wa Wazungu katika Afrika Magharibi, C. 1880 – 1919*

kimkataba kama walivyofanya Waingereza.

Waafrika nao walilikabili jambo hili kwa kutumia mbinu zote walizokuwa nazo yaani kukubali, kufungamana nao na kupigana. Kama itakavyoonekana, watawala wengi sana wa Kiafrika walichagua mbinu ya kupambana kijeshi kuliko kuwaridhia au kufungamana nao na kwa kweli upinzani huo uliendelea kwa muda mrefu sana kuliko katika maeneo mengine ya Afrika ya Magharibi kwa sababu mbili kuu. Sababu ya kwanza tuliyokwishaiona ni kwamba Wafaransa wenyewe waliwavamia kijeshi, jambo ambalo lilichokonoa ukinzani wa kimapambano. Sababu ya pili ni kuwa watu wa huko wengi walikwishasilimishwa, ukilinganisha na wengine wa Afrika ya Magharibi, hivyo, kama Crowder alivyosema, "kwa jamii za Kiislamu za Afrika ya Magharibi, kulazimishwa kutawaliwa na watu weupe kulikuwa na maana ya kuukubali ukafiri, jambo ambalo lisingekubalika kwa Mwislamu Mswalihina". Hivyo wenyeji waliwapinga Wazungu kwa nguvu na bidii zaidi ya wale wasiokuwa Waislamu. Tunaweza kudhihirisha maoni haya kwa kuangalia matukio ya himaya za Senegambia, Tukulor na Manden, na pia matukio ya Dahomey.

## Senegambia

Huko Senegal ambako Wafaransa walikwishaeneza utawala wao kwa kuitamalaki tangu 1854, mpinzani wao mkuu alikuwa Lat Dior Diop, (Dameli) Mfalme wa Kayor. Lat Dior alianza kupambana na Wafaransa tangu 1861 na alikuwa ameazimia kuzuia ujenzi wa reli iliyokuwa ipite katika falme zake. Tarehe 17 Novemba 1882 alituma barua kwa Gavana Servatius akimzuia kuanzisha ujenzi wa reli hiyo hata katika maeneo ya pembeni ya falme za Kayor. Katika barua hiyo alisema, "kwa muda ambao nitakuwa hai, na kuhakikishia kuwa nitaupinga ujenzi wa reli hii kwa nguvu zangu zote". Wakiwa wamepania kuijenga reli hiyo Wafaransa wakaamua kuivamia Kayor mnamo Desemba 1882. Kutokana na uzoefu wake Lat Dior Diop alijua kuwa hangeweza kuwashinda Wafaransa katika vita vya kawaida. Hivyo aliposikia ya kuwa Wendling walikaribia Kayor, aliondoka akaanzisha maskani huko Djoloff. Hata hivyo Kayor haikuchukuliwa hadi 1886 wakati ambapo ilitamalakiwa na amri ya kumfukuza Lat Dior kutoka Kayor ilipotangazwa. Lat alikasirika mno alipojulishwa tangazo hilo. Aliwatayarisha wafuasi 300 ambao walibakia waaminifu kwake na kuwaondoshea kiapo cha uaminifu wale wote ambao hawakuazimia kufa naye, kisha akaingia vitani kupambana na Wafaransa na washiriki wao, ambao walikuwa raia wake hapo awali. Lat Dior aliamua maisha yake katika vita hii. Tarehe 27 Oktoba ya 1886 yapata saa tano asubuhi aliwashtukiza Wafaransa na washiriki wao katika Kisiwa cha Dekhle akawa tia hasara kubwa. Yeye na watoto wake wawili na wafuasi wake themanini walifariki papo hapo. Kifo cha Lat Dior kiliharakisha mwisho wa uhuru wa Kayor na kuwarahisishia Wafaransa zoezi la kuitwaa nchi ile.




6.2 *Mataifa na Watu wa Afrika Magharibi mwanzoni mwa mgawanyo uliofanyika na Wazungu*

Himaya ya Tukulor

Katika himaya ya Tukulor, (taz. mchoro 6.2) Ahmadu alimrithi baba yake al-Hadj 'Umar, mwanzilishi wa himaya hiyo. Ahmadu, kama watawala wengine wa Kiafrika, alikusudia kuhakikisha ya kuwa himaya yao inadumu na kulinda uhuru wa ufalme wao. Ili aweze kufanya hivyo akachagua mikakati ya kushirikiana nao na papohapo kupambana nao. Hata hivyo yeye alitofautiana na watawala wengi wa eneo hilo akategemea zaidi mbinu ya kushirikiana nao kuliko kupigana kwa kutambua ya kuwa alihitaji zana na vita na fedha za kuimarisha utawala wake, mambo mawili ambayo yalimfanya afanye urafiki na maelewano na Wafaransa. Basi, kuanzia wakati alipochukua madaraka, yeye alikubali kushauriana nao. Makubaliano hayo yalifanyika kati yake na Luteni Mage, mwakilishi wa Wafaransa. Wote walikubaliana ya kuwa Wafaransa wangempa mizinga na kutambua utawala wake, naye Ahmadu angewaruhusu Wafaransa wafanye biashara katika himaya yake.

Ijapokuwa mkataba huo haukuthibitishwa na serikali ya Ufaransa, na wala Ahmadu hakupata mizinga, na ijapokuwa Wafaransa waliendelea kuwasaidia waasi na hata mnamo 1879 waliweza kuishambulia Sabusire, iliyokuwa ngome ya Watukulor huko Khassa, Ahmadu yeye aliendelea kufanya urafiki na Wafaransa. Hii ilimsaidia kwa vile aliweza kuyazima maasi ya ndugu zake mnamo 1874, na maasi ya maeneo ya Bambara, Segu na Kaarta katika miaka ya mwisho mwisho ya 1870. Wafaransa nao, walivyokuwa wanataka kutamalaki eneo la kati ya Senegal na Niger, pia waliuhitaji ushirikiano wa Ahmadu. Haishangazi basi kuona ya kuwa mnamo mwaka 1880 walianza tena makubaliano ambayo yalizaa mkataba wa Mango. Kufuatana na mkataba huo Ahmadu aliwakubalia Wafaransa kuendeleza biashara katika himaya yake, pia akawaruhusu waanzishe njia za meli katika mto Niger. Wafaransa nao kwa upande wao waliutambua utawala wa Ahmadu, wakamruhusu njia ya wazi kuifikilia Futa na kumwahidi kutoishambulia nchi yake wala kujenga ngome huko. Zaidi ya hayo Wafaransa walikubali kumlipa mizinga minne na bundiku 1,000 na kulipa kodi ya bunduki
200, mapipa 200 ya baruti, makasha 200 ya kutilia baruti na flinti 50, 000 kila mwaka.

Mkataba huu ulikuwa ushindi mkubwa wa kidiplomasia kwa Ahmadu, na kama Wafaransa wangeuthibitisha kwa nia safi na kuyatekeleza makubaliano yao, himaya ya Ahmadu ingedumu. Lakini ukweli ni kwamba hata Gallieni mwenyewe hakuwa na nia ya kuutekeleza mkataba huo, wala serikali yake haikuuthibitisha. Mwaka 1881 Wafaransa walianza kuishambulia himaya ya Ahmadu wakiongozwa na Luteni Kanali Borgnis - Desbordes aliyekuwa mkuu wa kikosi cha Upper Senegal, na kufikia Februari 1883 walikwishaukalia mji wa Bamako kuliojengwa kandokando ya Mto Niger, bila kipingamizi chochote. Hata hivyo kwa kuwa kimsingi Ahmadu hakujihisi salama nyumbani kama inavyodhihirishwa na mashambulizi yake ya Nioro, mji mkuu wa Kaarta, nchi ambayo wakati huo

ilitawaliwa na 'kaka' yake Moutaga, alikubali tena kufanya mkataba mwingine na Wafaransa mnamo tarehe 12 Mei 1887; Mkataba ambao uliitwa Mkataba wa Gori. Kwa mapatano ya Mkataba huo Ahmadu alikubali kuiweka himaya yake nchi ya ulinzi wa Wafaransa, nao Wafaransa wakaahidi kutoishambulia nchi yake na kuondosha amri ya kumpiga marufuku Ahmadu kununua silaha.

Mambo yalivyokuwa, kufikia 1888 Wafaransa walikwishayazima maasi ya Lamire, na kama itakavyoonyeshwa baadaye, walishafanya mkataba mwingine na Samori kwa hiyo hawakuwa na haja tena ya kushirikiana na Ahmadu. Matukio haya, pamoja na ukorofi wa kikosi cha Wafaransa, yalisababisha vita dhidi ya Ahmadu kama ilivyodhihirishwa na shambulio lao la ngome ya Wamkulor, iliyokuwa Kurdian, mnamo mwezi Februari 1889. Ngome hiyo ilikuwa imejengwa imara kiasi kwamba ilibidi kipigwa mizinga mikali kwa muda wa saa nane kwa kutumia bunduki ya milimeta 80 ya Archinard kabla ya kuzivunja kuta zake. Watukolor, ambao waliyakabili mafuriko haya ya risasi kishujaa, walipambana na Wafaransa kwa bunduki zao na baadaye wakaingia kwenye mapingano ya ana kwa ana. Wengi wao waliteketea na silaha zao mkononi.

Ahmadu, akiwa bado anakabiliana na matatizo ya utawala wake; aliamua kuyafanya mapambano haya yawe ya kidini. Aliwaomba Waislamu wote wa himaya yake kuchukua silaha na kuilinda dini yao. Barua za kuomba misaada zilitumwa Djolof, Mauritania na Futa. Hatua hizi hazikupata mafanikio ya kuridhisha hivyo Archinard baada ya kufanya matayarisho madhubuti na kupata silaha za kutosha zikiwemo "bunduki mbili za milimita 95" pamoja na " Sheli/fataki 100 za kisasa kabisa" alimteka mkuu wa utawala Ahmadu mnamo Aprili 1890. Kuanzia hapo alikwenda kwenye ngome ya Qussebou (Usebugu) iliyokuwa inalindwa na Wabambara waliokuwa bado wanamtii Ahmadu. Wote waliuawa katika mapigano hayo lakini nao pia waliwatia hasara kubwa maadui wao. Akiwa amekabiliwa na upinzani wa Kibuni wa Watukulor ulioendelea kwa muda mrefu Archinard aliamua kusimamisha mapigano na kumwomba Ahmad akubali kushindwa na kujiuzulu.

Ilikuwa ni wakati huu ambapo sasa Ahmadu alitupilia mbali silaha yake ya diplomasia na akaanza kutegemea jeshi. Mnamo Juni 1890 askari wa Ahmadu walikishambulia kituo cha reli cha Talaari na kuwatatiza Wafaransa kwa mapigano ya hapa na pale kati ya Kayes na Bufulabe. Wakati mmoja Wafaransa walipigwa kiasi cha kuwapoteza askari arobaini na tano waliouawa pamoja na majeruhi kutoka kikosi cha askari 125. Mnamo mwezi Septemba, mwezi ambao mji wa Koniakari kwa kawaida ulikuwa ukizingirwa na mafuriko, askari wa Ahmadu walijaribu kuuteka tena mji huo wakashindwa. Huko katika mji wa Nioro mnamo Desemba 1890 askari wa Ahmadu walijitahidi kulinda mji huo uliposhambuliwa na Wafaransa lakini walishindwa kwa vile Wafaransa walitumia bunduki kubwa za mm 85 na 90; hivyo Archinard aliweza kuingia Nioro terehe 1 Januari 1891. Baadaye sultani Ahmadu alijaribu kuukamata tena mji wa Nioro lakini alishindwa na kupoteza Masina ambako alipambana tena na Wafaransa katika pigano maarufu la



6.3 *Samori Ture (c. 1830 – 1900) baada ya kukamatwa na majeshi ya Kapteni Gouraud (kulia) katika Septemba 1898.*

Kor-Kori na baadaye akaihama nchi kwenda ukimbizini. Hata huko ugenini kwenye nchi ya Wahausa, Ahmadu aliendelea kuuthamini uhuru wake wa kukataa kabisa kutawaliwa na Wafaransa.

Somari na Wafaransa

Somari Ture alitofautiana na Ahmadu kwa vile yeye alichagua mkakati wa mapambano ya kivita dhidi ya Wafaransa tangu mwanzo, na hakupendelea sana mashauriano nao. Ingawa naye alitumia silaha zote mbili yaani diplomasia na mapambano ya kivita lakini aliegemea zaidi upande wa mapambano ya kivita. Hadi kufikia 1881 Somari alikwishajenga himaya kubwa katika sehemu ya kusini ya Savana ya Sudani (taz.mchoro 6.2). Ushindi wa eneo hilo ulimwezesha Somari kujenga jeshi kubwa lenye nguvu na nidhamu, tena lililokuwa na silaha za kisasa kutoka Ulaya kama vile bunduki za Gras na zile za Kropatschks ambazo zilikuwa kama za Gras lakini zilizoweza kuendelea kufyatua risasi. Jeshi lake liligawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza la askari wa miguu (sofa) na ambalo hadi kufikia 1887 lilikuwa na askari kati ya 30, 00 na 35, 000, na kundi la pili lilikuwa la Wapanda Farasi ambao hawakuzidi 3, 000. Kuanzia 1888 aliongezea shehena yake ya silaha kwa kupata bunduki mpya zilizopiga haraka zaidi hata kufikia 1893 akawa na bunduki 6,000. Hata hivyo hakuweza kupata silaha zozote zilizoweza kuwazuia Wafaransa katika vita vyao. Somari alipata silaha hizo kwa kuuza pembe za ndovu na dhahabu iliyopatikana kutoka machimbo ya dhahabu ya Bure huko kusini, na kutokana na mabadilishano ya watumwa kwa farasi katika mikoa ya Sahel na Mosi.

Kutokana na melezo hayo hapo juu inadhihirika ya kuwa Somari alikuwa amefikia kilele cha mamlaka yake alipokutwa na Wafaransa mnamo 1882. Mnamo Februari 1882, Wafaransa walimwamuru aondoke Kenyerean, soko muhimu ambalo kuondoka hapo kwake kungemfungia njia ya kuwafitikilia Wamandingo. Kama ilivyotazamiwa, Somari alikataa. Basi Wafaransa walimvamia wakiongozwa na Borgnis - Desbordes ambaye hata hivyo alilazimika kukimbia haraka. Ndugu yake Somari aliyeitwa Keme-Brema, aliwashambulia Wafaransa huko Wenyako karibu na Bamako mwezi Aprili. Ijapokuwa aliwashinda mnamo tarehe 2 Aprili, lakini kufikia tarehe 12 Aprili alishindwa na kikosi kidogo zaidi cha Wafaransa. Tangu wakati huo Somari aliwaepuka Wafaransa akakazania Kenedegu.

Mnamo 1885 Combes alipoutwaa mji wa Bure, mji ambao dhahabu yake ilikuwa muhimu kwa uchumi wa himaya ya Samori, Samori naye akaamua kuwafukuza Wafaransa kwa nguvu. Somari alitumia majeshi matatu kwa shughuli hiyo: moja la kwake na mengine ya Keme na Masara-Mamadi. Kwa kutumia mbinu ya shambulio la kutumia mikondo miwili, mji wa bure ulitekwa kwa urahisi na Wafaransa wakalazimika kung'oa kambi wakiogopa kuzingirwa. Hapo Samori alianza kujenga uhusiano mwema na Waingereza huko Sierra Leone akiwa na lengo la kutaka kuheshimiwa na Wafaransa. Baada ya kuuteka mji wa Falaba mwaka wa

1884 aliwatuma wajumbe wake kwenda Freetown kupendekeza kwa Gavana ya kuwa angependa sasa nchi yake iwe chini ya ulinzi wa Serikali ya Uingereza.

Ilivyokuwa pendekezo hilo halikufaulu Samori akawaendea Wafaransa na kuandikiana nao mkataba tarehe 28 Machi 1886, ambapo alikubali kuondoa majeshi yake hadi kingoni mwa Mto Niger lakini alibakiza haki yake ya kuutawala wabure na Wamanden wa Kangaba. Katika mkataba mwingine na Wafaransa wa 25 Machi 1887 ambao ulirekebisha ule wa mwaka uliopita, Samori aliachia ukingo wa kushoto wa Mto Niger kwa Wafaransa na kukubali kuiweka nchi yake chini ya ulinzi wa Wafaransa.

Huenda Somari alipotiliana mkataba wa pili na Wafaransa alitazamia Wafaransa wangemsaidia katika vita vyake dhidi ya Tieba, Mtawala (Faama) wa Sikasso. Somari alimshambulia mwaka 1887 na jeshi la askari 12, 000. Wafaransa nao walitiliana mkataba na Samori kwa vile walikusudia kuzuia mkataba wowote kati yake na Mamadou-Lamine, ambaye alikuwa anapigana na Wafaransa. Somari alipoona ya kuwa Wafaransa hawakuwa na ushirikiano naye, na kinyume chake walikuwa wanachochea upinzani na maasi kwa raia zake, na zaidi ya hayo walikuwa wakimzuia kupata silaha na vifaa vingine kutoka Sierra Leone, alianza kujitayarisha kukabiliana na Wafaransa kijeshi. Aliliunda jeshi lake upya kisha akatiliana mkataba na Waingereza mnamo Mei 1890 huko Sierra Leone. Mkataba huo ulimwezesha Samori kununua silaha za kisasa kwa miaka mitatu iliyofuata, na kila mwaka kiasi kikiongezeka.

Hata hivyo mapigano makubwa kati ya Samori na Wafaransa hayakutokea hadi 1892. Humbert, ambaye alikuwa amenuia kumshinda Samori, aliishambulia sehemu ya kati ya himaya ya Samori mnamo Januari 1892 akiwa na jeshi la askari hodari 1,300 wenye bunduki na wapagazi 3,000. Samori naye binafsi aliliongoza jehi lake la askari wateule 2,500 kupambana na Humbert. Kwa kukariri maneno ya Yves Peron, ijapokuwa askari hawa "walipigana kama mashetani, wakijihami kwa kila njia" walishindwa na hapo Humbert alifanikiwa kuteka Biasandougou, Samaukoro na Kerwane. Ni muhimu ijulikane hapa ya kuwa Humbert mwenyewe alikiri ya kuwa matokeo ya vita hivyo kwake yalikuwa ya thamani ndogo akilinganisha na hasara kubwa aliyoipata.

Kutokana na kushindwa vibaya huku, Samori alibakiwa na mambo mawili ya kufanya, ama kusalimu amri au kukimbia. Aliamua kutosalimu amri, akaamua kuihama nchi yake, akaelekea mashariki ambako alitarajia kujenga himaya mpya, isiyofikiliwa na Wazungu.

Akiendeleza sera yake ya kuchoma mashamba, Samori alielekea Mashariki kufikilia mto Bandama na Comoe. Mwanzoni mwa 1895 alipambana na kukishinda kikosi cha Wafaransa kilichotoka nchi ya Wabaule na ambacho kiliongozwa na Monteil. Kati ya 1895 na Januari 1896 aliushinda ufalme wa Abron (Gyanan) na sehemu ya magharibi ya Gonja. Hadi wakati huo alishafanikiwa kuanzisha himaya mpya katika bara ya Ivory Coast (Pwani ya Pembe) na nchi ya Waasante. (taz.

mchoro 6.2) Mnamo Machi 1897 mtoto wake Sarankenyi Mori alipambana na kukishinda kikosi cha Waingereza kilichoongozwa na Henderson, na Samori mwenyewe aliushambulia na kuuharibu mji wa Kongo mnamo Mei 1897, akaendelea hadi Boko ambako alipambana na kikosi cha Wafaransa kilichoongozwa na Caudrelier.

Akiwa amejikuta katikati ya Wafaransa na Waingereza baada ya kujaribu kuwachonganisha, bila mafanikio, kwa kuwarudishia Wafaransa nchi ya Bouna ambayo ilitamaniwa mno na Waingereza, Samori aliamua kurudi kwa marafiki zake Watoma huko Liberia. Njiani akashambuliwa ghafula na kukamatwa huko Geelemou na Gouand tarehe 29 Septemba 1898 kisha akapelekwa kuzuizini Gabon ambako alifia mwaka 1900. Kushikwa kwake kulifikisha mwisho kile msomi mmoja alichokiita, "vita virefu kuliko vyote dhidi ya adui mmoja katika historia ya Wafaransa katika kuitamalaki Sudan".

Dahomey

Behanzin, mfalme wa Dahomey (aboney) naye kama Samori alichagua mkakati wa mapambano katika kulinda uhuru wa dola yake. Mgongano baina yake na Wafaransa ulitokea katika mwongo wa mwisho wa karne ya 19 wakati Wafaransa walipotangaza nia ya kuilinda Port Nor, jimbo la aboney (taz. mchoro 6.1) na kuukalia mji wa Cotonou (Katonu) mnamo Februari 1890. Konde, mwana Sultani aliyeshika utawala Desemba 1889 kwa jina la Behanzin alijibu kwa kuyakusanya majeshi yake na kuushambulia mji wa Cotonou. Pia alitumia silaha ya kiuchumi dhidi ya Wafaransa kama vile kuiharibu miti ya mawese kandokando ya Porto Nor (Bandari Mpya).

Kwa mujibu wa maelezo yake, silaha ya kiuchumi iliwaharakisha Wafaransa kutaka amani. Tarehe 3 Oktoba Padre Dorgere aliwasili Abomey akiwa na mapendekezo ya amani. Wafaransa walimtaka Mfalme aukiri utawala wao juu ya Cotonou, na haki yao ya kutoza kodi ya forodha na kuweka kituo cha kijeshi, nao Wafaransa wangelipa kodi ya mwaka ya Faranga 20, 000. Mfalme alikubaliana nao na mkataba ukatiwa saini tarehe 3 Oktoba 1890.

Wafaransa lakini walinuia kuishinda Dahomey na walipata kisingizio kizuri wakati Balozi wa Porto Noro aliposhambuliwa tarehe 27/3/1882 na askari wa Kifon alipokuwa na safari katika mto Weme kwenye boti yake yenye bunduki. Kanali Dodds, Chotara wa Kisenegali, alitumwa kuongoza kikosi cha askari alipofika Cotonou mnamo Mei 1892 na akaanza safari yake ya miguu kwenda Abomey mnamo mwezi Oktoba. Wafon waliunganisha vikosi vyao vyote vitatu pamoja wakapata askari 12,000, wakaenda kupambana na jeshi la Wafaransa wavamizi. Hata hivyo ijapokuwa Wafon walitumia mbinu zote za jadi za mashambulizi ya machweo, kuwajia kwa hila, kuwateka na nyinginezo kama za vita vya msituni, walishindwa kuwazuia Wafaransa, wakapata hasara kubwa. Wafon

walipoteza kiasi cha askari 2,000 wakiwemo Waamazoni ambao walikuwa askari wa kike walioogopesha mno, na askari wengine majeruhi 3,000. Wafaransa walipoteza maofisa 10 na askari 67 tu.

Baada ya kuvunjika kwa jeshi la Wafon ilibakia kufanya amani. Dodds alipiga kambi huko Cana akakubali mapendekezo ya Behanzin lakini akaidai malipo makubwa kama fidia ya vita na kuwataka Wafon warudishe silaha zote. Masharti hayo hayakukubaliwa, kwani yalikuwa kama kuwatukana Wafon. Mnamo Novemba, 1892 Dodds alisonga mbele akaingia Abomey, ambako alikuta Behanzin keshalichoma moto eneo hilo kabla ya kwenda kwenye sehemu ya kaskazini ya himaya yake alikotulia na kuweza kuwakusanya askari wengine 2,000; askari ambao walifanya mashambulio kadhaa katika maeneo yaliyokaliwa na Wafaransa.

Mnamo Aprili 1893 washauri wa Behanzin walitoa mapendekezo mapya ya amani. Walikuwa tayari kutoa eneo la kusini mwa nchi yao kwa Wafaransa lakini hawakukubali Behanzin ajiuzulu. Basi Wafaransa wakatuma kikosi kingine cha askari mwezi Septemba kikiongozwa na Dodds ambaye sasa alikwisha pandishwa cheo kuwa Jenerali. Kikosi hicho kilifanikiwa kuitamalaki sehemu ya kaskazini ya ufalme wa Behanzin. Coutchilli aliteuliwa na kutawazwa kuwa mfalme tarehe 15 Januari 1894 na Behanzin akakamatwa baada ya kusalitiwa mwezi Januari tarehe 29.

## *Kutamalaki na Ukinzani uliotokea huko Afrika Magharibi iliyokaliwa na Waingereza: 1880 - 1900*

Wafaransa walitumia nguvu za kijeshi katika kulikalia eneo la Afrika Magharibi kati ya 188 - 1900 lakini Waingereza walitumia mbinu zote mbili, diplomasia na vita. Kwa kutumia diplomasia ya amani waliweza kuandikiana mikataba ya ulinzi na dola za Kiafrika kama walivyofanya huko kaskazini mwa Sierra Leone, Gold coast (sasa Ghana) na katika maeneo fulani ya Wayoruba. Katika maeneo mengine kama vile Asante na Ijebu, katika Uyoruba, katika Delta ya Niger na hasa huko kaskazini ya Nigeria kwa kiasi kikubwa walitumia nguvu. Katika upinzani wao dhidi ya Waingereza, wakazi wa maeneo hayo, kama wenzao waliokaliwa na Wafaransa, walitumia kila mbinu walizokuwa nazo, kama vile kupambana, kushirikiana nao au kukubali kwa hiari au pengine walizichanganya mbinu. Hebu tuchanganue matukio ya Asante, Kusini na Kaskazini mwa Nigeria, kama vielelezo.

### Asante (Gold Coast)

Hapakuwa na sehemu katika Afrika ya Magharibi ambako kulikuwa na mapambano ya muda mrefu baina ya Waafrika na Wazungu kama yalivyokuwa katika Gold Coast baina ya Waasante na Waingereza. Mapambano haya yalianza katika miaka ya 1760 yakaishilia katika vita baina yao mwaka 1824 ambapo Waasante waliyashinda majeshi ya Waingereza na rafiki zao na kumuua kamanda wao, Sir Charles Mac

Carthy aliyekuwa gavana wa gold Coast wakati huo. Baada ya miaka miwili Waingereza walilipiza kisasi katika mapigano ya Dodowa. Katika mwaka 1850 na mwaka 1863 vita nusura vitokee, kwa bahati viliweza kuepukwa. Lakini mnamo 1869 na 1872 Waasante walishambulia na kuyateka karibu maeneo yote ya kusini na pwani ya Gold Coast. Ili kuwashinda tena Waasante, serikali ya Uingereza iliunda kampeni kamambe ya kijeshi na wakaanza kupigana na Waasante wakiongozwa na ofisa mashuhuri sana wa Kiingereza wakati huo aliyeitwa Jenarali Garnet Wolseley. Likiwa na zana za kisasa kabisa jeshi hilo lilifanikiwa kuwarudisha nyuma askari wa Waasante, wakavuka mto Pra, wakawafuatilia hadi Kumasi ambako walipambana vikali na Waasante huko Amoafo karibu na Bekwai.

Ushandi huu wa Waingereza dhidi ya Waasante mnamo mwaka 1874 uliashiria matakio mapya na uliathiri kwa kiasi kikubwa upinzani wa Waasante dhidi ya Waingereza katika kipindi cha 1800 hadi 1900. Athari ya kwanza ilikuwa kumomonyoka kwa himaya ya Waasante. Katika mkataba wa Fomana, Waasante walitambua uhuru wa dola zilizokuwa chini yao kusini ya mto Pra. Nazo dola nyingi za Waasante zilizokuwa kaskazini ya Mto Volta zilijitenga. Hata uti wa mgongo wa Himaya hiyo uliokuwa umebakia nao ulianza kuvunjika. Ili kuhakikisha ya kuwa himaya ya Waasante haikuinuka tena Waingereza walizishawishi dola zilizoshiriki katika umoja wa Waasante kujitoa na kutaka uhuru, hivyo dola za Dwaben, Kohofu, Bekwai na Nsuta zilianza kutotii amri ya Mtawala wa Waasante yaani Asantehene. Aidha Asantehene aliangushwa baada ya vita ya 1874. Alipofariki mrithi wake aliyetawala kwa miaka saba tu, vita vya wenyewe kwa wenyewe vilizuka wakigomea nani awe mtawala mpaka Prempeh alipojitokeza, katika mwaka 1888, kama Asantehene mpya.

Kwa bahati nzuri Prempeh alidhihirisha kuwa alikuwa na uwezo wa kuuhimili msukosuko uliomkabili. Miaka mitatu baada ya kutawazwa kwake aliweza kuziunganisha tena dola zilizokuwa chini ya Umoja (Ushirikiano) wa Waasante. Waingereza wakiwa na wasiwasi kuwa wangelitwaa nchi ya Asante, wakajitolea kuiweka nchi hiyo chini ya ulinzi wao. Prempeh alipolikataa wazo hilo kistaarabu Waingereza wakapendekeza kuanzisha ubalozi hako Kumasi na kumlipa malipo ya kila mwaka mfalme wa Waasante na wengineo waliokuwa maarufu. Prempeh alikataa tena na kuwatuma wajumbe wake kwenda kwa Malkia wa Uingereza kumtaka "kuyaangalia na kuyachunguza mambo muhimu yanayohusu ufalme wetu". Ujumbe huu wa kidiplomasia uliondoka kuelekea Uingereza tarehe 3 Aprili 1895. Serikali ya Uingereza haikukataa tu kuupokea ujumbe wa Waasante, bali pia wakati ujumbe ulipokuwa ungali Uingereza, Serikali ya Uingereza ilimwagiza Gavana wa huko Pwani kuwa lazima ampokee Balozi wa Kiingereza na kulipa fidia ya vita, kiasi cha wakia 50,000 za dhahabu waliyopewa baada ya kushindwa mwaka 1874. Asantehene aliwakatalia Waingereza matakwa yao hasa kwa vile alikuwa anangojea majibu ya ujumbe wake huko Uingereza.

Waingereza wakitumia kukataliwa huku kama kisingizio, wakatuma kikosi

kilichoongozwa na Sir Francis Scott kupigana na Asantehene. Kikosi hiki kiliingia Kumasi Januari 1896 bila ya kufyatua risasi hata moja kwa sababu Prempeh na Washauri wake walikwishaamua kutopigana ila wakubali ulinzi wa Uingereza. Bila kujali uamuzi huo Scott na wenzake wakamkamata Prempeh, mama yake ambaye ndiye alikuwa Malkia, kaka yake na machifu maarufu wa vita na kuwapeleka kizuizini, kwanza huko Sierra Leone na baadaye katika Visiwa vya Shelisheli mnamo mwaka 1900 (taz. picha 6.2).

## Nigeria ya Kusini

Njia na mbinu walizotumia Waingereza kuiweka Nigeria (Kama tuijuavyo leo) chini ya mamlaka yao zilitofautiana kama vile Wanigeria walivyotofautiana katika kuwapinga. Nchi ya Wayoruba ilipatikana kwa kuwatumia mabalozi wa Wamisionari, na Kaskazini ya Nigeria ilipatikana kwa kutwaliwa na Kampuni ya *National African Company* (Kampuni ya Kitaifa ya Afrika) ambayo baada ya 1886 ilijulikana kama *The Royal Niger Company* (Kampuni ya Kifalme ya Niger) kwa Serikali ya Uingereza. Mbini kuu zilizotumiwa na Waingereza zilikuwa diplomasia na kutamalaki. Wanigeria nao walijaribu kujihami kwa kupambana kijeshi, kushirikiana nao kwa muda na hata kukubali kutawaliwa.

Kutokana na shughuli za Wamisionari, athari za Waingereza zilienea kutoka Lagos (iliyoanza kukaliwa mwaka 1851) hadi sehemu nyingi za nchi ya Wayoruba na pia mikataba kadhaa ya kutokomeza utumwa, ya biashara na ya uliuzi ilikwishafikiwa baina ya Waingereza na Watawala wa Wayoruba ilipofikia mwaka 1884. Katika mwaka wa 1886 utawala wa Uingereza uliweza kuwashawishi wenyeji wa Ibadan na Ekitiparpo (iliyoungamisha Ekiti, Ijesha na Egba) ambao walikuwa wamepigana vita tangu 1879 kuandikiana mkataba wa amani. Ijebu tu ndiyo dola ya Wayoruba iliyoweza kuwazuia Wamisionari, wafanyabiashara wa Kiingereza na utawala wa Lagos wasiwaingilie hadi kufikia miaka ya 1880. Wakiwa wamepania kuitawala nchi ya Wayoruba tangu mwanzo wa 1890, Waingereza wakaamua kulipa fundisho Ijebu ili waonyeshe maeneo mengine hasara ya kupinga kuenea kwa utawala wao. Kwa kutumia kisingizio cha kutukanwa kwa gavana wao Denton, mnamo mwaka 1892 Waingereza walituma kikosi imara cha askari 1,000 waliokuwa na bunduki, mizinga midogo na bunduki za Masksim kushambulia Ijebu. Waijebu nao kwa ushupavu wao waliweza kukusanya kikosi cha askari kati ya 7,000 hadi 10,000 lakini ijapokuwa walikuwa na wingi wa watu, walishindwa nguvu na wavamizi. Ilivyoelekea dola nyingine zote za Kiyoruba zilipata fundisho na halikuwa jambo la kushangaza kuona kwamba kati ya 1993 na 1899 dola za Abekouta, Ibadan, Ekiti - Ijesa na Oyo, zote zilikubali kufanya mapatano na kuandikiana mikataba na mabalozi wa Kiingereza. Waingereza waliilipua Oyo mwaka 1895 ili tu kuhakikisha ya kuwa Alafin ilikuwa imekubali kabisa kukaliwa na Wazungu. Dola ya Abekouta ilibakia na uhuru bandia hadi mwaka 1914.



**6.4** *Nana Prempeh I wa Asante (c. 1873 – 1931) wakati akiwa ukimbizini Seychelles (c.1908). Aliyekaa kulia kwake ni nana Yaa-Asantewaa, Malkia wa Edweso na kiongozi wa uasi wa Asante 1900, na kushoto mamake na babake.*

Wakati Wayoruba walichagua mkakati wa kukubali kutawaliwa, watawala wa ufalme wa Benin na baadhi ya watawala wa dola za Delta ya Niger walichagua mkakati wa mapambano. Ijapokuwa Benin ilifikia mkataba wa ulinzi na Waingereza mwaka 1892 hata hivyo iliunda uhuru wake kwa makini. Jambo kama hili halikuvumiliwa wakati huo, ndipo Waingereza walipoamua kuwaingilia kwa kutumia kisingizio cha mauaji ya kaimu-balozi wa Kiingereza na Waingereza wengine watano waliokuwa wakielekea Benin. Waingereza walituma kikosi cha maaskari 1500 kushambulia Benin mwaka 1897. Oba (mfalme) wa Benin alitaka kusalimu amri lakini machifu wake wengi walitayarisha jeshi la kupambana na washambulizi wa Kiingereza. Hata hivyo, walishindwa na mji wao mkuu ukachomwa moto baada ya vito vya thamani na sanaa zao kuporwa.

Katika Delta ya Niger, kama katika maeneo mengine ya Nigeria, Waingereza walikwisha kuandikiana mikataba y ulinzi karibu na machifu wote. Kufikia mwaka 1884, baadhi ya machifu (kama vile mfalme wa (Calabar na Bonny) waliwaruhusu wamisionari kuendesha shughuli katika dola zao lakini baadhi yao hawakufanya hivyo. Zaidi ya hayo, wengi wao walikuwa wakisisitizia kutambuliwa kwa uhuru na mamlaka yao ya kusimamia biashara na kuwatoza ushuru wafanyabiashara wa Kiingereza. Mabalozi wapya wa Kiingereza kama vile Hewett na Johnson hawakuweza kuvumilia masharti hayo. Mfano thabiti wa watawala walio simama kidete dhidi ya Waingereza na Wamisionari ni Jaja wa Opobo. Yeye alishikilia ya kuwa lazima ushuru ulipwe na wafanyabiashara wa Kiingereza na akaamuru kusimamishwa kabisa kwa biashara katika mto Niger mpaka kampuni moja ya Kiingereza ikalipa ushuru. Balozi Johnston alimwamuru Jaja aache kuwatoza wafanyabiashara wa Kiingereza ushuru. Badala ya kufanya hivyo Jaja alituma ujumbe kwenda kwenye ofisi ya makoloni kuilalamikia amri hiyo. Jaja bado alishikilia msimamo wake hata baada ya kutishwa na Johnston ya kuwa mji wake ungepigwa mabomu na meli za kivita. Basi Johnston akamdangaya Jaja apande meli yao moja mnamo 1897, ili aweze kumvusha salama, lakini akamkamata na kumpeleka Accra ambako alihukumiwa na kuwekwa kizuizini kwenye Visiwa vya West Indies. Dola nyingine za Delta zilipigwa na butwaa kwa jinsi mtawala huyo tajiri, maarufu na mashuhuri alivyofanyiwa ndipo wafalme wa Old Calabar, New Calabar Brass na Bonny walipoamua kusalimu amri na kukubali kutawaliwa na mabaraza yaliyowekwa kwa nguvu na Balozi Johnston.

Mtawala mwingine aliyewapinga Waingereza alikuwa Nana, gavana wa mto katika ufalme wa Itsikeri. Kama Jaja, Nana alishikilia kusimamia biashara katika mto Benin, kwa hiyo Waingereza wakatayarisha jeshi la kuuteka mji wake mkuu. Mnamo mwaka 1894 jaribio la kwanza la Waingereza lilishindwa lakini lile la pili la mwezi Septemba lilifanikiwa. Nana alikimbilia Lagos ambako alijisalimisha mwenyewe kwa Serikali ya Uingereza ambako hawakupoteza muda wakamshitaki na kumhukumu apelekwe kizuizini Gold Coast (ambayo sasa ni Ghana).

Kutamalaki na Ukinzani uliotokea Nigeria ya Kaskazini

Kama kushindwa na kukaliwa kwa Nigeria ya kusini kulisababishwa na kazi ya Serikali ya Uingereza ikisaidiwa na wafanyabiashara na Wamisionari, basi kushindwa na kukaliwa kwa Nigeria ya Kaskazini kulitokana na *National African Company* (Kampuni ya Kitaifa ya Afrika) (ambayo baada ya 1886 ilijulikana kama *Royal Niger Company* (RNC)) (Kampuni ya Kifalme ya Niger), na Serikali ya Uingereza, na mbinu kuu iliyotumiwa ilikuwa ile ya kutamalaki kwa nguvu za kijeshi kama walivyofanya Wafaransa huko Sudani ya Magharibi. Ushindi huu wa kijeshi ulitanguliwa na msururu wa mikataba kati ya watawala wa Niger ya Kaskazini na *Royal Niger Company* (Kampuni ya Kifalme ya Niger). Mikataba hii ilikuwa imewaniwa na Waingereza ili waweze kujipatia eneo hilo wenyewe na kuwazuia Wafaransa waliokuwa wanalijia kutoka magharibi na Wajerumani waliokuwa wanalifikilia kutoka mashariki.

Baada ya kuanzishwa kwa Kanuni ya "Utwaaji nchi kikamilifu" katika Mkutano Mkuu wa Berlin, na baada ya kuwazuia Wafaransa na Wajerumani, Kampuni ya RNC (Kampuni ya Kifalme ya Nigeria) sasa ilikuwa tayari kuingia. Milango ya kuingilia kaskazini ilikuwa kupitia Ilorin na Nupe, miji ambayo ilishikilia kutambuliwa kwa uhuru na utawala wao wenyewe, Hivyo mnamo mwaka wa 1897 Nupe ilivamiwa. Mfalme (Elsu) wa Nupe aliwakabili kishujaa wavamizi kwa jeshi la kati ya askari 25,000 na 30,000 wapanda farasi na wa miguu waliokuwa na silaha hasa za jadi kama nyuta, mikuki na majambia. Lakini Kampuni ilishinda mwishowe wakamtoa Mfalme (Elsu) madarakani na kumtawaza kibaraka wao. Mwaka huohuo Waingereza waliivamia Ilorin na baada ya mapambano makali, Ilorini nayo ilishindwa na kutawaliwa.

Ajabu ni kwamba watawala wengine wa kaskazini hawakutishwa na ushindi wa Waingereza. Kinyume chake maemiri (watawala) wote isipokuwa yule wa Zaria, wakichoshwa na chaki juu ya huyu kafiri, waliona ilikuwa afadhali kufa kuliko kusalimu amri na kupoteza nchi yao na imani yao.

Hivyo Waingereza wakalazimika kufanya mashambulio dhidi ya Kontangora mnamo 1900, dhidi ya Adamawa mnamo 1900, Bauchi mwaka 1902, na Kano Sokoto na Burwuni mnamo mwaka wa 1903. Watawala wote wa falme hizo walipigana kiume lakini hawakuweza kuwashinda adui zao waliokuwa na bunduki za kisasa kama vile zile za Maksim, na bundaki nzito zilizoweza kutupa risasi za uzito wa ratili saba (kilo 3¼ ), hivyo nao wakashindwa.

## *Ukinzani na Majibu ya Waafrika huko Afrika ya Magharibi 1900-1914*

Kama ilivyodhihirishwa katika habari zilizoelezwa hapo juu kufikia mwaka 1900 juhudi zote za wenyeji wa Afrika ya Magharibi za kuulinda uhuru wao zilishindwa. Kipindi cha kuanzia mwaka 1900 hadi kutokea kwa Vita Vikuu vya Kwanza kulijaa

shughuli nyingi za Waingereza kuingiza mifumo yao ya utawala na juu ya hapo, walianza kuziminya nchi hizo kiuchumi. Makamishena wa Wilaya na Makamishena wasafirio waliteuliwa, mahakama mpya zikaanzishwa, sheria mpya zikaingizwa, machifu wakathibitishwa na wengine wakavuliwa madaraka, kodi ya kichwa na kodi za mapato zilianzishwa na watu walishurutishwa kufanya kazi za kujenga barabara na reli. Mambo yote haya kwa vyovyote vile yalizalisha ukinzani wa namna mbalimbali.

Katika awamu hii ya pili, ijapokuwa kulikuwa na kutofautiana katika malengo yaliyotazamiwa, mikakati iliyotumiwa na wenyeji wa Afrika ya Magharibi kupata malengo hayo ilikuwa ileile. Malengo makuu yalikuwa matatu: kurudisha uhuru na utawala wao jambo ambalo lilikuwa na maana ya kuwafukuza kabisa watawala wa kikoloni; kutaka kusahihisha na kubadilisha baadhi ya mambo mabaya na ya ukandamizaji yaliyoletwa na mfumo wa kikoloni: au kutafuta namna ya kuishi ndani ya ukoloni huo. Mkakati uliochukuliwa katika awamu hii haukuwa ule wa ukubalifu wala ushirikiano isipokuwa ule wa upinzani, nao ulijitokeza kwa njia mbalimbali kama vile maasi, uhamaji, migomo ya aina zote, upelekaji wa wajumbe watetezi na mwishowe ukinzani wa kiitikadi.

Silaha maarufu kuliko zote iliyotumiwa na wenyeji wa Afrika ya Magharibi wakati huo ilikuwa uasi. Baadhi ya maasi maarufu yaliyowahi kutokea ni kama yale yaliyoongozwa na Mamodou Lamine wa Senegal kati ya miwaka 1885 hadi 1887, yale yaliyoongozwa na Fode Silla, mfalme wa Kimarabu wa Kombo na Fode Kabba mtawala wa Kiislam wa Niamina na wilaya za Casamance (Kasamansi) huko Gambia kati ya 1898 - 1901; maasi ya kodi ya vibanda ya 1898 huko Sierra Leone yaliongozwa na Bai Burch; maasi ya Waasante ya mwaka 1900 huko Gold Coast yaliongozwa na Yaa Asantewa, malkia wa Edwezo; maasi ya Waekumeku ya mwaka 1898 - 1900 na yale ya Aro huko Nigeria ya Mashariki kati ya miwaka 1898 na 1902; maasi ya Wabariba wa Borgu na Wasomba wa Atacora huko Dahomey kati ya 1913 na 1914; maasi ya Wamosssi wa Kouddougou (Kudugu) na Fada N'Gouma huko Upper Volta (sasa Burkina Faso) kati ya 1908 na 1904; maasi ya Walobi na Wadjula huko Sudani ya Wafaransa kati ya mwaka 1909 na 1909; maasi ya Porto Novo huko Dahomey; maasi ya Wabule, Wakouse, Wasassandra na Waguro wa Ivory Coast kati ya mwaka 1900 na 1914; na maasi mengine mengi katika maeneo mbalimbali ya Guinea kati ya mwaka 1908 na 1914: Ni jambo la kuvutia kuona kwamba maasi kama haya yaliongezeka ukali wake katika kipindi cha Vita Vikuu vya Kwanza.

Mfano mwingine halisi wa maasi yaliyotokea katika kipindi hiki tunachokihadithia ni yale maasi ya kodi ya vibanda ya 1898. Hayo maasi yalikuwa majibu ya Watemnme na Wamende wa Sierra Leone walipokasirishwa na utawala wa Kiingereza juu yao kwa kuwateua makamishena na Wilaya, kuongoeza polisi wa mipakani, kukomesha biashara ya utumwa na utumwa wenyewe na utekelezaji wa sheria ya 1896 ya ulinzi ambayo iliwezesha serikali kuuza maeneo ya nchi yasiyozalisha mali na kutoza watu kodi ya 5s. kwa mwaka kwa nyumba zenye

vyumba viwili na 10s. kwa nyumba zote kubwa zaidi katika eneo lote la Ulinzi. Machifu wote wa Temne walikubaliana kwa pamoja kukataa kulipa kodi hiyo na wakaasi chini ya uongozi wa mmoja wao aliyeitwa Bai Bureh. Watemne waliungwa mkono na Wamende ikawa karibu robo tatu ya wakazi wote walishiriki. Waasi walishambulia na kupora vituo vya biashara na kuua maofisa na askari wa Kiingereza na wote wale waliousaidia utawala wa kikoloni. Kufikia Mei 1988 vikosi vya waasi vilikaribia Freetown kiasi cha kilometa 40 ikabidi kombania mbili za askari jeshi ziletwe haraka kutoka Lagos kuulinda mji huo. Kiini hasa cha maasi hayo kilikuwa nini? Gavana wa Kiingereza huko Sierra Leone alipigwa na butwaa na maasi hayo akaweza kuyaelezea matukio hayo na maasi na upinzani wa jumla uliokithiri kwa utawala wa kikoloni kwamba yalisababishwa na mwamko wa kisiasa wa Mwafrika na thamani iliyoipa hadhi na uhuru wake. Mtazamo wa Cardew nao si rahisi kukosolewa na kwa kweli maoni hayo yalikuwa ya kweli kwa maasi mengi na vita vya msituni vilivyotokea huko Afrika ya Magharibi kati ya miaka ya mwisho ya 1890 na 1914.

## Uhamaji wa Umma

Licha ya maasi, mbinu nyingine iliyokuwa maarufu katika upinzani ni ile ya uhamiaji wa umma kupinga ukali wa utawala wa kikoloni. Mbinu hii ilikuwa ya kawaida zaidi katika makoloni ya Kifaransa ambako Waafrika hawakuweza kuunda majeshi ya kuwapinga kwa vile Wafaransa walisambaza vituo vya askari wao katika kila eneo walilolikalia. Hivyo Waafrika wakaamua kuhama ili wakwepe matendo waliyoyaona maovu na ya kuwanyanyasa. Kati ya mwaka wa 1882 na 1889 idadi ya Wafulani wa viunga vya mji wa Mtakatifu Louis ilipungua kutoka watu 300,000 hadi kufikia 10,000 tu. Kati ya mwaka 1916 na 1917 zaidi ya watu 12,000 waliondoka Ivory Coast kuelekea Gold Coast. Watu wengi pia walihamia Gambia kutoka Senegal wengine wakahama Upper Volta kuhamia Gold Coast na wengi wakatoka Dahomey katika kipindi hiki na kuhamia Nigeria. Ingefaa ikumbukwe hapa ya kuwa maasi haya na uhamiaji huo vyote vilitokea zaidi kwa wakazi wa vijijini na wa maeneo ya bara katika yale makoloni ambayo yalichukuliwa na wazungu kati ya mwaka wa 1880 na 1890. Huko pwani na katika miji mipya ambako wasomi weledi waliishi na ambako tabaka la wafanyakazi lilikuwa linainukia, upinzani baridi zaidi ulipendelewa. Upinzani huo ulikuwa migomo, ususaji, upinzani wa kisiasa kutumia magazeti; na zaidi ya hayo upelekaji wa saini na wajumbe kwa watawala wa wakoloni na kwa watawala wa nchi asili za wakoloni kwa kutumia vyama na mashirika mbalimbali.

Migomo

Migomo, kama chombo cha upinzani ilifahanikiwa zaidi baada ya Vita Kuu vya Kwanza kwani kabla ya hapo ilikuwa michache. Mgomo wa wafanyakazi wa reli ya Dakar - Mt. Louis ulianza mapema mnamo mwaka 1890; huko Dahomey wanawake walioajiriwa Cameroons waligoma mwaka 1891; wafanyakazi - wanyapara wakagoma huko Lagos mwaka 1897 wakidai mshahara mkubwa zaidi na mgomo mwingine uliotokea huko Cotonou na Grand Popo ulikuwa wa wapiga-makasia. Mgomo wa kwanza wa wafanyakazi wa bandari ulitokea huko Conakry Guinea mnamo mwaka wa 1919.

Upinzani wa Kisiasa

Upinzani wa kisiasa dhidi ya utawala wa kikoloni ulikuwa na nguvu sana katika Afrika ya Magharibi iliyotawaliwa na Wafaransa ambako *"Negritude"* (dhana ya weusi) ilianza kukna na kuenea kama dalili ya kupinga mfumo wa Wafaransa wa 'kuwasilimisha' wenyeji. Kwa mujibu wa Crowder, dhana hii "ama ilikataa nusunusu au kabisa vipengere mbalimbali vya utamaduni wa Kifaransa na kuonyesha ya kuwa kinyume cha maoni yaliyoenezwa na wakoloni wa kizungu, Afrika ilikuwa na historia na utamaduni wake wenyewe". Upinzani wa kisiasa ulionekana katika utamaduni wa dini pia, baina ya Wakristo, Waislamu na wale waliofuata Imani za Jadi (Wauminijadi). Basi, kama Olorumtimehin alivyoonyesha, Walobi na Wabambaro wa Sudani iliyotawaliwa na Wafaransa walijiunga pamoja wakapinga maenezi ya utamaduni wa Kifaransa pamoja na kuenea kwa dini za Kikristo na Kiislamu. Wafuasi wa dini ya Kiislamu hasa kanda ya Sudani ya Magharibi nao waliufufua Umahdi na kuanzisha ibada kama ile ya Mouridiyya iliyoongozwa na Shehe Ahmadu Bamba, na hata Shehe Hamollah alianzisha Uhamalliyya ambao ulipinga kuwapo kwa Wafaransa. Huko kwenye makoloni ya Waingereza ya Afrika ya Magharibi Wakristo wa Kiafrika waliasi dhidi ya wazungu kutawala mno makanisani na walionyesha kutokuridhika na kulazimishwa kupokea utamaduni wa liturjia ya kizungu. Jambo hili lilisababisha waumini hawa kujitenga na kanisa wakaanzisha makanisa yao ya Kimasihiya, au ya Kimilenia au ya Kiethiopia, yakiwa na mafunzo na liturjia za asili ya Kiafrika. Kanisa la *Native Baptist Charch* (Kanisa la Kiubatizo) ni mfano wa kanisa la kwanza kabisa la Kiafrika kuanzishwa Nigeria mwezi Aprili mwaka 1888.

Vyama vya Wasomi

Waafrika walioelimika Waliunda vyama na vikundi vingi, hasa hasa katika miji, kama vyombo vya kupinga mfumo wa ukoloni, uovu na ubaguzi wake katika kipindi hiki. Wanachama hao walitumia mgazeti, michezo, vijitabu, na matangazo mengine

kama silaha zao kuu. Baadhi ya vyama vilivyokuwa vinaukodolea macho ukoloni ni kama vile chama cha *Aborigines Rights Protection Society,* ARPS (Chama cha Ulinzi wa Haki za Wenyejiasilia) kilichoundwa huko Gold Coast mnamo mwaka 1897. Huko Senegal kulianzishwa chama cha *Young Senegalese Club* (Chama cha vijana wa Senegal) mwaka 1910, na huko Nigeria vilianzishwa vyama viwili, kimoja kilianzishwa mwaka 1908 na kuitwa *Peoples Union* (Muungano wa Umma) na mwaka 1912 *Anti-Slavey And Aborigines Protection Society* (Chama cha Kupinga Utumwa na kulinda Haki za Wenyejiasilia) kilianzishwa. Kile chama cha pili (ARPS) kilichokuwa hai zaidi kiliundwa kuipinga Sheria ya Ardhi ya 1896 ambayo ilikuwa iipe Serikali haki ya kufanya itakavyo na ardhi iliyodaiwa kuwa haifai. Chama hicho kilituma ujumbe kwenda London mwaka 1898 nao ukapokelewa na waziri wa nchi aliyehusika na makoloni. Ujumbe huo ulifanikiwa kuifuta sheria hii iliyokuwa imewachukiza mno. Kuanzia wakati huo chama cha Ulinzi wa Haki za Wenyejiasilia (ARPS) kilituma madai ya maadinshi kwa utawala wa ndani wa makoloni na kwa ofisi ya makoloni huko Uingereza kupinga baadhi ya sheria zilizokuwa matayarishoni. Chama hicho kiliweza kutuma ujumbe mara mbili kwenda Uingereza.Ujumbe wa kwanza wa 1906 ulitetea kufutwa kwa sheria ya miji ya 1894 na ujumbe wa pili wa 1911 ulikwenda kupinga Sheria ya Misitu ya 1910. Huko kaika Afrika ya Magharibi iliyotawaliwa na Wafaransa chama cha *Young Senegalese Club* (Vijana wa Senegal) kilichoanzishwa mnamo mwaka 1910 kilipigania haki sawa kwa nguvu kabisa.

Kutokana na mjadala huu itaonekana ya kuwa wakazi wa Afrika ya Magharibi walitafuta mbinu na mikakati ya kila aina kwanza kupinga kusimikwa kwa mfumo na utawala wa kikoloni na pili, baada ya kushindwa kwao waliendelea kupinga shughuli maalumu na taasisi maalumu za mfumo huo. Mikakati hii mbalimbali na mbinu zake vyote havikufanikiwa na kufikia mwisho wa kipindi hiki tunachokijadili, ukoloni ulishajikita na kuota mizizi katika bara lote la Afrika.

# 7

## *Juhudi na Ukinzani wa Waafrika: Afrika Mashariki 1880-1914*

Katika Afrika Mashariki kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Afrika, juhudi na ukinzani wa Waafrika dhidi ya kukaa na kutamaliki kwa Wazungu vilitegemea muundo wa kila jamii ya wakati huo.

Katika miaka ya 1890, kipindi kinachotangulia ukaaji wa Wazungu katika Afrika Mashariki, jamii za eneo hilo zilikuwa zimefikia viwango mbalimbali vya mfumo wa kijamii. Jamii nyingine, kama vile Waganda na Wanyoro wa Uganda, Wanyambo katika Tanganyika na Wanga katika Kenya, walikuwa wameunda kwa kiwango cha juu serikali kuu zenye madaraka. Katika jamii kama hizi, kupinga au kukubali kuingia kwa wageni katika nchi zao kulitegemea zaidi mfalme au utawala wote kwa ujumla. Jamii nyingine, kama vile Wanyamwezi katika Tanganyika au Wanga katika Kenya, zilikuwa katika jitihada za kuunda serikali kuu. Walakini, jamii nyingi sana katika eneo hili hazikuwa na serikali kama hizo. Lakini kukosekana kwa serikali kuu hakumaanishi kwamba hakuna serikali yoyote, kosa ambalo baadhi ya wageni waliojadili juu ya jamii za Kiafrika walifanya hapo zamani.

Aidha, jamii kadhaa zilikuwa na viwango mbalimbali vya mawasiliano baina yao na Wazungu na Waarabu, mataifa mawili yanayoathiri Afrika Mashariki sasa hivi. Kwa ujumla maeneo ya pwani yalikuwa na mawasiliano ya muda mrefu na Wazungu na Waarabu kuliko yale ya bara. Kati ya watu wa bara, Wakamba na Wanga wa Kenya, Wanyamwezi wa Tanganyika na Waganda wa Uganda ndio waliwahi kuwa na mawasiliano ya muda mrefu kuliko wengine kwa njia ya misafara ya biashara. Lakini tena viwango vya ukinzani dhidi ya wageni vilitofautiana kufuatana na viwango mbalimbali vya maingiliano na wageni.

Mbali na athari hizi za kibinadamu, kulikuwa pia na mabadiliko ya kimazingira yaliyokuwa yakitokea katika Afrika Mashariki katika miaka 1890. Mabadiliko haya pia yaliathiri namna wenyeji walivyolitazama swala la majilio ya wageni. Eneo lote lilipatwa na maafa ya kimazingira yaliyotokana na ukame uliosababisha njaa. Ugonjwa wa sotoka ulitokea. Tena, baadhi ya jamii ziliteswa zaidi na maafa haya ya asili kuliko nyingine. Jamii za wafugaji, kama vile Wamasai wa Kenya, yaelekea ndizo zilizoathirika zaidi kuliko nyingine zote. Familia kadhaa za Wamasai kama vile zile za kina Waiyaki na Njonjo zikakimbilia kwa majirani zao Wagikuyu. Na huko iliwabidi wachukue jukumu tofauti kulingana na jinsi walivyoliona swala la majilio ya ukoloni na jamii katika mazingira ya ukoloni. Wengine walikimbilia kwa Wanandi. Hata hivyo

wengine hawakuwa na budi kutoa huduma zao kama askari; kwanza kama mamluki wa mfalme Mumia wa Wanga kati ya Waluyia; pili kama askari wa wakala wa dola ya Uingereza wakiwa kati ya jeshi la uvamizi lililotumika katika kuteka nchi ambayo leo huitwa Kenya. Mfano huu wa Wamasai unaonyesha wazi aina ya mtawanyiko uliotawala njia za uchumi za jamii mbalimbali katika eneo hili kwa ujumla. Kwa hiyo, ukoloni ulifika katika eneo ambalo tayari lilikuwa na matatizo ya kiuchumi pamoja na matokeo yake yote.

## *Mnyang'anyiro wa Wazungu kwa ajili ya Afrika Mashariki na aina za Ukinzani wa Waafrika*

Mnyang'anyiro wa wakoloni kwa ajili ya Afrika Mashariki uligongamisha mataifa matatu: Usultani wa Zanzibar, Ujerumani na Uingereza. Watu wa kwanza kuingia katika mnyang'anyiro huu walikuwa Waarabu ambao walifanyia mambo yao yote Zanzibar. Maslahi yao, pwani na bara, yalikuwa hasa ya kibiashara, yakihusu uchuuzi wa watumwa na pembe za ndovu. Kabla ya miaka 1880 na 1890, wafanyabiashara hao Waarabu na Waswahili, waliridhika na kuendesha biashara zao kutoka mwambao. Lakini kati ya miongo ya mwisho ya karne iliyopita, maslahi ya Mwarabu barani Afrika mashariki yalianza kutishiwa na yale ya Mjerumani na Mwingereza ambao walikuwa wakijiimarisha polepole katika eneo hili. Kwa tishio hili, Waarabu walijaribu kujiimarisha kisiasa katika maeneo fulani kusudi walinde biashara zao. Kwa hiyo wakaanzisha koloni Ujiji, ufukoni mwa Ziwa Tanganyika, na katika Buganda walifanyia mapinduzi Wakristo baada ya kushiriki pamoja nao katika kumg'atua mfalme Mwanga. Wazungu waliokuwa bara walikuwa ni pamoja na wafanyabiashara na Wamisionari; wote hawa walitaka Afrika Mashariki iwe chini ya serikali zao ili wahakikishiwe usalama wao na vile vile waruhusiwe kuendesha shughuli zao bila kizuizi.

Mbinu za Wazungu kupenya barani zilitofautiana kutoka mahali hadi pengine. Lakini, kwa ujumla, zilidhihirishwa na matumizi ya nguvu pamoja - pale ilipowezekana - na umoja wa kidiplomasia na kabila moja dhidi ya jingine. Utumiaji wa nguvu ulifanywa kwa njia ya uvamizi ambao pia mara kwa mara uliandamana na uporaji mali.

Reli zilijengwa ili kurahisisha kuingia kwao bara. Reli ya Uganda, ambayo inaunganisha sehemu za ndani za Uganda, na Kenya pamoja na mwambao ilifika bondeni mwa Ziwa Victoria mnamo 1901. Kadhalika Wajerumani walianza kujenga reli na barabara mbalimbali. Reli ya kwanza ilianza kujengwa pwani Tanga baada ya 1891 na ikafika chini ya vilima vya Usambara mwaka 1905.

Majibu kutoka Kenya

Kama ilivyoelezwa tayari, majibu ya Waafrika juu ya yote haya yalikuwa kupambana kijeshi au kutumia diplomasia, ingawa wakati mwingine ama watu hawakushirikiana

au waliondoa kati harakati au waliacha mambo yawe yalivyokuwa. Mathalani Wanandi Kenya walipinga kijeshi ujenzi wa reli katika eneo lao. Kati ya watu wote wa Kenya, wao ndio waliopigana vita vya kijeshi dhidi ya ubeberu wa Waingereza kwa muda mrefu kuliko wote. Upinzani wao, ulioanza kunako miaka 1890 hivi, haukuisha mpaka kiongozi wao alipouawa na makamanda wa Kiingereza mwaka 1905. Kiongozi huyo alikuwa akienda kwenye mapatano bandia yaliyokuwa yametayarishwa nao. Tukio hili liliudhoofisha upinzani wa wananchi na hatimaye Waingereza wakalitwaa na kulikalia eneo lao.

Kwa wananchi kuweza kumpinga Mwingereza kwa kipindi kirefu namna hiyo kulitokana na hali ya jamii hiyo. Jamii yao ilikuwa imegawanyika katika vitengo mbalimbali na kila kimoja kilikuwa na visehemu vidogo vilivyoitwa *pororiet.* Morani kutoka kila *pororiet* walikuwa na jukumu la kulinda sehemu yenyewe. Kwa hiyo, Morani walilala katika kibanda kimoja. Mtindo huu ulikuwa unakaribiana na mtindo wa kuwa na jeshi la ulinzi. Majeshi haya yote ya visehemu yalikuwa chini ya uongozi wa *orgoiyot* au kiongozi wa kijadi. Kiongozi huyu ndiye aliamua lini jeshi lingeweza kufanya mashambulizi. Majeshi yaliunganishwa naye kupitia kwa mwakilishi wake binafsi aliyehudhuria vikao vya baraza katika kila sehemu. Kwa sababu nchi badala ya koo ndio iliyokuwa kitovu cha mtindo wao wa maisha, wananchi hawukuwa na mgogoro ya kikoo. Tokeo lake likawa jamii iliyoshikamana; na umoja huu uliwafanya wawe na nguvu za kijeshi kuliko majirani zao.

Hali hii inatofautiana sana na ile ya jamii nyingine katika Kenya. Mathalan katikati mwa nchi hii, kila kiongozi, kabila au ukoo ulikuwa na namna tofauti ya kuukabili uvamizi wa wageni hao. Mfano hasa ni ule wa akinzani wa Waiyaki kati ya Wagikuyu. Wazazi wake walikuwa na asili ya Wamasai ambao walihama na kukaa kusini mwa nchi ya Wagikuyu kwa sababu ya migogoro iliyotokea kwao katika karne ya kumi na tisa. Huko Waiyaki akawa maarufu hasa kwa sababu ya uhusiano wake na misafara ya wafanyabiashara. Kwanza alijenga urafiki na Kampuni ya *Imperial British East Africa Company* (I.B.E.A.C); watu ambao walimkosea na kumfikiria kuwa alikuwa mtawala mkuu wa Wagikuyu wote. Aliwezesha kupita kwa usalama msafara maalumu wa Court Teleki kusini mwa nchi ya Wagikuyu. Alifanya pia mkataba wa udugu wa damu na Frederick Lugard ambaye wakati huo alikuwa wakala wa Kampuni hiyo. Katika jamii ya Wakikuyu, sherehe ya udugu wa damu ilikuwa dalili ya juu ya imani baina yao. Baada ya mkataba huo, Waiyaki alimruhusu Lugard kujenga boma nchini mwake. Lakini baadaye maombi yake ya silaha yalipokataliwa na Kampuni, wawakilishi wa ubeberu wa Mwingereza, aliwageuka na kuteka kituo chao cha Dagoretti. Halafu tena akabadili mbinu zake na kujiunga katika juhudi za kidiplomasia pamoja na wageni hao ili kulinda hadhi yake lakini baadaye aliondolewa nchini. Tabia hii ya Waiyaki inaelezea jambo ambalo mara kwa mara halitajwi, kwamba hakuna mtu ambaye anaweza kuwa mpinzani au mwenye kushirikiana na wengine maisha yake yote. Watu hubadili mbinu zao kulingana na hali ilivyo na huenda kutokana na kuelewa vyema mazingira yanayowazunguka.

Mmasai Lenana pia alijiunga na Waingereza kinyume na kundi jingine la Wamasai waliopinga wageni nchini mwao. Mara nyingi wale ambao walijiunga na Waingereza walizawadiwa vyeo kama vile uchifu katika utawala wa kikoloni. Kwa hiyo Lenana, kama wengine wengi, alifanywa Chifu mkuu wa Wamasai Kenya.

Sehemu za pwani, familia ya kina Mazrui ilipinga utawala wa Kampuni ile (I.B.E.A.C). Upinzani huu uliongozwa na Mbaruk bin Rashid aliyeanzisha vita vya "gonga – kimbia" dhidi ya majeshi bora ya Waingereza. Iliwabidi walete vikosi vya majeshi ya Wahindi kuwasaidia ili wapate kumshinda. Alikimbilia Tanganyika (Tanzania), ambako aliangukia mikononi mwa Wajerumani.

Ndani kabisa ya nchi, Wakamba hawakupenda kuingiliwa na Waingereza katika mambo yao. Kujengwa kwa kituo cha Machakos na Kampuni yao (I.B.E.A.C) katika mwaka 1889 kulizua ugomvi kati ya Kampuni hiyo na wenyeji. Watumishi wa Kampuni walipora chakula na mali – hasa mbuzi na ng'ombe – kutoka maeneo ya kandokando. Waliyavamia pia madhabahu ambayo yaliheshimiwa na watu kama mahali patakatifu. Kwa kupinga kitendo hiki wenyeji hao, chini ya Msiba Mwea, walianzisha ususiaji wa kituo cha Kampuni mwaka 1890 kwa kutokukiuzia chakula. Usalama ulipatikana tu baada ya Lugard kufanya mkataba wa amani ambao ulihusisha mkataba wa udugu wa damu na wenyeji.

Kaskazini mwa Kenya, nyuma ya sehemu za Kisimayu katika Ogaden Somalia familia ya kina Mazrui na Wakamba walipinga uvamizi wa Waingereza. Huko nako ilibidi kuleta jeshi kutoka India kusaidia ndipo wakashinda mnamo mwaka 1899. Wataita, ambao walikataa kutoa hamali na kupinga misafara ya wafanyabiashara kuingia nchini mwao, walizingirwa mwaka 1897 na majeshi ya Kampuni yakiongozwa na Kapteni Nelson . Vita vilikuwa vikali hata Nelson mwenyewe pamoja na askari wake kumi na mmoja walijeruhiwa kwa mishale ya sumu ya Wataita kabla ya kuwashinda.

Sehemu nyingine Magharibi mwa Kenya, ile ya Waluyia, hali ilikuwa ni ile ile, wakiunganisha mapambano ya kijeshi na hila za kidiplomasia. Mfalme Mumia wa Wanga alikuwa hasa stadi katika matumizi ya diplomasia. Alihitaji kuungana na Waingereza ili wamsaidie kueneza utawala wake katika sehemu yote ya Kenya Magharibi, wakimsaidia kushinda mahasimu wa kandokando kama vile Waiteso na Waluo waliokuwa wakigombana naye mara kwa mara. Kadhalika Waingereza walimuona Mumia kama msaidizi wao katika kueneza utawala wao katika sehemu hiyo yote. Kusema kweli, utwaliwaji wa Kenya Magharibi na Waingereza uliwezekana hasa kwa msaada wake.

*Majibu Kutoka Tanganyika*

Hali ya mambo katika Tanganyika ilikuwa sawa na ile iliyokuwako Kenya. Yaani mbinu ziliunganisha matumizi ya nguvu za kijeshi na vile vile umoja wa kidiplomasia. Wambunga walipambana na majeshi ya Wajerumani katika mwaka


1891 na katika 1893 na wakati huo huo sehemu za ndani nyuma ya Kilwa zilizokuwa zikianzisha upinzani wa kijeshi chini ya Hassan bin Omari. Wamakonde walipinga kuingiliwa na Wajerumani mpaka 1899. Wahehe, chini ya mtemi wao Mkwawa, waligombana na majeshi ya Wajerumani mwaka 1891 na kuwaua wapatao 290. Wajerumani nao wakaamua kulipa kisasi. Mwaka 1894 walivamia eneo la Wahehe na kutwaa mji wao mkuu. Lakini kiongozi wao Mkwawa, akawatoroka. Baada ya kuwindwa miaka minne na maadui wake, alijiua kusudi asikamatwe nao.

Wenyeji wa pwani Tanganyika walifanya upinzani wao chini ya uongozi wa Abushiri. Abushiri alizaliwa mwaka wa 1845. Baba yake alikuwa Mwarabu na mama Mworomo. Alikuwa dhuria wa mmoja kati ya walowezi wa kwanza pwani , akiwa pia mmoja kati ya kabila ambalo lilijihesabu kuwa ni la wenyeji. Kama wengine wengi, alipinga utawala wa Usultani wa Zanzibar sehemu za pwani na hata akafikiria kudai uhuru. Alipokuwa kijana, aliwahi kufanya biashara ya pembe za ndovu bara. Kutokana na faida aliyopata, alijinunulia shamba na kupanda miwa. Alikuwa pia akiendelea na kampeni dhidi ya Wanyamwezi. Hayo yote yalimwezesha kukusanya wapiganaji ambao walikuja baadaye kutumiwa dhidi ya Wajerumani. Chini yake mnamo mwezi Septemba 1888, watu wa pwani waliipiga bunduki manuwari ya Wajerumani Tanga na halafu kuwaamuru kuondoka katika siku mbili . Baadaye walishambulia Kilwa na kuua Wajerumani wawili. Wakiuita "Uasi wa Waarabu", Wajerumani walimpeleka Herman Ven Wissman kuukomesha. Alifika Zanzibar mwezi Aprili 1889, akamshambulia Abushiri katika ngome yake karibu na Bagamoyo na kumng'oa. Alikimbilia Kaskazini sehemu za Uzigua ambapo alisalitiwa na kupelekwa kwa Wajerumani waliomnyongea Pangani Desemba 15, 1889. Hatimaye upinzani wa pwani ulikwisha Kilwa ilipopigwa mizinga na kutekwa na Wajerumani mwezi Mei 1890.

Mbali na wale waliotumia silaha za kijeshi ili walinde uhuru wao katika Tanganyika, kulikuwepo wengine waliochagua silaha ya diplomasia. Tukitaja mifano miwili tu, Marealle na Kibanga karibu na milima ya Usambara na Kilimanjaro katika Tanganyika walikuwa miongoni mwa walioshirikiana na Wajerumani kusudi washinde mahasimu wao. Hao, na wengine kama vile Wanga katika kenya, waliamini kuwa walikuwa wakiwatumia zaidi wao, kuliko walivyotambua.

## Majibu Kutoka Uganda

Katika Uganda pia kulikuwa na upinzani kama huo dhidi ya ukoloni wa Mwingereza. Kipindi kati ya 1899 na 1899 kulizuka mapambano kati ya majeshi ya Kabarega, mfalme wa Bunyoro na yale ya Lugard na wakala wengine Waingereza. Baada ya mapambano ambapo majeshi yake yalishindwa, Kabarega, akaamua kutumia diplomasia. Mara mbili alijaribu kusikilizana na Lugard lakini huyu alimkatalia katakata. Baadaye, alianzisha vita vya askari wa msituni, labda vya kwanza vya aina yake katika Afrika Mashariki. Aliondoka Bunyoro kuelekea kaskazini kwa Walango.




7.1 *Watu wa nchi za Afrika Mashariki, ikionyesha maeneo ya maasi ya Maji Maji*

Kutoka hapo aliyahujumu mara kwa mara majeshi ya Waingereza. Lakini ngome yake ilishambuliwa mwaka 1899, akashikwa na kuhamishwa kwanza Kisimayu na toka huko akapelekwa visiwa vya Shelisheli ambako alifariki mwaka 1923.

Mwanga, alipopewa ufalme mwaka 1894, alionekana kuwashuku Wazungu, hasa wamisionari wakati huo; kwa hiyo alizuia watu wake kuhusiana kwa namna yoyote ile nao. Wale Baganda ambao walifuata Ukristo na kutotii amri zake waliuawa kama wasaliti. Lakini, mfalme huyo alipinga vikali jitihada za Waingereza kutawala nchi yake hata walipokuwa wakijificha ndani ya kanzu za wamisionari. Ustadi wake katika diplomasia pia ulijidhihirisha katika namna alivyodanganya dini mbali mbali zilizokuwa zikipambana mara kwa mara. Wakati fulani, angeweza kushirikiana na makanisa ya Kikristo, Wakatoliki na Waprotestanti, dhidi ya Waislamu alipodhani kuwa Waislamu walikuwa na nguvu zaidi walitishia utawala wake. Wakati mwingine, angejiunga na Waislamu dhidi ya Wakatoliki, Waoprotestant au wote wawili kulingana na yule ambaye alidhani ni hatari kwa utawala wake. Ilipolazimika, alitumia mila za kijadi akijaribui kuwafukuza wageni kama ilivyotokea mwaka 1888. Wakati huu, alikusudia kuwapeleka wageni wote na wafuasi wa Waganda kwenye michezo ya kijadi majini. Nia yake ilikuwa kuwapeleka katika kisiwa kimoja katika Ziwa Victoria na kuwaacha kule wakifa kwa njaa. Walakini, mpango wake uligunduliwa na wageni ambao walimng'atua na kumteua kaka yake mtawala kibaraka. Baadaye katika mwaka 1889, Mwanga aliweza tena kuwa mfalme lakini akaondoshwa na akaungana na Kabarega nchini Lango ambapo wote wawili walitekwa na kuhamishiwa Kisimayu, alihofia mnamo mwaka 1903.

Lakini kulikuwa na Waganda wengine, hasa Baganda, waliojiunga kwa hiari tena kwa dhati na ubeberu wa Waingereza. Wakala waki Baganda, hasa baada ya mapatano ya 1900, ndio walichukua jukumu la kueneza ukoloni wa Mwingereza katika sehemu nyingine za nchi. Kakunguru, jemadari mmoja Muganda, alikuwa mashuhuri miongoni mwao. Yeye aliwazidi wengine wote katika kueneza utawala wa Mwingereza Mashariki na Kaskazini mwa Uganda. Mathalani, ni yeye ambaye alimshika Kabarega wakati Uingereza waliposhambulia ngome yake katika nchi ya Walango. Mapatano ya 1900 yaliwafanya Baganda wawe wabiya wa Waingereza katika kueneza ubeberu wa Waingereza katika eneo hilo. Baadaye chuki ya ukoloni ilikuja kuwaelekea zaidi Baganda kuliko Wakoloni wenyewe. Na mengi kati ya matatizo ya kisiasa yaliyoisumbua Uganda baadaye yalisababishwa na ubia huo kati ya Waingereza na Baganda.

## *Afrika Mashariki chini ya Utawala wa Mkoloni*

Walipong'oa upinzani Afrika 'Mashariki na kutawala barabara maeneo yaliyo athiriwa wakoloni walianza kuyapa maeneo hayo sura mpya ya kisiasa na, muhimu zaidi, ya kiuchumi. Kusudi lao lilikuwa kuugeuza uchumi wa Afrika Mashariki uwe wa utoaji nje bidhaa na kulifanya eneo hilo lifungamane na Ulaya. Hivyo, lilitakiwa

kuwa zaidi asili ya mali ghafi kuliko kuwa eneo la viwanda. Kama ilivyokwishaelezwa, moja kati ya shughuli za mapema za mkoloni ilikuwa kujenga reli Tanganyika mpaka sehemu za Usambara na Kilimanjaro na vile vile Kenya wakiunganisha pwani na bonde la ziwa Victoria. Sehemu ya Ukamba ndiyo ya kwanza Kenya iliyokaliwa na walowezi weupe mwishoni mwa 1890.. Lakini kati ya makabila yote ya Kenya, Wamasai kuliko wengine wote, ndio waliopoteza ardhi yao kwa ajili ya walowezi hao. Ardhi yao ilichukuliwa mara mbili. Ilichukuliwa mara ya kwanza mwaka 1904 wakati walipohamishiwa katika eneo tengo huko Laikipia, na mara ya pili mwaka 1911 walipotolewa kwenye ardhi yao ili walowezi weupe wapate mahali pa kuishi. Katika safari zote mbili serikali ya mkoloni ilidai kwamba ilikuwa imewekeana mkataba wa Wamasai kuihama ardhi yao. Hata hivyo katika safari ya pili, Wamasai walipinga uamuzi huo katika mahakama ya Waingereza; lakini kama ambavyo tungetegemea iliamuru kuwa Wamasai hawakuwa na haki. Wakati huo, walowezi weupe pia walikuwa wameanza kukaa Tanganyika. Hadi kufikia 1905 kulikuwa na walowezi 284, hasa katika sehemu za Usambara na Kilimanjaro.

Tangu mwanzo, Walowezi walijaribu kumiliki makoloni hayo. Kwa mfano katika Kenya, kunako mwaka 1902 hivi, waliunda Shirika la Wakulima na Wafugaji ili kuharakisha madai yao ya kupewa nyanda za juu za Kenya. Ingawa Wahindi walitumiwa katika ujenzi wa reli ya Uganda, lakini wao walitengwa mbali na eneo hilo. Eliot, gavana wa wakati huo, alikubaliana na madai hayo na kuwaweka Wahindi katika eneo lililokuwa kandokando ya reli. Sera ya kuwaweka Wahindi katika nyanda za juu hatimaye ilitumiwa na kila Balozi wa nchilindwa na kila gavana aliyekuja baada ya Eliot. Walipoona hivyo, Wahindi nao waliunda shirika lao binafsi lililodai kupewa sehemu ya nyanda za juu. Mwaka 1907, walipeleka swala lao kwa Waziri wa makoloni ya Uingereza, Winston Churchill, alipozuru Afrika Mashariki. Mgogoro huo haukutatuliwa mpaka kwenye miaka ya 1920. Hadi kufikia mwanzo wa Vita Vikuu vya Dunia, mazao ya kibiashara au uchumi wa mashamba makabwa Kenya ulikuwa hasa mikononi mwa walowezi weupe waliokataa kuwashirikisha Waafrika na Wahindi. Hali hii iliwafanya Waafrika wachukie kuwepo kwa Wazungu Kenya.

Hali katika Tanganyika na Uganda ilikuwa tofauti. Katika Tanganyika, ukianzia kusini mwa nchi, Waafrika walitiwa moyo, mwanzoni na wamisionari, na baadaye na maafisa wa kikoloni, kujiingiza katika uzalishaji wa wakulima wadogo wa mazao ya kibiashara hasa pamba na kahawa. Pia mashamba ya pamoja ya pamba yalianzishwa. Hadi kufikia mwaka 1908 Waafrika walikuwa wanasafirisha nje theluthi ya pamba iliyouzwa nje ya Tanganyika. Na mnamo mwaka 1912, mchango wa Waafrika katika usafirishaji nje wa zao hili ulikuwa zaidi ya asilimia sabini. Wakati huo huo, katika sehemu za Kilimanjaro kahawa iliyolimwa na Waafrika ilikuwa imefikia kiasi sawa na kile cha walowezi. Kadiri ya mabadiliko yaliyopatikana Tanganyika yanadhihirishwa na idadi ya wafanyakazi wa kulipwa ujira. Makadirio ya 1931 yalionyesha kuwa Waafrika waliolipwa ujira Tanganyika walikuwa 172,000 au takribani theluthi moja ya watu wazima wa jinsi ya kiume wakati huo.

Yamkini mabadiliko ya maana kuliko yote katika uchumi yalifanyika Uganda, ukilinganisha na yale ya Kenya na Tanganyika. Katika Uganda, Mkataba wa 1900 uligawa ardhi katika jitihada za kuunda tabaka la wenye ardhi ambalo lingetii mfumo wa mkoloni. Mgawanyo huu wa ardhi ukaleta matabaka tofauti na uhusiano wa kimali kwani sasa kulitokea mabwanyenye wenye kumiliki ardhi na wenye kukodi ardhi. Zaidi ya hayo, ilifahamika kuwa Uganda ilitakiwa kuwa nchi ambapo mazao ya kilimo ya Waafrika yangekuwa mengi kuliko pote. Hii ilikuwa sababu mojawapo iliyojitokeza kama kipingamizi cha kuwepo Wazungu walowezi wengi Uganda kama vile ilivyokuwa katika Kenya na Tanganyika. Kinyume na Kenya, lakini sawa na Tanganyika utawala wa kikoloni ulijitahidi kuweka mikononi mwa wenyeji uchumi wa Uganda. Mambo yaliyoanza Buganda yalienezwa baadaye katika sehemu nyingine za koloni hilo hasa Magharibi ambapo hali ya hewa ilikuwa nzuri kama Buganda. Hadi kufikia 1907, pamba iliyopatikana kwa namna hiyo ilifikia asilimia 35 ya mazao yote yaliyosafirishwa nje ya Uganda. Kwa ujumla, shughuli za kifedha zilikwishastawi vizuri katika Uganda, kama zilivyokuwa kwingineko Afrika Mashariki kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Wakulima waliuza mazao yao kwa wafanyabiashara Waasia na Wazungu. Uchumi wa fedha ulikwishaanza na misingi ya kujiingiza zaidi katika mfumo wa Kibepari ilikwishawekwa.

Matakwa ya mfumo huo yaliwakabilisha Waafrika na yaliyokwishatokea na yaliyoendelea kutokea bado kati yao. Haya ni pamoja na kuanzishwa kwa kodi ya nyumba, masharti ya kazi, kupoteza ardhi zaidi, kutokuwa na uhuru wa kisiasa na kuutengua utamaduni wao. Kodi hazikuanzishwa hasa kwa madhumuni ya kuinua uchumi, bali zilikuwa kama njia ya kuwaingiza kwa nguvu Waafrika katika mfumo wa ufanyaji kazi na uchumi wa fedha, mbali na nyumbani kwao. Wafanyakazi walihitajika katika mashamba ya walowezi na katika kazi za huduma kwa umma kama vile ujenzi wa barabara. Mara nyingi hali za kufanyia kazi kwa Waafrika zilikuwa ngumu. Kulikuwa na athari nyingine zilizoletwa na wakala wajanja zaidi wa ubeberu kama vile wamisionari na wafanyabiashara.

## Harakati za kupinga Ukoloni katika Afrika Mashariki mpaka 1914

Aina mbalimbali za mielekeo na majibu vilijidhihirisha kupinga au kukubaliana na jinsi kila moja ya shughuli za ukoloni ilivyotazamwa. Mwanzoni mwa ukoloni, kila eneo lilikuwa na mwelekeo tofauti isipokuwa katika maeneo machache ambako shughuli zao ziliratibiwa. Kenya, kama penginepo katika Afrika Mashariki, majibu ya mapema ya watu kama vile kina Mazrui na Wananchi yalikuwa na maoni ya kulinda uhuru wao dhidi ya tishio la wageni. Majibu yaliyotokea baadaye katika mabara ya nchi hizi yalikusudiwa kuwatoa watu katika kunyanyaswa na kutawaliwa na mkoloni. Ingawa haya hayakuwa mapambano ya kitaifa katika maana yake ya leo, kulikuwa na dalili za kuanza kwake. Kati ya Waluo wa Kenya Magharibi mwaka 1910, kupinga kutawaliwa na wamisionari kulisababisha kuanzishwa kwa kanisa huru chini ya John

Owalo. Na mwaka 1913 pakaja madhehebu ya Mumbo, chama kilichopinga utawala wa mzungu kwa kutumia dini na itikadi. Kutoka nchi ya Waluo, kilienea mpaka Gusii, dalili kwamba kiliweza kuenea katika sehemu nyingine za Kenya. Utawala wa ukoloni ukaamua kuizima dini hii kama walivyofanya na jambo lolote jingine lililotishia utawala wao.

Chama sawa na hicho kilichoelezwa hapo juu kilianza kwa Wakamba, Mashariki mwa Kenya. Huku kilipinga jinsi masetla walivyowatendea wafanyakazi Waafrika Ukambani. Hapa pia dini ilitumiwa kama kisingizio. Mambo yalianza mwuka 1911 wakati ambapo bibi mmoja aliyejulikana kama Siotume iliposemekana kuwa alikuwa amepagawa. Lakini, muda si mrefu, chama kilikuja kuchukuliwa na kijana anayeitwa Kiamba na kukigeuza kuwa chama cha kupinga ukoloni Kenya. Aliunda namna ya polisi iliyomsaidia katika tishio lake. Lakini alikamatwa na kufukuzwa.

Kwa ujumla, katika kipindi kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia, vyama vya kwanza kupinga ukoloni Kenya vilikuwa Magharibi na Mashariki mwa nchi hiyo. Pwani Wagiriama waliokuwa wakimpinga Mwingereza tangu karne ya kumi na tisa waliitumia fursa ya vita ili kuasi utawala wa mkoloni katika mwaka 1914. Waingereza walijibu kwa kuchoma moto nyumba zao na kuwanyang'anya mali yao. Wagirima kama kina Mazrui na wengine walitumia aina ya vita vya askari wa msituni, lakini baadaye walishindwa.

Uganda kulikuwa na usalama zaidi kuliko Kenya. Lakini katika mwaka 1911, Kaskazini mwa Uganda Waacholi waliasi utawala wa Waingereza. Walikuwa wanapinga namna yao ya kuajiri watumishi na sera ya kunyang'anya silaha. Jukumu, mojawapo kubwa la ukoloni lilikuwa kuhakikisha kuwa watawaliwa hawakuwa na uwezo wowote mbele ya unyonyaji wao mkatili. Kwa hiyo ilikuwa muhimu kwamba wasiwe na bunduki. Ndiyo maana waliwasaka na kuwanyang'anya silaha walizokuwa nazo. Waacholi walikataa kuzirudisha kwa hiari. Lakini, walishindwa katika mapambano ya kivita yaliyotokea.

Katika Afrika Mashariki, ukinzani muhimu kuliko wote dhidi ya utawala wa mkoloni wakati huo – Vita vya Maji Maji vilitokea Tanganyika; na katika vita hivi dini na ushirikina vyote vilitumika (taz. mchoro 7.1). Ushokoa, kodi, unyanyaswaji, na hali ngumu za kazi, yote hayo yalisababisha vita vya Maji Maji. Lakini, sababu hasa iliyoleta mapambano haya ilikuwa ni kuanzishwa mradi wa kulima pamba kwa pamoja. Watu walitakiwa kufanya kazi katika mradi huo siku ishirini na nane kwa mwaka. Lakini mapato hayakwenda kwao, badala yake walipewa mishahara midogo sana kiasi ambacho baadhi yao walikataa kuipokea. Kusema kweli Waafrika hawakuwa wakipinga kilimo cha pamba kwani wao wenyewe walikwishakubali kulima zao hilo kama zao la biashara. Ila walipinga mradi huo ambao ulikuwa ukiwanyanyasa na kuvuruga uchumi wao kwa kuwalazimisha kuacha mashamba yao binafsi na kufanya kazi katika yale ya huduma kwa umma.

Ili kuwaunganisha Watanganyika katika mapambano na Wajerumani, kiongozi wa chama, nabii Kinjekitile Ngwale, alitumia imani za kidini. Aliwafundisha kuwa



7.2 *Mwanga (c. 1866 – 1903). Mfalme wa zamani wa Buganda, na Kabarega (c. 1850 – 1823), Mfalme wa zamani wa Bunyoro wakiwa njiani kuelekea*

umoja na uhuru wa Waafrika wote lilikuwa jambo la msingi. Kwa hiyo hakuwa na budi kujiunga na kupigania uhuru wao dhidi ya Wajerumani katika vita ambavyo viliagizwa na Mungu. Pia wangesaidiwa na wahenga ambao wangefufuka. Chama, ambacho kilikuwepo tangu Julai 1905 hadi Agosti 1907, kilienea sehemu ya km mraba 26,000 ya theluthi ya Kusini mwa Tanganyika.

Vita vilianza katika wiki ya mwisho ya Julai 1905 na wa kwanza kuumizwa walikuwa mwasisi mwenyewe na makamu wake walionyongwa tarehe 4 Agosti 1905. Kaka yake alishika nafasi yake na kuchukua cheo cha Myamguni, mmoja kati ya miungu katika eneo hilo. Aliendelea kuwapa watu "maji", lakini hawakufaulu. Wahenga hawakufufuka kama ilivyoahidiwa na chama kilivunjwa vikali na watawala wa Kijerumani.

Uasi wa Maji Maji ulikuwa chama cha kwanza kikubwa cha kupinga Ukoloni katika Afrika Mashariki. Kama alivyonena John Iliffe, ilikuwa "jitihada ya mwisho ya jamii kongwe za Tanganyika kuukomesha ukoloni kwa nguvu". Tena kilikuwa chama halisi cha wakulima dhidi ya unyonyaji wa mkoloni. Katika Tanganyika, kilitikisa utawala wa Wajerumani ambao jibu lao halikuwa tu kukizima chama hicho bali pia waliuachilia mbali mradi wa kulima pamba kwa pamoja. Pia kulikuwa na mabadiliko katika muundo wa kikoloni, hasa katika kuajiri na kutumia watu namna ambayo ukoloni ungekubalika kwa Waafrika. Lakini kwa vyovyote vile vita vilishindwa, kushindwa ambako kwa hakika kulilazimisha "kuondoka kwa jamii kongwe".

Kwa ujumla, kati ya 1890 na 1914 mabadiliko makubwa yalitokea katika Afrika Mashariki. Ukoloni ulilazimishwa kwa nguvu na mara nyingi kwa ukali hata kama ukali wenyewe wakati mwingine ulifichwa katika umbo la sheria. Waafrika mwanzoni walitumia yote mawili, mapambano ya kijeshi na juhudi za kidiplomasia. Wakijaribu bila mafanikio kulinda uhuru wao. Pale ambapo Waafrika hawakushughulika kijeshi au kidiplomasia, walikubali au hawakujali, isipokuwa pale walipolazimishwa. Mwanzoni, ukoloni ulimaanisha kuunda upya maisha ya watu, kisiasa na kiuchumi. Kodi, kazi za kulazimishwa na kunyimwa haki za kisiasa vikaanzishwa. Baadhi ya Waafrika walipinga mabadiliko haya vikali na wengine wakasaliti amri. Katika Tanganyika na Uganda, baadhi ya wakulima Waafrika walitegemea mazao ya kibiashara yatokanayo na uzalishaji wa wakulima wadogo hasa pamba na kahawa. Kenya, Waafrika walikatazwa kupanda mazao ya kibiashara. Huko uchumi ulikuwa mikononi mwa masetla. Majibu mbalimbali ya Waafrika kuhusu hali hii yameelezwa kwa ufupi. Mengine yalikuja katika kipindi baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia.

# 8

# *Juhudi na Ukinzani wa Waafrika: Afrika ya Kati 1880-1914*

Katika Afrika ya kati, juhudi na ukinzani wa Waafrika dhidi ya kutamalakiwa na wazungu, vilikuwa na sura kadhaa kati ya miaka ya 1880 na 1914. Afrika ya kati inafafanuliwa kama eneo linalojumuisha tawala za Kongo ya Wabelgiji (Zaire), Rhodesia ya Kaskazinii (Zambia) Nyasaland (Malawi), Angola na Msumbiji. Kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Afrika karibu na kipindi cha mnyang'anyiro, Afrika ya Kati ilikuwa na wenyeji waliojitawala kwa falme au mifumo msonge ya kisiasa au hata katika tawala ndogo ndogo zaidi. Katika kundi la kwanza palikuwepo falme za Lunda na Luba huko Zaire, dola za Humbe na Chokwe huko Angola, ufalme wa Mwenemutapa huko Msumbiji, ufalme wa Undi kule Nyasaland, na dola nyingine nyingi zilianzishwa na Wanguni au Wakololo katika mabonde ya Zambezi – Limpopo. Kwa upande wa kundi la pili, palikuwepo tawala za Wayao na Watonga huko Nyasaland; tawala za Wabisa na Walala huko Rhodesia ya kaskazini, tawala za Wasena na Wachopi nchini Msumbiji na za Wakisama na Waloango huko Angola na Walonga na Wabewe wa Kongo ya Ubelgiji. (taz. picha 8.1). Licha ya kuwepo migawanyiko hii ya kisiasa au tofauti nyingine za kikabila na kimikoa, au kuwepo migogoro anuwai kati ya matabaka mbalimbali yaliyoanza kuchipua, bado mapambano halisi na ukinzani ndiyo njia kubwa iliyotumiwa na Waafrika kupinga kutamalakiwa na Ubeberu wa Kizungu.

Badala ya kuelezea tu shughuli za kupinga ukoloni zilivyoendeshwa katika nchi mbalimbali, tutaelekeza majadiliano yetu katika mitindo na ruwaza za ukinzani zilizotumiwa katika eneo hili la Afrika kwa ujumla. Tukiutazama ukinzani wa Waafrika kwa kuzingatia malengo waliyokuwa nayo, tunaweza kupata makundi makuu matatu:

(1) Ukinzani au mapambano ya kivita yaliyotaka kuudumisha uhuru wa jamii za asili;

(2) Ukinzani wa wenyeji ambao ulitaka kukomesha vitendo (vibaya) maalumu vilivyofanywa na dola ya wakoloni na;

(3) maasi ambayo yalilenga kuubomoa kabisa huu mfumo wa utawala wa kigeni ambao ndio uliozua madhala yote;



**8.2** *Gunguyane na wapiganaji wake.*


## *Jitihada za Kudumisha Uhuru: Kipindu cha Mapambano na Umoja*

Mikataba ya mapambano iliyotumiwa na Waafrika wa Kati ilikuwa na lengo moja - yaani kuwafukuzilia mbali wazungu na kulinda nchi yao, mtindo wa maisha ya nyenzo na maisha yao. Huko Nyasaland, kwa mfano, Wanguni wa Gomani walishambulia stesheni za misheni katika mwaka wa 1896. Kwa kiasi fulani hii ilitokana na kupinga athari ya kudhoofishwa iliyotokana na Ukristo. Huko Msumbiji, Wabarue walizikatisha tamaa jitihada za kutaka kuwajumuisha katika utawala wao usiokuwa wa wazi kwa kulitumia kanisa Katoliki kuubatiza Ukoo, Wayao, Wamakua, Wayeke, Wachikunde, Waovimbundu, na Wachokwe tukiwatata wachache tu, walikataa katakata jitihada za Wazungu za kuwakomeshea biashara ya watumwa na kuwaondolea ile dhima yao ya kuwa watu wa kati katika biashara. Kwa pamoja wakulima na wafugaji wengi walipigania zaidi kudumisha udhibiti wao na njia kuu za kuzalisha mali na kuwazuia wazungu kuwapokonya ardhi, wafanyakazi na wanawake.

Viongozi wa Kiafrika walitambua umuhimu wa kupunguza tofauti ya silaha iliyokuwapo baina yao na wazungu ili wasiangamizwe. Hivyo, jamii nyingi zilizokuwa zimeanza kushiriki katika biashara za kimataifa zilitumia nafasi hiyo kufikia hadi kwenye masoko ya silaha, na kwa njia hiyo zilijipatia hazina kubwa ya zana za kivita kwa kubadilishana na mateka. Wachokwe, Waovimbundu na Wachikundu, kwa mfano, walifanikiwa sana kujipatia silaha kiasi kwamba daima majeshi yao yalikuwa na zana bora zaidi kuliko zile za wapinzani wao wa Congo Free State na majeshi ya Wareno yaliyotaka kuwashinda. Watu wengine wa Afrika ya kati ambao hapo awali hawakujihusisha na shughuli za biashara, waliongeza kiasi cha mazao waliyoyasafirisha nchi za nje ili waweze kujinunulia bunduki za kisasa na barnti. Katika robo ya mwisho ya karne hiyo, kwa mfano, Waovambao, Washangaani na hata vizalia vya Wanguni kadhaa ambao hawakupenda mabadiliko waliyoanza kuyaona, walijipatia bunduki za kisasa kwa kuhofia kwamba hapo baadaye wangepambana na Wazungu.

Aidha, jamii nyingi kadhaa za kiafrika ziliongeza uwezo wao wa kujihami kwa kuimarisha ulinzi wa ndani. Wabarue walijenga mitambo ya zana za vita ambayo ilitengeneza baruti, bunduki na hata vipuri vya zana kubwa hususani mizinga. Majengo mapya na ghala ya kujihami yalijengwa, kwa mfano, mji wa ngome wa Jumbe wa Kota na *aringas* wa bonde la Zambezi na la Luangwa.

Ingawa hawa Waafrika wote walikuwa na dhamira moja ya kuzuia kuingizwa kwa utawala wa kigeni na kujipatia zana za kisasa lakini mbinu zilizotumiwa na kila kundi zilitofautiana sana. Katika dola zingine za Kiafrika, Waafrika walitumia ukinzani wa mapambano halisi ya vita ili kuzuia mapennyezo ya Wazungu hata bila kujali ubora wa silaha walizotumia Wazungu hao. Hivyo ndivyo alivyofanya Mwase Kasungu, kiongozi wa Wachewa, aliyewaongoza watu




8.1 *Watu na tawala za Afrika ya Kati, C. 1900*

wake kupambana na Waingereza bila mafanikio na hatimaye akaona bora kujiua kuliko kujisalimisha katika mwaka 1896. Kipindi hicho hicho, Wabihe wa huko Angola walilishambulia ghafla jeshi la wakoloni lililokuwa linatafuta kuweka vituo mbalimbali nchini mwao, ambavyo vingewasaidia wakoloni hao kuwasiliana.

Viongozi wengine wa Kiafrika waliamua kuepuka mapambano ya awali wakitarajia kwamba ama wangesaidiwa kuuimarisha zaidi uwezo wao wa kijeshi au kuweza kuwekeana mikataba ya "haki" ambayo kwayo uhuru wa dola zao ungeheshimiwa. Kwa karibu mwongo mzima Gungunyama alijitahidi kuwekeana mikataba na Waingereza na Wareno na alikuwa tayari kuwaachia mambo fulani fulani ambayo hayangeipotezea dola ya Shaangani uhuru wake. (Tazama picha 8.1). Ukoo wa kifalme wa Wabarue nao ulitumia sera iliyofanana na hii, walijitahidi kumshawishi Karl Peters, yule Mjerumani mpita njia, awaunge mkono. Ukinzani uliofanywa na Wabemba sehemu mbalimbali nchini mwao, mwishoni mwa karne, nao ulitokea baada tu ya kushindwa kwa mbinu zote za kidiplomasia zilizotumiwa kwa miaka ipatayo kumi na tano kati yao na Waingereza. Hata hivyo, mkakati huu, hatimaye uliwaingiza kwenye mapigano kutokana na wazungu kutaka kuyatimiza masharti ya "Utwaaji nchi Kikamilifu" yaliyowekwa kwenye mkutano wa Berlin.

Jamii nyingi za Afrika ya Kati ambazo hazikuwa na uwezo wa kutosha kuzuia Wazungu kuingia nchini mwao, au jamii ambazo hazikuelewa matokeo ya utawala wa kikoloni, mwanzoni zilikubali, kwa amani kabisa, kutawaliwa zilianza kuasi na kuanza kupigania uhuru wao tena. Mtindo huu wa kuchelewesha mapambano ulitumiwa mara kwa mara huko Kongo (Zaire) ambao wenyeji wake walidhani kuwa wawakala wa *Congo Free* walikuwa wafanyabiashara wenzi wao na wangeshirikiana nao katika mapambano yao dhidi ya wageni waliowakamata watu na kuwafanya watumwa wao. Mpaka baada ya maafisa wa *Free State* walipoanza kuwatoza wananchi kodi au kuwatumikisha kazi kwa lazima, ndipo walipogundua kuwa kwa makosa yao wenyewe walikuwa wanaupoteza uhuru wao. Katika kipindi cha kati ya mwaka 1885 na 1905 zaidi ya dazani moja ya vikundi "vilivyokandamizwa" huko Kongo ya chini na ya kati viligoma.

Pamoja na ukweli kuwa ukinzani wa awali ulitofautiana, ni kweli vilevile kwamba wapinzani wenyewe nao walitofautiana katika viwango walivyofikia katika kujitayarisha kushirikiana na kuungana na wengine. Kwa upande mmoja palikuwepo jamii kadhaa, ndogo na kubwa, ambazo zilipambana na uvamizi bila ya kuwa na nia ya kuunda ushirikiano mkubwa zaidi. Kwa mfano, huko Angola Wabihe, Wahumbe na Wangangwela, mwanzoni kabisa walipambana na wavamizi bila msaada wa majirani zao ambao nao pia waliwachukia sana Wareno hao. Ukitazama hata dola mbalimbali za Wanguni, utaona kuwa zilishindwa au hazikupendelea kushirikiana wakati zilipopigana kuwazuia Waingereza kujipanua huko Nyasa. Mnamo mwaka wa 1890 Wamaseke, Wagomani, Wampeseni walipambana na jeshi la kikoloni la Waingereza kila kundi likipigana peke yake;

jeshi ambalo kwa hakika halikuwa na maaskari wa kutosha. Lakini hatimaye wote walishindwa, na kushindwa huko kuliiwezesha Uingereza kuanzisha koloni la Nyasaland.

Tawala zingine za Kiafrika ziliazimia kupanua uwezo wao wa kijeshi kwa kuwa na ushirikiano mpana wa Kimbari au ushirika wa wote wale waliokuwa wanapambana na ukoloni. Kiongozi shupavu wa Wagaza aliyeitwa Gungunyane, kwa mfano aliwaomba Waswazi kuungana nao ili wapambane na Wareno. Wabarue nao walitengeneza mfumo mzuri wa ushirikiano ambao uliwajumuisha Watonga, Watawara na Washona waliokuwa wakiishi Rhodesia ya kusini (sasa yaitwa Zimbabwe). Kama ilivyokuwa kwa Wabarue, inaaminika kuwa ushirikiano huo wa muda ulitumiwa zaidi mahali ambapo hapo awali palikuwepo ushirikiano wa aina fulani wa kiuchumi, kindugu au kidini. Mara nyingi, hata wapinzani wa jadi walitupilia mbali tofauti za zamani na kuweka pamoja matatizo yao ya sasa na kushirikiana kuyakabili, hata kama ilihitaji kupigana vita kwa pamoja. Hali kama hii ilijidhihirisha vizuri wakati walunda (wa kati) na Washoke walipoungana kupigana dhidi ya jeshi la Congo Free State bila kujali uadui waliokuwa nao zaidi ya karne moja.

Kwa kuwa jitihada za akinzani hazikufanikiwa kupata ushindi wa kisiasa, kuwa tabia ya baadhi ya wachambuzi au wanahistoria kupunguza au hata kuyapuuza kabisa mafanikio sisisi ya kijeshi na aghalabu hata kudai kuwa hapakuwepo mafanikio yoyote ila kushindwa tu. Ni kweli kwamba tawala nyingi za Kiafrika zilishindwa na wazungu lakini wakati huo huo mapambano mengine yalifanikiwa kabisa kuwaondoa Wazungu au kuwapatia hasara kubwa. Huko Angola ya kusini, kwa mfano, Wahumbe na Wakuamato walifanikiwa kuyarudisha nyuma mashambulio kadhaa ya Wareno, na katika vita vya 1904 walifanikiwa tena kuwaua maaskari wazungu wapatao 300 kati ya maaskari 500 waliokuwepo vitani. Wachikunda nao, mara kwa mara walilishinda jeshi dhaifu la Lisbon katika mwongo wa mwisho wa karne ya kumi na tisa, ambapo huko Nyasaland ya kaskazini Wayao waliweza kulizuia kabisa jeshi la Waingereza kujiingiza nchini mwao kwa muda wa karibu miaka mitano. Huenda kikundi kilichofanikiwa zaidi kuliko vikundi vyote kilikuwa kile cha muungano wa Waswahili na Wamakua ambacho kilifanikiwa kukaa nje ya utawala wa Wareno hadi mwaka wa 1916; na WaCuamato wa WaCuanhama ambao hawakushindwa hata mara moja mpaka mwaka 1915.

Pamoja na mafanikio hayo waliyopata kwa taabu, hatimaye, vita vyote vya kupigania uhuru vilishindwa. Kushindwa huko kwa Waafrika kuwazuia Wazungu kujiingiza zaidi barani mwao kulitokana na mambo kadhaa na mengi kati ya hayo yalitokea hata kabla ya kugawanywa kwa Afrika. Mambo hayo, yalikuwa ni pamoja na kuanza kushindwa mwanzoni kwa dola nyingi zenye nguvu, tofauti za ndani za tabaka lililokuwa likitawala na mara nyingine tofauti zilizojitokeza kati ya tabaka hilo na watu waliotawaliwa. Matokeo yake kwa jumla yalipunguza uwezekano wa

kupanua au kuunganisha pamoja juhudi zote za kupambana na ukoloni, ambako kulikuwa kunahitajika sana ili kuwakabili wazungu ambao walikuwa na mbinu na silaha za kivita bora zaidi kuliko za Waafrika. Uhasama uliokuwepo miongoni mwa Waafrika nao ulichangia sana kuwawezesha Wazungu kutekeleza siasa yao ya "Watenge Uwatawale" ambayo ilitumiwa kwa ustadi mkubwa na Harry Johnston pamoja na maafisa wengine wa kikoloni. Kwa mfano Wareno walisaidiwa na Wainhambane kuwapiga.

Washangaani walisaidiwa tena na Watonga kuwapiga Wabarue, na halafu wakasaidiwa tena na Wasena kuwashinda Wabarue. Huko Kongo watu wengi walishirikiana na Wabelgiji ili kujikomboa kutoka utawala wa Wayeke au Waarabu au hata kutoka kwa wasaka watumwa. Aidha, watawala wengi wa Kiafrika walielewa ya kwamba kushirikiana kwao na Wazungu kungewasaidia kuzipanua zaidi dola zao. Fikra kama hizi ndizo zilizowafanya na Tipp Tip na watoto wa Msiri kuisaidia *Congo Free State.*

Ni dhahiri kuwa kama Waafrika hawangewasaidia hawa Wazungu kwa njia moja au nyingine, basi Wazungu hawangeweza hata kidogo kuingiza utawala wao kwa urahisi na kwa gharama ndogo kabisa kama walivyofanya. Kwa mfano, zaidi yaasilimia tisini ya majeshi ya Wareno yaliyoshinda vita kwenye bonde la mto Zambezi mwaka 1902 walikuwa maaskari Waafrika. Hali kama hiyo ilijidhihirisha pia huko Angola, ingawa si kwa kiwango kikubwa kama kile cha Zambezi.

## *Ukinzani wa Ndani wa Awali Dhidi ya Utawala wa Kikoloni na Ubepari kwa Jumla*

Tofauti kabisa na ukinzani uliofanywa wakati wa ukoloni ulipokuwa unaingia, ambao lengo lake kuu lilikuwa lile la kutetea na kuudumisha uhuru, ukinzani wa wakulima na wafanyakazi mwanzoni mwa karne ya ishirini ulichochewa na jitihada mbalimbali zilizofanywa na tawala za kikoloni za kuziimarisha zaidi tawala zao na kuanzisha mahusiano ya kibepari miongoni mwa wananchi, mambo ambayo yangewarahisishia wakoloni kunyonya mali asili na nguvu za wananchi wa Afrika ya kati. Ingawa lengo la mtalaa huu sio kuchambua na kulinganisha kwa undani mifumo ya kiutawala ya Wareno, Waingereza, na Wabelgiji, lakini ni vizuri tuchunguze angalau kwa ufupi madhambi waliyowatendea wananchi na ambayo yalisababisha kutokea kwa ukinzani wa ndani wa kila aina katika sehemu anuwai.

Jambo la kwanza kabisa walilolifanya maafisa wa kikoloni lilikuwa kuweka mfumo thabiti wa utawala ambao ungetumiwa kuwadhibiti kikamilifu wale watu waliowatawala. Wakiwa na lengo hilo, waliwafukuza kazi viongozi wengi wa jadi ambao hawakutaka kushirikiana nao hata wakavuka miiko ya kidini na kiutamaduni ya utakatifu wa ufalme. Ili kuimarisha utawala wao dhaifu, Wazungu hawa walianzisha jeshi la polisi na ulinzi lililoitwa *Force Publique of the Congo* au

"Jeshi la Umma" huko Kongo: au *Guerras Pretas* huko angola. La Msumbiji liliitwa *Sepais,* na huko Rhodesia ya kaskazini na Nyasaland likaitwa *British Native Police of Northern Rhodesia* (Jeshi la Kiingereza la polisi Wenyeji) lililosimamia shughuli za "machifu wa kikoloni" na kuwatisha wananchi wengine.

Ili waweze kuwapata manamba wa kufanya kazi katika miradi mbalimbali ya serikali, au katika shughuli zingine za kibepari, wakoloni waliamua kutumia mbinu ya kuwalazimisha watu wawafanyie kazi na kuwatoza kodi kwa nguvu. Huko Kongo, wananchi walilazimishwa kukusanya utomvu wa mipira na kufanya kazi kwenye reli iliyokuwa inajengwa au kwenye migodi. Huko Msumbiji makampuni makubwa kadhaa yalinufaika na utaratibu wa watu kulazimishwa kufanya kazi. Baadhi ya wananchi wa Msumbiji walisafirishwa hadi Rhodesia ya kusini, Afrika ya Kusini na Sao Tome. Katika mashamba makubwa ya kokoa huko Sao Tome, wananchi hawa wa Msumbiji walijumuika na wananchi wengine kutoka Angola.

Wakulima wengine waliobaki nyumbani nao hawakupona kulazimishwa kufanya kazi. Wengi wao walilazimishwa kwa mujibu wa sheria za nchi zao, kuwafanyia kazi umma bure kwa muda wa majuma kadhaa na bila hivyo walijikuta wakifungwa gerezani. Aidha, walitakiwa kuyatekeleza madai yote yaliyotolewa na maafisa wa kikoloni na aghalabu walilazimishwa hata kuyauza mazao yao kwa bei za chini sana.

Madhala haya yote yaliwachochea wakulima na wafanyakazi kuanzisha ukinzani wa kila aina ambao ulielekezwa zaidi katika lengo la kuondoa tatizo fulani maalumu na wala siyo katika kuutekeleza mfumo katili ambao ndio ulioyazuia matatizo yote hayo. Kutokana na kukatishwa katishwa kwa ukinzani huo wa wenyeji, wachunguzi wa wakati huo na hata wanahistoria wanaelekea kuupuuza kwa kiasi kikubwa ukinzani huo. Hata hivyo, ukinzani wa "siku baada ya siku", kujitoa katika "ujambazi - jamii" na maasi ya wakulima ni matukio muhimu sana katika historia ya ukinzani wa ukoloni huko Afrika ya Kati.

Sawasawa kabisa na walivyofanya watumwa wa Amerika ya kusini, wakulima wengi wa Kiafrika walipendelea kuupinga utawala huu katili kisirisiri. Inaonekana kuwa hali hii ilitokana na vikundi hivi vya ukinzani kutokuwa na nguvu za kutosha kupambana na wavamizi wao kivita.

Badala yake, vilidhihirisha chuki yao, kwa kukwepa kulipa kodi, kutegea kazi au kuzifanya polepole mno, au hata kuharibu zana za kazi kisirisiri. Watu wengi sana walikwepa kulipa kodi katika eneo lote la Afrika ya Kati. Ilikuwa kawaida kabisa sehemu hizi, mara watu walipomwona mkusanyaji kodi anakuja, basi watu wote au walio wengi katika kijiji fulani, walikimbilia mafichoni asikokujua mkusanyaji kodi huyo, mpaka aondoke ndipo watu hao walirudi. Huko Rhodesia ya kaskazini Wagwemba, na Watonga wamesifiwa kuwa walikuwa wakwepaji hodari, kama majirani wao Wabisa na Waunga wanavyosemekana kuwa walikuwa wakikimbilia katika vinamasi vya Bagwelu. Huko Msumbiji, wakwepaji

walikuwa ni haba.

Wakulima nao kwa upande wao walijitahidi kubuni mbinu za kujipunguzia au kukwepa kabisa adha ya kulazimishwa kuwafanyia Wazungu kazi. Wakati mwingine wakulima walichukizwa sana na adha hizo hata wakaamua kupigana vita, kama walivyofanya Wanamuhana na Walungu na Rhodesia ya kaskazini, ambao waliamua kuchukua silaha na kuwafukuzilia mbali wakoloni. Aidha, chuki hizi za watu kulazimishwa kuwatumikia wazungu ndizo zilizosababisha mgomo wa Wamanjaga mwaka wa 1893-4 huko Kongo ya chini pamoja na migomo mingine mingi iliyotokea katika mashamba ya mipira. Mbinu zingine walizotumia watu kujihami ni pamoja na watu kujifanya wagonjwa, kufanya kazi polepole, migomo, na hata kutoroka. Katika wilaya ya Abercorn huko Rhodesia ya Kaskazini maafisa wa kikoloni walilalamika kila mara ya kwamba Waafrika "walitegeana, kila mara ilibidi wasukumwe." Hatimaye wafanyakazi waligoma kufanya kazi mpaka wahakikishiwe kuwa watapewa mshahara. Wafanyakazi wengine walioudhika waliamua kuharibu zana za kilimo, wakachoma nyumba na kuiba kwenye bohari za makampuni ya kibepari, au kwenye maduka ya wafanyabiashara wenyeji, na pia waliharibu njia za usafirishaji na mawasiliano.

Wakati mwingine watu walihamia kwenye sehemu zingine nje kabisa ya mipaka yao ikiwa ni njia mojawapo ya kuonyesha kutoridhika kwao. Ingawa si rahisi kutoa tathmini sahihi kabisa ya uhamaji huo, lakini ni dhahiri kuwa uhamaji huo ulikuwa wa kiwango kikubwa. Taarifa za Waingereza zimeonyesha kuwa watu wapatao 50,000 walioishi katika bonde la Zambezi walikimbilia Rhodesia ya kusini na Nyasa kati ya mwaka 1895 na mwaka 1907 wakiwa na matumaini kuwa ukoloni wa Kiingereza ungekuwa na huruma zaidi. (Taz. kielelezo 8.1). Huko Nyasaland Watonga na Watumbuka wengi walioishi kandokando ya Ziwa Nyasa walihama kutoka Rukuvu hadi nje kabisa ya eneo lililotawaliwa na Waingereza ili kukwepa kulipa kodi.

Watu wengi walitumia mkakati wa "kujitoa" na hii ilisababisha kuzuka kwa kambi kadhaa za wakimbizi katika sehemu za maficho. Baada ya kuivuka mipaka, ya kimataifa ya nchi zao, wakulima hawa, wakiwa wametoroka kutoka kwao kutokana na kutotimiza wajibu wao "kisheria", walijiundia makazi yao ya kujitegemea. Hali hii ilijitokeza mara kwa mara miongoni mwa 'waasi' wa Kibemba ambao walikimbilia ndani zaidi ya nchi yao. Hali kama hiyo ilitokea pia kwenye mkoa wa Gambo huko Angola ya kusini, mkoa ambao baadaye uligeuka kuwa maficho ya watoro au waliozinduliwa; na walijificha pia kwenye milima ya Gaerezi ambayo huzitenganisha nchi za Msumbiji na Rhodesia ya Kusini, na katika misitu au katika sehemu za milima huko Kongo.

Jamii zingine kimbizi hazikuridhika na kukaa nje ya utawala wa Wazungu bila kufanya lolote, kwani, jamii hizo aghalabu zilikuwa zikifanya mashambulio ya mara kwa mara kwa tawala mbalimbali za kikoloni. Walisambulia vile vile ishara mbalimbali za ukandamizwaji kama vile mashamba makubwa, waandikishaji

manamba, wakusanyaji kodi, na polisi waafrika. Yote haya walifanya katika jitihada zao za kulinda vijiji vyao vya kiukoo dhidi ya adha za kunyanyaswa au kunyonywa na Wazungu. Eric Hobsbawn amewahi kueleza kuwa 'majambazi jamii' ya Sisili au Brazil ya Kaskazini - Mashariki yalikuwa ni jumuiya za watu zilizoongozwa na viongozi ambao watu wao hawakuwaona kuwa ni wahalifu pamoja na ukweli kuwa walikuwa wakikiuka sheria kadhaa za kikoloni. Kiongozi maarufu wa 'majambazi jamii' anayefahamika ni Mapondere, ambaye alipambana na majeshi ya Rhodesia ya kusini na yale ya Wareno kati ya mwaka 1892 na 1903 na wakati huo huo alizizuia jitihada za wakoloni kutaka kuwatoza wananchi kodi, kuwatumikisha kazi bure, au maafisa wa makampuni ya kibepari waliotaka kuwanyonya au kuwatukana wakulima.

Mapondera akiwa na kikosi chake imara aghalabu alishambulia bohari za Camphanhia de Zambezia (Kampuni za Zambezi) na maduka ya wafanyabiazshara wa vijijini ambao Mapondera aliwaona kuwa walikuwa na ishara za unyonyaji wa kiuchumi. Aghalabu Waasi hawa walinusurika kuangamizwa hususani kutokana na kuungwa mkono na wananchi ambao mara kwa mara waliwapa misaada ya chakula, baruti, na taarifa zingine muhimu. Vikundi vingine kadhaa vya 'majambazi jamii' vilikuwepo huko Msumbiji ikiwa ni pamoja na kikundi cha mrithi wa Mapondera, cha Dambvakushambam, cha Moane cha Samakungu pamoja na kule kwenye milima ya Huila huko Angola ya kusini. Ushahidi huu unathibitisha kuwa ukinzani wa aina hii ulitumiwa kw wingi na ingefaa uchunguzi ufanywe kuona kama ulikuwepo katika sehemu zingine zote za Afrika ya Kati.

Wakati mwingine hata yale majeshi yaliyoandikishwa kuwaangamiza waasi fulani nayo yaliasi ili kupinga uonevu wa wakoloni ambao wao walishindwa kabisa kunzoea. Kwa kawaida mishahara ya chini sana, adhabu mbalimbali zilitolewa na wakoloni, na tabia za kigeugeu za hawa Wazungu ni badhi ya mambo yaliyowakera sana wananchi na kuwafanya waamue kuasi. Maasi makubwa kabisa yanayofahamika yalitokea huko Congo Free State mwaka wa 1895, ambako kikosi kizima cha Luluaborg kiliasi. Kikiongozwa na askari wa cheo cha chini tu, kilifanikiwa kumwua kamanda mkuu wa kikosi hicho hasa kutokana na utawala wake katili. Waasi hao walifanikiwa kutawala sehemu kubwa ya jimbo la Kasai kwa zaidi ya miezi sita, lakini baadaye walishindwa na majeshi yaliyoendelea kumtambua kamanda aliyeuawa. Miaka miwili badaye sehemu kubwa kabisa ya jeshi la ardhini nayo iliasi.

Aidha wakati wa ukoloni, palikuwepo pia maasi madogomadogo mengi ya wakulima yaliyodumu kwa muda mfupi tu. Ilitokea mara chache sana wakulima kuimarisha au kupanua sehemu walizozishinda au kubadili lengo lao la kuzishambulia ishara tu za kuonewa na badala yake walenge kuushambulia mfumo mzima wa ukoloni na ubepari. Kwa kawaida migomo ilichoehewa na tabia ya wakoloni kuzidi kudai kodi au kuzidi kuwalazimisha wananchi kuwafanyia kazi. Katika (bonde la Zambezi) *Zambezi Valley* kati ya 1890 na 1905 kulitokea maasi

asiyopungua kumi na sita. Migomo hii mingi ilifanywa dhidi ya *Campanhia de Mozambique* (Kampuni ya Msumbiji) na *Campanhia de Zambezia* (Kampuni ya Zambezi), Kampuni ambazo zilipewa sehemu kubwa ya Msumbiji ya Kati. Wakati huo huo palikuwepo pia maasi madogo madogo huko Angola. Maasi ya Waila, Wagwemba, Watonga na Walunda wa Magharibi katika mwongo wa kwanza wa karne hii yaliwahusu maafisa wa Kiingereza wa Rhodesia ya Kaskazini; ambapo huko Kongo inakadiriwa kuwa palikuwepo maasi ya wenyeji zaidi ya kumi kila mwaka.

Pale Waafrika waliposhindwa kuonyesha bayana chuki yao kwa ukoloni au chuki dhidi ya ubaguzi waliofanyiwa katika makanisa yaliyotawaliwa na Wazungu, aghalabu waliamua kuanzisha makanisa yao huru au ya pekee ili kurekebisha malalamiko yao. Na kuongezeka kwa haya makanisa huru kulitokea sana huko Nyasaland na Rhodesia ya Kaskazini katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini. Inaelekea kanisa maarufu sana la aina hiyo lilikuwa lile Kanisa la Ethiopia lililoanzishwa na Eillie Mokalapa. Mokalapa na wafuasi wake daima walipinga ubaguzi waliofanyiwa na wamisionari Wazungu na ile hali ya Waafrika wenye ujuzi kuwekewa vikwazo vingi vya kupandishwa madaraja kazini mwao. Lengo lao la muda mrefu lilikuwa ni kuwadhihirishia Wazungu kuwa Waafrika nao walikuwa na uwezo wa kutosha kabisa kujiendeshea shughuli zao za kidini au za kimaisha bila ya kuwategemea sana Wazungu. Yapo makanisa mengine kama *Watchtower* la Rhodesia ya kaskazini au AME la huko Msumbiji ambayo nayo yalikuwa na mipango kama hiyo hiyo.

Licha ya kuwepo kwa ukinzani huu huko vijijini, nia ya kuleta mabadiliko katika kanisa ilianza kuenea mijini pia ambako wasomi Waafrika na Machotara walianza kugundua haraka haraka kuwa misingi ya usawa waliyohubiriwa na Wamisionari haikukwepa kuingiza ubaguzi wa kijamii, kiuchumi, na kisiasa. Machotara wasomi wa Angola, kama Jose Fontes Pereira, walikuwa miongoni wa watu wa awali kabisa kuonyesha kutokuridhika na kuchukizwa kwao. Baada ya kuiga utamaduni wote wa Kireno, walichukia sana walipoona kuwa bado walibaguliwa na Wareno waliohamia nchini humo mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Katika kuyalinda maslahi na hadhi yao, walichapisha tahariri na ishara nyingi wakilaani hali ya kushuka kwa hadhi yao, na wakati huo huo wakiuomba utawala wa Lisbon kuwahakikishia kuwa hadhi yao itaendelea kuheshimiwa na kuomba kunyonywa kwa Waafrika kukomeshwe. Madai haya hayakusikilizwa na ndipo walipoamua kuunda chama cha kwanza cha Machotara ili kiwasaidie kudai haki hizo mwaka 1906. Miaka minne baadaye Machotara wote wasomi kaktika makoloni ya Ureno yaliungana. Katika kipindi hicho hicho, huko Msumbiji nako kulianzishwa vikundi vya wasomi wapenda mbabadiliko. Kikundi kilichokuwa maarufu zaidi ni kile cha *Associacao African* (Chama cha Waafrika) ambacho kilichapisha gazeti la *Brado Africano*, lililokuwa gazeti la kwanza kabisa la ukinzani nchini Msumbiji.

Pia, katika kipindi hicho hicho huko Nyasaland na Rhodesia ya Kaskazini wafanyakazi walimu na watarazaki wengine Waafrika walikuwa wakiunda vyama ambavyo vingehakikisha kuwa hadhi yao ya juu inaendelea kulindwa na walidai pafanywe mabadiliko katika mfumo mzima wa ukoloni uliokuwepo wakati huo. Kati ya mwaka 1912 na 1918 kuliundwa vyama kadhaa vya aina hiyo ikiwa ni pamoja na *North Nyasa Native Association* (Chama cha Wenyeji wa Nyasa ya Kaskazini) na *West Nyasa Association* (Chama cha Nyasa Magharibi). Vyama hivi vilikuja kuwa maarufu sana katika siasa za Afrika ya Kati katika kipindi chote cha kati ya vita.

## *Maasi dhidi ya Ukoloni hadi mwaka 1918*

Maasi yaliyotokea dhidi ya ukoloni yalitofautiana na ule ukinzani wa wenyeji katika ukubwa na malengo yake. Ukinzani wa wenyeji ulichukua muda mfupi na haukupangwa vizuri lakini maasi haya yalipangwa vizuri na yaliwahusisha karibu wananchi wote wa Mbari kadhaa. Kushiriki kwa wingi kwa wukulima wadogo katika baadhi ya mapambano haya kunaashiria kuwa suala la matabaka ya watu nalo lilianza kupewa umuhimu mkubwa. Jambo jingine lililoambatana na msingi huu mpana ni kule kueleza upya na kuyapanua malengo ya maasi hayo. Hapo watu wakaanza kupuuza yale maasi yaliyolengwa kwenye kutatua tatizo moja tu maalumu na wakapendelea zaidi mkakati ambao ulilenga katika kuutokomeza kabisa mfumo mzima wa ukoloni ambao ndio ulikuwa chimbuko la madhala hayo.

Kuanzia mwaka 1885, wakati ambapo baadhi ya sehemu katika Afrika ya kati zilitamalakiwa kwa mara ya kwanza, hadi mwaka 1918, palitokea zaidi ya maasi ishirini. Maasi haya yalitokea katika makoloni yote yaani Angola, Msumbiji, Nyasaland, Rhodesia ya Kaskazini, na hata Kongo, ingawa maasi mengi zaidi yalitokea katika makoloni ya Wareno na kule Kongo ambapo utawala wa kikoloni ulikuwa mkali mno. Lakini wakoloni hao hawakuwa na utawala wala mfumo wa jeshi thabiti na hivyo walitoa mwanya wa maasi hayo kutokea mara kwa mara.

Hata kama maasi haya yalitofautiana kwa kiasi fulani, lakini kama ukiyachambua kwa undani, utagundua kuwa yalikabiliwa na matatizo ya kiutawala yaliyofanana, ambayo hatimaye, yalizua sifa zilizofanana na kufanya iwe vigumu sana kwa maasi hayo kushinda. Matatizo ya msingi yaliyohitaji kutatuliwa ni kama vile kumpata kiongozi mwenye hadhi, wito na uwezo kamili wa kuwahamasisha watu na kuelekeza juhudi zao katika lengo lililokusudiwa; uwezo wa kuamua kanuni zilizofaa kutumia kuwaunganisha watu wengi zaidi walioupinga ukoloni na kutafuta njia na mahali pa kujipatia zana za vita nzuri na za kutosha.

Hapo mwanzoni jitihada za kutaka kuendelea kuwa huru zilishindwa hususani kutokana na kuuawa kwa baadhi ya hawa viongozi maarufu na wenye juhudi kama Mwase Kasungu - kiongozi wa Wachewa, na Msiri, kiongozi wa Wayeko, au kuwekwa kwao kizuizini kama ilivyotokea kwa Gungunyane na ukoo

wa kifalme wa Wabarue. Hata hivyo, baadhi ya koo hizi za kifalme zilisalia na kuendelea kuongoza. Mifano ni kama ile ya mtawala wa Mwenemutapa, Chioko, aliyeyaongoza maasi ya mwaka 1897, Mtawala wa Dembo, Gazuangonongo aliyeongoza maasi mwaka 1808 na mfalme Mushidi wa Walunda aliyeyaongoza maasi makubwa kuanzia mwaka 1905 hadi mwaka 1909. Dhima hii, iliyochukuliwa na baadhi ya koo za kifalme inadhihirisha kuwa yale madai ambayo huelekea kudumisha nafasi za tawala za jadi hayana mashiko yoyote.
Licha ya hizi koo za kifalme kuongoza maasi haya, hata watu wa kawaida tu nao walijitokeza kuongoza. Kwa mfano, Maguiguana mfalme Gungunyane na kiongozi wa vita aliongoza maasi ya Shangaani ya mwaka 1897. Sajenti Kondolo naye baada ya kuchukizwa na mambo mbalimbali yaliyotokea katika jeshi, (Force Publique) aliyaongoza maasi ya jeshi ya mwaka 1897.

Viongozi mashuhuri wa dini pamoja na wawakilishi wa mizimu nao pia walisaidia kuwaongoza watu. Uongozi huu ulikuwa mwendelezo wa kimantiki wa fikra ya kuwa dhima yao ya kihistoria ni kuwa walezi wa kiroho wa nchi nzima. Katika mwaka 1909 mhubiri wa Watonga Maluma aliamuru mabwanyenye wote wa kikoloni nchini Nyasaland wafukuzwe na amri hii ilisababisha kuzuka kwa vita baina ya Watonga na Wazungu, Aidha, mhubiri maarufu wa Wambona naye alisaidia sana kuwaongoza wananchi katika maasi ya Massingire ya mwaka 1884, na wakati huo huo mhubiri wa kike Nkoine alisaidia sana kuchochea maasi ya Ikaya huko Kongo yaliyodumu kwa miaka mitano hadi mwaka 1921. Hakuna mahali pengine ambapo uongozi wa kidini ulipewa umuhimu mkubwa kupita bonde la Zambezi, Huko wawakilishi wa mizimu ya Washona ndio walioyachochea maasi yaliyotokea mnamo 1897, 1901, na 1904.

Waumini wa kikristo wa Kiafrika waliokengeushwa nao waliongoza baadhi ya shughuli za kuupinga ukoloni. Miongoni mwa hawa viongozi waumini wa kikristo ni pamoja na Kamwana na John Chilembwe wote wawili kutoka Nyasaland. Kamwana akiwa muumini wa *Watchtower* (Mnara wa Uchungulizi) alitabiri kuwa kungetokea tawala mpya za Kiafrika mwaka 1914 zilizotumwa na Mungu, na akawaomba wafuasi wake wakwepe kufanya ukinzani wa kumwaga damu dhidi ya Waingereza mpaka wakati huo ufike. Chilembwe kwa upande wake akiwa anatarajia kuwa kungetokea Dola za Kiafrika zenye baraka za Mungu aliwaongoza waamini wake kufanya maasi ya mwaka 1915 ambayo pamoja na kushindwa kwake, yalikuwa muhimu sana kwa heshima ya wananchi.

Viongozi wengine wote kama Chilembwe, walitambua umuhimu wa kuungana na makabila mengine ili kuwa na umoja wenye nguvu zaidi. Kwani, kushindwa kwa vita mbalimbali za kupinga ukoloni kulidhihirisha kuwa dola moja peke yake haikuwa na uwezo wa kutosha kuzuia uvamizi wa Wazungu. Juhudi za kuunda vikundi vipana zaidi vya kimapinduzi zilikuwa na ruwaza kuu tatu. Kwanza ilikuwa ni juhudi za kuhuisha tena mahusiano ya kihistoria miongoni mwa wale waliohusiana kiutamaduni ili kuziingiza tawala nzima nzima katika maasi

hayo. Kwa mtindo huo, temi za Ovambo ziliungana na vikundi vya Guamato katika maasi ya 1907. Waasi hawa walifikiria pia kuvishirikisha vikundi vingine vyenye nguvu, ambavyo kutokana na kule kuwa mbali au pia kutokana na tofatuti zao za zamani, hapo awali havikufikiriwa kuwa navyo vingeweza kushirikishwa. Wabailundu waliweza kusaidiwa na makabila ambayo waliwahi kuyatawala siku za nyuma kama Wakasongi, Wachivanda, na Wangalanga, ambapo huko Msumbiji, Wasena ambao katika vita vya Wabarue vya mwaka 1901 waliwasaidia Wareno, miaka kumi na sita baadaye waliwaunga mkono Wabarue wakiwa sehemu ya chama cha Waafrika wa Zambezi, katika juhudi za kupigana ili kuung'oa utawala dhalimu wa kikoloni. Hatimaye viongozi wa maasi haya, walielekeza madai ya kiuchumi hususani kwa wakulima na wafanyakazi wa vijijini waliokengeushwa na ambao wao binafsi waliyapinga vikali madai yaliyotolewa mara kwa mara na maafisa wa kikoloni na marafiki zao wa kibepari.

Hapo, waasi waliwasihi wote wale waliodhulumiwa kiuchumi kujiunga katika maasi ili waweze kukomesha kule kulazimishwa kulipa kodi au kulazimishwa kufanya kazi bila malipo pamoja na kuutokomeza kabisa mfumo mzima ulioyazua madhala haya. Hapo awali Chama cha Wakamwana huko Nyasaland kilitegemea misaada kutoka kwa Watonga walioishi kando kando ya Ziwa lakini haraka sana baadaye kiliungwa mkono na wakulima wa Kinguni wa Kisenga na wa Kitumbuka waliokuwa wanaonewa. Maombi ya Chilembwe kwa watu wa vijijini nayo hayakuwa na hisia nyingi za Kimbari na badala yake yalielezea zaidi nia ya kuukomesha unyonyaji na kujenga Taifa la Kiafrika lililoagizwa na Mungu.

Suala la kutafuta silaha halihitaji kujadiliwa kwa kirefu hapa. Inatosha tukisema kuwa waasi walijitafutia silaha kwa kutumia njia za kila namna kama vile kufanya biashara za siri na Wazungu, Waasia, au wafanyabiashara Waafrika; kuvamia na kuiba katika bohari za Wazungu, kuzipata kutoka kwa polisi walioasi wa Kiafrika kwa kushirikiana na majirani ambao bado walikuwa huru na wakati mwingine hata kujenga mitambo yao wenyewe ya kutengenezea silaha na baruti. Wakati baadhi ya Waasi kama Wabarue na Wakuamato walifanikiwa kujipatia kiasi kikubwa cha zana za kivita, kwa bahati mbaya hawakuwa na shabaha kama waliyokuwa nayo wapinzani wa awali.

Kutokana na hizi pande mbili kuwa na tofauti kubwa sana ya uwezo wa kivita na kutokana na kuongezeka sana kwa polisi na maaskari wa Kiafrika waliowasaidia Wazungu, haishangazi hata kidogo kuona kwamba, hatimaye Maasi haya yote yalizimwa. Hata hivyo, baadhi ya maasi hayo yalijipatia ushindi mkubwa, hata kama ushindi huo ulidumu kwa muda mfupi tu, kitu ambacho kinasaidia kuipinga imani ambayo ilikuwepo kwa miaka mingi kuwa Waafrika daima ni watii. Wabailungu kwa mfano, waliwafukuzilia mbali Wareno kutoka milima ya Ovimbundu katika mwaka wa 1904. Na, miaka mitatu baadaye Wareno walishindwa tena na WaCuamanto huko Angola ya Kusini. Huenda mafanikio ya

kijeshi ambayo yalikuwa makubwa kuliko mengine yote ni yale ya Wabarue na washiriki wenzao, ambao katika maasi yaliyofanywa mwaka wa 1917 walifanikiwa kulikomboa bonde lote la Zambezi ijapokuwa kwa muda mfupi tu.

## *Hitimisho*

Mtalaa huu umechunguza mitindo mbalimbali ya siasa na ukinzani wa Waafrika dhidi ya kuingiliwa na utawala wa Wazungu. Kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha hii tumejaribu kutoa ushahidi juu ya wingi na uwezo wa vikundi mbalimbali katika shughuli hii ya kuupinga ukoloni. Juhudi za Waafrika kutaka kuendelea kuwa huru, zilikwamishwa na kundi (dogo) la Waafrika waroho waliowasaidia Wazungu na ambao bila misaada yao, Wazungu hao hawangeweza kupenyeza utawala wao kwa urahisi kama walivyofanya. Hivyo palikuwepo mapokeo ya kupambana na ukinzani na mapokeo ya kushirikiana. Ingawa muktadha wa kisiasa umebadilika lukini mvutano kati ya hizi nguvu mbili zinazoshindana, umeendelea kuwa kitu muhimu sana wakati wa harakati za kupigania uhuru za miaka ya 1960 na 1970 katika eneo hili la Afrika ya Kati na Afrika ya Kusini.

# 9 Juhudi na Ukinzani wa Waafrika: Afrika ya Kusini

## *Afrika ya Kusini: Wakati Utawala wa Kikoloni Ulipoingia*

Kama ilivyokuwa katika sehemu zingine za bara hili mambo waliyoyafanya Waafrika wa Afrika ya Kusini kuhusiana na majiliano ya Ukoloni Kusini mwa Afrika katika karne ya kumi na tisa, yaliathiriwa na kani kuu za kihistoria zilizokuwepo wakati huo. Kuhusu sehemu hii, kani hizo zilikuwa ukoloni wa kisetla wa kujipanua, ukristo, elimu ya kimisheni, na hatimaye mapinduzi ya Wazulu na matokeo yake B uhamiaji wa Wamfecane na Wanguni.

Masetla wa Afrika ya Kusini, tofauti na wenzao katika sehemu zingine za Afrikas, tangu mwanzo walipendelea kujitengenezea makazi ya kudumu katika haya mazingira mapya, yaliyokuwa na hali nzuri ya hewa, ardhi ya kilimo yenye rutuba, wafanyakazi wa Kiafrika waliolipwa mishahara kidogo na madini mengi. Hivyo, wakati wa mkutano wa Berlin kuhusu Afrika (1884-5) Waingereza na Makaburu walikuwa wamegombania sehemu za Afrika ya Kusini kwa zaidi ya miaka sabini, na Makoloni manne ya kisetla yalikwisha kuanzishwa. Makoloni haya yalikuwa ni pamoja na makoloni ya Cape Colony na Natal ambayo wakazi wake wengi walikuwa watu weupe waliozungumza Kiingereza wapatao 185,000 kwa koloni la Cape Colony na 20,000 kwa Natal. Mengine ni South Afrikan Republic (Jamhuri ya Afrika ya Kusini) na Orange Free State kila koloni likiwa na wazungu weupe waliozidi 50,000 waliozungumza Kiafrikana. Katika makoloni haya, Waafrika ambao ndio waliokuwa wengi na waliokuwa wenyeji wa asili walitawaliwa na Wazungu wachache.

Katika mapatano ya *Sand River Convention* ya 1852 Waingereza na Waafrikana walikubaliana wasiwauzie bunduki Waafrika popote walipokuwa Afrika Kusini. Hivyo wakati ambapo mataifa ya Ulaya yaliipitisha sheria ya Jumla ya Brussels (Brussels General Act) ya mwaka 1890 iliyowakataza Wazungu kuwauzia bunduki Waafrika, Wazungu wa Afrika ya Kusini walikuwa wamekwishaanza kutekeleza kwa muda sera ya utaratibu wa kuwanyang'anya Waafrika bunduki walizokuwa nazo. Aidha, Waafrikana, Wakoloni wa Kiingereza, na serikali ya Kiingereza walikuwa na mtazamo mmoja wa kiubaguzi licha ya kuwa na tofauti kadhaa za kisiasa na kiuchumi miongoni mwao. Walielewa kuwa ilikuwa ni kwa faida yao wote, kutamalaki, kuwatawala na kuwanyonya Waafrika. Mambo haya yote yalibana sana juhudi na upinzani wa Waafrika, hali ambayo ilipunguza uhuru wa kuchagua kile walichotaka kukifanya.

## *Mapinduzi ya Wazulu na Matokeo yake*

Zaidi ya hayo kulikuwa na matukio ya kihistoria yaliyotokea kote Afrika ya kusini mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Haya yalikuwa ni pamoja na mapinduzi ya Wazulu na Wamfecane katika Afrika ya Kusini; uhamaji wa Wanguni kutoka katika eneo la Wandebele kwenda Rhodesia ya Kusini (sasa Zimbabwe), Wakololo kuingia Rhodesia ya Kaskazini (sasa Zambia) na Wanguni kuhamia Nyasaland (sasa Malawi) na Tanganyika (sasa Tanzania) shughuli za Wabemba huko Zambia ya kaskazini; muungano wa Wayao na Waswahili; na biashara ya watumwa nchini Malawi. Baadhi ya matukio haya yalienea kwa haraka sana na yalisababisha mabadiliko ya haraka ya kisiasa, kiuchumi-jamii, na kijeshi katika jamii nyingi za Kiafrika katika eneo lote la Afrika ya kusini. Hiki kilikuwa kipindi cha kujenga Taifa, na kujipanua kisiasa na wakati huu watu walishuhudia tawala zenye nguvu sana na uongozi imara zikianzisha miliki zao kwenye maeneo yaliyokuwa dhaifu. Ijapokuwa yalikuwa na faida zake mabadiliko haya makubwa yalileta uharibifu usiopimika kwa watu na maumbile ya nchi. Mabaa ya asili kama vile ukame, magonjwa, na njaa nayo yaliandamana na ghasia hizi na kuongeza kiwango cha uharibifu uliotokana nayo. Huku kuendelea kutokea sawia kwa ugomvi na mabaaa mbalimbali ndiko kulikosababisha kutoweka kwa hali ya amani hata jamii ndogo ndogo zikakata tamaa na kuamua kuishi katika mapango au kwenye makazi duni vileleni mwa milima ili kuepuka kushambuliwa tena na wavamizi. Pakazuka tabaka la watawala, tofauti za kitabaka, na kutozwa kodi bila uwukilishi wala uelekezi wa kisiasa. Matokeo yake yakawa kuibuka kwa watawala wa watawaliwa, wakandamizaji na wakandamizwaji, na matajiri na maskini.

## *Shughuli za Kimisheni*

Ukristo na Elimu ya kimisheni navyo vilikuwa vitu muhimu ambavyo viliathiri mwelekeo na aina ya ukinzani wa Waafrika dhidi ya kutamalaki kwa Wakoloni. Wamisionari walikwisha jenga tabaka la Waafrika waliokuwa wainjilisti, walimu, waandishi wa habari, wafanyabiashara, wanasheria, na makarani ambao wengi wao walikubali kuwa utamaduni wao ulikuwa duni, na kuamini kuwa ukoloni wa masetla ulikuwa hauepukiki na waliintukuza Mzungu na kutamani nguvu, utajiri na teknolojia aliyokuwa nayo. Mifano ya watu kama hawa ni Tiyo Soga (1829-71), Mmisionari wa Kiafrika wa kwanza kufanywa kasisi huko Uingereza na kanisa la Muungano wa Presbiteri, naye akawa mwasisi wa misheni ya Mgwali ambako alihubiria Waafrika na Wazungu. Mwingine ni John Langalibabele Debe, Waziri wa kimethodisti, mfuasi imara wa Booker T. Washington , Rais-mwasisi wa *Zulu Christian Industrial School* (Shule ya Ufundi ya Kikristo ya Zulu), Rais wa *Natal Bantu Business League* (Muungano wa Biashara za Wabantu na Natal na Rais wa kwanza wa *African National Congress* (Chama cha Kitaifa cha Waafrika) ((ANC). Mwingine ni John Tengo Jabavu ((1859-1921) muumini wa kimethodisti, mhariri na mwasisi wa (kamusi ya)

Kiingereza-Xhosa, na kitabu cha *Imwo Zabantsudu*: na Walter Rubusana, Waziri wa kimadhehebu na Mwafrika pekee ambaye aliweza kuchaguliwa kuingia katika Baraza la Cape Provincial Council.

Kiitikadi, hawa Waafrika waliosomea kwenye misheni walipendana na kuwa na msimamo mmoja wa kutobagua watu waliofuatwa na wamisionari na wanachama wa *Aborigines Protection Society* (Chama cha Ulinzi wa Wenyejiasili (APS). Walipendelea zaidi ukatiba mabadiliko ya polepole, na usilimisho wa kiutamaduni kama walivyotetewa na Wazungu waungwana wachache miongoni mwa masetla. Lakini wakati huo huo walikuwa wafuasi wa imani ya Booker T. Washington ya *black economic self-determination* (azma binafsi ya mtu mweusi kuamua mtindo wake wa kiuchumi) na wafuasi wa siasa yake ya kale ya tajamala.

Kama walivyokuwa wamisionari, wao nao waliuona umma wa Waafrika kama watu "wajinga" na "washenzi-bora" na walijipa jukumu la kuirekebisha Afrika ya kale kwa kuingiza maendeleo ya magharibi wakitumia vitu kama ukristo, elimu, ubepari na viwanda vya kisasa. Kwa ujumla kwa kiasi fulani walikubali upanuzi na kutamalaki kwa wakoloni; kwani kama ilivyokuwa kwa wamisionari wao nao walihusisha ukoloni na Ukristo au "ustaasrabu" kwa kiasi fulani, kutokana na kutishwa na "ubora wa ajabu" wa zana za kivita za Wazungu hao. Kwa hali hiyo, wao walilaani na hawakujiunga na ukinzani wa Kiafrika dhidi ya ukoloni na kuufananisha upinzani huo na upagani au hali ya kurudi nyuma.

## *Mitindo ya Juhudi za Waafrika na Ukinzani wao*

Mambo yaliyotajwa hapo juu yaliathiri vikubwa muundo wa hali ya mikakati iliyotumiwa na Waafrika katika kuukubali ubeberu na ukoloni wa Wazungu uliokuwa unajipenyeza kwa haraka. Kwa ujumla, kulikuweko na aina tatu tofauti za mitindo ya juhudi na ukinzani wao: (1) ule mtindo wa mapambano ya kutumia nguvu kama ilivyodhihirishwa na Wazulu, Waghanganana, Wabemba, Wayao na Wanguni; na falme kuu za Mangwende (2) ule wa udhamini au hifadhi uliochaguliwa na Wasoto, Waswazi, Wangwate, Watswana na Walozi, tawala huru zote zilizohitaji kulindwa na Waingereza dhidi ya uvamizi wa Wazulu, Wandebele, Wabemba, Wanguni na Makaburu. (3) ule mtindo wa kuungana ambao ulitumiwa na miliki ndogo ndogo nyingi, mateka wa vita, na wakimbizi kama Wakoikoi, Waxhosa, Wapondo, Wathembu, Wangengu na Wahlubi katika Afrika ya Kusini. Wabisa, Walungu na Wasenga katika Rhodesia Kaskaziuki; na Wacewa, Wanyanja, Wankonde na Watonga, Wanyasaland, kwa mategemeo kwamba wangepata amani usalama na kulindwa.

## *Siasa na mapambano ya Wazulu, Wandebele na Wayao*

Mapambano ya vita, kutamalaki na uharibifu havikuweza kuepukika kwa Wazulu, Wandebele, Wabemba na Wayao kwa sababu wao na wakoloni wa Kizungu walitaka

kutawala sehemu zilezile na watu walewale. Kama kundi, wao walikalia au kuitawala sehemu yenye watu wengi, rutuba nyingi na madini mengi kuliko sehemu zingine zote za huku Afrika ya Kusini. Masilahi yao ndiyo yaliyofanya iwe vigumu kukubaliana au kushirikiana na Wazungu. Hivyo, wale wenye nguvu zaidi tu ndio walioishi.

### *Wazulu*

Wazulu ndio lililokuwa taifa la Kiafrika lenye nguvu zaidi kusini mwa Limpopo; Wandebele katikati ya Limpopo na sehemu za Zambezi, Wabemba katika Rhodesia ya kaskazini, na Wayao na Nyasaland ya Kusini na ya Kaskazini. Hadi kufikia mwanzoni mwa miaka ya 1870, Wazulu walikuwa wamefanikiwa kudumisha utawala, uhuru na usalama wao. Aidha, walifanikiwa kuzuia kujipenyeza kwa wamisionari, wafanyabiashara wa Kizungu, waweka mikataba, na watafuta manamba, ambao wakati huo walifikia hitimisho ya kwamba dawa ya pekee ya Avichwa maji@ hawa ingekuwa kutamalaki nchi zao na kuzivunjilia mbali tawala zao. Makaburu na Wareno kwa tabia walikuwa wakaidi sana nao walifuata sera ya kushambulia na kutamalaki.

Hivyo, Wazulu chini ya uongozi wa Catshwayo, na Wandebele chini ya uongozi wa Lobengula nao waliamua kutumia mkakati wa mapambano; kwanza walitumia mbinu ya diplomasia na baadaye mapigano ya silaha. Kwa mujibu was mkakati huu Ceteshwayo kwanza aliendelea na sera za nje za kujitenga na kutokupigana; kama alivyofanya mtangulizi wake Mpande. Maadui wake wa zamani wakiwa ni makaburu wa Transvaal, Cetwayo alidumisha ushirikiano mzuri na wakoloni wa Kiingereza wa Natal halafu akaanzisha urafiki na Theophilus Shepatone, Waziri maarufu wa masuala ya Waafrika huko Natal. Lakini, baada ya Waingereza kuitwaa Transvaal mwaka wa 1877 na kumteua Shepatone kuutawala, mfumo Cetwayo wa ushirikiano ulianguka mara moja. Hapo Shepstone aliwaunga mkono makaburu, ambao walikwisha kuuvuka mto Buffalo hadi nchi ya Wazulu wakajikatia sehemu za mashamba na kuanza kudai kuwa ni sehemu zao.

Cetshwayo alishitaki kwa muadhama Henry Bulwer, gavana mwanajeshi wa Natal, ili asuluhishe mgogoro wa mpaka baina ya Wazulu na makaburu. Muadhama Henry aliteua tume ya mipaka ambayo iliuchunguza mgogoro, na kuamua kwamba madai ya makaburu hayakuwa halali na tume iliwaamuru makaburu warudi upande mwingine wa mto Transvaal. Hata hivyo, akiwa ameazimia kulivunjilia mbali taifa la Wazulu ili aweze kujenga shirikisho la makoloni ya masetla, kamishna mkuu mpya wa Kiingereza Bartle Frere, alificha ripoti na mapendekezo ya tume hiyo. Alitumia kisingizio cha baadhi ya Wazulu waliovuka mto Buffalo kuwarudisha wake wa mtemi Sirayo kumwamuru Cetshwayo kuwakamata Wazulu hao ili washitakiwe. Aliifuatilia amri hii na kutoa mkatabat arehe 11 Desemba, 1878. Baadhi ya madai yake yalikuwa kwamba watu hao waletwe pamoja na ng=ombe 500, halafu kulinyang=anya silaha jeshi lote la Wazulu katika muda wa siku 30, kuwaruhusu wamisionari kuingia nchini mwao na kuruhusu kuwekwa mkazi mmoja wa Kiingereza nchini humo. Frere alielewa

kabisa ya kwamba hakuna mtawala yoyote huru na anayejiheshimu ambaye angeyakubali madai haya magumu.

Mnamo Januari 11, 1879 chini ya amri ya Lord Chelmsford, Jeshi la Kiingereza likiwa na zaidi ya maaskari 7,000 (Wazungu waliojitolea 1,000 na Waafrika wasaidizi 7,000) waliishambulia nchi ya Wazulu kutoka pande tatu. Tarehe 22 Januari 1879 jeshi la Wazulu lilijibu kwa kufanya mashambulio ambayo hayatasahaulika. Katika mapigano ya *Islandhlawala,* Wazulu waliwaua wavamizi 1,600 na kuwarudisha nyuma wengine waliobakia. Lakini tarehe 4 Julai majeshi ya Kiingereza yalirudi tena yakashambulia na kuliteka taifa la Wazulu. Ceteshwayo akahamishiwa Cape Town na himaya ya Wazulu ikagawanywa katika temi kumi na tatu, ambazo zilitawaliwa na watemi vibaraka. Miongoni mwa watemi hawa alikuwapo mpinzani mkuu wa Cetshwayo Zibbebbu, Hamu Catshwayo, binamu yake, ambaye aliamua kupigana upande wa Waingereza wakati wa vita, na mzungu aliyeitwa John Dunn. Hata hivyo, kiwango cha nadui kati ya watemi hawa kilikuwa kikubwa sana na tishio la machafuko ya kiutawala liliongezeka upesi kiasi kwamba ilibidi Cetshwayo arudishwe kuja kutawala ingawa Zibbebbu aliruhusiwa kuendelea kuitawala sehemu yake. Lakini, haukupita muda pakazuka vita vya wenyewe kwa wenyewe baina ya majeshi ya Cetshwayo na Zibbebbu. Cetshwayo alikufa alipokuwa akikimbia wakati wa kilele cha vita hivyo mwaka 1884. Taifa hilo la Wazulu ambalo sasa likiwa limefifia sana liliwekwa chini ya uongozi wa Dinizulu, mtoto wa kiume wa Cetshwayo aliyekuwa na umri wa miaka 15 tu, na ambaye nguvu zake na mamlaka vilitegemea sana misaada ya Wazungu. Hatimaye Wazulu walilazimika kusalimu amri na kutawaliwa na Waingereza.

Wandebele

Kuanzia mwaka 1870 hadi 1890, Lobengula, kama Cetshwayo wa Uzulu, kwa uangalifu mkubwa alifanikiwa kuufuata mkakati wa kidiplomasia aliotayarisha vizuri katika kulinda maslahi ya taifa la Wandebele. Alikataza uhamaji holela na aliwaeleza Wazungu wageni kuwa yeye hakupendelea kuruhusu watu kuchimba madini au kuwinda wanyama nchini mwake. Pamoja na haya, pia alitumia mbinu zingine kadhaa, kwa mfano, kila mara alihama kutoka mji mmoja hadi mwingine, kuchonganisha taifa au kampuni au mtu mmoja na mwingine na kuahirisha kutoa uamuzi ili kuwakatisha tamaa wale waweka mikataba wasiovumilia au wenye wasiwasi. Kama mkakati wa muda mrefu, Lobengula alipanga kuanzisha ushirikiano wa kijeshi au kujiweka chini ya ulinzi wa serikali ya Kiingereza ili nchi yake isishambuliwe na Wajerumani, Wareno au Waafrikana na hatimaye aweze kudhibiti kupanuka kiholela kwa ukoloni katika sehemu hii ya Afrika ya Kusini.

Aina hizi za ukinzani wa kidiplomasia zinaelekea zilifanikiwa hadi mwaka wa 1888 ambapo mfadhili mmoja wa Afrika ya kusini, Cecil John Rhodes, aliwashawishi Mwadhama Hercules Robinson, kamishna mkuu, na Mwadhama Sidney

Shippard, Naibu kamishna wa Becfwanaland ili aweze kupata msaada wa mchungaji John Smith Moffat. Mchungaji Moffat aliondoka Matebeleland mwaka wa 1865 baada ya kushindwa kabisa kuwabadili Wandebele kuwa Wakristo. Hatimaye Moffat aliamua kuwa kamishna msaidizi wa Shippard. Moffat alitamani Wandebele watawaliwe na wakoloni ili kulipiza kisasi cha kushindwa kwake hapo awali. Pia aliwachukia Mzilikazi, Lobengula na utawala wao mzima wa kisiasa kwa kufaulu kuukataa Ukristo.

Hivyo, Moffat aliamua kumwunga mkono Rhodes na kampuni yake ya *Chartered Company* (Kampuni ya Kukodi). Kwa mara ya kwanza akajifanya kuwa ni mshauri wa kiroho ambaye hakuhitaji madini wala wanyama wala kutamalaki. Moffat alimshauri Lobengula Aashirikiane@ na Waingereza badala ya kushirikiana na Makaburu, Wareno, au Wajerumani na akamshawishi atie saini mkataba, ambao tangu wakati huo umejulikana kama AMkataba wa Moffat@ tarehe 11 Februari 1888. Kwa mujibu wa masharti ya mkataba huo, Lobegnula aliahidi kuacha kuandikiana au kuwekeana mikataba na taifa lolote jingine la kigeni au kuuza, kutoa au kuachia nchi yote au sehemu yake bila ya taarifa au ruhusa ya kamishna mkuu wa Malkia katika Afrika ya Kusini. Baada ya mkataba huu kuanza kutumika, kipindi cha Uingereza kuikalia Rhodesia kilianza. Moffat alikwishaziweka nchi za Matebeleland na Mashonaland chini ya utawala wa Waingereza. Mapema baadaye, makundi ya waweka mikataba wa Kiingereza na makampuni kadhaa yalimwendea Lobengula yakitafuta hati za kumiliki madini na ardhi huko Matebeleland na Mashonaland.

Baada ya kugundua hali hii, Rhodes aliwatuma Rudd, Thompson na Maguire wakamwombe Lobengula mkataba wa kuhodhi ardhi, ambao ungetumiwa kuombea mkataba wa kifalme ambao ungekataza kabisa waweka mikataba na makampuni mengine ya Kiingereza kuingia humo. Makubaliano haya ambayo yalikuja kujulikana kama Mkataba wa Rudd yaliweza kupatikana hasa kutokana na maafisa wa Kiingereza wakishirikiana na wamisionari, hususani Moffat, kumhadaa Lobengula.


Mkataba wa Rudd ulikuwa na sehemu tofauti mbili zilizohusiana sana. Sehemu ile iliyoandikwa na ambayo ilikuwa muhimu na ya manufaa kwa wazungu wenye mkataba; na sehemu ya makubaliano ya mdomo ambayo ilikuwa ya manufaa zaidi kwa Lobangula. Kwa mujibu wa sehemu ya mkataba iliyoandikwa B yaaui kielezo cha mapendekezo yaliyowasilishwa kwa Lobengula mfalme aliwapa Wazungu chuma na madini yote yaliyokuwapo katika miliki yake yote na aliwapa ruhusa ya kufanya chochote walichokiona kuwa ni cha lazima ili kuyapata madini hayo. Aidha, Lobengula aliahidi kwamba hangewapa watu wengine wowote ardhi au haki za kuchimba madini bila kuomba ruhusa kutoka kwa wapewa mkataba (Wazungu). Kama malipo yao, wapewa mkataba walikubali kumlipa Lobengula pamoja na warithi wake kiasi chya paundi 100 za Kiingereza kila mwezi, bila kikomo. Walikubali pia kumpa bunduki za mifuo 1,000 na risasi 100,000. Wazungu hawa walikubali pia kutoa mashua ya kivita yenye bunduki ambayo ingetumiwa kwa ulinzi katika mto wa Wambezi.

Hata hivyo, mapatano yalipokuwa yakiendelea, mfalme aliyaongeza masharti fulani, ambayo yaelekea yeye aliyaona kuwa ni ya msingi zaidi na hivyo kuwa sehemu muhimu ya mapatano. Kwa mujibu wa Heln, Lobengula alisema hayo na Wazungu wakakubali kwamba: (1) Wapewa mkataba (wazungu) wangewaleta wazungu wasiozidi kumi kila wakati ili washughulikie kuchimba madini katika eneo hilo.(2) Wachimbaji hao hawangechimba karibu na miji. (3) Wazungu wangetii sheria za nchi yake na kwa hakika wangekuwa kama raia wake na (4) Kwamba hao wangepigana kuilinda nchi hiyo chini ya amri ya Wandebele kama msaada huo ungehitajika. Kwa bahati mbaya masharti yote haya ya mdomo hayakuandikwa kwenye mkataba halisi, na hivyo, kwa mujibu wa sheria za mikataba za wazungu masharti haya hayangeweza kufuatwa wala kuchukuliwa kama sehemu ya ule mkataba.

Watafuta mikataba wengine waliokasirika, na pia Waafrika wasomi kama John Kumalo na John Makunga, kwa huruma walimtafsiria Lobengula na *mainduma* wake (wazee wa Baraza) ule mkataba ulivyosema, na hapo ndipo Lobengula na wazee wake walipogundna kuwa walikuwa wamedanganywa. Walielezwa pia kwamba tayari mkataba huo ulikwishachapishwa katika magazeti ya Wazungu na kwamba Rhodes alikwisha kuiunda kampuni ambayo ingezikalia miliki za Wandebele na Washona. Kihoro, hofu, na kuchanganyikiwa kulilikumba taifa lote la Wandebele baada ya watu wao kuelewa maana hasa na matokeo ya baadaye ya mkataba huo. Baadhi ya wazee na wanajeshi walikasirika sana na Lobengula naye alifadhaika sana na kupata wasiwasi kwamba angepoteza mamlaka yake.

Lobengula alichapisha tangazo la kuukataa ule mkataba katika gazeti la Bechuanaland News (Habari za Bechuana) la Februari 1889. Akaamuru kikosi cha Mbezu kimuue *Induma* Lotshe, aliyewaunga mkono Waingereza, pamoja na wake, watoto na mifugo yake yote. Aidha, Lobengula alimwandikia Malkia Victoria barua na kumtumia ujumbe wa watu kumwomba aukatae mkataba ule au kutangaza kuwa miliki za Matebeleland na Mashonaland zimekuwa chini ya ulinzi wa Uingereza, Mwezi Januari 1889 alituma ujumbe uliokuwa *Mainduna* Motshede na Babiyanea ambao walizungumza na Malkia Victoria na baadhi ya watu mashuhuri wa Aborigines Protection Association (Chama cha Ulinzi wa Wenyejiasilia). *Mainduna* wakarudi na salamu za malkia tu, lakini Malkia hakuukataa huo mkataba. Rhodes akaipata kampuni moja ya kifalme kuitawala sehemu hiyo. Mwanzoni mwa 1890 wapelelezi wake walitembea kutoka Afrika ya Kusini, wakapitia Matebeleland hadi Mashonaland na wakaipandisha bendera ya AUnion Jack@ huko Salisbury tarehe 12 Septemba 1890.

Lobengula, kama alivyofanya Cetshwayo, alijaribu kuepusha umwagaji damu kwa kuelezea uchokozi waliofanyiwa kwa Jameson, Rhodes na Serikali ya Uingereza. Lakini wakati huo hakuwatena tena na marafiki wa Kiafrika wala Wazungu. Idadi kamili ya wavamizi walioishambulia miliki ya Matebeleland ilikuwa na maaskari 1,200 kutoka Mashonaland na Afrika ya Kusini pamoja na kikosi cha Kiingereza cha askari 200 wa polisi wa mpaka wa Bechuanaland. Halafu walikuwepo Waafrika




**9.1** *Watu na tawala za Kusini mwa Afrika, zikionyesha uhamaji wa Wanguni na eneo la Wachimurenga.*

wasaidizi wapatao 1,000 ambao walikuwa Washona Wamfengu, Wakoikoi, Machotara na kati yao 600 walikuwa Wangwato wapanda farasi, walioongozwa na Kagama.

Kuliko kuwatumbukiza askari wake wapatao 20,000 katika mapambano ya hatari dhidi ya masetla waliokuwa na silaha bora zaidi wakisaidiwa na Waafrika, Lobengula pamoja na watu wake walihama nchi yao na kukimbilia kaskazini kuelekea Rhodesia ya Kaskazini. Lobengula, naye kama Cetshwayo, alikufa wakati wa kutoroka kutokana ama na ugonjwa wa ndui au ugonjwa wa moyo. Basi, kwa kukosa uongozi, taifa la Wandebele likaanza kuvunjika. Maunduna wa Kindebele mmoja mmoja walikwenda kujisalimisha kwa Jameson chini ya mti wa Indaba (mkutano). Nao Masetla mara moja wakaanza kuchukua mashamba na madini waliyodai kuwa yao. Hadi mwishoni mwa mwaku wa 1895, kampuni hiyo ilikwisha kuanzisha utawala wa Kiafrika uliofanana na ule wa makoloni ya Cape Colony na Natal; pamoja na kuanzisha kodi ya nyumba, masharti, na ruhusa kwa lengo la kuwanyang=anya Waafrika ardhi, mifugo, na madini yao na vilevile kuwalazimisha kuwatumikia Wazungu.

## *Juhudi na Ukinzani wa Wangwato, Walozi, Wasotho, Watswana na Waswazi mtindo wa Udhamini au Uhifadhi:*

Tofauti na Wazulu na Wandebele, makabila ya Wangwato, Walozi, Wasotho, Watswana na Waswazi waliuchagua mkakati wa kuwa nchi-lindwa au kuwa chini ya wakoloni kupitia wamisionari wa kibeberu-utu waliotumia mfumo wa ASerikali B kutoka B Shule ya London@ kama wakala wao wakuu. Kuchaguliwa kwa watawala wa watu hawa hakushangazi. Sifa moja iliyojitokeza kwa watawala wote walioupendelea utawala wa wamisionari kama Kagama wa Watswana, Mosheshe wa Wasotho, Lewanika wa Wabarotse na Ngwane wa Waswazi ni ule udhaifu wao wa kisiasa na kijeshi kwa jumla. Falme zao zilikuwa hususani kutokana na mapinduzi ya kijeshi. Mwaka 1875, kwa mfano, Khama alimfukuza baba yake Sekgoma, na kaka yake Kgamane naye akajitangaza kuwa mfalme. Kaka yake Kgamane alikimbia, pamoja na wafuasi wake, hadi upande wa Transvaal wa mto Limpopo alikoanzisha utemi wake. Wale wangwato watiifu na wasiopenda mabadiliko hata hivyo, waliendelea kumtambua Sekgoma aliyepinduliwa. Baadaye mwaka wa 1885 Lewanika naye aliangushwa na kulazimika kukimbilia kwenye makao makuu ya Kagama. Alirudi tena mwaka wa 1885 na kumpindua Talila Akafuna, aliyekuwa amemwangusha. Hivyo hawa wafalme waliopendelea uhifadhi wa wamisonari wakati wote walikuwa kwenye hatari ya kushambuliwa na hapo kuzaka vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilileta wasiwasi mwingi nchini mwao.

Juu ya hayo, temi zao ziliponea chupu chupu mapinduzi ya Wazulu na Wanguni. Hata hivyo, Wasotho na Waswazi daima waliendelea kushambuliwa na Wazulu, ambapo kwa upande mwingine, Wangwato, Watswana, Wakwene na Walozi walishambuliwa mara kwa mara na Wandebele. Tena walisumbuliwa pia na makaburu

"Maharamia" waliokuwa wanatafuta ardhi kwa bidii na hivyo, kuanzisha mashambulio kwa kuwatumia makomando katika vijiji ambavyo waliteka mifugo na manamba; hata wakaweka mikataba ya "urafiki" hapa na pale, na machifu waliokuwa jirani nao, tena wakaendelea kudai haki za kumiliki ardhi na maeneo zaidi. Kutokana na uhalifu huo Wazulu, Wandebele na Makaburu daima wakawa maadui.

Pamoja na kuchukia sana kanuni za ustaarabu wa kimagharibi na ukoloni, bado walihitaji sana misaada ya kigeni kuwahakikishia kuishi kwao. Hivyo, hatimaye walikubali kushirikiana na wamisionari na kuona uhifadhi wa Uingereza (Ulaya) kama zana muhimu katika sera zao. Kwa sababu hiyo watemi hawa waliwaendea wamisionari hasa ili wapewe mawaidha au miongozo ya kiroho kuhusu masuala yaliyowahusu Wazungu, na walijaribu kuyabadili kwa ujanja ili yawasaidie kuendeleza hali ya ndani iliyokuwa inatetereka. Palikuwapo wazungu waliopatana na hawa Wafalme wa Kiafrika kwa mfano Colliad alikuwa rafiki mkubwa wa Lewamika na Mackenzie akawa msiri mkubwa wa Kagama na Casolis akawa Waziri wa mambo ya nje wa Moshoeshoe.

Kutokana na hali halisi ilivyokuwa hawa watemi walilazimika kukubali kwa haraka Ukristo na udhamini huo. Mgana na Lewamika wakawa Wakristo na kama ilivyo kawaida waumini wowote waliookoka aghalabu huthibitisha kuwa waongofu zaidi hata kuwapita wamisionari. Hawakuacha mapokeo, Imani na Miviga ya mababu zao tu, bali pia walitumia nyadhifa zao kuingiza mambo mbalimbali yaliyohusu ustaarabu wa "ukristo" wa magharibi nchini mwao. Waliwapiga marufuku watu kunywa pombe au vinywaji vingine vinavyolevya, wakatunga sheria kali za pombe ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku watu kutengeneza pombe za Kiafrika. Kadiri walivyowakengeua watu wao walipochukua hatua kama hizo, ndivyo walivyolazimika kuwategemea zaidi wamisionari.

Wamisionari hawa wenye "huruma" kwa upande wao walikuwa tayari wakati wote kuwasaidia watawala hawa. Hawakuupinga ukoloni wenyewe bali hawakupenda kujipanua bila kudhibitiwa kwa wakoloni wa afrika ya kusini, hususani makaburu na Rhodes na vile vile walichukia fujo zilizotokea mipakani na unyonyaji ambao uliathiri vibaya ufanisi wa shughuli zao walizozoea kuzifanya. Wakati huo huo, walisisitiza hoja ya Waafrika kuwa na uhifadhi wa mabeberu. Walitamani kusawazisha mwingiliano wa kiutamaduni baina ya wanaotawala na watawaliwa na kumlinda na "kumstaarabisha Mwafrika" katika jitihada za kumfanya awe "mtu wa maana zaidi" katika jamii mpya ya kikoloni. Wakatumia barua au ujumbe wa watu au kwenda wao wenyewe au kumshawishi kamishna mkuu, au Ofisi ya Makoloni, au vikundi vya watu wenye huruma huko Uingereza, ili kupata ulinzi huo.

Kutokana na juhudi hizo pamoja na wamisionari, wafalme hawa, kwa kushawishi kutuma maombi, au kutuma ujumbe wa watu kwa "Malkia Mkuu wa Waingereza" (kama zile za Kagama mwaka 1876, ujumbe uliotumwa Uingereza na Kgama na Sebele ukifuatana na Mchungaji Willoughby mwaka wa 1895, na ule wa Kaimu Malkia wa Swaziland pamoja na Baraza lake kwenda Uingereza mwaka 1894) ndipo Nyasaland, Bechuanaland zilipopata udhamini wa Waingereza kuanzia mwaka wa 1883 hadi 1903. Hivyo, kwa kukataa kuuhifadhi utamaduni wao na kushirikiana na

wamisionari wenye "huruma" - waliowapinga Makaburu, Wazulu, na Wandebele wafalme hawa walifanikiwa kulinda uhuru wao hadi wakati wa mwanzo wa mnyang'anyiro na hatimaye walifanikiwa kupata ulinzi wa Waingereza; hivyo ukoloni wa ndani wa Masetla ukashindwa.

## *Juhudi na Ukinzani wa Wahulubi, Wampondomise, Wabhaka, Wasega, Wanjanja, Washona, Watawala n.k.*

Mtindo wa Ushirikiano:

Kwa ndani, vikundi hivi vyote havikuwa na umoja wa kisiasa na kiulinzi kuweza kuhimili vishindo vya wakoloni vilivyokuwa vinaongezeka kila siku. Aidha, hawakuwa na ushirikiano wa kidiplomasia au kijeshi na majirani wao. Badala yake kila mara walivamiana, wakapigana na kwa ujumla hawakuaminiana. Miundo ya vikundi vyao ilitofautiana kuanzia na ile mikubwa ya uchifu mzima hadi vikundi vidogo vidogo vya wakimbizi, wahamaji, watumwa waliotekwa, na hata ama za wakoloni au za wamisionari. Wengi wao walikuwa mateka wa vita vya Wazulu, Wandebele, Wabemba, Wayao na Wanguni.

Wakati ambapo baadhi ya vikundi hivi vidogo kama temi za Wabarwe, Wamangwende, Wamakoni na Wamutasa walichagua kutumia akinzani wa mapambano ya silaha dhidi ya wakoloni kama Waxhosa walivyofanya, hapo hapo vikundi vingine vingi kama Wahulubi, Wampondomise, Wabaka, Wasega, na Wanjanja walishirikiana na Wazungu katika matumaini ya kudanganywa ya kuwa wangehakikishiwa kulindwa na kuwa salama. Kwa ujumla, hizi jamii ndogo ndogo zilikuwa na tabia ya kubadilibadili uhusiano wa kidiplomasia na kuelekea kwenye upande unaokuwa na nguvu zaidi au kujifanya kuwa hawafungamani na upande wowote, lakini wakati huohuo wakitumia ujanja na hila kunufaika na ule upande wenye nguvu zaidi. Washona, Watonga, Watawara, Wandau na Wavenda aghalabu waliitumia mikakati hii katika karne za kumi na nane na kumi na tisa wakati wa mgogoro baina ya enzi za Changanure na Mwene Mutapa ambapo Wasotho, Wapondo, Wamfengu, Wathembu, na Watonga walizitumia wakati wa umoja wa Mtetwa na Ndwande. Hivyo watu hawa, walio wengi, walishirikiana na Waingereza dhidi ya Wazulu Wandebele, Wabemba, Wangoni, na Wayao. Juu ya hiyo, vikundi vidogo vidogo kadhaa, kwa mflano Wamfengu, Wathembu, Wanjanja, Wachewa na Watawala walikaa chini ya majeshi imara kwa muda fulani. Matokeo yake ikawa kwamba miongoni mwao walikuwepo Wakristo na wakati mwingine Waafrika wasomi, ambao siyo tu kwamba waliakataa utamaduni wa jadi, bali pia waliupiga vita utawala wa jadi, hali ambayo ilimnufaisha mkoloni.

Hivyo, kwa kushirikiana nao, kuwalinda na pengine kuwakomboa, Waingereza waliweza kuwagawa na kuwashinda kwa urahisi kabisa. Hatimaye, walianzisha makazi ya kudumu ya masetla katika sehemu hizi.

## *Juhudi za Ukinzani wa Waafrika, 1895 B 1914*

Hadi mwishoni mwa miaka ya 1890 karibu wananchi wote wa Afrika ya Kusini walikuwa wametawaliwa na wakoloni ama kikamilifu au nusu nusu na popote walipokuwa walikuwa chini ya ukandamizwaji wa aina moja au nyingine, kiuchumi, kisiasa au kidini.

Baada ya muda mfupi tu, kodi ya nyumba, kazi za kulazimishwa, kuuliwa kwa imani na desturi za jadi, na hususani kuwapokonya wananchi ardhi, vyote hivi vilianzishwa. Mwingilio huu wa wageni uliongezeka sambamba na kuongezeka kwa mahitaji ya Wazungu ya kuwapata manamba Waafrika ambao wangefanya kazi mashambani mwao au kwenye migodi kwa ujira mdogo. Pia waliwatoza kodi ya nyumba, kulipia angalau sehemu ya gharama za uendeshaji. Waafrika walilazimika kuhama makwao ili kuwaachia nafasi masetla wazungu na kutumika kama wanajeshi wa "kujitolea" katika Rhodesia (ya kaskazini na kusini), na huko Nyasaland watawala wa kampuni ya kukodiwa walizihamisha nzima nzima "sheria za wenyeji" wa Afrika Kusini. Huko Rhodesia ambapo makazi ya masetla yalikuwa mengi kuliko pengine pote, utawala haukuvumilia kipingamizi chochote katika shughuli zao za kiuchumi hata kama ilibidi kuwaua Washona au kuwapokonya haki zao. Utawala huo mara moja ulichukua ardhi, mifugo, mazao na akiba ya chakula cha Washona na wakawatumikisha Washona kwa nguvu ili kakidhi mahitaji ya masetla ambao walivutwa kuja Mashonaland baada ya kuahidiwa kuwa maisha huko yangekuwa mazuri, rahisi na ya anasa zaidi. Juu ya yote, usawa ulioanzishwa na wakoloni ulikuwa wa kubahatisha na ulikuwa na dosari nyingi. Pamoja na haya pakatokea mabaa mengine ya asili, ikiwa ni pamoja na kuzuka kwa ndui, ugonjwa wa sotoka, ukame na baa la nzige.

Waafrika bila shaka hawakukaa kimya tu wakiyatazama haya matatizo bila kujali. Katika hali hii ya ukoloni, kutokuwa na ardhi, kakandamizwa na kushindiliwa ustaarabu wa magharibi, Waafrika wengi kwa mfano Waxhosa waliamini kwamba matatizo yao yote yalisababishwa na hao wazungu. Chaki dhidi ya utawala wa kigeni ilianza kuzaa mwelekeo wa kuanza kuwapinga wazungu, na kuimarisha umoja miongoni mwa viongozi wa kisiasa, wafuasi, wachungaji na hata miongoni mwa vikundi ambavyo hapo awali vilikuwa havipatani. Mifano ya mielekeo hiyo ambayo ilikuwa na lengo la kuungamisha mfumo wa kikatili na kikoloni *CHIMURENGA* ya Wandebele na Washona ya 1896 - 1877, maasi ya Wahorero ya 1904 na maasi ya Wabambata au Wazulu ya mwaka 1906.

### Chimurenga ya Wandebele, Wamashona

Chimurenga B kama Wamashona walivyouita ukinzani wao wa kutumia mapambano ya silaha, ulianza Machi 1896 katika Matebeleland na Juni 1896 huko Mashonaland. Tukio la kwanza lilikuwa la polisi Mwafrika, aliyeajiriwa na kampuni iliyotawala



9.2 *Lobengula (c. 1836 – 1894), Mfalme wa Wandebele, 1870 – 1894*

humo, kuuawa Machi 20. Wazungu walishambuliwa kwa mara ya kwanza katika mji wa Essexvale Machi 22, ambapo Wazungu saba na Waafrika wawili waliuawa. *Chimurenga* ikaenea haraka katika Matebeleland na Mashonaland (Taz. Kielelezo 9.1). Kwa muda wa juma moja tu Wazungu 130 wakawa wamekwisha kuuawa huko Matebeleland. Waafrika walikuwa na silaha za kisasa kama bunduki za mifuo, bunduki za tembo, masketi, metifodi na bunduki fupi za kasiba pana pamoja na silaha za jadi kama mikuki, mashoka, marungu na pinde na mishale. Kwa haraka kampuni iliwakusanya Wazungu waliokuwepo Matebeleland kuunda Jeshi la *Matebeleland Relief Force* (Jeshi la kujikomboa la Matebeleland) ambalo lilikuwa na vikosi vya Kiingereza, na *Rhodesia Horse Volunteers* (kikosi farasi) cha wa Rhodesia (masetla), pamoja na Waafrika waliojitolea. Wakati wa kilele chake jeshi hilo lilikuwa na Wazungu 2,000, Wangwato 250 waliotumwa na Kgama, *Colonial South African Natives* (wenyeji wa kikoloni) (wa Waafrika ya Kusini) 200, na Waafrika wa Rhodesia wapatao 150 wote wakiwa chini ya amri ya maulana Frederick Cumngton B mzoefu wa vita baina ya Waxhosa na Masetla.

Ama kwa hakika vita vya *CHIMURENGA* viliendeshwa kama vita vya msituni. Askari wapanda farasi walitegemea zaidi kuzingira na kuteketeza. Wazungu hao waliteketeza mazao, na kuteka ng=ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nafaka na kuwaacha Waafrika wafe na njaa na wao wajitajirishe.

Huko Matebeland vita vya *Chimurenga* vilianza Machi na kumalizika Desemba 1896, na kutokana na kampuni kuhofia kuwa *Chimurenga* ingedumu kwa muda mrefu au kwamba hali ya vita ingesababisha kampuni ifilisike pengine kuilazimisha Uingereza kuibadili nchi hiyo kuwa chini ya udhamini badala ya kuwa koloni, hatimaye walikubali kupatana. Kilichofuata kilikuwa mazungumzo ya amani baina ya Rhodesia na *Mainduna* wa Kindebele, mazungumzo ambayo yalianza Agosti 1897 hadi Januari 1898 wakati ambapo Rhodes aliwateua miongoni mwa wateuliwa kumi wa kampuni, machifu sita na wa *Chimurenga* (Mainduna Dhliso, Sowabulana, Mhugulu, Sikombo, Khomo na Nyamanda) akawapa ardhi ya kuishi, akawapa msaada wa ratili 5,000,000 za nafaka, na akawaahidi kurekebisha malalamiko yao kwa kampuni iliyokuwa ikiwatawala.

Baada ya kupata ushindi na amani huko Matebeleland, kampuni ikaelekeza nguvu zake kwenye Chimurenga ya Washona ambayo ilikuwa inaendelea tangu Juni 1896 na ikaendelea kwa kukatizwakatizwa mwaka 1897 hadi 1903. Vikosi vilivyoongoza vita vya Chimurenga vilikuwa kwenye temi za Mashayamombe, Makoni, na Magwende nchini Mashonaland; lakini temi zingine ndogondogo kama za Nyandoro, Seke, Whata, na Chota vilijiendeshea *Chimurenga* zenyewe au kwa kushirikiana na wengine.

Vita vya Chimurenga, kama vile hekaya za Waxhosa za kuua ng=ombe, vimeelezwa na wanahistoria wenye mtazamo wa Kizungu kuwa ni wa kikale na kimelani kutokana na nafasi muhimu waliyopewa watabiri na wahubiri wa jadi waliojulikana kama *Wasvikiro*. Wasvikiro viongozi walikuwa wa Matebeleland Kagubi

wa Mashonaland na Nehanda (Msvikiro mwanamke) wa Mashonaland ya kati na kaskazini, pamoja na watabiri chipukizi wenyeji wa humohumo. Hawa Wasvikiro waliwaeleza Wandebele na Washona kuwa Wazungu ndio walioleta mateso yao yote, yaani kushurutishwa kazi, kulipishwa kodi ya nyumba, kuchapwa viboko, pamoja na mabaa ya asili kama yale ya nzige, sotoka, na ukame. Waliwashawishi Waafrika wengi kuamini ya kwamba Mungu wa Washona *Mwasi* (mlimo kwa Kindebele) baada ya kushitushwa na mateso ya watu wake, alikwisha kutoa amri Wazungu wafukuzwe nje ya nchi na kwamba Waafrika hawakuwa na haja ya kuwa na wasiwasi kwani *Mwasi* alikuwa upande wao, naye angezibadili risasi za Wazungu kuwa maji. Kwa ujumla Waafrika wengi waliamini kwamba Wasvikiro walikuwa wakitangaza amri za *Mwasi* na kwamba kutokuzitii amri hizo kungeleta mateso zaidi kwa temi mbalimbali za humo na kuleta mikosi kwa watu binafsi.

*Wasvikiro* hasa walikuwa watabiri wanamapinduzi waliozieleza sababu halisi za *Chimurenga* na makubaliano ya watu ambayo bila kuwapo basi matangazo yao hayangeaminika na kufuatwa. Aidha, wakiwa ni wahifadhi wa mapokeo ya Washona yana taasisi zilizojulikana popote kuhusu masuala anuwai ya maisha ya Washona, walihofia kuwa walikuwa wanapokonywa hiyo dhima yao na wamisionari Wazungu. Cha muhimu zaidi, ile nafasi ya kuongoza ya *Wasvikiro* ilitokana na mgawanyiko wa kisiasa na kijeshi wa Wandebele, na hususani, wa Washona.

Wasvikiro ndio watu pekee ambao mawazo yao yalivuka mipaka ya ufalme mmoja. Majimbo ya kiroho ya Mukwati, Nehanda, Kagubi yalienea katika falme zaidi ya moja. Tofauti na machifu wakuu, hawa Wasvikiro walikuwa na mfumo mzuri sana wa siri wa kuwasiliana ambao uliwawezesha kubadilishana taarifa mbalimbali na kuratibu shughuli zao kwa ustadi mkubwa.

Kagubi na Nehanda walikuwa na uwezo mkubwa wa kuwashawishi machifu wa sehemu zingine kama Muchemwa huko Magwenda, Mhiripiri wa Makoni, na Panasha wa Nyandoro. Lakini Kagubi alikamatwa Oktoba na Nehanda akakamatwa Desemba 1897. Machi 2, 1898 walishitakiwa kwa makosa ya kuua na wote wakahukumiwa kunyongwa.

Baada ya kukosa uongozi, kukosa bunduki na silaha zingine, kuwakosa *Wasvikiro*, wafalme wa Washona walianza kushindwa mmoja baada ya mwingine kuanzia mwaka wa 1897. Tarehe 4, Septemba Makoni alitiwa pingu, akafungwa kitambaa machoni na kupigwa risasi. Vivyo hivyo hata Mashayamombe, ambaye alikuwa karibu ayazuie kabisa mawasiliano yote kati ya Salisbury na Bulawayo, alishindwa na kuuawa Julai 25. Kati ya mwezi wa Julai na Septemba masetla walifanikiwa kuzingira falme kadhaa katika Mashonaland ya kati. Mangwenda alishindwa Septemba, lakini mtoto wake jasiri pamoja na wazee kadhaa wa Baraza lake waliyaendeleza mapambano hayo hadi 1903 wakati vita vya *CHIMURENGA* vilipokomeshwa kabisa. Watu waliouawa katika *Chimurenga* wanakadiriwa kuwa Wazungu 450 na Waafrika 8,000 ambapo Wazungu 188 walijeruhiwa. Kati ya Wazungu 450 waliouawa, 372 walikuwa masetla wakazi ambao wanawakilisha moja

ya kumi (1/10) ya idadi kamili ya Wazungu wote waliokuwapo katika koloni hilo. Waliosalia walikuwa maaskari wa Kiingereza na maaskari wa kukodiwa.

Waherero

Mwaka wa 1904 Waherero walipozidiwa na adha za utawala wa kikoloni walitumia fursa ya kujitoa nchini mwao kwa majeshi ya kijerumani kwenda kuzima maasi miongoni mwa Wabondelswati, na wakaasi Januari 10 kwa kuwaua Wajerumani 100, kuyaharibu mashamba kadhaa na kuteka ng'ombe. Basi Theodor Leutwein, kamanda wa Kijerumani, aliondolewa na badala yake akawekwa Jenerali Von Trotha ambaye aliazimia kupata ushindi kamili wa kivita na kuwaangamiza kabisa Waherero kwa kutumia mbinu za kikatili na mauaji. Kati ya asilimia 75 na 80 ya idadi ya Waherero wote ambao yakadiriwa kuwa walikuwa 60,000 B 80,000 walichinjwa. Wengine 14,000 waliwekwa katika makambi ya magereza, wengine 2,000 walikimbilia Afrika ya Kusini. Samwel Maherero na wafuasi wake 1,000 walilivuka jangwa la Kalahari hadi Bechuanaland. Baada ya maasi ya Waherero, Hendrik Witbooi mkuu wa Wanama, naye aliasi na uasi huu uliendelea hata baada ya kifo chake hadi mwaka wa 1907.

Waafrika walinyang'anywa ardhi na mifugo yote, wakazuiwa kuunda vikundi vya kimbari au kufanya sherehe mbalimbali za kijadi. Wakakosa njia nyingine yoyote ya kujikimu isipokuwa kuajiriwa na masetla Wazungu. Miungu na wachungaji wao wa jadi waliposhindwa na hapo kuonekana duni, waliamua kubatizwa na kuwa Wakristo. Ndipo mwaka wa 1915 majeshi ya Afrika ya Kusini yakaitwaa Afrika Kusini Magharibi na kuiweka chini ya sheria za kijeshi hadi mwaka wa 1921. Tarehe hiyo, Wazungu wa Afrika ya Kusini wapatao 10,673 waliungana na masetla wa Kijerumani ambao hawakuhamishiwa Ujerumani. Waafrika wakaruhusiwa kulima kilimo cha kujikimu katika sehemu kama zisizo na rutuba na hivyo wakalazimishwa kutegemea zaidi kazi za utumwa kwa maisha yao.

## *Hitimisho*

Hadi mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini, kwa kweli hapakuwepo na ufalme wa wenyeji hata mmoja. Hivyo Waafrika walio wengi walikuwa wameingia katika ukinzani wa kiwango cha tatu ambao ulitawaliwa zaidi na harakati za kujipatia maisha bora ya amani chini ya utawala, uchumi na utamaduni wa kikoloni. Ama kwa hakika huu ulikuwa ukinzani wa aina tofauti na mikakati iliyotumiwa awali kupinga wakoloni kushinda au kutamalaki, na ukinzani huu unafaa uandikwe katika sura tofauti katika historia ya Afrika. Kwani, hadi wakati huu viongozi wote wa jadi wa kidini na kisiasa walikwishashindwa wakatawaliwa na kukandamizwa. Wafalme wa jadi waliondolewa na badala yake pakawekwa makatibu wa masuala ya wenyeji kwa mfano Theophilus Shepstone wa Natal, au wale walioitwa makamishna wa wenyeji au “Idara za Wenyeji”

mahali pengine. Umma wa Waafrika uliitwa "Tatizo la Weusi", na kama Jabavu alivyowaelezea, "hawakuwa na ardhi, hawakuruhusiwa kupiga kura, watumwa, fakiri, waliodharauliwa na jamii, katika ardhi ya mababu zao ambao hawakuwa na matumaini yoyote katika maisha yao ya baadaye". Aidha, hawa walikuwa ndio Waafrika wa kwanza kupambana na tatizo la utambulisho lililoanzishwa na mipaka bandia iliyowekwa na wakoloni, ambayo ilitenga vikundi vya lugha, utamaduni na historia, kwa kuleta utamaduni mpya katika migodi, mashamba, au katika makazi ya Wazungu, katika makanisa na mashule na katika sehemu zote zilizotawaliwa na masetla. Pamoja na kushindwa kwao, Waafrika walirithisha tabia ya kuupinga utawala wa kikoloni, heshima kwa watu wa mbari mbalimbali, na hali ya kutambua na kuheshimu utamaduni, historia, rangi, na utaifa wao kwa vizazi vilivyofuata baadaye kote Afrika ya Kusini.

# 10

## *Malagasi Kuanzia 1880 mpaka 1936*

Malagasi, kile kisiwa kikubwa karibu na mwambao wa Afrika ya Mashariki, haikuweza kukwepa ubeberu wa ukoloni wa Ulaya wa miongo miwili ya mwisho ya karne ya kumi na tisa, Wafaransa walitamalaki na kukitawala kisiwa hicho baada ya vita viwili vya mwaka 1883 mpaka 1885 na mwaka 1894 mpaka 1895. Kama walivyofanya Waafrika wengi, wananchi wa Malagasi walisimama imara na kujikusanya pamoja ili, kwanza kukipinga kile kitendo cha kutamalakiwa na kutawaliwa, halafu kuyapiga vita yale maovu ya utawala wa kikoloni na baadaye kujinyakulia tena uhuru wa nchi yao.

Katika mwezi wa Februari, 1922, Mfalme wa milki ya Merina, Radama I ambaye alitambuliwa kuwa ndiye 'Mfalme wa Malagas' kwa mujibu wa Mkataba kati ya Waingereza na Wamerina wa mwezi wa Oktoba, 1817, alijitangazia ufalme wake juu ya kisiwa kizima cha Malagasi. Hatua hii ilitambuliwa na Wafaransa baadaye katika mwaka 1862, ingawa bado waling'ang'ania madai yao juu ya vituo vyao vya zamani vya biahara na pia juu ya sehemu lindwa za Sakalava na Antakarana. Ili kuhakikisha uhuru wa kisiwa hiki unakuwa thabiti, Rainilaiariveny ambaye alikuwa Waziri Mkuu mwaka 1864, alianza kujaribu kuifanya nchi iwe ya kisasa na pia iwe katika 'Hali ya ustaarabu'. Kwa hivyo aliwapa watumwa uhuru wao mwaka 1877, akauweka mfumo wa sheria katika hali ya kisasa mwaka 1878 na kutangaza katiba mpya mwaka 1881.

Pamoja na juhudi zote hizi za kuleta hali ya kisasa humu Kisiwani lakini Wafaransa, wakisukumwa na Wabunge wa Kifaransa wa Kisiwa cha Reunion ambao walihitajia mahala ambapo pataweza kuwaondolea tatizo la wingi wa watu katika Kisiwa chao, kikundi cha kikatoliki cha mrengo wa kulia na kikundi cha wakoloni kilichoazimia kuziondosha athari za Kiingereza katika shughuli za kidini na za kiuchumi, walikivamia kisiwa hiki mnamo mwezi wa Mei mwaka 1883. Wakazipiga mabomu bandari zilizokua pande za kaskazini-magharibi na mashariki ya kisiwa, na kuiteka Tamatawe. Vita vya kwanza kati ya Wafaransa na Wamerina vikaendelea na huku vikisitasita mpaka vilipokomeshwa kabisa na mkataba baina ya dola hizi mbili katika mwezi Desemba, 1885. Badala ya kuleta amani, mkataba huu ulizidisha mvutano kati ya Wafaransa na Wamalagasi kwa sababu Wafaransa waliyafasiri masharti ya mkataka huu, ambayo hayakuelezwa kwa uwazi, kumaanisha kwamba Malagasi imekuwa nchilindwa ya Ufaransa wakati serikali ya Malagasi chini ya Malkia Ranavolana na Waziri Mkuu Rasinilaiarivony ilikana jambo hili.

Kwa hivyo kukatokea hali ya mvutano baina ya Waziri Mkuu wa majenerali wakazi mbalimbali wa Kifaransa kadri hali ya suitafaharau baina yao ilivyozidi. Bila ya



**10.1** *Ranavalona III, Malkia wa Madagascar (1883 – 1897) amevaa nguo rasmi.*

kusubiri matokeo ya mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea bila ya kumalizika kuhusu swala la kuweka mipaka ya Wafaransa katika eneo la Diengo Suarez, jeshi la wanamaji wa Kifaransa likaiteka sehemu kubwa ya kusini mwa bandari hiyo. Mgogoro wa pili juu ya *exequator* (yaani waraka rasmi unaomtambua na kumpa madaraka afisa wa kibalozi unaotolewa na serikali iliyompokea afisa huyo), uliitawala historia ya mahusiano kati ya Wamalagasi na Wafaransa tangu mwaka 1885 mpaka 1895. Jenerali Mkazi alidai *exequator* ili aweze kuthibitisha kwamba Malagasi ilikuwa nchilindwa lakini Rainilaiarivony alikataa kutoa waraka huo kwa sababu ya kulinda uhuru wa ufalme wa nchi hiyo. Mpaka yalipotiwa sahihi makubaliano kati ya Waingereza na Wafaransa katika mwaka 1890 ambayo kwayo Wafaransa waliitambua Zanzibar kama nchilindwa ya Waingereza na Waingereza wakakubali kutambua Malagasi kama nchilindwa ya Wafaransa, Waziri Mkuu aling'ang'ania msimamo ule ule aliouchukua tangu mwanzo.

Shida hizi za kidiplomasia zilizidishwa na matatizo ya ki-uchumi yaliyokuwa yameukabili ufalme wa Malagasi. Ili iweze kulipa madeni iliyodaiwa na Ufaransa serikali ya Malagasi ilikopa kutoka kwa *Comptoir National d' Escompte de Paris* (CNEP) na dhamana ilikuwa yale mapato ya forodha kutoka bandari sita kubwa za Malagasi, yaani, Tamatave, Majunga, ambao walichaguliwa na benki ya Kifaransa lakini waliolipwa na mamlaka ya kifalme walisimamia ukusanyaji wa ushuru, jambo ambalo liliikosesha Malagasi sehemu kubwa ya mapato.

Matatizo haya ya kifedha, pamoja na kule kusukikilia kwa Le Myre de Vilere, General-Mkazi wa kwanza wa Kifaransa, kulimlazimisha Waziri Mkuu kuwapa Wazungu ruhusa kubwa ya kuchimba shaba nyekundu huko Betsileo, kuchima dhahabu huko Boina na kukata miti. Ruhusa ya kuchimba dhahabu katika mashapo ya Suberibie katika jimbo la Maevatana ambalo lilijulikana sana kwa ule mtindo wake wa kuwafanyisha watu kazi za migodi kwa nguvu iliipatia serikali pato dogo sana. Kwa upande mwingine ilichangia katika kudhoofisha mamlaka ya serikali kwa sababu wafanyakazi wengi walikimbia na kwenda kuwaunga mkono faharalo (wale askari wa mgambo) na kwa hivyo kusababisha hali ya wasiwasi katika sehemu ya Kaskazini-Magharibi ya kisiwa cha Malagasi.

Mapato ya forodha hayakuweza kutosha kwa ajili ya malipo ya kila baada ya miezi sita yaliyotakiwa kupelekwa CNEP kwa vile ruhusa walizopewa wageni hazikuleta matokeo yaliyotarajiwa. Kwa hivyo, ili kuongeza mapato, serikali ya kifalme iliongeza aina za kodi na kutilia mkazo ule mtindo wa kuwafanyisha watu kazi kwa nguvu.

Baadhi ya watu walikataa kufanya kazi walizotarajiwa kuzifanya chini ya *Fanompoana* (mfumo wa kazi za Ushokoa), wakati mwingine walijigeuza majambazi, na vikundi vya waporaji vilijusurisha hata kuuhukumu mji mtakatifu wa Ambohimanga mwaka 1888 na pia mji mkuu wa Malagasi katika mwaka 1890.

Machafuko haya, ambayo yalihatarisha maslahi ya yale matabaka yaliyofaidika katika jamii na pia maslahi ya wafanyakazi wa kigeni, yalimshangaza General B Mkazi na pia yalidhihirisha mgogoro mkubwa wa mamlaka uliokuwepo katika 'ufalme wa Malagas'.

Bunge la Ufarasa liliichukulia fursa kubwa hali hii ya mgogoro na ilimpeleka Malagasi yule La Myre de Vilers, ambaye alikuwa Generali B Mkazi wa kisiwa hiki kuanzia mwaka 1886 mpaka mwaka 1889, pamoja na mpango wa kuifanya Malagasi iwe nchilindwa hasa. Rainilaiairivony alipoukataa mpango huu, Bunge la Ufaransa liliamua kwa kura ya walio wengi sana kuanzisha vita, na kisiwa hiki kikavamiwa mwaka 1894 chini ya uongozi wa General Duchesne. Jeshi la Kifaransa lilishinda nguvu jeshi rasmi la Malkia ambalo lililazimika kukimbia. Jeshi hilo la Kifaransa likauteka mji wa Antananarivo tarehe 30 Septemba, mwaka 1895.

Malagasi kutamalakiwa na kutawaliwa kwa urahisi kama hivi si jambo la kushangaza. Hii ni kwa sababu muda mchache kabla ya kutamalaki huku kwa Ufaransa, Ufalme wa Malagasi ulikwishadhoofishwa na mivutano mikubwa ya ndani kwa ndani. Kwa upande wa kiserikali, kubatizwa kwa Malkia Ranavolana wa Pili kulikuwa ndiyo mwanzo wa kuanguka kwa ile mila ya kuabudu wahenga, mwanzo wa kutoweka kwa madhabahu ya kifalme na mengineyo yaliyokuwa mitaani ambayo ndiyo yaliyokuwa msingi wa siasa na dini katika Imerina ya jadi; kubatizwa huku pia kulikuwa ndiyo mwanzo wa kuchomoza kwa kikundi bora kilichokuwa cha Wakristo.

Shughuli za kisiasa, kiuchumi na kidini zote ziliingiliana. Wafuasi wa *Eglise Du Palais* (Kanisa la Kasri) hawakudhibiti shughuli za nchi tu, kama vile ukaguzi, elimu, kuandikisha watu katika jeshi na kuwaandikisha kwa kazi za lazima, bali pia walichukulia fursa nyadhifa zao na mfumo wa kiuchumi uliokuwepo ili kujitajirisha kwa njia ya biashara na kwa mpango wa kukopesha pesa. Wadhamini wa madhabahu na watukufu wengine wa kienyeji ambao walinyimwa madaraka na marupurupu yao ya jadi waliwapinga viongozi wa nchi ama kwa kukimbia au kwa kukataa kujenga makanisa au kwa kuyachoma moto yaliyokuwepo.

Zaidi ya haya, Wamerina walioufuata Ukristo si wote walioliunga mkono kanisa rasmi la nchini. Wale ambao hawakujiunga na kanisa rasmi, bali walifuata Ukristo wa kienyejienyeji ambao msingi wake ulikuwa Biblia pamoja na historia na ngano za kienyeji walikuwa ni kikundi bora cha wasomi ambacho kingeweza kufanya madai ya uongozi wa kisiasa. Watu hawa walijishughulisha na biashara na walifanya mtindo wa kuhubiri fikra zao siku za soko. Wakriskto wengine walipinga kule kutawaliwa na kanisa rasmi kwa kukimbilia kwenye Ukatoliki au kwa kujiweka chini ya himaya ya mtukufu yeyote. Wengine walipigania uhuru kama wale wapinzani wa Ambatonakanga ambao mwaka 1893 walianzisha kanisa lao wenyewe lililoitwa kwa jina la *Tranozozoro*, yaani nyumba au kanisa la nyasi. Harakati hizi za upinzani zilimea katikati ya mji mkuu, ambao ndio uliokuwa ngome ya Ukristo na ulishuhudia ile hali ya hamkani iliyojidhihirisha miongoni mwa baadhi ya waumini.

Maafisa hawa wanabiashara walijilipizia hasara walizozipata kwa kuutumilia kikamilifu kwa maslahi yao wenyewe ule mfumo wa kazi za kulazimishwa, kwa kutumia ardhi ili kutenga uchumi na kwa kujishughulisha na ukopeshaji wa mapesa. Waliowapinga

mabepari hawa na waumini wa *Palace Church* (Kanisa la Kasri)) walikuwa wakulima wadogo wadogo na vibarua wa kutwa ambao walikuwa wakidaiwa na watu hawa na pia wakiumizwa sana na *fanompoana* (ule mfumo wa kazi za kulazimishwa). Haya yote yaliudhoofisha mfumo wa kijamii na utaratibu wa serikali na yalidhihirisha kuweko kwa mgogoro mkubwa katika 'Ufalme wa Malagasi' ambao kwa sababu hizi ulishindwa kuchuana na kikosi maalumu cha Kifaransa.

Pia kulikuwa na kushindwa kwa uongozi. Rainilaiarivoy, ambaye alikuwa anazeeka na akitawala kwa mabavu, alikuwa hapendwi tena na watu. Wakati ilipombidi kuuviza mfululizo mzima wa njama zilizomkabili, ambazo ziliwahusisha rafiki zake na hata wanawe mwenyewe, Rainilaiarivony hakuweza kuwa na imani kamili juu ya viongozi wakubwa wa serikali ambao waliumezea mate ule wadhifa wake mtukufu na kutumaini kwamba siku moja watachukua wao mahala pake.

Hali kadhalika, jeshi la kifalme halikuwa na uwezo wa kuchuana na wale wavamizi. Jeshi hilo lilikuwa limekwisha paraganyika kwa vile askari wengi waliitupa mkono na pia kwa sababu lilikuwa halina nidhamu kutokana na ile tabia ya ufisadi na tamaa ya pato. Si askari na si maafisa wao, wote hawa walikuwa hawakupata mafunzo sawa sawa ya kijeshi na wakati huohuo kulikuwa na mgogoro na kutoafikiana katika jeshi lenyewe.

Zaidi ya haya, Rainilaiarivony aliweza kuwadhalilisha wanajeshi wa *Kimainty* na kuwatoa wanajeshi wa *Kiandriana* ambao walikuwa ndio uti wa mgongo wa majeshi ya karne ya kumi na nane na kumi na tisa, lakini alishindwa kuunda jeshi lililopata mafunzo sawa sawa na lililoongozwa vilivyo na maafisa waliokuwa na imani naye na wenye ari ya kuuhifadhi uhuru wa nchi yao. Nchi iliyokosa nidhamu na kuwa imegawanyika kiasi hiki haingeweza kusimama; kwa hivyo Malagasi ilishindwa kusimama.

## *Harakati za Menalamba huko Imerina*

Kutekwa kwa Tananarive, ambako kulisababisha kuanguka kwa ulimwengu wa Kikristo mjini kulichochea mkusanyiko wa watu waliokuwa mashambani kwa madhumuni ya kutetea amali za wahenga. Machafuko ya Amboanana, yaliyotokea mwezi wa Novemba, mwaka 1895 katika sikukuu ya *Fandroana*, yaani siku ya kuzaliwa Malkia na ya mapumziko kwa wananchi, yaliyokuwa ndio mwanzo wa harakati za wananchi za kuupinga uvamizi wa Kifaransa. Uasi huu mkubwa ulijulikana kwa jina la *Menalamba* (au 'Vitambaa Vyekundu') kwa sababu waasi 'walizitia nguo zao rangi nyekundu ya udongo wa nchi yao ili wasiweze kuonekana upesi kwa mbali'. Waasi hawa waliikamata Aribonimano, wakamuua balozi pamoja na mhubiri dini wa Kiingereza pamoja na familia yake na wakadai kuondoshwa kabisa kwa ibada na shule za Kikristo na pia huduma za kijeshi na kazi za kulazimishwa. Mwezi wa Machi, 1896, harakati nyingine zilitokea sehemu za kaskazini na kusini mwa Imerina, na zilidai kurejeshwa kwa imani za kale na kuondolewa

kwa tabaka tawala na zilikuwa vilevile na madhumuni ya kumlazimisha Mfaransa kuondoka.

Wamenalamba walichukua silaha za askari waliokimbia kutoka kwa *foloalindahy* au walizinunua kwa wafanya biashara wa Kihindi au wa Kichotara, jambo linaloonyesha kwamba mawasiliano na sehemu za pwani yalikuwa rahisi. Vikosi hivi viliundwa kwa taratibu zile zile kama vikosi vya kifalme pamoja na kuwepo kwa orodha ya vyeo na mgawanyo wa askari katika vikoki maalumu. Vikosi hivi viliwashambulia wawakilishi wa watawala wachache ambao waliwaona kwamba wamechukua madaraka kinyume na sheria na pia kusababisha kushindwa vitani; na vile vile waliwashambulia waenezi wa dini wa kigeni na wahubiri watembezi wa Kimalagasi ambao walionekana kuwa ni maadui wa imani za jadi . Kwa hivyo walianza kuchoma makanisa na mashule na kurejesha dini ya wahenga katika pahala pake pa heshima. Lakini baadhi ya vitendo vya *Wamenalamba* viliwakasirisha baadhi ya wananchi. Miongoni mwa mbinu zao ulikuwa ule mtindo wa kushambulia sehemu za soko kwa madhumuni ya kueneza hofu na pia kudhoofisha kile chombo ambacho kilikuwa ndiyo alama ya unyonyaji uliotokana na atawala wachache; hujuma hizi za soko pia zilikuwa na lengo la kuwapatia mahitajio yao. Hujuma hizi, pamoja na uvamizi wa mazao walioufanya vijijini ambako watu hawakuwaunga mkono, ziliwawezesha kuvuruga kwa urahisi mawazo ya wakazi wa kudumu ambao walishindwa kutofautisha baina ya *Wamenalamba* na *Jirika* au waporaji na majambazi. Wakoloni na marafiki zao wa kienyeji waliitumia fursa ya mvurugano huu kuwatenga waasi.

Upinzani uliofanywa na wananchi walio wengi huko Imerina ulishindwa kwa sababu ya ukali wa hatua za ukandamizaji zilizochukuliwa, lakini zaidi kwa sababu ya kutokuwepo kwa utaratibu kati ya vikundi mbalimbali na pia kwa vikundi hivi kushindwa kujiunga na harakati za uasi zilizoanza katika majimbo mengine ya Malagasi.

## *Upinzani wa walio wengi katika majimbo yaliyokuwa chini ya mamlaka ya kifalme*

Katika baadhi ya majimbo, majibu hya wananchi kuhusu kutamalakiwa kwa Wafaransa yalitokana na kuathiriwa kwa wananchi hao na *Menalamba.* Katika mwaka 1896, katika jimbo la *Mampikony* upande wa Kaskazini-Magharibi, Rainitavy, ambaye alikuwa gavana wa zamani wa Merina, alikiandikisha uaskari na kukipa silaha kikundi cha mchanganyiko cha wakimbizi wa Kimarina kutoka jeshi la kifalme na wachungaji wanyama la Kisakalava kwa madhumuni ya kuunda kikundi cha *Menalamba* cha Rabozaka. Haya ndiyo maasi peke ya Kimenalamba ambamo maswali ya biashara yalichukulia nafasi muhimu; madhumuni yalikuwa kudhibiti biashara ya mkoa ambayo karibu ilimilikiwa na Wahindi na Machotara peke yao.

Katika zile wilaya zilizodhibitiwa sana, na kwa hivyo zikinyonywa sana, kushindwa kwa Tananarive mwezi wa Septemba mwaka 1895 kulikuwa ndiyo ishara ya

kuanza kuwashambulia Wamanamboninahitra, ambao wengi wao walikuwa maafisa wafanya biashara, pamoja na wahamaji wa Kimerina na wageni. Katika wilaya ya mashariki, kwa mfano, yale machafuko yaliyosababishwa na 'Wavorimo=, mbari ndogo iliyoishi katika sehemu ya chini ya eneo la Mangoro, yalianzisha mfululizo wa maasi yaliyoleta hali ya wasiwasi katika jimbo hilo kwa kipindi chote cha mwaka wa 1896. Mwanzoni maasi haya yaliwakamia wale watawala wachache wa Merina peke yao. Lakini zile hatua kali zilizochukuliwa na vikosi vya jeshi la ukaliaji kukomesha maasi hayo ziliwafanya Wabesimisaraka wawachukie Wafaransa pia. Baada ya hapo tena waasi wakazidisha vita vyao na wakawashambulia Wafaransa na Wamerina pia. Harakati hizi hazikuanza kufifia mpaka mwezi Desemba, 1896, na zilitoweka kabisa zilipoanzishwa zile hatua alizozichukua Generali Gallieni za kuwaondoa wawakilishi wa watawala wachache na kuwaweka machifu wa kienyeji badala yake.

## *Ukinzani wa wananchi walio huru*

Hapo mwanzo Wafaransa walifikiri kwamba kwa kuiteka Tananarive walikuwa wamekwishaweza kukidhibiti kisiwa chote. Lakini baada ya kuzikomesha zile harakati za *Menalamba* na kwa njia hiyo kuweza kuikalia Imerina, waligundua kwamba ilibidi pia wayateke yale majimbo yaliyokuwa huru. Wale watu ambao walikuwa hawajapata kutawaliwa na mfalme walichukua silaha zao na kuziviza juhudi za Wafaransa za kutaka kujipenyeza. Lakini katika Ambogo, mfano wa jimbo ambalo sifa yake kubwa ilikuwa ni mgawanyiko wake kisiasa katika visehemu kadha vidogovidogo Wafaransa walitumia mbinu mbalimbali ili waweze kutawala. Wakati walipokuwa wakijaribu kutafuta makubaliano baina yao na watawala wa sehemu za mwambao na sehemu za bara Wafaransa, kuanzia mwaka 1897, walianzisha vituo vya kijeshi katika vijiji vikubwa ili waweze kulinda usalama katika mkoa. Juu ya yote haya, mapema mwaka 1899 kulizuka machafuko chini ya uongozi wa machifu wakuu yaliyotokana na kule kuchukizwa kwa wananchi kutawaliwa na wakoloni. Lakini ilivyokuwa vile vikundi vya wapinzani vilikuwa vimetawanyika sehemu mbalimbali na havikuweza kuungana pamoja kumkabili adui, vikundi hivi vilishindwa na Wafaransa.

Kutekwa kwa Menabe, ambayo ilikuwa na utawala wa kifalme, na ilikuwa kubwa na ikiendeshwa vizuri, kulianza mwaka 1897. Mfalme Toera na machifu wake wakuu walitaka kusalimu amri, lakini Majoe Gerad, ambaye ndiye aliyekuwa mkuu wa shughuli za kivita, badala ya kusalimu amri kwao, aliona bora kuuteka mji mkuu na 'kuwaua Wasakalava wote walioshindwa kukimbia, miongoni mwao akiwa Mfalme Toera'. Kitendo hiki cha ukatili kilizusha haraka za upinzani zenye muundo madhubuti na zilizoongozwa na Ingereza, ndugu na mrithi wa Toera, ambazo zilisambaa katika Menaba nzima na kuendelea mpaka mwaka 1902. Watu wa Antandroy na Mahafale sehemu ya kusini, pia walizipinga juhudi za Wafaransa za kutaka kujipenyeza na hawakusalimu amri mpaka

mwaka 1904.

Kutokana na sera yake ya kuinyakua nchi kidogo kidogo Gallieni aliweza kudai katika mwaka 1904 au karibu na wakati huo kwamba shughuli ya kutamalaki kukikalia na kukiunganisha kisiwa imemalizika.

## *Nchi iliyoungana na kuwa kitu kimoja kutokana na kusalimu amri kwake chini ya Ufaransa na kupinga kwake utawala wa Kikoloni*

Hatua za Malagasi za kupinga juhudi za wakoloni za kuiteka nchi na kujipenyeza zilizomalizika mwaka 1904 zilikuwa za bure. Kirasmi, shughuli za kijeshi zilikuwa zimekwishamalizika na mifumo ya kikoloni katika shughuli za utawala, uchumi na utamaduni ilianzishwa na Gagllieni ili kuiwezesha Ufaransa kuimarisha utawala wake moja kwa moja pamoja na 'kuistaarabisha' na kuisilimisha Malagasi. Lakini mwaka huo huo wa 1904 ulishuhudia kuanza kwa kipindi kipya cha mapambano ya wananchi wa Malagasi dhidi ya madhila na unyonyaji wa kikoloni pamoja na juhudi za wakoloni za kutaka kuvuruga utu wao wa kitaifa na kubadilisha mwenendo wao wa kimaisha.

Kwa upande wa utawala, ukoloni uliuporomoa ule mfumo wa kisiasa uliokuwepo muda mrefu sana. Huko Imerina Gallieni aliuondoa ufalme tarehe 28 Februari, mwaka 1897 na pia marupurupu ya mabwanyenye tarehe 17 mwezi wa Aprili. Katika sehemu nyingine za nchi Gallieni hakuziondoa kisheria zile tawala zilizokuwepo za aina mbali mbali. Badala yake alijaribu, kama alivyoamriwa na Waziri, kuukomesha utawala wa Merina na kuanzisha 'siasa ya makabila'' ambayo ilikwishajaribiwa huko Sudan ya Kifaransa na Indo-China. Kwa hiyo watawala wa zamani na watoto wao waliingizwa katika shughuli za utawala kama ni 'magavana wenyeji', na wakati huo huo 'nchilindwa za ndani' ziliundwa katika tawala za kifalme zilizoenea upande wa magharibi wa kusini-magharibi. Mfumo huu haukuwa wa kuridhisha, na kuanzia mwaka 1905 na kuendelea idadi ya wasaidizi wa Kimarina iliongezeka kupita kiwango kwa vile Wamerina walionekana wanafaa zaidi kwa shughuli za 'maendeleo na marekebisho' kuliko watu wengine. Gallieni vile vile aliwaleta masetla wa Kifaransa na wafanyakazi wahamiaji wa Kisiasa katika koloni jipya, jambo ambalo liliwaudhi sana wenyeji. Na mwisho Gallieni aliifanya itumike katika kisiwa kizima ile sera ya *fokonolona* ambayo ilizifanya jamii za vijijini ziwe na dhamana ya pamoja katika shughuli zao; pia alirejesha tena ule mpango wa kifalme wa kufanyisha watu kazi kwa lazima.

Kuunganishwa kwa eneo lote la Malagasi kulikamilishwa kwa kuchukuliwa hatua tatu. Ya kwanza ilikuwa kusanifisha taratibu za utawala (baina ya mwaka 1927 na 1933 majaribio matatu yalifanywa ya kuweka mipaka ya utawala wa mitaa). Hatua ya pili ilikuwa kuanzisha na kusambaza *fokonolana* kiutawala kama chombo cha kuendeshea mamlaka. Hatua ya tatu ilikuwa kuanzisha mkusanyiko wa sheria kwa kuunda katika mwaka 1901, 'sheria za kienyeji' zilizokuwa ndio msingi wa kuendesha upande wa utawala haki ambazo

ziliumanisha pamoja mahakama na chombo cha utekelezaji sheria.


Kwa wananchi wa Malagasi, ukoloni ulimaanisha kwamba vile vile kisiwa hicho kilichoitwa 'maendeleo' ya koloni hili kilipambana na matatizo ya vibarua. Gallieni aliurejesha tena ule mpango wa Merina wa kifalme ulioitwa *fonompoana* na akaamua kutumia mpango huo katika kisiwa kizima katika mwaka 1896 na 1897; kwa hivyo kila mwanamume wa Kimalagasi aliyekuwa na afya kamili mwenye umri kati ya miaka 16 na 60 aliwajibika kufanya kazi bila ya malipo siku hamsini katika mwaka. Ofisi iitwayo '*Office Central du Travail*' ilianzishwa mwaka 1900 na ilikabidhiwa kazi ya kurahisisha taratibu za kuandikisha wafanyakazi kwa ajili ya kampuni za kibinafsi. Walipoona wamekabiliwa na upinzani wa Wamalagasi dhidi ya kuandikishwa watu kazi kwa njia yoyote ile, watawala walilibeba wao jukumu hili na katika mwaka 1926 walianzisha chombo kiitwacho Service de la Main d'oeuvre pour les Travaux d'Interest General' (SMOTIG) ambacho kiliwataka wale watu ambao hawakutakiwa kutoa huduma za kijeshi badala yake kufanya kazi kwa muda wa miaka mitatu ambayo baadaye ilipunguzwa na kuwa miwili katika sehemu za majenzi za koloni hili. SMOTIG, ambayo Wamalagasi waliiona imewaletea 'utumwa wa kificho' ilichukiwa sana siyo tu na wale waliofanyishwa kazi kwa mabavu lakini pia na wale wengine ambao walipoteza kazi zao kutokana na mpango huu.

Madhila haya ya kikoloni yalizidishwa kwa watu kunyang'anywa ardhi zao ambazo zilichukuliwa na kugawiwa kwa masetla. Chini ya sheria iliyopitishwa mwaka 1926 serikali ilitangazwa kuwa ndiyo yenye kumiliki 'ardhi yote tupu isiyo na mwenyewe ambayo haijaimarishwa, wala kuzengewa, wala kutolewa kwa madhumuni maalumu kuanzia tarehe ya kupitishwa sheria hii.'

Pirikapirika za mwanzo dhidi ya mfumo wa Kikoloni

Mabadiliko haya ya kisiasa na kiuchumi yaliathiri sana mifumo ya kijamii, yakasababisha kuvunjika kwa koo kadhaa na kuvuruga maadili na mwenendo wa wahenga. Huko Imerina idadi kubwa ya shule iliyoongezeka na uandikishaji kwa wingi wa wafanyakazi wa serikali wa ngazi za chini ulileta mgongano miongoni mwa watawala wachache wa zamani ambao walikuwa wamenyimwa madaraka yao baada ya kutekwa na miongoni pia mwa kile kikundi bora kipya kilichopata mafunzo kwenye shule za kikoloni ambacho kilihisi kinakoseshwa nyadhifa dhamana katika mfumo wa kikoloni. Kwa hivyo madhara ya za kikoloni yaliathiri ngazi zote za jamii ya Malagasi na kuchochea mapambano ya aina mbalimbali.

La kwanza katika mapambano haya ni yale maasi yaliyotokea mwezi wa Novemba, 1904 katika jimbo la Farafangana ambayo yalisambaa kwa haraka sana upande wa magharibi kutokana na mawasiliano ya kijadi yaliyokuwepo hapo kale kati ya watu wa Mashariki na watu wa Bara (kielelezo namba 10.1). Waasi wakiongozwa na machifu wa Mbari za Bara na za sehemu za kusini-mashariki au na wanamgambo walioasi kama vile Koplo Kotavy, walivishambulia vituo vya kijeshi vya Ampariby, Begogo na Esira na sehemu




**10.2** Upinzani, maasi na Uzalendo Madagaska, 1896-1935

walizopewa watu maalumu miongoni mwao ikiwemo *Emeraude* ambapo walimuua mwenyewe, Luteni Conchon. Wale askari wa miguu walioandikishwa mitaani ama waliviacha vituo vyao Tsivory ua Bekitro au walijiunga ua waasi kama ilivyotokea huko Antanimora.

Tokeo la pili muhimu ni kule kuweko kwa kikundi cha Sadivahe (1915 mpaka 1917). Hiki kilikuwa kikundi cha uasi cha wakulima ambacho mwanzo kilianza sehemu za kusini-magharibi katika ufukwe uliokuwa upande wa kushoto wa mto Menerandra katika mwezi wa Februrari mwaka 1915 ua kutapakaa kwa haraka sana sehemu za Ampanily na Tsihombe. Watu wa *Sadiavahe* waliiba ng'ombe, wakavishambulia vijiji, wakakata nyaya za simu, na wakakimbilia sehemu za kujificha mbali kabisa na vituo vilivyodhibitiwa na utawala. Waliunda vikundi vyenye watu kuanzia kumi mpaka arobaini tu ambayo viliweza kwenda pahala mbali mbali kwa wepesi sana. Miongoni mwa sababu zilizovifanya vijiji vizima kuwaunga mkono Wasadiavahe ama kwa dhahiri au siri ni ule umaskini mkubwa wa watu uliosababishwa na kunyesha kwa mvua zilizokuwa za nadra lakini zilizokuwa kubwa sana, utozaji wa kodi ya ng'ombe na taathira kubwa za Vita vya Kwanza vya Dunia ambavyo vilisababisha kukusanywa kwa watu ili kwenda vitani na pia kuleta uhaba wa chakula.

Namna nyingine ya kuupinga ukoloni ilikuwa kwa njia ya mgomo; yaani kukataa kutii amri, kutupilia mbali kila kitu ambacho kilionekana kuwa ni alama ya 'ustaarabu' lakini kilihusika sana ama na ukoloni au kuwepo kwa wageni, kuwazuia watoto kwenda shule ambako kulionekana na baadhi ya watu kuwa ni aina ya 'kufanyishwa kazi kwa nguvu kwa kikoloni', na mwisho, kuvihama vijiji vilivyoanzishwa kando ya barabara sehemu za kusini katika juhudi za kuweka watu pamoja. Kugoma huku kushirikiana hakukulnekana kwa wakoloni kuwa ni jambo la hatari.

Aina ya nne ya kupinga ukoloni ni zile harakati za chama cha siri kilichojulikana kwa jina la *Vato Sakelika* ((VVS) maana ya jina hilo ikiwa 'chenye nguvu na ugumu kama jiwe na chuma'. Chama cha VVS kiliundwa mwezi wa Julai, mwaka 1913 huko Antananarive na wanafunzi saba kutoka chuo cha utibabu cha mji huo, ambacho kilikuwa ni chuo pekee kilichotoa mafunzo ya shahada ya juu kabisa iliyoweza kupatikana na wananchi wa Malagasi wakati huo; kuundwa kwa chama hiki kulifuatia mara tu baada ya kuchapishwa kwa mfululizo wa makala yaliyoandikwa na padri wa Kiprotestanti Ravelojaona, yenye jina la 'Japani na Wajapani'. Makala haya yaliwataka Wamalagasi wasige mfano wa Japani ambako mambo ya kileo na ya kijadi yalioanishwa kwa ustadi. Wanafunzi hawa waliungwa mkono na makarani na wafanyakazi maofisini na walimu wa shule za msingi. Ingawa VVS kilikuwa kikundi cha siri, ,kilieleza maoni yake kwa uwazi magazetini kwa njia ya kuwataka Wamalagasi kujitolea muhanga kwa ajili ya nchi yao ili wananchi waweze kuendelea na kuishi katika hali ya uhuru wa heshima. Kwa vile kilikuwa ndicho kilichobeba ujumbe wa taifa, chama hiki cha siri kilikuwa tishio lisiloweza kustahamilika kwa upande wa utawala, hasa wakati wa vita. Wafaransa walichukua hatua

kali kuziviza harakati hizi. Miongoni mwa hatua hizi kulikuwa na adhabu ya kazi ngumu, kupelekwa wakosaji kambini huko Nosy Lava, kupiga marufuku lile gazeti ambalo wahariri wake walihusika na harakati hizi na mwisho kufukuza kazi watumishi wa serikali.

Ukali wa hatua zote hizi unaonyesha vipi wakoloni walikwisha utambua uzalendo mchanga uliojitokeza miongoni mwa kile kikundi bora katika jamii ua vipi waliyahofia matokeo yake. Matokeo ya hatua hizi za ukandamizaji yalikuwa kuwafanya Wamalagasi waache mambo yao ya kisirisiri na kuanzia hapo kupeleka madai yao ya kisiasa bayana kwa njia ya kampeni magazetini, kwa kuanzisha vyama vya wafanyakazi na kadhalika.

Juhudi za kutaka kurejesha heshima

Miaka kumi iliyofuatia Vita vya Kwanza vya Dunia ilikuwa kipindi muhimu kwa sababu ya mwamko uliokuwa ukizidi kukua uliojidhihirisha katika nchi nzima na kwa kuanzishwa na kuimarishwa kwa harakati za kizalendo. Mabadiliko haya muhimu katika historia ya Malagasi yanaweza kuhesabiwa kuwa yameanza pale wale waliokuwa askari wa vita waliporejea Malagasi. Huku wakijifaragua katika utukufu waliojipatia, majamadari hawa ambao waliamini kwamba wameitumikia Ufaransa kwa namna ile ile Mfaransa yeyote alivyoitumikia nchi yake, walidai haki zile zile walizokuwa nazo Wafaransa, na katika dai hili waliungwa mkono na wananchi wenzano wengi. Kwa hivyo, chini ya uongozi wa Ralaimongo walianza mapambano ya muda mkubwa ya kujaribu kujipatia uraia wa Kifaransa.

Ralaimongo (1884-1942) ambaye kwanza alikuwa mwalimu wa Kiprotestanti wa shule ya msingi, halafu akawa karani, halafu mwanafunzi huko Paris, halafu askari aliyepigana vita na halafu mjamaa, alikuwa ndiye mwanzilishi halisi wa harakati za uzalendo. Aliporejea Malagasi mwaka 1922 alikaa Diego Suarez ambayo yalikuwa ndiyo mazingira mwafaka kabisa ya kuenezea propaganda kwa sababu ya kuwepo pale kwa wafanyakazi katika ghala ya silaha za manuwarini na pia kwa sababu ya matatizo magumu yaliyokuwepo kuhusu kumiliki ardhi katika sehemu tambarare za Mahavavy na katika jimbo la Antalaha. Mpaka mwezi wa Mei, 1929 Diego Suarez na siyo Tunanarive, ndio kilichokuwa kitovu cha harakati za uzalendo ambazo mbali ya kupigania haki sawa pia zilipinga maovu yasiyovumilika yaliyotokana na mfumo wa kikoloni.

Harakati hizi ziliungwa mkono kwa dhati na jamii ya watu wa biashara ambayo ilionyesha hamasa zaidi kuliko watumishi wa serikali walioogopa kutiwa adabu za kitawala. Harakati hizi, kwa kweli, zilipata msaada wa fedha kutoka kwa wafanya biashara hasa wale waliokuwa katika mji mkuu.

Kikundi cha Ralaimongo, ambacho kilipata nguvu kwa kuungwa mkono na Ravoahangy, mwanachama wa zamani wa kile kikundi cha VVS, Emmanuel Razafindrakoto, Abraham Razafy, mwandishi katika tawi la Tananarive la Chama cha Kifaransa cha wafanyakazi na Jules Ranaivo, kiliungwa mkono pia na wazungu wenye siasa

ya mrengo wa kushoto miongoni, nwao wakiwa Albertini, mwanasheria, Dussao, Planque na Vittori. Katika juhudi za kuwakilisha na kutetea madai yao kuanzia mwaka 1927 na kuendelea walichapisha magazeti mawili, moja *'L'Opinion'* huko Diego Surez na la pili *'L'Aurore'* Malagachi huko Tananarive, ambayo yalibidi kupambana na maudhi madogo madogo ya kila aina kutoka kwa watawala. Upande wa siasa kikundi hiki kilidai kwamba 'uendeshaji wa maslahi ya jumla ya wananchi uwe mikononi mwa Baraza Kuu lenye madaraka makubwa'; kilidai pia kuondoshwa kwa Gavana Mkuu na kuwakilishwa kwa Malagasi katika Serikali ya Ufaransa.

Sambamba na shughuli za kikundi cha Ralaimongo kulizuka tena machafuko ya kidini katika madhehebu ya *Tranzozoro.* Mjadala uliochipuka upya kati ya waumini wa Kimalagasi na mapadri wa Kiprotestanti wa Kizungu haukumalizika mpaka mwaka 1929 ilipotolewa hukumu na baraza la *'Counseil du Contentieux'* ambalo liliyatambua madhehebu ya 'Tranzozoro' kuwa ni misheni ya kienyeji. Kuanzia hapo tena madhehebu haya yalipigania haki ya kujipatia serikali ya ndani chini ya mwamvuli wa harakati za kupigania uhuru wa dini ambao viongozi wake walikuwa Ralaimongo na Dussac. Baada ya kutayarisha kwa kushirikiana na Ralaimongo na Ravoahangy, lile dai la *Petetion de Indegenes de Madagascar* la kutaka uraia wa Kifaransa na kuondoshwa kwa utawala wa 'kienyeji' na kudai marupurupu ya kijamii na kitamaduni yaliyoanzishwa chini ya Jamhuri ya Tatu, Dussac aliwasili Tananarive mwezi wa Mei, 1929 kufahamisha madhumuni ya madai haya. Mkulano uliopangwa uwe tarehe 19 Mei, ambao 'raia wa Kimalagasi' walizuiwa kuhudhuria, uligeuka na kuwa maandamano makubwa katika barabara za mji mkuu ambayo waandamanaji wake walikariri matamko yaliyokuwa dhidi ya serikali kama vile 'Uishi uhuru na haki ya kukutanika' na 'Ianguke Serikali ya Kienyeji'. Maandamano haya makubwa yaliyokuwa ni ya mwanzo yalikuwa ni ishara ya daraja muhimu katika ukuaji wa harakati za uzalendo. Matokeo ya tarehe 19 Mei, 1929 yalikuwa ni kilele cha harakati za kupigania usawa na ndio chanzo cha mapambano ya kweli ya kisiasa yaliyochukua sura ya kampeni za kueneza fikra za kisiasa, kuanzisha vyama na sera za kisiasa na kuchomoza kwa magazeti ya aina mbalimbali na yenye wafuasi wengi.

Ralaimongo; aliyekuwa amehamishiwa katika Bandari ya Berge, aliwashajiisha wakulima kuendeleza aina ya upinzani ilivyofuatwa na Gandhi. Katika mwaka 1931 Ralaimongo alilitaja kwa uwazi swala la uhuru wakati alipokuwa akijibu hotuba ya Paul Reynaud, Waziri wa Makoloni, hotuba ambayo ilipinga madai ya kutaka kugeuzwa jumla jamala kwa uraia. Katika gazeti la *'L'Opinion'* la tarehe 20 mwezi wa Julai mwaka 1934 Ravoahangy aliamsha mawazo juu ya 'haki ya kimaumbile na isiyonyakulika ya kuweza kuunda taifa lililo huru'. Koanzia mwaka 1935 na kuendelea magazeti mengine yaliyodhihirisha wazi kwamba yana mtizamo wa kizalendo yalianza kuchomoza. Gazeti la *'Ny Fierenana Malagasy'* (Taifa la Malagasi) na la *'Ny Rariny'* yalishikilia moja kwa moja kwamba Malagasi iwe huru. Lakini kwa sababu chungu nzima harakati hizi ziilipoteza kasi zake. Kwanza jamii ya wafanyabiashara ambayo ilipata pigo kubwa kutokana na mgogoro

wa kiuchumi wa mwaka 1930 ilisita kuwaunga mkono. Pili, watumishi wa serikali, kwa kuogopa kujihatarisha na kukosa kazi zao pia walirudi nyuma. Tatu, mapadri wa Kiprotestanti ambao walifadhaika walipoona mambo yameelekea upande wa siasa walirudi nyuma, na kubaki makanisani mwao. Mwisho wananchi wa Malagasi wa tabaka la kati waliamua kwa utaratibu kusubiri kwanza na kutazama mambo yanavyokwenda na wakahiari zile tija za moja kwa moja za kibinafsi zilizopatikana kutokana na uraia wa Kifaransa. Pakihitajika Muungano wa Wananchi kwa pamoja kuweza kuzipa harakati za uzalendo msukumo mpya.

## *Hitimisho*

Harakati za wananchi wa Malagasi dhidi ya mashambulizi ya Kifaransa ambazo zilitumia silaha zilitumia silaha zilitawanyika ovyo na zilikosa uratibu sawa sawa zilishindwa kuzuia kuanzishwa kwa mfumo wa kikoloni. Lakini mantiki ya ukoloni na mshituko walioupata Wamalagasi ambao walikabiliwa na hatari ya kupoteza sifa zao za pekee iliwafanya wachukue hatua kadha katika juhudi za kurejesha heshima yao. Yale mapambano dhidi ya madhila ya ukoloni yalisababisha kuzaliwa na kumea kwa kasi kubwa kwa harakati za kizalendo. Lakini ulipofika mwaka 1935 hitilafu nyingi zilizokuwepo za kimkoa, kidini na kijamii zilidhoofisha harakati za kizalendo na kuufanya utawala mpya ubaki katika hali iliyoonyesha kuwa imara kabisa.

# 11

## *Liberia na Ethiopia 1880-1914 Kuendelea kwa Dola Mbili za Kiafrika*

Kama ilivyo katika nchi nyingi za Kiafrika, dola ya Liberia na dola ya Ethiopia vile vile zilikabili msukosuko wa ubeberu wa kikoloni wa Kizungu na zilifanywa zihimili viwango mbali mbali vya mashambulio na uchokozi katika miaka ishirini ya mwisho ya karne ya kumi na tisa. Lakini, kinyume na nchi nyingine, nchi hizi mbili ziliweza kuukabili msukosuko huu na kuweza kujiweka katika hali yao ya uhuru. Maswali ya kuvutia ambayo sura hii itayashughulikia ni vipi nchi hizi mbili zilinusurika na utawala wa kikoloni wa Kizungu na mabadiliko gani makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yalitokea katika nchi hizi wakati wa mnyang'anyiro.

### *Mashambulizi ya Wazungu katika nchi ya Liberia na Ethiopia 1880 - 1914*

Nchi zote mbili, yaani Liberia na Ethiopia, zilikuwa na mahusiano ya kirafiki na madola ya Kizungu mpaka mwaka 1897. Lakini katika kipindi cha mnyang'anyiro kuanzia 1880 na kuendelea mahusiano haya yalianza kubadilika.

Liberia

Ubeberu wa Kizungu huko Liberia katika kipindi tunachozingatia ulijitokeza katika hali tatu. (1) Uporaji wa ardhi ya Liberia uliofanywa na madola ya Kizungu. (2) Kuingilia sana mambo ya ndani ya Liberia.(3) Kudhibitiwa kwa uchumi wa Liberia na wafanyabiashara, mastadi wa shughuli za kifedha, watu waliopewa haki maalumu, na mabingwa wa mipango ya biashara, wote hawa wakiwa Wazungu ambao madola haya yalikuwa na imani nao na pia yaliwapa misaada.

Katika kuuitikia mwaliko wa wakazi wa Vai wa sehemu ya kaskazini-magharibi ya Liberia na wa Sierra Leone, na pia mwaliko wa wafanyabiashara wa Kiingereza aliokuwa sehemu za pwani za Vai, na huku ikimezea mate biashara na mapato ya Sierra Leone, Uingereza iliingilia mambo ya Liberia eti kwa madhumuni ya kuwahifadhi watu wa Vai na wafanyabiashara wa Kiingereza kutokana na amri na matakwa ya Liberia. Baada ya mazungumzo yasiyoleta tija yoyote na yaliyokuwa yakisitasita kati ya wawakilishi wa


Uingereza, wa Waliberia na wa wakazi wa Vai, mnamo mwezi wa Machi, 1882, Uingereza ilijinyakulia sehemu kubwa ya Vai ambayo ilikuwa chini ya machifu mpaka kufikia Sierra Leone. Ingawa machifu wa Vai hawakutaka utawala wa Kiingereza, walitaka Uingereza iingilie kati tu kusawazisha mambo. Watu wa Liberia, wakishangazwa na hatua iliyochukuliwa na Waingereza lakini bila ya kuwa na uwezo wa kufanya lolote, walitoa 'Taarifa na Malalamiko' yenye mhemko kupinga kitendo hicho. Taarifa hiyo ilipelekwa kwa madola yote yaliyokuwa na mahusiano na kimkataba na Liberia ikiwaomba kuisaidia Liberia na kuingilia kati 'kuzuia hali ya mambo ambayo ilitishia kuiangamiza' nchi hiyo. Lakini ombi la Liberia liliangukia patupu. Kwa hivyo katika mwezi wa Novemba, 1835 Liberia ilitia sahihi mkataba na Uingereza ambayo iliweka mipaka kati ya Liberia na Sierra Leone kwenye mto wa Mano, jambo ambalo halikuwa na maslahi kwa Liberia.

Vile vile Wafaransa walijinyakulia sehemu ya kusini-mashariki ya Liberia baina ya mto Cavalla na mto Pedro katika mwezi Mei, 1891 wakichakulia fursa kule kutoridhika kwa wakazi wa sehemu hizi na sera ya biashara ya Liberia na pia kule kutokaliwa sawa sawa kwa eneo hili na Liberia. Kwa mara nyingine tena wananchi wa Liberia walitoa ombi lililojaa mhemko kwa 'dola zote za kistaarabu za Kikristo za ulimwenguni' kuingilia kati kwa niaba yao, lakini ilikuwa kazi bure.

Ili kuzuia ardhi ya Liberia kungiliwa zaidi, serikali ya Liberia ilipeleka wajumbe Washington mwaka 1890 na London mwaka 1892 kuzitaka nchi mbili hizi zijitolee kuhifadhi ardhi ya Liberia kwa ukamilifu wake, lakini hakuna nchi hata moja kati ya mbili hizi iliyokubali kujifunga hivyo.

Liberia ilipoteza ardhi zaidi kwa Uingereza na Ufaransa baina ya mwaka 1892 na 1914 wakati madola haya yalipokuwa yakishindana kusonga mbele katika juhudi za kutaka kulikalia bara la Afrika na baadaye walipoweka mipaka baina ya ardhi zao na Liberia. Katika mwaka 1907, Ufaransa ikisaidiwa na Marekani iliwasambika Liberia mkataba ulioamuliwa upande mmoja tu,ambao uliipatia Ufaransa sehemu nyingine zaidi ya ardhi ya Liberia mbele ya mto Makona.

Labda kwa kuionea kijicho Ufaransa kwa kujipatia ardhi ya Liberia katika mwaka 1907, Uingereza nayo ilishikilia kwamba ipate eneo la Kanre-Lahun ambalo ilikuwa imekwisha likalia tangu mwaka 1902. Baina ya mwezi Novemba 1909 na mapema 1910, serikali ya Liberia ilijaribu bila ya kulaulu kulipata eneo la Kanre-Lahun kutoka kwa Uingereza kwa njia ya kuwashawishi. Swala hili mwisho lilisawazishwa mwezi wa Januari, 1911 kwa mkataba kati ya Liberia na Uingereza; na kwa mujibu wa mkataba huu Uingereza ilibaki na miliki ya jimbo la Kanre-Lahun lakini iliipa Liberia ardhi mbaya iliyokuwa baina ya Mto Morro na Mto Manna pamoja na fidia ya ,4,000 ili iweze kuimarisha ardhi hiyo. Liberia pia ilipata haki ya kupitisha meli zake bila ya malipo katika Mto Mano. Uwekaji wa mwisho wa mpaka baina ya Liberia na Sierra Leone ulifanyika mwaka 1915. Kwa hivyo Liberia ilinusurika na matishio na mashambulio ya Waingereza na Wafaransa lakini si kwamba haikuathirika.




**11.1** Ethiopia na unyang'anyanaji wa Afrika

Ethiopia

Vitimbi vya kibeberu vya Ulaya vya kutaka kunyakua ardhi na uhuru wa Ethiopia vilikuwa na hatari kama vile vilivyofanywa dhidi ya Liberia (taz. kielelezo 11.1). Mwanzo wa vitimbi hivi unaweza kuonekana mwaka 1869 wakati mhubiri wa Kilazeri wa Kitaliana, Guiseppe Sapeto, alipoinunua bandari ya Assab iliyopo Bahari ya Sham kutoka kwa Sultani wa pahala hapo kwa thamani ya dola 6,000 za Malikia Maria Theresa. Bandari hiyo ikawa mali ya kampuni ya meli ya kibinafsi ya Kitaliana, Societa Rubattino, na katika mwaka 1882 bandari hiyo ilitangazwa kuwa koloni la Italia.

Ingawa Yohannes alikuwa mzalendo mashuhuri, hakushughulishwa sana na kuja kwa Wataliana kama alivyoshughulishwa na kuondoka kwa Misri ambayo wakati ule iliitawala sehemu kubwa ya Bahari ya Sham na Ghuba ya Aden, sehemu za pwani za Afrika pamoja na sehemu za bara zilizokuwa karibu karibu. Kwa hiyo Mfalme huyu upesi upesi aliandikiana mkataba na Uingereza tarehe 3 Juni, mwaka 1884. Kwa mujibu wa mkataba huo Mfalme huyu alijifunga kupa Uingereza msaada na badala yake Uingereza ilikubali kurejesha maeneo yaliyokuwa katika mpaka wa Sudan ambayo hapo nyuma kidogo yalikuwa yamekaliwa na Misri. Lakini nguvu za mkataba huu zilikuwa za muda mfupi tu, kwani tarehe 3 Februari, 1885 Wataliani waliiteka Massawa na wakajipenyeza mpaka kwenye vijiji vya Sahati na Wia. Walifanya hivyo kwa kibali cha Uingereza ambayo ilipendelea kuwaona Wataliani wanajitawanya katika sehemu hizi kwa tamaa kwamba kwa njia hii Uingereza itaweza kuzuia kuenea kwa Wafaransa, ambao walikuwa washindani wao wakubwa katika mnyang'anyiro wa Afrika. Ras Alula, shujaa maarufu wa Kiethiopia, alipinga kujiingiza haku kwa Wataliani, lakini jawabu la Wataliani ilikuwa kuzijengea maboma zile sehemu zilizosababisha ugogoro, na kwa kupeleka majeshi zaidi ambayo yalizuiwa na Ras Alula huko Dogali katika mwezi wa Januari, 1887. Wavamizi hapo tena waliwaondoa watu wote wa sehemu za Sahati na Wia. Huku wakilalamika juu ya mauaji yaliyotokea huko Dogali, wavamizi hawa walizuia meli zote zilizokuwa zikileta vitu Ethiopia.

Vita kati ya Wataliana na Yohannes vilionesha viko njiani lakini Wataliani ambao walikuwa na hamu ya kuyakwepa mapigano ya taabu ya milimani waliwashawishi Waingereza waingilie kati. Mwana Diplomasia wa Kiingereza, Sir Gerald Portal, alipelekwa kwa Mfalme kumtaka akubali kwamba Wataliani wazikalie sehemu za Sahati na Wia na pia sehemu ya Senahiti (au Bogas) ambayo Wamisri walikuwa wameichukua mwaka 1884. Yohannes aliposomewa mapendekezo haya aliyakataa moja kwa moja na kwa hasira alimwandikia barua Malkia Victoria na kueleza kwamba ikiwa malkia huyo anataka kuleta amani basi iwe wakati Wataliani wako kwao na Waethiopia katika nchi yao.

Yohannes, wakati kakabiliwa na tishio lililokuwa likiongezeka kutoka kwa Italia, aliimarisha ulinzi wake kwa kuwasongeza mbele zaidi askari waliokuwa katika mpaka wa Sudan. Walipoona kwamba sehemu ile haikuwa na ulinzi, wafuasi wa Mahdi walipashambulia pahala hapo. Mfalme aliharakisha kwenda Matamma na kuwazuia, lakini karibu na mwisho wa mapigano ambayo yalimalizikia ushindi, Yohannes aliuwawa kwa



**11.2** *Menelik, Mfalme wa Washoa, 1856 – 1859; Mfalme wa Ethiopia 1889 – 1935*

risasi iliyojiendea ovyo. Habari za kifo chake zilifanya jeshi lake likimbie. Palizuka hali ya kuchanganyikiwa kwingi Ethiopia ya kaskazini yote na hasa kwa vile nchi ilikuwa imekabiliwa na tauni ya ng'ombe pamoja na njaa iliyofuatwa na kuzagaa kwa ndui na kipindupindu. Katika kipindi hiki cha shida Wataliani walisonga mbele kwa haraka. Ilipofika mwisho wa mwaka 1889 walikwishajikalia sehemu ya nyanda za juu za kaskazini ambapo walianzisha koloni la Eritrea ikiwa na mji mkuu wa Asmara.

Wakati Mfalme Yohannes alipokuwa akichuana vikali na mashambulio ya Misri na Italia, Menelik, mtawala wa Shoa, ambaye kwa jina alikuwa chini ya Mfalme Yohannes, aliendeleza mahusiano ya kirafiki na Italia (taz. picha 11.1). Mawasiliano na Italia yalikuwa muhimu kwa Menelika kwa sababu yalimwezesha kupata madaktari na silaha kwa wingi kutoka kwa Wataliani. Kutokana na urafiki huu, na Menelik akiwa Mfalme wa Shoa (1865-1889), aliweza kujichukulia kwa nguvu majimbo yenye utajiri ya Arussi, Harar, Kulo na Kunta yaliyokuwa sehemu ya kusini na kusini-mashariki naGurage na Wallaga upande wa kusini-magharibi.

Urafiki huu ulifikia kilele tarehe 2 Mei, 1889 muda ambao ni chini ya miezi miwili baada ya kifo cha Mfalme Yohannes, kwa kutiwa sahihi Mkataba wa Amani na Urafiki kati ya Menelik na Italia katika kijiji cha Ethiopia cha Wuchale.

Mkataba wa Wuchale ambao ulikuwa ndio chanzo cha mahusiano kati ya nchi mbili hizi kubadilika, ulikuwa na sehemu ambazo zilileta faida kwa wote wawili. Katika mkataba huu Menelik aliyatambua mamlaka ya Italia juu ya sehemu kubwa ya Eritrea pamoja na Asmara, wakati Italia, kwa upande wake, ilimtambua Menelika kuwa ndiye Mfalme- hii ilikuwa mara ya mwanzo kutambuliwa hivyo - na kumuahidi kwamba anaweza kuagiza silaha na risasi kupitia ardhi ya Italia. Sehemu muhimu kabisa ya mkataba ilikuwa Kifungu cha XVII ambacho baada ya muda mfupi tu kilikuwa ndio msingi wa mivutano Ugomvi ulitokana na kule kuandikwa mkataba huo kwa lugha mbili, Kiamheri na Kitaliani, na tofauti muhimu iliyokuwepo kimaana kati ya namna kifungu hiki kilivyoandikwa katika lugha ya Kiamheri na ya Kitaliani. Mkataba ulioandikwa Kiamheri ulieleza kwamba Menelik angeweza kutumia huduma za wakuu wa kitaliani katika mawasiliano yoyote aliyotaka kufanya na Madola mengine; ule mkataba ulioandikwa kwa Kitaliani ulieleza kwamba kufanya hivyo ilikuwa ni lazima. Kutokana na kifungu hiki Wataliani waliitangaza Ethiopia kuwa himaya yao na jambo hili lilitambuliwa na madola ya Ulaya. Ili kutilia nguvu madai yao Wataliani waliukalia mji wa Adowa mwezi wa Januari, 1890 na baadaye wakamwarifu Ras Mangasha, mtoto wa Yohannes na mtawala wa jimbo la Tigre, kwamba hawataondoka mpaka Menelik aikubali tafsiri yao ya Mkataba wa Wuchale.

Menelik alikataa kukubali tafsiri hii na baada ya taahira ya miaka kadha, ambayo aliichukulia fursa kwa kuagiza silaha nyingi hasa kutoka Ufaransa na Urusi na kuyateka majimbo chungu nzima, yakiwemo kati yao majimbo ya Kaffa, Wolamo, Sidamo, Bale na kusini na kaskazini mwa Boran Galla, Menelik aliupinga kabisa mkataba wa Wuchale mwezi wa Februari, 1893. Tarehe 27 Februari, Menelik aliyaarifu madola ya Ulaya na alipozungumzia madai ya Italia aligusia tamko la Biblia na kutangaza kwamba 'Ethiopia haimhitaji yeyote, inanyoosha mikono yake kwa Mungu! Alisema haya huku yuko katika hali ya kuwa ana nguvu, kwani wakati huu alikuwa na bundaki 82,000 na mizinga ishirini

na nane.

Mapigano kati ya Wataliani na Waethiopia yalianza mwezi wa Desemba 1894 wakati Batha Hagos, chifu wa Kieritrea, alipoupinga utawala wa Kitaliani. Mapema Januari, 1895 Wataliani waliishambulia Ras Mangasha, huko Tigre na kuikalia sehemu kubwa ya jimbo hilo. Menelik alitoa amri kwamba jeshi lake lijizatiti kwa vita tarehe 17 Septemba na akaelekea kaskazini pamoja na jeshi kubwa ambalo lilipata ushindi mkubwa huko Amba Alegi tarehe 7 Desemba na Magale mwisho wa mwaka huo. Wataliani hapo tena waliangukia Adowa na baada ya kukaa kwa muda bila ya kufanya jambo lolote mapigano ya mwisho yalitokea.

Menelik alikuwa katika hali ya kuwa na nguvu zaidi kuliko Wataliani. Aliungwa mkono na wakazi wa Adowa ambao uzalendo wao ulishika kasi kutokana na kuporwa kwa ardhi ya Eritrea na Wataliani kwa madhumuni ya kuwaweka makaburu wa Kitaliani katika sehemu hiyo. Kwa hiyo wakazi wa Adowa walikuwa tayari kuyaonesha majeshi ya Menelik njia za kupita na pia kuwapa habari za harakati za adui. Kwa upande wao, Wataliani ilibidi wapambane na chuki za wakazi wa sehemu hizi na pia hawakuwa na ramani sahihi; kwa hivyo walijiendea ovyo katika nchi waliokuwa hawaielewi vyema. Pia jeshi la Menelik lilikuwa kubwa zaidi. Jeshi hilo lilikuwa na zaidi ya watu 100,000 wenye bundaki za kisasa; aidha kulikuwa na askari wengine waliokuwa na bunduki za kale na mikuki. Wavamizi wao walikuwa na watu 17,000 tu ambao kati yao 10,596 walikuwa ndio Wataliani, waliobaki wakiwa askari wa Kieritrea. Wataliani walikuwa na afadhali kwa upande wa mizinga lakini kwa vile hiyo mizinga yenyewe ilikuwa hamsini na sita tu, wakati Menelik alikuwa na arobaini, tofauti hii haikuweza kuwapatia ushindi.

Matokeo ya mapigano ya siku ile hapo Adowa yalikuwa ushindi mkubwa kwa Menelik, na kushindwa kabisa kwa adui zake. Katika vita hivi maafisa 216 wa Kitaliani na maafisa wa Kitaliani wasokuwa na vyeo vya juu pamoja na wanajeshi wao wa kawaida wakiwa 2,918 kwa jumla na askari 2000 wenyeji, wote hawa waliuawa. Mbali ya hawa kulikuwa na askari 954 wa Kitaliani waliopotea kabisa, na Wataliani 470 na askari wenyeji 958 walijeruhiwa. Jumla ya Wataliani waliojeruhiwa ilikuwa asilimia 40 ya jeshi lao lote ambalo lilishindwa kabisa na kupoteza mizinga yao yote, achilia mbali bunduki 11,000.

Tarehe 26 Oktoba, kutokana na kushinda kwa Menelik, Wataliani waliukubali Mkataba wa Amani wa Addis Ababa ambao uliufuta Mkataba wa Wuchale na waliutambua uhuru kamili wa Ethiopia.

Mapigano ya Adowa yalimpa Menelik heshima kubwa kimataifa. Wafaransa na Waingereza walipeleka wajumbe wa kidiplomasia kutia sahihi mikataba naye, na mabalozi wengine waliwasili kutoka kwa Wamahdi wa Sudan, kutoka kwa Sultani wa Utawala wa Uturuki na kutoka kwa Mfalme wa Urusi.

Matokeo ya vita hivi yalikuwa na umuhimu mkubwa katika historia ya mahusiano kati ya Ulaya na Afrika. Ethiopia walijipatia heshima katika eneo lote la Bahari ya Sham.

Wasomi wa Kimarekani wenye asili ya Kiafrika walionesha hamu kubwa ya kutaka kujua habari za Ethiopia, ambayo ilikuwa ndiyo nchi ya mwisho ya Kiafrika chini ya Sahara ambayo ni huru. Yule Mhaiti, Benito Sylvain, mmoja kati ya waanzilishi wa Umoja wa Afrika yote, aliizuru Ethiopia mara nne baina ya mwaka 1889 na 1906 huku

amechukua barua zilizokwenda na zilizotoka kwa Rais Alexis wa Haiti; na William H. Ellis, Mmarekani mweusi mwenye asili ya Cuba alizuru Ethiopia mara mbili baina ya 1903 na 1904 na alikuwa wa mipango kuhusu maendeleo ya uchumi na ya kuwapatia makazi Wamarekani weusi. Taathira za Ethiopia zilifika Afrika Kusini ambako miaka ya nyuma kidogo watu walivutiwa na ule utabiri wa Kibiblia uliosema Ethiopia ilinyoosha mkono wake mpaka kwa Mungu. Kanisa la Ethiopia lilianzishwa Afrika Kusini mwaka 1900. Kule kuzidi kutambuliwa kwa Ethiopia kulidhihirisha kilipotokeza, katika mwaka 1911, kitabu kiitwacho Ethiopia bila Minyororo, kilichoandikwa na msomi wa Gold Coast aliyeitwa J.E. Casely Hayford ambacho aliwatunukia 'Wana wa Ethiopia Duniani kote!

## *Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii na Kujiingiza kwa Wazungu katika Mambo ya Ndani ya Liberia na Uhabeshi 1880-1914*

### Liberia

Katika kipindi kinachozingatiwa Liberia na Ethiopia hazikukabiliwa tu na vitisho na uvamizi kutoka nje bali pia zilikumbwa na matatizo ya ndani ya kiuchumi na ya kijamii ambayo zilijaribu kuyatatua na kuweza kufikiria viwango mbali mbali vya fanaka. Yaliyokuwa magumu hasa ni yale matatizo ya ndani ya kiuchumi na kijamii yaliyoikabili Liberia katika kipindi hiki. Mnyang'anyiro na kugawanywa kwa Afrika kulilazimisha Serikali ya Liberia kwenda ndani zaidi katika sehemu za bara la Liberia ili kuvitia nguvuni vikundi vya mbari za kienyeji na kuanzisha utawala wa aina ya kikoloni huko. Kila sehemu ya utawala iliendeshwa kupitia wenyeji kwa kuwatumia machifu wakuu wa sehemu hizo ambao walishirikiana na kamishna wa eneo hilo aliyechaguliwa na serikali. Hadi kufikia mwaka 1914 wengi kati ya makamishna hao walikuwa ni Waliberia waliotoka Marekani au maafisa wa kienyeji wa jeshi waliokuwa wamepata elimu. Utawala huo kwa jumla ulikuwa wa kifisadi na wenye kuleta madhila. Wengi kati ya hao makamishna pamoja na wasaidizi wao na wanajeshi walikuwa wakilipwa pesa kidogo na pasi na mpango maalum, na walikuwa nadra kupitiwa na kuangaliwa na wakuu wa Monrovia, kwa hivyo waliyanyonya majimbo yao kwa kuwalazimisha wakazi kuwapa chakula, kuwafanyisha kazi katika mashamba yao ya kibinafsi na pia kwa kuwatoza faini na kodi kubwa sana.

Kwa hiyo haishangazi kwamba Waafrika wenyeji walipinga si tu kule kutamalikiwa kijeshi na kutekwa na mamlaka ya Serikali ya Liberia - kama Waafrika wa sehemu nyingine walivyopinga kutekwa na Wazungu - bali pia waliyapinga yale maovu ya kupindukia yaliyotendwa na utawala wa Liberia, Mpaka walipovunjwa kasi na wanamgambo wa Kiliberia, pamoja na Jeshi la mpakani la Liberia na pia manuwari za Kimarekani, watu wa Kru walifanya upinzani wa mara kwa mara hasa kuanzia mwaka 1915 mpaka 1916; wakazi wa Grebo walifanya upinzani mwaka 1910, watu wa Kisi mwaka 1913, wakazi wa Kpele na wa Bandi kuanzia mwaka 1911 mpaka 1914, Wagio na watu wa Mano kuanzia 1913 mpaka 1918, Wagbolbo Grebo kuanzia 1916 mpaka 1918, Wagola kuanzia na Wabandi kuanzia 1918 mpaka 1919, wa Joquelle Kpele kuanzia 1916



**11.3** *Walimu na wanafunzi wa Chuo cha Liberia, 1900*

mpaka 1920 na Wasikio katika mwaka 1921. Vita hivi vilivyoendelea kwa muda mrefu katika sehemu mbalimbali na gharama na uzembe wa 'utawala wa kienyeji' vilichochea kungiliwa na wageni katika mambo ya nchi na kuathiri vibaya mali, watu na mali nyenzo za serikali.

Mapato ya serikali siku zote yalikuwa si ya kuridhisha. Wengi kati ya Waliberia wa Kimarekani walipendelea shughuli za kibiashara kuliko kilimo, na walipata pigo kubwa kutokana na hali mbaya ya uchumi duniani iliyokuwepo mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Ilipofika 1890 wakazi wa Kijerumani, Wakiingereza na Wakidachi ndiyo waliokuwa wameitawala biashara ya nje. Bidhaa kubwa ya kusafirisha ya Liberia tangu 1860 ilikuwa kahawa. Lakini kwa sababu ya hali mbaya ya uchumi na vile vile mashindano yaliyokuwepo kwenye soko la dunia kati ya kahawa hii na ile ya Brazil iliyokuwa bora zaidi, bei ya kahawa ya Liberia ilianguka sana kuanzia mwaka 1898 na kuendelea. Yale matokeo ya kupungua kwa zao la kahawa la Liberia na kupungua kwa kiasi kilichoweza kusafirishwa, na kule kupungua kwa jumla kwa kima na thamani ya biashara ya nje, kulipunguza sana mapato ya serikali ambayo yalitokana na ushuru wa forodha na kodi nyingine kutokana na biashara na shughuli za upakiaji melini. Vile vile serikali ilikuwa haina njia za kuweza kukusanya mapato kutoka kwa wakazi wa Liberia ambao waligoma kulipa, na kutoka kwa wafanyabaishara wa kigeni; pia hawakuwa na mbinu za kukomesha magendo.

Ili isifilisike, serikali mara kwa mara ilikopa fedha nyingi kutoka kwa Waliberia na wafanyabiashara wa kigeni ili iweze 'kuendesha walau shughuli zake za kawaida kabisa'. Ilikopa $ 10,000 mwezi wa Novemba, 1896 kwa riba ya asili mia 9 kutoka kwa kampuni ya biashara ya Kijerumani, A. Woermann and Company ili iweze 'kukubali gharama za hivi sasa za kuendesha Serikali', na ilikopa $15,000 mwezi wa Februari, 1898 kutoka kwa kampuni ya Kidachi, Cost Afrikaanche Cie, kulipa gharama za Baraza la kutunga Sheria la Liberia; hii ni mifano michache tu. Pia Serikali ya Liberia ilikopa ,100,000 mwaka 1871, ,100,000 mwaka 1906 na $700,000 mwaka 1912 kutoka Serikali ya Uingereza na mabwana fedha wa Kizungu kwa masharti magumu. Ili kujilipizia madeni haya Waingereza walichukua wao uendeshaji wa shughuli za malipo ya forodha kuanzia mwaka 1896 na baada ya hapo walifuatiwa na mpango uliojulikana kwa jina la 'upokeaji wa Kimataifa' ambao ulianza mwaka 1912.

Kuanguka kwa biashara na kilimo Liberia pamoja na kupungua kwa misaada ya kigeni kuanzia mwisho wa karne ya kumi na tisa kuliifanya serikali ya Liberia iwanyonye Waliberia wenyeji kwa njia ya kuwafanyisha kazi badala ya kodi, kuwatoza kodi ya kichwa pamoja na malipo mengine na pia kuwafanya waitegemee serikali kuwapatia kazi. Mashindano ya kutaka kuzidhibiti kazi hizi za serikali yalizidi kati ya vyama vya siasa na yale makundi yaliyokuwa yakipigania maslahi fulani fulani kama vile kikundi kilichojulikana kama 'mababa waanzilishi', (yaani wale Waliberia waliotoka Marekani ambao walifanya maskani yao Liberia kabla ya Uhuru) na kile kilichojiita 'watoto wa nchi' (yaani Waliberia wa Kimarekani waliozaliwa Liberia).

Juu ya matatizo yote haya, kiwango fulani cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kilipatikana. Mwaka 1900 Serikali ya Liberia ilikifungua tena Chuo cha Liberia ambacho

kilikuwa kimefungwa tokea mwaka 1895 kwa uchache wa fedha na maendeleo.

Mwaka uliofuata mhandisi wa Kiliberia wa Kimarekani aitwae T.J.R. Faulkner alianzisha simu ya mwanzo ya Liberia iliyoiunganisha Monrovia na miji mingi ya jirani nchini Liberia. Mwaka 1900, kituo cha 'cable' huko Monrovia kilichojengwa na kampuni ya Kijerumani kilifunguliwa na kuweza kuiunganisha Liberia na nchi nyingine duniani. Mwaka 1906 mpaka 1907, kampuni ya Kiingereza iitwayo Liberian Development Company, ilijenga barabara nyingi za magari kuanzia Monrovia na kwenda ndani kwa kutumia sehemu fulani ya ule mkopo wa mwaka 1906. Kadhalika, kampuni nyingine za kigeni zilipata ruhusa kuendeleza shughuli za kugema mpira, kuchimba madini, na kadhalika, kutoka serikali ya Liberia.

## Ethiopia

Kama Liberia, Ethiopia ilikuwa na mabadiliko muhimu ya kiuchumi kuanzia miongo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa.

Menclik alikuwa na hamu ya kuifanya nchi yake ya kikale iwe katika hali ya kisiasa na alionesha hamu ya kuanzisha mambo mapya ya kila aina. Kwa hivyo, utawala wake ulishuhudia mambo mengi mapya yasiyopata kuwepo katika historia ya Ethiopia. Jambo la kwanza na moja katika mambo muhimu kabisa lilikuwa kuanzisha katika miaka ya kati ya 1880, mji mkuu wa Addis Ababa, jina hilo likiwa na maana sisisi ya 'Ua Jipya', ambao ilipofika mwaka 1910 ulikuwa na wakazi wa kiasi 100,000. Ujenzi wa madaraja ya kwanza ya kisasa pia ulifanyika katika kipindi hiki na ulipunguza shida ya mawasiliano iliyokuwepo nchini. Katika mwaka 1892 utaratibu wa ulipaji kodi uliundwa upya na malipo ya sehemu moja katika kumi ya mshahara yalianzishwa jeshini; mpango ambao ulikomesha mtindo wa tangu jadi wa wanajeshi kunyakua ngawira kutoka kwa wakulima. Mwaka 1894 sarafu ya mwanzo ya kitaifa ilitolewa, kama tangazo rasmi lilivyosema, ili nchi yetu izidi kuwa na heshima na biasharn yetu istawi'. Wakati huu huu mfumo wa posta ulikuwa ukitayarishwa. Stempu za posta ambazo ziliagizwa kama zile sarafu zilizoagizwa kutoka Ufaransa, zilianza kuuzwa mwaka 1845 na sheria ya kuanzisha vituo vya posta ilitolewa mwaka 1894. Washauri wa Kifaransa walitumiwa katika kuendeleza hnduma na Ethiopia iliingia katika Umoja wa Kimataifa wa Posta mwaka 1908. Haki ya kuanzisha njia ya reli kutoka Addis Ababa mpaka bandarini ya Djibouti ya Somalia ya Kifaransa ilitolewa mwaka 1894, lakini matatizo ya kifundi, kifedha na kisiasa yalikuwa makubwa sana hata yakafanya maendeleo yawe ya taratibu mno.Wakati huu nyaya mbili za telegrafu zilianzishwa katika kipindi cha mwisho cha karne ya kumi na tisa. Mapema katika karne ya ishirini barabara za mwanzo za kisasa zilijengwa baina ya Addis Ababa na Addis Alam na pia baina ya Harrar na Dire Dawa; hiyo ya kwanza ilijengwa na wahandisi wa kitaliani na ya pili ilijengwa na Wahandisi wa Kifaransa.

Miaka ya mwisho mwisho ya utawala huu ilishuhudia kuanzishwa kwa vyombo mbali mbali vya kisasa. Beuki ya Abyssinia ilianzishwa mwaka 1905 chini ya Beuki ya Taifa ya Misri iliyokuwa ikimilikiwa na Uingereza. Hoteli ya kwanza ya kisasa huko Addis Ababa, iliyokuwa ikiitwa Etege, ilianzishwa na Malkia Tayta mwaka 1907. Shule iliyoitwa

Menelik II ilianzishwa kwa msaada wa walimu wa Kikopti kutoka Misri mwaka 1908. Hospitali ya Menelik II, ambayo ilianzishwa ili ichukue mahala pa kituo cha Msalaba Mwekundu cha Kirusi kilichoanzishwa wakati wa vita vya Adowa, ilijengwa mwaka 1910, na mashine ya serikali ya kupigia chapa ilianzishwa mwaka 1911. Katika mwaka 1907, kudhoofika kwa afya yake, na kuongezeka kwa ugumu wa shughuli za kiserikali kulimfanya Menelik, kuanzisha baraza la Mawaziri la Ethiopia ambalo, kwa mujibu wa mwandishi wa historia Gabra Sellase, lilitokana na 'hamu ya kuanzisha mila za kizungu' aliyokuwa nayo Menelik. Kwa hivyo ilipofika mwisho wa utawala wa Menelik, Ethiopia ilikwishawekwa katika misingi ya maendeleo ya kisasa.

## *Matokeo ya mnyang'anyiro na kugawanywa kwa bara la Afrika kwa upande wa Liberia na Ethiopia*

Mnyang'anyiro wa Afrika na kugawanywa kwake kulikofanywa na Wazungu vilikuwa na taathira za kuvutia lakini zilizotofautiana juu ya Liberia na Ethiopia. Kwanza, nchi mbili hizi zilikuwa ndizo nchi pekee katika bara zima la Afrika zilizosalimika na hujuma za kibeberu na kuweza kubakia na uhuru wao. Lakini kama ilivyoonyeshwa hapo juu, Ethiopia siyo kuwa ilisalimika tu lakini iliweza pia kupanua mipaka yake ya upande wa kusini na mashariki; katika kipindi hiki hiki, Liberia ilipoteza sehemu kubwa ya ardhi yake ambayo ilichukuliwa na Uingereza na Ufaransa. Swala la kuzingatia ni, kwa nini nchi hizi zote mbili ziliweza kunusurika wakati moja ikapoteza ardhi na moja ikajipatia ardhi zaidi.

Ethiopia na Liberia zilinusurika kwa sababu kadha, na sababu moja kubwa ni ile imani thabiti waliokuwa nayo watu wa nchi zote hizi mbili kwamba, wamejaaliwa na Mungu wanusurike, imani ambayo iliipa nguvu kubwa ile azma yao ya kupinga juhudi zote za Wazungu kutaka kuzivamia na kujipenyeza katika nchi hizi mbili. Kufanyishwa kazi kitumwa walipokuwa Marekani kulipandikiza katika hisia za wananchi wa Liberia imani thabiti kwamba Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kudhibiti na kuendesha majaaliwa ya Taifa. Maraisi wengi wa Liberia walikuwa pia wahubiri wa dini. Kwa kweli wananchi wa Liberia waliamini siku zote kwamba kuna mkono wa Mungu katika kila tokeo muhimu katika historia yao. Imani hii ndiyo msingi wa yale maneno yanayokaririwa mara kwa mara ya Mfalme Menelik wa Ethiopia aliyoyatamka mwaka 1893 kwamba, Ethiopia haimhitaji mtu yeyote; inanyoosha mkono wake kwa Mungu. Hapana shaka kwamba imani hii madhubuti ya watu wa nchi hizi iliwajaza hamasa ambazo zinatusaidia kufahamu vipi walifaulu kuzishinda hujuma za Wazungu.

Sababu ya pili muhimu iliyoziwezesha nchi zote mbili kusalimika ilikuwa ya kidiplomasia. Kwa upande mmoja Ethiopia na Liberia ziliweza kugonganisha dola moja ya Kizungu na ya pili na waliweza kuzipinga kwa njia za kidiplomasia juhudi za mlango wa nyuma walizozitumia wakoloni. Menelik kwa hakika aliweza kuwagonganisha vichwa Wataliani, Wafaransa na Waingereza.

Liberia pia mara kwa mara ilimgonganisha Mfaransa na Mwingereza na

Mwingereza na Mjerumani, na pia haikuchelea kumleta Mmarekani kuja kupiga kelele zake za vitisho ili kuyakimbiza madola haya.

Kwa upande mwingine hapana shaka kwamba kusudio la madola ya kibeberu kuzuia dola yoyote kati yao kuwa na mamlaka pekee juu ya mojawapo kati ya nchi mbili hizi lilikuwa moja katika mambo yaliyosaidia kuzinusuru nchi hizi. Kwa sababu za kiuchumi, Ujerumani, Ufaransa na Uingereza zilikuwa tayari kuona yeyote kati yao akiitawala Liberia pekee; wakati huo huo, kwa sababu za kihisia, Marekani iliazimia kuhakikisha kwamba Liberia inabaki kama ilivyo. Kwa hivyo wakati mwingine Marekani ilipeleka manuwari zake ndogo kuilinda bahari ya Liberia ili kuviza tamaa za Ufaransa na Uingereza za kutaka kuigawa mapande nchi hii, ati kwa kisingizio kuwa haiwezi kuilinda mipaka yake. Mara nyingine Marekani ilitumia njia za kidiplomasia kuwapa onyo juu ya hukumu ambayo historia itaitoa pindi mmoja wao akijaribu kuuvuruga uhuru wa Liberia. Kwa hivyo katika mwaka 1879 na 1898 Marekani iliizionya Ufaransa na Ujerumani zisiinyakue Liberia au kuigeuza mahamia. Vile vile kwa sababu za kivita, Uingereza, Ufaransa, na Italia hazikuwa tayari kuiona dola yoyote kati yao ikiitawala Ethiopia.

Lakini kwa upande wa Ethiopia kuna jambo moja muhimu na la aina ya pekee ambalo lazima litajwe wakati inapoelezewa vipi Ethiopia iliweza kusalimika, jambo ambalo pia linafahamisha vipi Ethiopia iliweza kupanua mipaka yake katika kipindi kinachozingatiwa; jambo lenyewe ni zile nguvu zake za kijeshi. Pindi Menelik angelishindwa katika vita vya Adowa, bila ya shaka Ethiopia ingelikuwa koloni la Italia mwaka 1896. Lakini kama ilivyoonyeshwa hapo juu, nguvu za Ethiopia za kijeshi, ambazo zilizizidi nguvu za kijeshi za Italia zilizokuwepo Afrika ziliiwezesha siyo tu kushinda katika vita vya Adowa, bali ziliiwezesha pia kupanua mipaka yake katika mwaka 1880 na mwaka 1890.

Lakini ikiwa Liberia na Ethiopia zilisalimika, Liberia ilisalimika huku imeharibiwa na kudhoofishwa na haya ni matokeo ya udhaifu wake wa kijeshi na ile hali isiyoridhisha kabisa iliyokuwa ndani ya nchi. Jeshi la wanamaji la Liberia, siku zote lilikuwa na manuwari ndogo moja au mbili tu. Jeshi lake lilikuwa la mgambo la Waliberia wa Kimarekani hadi mwaka 1908 jeshi la Mpakani la Liberia lilipoundwa kulipa mwega. Mpaka mwaka 1914 idadi ya hao askari wa mgambo ilikuwa chini ya watu 2,000 kwa mwaka mmoja wowote na kwa jumla ya askari hawa walikuwa hawakupata mafunzo sawa sawa, hawalipwi vilivyo na hawana vifaa vya kuridhisha. Jeshi hilo halikuwa na usafiri wa haraka wakuweza kuwapeleka sehemu za mapigano. Katika mwezi wa Desemba, 1913 Jeshi la Mpakani la Liberia, ambalo halikuwa na uhodari wowote kama lilivyokuwa jeshi lao la mgambo, lilikuwa na maafisa watatu wa Kimarekani na saba Wakiliberia na zaidi ya watu 600 walioandikishwa ambao waliwekwa kwenye vikosi zaidi ya kumi na mbili vilivyokuwa sehemu za bara za nchi hiyo. Mpaka mwaka 1914 afisa aliyekuwa dhamana wa kila kikosi alifanya kazi za kijeshi na pia za utawala katika eneo lake. Kwa hivyo afisa huyo alipokea amri kutoka Idara ya Vita na Idara ya Mambo ya Ndani; pia aliripoti kwa idara zote mbili hizo (na hakuna idara hata moja kati ya hizo mbili iliyoratibu shughuli zake na za mwenziwe). Udhaifu wa kijeshi wa Liberia ambao ulikuwa tofauti kabisa na nguvu za kijeshi za Ethiopia unaweka wazi sababu za Liberia kushindwa kuihami ardhi yake

kutokana na kujiingiza kwa Wazungu wakati wa Mnyang'anyiro.

Hali ya ndani pia haikuridhisha. Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, na kwa sababu zilizokwishatajwa, Serikali ya Liberia maisha ilikuwa karibu na kufilisika, na ilidaiwa madeni makubwa sana na wageni na wananchi. Ilipofika Januari, 1908, deni la Liberia kwa Uingereza, kwa mujibu wa Balozi Mkuu wa Kiingereza aliyekuwa Monrovia, lilikuwa ,60,000 kila mwaka 'kwa miaka chungu nzima' na ilipofikia Septemba, 1905, deni lake kwa wafanyabiashara wa Kijerumani waliokuwa Liberia lilikuwa $120,000. Kudaiwa huku kuliyawezesha madola ya kibeberu mara kwa mara kuingilia mambo ya ndani ya Liberia katika kipindi kinachozingatiwa kwa kima ambacho mabeberu hao hawakupata kufanya huko Ethiopia ambako hawakupata kupewa sababu au kisingizio cha kufanya hivyo. Muda wote wa miaka 30 ya mwisho ya karne ya kumi na tisa, madola ya kibeberu yalipeleka mjumbe baada ya mjumbe huko Liberia kutoa msaada wa kuwalipia madeni yake kama Liberia ilikubali kujiweka chini ya himaya ya madola hayo, kama Ufaransa ilivyofanya mwaka 1879. Ujerumani mwaka 1887 na Hispania mwaka 1886; na kila moja kati ya hawa ilijitolea kusimamia shughuli za Liberia za kifedha na kutayarisha shughuli zake za ulinzi. Wakati huo huo mabalozi wa wakilishi kwa madola hayo waliokuwa nchini waliwatazama kwa bezo wananchi wa Liberia na mara kwa mara wageni hao walizishutumu sheria za baishara za Liberia, zile za forodha na zile za uraia; aidha waliitia shindo serikali walipotaka isawazishe malamiko ya raia wa nchi zao kama ilivyofanya Uingereza mwezi wa Septemba mwaka 1869, Agosti, 1870 Aprili, 1871 Februari na Juni 1882, Novemba 1886 na mwisho Januari 1909. Ujerumani vile vile ilileta manuwari zake ndogo kuitishia Liberia mwezi wa Februari na Oktoba, 1881 na Agosti 1897 Januari na Septemba 1898 na Desemba 1912.

Kuingilia huku kwa Wazungu katika mambo ya Liberia kulileta taathira iliyofika mbali upande wa siasa na jamii ya Liberia. Kwanza iliwagawa Waliberia katika kikundi kilichowapendelea Waingereza na kikundi kilichowapendelea Wamarekani, na vikundi hivi vilitayarisha maandamano makubwa, upande mmoja ukiunga mkono maandamano ya Barclay yaliyofanyika Monrovia na upande mwingine ukiwa dhidi ya Barclay; maandamano haya yalifanyika mwezi wa Januari 1909. Vile vile kule kuajiriwa kwa Wazungu kwa mishahara mikubwa ili waweze kuleta mabadiliko waliyotakiwa na madola ya kigeni kulikuwa mzigo mkubwa kwa Serikali ya Liberia ambayo tangu hapo pato lake lilikuwa dogo. Ingelikuwa si kule kujiingiza kati kwa Marekani, lazima zitambuliwe juhudi za Waziri Mkazi wa Marekani aliyekuwa Monrovia, Ernest Lyon, Mmarekani mwenye asili ya Kiafrika aliyeunga mkono kabisa harau ya Liberia na viongozi wake ya kutaka msaada wa Marekani kuanzia mwaka 1909 na kuendelea, basi bila ya shaka yoyote Liberia ingeliangukia mikononi mwa madola ya kibeberu.

Ethiopia haikuwahi kuingiliwa kwa mfululizo na madola ya kibeberu ya Ulaya katika mambo yake ya ndani. Kinyume ya haya, ila kwa sababu ya ushindi wa Adowa, Ethiopia ilipewa kila heshima na ilikubaliwa katika mkusanyiko wa madola karibu kama ni mmoja kati yao. Katika kile kipindi ambacho Liberia ilikuwa takriban imezungukwa na madola ya kibeberu, tukizingatia udhaifu wa Liberia kwa upande wa kijeshi, na zaidi ule mtafaruku uliokuwa ndani ya nchi uliosababishwa kwa kiasi fulani na kudhoofika kwa

wenyewe kiuchumi, na vile vile kule kuingiliwa na Wazungu katika mambo yake ya ndani. Jambo la kushangaza siyo kwamba Liberia iliweza kunusurika ingawa huku inaugua na imedhoofu, bali kuwa vipi imeweza alau huko kubakia hata katika hali hiyo.

# 12

## *Vita vya Kwanda vya Dunia na Matokeo yake*


Ilikuwa katika mwongo wa mwisho wa kuimarisha ukoloni katika Afrika Vita vya Kwanza vya Dunia vilipoanza. Kimsingi, vita hivi vilikuwa ni ugomvi kati ya madola ya Ulaya, lakini viliikumba Afrika moja, kwa moja na pia kwa namna isiyo dhahiri, kwa sababu ylipoanza mapigano sehemu kubwa ya Afrika ilikuwa imetawaliwa na hayo madola yaliyokuwa yakipigana. Habari nyingi zimeandikwa kuhusu mapigano ya Wazungu yaliyotokea Afrika wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia na matokeo yake ya kugawanywa kwa ardhi iliyokuwa chini ya Wajerumani kwa dola zilizoungana ambazo ndizo zilizokuwa zimepata ushindi; hii ilikuwa sura ya mwisho katika mnyang'anyiro wa Afrika. Hakuna habari nyingi zilizoandikwa kuhusu taathira ya vita hivi juu ya Waafrika na juu ya miundo ya utawala ambayo ilianzishwa na Wazungu hivi karibuni na kulazimishwa kutumiwa kwa Waafrika ambao wao waliwatamalki. Hizo ndizo mada ambazo sura hii itahusika nazo hasa. Lakini ni muhimu kutoa maelezo mafupi juu ya vita vilivyopiganwa ikiwa tunataka kuielewa vilivyo taathira ya vita hivi juu ya Afrika.

### *Vita hivi katika Adhri ya Afrika*

Athari ya kwanza kwa Afrika iliyotokana na kutangazwa kwa vita huko Ulaya ni kuvamiwa kwa makoloni ya Ujerumani na Madola yaliyoungana.

Mapigano yaliyofanyika Afrika yanaweza kugawanywa katika awamu mbili tofauti. Katika awamu ya kwanza ambayo ilichukuwa wiki chache tu Madola yaliyoungana yalijishughulisha na kutaka kuuviza uwezo wa Ujerumani wa kuvamia nchi nyingine na kuhakikisha kwamba vikosi vyake vya manuwari havitaweza kuzitumia bandari zake za Afrika. Kwa hivyo bandari za Lome huko Togo, Duala, Cameroon, Lederitz Bay na Swakompmund huko Afrika ya Kusini-Magharibi zilikaliwa mara tu baada ya vita kuanza. Katika sehemu za Afrika Mashariki zilizokuwa chini ya Ujerumani manuwari za Uingereza ziliivamia Dar es Salaam na Tanga katika mwezi wa Agosti, na ingawa hakuna hata bandari moja kati ya hizi mbili ambayo ilichukuliwa baadaye katika vita, bandari hizo hazikuweza kutumiwa na manuwari za Kijerumani. Huko Misri, Mturuki alipojiigiza vitani upande wa Mjerumani ulinzi wa Kiingereza kwenye Mfereji wa Suez uliongezwa na jeshi la Uturuki lililokwenda huko kufanya mashambulizi lilishindwa na kurejeshwa nyuma mwezi Februari, 1915.

Kampeni za awamu ya kwanza ya vita zilizotokea katika Afrika zilikuwa muhimu sana katika mkakati wa kijumla. Kampeni za awamu ya pili zilikusudiwa ziyateke makoloni ya Kijerumani yaliyokuwa Afrika, kwanza kwa madhumuni ya kuyazuia



12.1 *Kampeni ya Kidachi ya Afrika Mashariki: wanajeshi wa kikosi cha Waingereza wakiteremka huko Lindi, Desemba, 1917*

yasitumike kama vituo vya kuyapindua mamlaka ya madola yaliyoungana juu ya makoloni yao wenyewe, mamlaka ambayo mara nyingi yalikuwa dhaifu; na pili, kwa madhumuni ya madola yaliyoungana kugawana miongoni mwao makoloni hayo ya Kijerumani pindi ukipatikana ushindi wa Muungano wa jumla. Kwa hivyo sehemu za Wajerumani huko Afrika Kusini-magharibi zilitekwa katika kipindi cha miezi sita lakini mapigano huko Cameroon yalichukua muda mrefu ambao ulipindukia miezi kumi na tano. Mapigano yaliyoendelea Afrika Mashariki yalichukua muda mrefu zaidi. Von Lettow-Vorbeck akiwa anajua kwamba hapakuwa na uwezekano wa kuyashinda majeshi ya maadui ambayo yaliyazidi majeshi yake zaidi ya mara kumi, alidhamiria kuyaviza majeshi hayo alau kwa kutumia mbinu za vita vya msituni. Mpaka mwisho wa mapigano bado alikuwa hajashindwa na alikuwa bado akiongoza vikosi vyake vilivyokuwa taabani kwa kupitia sehemu za Mreno za Afrika Mashariki na kwenda navyo mpaka Rhodesia kusini ambako alipata taarifa ya mkataba wa makubaliano ya kuacha vita uliofanyika Ulaya.

## *Kuhama kwa Idadi Kubwa ya Wazungu*

Vita vilishuhudia kuhama kwa idadi kubwa sana kwa Wazungu waliokuwa wakifanya kazi sehemu za utawala na za biashara, yaani kuhama kutoka makoloni ya Madola yaliyoungana yaliyokuwa Afrika na kuelekea eneo la vita la magharibi au kwenda kujiandikisha katika vikosi vilivyokuwa na vituo hapo hapo mitaani ili kwenda kupigana katika sehemu nyingine za Afrika. Katika baadhi ya sehemu idadi ya Wazungu ambayo tangu hapo ilikuwa ndogo sasa ilipungua kwa zaidi ya nusu. Sehemu nyingine huko Nigeria ya kaskazini kama vile Borgu, kwa muda mrefu wakati vita vinaendelea zilikuwa hazina hata afisa mmoja wa Kizungu. Huko Rhodesia ya kaskazini idadi inayofikilia asilimia arobaini ya watu wazima wa Kizungu ilikuwa iko vitani. Katika sehemu ya Afrika iliyoko chini ya Sahara ambayo ilitawaliwa na Mfaransa kwa jumla, Wazungu wote wenye umri wa kuweza kupigana walitayarishwa kwa vita na katika Afrika Mashariki iliyokuwa chini ya Mwingereza Wazungu waliandikishwa kwa kazi za vita. Kwenye baadhi ya sehemu, hasa sehemu za mashambani, kulizuka uvumi kwamba Wazungu walikuwa wanahama kabisa.

Matokeo ya kuhama huku yalikuwa kuzorota, kama si kusimama kabisa, kwa huduma nyingi za lazima ambazo zilikuwa zikiendeshwa na Wazungu. Katika baadhi ya kazi ilibidi Waafrika wapate mafunzo maalum, kama ilivyokuwa Senegal, ili waweze kujaza nafasi tupu zilizozurika. Katika sehemu ya Afrika Magharibi ya Waingereza, kazi nyingine ambazo mpaka wakati huo zilikuwa zimewekwa kwa ajili ya Wazungu tu, sasa zilikuwa zinafanywa na Waafrika, jambo ambalo kama Richard Hathbone alivyoonyesha, linasaidia kuelezea utiifu ambao Waafrika waliosoma waliuonyesha wakati wa vita. Misri tu ndiko kulikokuwa na kuongezeka halisi kwa idadi ya Wazungu, kwa sababu kulimiminika majeshi ya Kiingereza yaliyokuwa yakiitumia Misri kama ni kituo cha madola yaliyoungana cha kuishambulia Mashariki ya Kati.

Kwa upande wa Waafrika jambo la kushangaza zaidi kuliko kule kuhama kwa Wazungu kwa wingi, ni kule kuonekana kwa Wazungu wakipigana wenyewe kwa

wenyewe, kitendo ambacho hawakupata kukifanya walipokuwa wameikalia Afrika. Zaidi ya haya, Wazungu walifika hata kuwashajiisha raia wao waliovaa sare ya vita kuwaua 'maadui' wa Kizungu ambao mpaka wakati ule walikuwa katika mbari ambayo, kwa sababu ya rangi yake, ilifanywa kama ni mbari takatifu na kuuvunja utakatifu huo kulimfanya mhalifu apate adhabu kali.

## *Kushirikishwa kwa Waafrika katika Vita*

Isipokuwa tu katika mapigano yaliyokuweko katika sehemu za Mjerumani za Afrika Kusini-Magharibi, Afrika ilitoa mchango mkubwa katika ushindi iliopatikana na madola yaliyoungana katika mapigano yaliyofanyika sehemu za Afrika. Majeshi ya Kiafrika yalitakiwa wakati wa vita siyo tu kupigana katika ardhi ya Afrika lakini pia kuyapa mwanga majeshi ya Kizungu katika sehemu za mapigano zilizokuwa upande wa Magharibi na Mashariki ya kati. Vile vile walisaidia katika kukomesha vitendo mbalimbali vya uhalifu vilivyotendeka dhidi ya utawala wa kikoloni kama walivyosaidia katika kutamalakiwa kwa Afrika na Wazungu.

Zaidi ya majeshi milioni moja yaliandikishwa wakati wa vita kuongeza idadi ya majeshi yaliyowekwa na watawala wa kikoloni ambayo kwa kawaida yalikuwa madogo. Mbali ya majeshi waliandikishwa wachukuzi kwa wingi sana-wakihitajika wachukuzi watatu kwa kila askari mmoja anayepigana vitani. Zaidi ya hivyo Waafrika wa kaskazini waliandikishwa kwenda kufanya kazi katika sehemu za viwandani zilizoachwa tupu na Wafaransa waliochukuliwa jeshini. Kuhamia kwa hiari kwa wafanyakazi wa Kialgeria huko Ufaransa kulianza wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia. Kwa jumla, zaidi ya Waafrika 2.5 millioni, au ziaidi ya asili mia moja ya watu wote wa Bara la Afrika, walihusishwa katika namna fulani ya kazi za vita. Watu walioandikishwa kwa sababu ya kupigana au kwa shughuli za uchukuzi walipatikana kwa njia tatu. Njia ya kwanza ni ya kujitolea; Waafrika walijitolea kwa hiari yao bila ya kulazimishwa. Ndiyo maana mapema katika vita vya sehemu za mapigano za Palestina na Syria idadi kubwa ya wakulima maskini walitoa huduma zao kwa malipo ambayo yakilinganishwa na hali zao yalikuwa ya kuvutia.

Njia ya pili ilikuwa uandikishaji uliofanyika kwa kupitia kwa machifu ambao walitarajiwa kutoa idadi fulani ya watu kama ilivyotakiwa na maafisa wa kisiasa. Katika baadhi ya sehemu hapakuwa na taabu ya kuwapata watu ambao walijitolea ki kweli kweli; katika sehemu nyingine watu walichukuliwa kwa nguvu na machifu na halafu walipelekwa kama watu waliojitolea wenyewe.

Njia ya tatu na ambayo ndiyo iliyotumika sana ilikuwa kuandikisha watu kwa lazima. Katika sehemu za Afrika chini ya Sahara zilizokuwa chini ya Mfaransa, Sheria ya mwaka 1922, iliyokuwa na lengo la kuanzisha jeshi la kudumu la Kiafrika, iliwataka wanaume wote wa Kiafrika wenye umri baina ya miaka 20 na 28 watoe kwa lazima huduma za kijeshi kwa muda wa miaka minne. Baada ya vita kuanza, wakati Afrika Magharibi peke yake ilikuwa na askari 14,785 wa Kiafrika, iliamuliwa kuandikisha askari 50,000 zaidi wakati wa kampeni ya kuandikisha askari ya mwaka 1915 mpaka 1916.

Machifu walipewa idadi fulani ya watu kuijaza na waliwakamata wageni na wale waliokuwa watumwa zamani ili kukwepa kuwaandikisha jamaa zao au watu waliowategemea machifu hao. Wakati ilipokuwa ikihaha kutafuta watu zaidi pamoja na kuwa na matumaini kwamba Mwafrika mwenye sifa bora huenda akafuzu pale Wafaransa waliposhindwa, serikali ya Kifaransa ilimchagua Blaise Diagne katika mwaka 1918 awe Balozi mwenye dhamana ya kuandikisha askari wa Kiafrika. Wakati lengo walilopewa lilikuwa kuandikisha watu 40,000, vikundi vya Blaise Diagne viliandikisha watu 63,378. Lakini wachache tu kati ya wote hawa ndio walioiona sehemu ya mapigano kwa sababu vita vilimalizika mwezi wa Novemba, 1918.

Uandikishaji watu kwa lazima pia ulitumika ili kuweza kupata askari na wachukuzi katika sehemu ya Afrika Mashariki iliyokuwa chini ya Uingereza kama ilivyotakikana kwa mujibu wa amri ya mwaka 1915, kuhusu huduma za lazima, ambayo iliwataka wanaume wote wenye umri kati ya miaka 18 na 45 watoe huduma za kijeshi. Sheria hii ilianzishwa katika mahamia ya Uganda mwezi Aprili mwaka 1917. Kuandikishwa wachukuzi kwa lazima huko Rhodesia ya Kaskazini kulimaanisha kwamba katika sehemu kubwa ya vita zaidi ya theluthi ya watu wazima wa eneo hili walikuwemo katika utoaji wa huduma za uchukuzi. Katika Ageria, Tunis na hata Moroko ambayo ilikuwa bado imetekwa, raia wa kikoloni walilazimishwa kwenda vitani. Inakisiwa kwamba zaidi ya askari 483,000 wa kikoloni kutoka Afrika nzima walifanya kazi katika jeshi la Kifaransa wakati wa vita, wengi kati yao wakiwa wameandikishwa kwa nguvu. Wabelgiji, huko Kongo waliwaandikisha kwa nguvu wachukuzi hadi kufikia idadi ya 260,000 wakati wa mapigano ya Afrika Mashariki.

Wakati vita vilisababisha watu wengi kufa na kujeruhiwa katika Afrika, pia vilisababisha kwa namna isiyo ya moja kwa moja, vifo vingi kutokana na kuenea bara zima la Afrika katika mwaka 1918-1919 maradhi ya influenza ambayo yalisababishwa na wanajeshi na wachukuzi kwaliokuwa wakipita huku na huko wakati wa kurudi nyumbani.

## *Changamoto ya Waafrika kwa Utawala wa Kizungu*

Wakati wa vita ulishuhudia kuenea kwa uasi na harakati za kupinga mamlaka ya utawala wa kikoloni katika sehemu kubwa ya Afrika - sehemu ya Afrika Magharibi iliyokuwa chini ya Ufaransa, Libya, sehemu za Afrika Mashariki zilizokuwa chini ya Mreno na Mjerumani na sehemu ya Afrika Magharibi iliyotawaliwa na Mwingereza. Maswala kadhaa yanajidhihirisha katika uasi uliotokea wakati wa vita: kwa vile ile hamu ya kutaka kujinyakulia uhuru uliotoweka, chuki juu ya hatua zilizochukuliwa wakati wa vita hasa aandikishaji wa askari kwa mabavu, kufanyishwa kazi kwa nguvu, kuvipinga vita kwa sababu za kidini, hasa upande wa Umoja wa Waislamu, shida za kiuchumi zilizosababishwa na vita na kutoridhishwa na mambo fulani katika mfumo wa kikoloni ambayo taathira zake katika sehemu nyingi zilisadifia kuchomoza katika miaka ya vita. Kuna swala la mwisho ambalo ni muhimu, hasa katika Afrika Kusini nalo ni kuweko kwa mapenzi ya Ujerumani miongozi mwa raia wa madola yaliyoungana.

Hamu ya kutaka kujinyakulia uhuru inadhihirisha kwa uwazi katika uasi wa Borgawa na Chori-Ije huko Dahomey ya Ufaransa uliofanywa na vikundi mbali mbali vya Kiigbo katika jimbo la Owerri, Nigeria na katika uasi mwingi uliotokea Afrika Magharibi dhidi ya mamlaka ya Ufaransa. Huko Misri, ghasia za Wafd zilizotokea mara tu baada ya vita zilihamasishwa sana na hamu ya kuitupilia mbali himaya ya Kiingereza ambayo karibuni tu walisambikwa nayo. Katika Malagasi, Wamalagasi mia tano, wengi wao wakiwa wasomi, walikamatwa mwishoni mwa mwaka 1915 na kutuhumiwa 'kuanzisha chama cha siri kilichoundwa madhubuti kwa lengo la kuwafukuza Wafaransa na kurejesha serikali ya Wamalagasi.

Mawazo ya kidini, hasa ya Umoja wa Waislamu yalikuwa ndio msingi wa baadhi ya uasi. Harakati za udugu wa Sanusi huko Libya, ambao bado ulikuwa unapinga kuweko kwa Wataliani katika nchi yao na kuvamia kwa umoja huo kwa sehemu ya mashariki ya Misri mwezi wa Novemba, 1915, kwa kiasi fulani, kulikuwa kama ndio jawabu ya wito wa Uturuki wa kupigana *Jihadi.* Ingawa walirejeshwa nyuma nchini Libya wanachama wa umoja huo pamoja na Walibya wengine waliwashinda kabisa Wataliani katika vita vya al-Karadabiyya, na kulikuwa kushindwa kubaya kabisa kwa Wataliani tangu vile vita vya Adowa, mwaka 1896. Kisha waliwafukuza Wataliani ambao walilazimika kupeleka sehemu kubwa ya jeshi lao katika sehemu za pwani: ambako kulikuwa na majeshi ya Austria. Kwa hivyo hadi kufikia mwaka 1917 Italia ilikaribia kabisa kuipoteza Libya. Ushindi huu ulisababisha kuanzishwa kwa Jamhuri ya Tripolitania (al-Djumhuriyya el-Tarabulsiyya) tarehe 16 Novemba mwaka 1918 katika Libya Magharibi na utawala wa Cyrenaica katika Libya ya Mashariki. Italia ilizitambua nchi hizi mwaka 1919 na ikalipa kila moja bunge lake. Chini ya Mkataba wa al-Radjma mwaka 1920, Italia ilizipa nchi haki zaidi. Mwezi wa Januari, 1922 nchi hizi mbili zilikubali kuunda umoja wa kisiasa na zilimchagua Idris al-Sanusi, Kiongozi wa Sanusiyya, kuwa mkubwa wa muungano huo na zikaunda kamati kuu iliyokuwa na makao makuu yake huko Gharyan.

Uasi wa Libya uliathiri matukio katika kusini mwa Tunisia, ambako askari 15,000 Wakifaransa walihitajika kuviza uasi uliotokea huko na pia uliotokea miongoni mwa Watawarik na Islam wengine wa Niger ya Ufaransa na Chad ambako chuki za Kiislam juu ya utawala wa kikafiri, ukame wa mwaka 1914 na kuandikishwa watu jeshini kwa kasi viliwafanya watu wawe katika hali ya kutoridhika kabisa. Mwezi Desemba 1916 majeshi ya Sanusi yalivamia Niger, ambako waliungwa mkono na Kaossen, Kiongozi wa Kel-Air Tawarik, Firhun, Mkuu wa Oullimiden Tawarik na Sultani wa Agades. Waliiteka Agades na ikawa lazima kuunda jeshi la ujima la Wafaransa na Waingereza ili kuweza kuwashinda.

Si uasi wa Kiislamu tu uliokuwa tishio kwa madola ya Muungano katika koloni zao. Uasi wa John Chilembwe huko Nyasaland (sasa Malawi) wa Januari, 1915 ulikuwa na hisia za ndani za Kikristo na harakati za kikundi cha Watchtower cha kitawala huko Rhodesia zilihubiri kwamba dunia ilikaribia kwisha na zilihimiza watu waache kuyatii mamlaka yaliyoandwa. Kikundi hiki ilitumia kama sababu zile ghasia zilizosababishwa na Von Lettow Vorbeck huko Rhodesia ya Kaskazini mwisho wa vita. Pia kulikuwa na harakati zilizotabiri shari ambazo zilisambaa sehemu kubwa ya eneo la ufukwe wa Niger

zikiongozwa na Garric Braide, ambaye pia akiitwa Elija wa Kwanza, aliyetabiri kwamba utawala wa Kiingereza ulikuwa unakaribia mwisho wake. Huko Ivory Coast Mtume Harris alihamishwa mwezi Desemba, 1914 kwa sababu 'matokeo huko Ulaya yanahitajia sasa zaidi kuliko hapo zamani kuweko kwa hali ya utulivu miongoni mwa watu wa koloni hilo....! Huko Nyanza, Kenya madhehebu ya Mumbo umbayo yalikua kwa haraka sana katika miaka ya vita yaliikataa dini ya Kikristo na kutangaza kwamba 'Wazungu wote ni adui zenu' lakini wakati karibu unakuja ambao watatoweka katika nchi yetu!

Labda sababu muhimu kabisa ya uasi ilikuwa kule kuandikishwa watu uaskari na uchukuzi kwa mabavu. Chuki juu ya kuandikishwa huku kwa nguvu zilikuwa kubwa hata kufika kuupa hamasa kubwa uasi wote uliotokea katika makoloni ya Kifaransa yaliyokuwa sehemu ya Afrika chini ya Sahara na kuamsha upinzani katika koloni la Gold Coast ambalo kawaida lilikuwa katika hali ya amani. Uasi wa John Chilembwe ulisababishwa na kuandikishwa kwa Wanyasa jeshini na kufa kwao kwa wingi katika wiki za mwanzo za vita na Mjerumani.

Shida za kiuchumi zilizosababishwa na vita bila ya shaka zilikuwa nyuma ya upinzani dhidi ya watawala wa kikoloni na hata ziliuchochea upinzani huo. Uasi uliotokea magharibi ya kati ya Nigeria na katika sehemu za ufukwe wa Niger mapema katika vita hauwezi kueleweka isipokuwa kwa mnasaba wa bei za mazao ya miti ya mawese na kuanguka kwa biashara kulikosababishwa na kutolewa kwa Wajerumani katika biashara wakati wao ndio waliokuwa wateja wakubwa.

Katika Afrika Kusini uasi wa Waafrika mwisho wa mwaka 1914 dhidi ya uamuzi wa serikali wa kuyaunga mkono Madola yalioungana uliosababishwa na kuwapendelea Wajerumani na kuwachukia Waingereza.Huko Uganda, mara tu baada ya kuanza mapigano, Nyindo, Chifu Mkuu wa Kigezi, alishawishiwa na ndugu yake wa kambo, Wami wa Ruanda, kufanya uasi dhidi ya Waingereza kwa niaba ya Wajerumani.

Mara nyingi, hasa huko Nigeria, maasi wakati wa vita hayakusababishwa moja kwa moja na zile hatua maalumu zilizochukuliwa katika kipindi hicho, mara nyingi maasi hayo yalilenga kuyapinga yale maovu ya utawala wa kikoloni kama vile kutozwa kodi kulikoanzishwa Yoruba kwa mara ya wanza mwaka 1916. Kutozwa kodi huku, pamoja na madaraka zaidi waliyopewa watawala wa jadi chini ya siasa ya 'utawala kupitia wenyeji' kulisababisha maasi ya Iseyin. Katika sehemu za Afrika Magharibi iliyokuwa chini ya Mfaransa kuwekewa kwa *indigenat* (sheria ya kibaguzi), kuundwa upya kwa mipaka ya utawala, kukandamizwa kwa machifu au kodi walizozitoza wale machifu ambao hawakawa na mamlaka ya jadi, yote haya yalikuwa ni sababu kubwa za maasi yaliyotokea katika kila koloni lililokuwa katika muungano.

Maasi haya, sababu zake na ziwe zozote zile, yalikomeshwa bila ya huruma na mamlaka ya kikoloni. 'Waasi' walipelekwa jeshini kwa nguvu, walipigwa viboko na baadhi walinyongwa, machifu walihamishwa nchini au walifungwa na vijiji vilivunjwavunjwa, yote haya yakifanywa kama ni ovyo. Lakini si kila aina ya uasi ilitumia nguvu. Watu wengi walijaribu kuepukana na madhila yaliyowapata kwa kuhama nchi au kwa njia nyingine za kukwepa. Ndiyo maana idadi kubwa ya raia wa Kifaransa huko Senegal, Guinea, Haut-Senegal-Niger na Ivory Coast, ambao inakisiwa kwamba walikuwa kiasi cha watu 62,000,

walichukua ile hatua iliyoitwa A.I. Asiwaju kwa jina la 'kupinga kwa kuhama' na kuhamia nchi jirani ambazo zilikuwa chini ya Mwingereza. Ili kukwepa kuandikishwa kwa nguvu wakazi wa vijiji vizima walikimbilia mwituni. Vijana walihiari kujitia vilema kuliko kulitumikia jeshi la kikoloni.

## Matokeo ya Kiuchumi ya Vita

Kutangazwa kwa vita kulileta mparaganyiko mkubwa wa kiuchumi katika Afrika. Kwa jumla vita vilifuatiwa na kushuka kwa bei ya vitu muhimu vilivyotokea Afrika wakati habari kwamba bidhaa kutoka nchi za nje zitakuwa adimu zilifanya bei za bidhaa hizo kupanda. Uganda kulikuwa na ongezeko la ghafla la asilimia 50 katika bei ya bidhaa za nje. Mfumo wa biashara kati ya Afrika na Ulaya ulibadilika kabisa kutokana na kuondoshwa Wajerumani katika ardhi za Madola ya Muungano, ambako katika sehemu fulani fulani, kama vile Sierra Leone, Wajerumani walihusika na asilimia 80 ya biashara ya kuagiza na kusafirisha bidhaa. Ujerumani, ambayo ndiyo iliyokuwa mfanyabiashara mkubwa na Afrika sasa ilikuwa karibu imetolewa kabisa katika shughuli za biashara katika Afrika kutokana na kufukuzwa kwa raia wake, kukamatwa kwa mashamba yao, majumba yao jya biashara na viwanda vyao, yote haya yakifanywa na yale madola yaliyokuwa yamezikalia ardhi zake. Hali mbaya ya uchumi iliyokuwepo baada ya kuanza vita baadaye ilibadilika kwa kunyanyuka kwa biashara ya zile bidhaa zilizohitajika katika kusaidia juhudi za vita za Madola ya Muungano. Kwa hivyo pumba ya Misri ilipanda kutoka E3 kwa kilo mia mpaka ikawa E8 katika mwaka 1916-1918. Lakini kuongezeka kwa mahitajio hakujaonekana siku zote hakukudhihirishwa na kuongezeka kwa bei kwa sababu serikali za kikoloni mara nyingi zilidhibiti bei walizokuwa wakiwalipa hao waliotengeneza bidhaa hizo. Baadhi ya nchi kama vile Gold Coast ambayo zao lake kubwa la kakao halikuhitajika sana, ziliathirika vibaya kipindi chote cha vita.

Wakati bei za bidhaa za kusafirisha nje na ujira wa wafanyakazi kwa jumla viliteremka japo kuwa mahitaji ya mali ghafi na wafanyakazi yaliongezeka, bidhaa zilizoagizwa kutoka nje, wakati zilipopatikana zilipenda muda wote wa vita. Hali hii iliwaathiri Waafrika waliokuwa katika sekta ambazo watu wakilipwa ujira au katika sekta nyingine zilizokuwa zikitoa mazao ya kusafirisha nje.

Vita pia vilishuhudia kujiingiza ziadi kwa serikali katika uchumi wa makoloni ya Kiafrika, ama kwa njia ya kudhibiti bei au kwa kuangizia mazao ya chakula, kulazimisha ulimaji wa mazao au kuandikisha wafanyakazi katika miradi muhimu au kutenga nafasi maalumu melini kwa vitu vilivyotaka kusafirishwa nje. Kwa jumla, kujiiingiza kama huku kulipendelea maslahi ya vyombo vya ile dola ya kikoloni vilivyohusika na usafirishaji na uagizaji wa bidhaa.

Mahitaji ya mazao ambayo kijadi yakitumiwa na wenyeji tu, kama vile viazi vikuu, mihogo na kunde, kwa ajili ya kuyalisha Madola ya Muungano Ulaya na kwa ajili ya majeshi yaliyokuwa Afrika au Mashariki ya Kati yaliwaongezea shida wale waliokuwa katika sekta ya wachumia tumbo. Na pale mazao ya kutumia watu wenyewe yalipoagizwa kama ilivyotokea mara nyingi, au yaliponunuliwa kwa bei ya chini kuliko ile ya sokoni

wenye bidhaa hizo waliumia. Ndiyo maana mwishoni mwa vita *Fallahim* (wakulima) wa Misri walipata shida sana kuweza kuishi hasa ukitazama ughali wa vitu ulivyokuwa na pia ukitazama ule mtindo wa kuagizwa kwa matumizi ya watu wengine kwa mazao ya wanyama wao.

Kuandikisha kwa majeshi na wachukuzi kulisababisha upungufu wa wafanyakazi katika sehemu nyingi za Afrika wakati wa vita. Kuenea kwa maradhi ya influenza katika Afrika Mashariki na Kati kuliwaathiri wachukuzi waliokuwa wakirudi nyumbani na kusababisha upungufu mkubwa wafanyakazi huko Rhodesia na Kenya. Upungufu huu ulitokea upande wa wafanyakazi wa Kiafrika na wa Kizungu. Upungufu wa bidhaa za kuagizwa nje huenda ukawa ndio sababu ya kuanguka kwa uzalishaji mali katika nchi, kama Misri, ambazo kilimo chake kilitegemea mbolea, pembejeo na mitambo ya kumwagilia maji vilivyoagizwa kutoka nje; lakini upungufu huu ulishajiisha, katika baadhi ya nchi, kuanzishwa kwa viwanda vya kutengeneza nchini vitu vyao wenyewe badala ya vile vilivyokuwa haviwezi kuagizwa, hasa huko Afrika Kusini ambako uwezekano wa bidhaa za nchini kupata masoko nchi za ng'ambo ulitambuliwa wakati huu. Katika Kongo ya Wabelgiji, ambayo ilikuwa haina mawasiliano na Ubelgiji kwa sababu Ubelgiji ilikuwa imekaliwa na adui, vita vilikuwa shajiisho kubwa lililoifanya Kongo izidi kujitegemea. Kumiminika kwa vikosi vya Kiingereza huko Misri na kuingizwa kwa ,200 milioni katika uchumi wake wakati wa vita kulikuwa ni shajiisho muhimu kwa ukuaji wa viwanda.

Vita vilianzisha matumizi ya magari na pamoja na tukio hili kulianzishwa barabara za kupita magari katika sehemu nyingi za Afrika. Karika Afrika Mashariki mapigano dhidi ya Wajerumani na tatizo la kusafirisha vitu yalisababisha kujengwa kwa njia nyingi za magari. Katika zile sehemu zilizokuwa na harakati za vita zilizokuwa zikiendelea na kulikohitajika urahisi wa usafiri bandari zilianzishwa kwa haraka. Mombasa, Bizerta, Bandari ya Harcourt na Dakar zote hizi ni mifano mizuri ya bandari hizo. Huko Nigeria, migodi ya makaa ya Enugu ilifunguliwa wakati wa vita kwa matumizi ya nishati ya reli.

Kwa jumla mapato ya serikali yalipungua wakati wa vita kwa sababu yalitegemea sana ushuru kutokana na uagizaji bidhaa nje. Kwa hivyo, isipokuwa pale tu mahitajio ya kijeshi yalipofanya iwe dharura, shughuli za majenzi zilisita na mipango ya maendeleo yaliwekwa kando mpaka baada ya vita.

## *Matokeo ya Vita Upande wa Kijamii na Kisiasa*

Matokeo ya kijamii ya vita hivi kwa upande wa Afrika yalitofautiana sana baina ya eneo moja na jingine na yalitegemea kiasi gani sehemu fulani ya bara hili ilihusika na vita hivyo hasa kuhusu kima cha uandikishaji wa watu wake au harakati za kivita zilizokuwemo katika sehemu hiyo. Ukilinganishwa na ule utafiti uliofanywa juu ya matokeo yavita upande wa kisiasa katika Afrika, itaonekana kwamba utafiti uliofanywa juu ya matokeo ya kijamii ni mdogo. Juu ya hivyo, taathira ya matokeo ya kijamii juu ya askari, wachukuzi na vibarua waliong'olewa kutoka ulimwengu mdogo wa vijijini mwao na kupelekwa maelfu ya

maili mbali na kwao na taathira walioileta watu hawa katika jamii zao waliporudi vitani ni mada muhimu katika historia ya ukoloni.

Hapana shaka kwamba vita viliwafunua macho Waafrika weusi hasa wale waliokuwa wasomi. Katika sehemu nyingi za Afrika vita vilitoa mwanga, ikiwa siyo kwa harakati za kizalengo, basi walau katika kuuendeleza miongoni mwa wasomi ule mtindo wa kuhoji mambo na kutokukubali moja kwa moja bila ya kusaili kila kinachowahusu bwana zao wa kikoloni.

Huko Guine, kurudi kwa askari vitani kulianzisha migomo na uasi katika kambi za kuondosha hali ya vita na pia kushambuliwa kwa mamlaka ya machifu.

Ikiwa vita vilishuhudia kumalizika kwa juhudi za Waafrika za kujipatia tena uhuru waliokuwa nao kabla ya ukoloni, vita hivi pia vilishuhudia madai ya kutaka kushiriki katika shughuli za serikali mpya waliyosambikwa nayo na Wazungu. Madai haya yaliyohamasishwa na zile hoja 14 ambazo Rais Woodrow Wilson alizitoa wakati wa kujibu mapendekezo ya Warusi ya tarehe 17 Oktoba, 1917, yalitaka amani ya mara moja bila ya utekaji wala ulipaji fidia na yalidai hata uhuru wa kujiamulia. Chama cha Sa'd Zaghlul cha Wafd huko Misri kilipata jina lake kutokana na ujumbe ambao Sa'd Zaghlul alijaribu kupeleka katika Mkutano wa Amani wa Versailles kuzungumzia swala la kurejeshwa Misri uhuru wake. Vile vile huko Tunisia, ingawa mwakilishi wa serikali aliyekuwepo wakati wa vita, Alaphetite, aliwadhibiti wazalendo wa Tunisia sawa sawa kama Waingereza walivyofanya Misri, bada ya vita viongozi walimpelekea simu Rais Wilson wa Marekani kutaka msaada wake katika madai yao ya uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe.

Ingawa hoja 14 za Wilson hazikuhamasisha madai ya uhuru moja kwa moja katika sehemu za Afrika Kusini mwa Sahara, lakini mawazo ya kiungwana ya Wilson yaliwapa tamaa wazalendo wa Afrika Magharibi kwamba wataweza kuushawishi Mkutano wa Amani wa Versailles na pia uliwapa moyo wa kudai haki ya kuwa na sauti kubwa zaidi katika shughuli za nchi yao. Huko Sudan hoja 14 za Wilson pamoja na hamasa zilizotokana na uasi wa Waarabu wa mwaka 1916 ziliupa mwelekeo mpya uzalendo wa Sudan huku zikiathiri mwelekeo wa kizazi kipya cha vijana waliokuwa na mwamko wa kisiasa na waliopata mafunzo kwenye shule za serikali na kupata maarifa ya kisasa ya Kimagharibi.

Katika majimbo mengi ambayo yalitoa mchango mkubwa wa binaadamu na vifaa katika juhudi za vita, palikuwa na tamaa kwamba patapatikana walau tunzo, na tunzo yenyewe itakuwa kupatikana kwa mabadiliko ya kijamii na kisiasa. Na kwa hakika Blaise Diagne aliahidiwa mabadiliko kadhaa baada ya vita katika sehemu ya Afrika ya Weusi iliyokuwa chini ya Mfaransa ikiwa angweza kuandikisha watu zaidi ambao Ufaransa iliwahitajia kwa kuwapeleka katika sehemu za mapigano zilizokuwa Ulaya. Daigne alifanya hivyo lakini yale mabadiliko hayakufanywa. Mchango wa Algeria katika juhudi za vita uhituzwa kwa kuwapatia watu wa Algeria maendeleo ya kiuchumi na kisiasa ambayo yalipingwa na makaburu wa Kifaransa na ambayo Emin Khalid (mjukuu wa Abdalkadir ambaye aliwahi kuukosoa vikali utawala wa Kifaransa na akahamishwa nchini mwaka 1924) aliyaona kuwa hayatoshi. Yeye ameitwa, kwa haki kabisa, mwanzilishi kwa harakati

za kizalendo za Algeria. Huko Tunisia ujumbe wa watu thelathini wakiwakilisha jamii ya Kiarabu ulimtaka Bey kuanzisha mabadiliko ya kisiasa na kukumbusha muhanga umbao Tunisia iliutoa katika vita. Bila ya shaka sehemu kubwa ya hamasa zilizosababisha kuundwa kwa *Destur*, yaani Chama cha Katiba, zilitokana na askari waliorudi vitani na vibarua ambao walikuwa hawakuridhika na hali yao duni katika nchi yao wenyewe. Katika sehemu ya Afrika Magharibi iliyokuwa chini ya Mwingereza, magazeti umbayo kawaida yalikuwa na utiifu mkubwa kwa Waigereza na yakiwapinga Majerumani, yaliamini kwumba tunzo yao kwa utiifu huu itakuwa kupewa kwa kikundi bora cha wasomi nafasi muhimu katika utoaji wa maamuzi uliokuwa ukifanywa na wakoloni.

> Vita vilihamasisha siyo tu uzalendo wa Kiafrika bali pia uzalendo wa Kizungu hasa Afrika Kusini. Huko Afrika Kusini, ingawa maasi ya Waafrikana yalivizwa haraka, ile imani iliyoyahamasisha maasi hayo haikuvia. Kwa hivyo kwa kweli kabisa, uzalendo wa Kiafrikana wa kisasa ulioanza wakati wa Vita vya Makaburu ulizaliwa hasa wakati wa maasi ya mwaka 1914. Ingelikuwa Vita vya Kwanza vya Dunia havikutokea, Makaburu wangeliweza kujirekebisha kwa vizuri zaidi na ile sera ya suluhu ya Botha na Smuts. Vita hivi viliwafanya Makaburu wajiamulie kuunda kikundi kilichochukua sura ya Afrikaner Broederbond, kwanza kwa siri na baadaye kuchukua sura ya Chama cha Kizalendo ambacho kilikuwa 'kimetakasika' zaidi.

Huko Kenya, masetla wa Kizungu walivitumia vita kuleta mabadiliko makubwa ya kisiasa dhidi ya serikali ya kikoloni. Masetla hawa wakapata haki ya kuchagua wawakilishi katika Baraza la Kutunga Sheria, ambamo baada ya mwaka 1918 mlikuwa na wajumbe wengi zaidi waliowakilisha masetla. Marupurupu mengine yaliyopatikana na kule kupasishwa kwa Sheria ya Ardhi ya Mfalme ambayo iliwezesha kuweko kwa ubaguzi wa kitaifa katika sehemu za milimani za Wazungu na katika ule mpango wa makazi ya askari wa vita ambao ulitenga sehemu kubwa ya ardhi ya Nandi kwa ajili ya makazi ya askari wa Kizungu baada ya vita.

Uzalendo wa Kenya ulipata msukumo mkubwa kutokana na kupinga kwa wananchi yale marupurupu waliojipatia Wazungu hasa kuhusu ardhi. Kwa hivyo Chama cha Wakikuyu umbacho wanachama wake wengi walikuwa machifu, kilianzishwa mwaka 1920 kutetea maslahi ya Wakikuyu kuhusu ardhi ya Chama cha Vijana wa Kikuyu cha Harry Thuku, kilichoundwa mwaka mmoja baadaye, kilikuwa na lengo la kutetea maslahi kuhusu ardhi na wafanyakazi wa Kiafrika.

Huko Afrika Kusini, kuzaliwa kwa uzalendo wa Kiafrika na pitikapirika za kijamhuri wakati wa vita viliwashughulisha sana viongozi wa Kiafrika wa Swaziland na Basutoland (sasa Lesotho). Viongozi hawa walihofia kwamba nchi zao zitamezwa na Afrika Kusini umbayo ilizidi kuendeleza sera ya kibaguzi kama ilivyodhihirika katika masharti ya Sheria ya Ardhi ya Wananchi ya mwaka 1913. Katika Afrika Kusini yenyewe baada ya vita Chama cha Kizalendo cha Waafrika wananchi ambacho baadaye kikawa Chama cha Kizalendo cha Waafrika kilimpelekea barua Mfalme George wa Uingereza ukieleza mchango uliotolewa na Waafrika katika mapigano yaliyofanyika Kusini Magharibi ya Afrika na katika Afrika Mashariki na pia huko Ufaransa, na kukumbusha kwamba vita hivyo vilipiganwa ili kuwagomboa watu kutokana na madhila na ili kila taifa liwe na haki

ya kujiamulia umamlaka wake. Chama hicho kiliarifiwa na Ofisi ya Mambo ya Makoloni ya Uingereza kwamba Uingereza haitaweza kuingilia mambo ya ndani ya Afrika Kusini, na pia kuwa yale maoni ya Chama cha Kizalendo hayakufikishwa mbele ya Mkutano wa Amani.

Mwisho, vita vilishuhudia mabadiliko makubwa katika mtizamo wa kimataifa kuhusu swala la ukoloni. Kabla ya vita madola ya wakoloni wa Ulaya yaliwajibika kwa wao wenyewe tu. Baada ya vita, lile wazo kwamba kuwatawala wale wanaoitwa eti watu walioko nyuma ni 'jukumu la takatifu' ingawa ilijidhihirisha katika miaka ya 1890, kwa mfano pale ilipokatazwa kuwazuia pombe Waafrika, sasa wazo hili lilihifadhiwa katika ile dhamana ambayo iliyapa Madola ya Muungano utawala wa makoloni ya Ujerumani kwa niaba ya Umoja wa Mataifa ambao ulifanywa 'ndio dhamana kwa kuendeleza kwa kiwango cha juu kabisa maslahi ya hali na mali na maendeleo ya kijamii ya wakazi wake'. Kinadharia hii ilisisitiza umuhimu wa ule msingi wa uwajibikaji wa kimataifa. Uhuru wa watu wa kujiamulia mambo yao wenyewe ambao mwanzo ulitangazwa katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kimataifa wa Nchi za Kijamaa uliofanyika London mwaka 1896 pia ulisisitizwa na kiongozi wa dola kuu duniani, Woodrow Wilson wakati taifa chipukizi la Kirusi lilikuwa likishambulia kila aina ya ukoloni uliokuwa Afrika.

Ingawa hali ya watu waliotawaliwa ilikuwa haikubadilika na kuwa bora zaidi katika ile miaka baada ya vita, wakati hata juhudi za hiari za kuleta mabadiliko zilivizwa na hali mbaya ya uchumi, maswali ya ndani yalianza kuulizwa kuhusu uhalali wa ukoloni. Na ilikuwa katika hali hii ndipo zilipopandwa mbegu za harakati za kizalendo ambazo mwishowe zilizaa uhuru kwa nchi nyingi za Kiafrika.

## *Hitimisho*

Kwa hivyo basi Vita vya Kwanza vya Dunia vilianzisha mabadiliko katika historia ya Afrika ambayo hayakuwa yakusisimua kama vilivyokuwa Vita vya Pili vya Dunia, lakini juu ya hivyo yalikuwa muhimu katika sehemu nyingi. Moja katika urithi muhimu uliopatikana ni kupanguliwa kwa ramani ya Afrika, na kuliweka bara hilo katika hali yake ya sasa. Ujerumani ilipigwa teke kama ni dola tawala na pahala pake palichukuliwa na Ufaransa na Uingereza huko Cameroon na Togo, na kuchukuliwa na Afrika Kusini huko Afrika Magharibi na Uingereza na Ubelgiji katika sehemu ya Afrika Mashariki iliyokuwa chini ya Mjerumani, Ubelgiji ikajipatia maeneo madogo madogo lakini yenye watu wengi huko Ruanda na Urundi (sasa Rwanda na Burundi). Mapatano yenye utata yaliyofanyika Versailles kuhusu ugawaji mpya wa ardhi hizi kwa Madola ya Muungano yaliyoshinda kwa hakika ni sehemu ya historia ya Ulaya ingawa ugawaji wa Togo na Cameroons uliofanywa bila ya kuzingatia maswala ya kihistoria na ya kikabila ya nchi hizi uliwatia uchungu mkubwa baadhi ya wananchi wa maeneo haya hasa Waewe na Togo.

Na huu ukawa ndio mwisho wa kuigawa Afrika na wa juhudi za Waafrika kutaka uhuru kwa msingi wa nchi zilivyokuwa kabla ya kugawanywa Afrika. Ingawa kipindi hiki kilikuwa cha mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi kwa nchi nyingi za Kiafrika pia kilianzisha kipindi cha miaka ishirini ya utulivu katika utawala wa Kizungu isipokuwa

mahala kama Moroko ya Mfaransa na Wahispania, Mauritania ya Ufaransa na Libya ya Italia.

Hata hivyo, mawazo ya uhuru wa kujiamulia mambo wenyewe na ya uwajibikaji wa madola ya kikoloni yaliyokuwa yamekwishapandikizwa katika vita hivi yaliathiri sana wakati kwa kipindi cha amani kilichofuatia yale maendeleo ya harakati changa za kizalendo. Lakini ilibidi vitokee vita vya pili ndipo upatikane mshituko uliowcza kugeuza maombi ya wazalendo ya kutaka kushirikishwa katika shughuli za serikali yakawa madai hasa ya kutaka kuendesha serikali wenyewe.

tayari kubeba mzigo mkubwa wa gharama za kuendeshea makoloni moja kwa moja, wakati ilikuwa inaaminika kijumla kwamba kuhusisha tawala za jadi katika kuongoza kungeleta mfarakano mdogo sana wa kijamii na hivyo kuhakikishiwa ushirikiano wa wenyeji. Sababu ya mwisho ilikuwa ni kushindwa kwa siasa ya usilimishaji au utawala wa moja kwa moja ambayo ilitumika sana katika karne ya kumi na tisa. Ama kwa mintaarafu ya Wafaransa katika jamii zao nne huko Senegal au Waingereza katika makoloni yake ya huko Sierra Leone, Gold Coast na Lagos, siasa ya usilimisho, hadi kufikia mwisho wa karne ya kumi na tisa, ilifadhaisha sana, sio tu kwa ajili ya upinzani wa kiutamaduni wa Waafrika waliohusika, bali pia kutokana na mapambano yaliyokuwa yanaongezeka baina ya Wakoloni kwa Kizungu na Waafrika waliopata elimu ya Kimagharibi nchini mwao.

Kwa kweli ilikuwa ni huku kukosekana kwa ushirikiano baina ya wakoloni wa Kizungu na Waafrika walioelimika mwishoni mwa karne ambako kulizua kukosekana bandia kwa watumishi wa utawala, kwa vile serikali mpya zilianza kuweka pingamizi katika kuwaajiri Waafrika wenye ujuzi wa juu katika utawala.

Kutokana na mambo haya, hakuna serikali ya kikoloni iliyofikiria mara moja kuondolea mbali mifumo ya kijamii na kisiasa iliyokwishakuwepo. Walakini matakwa ya msingi ya mfumo wa kikoloni yalikuwa na matokeo ya kudhoofisha na kubomoa taasisi za msingi za Kiafrika. Ukweli kwamba serikali nyingi za Kiafrika zilipatikana kwa ushindi wa vita au kwa kuwahamisha mbali na kwao au kuwaondosha madaraka baadhi ya machifu, umesababisha taasisi nzima ya uchifu kudhalilika. Utozaji kodi iliyopangwa Ulaya ilikuwa ni hatua nyingine ya uharibifu wa kikoloni, huku hata jitihada za wastani zilizoelekezwa kwenye kile siku hizi kinachoitwa maendeleo ya kisiasa pia ziliathiri taasisi za wenyeji. Kwa sababu hizi utawala wa moja kwa moja usingweza kutekelezwa vema na hivyo ulilazimika kufanyiwa marekebisho katika namna mbalimbali na serikali tofauti za kikoloni.

## *Muundo wa Utawala wa Kikoloni*

Kuanzia jumla ya Sultani wa Moroko hadi kitala cha chifu wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, maafisa tawala wa kikoloni wa Kizungu waliwatafuta na kuwaajiri "Watawala wa Jadi" kama wasaidizi au mawakala ili kwa kupitia kwao utawala wa kigeni uweze kutekelezwa kwa uthabiti kwenye jumuiya ya Kiafrika kwa ujumla. Juu kabisa ya mfumo wa utawala kulikuwa na Gavana au Gavana Generali ambaye japo hatimaye aliwajibika kwa serikali ya kwao mara nyingi alikuwa na hadhi kkama Mtawala. Kwa kawaida katika kipindi kati ya vita alikuwa anasaidiwa na aina fulani ya Baraza la ushauri au Kamati ambayo ilijumuisha makundi yote mawili, "Maafisa" au Watawala na "Wasio Maafisa" au wawakilishi wa maslahi ya kikoloni au kibiashara. Utaratibu wa utawala wa kikoloni wa kutawala kutoka makao makuu katika mifumo ya Kifaransa, Kireno na Kibelgiji ulisababisha kuacha madaraka ya Bunge huko huko Ulaya. Walakini, katika milki za Kiafrika za Waingereza, Halmashauri za kikoloni zilizuka kama vyombo vya Bunge vya wenyeji vikiwa na wajumbe walioteuliwa au kuchaguliwa au yote kwa pamoja na vikiwa na majukumu mbalimbali kuanzia ushauri hadi utungaji wa sheria. Walakini, idadi na njia

ambazo kwazo wawakilishi walichaguliwa zilihakikisha kwa dhati kwamba athari za utawala wa kizungu katika kipindi kati ya vita hazingeweza kuvurugwa vibaya au kutishiwa.

Utaratibu muhimu kupita taratibu zote za kikoloni ulioanzishwa ulikuwa ni ule wa kuwa na eneo la wilaya au mkoa, eneo lililoitwa Cercle, katika Afrika Magharibi ya Wafaransa. Kuendelea kutumia istilahi hii ya kijeshi ilikuwa ni kumbukumbu ya jinsi makoloni yalivyopatikana. Katika eneo la Cercle, Afisa Tawala wa Kizungu aliendesha utawala wa kikoloni na kuelekeza shughuli zote za Wazungu waliokuwa chini yake na watawala wa Kiafrika walioorodheshwa katika utawala wa kikoloni.

Eneo muhimu sana la Kiafrika na ambalo lilikuwa linajadiliwa sana lilikuwa lile la chifu wa Wenyeji. Kwa kweli kila serikali ya kikoloni katika Afrika ya watu weusi ilitegemea chifu ama awe wa jadi au mteule katika madaraka, alikuwa kitu cha msingi katika mfumo wa utawala.

Japokuwa hakuna mchunguzi au mhakiki aliyewahi kutilia shaka wazo kwamba shughuli za uchifu zilikuwa sehemu muhimu katika mfumo wa ukoloni katika bara zima kumekuwepo na mijadala ya kitaaluma kuhusu jinsi machifu hawa walivyotumiwa na serikali kuu za Kizungu. Swala kuu limekuwa likijikita kwenye tofauti kati ya utawala wa moja kwa moja na ule wa kupitia kwa wenyeji tofauti kati ya ujumbe wa utawala wa Wazungu uliopelekwa kwa watawala Waafrika kudhibiti kwa Wazungu madaraka ya Kijadi ya watawala hao.

Maelezo maarufu kuhusu umuhimu wa "Tawala za Wenyeji" kwa mamlaka ya kikoloni yalikuwa yale yaliyotolewa na Kugard. Kutokana na sababu zilizokwishatolewa hapo juu, hasa upungufu wa watumishi na fedha na kutokana na imani yake kwamba kutumiwa kwa taasisi kza wenyeji zilizopo kulikuwa ndio njia bora ya utawala wa kikoloni, Lugard alikataa utawala wa moja kwa moja na kupendelea utawala wa kupitia kwa wenyeji kambao sasa aliendeleza kama nadharia alipokuwa Balozi wa Nigeria ya Kaskazini kati ya mwaka 1900 na 1907. Muhtasari mzuri wa siasa yake unapatikana katika mkusanyiko kwa maelekezo aliyotoa kwa maafisa wake mwaka 1906, ambamo aliahidi kuwepo kwa "serikali moja ambayo ndani yake machifu wa wenyeji wana kazi zilizofafanuliwa wazi na vyeo vinavyotambulika kwa namna sawa na maafisa wa Kiingereza". Kwa hiyo msingi wa kile ambacho kingekuwa mfumo wa utawala wa kupitia kwa wenyeji ulikuwa ushirikiano na sio udumishaji, pakiwa na Mtawala Mkazi wa Kiingereza akifanyakazi hasa za ushauri na sio za utendaji na pakiwa na "Chifu" wa Kiafrika, kwa mfano Emir wa kabila la Wafulani, aliyeendelea na majukumu yake ya kijadi ambayo kwa sasa yaliongozwa kwa uangalifu, na sio kubanwa mno na utawala wa mabavu wa kikoloni.

Kwa hiyo, ikiwa umuhimu wa utawala wa Lugard ulikuwa ni kutumia uwezo uliokuwepo, jambo jingine zaidi lilikusudiwa. Marekebisho kufuatia kaida za Kizungu yalitarajiwa katika maswala kama vile sheria na kodi. Kazi hii ilitegemea sana maarifa waliyokuwa nayo maafisa tawala wa Kizungu juu ya mila za wenyeji na taasisi zao na bila shaka kiwango ambacho tawala za wenyeji zingekubali kufanya marekebisho hayo kuelekea maendeleo ya kisasa kwa kutumia taasisi zao hizo hizo.

Uwanda huu mpana wa utawala wa kupitia kwa wenyeji katika Nigeria ya

# 13

# Mbinu na Taasisi za Utawala wa Kizungu

## Sera ya Wenyeji

Wakati wa kutamalakiwa kwa Afrika na mataifa beberu ya Ulaya au muda mfupi tu baada yake, Sera kadhaa zinazohusu wenyeji ziliwekwa na tawala za makoloni mapya. Ingawa sera hizi zilitofautiana, kulikuwa na makubaliano ya kiujumla ya kinadharia na kimatendo kwamba utawala wa kikoloni unaweza tu kuwa makini kwa kuwatumia wenyeji na taasisi zao katika wajibu fulani fulani. Zaidi ya hayo ilikubalika kwamba madhumuni ya kuwepo kwa Wazungu yatafsiriwe kama ni ya madaraka au udhamini, au chambilecho Sir Fredrick (baadaye Maulana) Lugard, "Mamlaka kuwili" (*Dual Mandate*). Mwelekeo huu wa kiuhaba wa udhamini au madaraka ambao ulishika sana katika Ulaya kuhusu Afrika ya ukoloni, ulifanywa wa kimataifa na kutekelezwa chini ya utaratibu wa udhamini ulioanza tangu vita ya kwanza ya dunia.

Hata hivyo katika lugha hii fasaha bado kunadhihirika fikra nyingine ya kuwepo kwa utamaduni bora na taifa bora iliyojengwa katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa na ambayo kwayo mara kwa mara Mwafrika alichukuliwa kama mtoto au "asiye-komaa". Fikra hii ya pili kisha ilizaa imani iliyoenea sana kuwa utawala wa Kizungu ulilazimika kudumu kwa muda mrefu sana. Kwa yale maeneo machache ambayo tayari yalikuwa na wakazi wengi wa Kizungu na ambayo bado yalikuwa yanapokea wahamiaji zaidi katika kipindi hiki utawala wa Kizungu ungekuwa wa kudumu. Hata hivyo katika nchi hizo, isipokuwa Afrika ya Kusini ambapo siasa kali ya ubaguzi ilikuwa tayari kimekwisha anzishwa, fikra kuhusu maendeleo ya ushirika zilikuwa kila mara zinazungumziwa. Zaidi ya hayo, siasa ya kikoloni haikuwa na malengo dhahiri na kamili, bali ilikuwa na dhana zisizoeleweka vizuri kama 'Serikali ya Madaraka' katika ambo lake la Kiingereza na 'Kuchanganyika Kisiasa' katika umbo lake la Kifaransa na Kireno.

Zifuatazo ni sababu za makubaliano ya kijumla ya kile ambacho kingeitwa utawala wa pamoja au "utawala kwa kupitia wenyeji", ambao ulitumia utawala wa jadi karika tawala za kikoloni lakini katika wajibu duni: Kwanza, kupenyezwa kwa haraka sana ndani ya Bara la Afrika na Wazungu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa hakukulingana na kiasi cha wafanyakazi Wazungu waliokuwepo tayari kuongoza maeneo mapya yaliyopatikana. Pili kwa kuwa kupenyeza huko kuliendelea mpaka kwenye maeneo mengi ambayo bado yalikuwa hayajaingiliwa na utamaduni wa Kizungu, utawala wa moja kwa moja wa aina yoyote ile usingewezekana. Tatu hakuna serikali ya kibeberu iliyokuwa



**13.1** *Frederick, Lord Lugard (1858-1945)* Balozi wakati huo akiwa Gavana wa Nigeria Kaskazini, 1900 – 1907, 1912 – 1914; Gavana wa Nigeria, 1914 – 1919



**13.2** *Louis-Gabriel Angoulvant,* Luteni-Gavana wa Burkina Faso, 1908 – 1916

**13.3** *General Joseph Simon Gallieni* (1849 – 1916), Commandant - Superieur wa Sudani ya Wafaransa 1886 – 1888; Gavana-Jenerali wa Madagascar 1896 – 1905



**13.4** *Albert Heinrich Schnee (1871–1949),* Gavana wa Afrika Mashariki ya Wadachi, 1912 – 1918



kaskazini unaweza kulinganishwa na mwingine ambao kama ilivyokuwa kwa Lugard, ulipata mafanikio mengi kwenye maeneo yaliokaliwa na taasisi za kisiasa za Kiislamu. Tukiangalia nje zaidi ya Afrika, mfumo huu wa utawala wa kupitia kwa wenyeji ulipewa tafsiri ya kinadharia na Wafaransa; kile walichokiita *a politique d' association* (sera ya umoja) kilitambuliwa sana mwanzoni mwa karne hii na kilitafautishwa, kwa raghba na wazo kongwe la siasa ya usilimisho. Siasa hii ambayo kwanza kabisa ilipendekezwa kwa ajili ya Indo-China na baadaye kuenezwa kama siasa ya Afrika, "Umoja" ilikuwa njia ya kuendesha shughuli za kikoloni katika maeneo kadhaa tu. Ni huko Moroko tu ambako Wafaransa waliuzingatia sana, na hasa kwa ajili ya umuhimu uliotolewa kwa shughuli za wenyeji na Balozi Mkazi Louis - Hubert Lyautey, ambaye, katika siku za mwanzo za utawala wa nchi lindwa hiyo alitawala kwa kutumia amri chache tu kutoka Serikali ya Ulaya. Nchini kote Moroko, mfumo wa serikali za kisharifu ulidumishwa, wakati ambapo katika ngazi ya wenyeji, shughuli za kiutawala zilikuwa sawa kabisa na zile zilizopendekezwa na Lugard. *Controleur Civil* (Mdhibiti wa Raia) wa Kifaransa alitakiwa awe na wadhifa wa ushauri na akaguzi kwa *Cadi* (Kadhi) afisa wa Kiislamu aliyeshughulikia sheria kwa mujibu wa *Sharia*. Mpango ufanano na huu ulikuwa katika eneo la Moroko lililokuwa linatawaliwa na Wahispania ambapo *Cadi* (Kadhi) alikuwa anongozwa katika majukumu yake na Inventore (Mtakwimu/Mdhibiti Raia), Mhispania anayelingana na *Controleur Civil.* Cadi (Kadhi) alibakishwa pia kiutawala katika nchi ya Somalia iliyokuwa chini ya Waitalia, lakini huko aliungana katika wadhifa wa serikali ya wenyeji na machifu wateule.

Kinadharia utawala huo wa kupitia kwa wenyeji ulitumika pia katika shughuli za kikoloni za Wafaransa kusini mwa Sahara, lakini utekelezaji wake ulikuwa tofauti, kwa maana kule, Wafaransa walitumia tawala za wenyeji moja kwa moja katika utawala wao wa kikoloni. Lakini tawala hizo za wenyeji siku zote zilikuwa dhalili ya utawala wa Wafaransa. Wareno nao walifanya vivyo hivyo.

Mfumo wa Lugard wa utawala wa kupitia kwa wenyeji, ulifanikiwa mwanzoni huko Nigeria ya kaskazini ijapokuwa ulikashifiwa na baadhi ya wahakiki kuwa ulikuwa mtindo usiotaka mabadiliko. Baadaye, baada ya vita, mtindo huu ulienezwa kote katika Afrika ya Waingereza, ikiwa ni pamoja na Uganda na nchi mpya zilizopatikana kutoka kwa Wajerumani yaani Tanganyika na Cameroon. Mfumo huu ulitumiwa pia na Wabelgiji huko Kongo baada ya mwaka 1920. Ijapokuwa hali haikuwa muruwa sana na matokeo hayakuwa mazuri zaidi katika sehemu nyingine kama ilivyokuwa katika jimbo la Wahausa - Wafulani huko Nigeria, Waingereza walijaribu kufuata mikondo ya mila za wenyeji ili hata zile taasisi mpya zilizobuniwa kama vile Halmashauri za wenyeji zifanane na mifumo ya uongozi wa wenyeji. Hitilafu zaidi ya mfumo huu ilikuwa Afrika ya Kusini wakati dhana ya "Utawala wa Wenyeji" ilipokuwa ni njia ambayo kwayo Wazungu wachache waliwahakikishia watawala wa tawala za wenyeji kupewa maeneo ya nchi ambayo wangekaa wao tu (yaani rizani); maeneo ambayo sasa yametengwa kutokana na sera ya ubaguzi.

Katika sehemu yote ya Afrika Kusini mwa Sahara katika kipindi kati ya vita, Chifu alikuwa ni wakala wa serikali na sio 'mtawala wa kienyeji' na kazi na wadhifa wake

wa jadi ulinyongea sana au kupunguzwa. Mtengo huu wa madaraka hata katika mikoa iliyoingizwa kwenye utawala wa kupitia kwa wenyeji unaelezeka kwa urahisi sana. Ni dhahiri kwamba kazi za kijadi zilipanuliwa na mahitajio mapya kama vile ukusanyaji wa kodi, kufanya sensa, au kuandikisha vibarua na kuandikisha askari kwa lazima. Mahali popote palipoonekana kwa macho ya Wazungu kuwa hapakuwa na watu wenye sifa za kushika madaraka ya watawala wa jadi, watumishi wengine kama vile wazee wa vita, maafisa wadogo wa jeshi au makarani waliteuliwa kama machifu. Hivi ndivyo ilivyokuwa katika makoloni ya Wafaransa na Wareno ambapo sheria za jadi za kuwateua watu kwa ajili ya uchifu zilikuwa mara nyingi walikuwa wanapewa umaarufu huo wa kisiasa ambao hawakuwa nao tangu awali au wakati mwingine walikuwa wanawekwa katika jamii kambazo kwa asili hazikuwa na machifu, sehemu ambazo awali machifu walikuwa hawahitajiki kwa utawala. Mifano ya hali hizi mbili zilizojitokeza inaonekana kati ya Waigbo wa Nigeria, Wakikuyu wa Kenya na Wateso wa Mashariki mwa Uganda.

Ulipoanzishwa utawala wa Kizungu, Machifu walighilibiwa kana kwamba walikuwa maafisa tawala ambao wangeliweza kuhamishwa, au kuondolewa ili kukidhi haja za wakoloni. Uchifu ulifutwa mahali ambapo ulionekana kuwa haukuhitajika na uliundwa pale ambapo ulionekana utakuwa na manufaa. Pengine mfano mmoja muhimu wa utaratibu huu ulitokea kule Kongo ya Ubelgiji (sasa Zaire) ambapo baada ya mwaka 1918 idadi ya *Chefferies* (Falme au Dola) ilipunguzwa kutoka 6095 mwaka 1917 hadi 1212 mnamo mwaka 1938. Zaidi ya hayo eneo jipya kabisa la utawala lililoitwa *le Sectur* (Kata) lilianzishwa kwa madhumuni ya uimarishaji. Kwa misingi hiyo hiyo Wafaransa pia katika Afrika ya Magharibi waliunda eneo la utawala la kuviweka vijiji katika Centon (Kantoni) ambayo kama alivyosema gavana mmoja "huwekwa chini ya madaraka ya *Indigenous Adminsitrative Agent*" (Mtawala Wakala wa Kienyeji) ambaye hupewa jina la *Canton Chief* (Mkuu wa Kantoni).

Afisa tawala wa kienyeji alionekana kama kikwazo katika mfumo huo. Hata afanyeje, alionekana kama Chifu. Aliyekuwa wakala mharibifu kwa kuhusiana na mambo haya alikuwa Afisa tawala wa kineyji. Kwa madhumuni aliyokuwa nayo mwenyewe mara nyingi Chifu. Delavignette aliielezea hali hii kwa utoshelevu aliposema kwamba afisa tawala wa kikoloni hakuwa afisa tawala hata kidogo bali Kamanda na alitambuliwa hivyo na Jumuiya ya Waafrika iliyokuwa chini yake. Kazi yake kuu alidai kwa dhati kuwa "ni kutenda kama mkuu". Kazi iliyotengwa na ambayo haikuwa ya uharibifu ambayo Lugard alidhani kuwa Mtawala Mkazi wa Kiingereza angeliitekeleza huko Nigeria ya Kaskazini ilikataliwa na Maafisa Tawala wa Kifaransa na Kireno katika nchi zao. Wakati maafisa tawala katika nchi ya Somali ya Waitalia walifanana sana na wale wa Kiingereza katika uhusiano wao na Machifu wa kijadi, hata hivyo kati ya makundi haya mawili Azimio la Lugard lilibidi kurekebishwa kulingana na matakwa ya utawala wa kikoloni na wajihi wa wahusika wanaotekeleza azimio hilo.

## *Madhumuni ya Uanzishaji wa Ukoloni*

Tukichunguza kwa yakini madhumuni halisi ya utawala wa kikoloni yalikuwa na mipaka. Katika umbo lake la kawaida, madhumuni yake yalikuwa ni kudumisha amani, kubana matumizi na kuunda jeshi la vibarua ambao hapo awali walitumiwa kama wapagazi na baadaye wakawa wajenzi wa barabara na reli, na pia kwa madhumuni ya biashara. Kwa ujumla, madhumuni haya yaliongezwa katika kazi za utawala wa jadi na yalitekelezwa kwa njia tatu. Kutengua mifumo ya sheria, matumizi ya kazi za shokoa na utozaji wa kodi ya kichwa kwa nguvu.

Kuanzishwa kwa taasisi za sheria za Kizungu kwa kawaida kulifanutwa kwa kuzingatia sheria za jadi za Kiafrika na za Kiislamu pale ambapo zilikuwepo kama vile katika nchi ya Somali ya Waitalia; lakini hata hivyo taasisi hizo za Kizungu zilisababisha kurekebishwa kwa taasisi za jadi. Mara kwa mara kulikuwa na jitihada a kuwa na taratibu mbili za kutoa hukumu ambapo katika kesi za madai zinazowahusu Waafrika zilihukumiwa kulingana na taratibu za sheria za kijadi, wakati ambapo kesi za jinai na madai zilizowahusu Wazungu ziliangukia kwenye utaratibu wa mahakama za kikoloni.

Walakini, kila mahali, ukiondoa makoloni ya Kireno, mfumo wa mahakama ulikuzwa na kutekelezwa kulingana na mahitajio ya Waafrika kama yalivyoonekana machoni mwa Wazungu. Katika mwongo wa kwanza wa karne hii kulikuwa na jitihada maalumu za Wataliani katika nchi ya Somalia na Wajerumani katika Afrika ya Mashariki kupanua kazi za kutoa hukumu za machifu wa Kiafrika au mahakimu. Katika kipindi hicho hicho moja kati ya jitihada kama hizo iliyokuwa na mafanikio na fasaha zaidi ilikuwa ile ya Lugard ya utekelezaji wa "Baraza la Wenyeji" ambalo katika fikra zake lilikuwa ni chombo cha "kujenga tabia ya uwajibikaji na kukuza kati ya jamii ya Kishenzi tabia ya nidhamu na heshima kwa utawala". Mabaraza haya yakiwa yanaongozwa na Waafrika na kuelekezwa hasa katika shughuli za wenyeji, yalitakiwa yawe karibu iwezekanavyo na sheria za jadi za Kiafrika, na kufanyiwa marekebisho pale ambapo mila za msingi hazikuandamana na kawaida za msingi za Kiingereza. Kielezo cha Lugard kilianzishwa katika milki nyingi za Kiingereza na nchi za udhamini na pia kuigwa na Wabelgiji katika nchi ya Kongo.

Mfumo tofauti na huu ulikuwa ule wa Wafaransa ambao ulikusudiwa kubomoa utawala wa Kiafrika na hatimaye kumfanya afisa tawala kuwa afisa mwajibikaji wa hukumu. Walakini jambo la ajabu na lisilo la usawa katika mfumo wa Wafaransa ililikuwa ni *Indigenat* (Baraza la Wenyeji). Likiwa limeanzia huko Algeria katika miaka ya 1870 baraza hili liingizwa Afrika ya Magharibi ya Wafaransa katika miaka ya 1880 na kudumu kutumika na nchini Algeria hadi mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili. Kwa mujibu wa marekebisho yaliyomo katika tamko la 1924, tamko lilimhusu Afisa tawala wa Ufaransa yeyote kuweka adhabu hadi kufikia kifungo cha siku kumi na tano au faini kwa makosa mbalimbali kuanzia kushindwa kulipa kodi kwa wakati hadi kuonyesha dharau kwa maafisa wa Kifaransa.

Jambo ambalo athari yake ilipenya kila mahali kuliko mfumo wa sheria lilikuwa ni kodi za kichwa ambazo kila Mwafrika mwanamume aliyekuwa mtu mzima hatimaye

alipambana nazo. Ikiwa hasa zimebuniwa kama kigezo kimojawapo cha kufanya shughuli za kikoloni kujilipia zenyewe, zilifikiriwa pia kuwa zingeliwalazimisha Waafrika kuingia kwenyevitega uchumi vya Kizungu na kupanua uchumi wa fedha. Hadi kufikia mwanzoni mwa karne ya ishirini kodi hizi zilirekebishwa kwa vile hapakuwepo na taasisi yoyote ya kikoloni ambayo ilipitia kile kilichoonekana kama duara dhahiri la maendeleo. Kodi ya "Kibanda" ilikuwa ndio mfumo katika miaka ya mwanzo ya utawala na ilikuwa ndio chanzo cha ukaidi na ukinzani. Kwa ujumla kodi ya kibanda ilibadilishwa katika mwongo wa pili wa karne ya ishirini na kuanzishwa kwa kodi ya kichwa ambayo ilidumu kama mfumo mkuu hadi mwishoni mwa utawala wa kikoloni. Mwishowe kulikuwa na kodi ya mapato, iliyoanzishwa katika miaka ya 1920 katika makoloni mengi ya Kiingereza na Kongo ya Wabelgiji, lakini basi kimsingi iliathiri wasio Waafrika ambao kwa ujumla ndio pekee waliokuwa na mapato ya kutosha yaliyowafanya watakiwe kulipa kodi hiyo.

Ndani ya ruwaza hii ya ujumla kulikuwa na tofauti nyingi za kimkoa mojawapo ikiwa ile inayohusiana na fikra za Lugard kuhusu utawala wa jadi. Kama alivyoandika katika kitabu chake Dual Mandate "Kodi..... ni kama msingi wa mfumo mzima, kwani hutoa uwezo wa kumlipa Emir na maafisa wake. Taasisi iliyotumika kutekelezea jambo hili ilikuwa ni "Hazina ya Wenyeji". Wazo lilibuniwa na Sir Charles Temple aliyefanya kazi chini ya Lugard huko Nigeria ya Kaskazini. Kila tawala ya wenyeji ilikuwa irudishiwe asilimia fulani ya kodi zilizokusanywa katika wilaya yake. Kiasi hiki kilikuwa kiunde sehemu ya Hazina ya wenyeji ambayo iliongezewa zaidi mfuko wake na vitu kama ada mbalimbali za leseni na faini zilizokusanywa katika mabaraza ya hukumu. Kutokana na hesabu hii Emir au Chifu alitakiwa achote kiasi cha matumizi yake na kutoa mishahara ya watu walio chini yake. Kiasi kilichobaki kilikuwa kitumike kwa ajili ya huduma za jamii na matengenezo. Mpango huu ambao kwa asili ulitumika katika eneo la utawala wa Emir, ulienezwa na utawala wa kupitia kwa wenyeji sio tu katika milki za Waingereza katika pwani zote mbili badi pia katika Kongo ya Wabelgiji.

Katika nyenzo zote za kikoloni, mfumo wa kodi ndio kwa uhakika iliotia nguvu maendeleo ya urasimu wa utawala wa kikoloni. Katika mfumo huo afisa tawala alikuwa na kazi sawa na Chifu wa Kiafrika ambaye katika kukadiria na kukusanya kodi mara nyingi akisaidiana na halmashauri za wenyeji za Wazee au watu maarufu, alimkumbusha kila mmoja madaraka ya kitawala ya utaratibu mpya. Zaidi ya hayo wakusanyaji kodi baadaye walionekana kama wakala wa utawala na kuwa sehemu ya mabwana wa kikoloni. Watu miongoni mwao waliokuwa na mgogoro mkubwa bila shaka walikuwa ni maakida ambao walitumiwa na Wajerumani katika Afrika ya Mashariki. Hawa walikuwa ni maafisa waliokuwa wazungumzaji wa Kiswahili ambao walifanyakazi pwani kabla ya utawala wa Kizungu. Walitumika katika nyadhifa mpya za kukusanya kodi na kuandikisha vibarua kwa ajili ya utawala wa Wajerumani.

Kuanzishwa kwa kodi za pesa kuliambatana kwa kitambo kidogo na kodi za kazi, kielelezo dhahiri cha jitihada za Wazungu za kunyonya binadamu katika makoloni yao. Kodi ijulikanyo kama *Impot de Cueillete* ilikuwa ni kodi ambayo kwayo mpira mwitu ulivunwa katika Congo Free State na ndiyo kodi iliyoshutumiwa sana kati ya kodi za aina hiyo, ijapokuwa kodi ya Wafaransa iitwayo *Prestation* iliyodaiwa wanaume wote katika

Afrika ya Magharibi na ya Ikweta ya Wafaransa isipokuwa tu kama mtu ametoa fedha, ilidumu hadi mwaka 1944. Kinyume chake Wajerumani nchini Cameroon waliruhusu kodi iliyoshikwa kwa kila mtu ilipwe kwa kazi. Katika sehemu fulani za Uganda, Waingereza waliendelea na kodi ya Luwalo, kodi iliyokuwepo kabla ya ukoloni ya kufanya kazi mwezi mzima, hadi mwaka 1938, ambayo ilibadilishwa na kuwa kodi ya fedha. Hata hivyo kodi za aina hiyo zilikuwa badala ya shokoa zilizotumiwa na serikali zote za kikoloni.

Katika kuendelea kusumbuliwa na upungufu wa wafanyakazi kwa ajili ya miradi mipya na kazi mpya ambazo zilipendekezwa na utawala wa kikoloni, maafisa tawala wa Kizungu waliingiza ukandamizaji wao kabla ya mwisho wa karne kuptia mfumo wa ushokoa ambao mara nyingi ulikidhi haja za kibinafsi na zile za kijamii. Ni kweli kwamba ushokoa huo wa wazi ulipungua mwanzoni mwa karne ya ishirini kwa ajili ya kupungua kwa haja ya wapagazi pamoja na kuchelea malalamiko ya kimataifa kuhusu swala hili. Lakini japo matumizi yalirekebishwa, kazi hizo zilibaki kama sehemu muhimu ya utawala wa kikoloni hadi Vita vya Pili. Walau hivi ndivyo ilivyokuwa kwa serikali za kikoloni za Wafaransa ambazo kama ilivyokuwa Afrika ya Magharibi, bado ilitumia idadi kubwa ya Waafrika kwa kupitia kodi ya *Prestation* hasa katika ujenzi wa reli hadi baada ya Vita Vikuu vya Pili.

Mifumo ya uonevu kupita yote ni ile iliyokuwepo katika koloni la Ujerumani la Kusini Magharibi ya Afrika na katika Muungano wa Afrika ya Kusini. Siasa za Muungano bila shaka zilienezwa huko Kusini Magharibi mwa Afrika wakati ilipokuwa nchi ya udhamini baada ya vita. Lakini siasa za Wajerumani kabla ya hapo zilifanana kwa asili na uzito na zile zilizobuniwa na Muungano. Sheria za vibali ziliwekwa na vitambulisho pia, zote hizi zikiratibisha matembezi ya Waafrika. Waafrika ambao hawakuwa na mikataba ya kazi walikumbwa na sheria ya wazururaji na mikataba ya kazi ilibuniwa ili kumpa mwajiri wa Kijerumani manufaa makubwa. Katika Muungano, kulikuwa pia na sheria za vibali na sheria za kupinga uzururaji. Sheria ya wenyeji, *Native Administration Act,* (Maeneo ya Miji), ya mwaka 1923 na sheria za utawala wa wenyeji ya mwaka 1917 zilisisitizia sheria za awali za vitambulisho wakati sheria nyingine kama vile Apprenticeship Act, (Sheria ya Uanagenzi) ya mwaka 1922 ilibana kikamilifu aina za kazi ambazo kwazo Mwafrika anaweza kuajiriwa.

## *Vyombo vya Udhibiti na Utawala*

Kama walubiri wao wa dhati waliyopendelea kusema utawala wa kikoloni ulipatikana kwa ncha ya upanga na kudumishwa kwa nchi ya upunga. Zikiwa na fikra hii kichwani serikali zote za Kizungu zilianzisha majeshi yaliyoandikishwa kutokana na wenyeji. Ijapokuwa utaratibu na ubora ulitofautiana kulingana na haja za mkoa na nchi, majeshi hayo ya kikoloni kimsingi yalifanya kazi za kipolisi katika vipindi kati ya vita na walishirikiana na vikosi vilivyoundwa baadaye vya kipolisi katika wadhifa huo.

Lakini kwa kuwa kila mara walilazimishwa kufanya kazi kwenye maeneo ambayo yalikuwa tofauti na kwao kimila na Kimbari, wanajeshi wa Kiafrika walikuwa wametengwa najamii zao na mara nyingi walikuwa wanapokelewa kwa chaki na wenyeji waliopmbana

nao kwa nguvu. Kutokana na hali hii kadhalika kutokana na Wazungu kuwanyima Waafrika nafasi ya kushika kazi za madaraka, jeshi halikuweza kujihusisha na siasa katika vyama vya kupigania uhuru kama walivyofanya wenzi wao huko Asia na Mashariki ya Karibu.

Walakini hata katika kipindi kati ya vita kilichojulikana na watu wa wakati huo kama kipindi cha "amani ya kikoloni" shughuli za kijeshi bado ziliingilia sana shughuli za Waafrika. Nia iliyohubiriwa na watu wa Ulaya ya kuweka Afrika huru kabisa kivita kwa kweli haikuweza kufikiwa. Wafaransa walianzisha sheria ya kuandikisha askari kwa lazima mnamo mwaka 1919 ambapo kiasi cha Waafrika 10,000 walitakiwa kupatikana kila mwaka. Waingereza walianzisha *Sudanese Defence Force* (Jeshi la Ulinzi la Sudan), likiwa na maafisa wa Kisudani na Kiingereza lakini kimsingi likiwa limeelekezwa kwenye haja za msingi za kifalme huko Mashariki ya Karibu kadhalika na Afrika ya Mashariki.

*Force Publique* (Jeshi la Serikali) la Kongo ya Wabelgiji likidhihirisha tabia za jeshi la kumiliki na jeshi la polisi lilikuwa kila mara linatumwa katika enzi hii kuzima upinzani ambao ulikuwa umejitokeza kwa mfumo wa chama cha dini mbalimbali.

Taarifa hii ya maendeleo ya kijeshi katika Afrika katika kipindi kati ya vita haidhoofishi madai kwamba makusudio potofu ya njia na vitendo vya kikoloni ni yale ambayo hapo awali yalionekana bora sana. Hakuna shaka kwamba ujenzi wa urasimu wa kikoloni umetoa maandalizi ya vyama visivyokusudiwa na kuelekea kwenye uhuru wa kitaifa. Watu bora wapya wa kisiasa wakiwemo makarani wa ngazi za chini na machifu wateule katika huduma mbalimbali za kikoloni walikuwa wanajitokeza polepole hasa katika makoloni ya Waingereza. Shule za mafunzo kama ile ya Ecole William Ponty mjini Dakar zilifanya matayarisho ya wakufunzi na maafisa tawala ambao walitegemewa sana na utawala wa kikoloni. Kimsingi katika maeneo ya mijini "Wimbi la mabadiliko" lilikuwa linaanza kujitokeza.

Bado haya siyo yale ambayo maafisa tawala wa kikoloni waliyoyakusudia. Hata ikiwa walisisitizia juu ya "Utukufu wa wenyeji" walifanya hivyo kwa fikra kwamba ustawi wa jamii wa Waafrika unaweza tu kuwa hakika na kuundwa barabara kijamii na kiuchumi na wao. Kama alivyosema Lord Cromer, Serikali safi na Serikali huru zilikuwa zinapinga kimalengo katika muktadha wa ukoloni. Kwa hiyo mfumo wa kikoloni ulikuwepo kama mtindo wa kiimla na kamwe haukuwa umeukiliwa kutoa madaraka ya kisiasa kwa Waafrika ambao ulisemekana kuwatumikia. Tabia yake kuu ilikuwa ya ubaba, uliokubali kuwepo kwa mgawanyiko wa madaraka, ilipokuwa hapana budi pale tu ambapo kulikuwa na idadi ya masetla wa Kizungu.

Hata mahali ambapo taasisi za Bunge zilianzishwa ili kutoa namna fulani ya serikali ya madaraka ya kikoloni, utaratibu huu uliwekwa ili kuimarisha nguvu za weupe. Nchini Algeria kwa mfano, mfumo wa jamii mbili za wapiga kura ulioidhinishwa kwa sheria za Jonnart ya mwaka 1919 ulitoa nafasi chache kwa Waarabu kuliko Wazungu katika *Delegations Financieres* (Bunge la Wafadhili) chombo cha kwanza cha Bunge kinachowakilisha makundi ya kimaslahi na sio eneo la uchaguzi. Katika Afrika ya Kusini, Mwafrika hakushiriki hata kidogo katika utaratibu wa Bunge ulioanzishwa kule. Sheria ya *"Representation of Natives"* (Uwakilishi wa Wenyeji) ya 1936 iliwaondosha kabisa

Waafrika katika orodha ya wapiga kura na kufanya hadhi yao kisiasa katika nchi nzima kiasi kwamba walibakia tu na uwezo wa kuwachagua Wazungu wachache kuwakilisha "maslahi ya wenyeji". Katika makoloni haya makubwa mawili ya Masetla kama ilivyo katika makoloni mengine ambamo kulikuwa na wakazi wa Kizungu wale walionekana walikuwa wachache kiidadi lakini wengi kisiasa kinyume kabisa cha serikali ya kidemokrasi katika mfumo wa kizungu.

Tofauti za mbinu za kikoloni hazikuwa muhimu kihistoria kama ilivyokuwa kufanana katika kutathmini hali ya kikoloni. Mbali na matamko yaliyohifadhiwa katika nyaraka za Umoja wa Mataifa, pamoja na kutojali nafasi yao kiulimwengu iliyodhoofishwa na vita ya dunia, serikali za Kizungu katika Afrika hazikushughulikia mawazo ya Uhuru wa kisiasa wa Waafrika katika kipindi kati ya vita. Ukiondoa Misri, Afrika ilionekana kama Kontinenti ambalo ukoloni utakaa kwa muda mrefu, na mbinu za kikoloni ziliundwa ili kukidhi maslahi na makusudio ya kizungu. Kwa hiyo shughuli muhimu ya kisiasa ilikuwa ile ya kumrekebisha Mwafrika kufuata malengo ya Kizungu, bila kujali kama shughuli fulani ya kikoloni iliyofuatwa ilikuwa ya kuzunguka au la.

Jambo muhimu kupita yote katika maendeleo ya kihistoria ya kipindi kati ya vita lilikuwa ni jinsi mfumo wa kikoloni ulivyoanzisha mfumo wa kijumla wa utawala ambamo serikali za kitaifa zitaingizwa ndani katika mwongo wa kwanza wa uhuru. Marekebisho haya ya mwanzo ya shughuli za kisiasa katika muundo ulioandaliwa na Wazungu ulikuwa ndio mpango mkuu wa kufeta maendeleo ya kisiasa ambayo yalianzishwa na Wazungu, lakini kwa ajili ya matumizi yao katika Afrika ya wakati huo.

# 14 Uchumi wa Kikoloni

## *Kutamalaki na Uhusiano Mpya wa Uzalishaji Mali: 1880-c.1910*

Katika muda huo huo ambapo serikali za kikoloni zilikuwa zinaanzisha taasisi na miundo mbalimbali kwa ajili ya utawala wa makoloni yao, ilikuwa pia inaanzisha mfumo wa kiuchumi kwa ajili ya kunyonya mali asili za makoloni hayo. Mfumo wa kiuchumi wa kikoloni haukufikia upeo wake hadi majilio ya Vita vya Pili vya Dunia.

Waafrika walishuhudia ushahidi wa kwanza ulio dhahiri wa uchumi mpya katika sura ya ujenzi wa barabara, reli na simu. Mawasiliano na njia za simu vilikuwa ndio msingi wa ushindi na vilikuwa ndio zana muhimu sana katika maeneo yaliyomilikiwa ili baadaye yawe kianzio cha mashambulizi zaidi. Walakini, barabara na reli chache sana zilitumiwa kivita; na reli hizo ambazo zilirahisisha kutamalaki zilitumika kwa usafirishaji wa karanga, pamba na kadhalika.

Uchumi wa Pwani ya Afrika kwa haraka ukafanywa utegemee uchumi wa serikali ya kikoloni inayotawala na wakati huo huo watu wa bara kwa kawaida walikuwa wa mwisho kuingizwa katika mfumo wa ukusanyaji wa mazao, uzalishaji wa mazao ya biashara na kazi za ujira. Kiasi kikubwa cha fedha kilitakiwa ili kuzijengea baadhi ya bandari za Afrika vina virefu karibu na gati na uwezo thabiti wa kupakulia mizigo; lakini huu haukuwa mzigo mzito kuliko mtaji uliotumika katika utengenezaji barabara na reli za kwenda bara. Kwa hiyo umbali kutoka pwani ulikuwa moja ya vigezo vya uamuzi wa kuona ni mapema kiasi gani uchumi wa kikoloni utaanzishwa.

Jambo muhimu sana lililoathiri kuanzishwa kwa uchumi wa kikoloni lilikuwa ni kwa kiasi gani sehemu mbalimbali za Afrika zilikuwa tayari zinashiriki katika uchumi wa dunia. Kanda za utumwa kutoka Senegal hadi Sierra Leone, kutoka Gold Coast (sasa Ghana) hadi Nigeria na kutoka Mto Kongo hadi Angola zilikuwa ni kanda za pwani za kwanza kuvamiwa na wakoloni wa Kizungu. Katika maeneo haya, faida za uchumi za kikoloni zilizuka hata kabla majilio rasmi ya utawala wa kikoloni, kwa sababu ya jitihada za pamoja kati ya Waafrika na Wazungu za kushamirisha bidhaa za kusafirisha nchi za nje ambazo zilikuwa vibadala "halali" vya watumwa. Watawala, wafanyabiashara mabingwa na sekta nyingine za wananchi katika Afrika ya Magharibi waliona faida katika kudumisha mkataba wa biashara ya nje na uwezo wa kupata bidhaa za nje.

Katika upande wa Mashariki mwa Kontinent, biashara katika bahari ya Hindi haikuwa hasa imeelekezwa kwenye nchi za Ulaya, na wala biashara ya masafa marefu nje ya Afrika Mashariki haikuwa imetawaliwa na Wazungu au Machotara wa Kizungu. Wakoloni ilibidi wachukuwe nafasi za wafanyabiashara wa Kiarabu, Kiswahili na Kihindi.

Wakianzia safari yao kutoka miji ya pwani ya Waswahili, wakoloni wa Kizungu walifuata njia waliyopitia Waarabu wakitafuta kituo cha mwisho cha njia za misafara katika mkoa wa Ziwa hadi kufikia miaka ya 1880, Mnyang'anyiro ulikuwa umeanza katika eneo la Ziwa Vikctoria ambapo katika pwani zake vitega uchumi vya kikoloni vilikuwa vinaanzishwa haraka dhidi ya shughuli za biashara zilizokwisha kuwa za hali ya juu za uchumi wa Kiafrika. Baada ya Waingereza kumaliza ujenzi wa reli yao kutoka Mombasa hadi Ziwa Viktoria mnamo mwaka 1902 reli ikavutia kwa haraka uchukuzi wa mizigo ambayo zamani ilikuwa ikipitia katika misafara iliyokuwepo Kusini zaidi huko Tanga na Bagamoyo. Kutokana na mashindano ya Waingereza, Wadachi nao wakaanzisha reli ya kutoka pwani hadi bara mnamo mwaka 1905 na hii ilipitia katika njia za watumwa na pembe za ndovu hadi Ziwa Tanganyika. Na huko ndani kabisa mwa Afrika ya Kati pia ni njia za biashara ya Waarabu ambayo iliwapa wakoloni wa Kizungu msingi wao wa awali wa kiuchumi.

Afrika ya Kaskazini ilijumuisha baadhi ya sifa za Mashariki na Magharibi mwa Afrika na kuziweka katika kiwango cha juu. Mwnazo wa ukoloni wa Kizungu huko Misri unarudi nyuma tangu safari ya *Napoleon* ya mwaka 1798. Kuwepo kwa Wazungu katika karne ya kumi na tisa kulivuruga uvumbuzi wa kiuchumi wa Mohammad Ali. Baada ya kuchangia katika kushindwa kwa ukuzaji viwanda vya Misri, Waingereza na Wafaransa walitafuta mbinu za kutawala na kudhibiti biashara ya Wamisri na kujiingiza katika biashara ya ndani katika maswala ya ardhi na rehani. Nchini Algeria ukinzani mkali dhidi ya Wafaransa ulikuwa bado haujaisha katika miaka ya 1870, lakini katika wakati huo nchi ilikuwa tayari imekwishaingiliwa na kilimo cha Kisetla ambacho kilikuwa ndio sifa kuu ya uchumi wa kikoloni wa Algeria na ambacho kilijitokeza katika viwango mbalimbali katika sehemu zilizobaki za Maghreb na Libya. Tunisia iliingia katika enzi ya ukoloni mnamo mwaka 1881/82 ambapo Moroko na Libya zilikuwa zimeungana nusu mnamo mwaka 1912. Wahamiaji wa Kiitalia nchini Libya walikuwa wachache kuliko wenzao Wafaransa huko Maghreb, na Kilimo cha Masetla huko Tripolitania kilibaki kusubiri kushindwa kikamilifu kwa wananchi wa Libya kwenye miaka ya 1931. Serikali za Kizungu zilifanya shughuli za kiuchumi za Afrika Magharibi kuwa tegemezi kwa kupitia nguvu za Mtaji wa fedha. Afrika ya Kaskazini iliingia kwenye enzi ya ubeberu wakati kiasi kikubwa cha mtaji kilitumika kutegea uchumi katika mfereji wa Suez na wakati ambapo mikopo ilikuwa inatolewa kwa tabaka tawala kutoka Misri hadi Moroko. Hali hii ilifikia upeo wake mnamo mwaka 1880; hali ambayo ilizifanya serikali za wenyeji kulazimika kuwatii wakoloni na hatimaye kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni na moja kati ya mataifa ya Ulaya yaliyopendezewa. Kwa hiyo japo uchumi wa kikoloni ulikuwa na mwanzo wa kipindi kirefu huko Afrika ya Kaskazini, hatuwezi kusema kwamba ulikuwa kweli umeanzishwa hadi ilipofika miaka ya 1890 wakati mtaji wa kuhodhi ulipokuwa umeshamiri huko Ulaya. Huko Kusini mwa Afrika pia mambo yalikuwa hivyo hivyo.

Hadi ulipofika wakati wa mgawanyo wa kibeberu, makazi ya Wazungu huko Afrika ya Kusini yalikuwa ya makumi ya maelfu ya Wazungu waliokuwa wamedumisha uhusiano wa kiuchumi na Waafrika. Uhuru wa kiuchumi wa Waafrika ulidhoofishwa kwa njia ya kunyang'anywa ardhi na wafanyakazi wa Kiafrika kuwekwa chini ya amri ya Wazungu. Mnamo karne ya kumi na tisa, Wazungu na Waafrika "walijihusisha katika

kuunda mikataba mipya ya kiuchumi na kijamii". Mikataba hii mipya awali ya yote ilikuwa ya kikoloni tu kwani iliwaunganisha pamoja wageni wachache na wenyeji walio wengi katika uhusiano wa mabwana na watwana. Lakini punde si punde mikataba hii ikiwa ni uhusiano wa kikoloni uliosababishwa na kuingizwa kwa mitaji mikubwa kutokana na kugunduliwa kwa almasi na dhahabu.

Uchimbaji wa almasi na dhahabu nchini Afrika Kusini usingeweza kufanyika bila ya teknolojia ya kisasa na vile vile mitaji mikubwa. Sio serikali ya Uingereza wala makampuni pekee ya madini yaliyoanzishwa tangu miaka ya 1870, ambayo yalikuwa na nia ya kuacha rasilimali ya madini kwenye madaraka ya Makaburu au kutoa kipaambele kwenye makampuni ya kilimo cha kisetla yenye ardhi yenye rutuba, maji, malisho na ng'ombe wakati ardhi hafifu na wafanyakazi wa Kiafrika walitumainisha upatikanaji wa ziada kubwa ambayo ingesafirishwa Ulaya. Baada ya Ugunduzi wa almasi ya Kimberly (1870) na hasa baada ya mgomo wa machimbo ya dhahabu wa Witwatersrand (1886), mabwanyenye walikusudia kutawala mifumo yote ya kijamii iliyokuwepo kabla ya ubepari nchini Afrika ya Kusini bila ya kujali utaifa. Vita baina ya Waingereza na Makaburu (1899-1902) vilikuwa pia vya kupinga ubeberu ijapokuwa kwa nia ya kupotosha kwani wakati huo huo walipigania uimarishaji zaidi wa ukoloni wa Kisetla. Kushindwa kwa majaribio ya Makaburu ya kuweka utawala wa Kisetla na kuangamizwa kwa Waafrika wa eneo hilo kama ilivyojadiliwa kwenye sura ya 9 ndio chanzo cha ujenzi wa uchumi wa kikoloni wa Afrika ya Kusini ambao bila shaka yoyote, ulikuwa umeelekezwa kwenye uhamishaji wa mali ghafi, faida na pembejeo nyingine hadi Ulaya.

## *Mtaji na Nguvu C. 1900 - C. 1920*

Ukinzani wa Waafrika ulisaidia kimsingi kupunguza kasi ya ukoloni wa kiuchumi kwa kiasi cha miongo mitatu kati ya 1880 na 1910. Zaidi ya hayo, upendeleo wa kufanya hivyo kwa upande wa mtaji wa kuhodhi wa kizungu ulikuwa mdogo. Afrika ilipata kipaambele wakati wa enzi ya wafanyabiashara ya kulimbikiza, lakini hali ya wasiwasi ya karne ya kumi na tisa iliendelea kuwepo katika miaka ya mwanzoni ya ukoloni, pamoja na kuwepo kwa ongezeko katika udhibiti wa kisiasa - kiuchumi ambao ulifuata baada ya mgawanyo na kutamalki. Ikitazamwa katika haja ya kiulimwengu ya kutega uchumi ya ubepari wa kuhodhi hadi kufikia Vita vya Kwanza vya dunia, takwimu zinazohusu ukuaji wa uchumi na kikoloni wa Kiafrika haziridhishi. Muhimu katika takwimu hizi ni zile zilizohusu bidhaa za kuingiza nchini na za kusafirisha nje, kwani sekta hiyo ilikuwa ndiyo sifa muhimu ya uchumi wa kikoloni. Kiasi cha mizigo iliyoingizwa nchini kipi kilipanda polepole sana na kubakia kilivyo kama ilivyokuwa katikati mwa karne ya kumin na tisa, na hakikutofautiana sana na hali ilivyokuwa wakati wa enzi ya utumwa. Nguo za pamba ziliendelea kutawala biashara ya kubadilishana kati ya Ulaya na Afrika katika kipindi chote kilichotajwa, ijapokuwa vifaa vingine vya matumizi ya nyumbani kama vile vifaa vya jikoni, radio, baiskeli na mashine za cherehani baadaye vilipendwa sana.

Uzalishaji wa bidhaa za kuuza nchi za nje katika Afrika uliongezeka polepole na sio kwa uthabiti kila mara. Grafu ya kawaida ya uzalishaji wa mazao ya chakula ya Afrika

katika mfumo wa kikoloni katika hatua yake ya kwanza ilikuwa na kiasi kidogo katika kipindi chote cha miongo miwili ya karne hii, ikifuatiwa na hatua ya pili yenye ongezeko la kuridhisha hadi mwaka 1930. Pamba, mafuta ya chikichi, kahawa, karanga na kakau vinadhihirisha hali hiyo katika maeneo yanayohusika katika kontinenti.

Kiasi kidogo tu cha fedha za kigeni kilitumika katika viwanda vya Afrika na kilimo katika kipindi cha mwanzo cha ukoloni. Afrika ya Kusini ilikuwa kwa mara nyingine mfano dhahiri wa kinyume cha sehemu nyingne. Kwa kiasi fulani Algeria nayo ilivutia mitaji ya kisetla na madini. utumiaji wa nguvu wa wazi au kwa kujificha nyume ya sheria za serikali mpya za kikoloni ndio kimsingi uliohusika na kuleta wafanyakazi na mazao ya biashara sokoni. Mitindo ya wazi ya kazi za ushokoa na mitindo fiche ya utumwa kama vile "Ajira za Mikataba" zilizotumiwa na Wareno nchini Sao Tome au Kongo chini ya Mfalme Leopard ilikuwa ni mambo maarufu katika kuimarisha uchumi wa kikoloni katika Afrika.

Mwanzoni mwa utawala wa kikoloni, wakati mwingine mitaji ya binafsi ilifanya kazi za kipolisi na kuwashurutisha watu kwa niaba yao wenyewe. Hivi ndivyo ilivyokuwa katika makampuni yaliyokodiwa na kuruhusiwa ambayo yalikuwa madhubuti katika Afrika ya Kusini na Kati na nchini Nigeria na Afrika ya Mashariki iliyo chini ya Wajerumani. Walakini makampuni yaliyokodiwa hayakumudu shughuli za serikali za kutumia nguvu. Kwa hiyo nchi za Ulaya zilibidi kuchukua madaraka moja kwa moja katika makoloni yao hasa katika miaka ya 1890; serikali za kikoloni zilizoanzishwa nchini zilisimamia uchumi kwa niaba ya mabepari binafsi. Mabepari binafsi walipewa fidia kwa kuachilia mbali marupurupu yao ya kisiasa na hivyo kuonyesha wazi maslahi gani ya kitabaka yalikuwa yanatekelezwa na serikali za kikoloni. Ulipaji wa fidia ulikuwa ndiyo njia ya kutoa fedha kwa makampuni hayo ili yaweze kuimarisha vema vitega uchumi vyao kuliko ilivyokuwa wakati walipokuwa kwenye hali ya kivita na Waafrika.

Serikali za Ulaya na serikali zao wenza katika Afrika zilibidi ziendelee na matumizi ya nguvu za kiserikali kwa ajili ya unyonyaji wa kiuchumi, kwa vile uchumi wa kikoloni ulitakiwa uendelee kutiliwa nguvu kutokana na upinzani uliokuwa ukitoka kwa Waafrika. Katika sehemu kadhaa ilibidi ardhi ya Waafrika ikamatwe kwanza kabla ya mifumo ya kijamii na kiuchumi ya kisetla kuweza kustawi. Njia za barabara na reli ziliweza kujengwa tu kwa msaada wa serikali na njia mojawapo ilikuwa ni kuwaandikisha wafanyakazi wa Kiafrika kwa nguvu. Matumizi ya utozaji kodi ili kujenga uchumi na fedha ni nyenzo iliyojulikana sana ambayo haina haja ya kujadiliwa kwa urefu hapa. Utozaji wa kodi bila shaka lilikuwa jambo muhmu katika kuwasukuma Waafrika hasa kwenye kazi za ujira au uzalishaji wa mazao ya biashara. Ongezeko la kodi lililotokea baadaye liliwadidimiza zaidi Waafrika kwenye shughuli hizi.

Serikali za kikoloni zilitofautiana kulingana na aina ya nguvu waliyotumia katika makoloni yao. Mabaki ya utumwa yaliyokomeshwa kwa sababu yalipitwa na wakati. Upigaji viboko na kutumia vibaya miili ya Waafrika kulikofanywa na waajiri kwa Kizungu kulichukiwa sana na kwa kawaida kutungiwa sheria dhidi yake katika mwongo wa pili kwa karne hii. Serikali za kikoloni, kama ilivyo katika serikali nyingine, zilijaribu kudumisha zenyewe pekee uwezo juu ya mbinu za kisheria za kimabavu. Wakati huo huo, walitaka

kuwahakikishia tena wategaa uchumi wa Ulaya na masetla kwamba mamlaka ya serikali bila wasiwasi yalikuwa kwa ajili yao. Kwa hiyo badala ya upigaji viboko kwa amri ya waajiri kulikuwa na upigaji viboko kwa amri ya hakimu ambao ulitumika sana kuliko ulivyotumika kwa wafanyakazi wa Ulaya. Masharti ya kazi kwa Waafrika yalibaki kduni katika kipindi chote cha miaka ya 1930; kosa la kuvunja mkataba lilishughulikiwa sio kama kosa la madai bali kosa la jinai.

Mchanganyiko wa mtaji kwa Ulaya na kazi za ushokoa za Waafrika ulitoa ziada kubwa katika mazao yaliyokusudiwa kwa matumizi ya Ulaya na kwa ajili ya kusafirisha nje. Mazao na madini yalisafirishwa nje na faida iliondoshwa nchini kwa vile mitaji katika makampuni ya madini na mashamba makubwa pamoja na makampuni ya kutoa na kuingiza bidhaa haikuwa ya wenyeji. Hata hivyo, kiasi fulani cha fedha iliyokusanywa kilitumika tena katika vitega uchumi. Hali hii iliruhusu mitaji ya Afrika ya Kusini kuwa mikubwa sana, kadhalika hali hii ilihharakisha umilikaji wa pekee miongoni mwa makampuni ya biashara ya Afrika ya Magharibi, na kuyawezesha kusaidia na kuunganika na makampuni ya uzalishaji na usambazaji ya Ulaya. Nchini Algeria na Afrika ya Kusini na kwa kiasi fulani nchini Tunisia, Kenya, Rhodesia zote mbili (Zambia na Zimbabwe na Nyasaland (sasa Malawi), mtiririko wa fedha wa awali kutoka uchumi wa kikoloni pia ulileta hali nzuri ya maisha pamoja na uwezo mkubwa wa kiuchumi kwa Masetla wa kizungu.

## *Kushiriki kwa Waafrika katika Uchumi wa Kikoloni 1920-1930*

Matumizi ya nguvu katika uhusiano wa kiuchumi yalikuwa thabiti katika miaka ya ujenzi wa uchumi wa kikoloni katika Afrika lakini ukaendelea kupunguza umuhimu wake, kwanza katika makoloni ya Waingereza na Wajerumani yakifuatiwa na yale ya Wafaransa na kisha ya Wabelgiji na Wareno.

Kila mara Waafrika waliuchukulia uchumi mpya wa kikoloni kama suala muhimu la maisha - utaratibu mpya ambao wasingeweza kuubadili na ambao kwa namna nyingi walikuwa tayari kuupokea. Hata hivyo awamu mpya ilianza katika miaka ya 1920 wakati Waafrika walipoanza kuonyesha athari zao katika mambo mengi yaliyowahusisha katika uchumi huu. Katika kipindi hiki waliendelea kutekeleza majukumu yao kama waajiriwa katika machimbo ya madini nchini Afrika ya Kusini na katika mashamba makubwa kwenye nchi za Kongo na Afrika ya Mashariki na Kati. Vibarua hawa walishawishiwa kutoka mbali. Tanganyika (Tanzania) iliingiza watu wengi kutoka Nyasaland, Rhodesia ya Kasakzini (Zambia) Msumbiji na Rwanda - Urundi (sasa Rwanda na Burundi).

Walakini, vibarua hawa walikuwa sehemu kidogo tu ya jamii nzima ya Waafrika watu wazima. Bila shaka kilimo cha mazao ya biashara kilichukua sehemu kubwa ya Waafrika na kuweka singi kwa kile kilichoitwa *economie de traite* (Mfumo wa uchumi ambao bidhaa zilizoagizwa toka nje zilikuwa zinabadilishwa kwa mazao ya biashara ambayo yalikuwa ghafi au yaliyotengenezwa kidogo). Mazao ya biashara yaliwapa Waafrika nafasi kubwa kidogo ya kufanya mambo yao kuliko kazi za ujira. Wakati mwingine kulikuwa na uchaguzi baina ya mazao ya kusafirisha nje. Mazao ya chakula yalipandwa kwa ajili ya matumizi ya familia, wakati mwingine kwa ajili ya kuuza mitaani

na mara chache sana kwa ajili ya kuuza nchi za nje. Wakulima wa Kiafrika walitumia nafasi hii finyu katika kuamua aina na kiasi watakachopanda au watakachotayarisha kuuza nje. Bei zilikuwa zinapangwa na mawakala wa nchi za Ulaya, lakini hata hivyo bei za mazao ya kilimo hazikuathiriwa sana wakati wakulima walipoamua kubadilisha mazao ya kulima au kupeleka mazao yao kwenye soko la wenyeji. Mambo yaliposhindikana sana wakulima walitumia mbinu "Kuchelewesha" uuzaji wa mazao yao, hata kama hali hii ingemaanisha hasara kubwa kwa upande wao.

Wakati kilimo cha mazao ya biashara kilikuwa bado kinaendelea kushurutishwa katika baadhi ya jamii za Kiafrika, Waafrika wengine walikuwa wanakiendesha kwa dhati huku wakikabiliwa na dharau na uhasama wa wazi. Walidai muundo-mbinu wa usafiri na masoko; wakaitumia vema nafasi mara tu ujenzi wa reli ulipomalizika. Mara nyingi, walipenyeza maeneo fulani mapema hata kabla serikali ya kikoloni haijajenga madaraja na barabara za kufikia huko. Mbegu kwa ajili ya mazao mapya zilichukuliwa kutoka kwa Waafrika wakoloni ambao walikuwa tayari wanajishughulisha na kilimo. Kakau na kahawa ndio mazao mawili ya biashara muhimu na yaliyojulikana sana na ambayo upanuzi wake ulitegemea aidi uwezo wa Waafrika. Mazao madogo kama vile chai, tumbaku na pareto kadhalika yalichukua msimamo huo huo. Zaidi ya hayo, Waafrika walipigania zaidi mazao ambayo yaliwapa fedha nyingi kuliko mengine. Kwa hiyo kipindi cha mwisho cha miaka ya 1920 na mwanzoni mwa miaka ya 1930 kulikuwa na juhudi za dhati kwa upunde wa Waafrika katika sehemu nyingi za nyanda za juu za Tanganyika za kupanda kahawa aina ya *Arabica* kuliko kwenda kwenye kazi za kuajiriwa au kupanda kahawa aina ya *Robusta* yenye kipato kidogo. Waafrika walishinda kwa kupanda mimea ya kahawa haraka zaidi kuliko ambavyo utawala wa kikoloni ungeliweza kuiharibu.

Sehemu ambayo kilimo cha wakulima wadogo wadogo kilijiimarisha kama sehemu muhimu ya uchumi wa kikoloni, kiliendeshwa kama ilivyo machimbo ya madini ana mashamba makubwa katika kuwaleta vibarua kutoka kwenye eneo kubwa zaidi kuliko ukanda halisi wa uzalishaji. Ukulima wa karanga wa Senegambia ulivutia sana manamba kutoka bara ya Mito Niger na Senegal; Kakau nchini Gold Coast (sasa Ghana) na nehini Ivory Coast zilipata manamba kutoka Upper Volta wakati kwakulima wa kahawa wa Uganda walipata manamba kutoka Ruanda - Urundi na Tanganyika ili kupanua kipato (angalia kielelezo 16.1). Kwa pamoja akulima wa mazao ya biashara na kazi za ujira au machimbo ya madini na kilimo ulikusanya Waafrika wengi walioshiriki moja kwa moja katika uchumi wa kikoloni. Hata hivyo shughuli nyingine nyingine zilikuwa zinaanzishwa au kurekebishwa na uhusiano mpya wa kiuchumi. Biashara ya mbao ilizuka nchini Gabon na katika viwango tofauti shughuli hizo za biashara ziliendeshwa mahali popote palipokuwa na hifadhi ya misitu. Njia za usafirishaji lilikuwa swala muhimu kwa ujumla. Maelfu ya Waafrika walipata kazi za ujira bandarini na kwenye magari moshi, hasa wakati upagazi wa kutumia kichwa ulipopungua baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia.

Wakati uchumi wa kikoloni ulipoanza kukomaa, hapakuwepo na hata sekta moja ya jamii ya Kiafrika iliyoacha kujishughulisha na uchumi. Paoja na kuwa na sifa ya kutopenda mabadiliko, vikundi vyote vya wafugaji viliigizwa katika uchumi wa fedha katika miaka ya 1920 au pengine kabla. Waliuza nyama kwa matumizi ya mitaani na mara

kwa mara kwa ajili ya kuuza nje pamoja na ngozi. Katika nchi ambazo baadaye ziliitwa Somalia hali hii ndiyo iliyokuwa utambulisho mkubwa wa uchumi kwa kikoloni. Waafrika kwa kawaida walijitoa wenyewe kufanya kazi ya kipato kilichowaletea faida na waliyopendezewa wao nayo. Maafisa tawala wa kikoloni, wamisionari na makampuni binafsi waliajiri makarani wa ngazi za chini, mafundi mchundo (kwa ajili makundi mawili mwanzoni) waalimu. Kichocheo cha kupata elimu kilikuwa ni kazi hizi, hasa kwa vile zilikuwa zinahusiana sana na maisha ya mjini yaliyokuwa yanazidi kupendwa. Watoro wa shule za msingi au wale ambao kwa sababu moja au nyingine hawakuweza kupata kazi bora za ujira walijaza pengo la uchumi wa kikoloni kama watumishi wa nyumbani au kama polisi au wanajeshi au kujiingiza katika shughuli za kihuni za mijini kama vile umalaya.

Ujira ulikuwa mdogo sana. Nyongeza ziliwekewa pingamizi, uwezo wa kununua vitu ulipunguzwa kwanza kwa sababu ya kushuka kwa dhamani ya fedha pili kwa sababu ya ujira mdogo au ujira kuachwa nyuma na kupanda kwa bei za vitu. Masetla ua wakazi wengine na mameneja wa vitega uchumi vya wageni waliungana ili kuweka ujira chini ua kufanya kazi iwe nusu umwinyi kwa kkutoa vipande ambavyo vilipunguza sana uhuru wa waajiriwa wa kubadili kazi kutoka mwajiri mmoja hadi mwingine. Katika kipindi chote kinachozungumziwa, waajiri walibaki kuwa maadui wa vyama vya wafanyakazi ambavyo vingesababisha upandaji wa kiwango cha ujira. utaratibu mbaya wa kazi au vipande vya kazi ulitumiwa sana na wafanyakazi hawakupewa marupurupu ya ugonjwa, ulemavu, kutoajiriwa na uzee. Hata hivyo uhamaji wa mara kwa mara wa kiasi kikubwa cha manamba, kiwango chao cha chini cha ujuzi wa kazi na kuenea kwa ubaguzi wa rangi, yote haya yaliongezea madhara kwa mfanyakazi Mwafrika katika kupambana na makabaila katika masuala ya ujira na *mazingira* ya kazi.

## *Utegemezi na Mpomoko 1930 -5*

Uhusiano wa uzalishaji wa kikoloni ulijengwa Afrika kwa kipindi fulani cha miaka, wukati ambapo chumi nyingi za kujitegemea za Waafrika zilikuwa ama zinatokomezwa na zinabadilishwa na kumilikiwa. Uhusiano kati yao ulivunjwa kama ilivyokuwa katika biashara ya kupitia Sahara na biashara katika ukanda wa maziwa ya Afrika Mashariki na Kati. Viango vilivyokuwapo hapo awali kati ya Afrika na sehemu zingine za dunia viliathiriwa vibaya sana, hasa vile vya India na Uarabu. Idadi kubwa ya chumi pekee za kikoloni zilijitokeza. Mgawanyo wa kiuchumi haakuwa sawa na mgawanyo wa kisiasa. Kwa vile serikali zenye nguvu za kibepari ziliyanyonya makoloni ya nchi dhaifu. Lakini Uingereza ilibidi ikubali kuingizwa kwa mitaji ya Marekani nchini Afrika ya Kusini baada ya kuandwa kwa Shirika la *Anglo-American* Corporation (Shirika la Waingereza na Wamerikani) mnamo mwuka 1917. Hata hivyo, mipuka nasibu ya kisiasa ilichukuliwa kama mipaka ya chumi, kila uchumi ulikuwa wa kiwango kidogo, sio yakini na kila mmoja akiwa umeelekezwa Ulaya. Chumi hizi zilikosa viungo vya kikontinenti, kikanda au vya ndani kwa ndani.

Kwa hiyo, kwa ufafanuzi, uchumi wa kikoloni ulikuwa ni upanuzi wa ule wa

serikali ya kikoloni. chumi za Waafrika ziliunganishwa kwanza na ule uliokuwepo katika koloni lao na pili na chumi za mataifa yanayoongoza ya ulimwengu wa kibepari ukoloni uliyabana makoloni ya Afrika kwenye uzalishaji wa mali ghafi kwa ajili ya kupeleka nje na kisha kuyaweka makoloni hayo yategemee nchi zilizoendelea za kibepari kwa bidhaa za viwanda na teknolojia.

Mgawanyo huu imara wa kazi wa kimataifa ulijitokeza miongoni mwa chumi za kikoloni kama tofauti kati ya uzalishaji na ulaji. Kiasi kikubwa cha mazaokatika uchumi wa fedha unaendelea kukua haukukusudiwa kutosheleza mahitaji ya wenyeji. Kinyume chake bidhaa mbalimbali zilizopatikana katika masoko ya rejareja ziliendelea kuwa za kigeni. Ufundi wa wenyeji ulipata pigo kubwa kutokana na ushindani kutoka Ulaya au udanganyifu kulingana na hali ilivyokuwa katika kipindi kabla ya ukoloni. Wakati uchumi wa kikoloni ulipokuwa umeimarika sana katika miaka ya 1920, Waafrika walikuwa wanazalisha kile ambacho walikuwa hawatumii na kutumia kile ambache walikuwa hawuzalishi. Kwa kweli mahitaji ya ndani hayakuchochea utumiaji mkamilifu wa mali ya asili. Zaidi ya hayo, wakoloni waliharibu baadhi ya mali za asili za Waafrika na kutotilia maanani nyingine, kwa sababu kigezo chao kilikuwa ni ubora wa mali hiyo huko Ulaya kuliko Afrika. Kutokana na haya yote, ni dhahiri kuwa utawala wa kikoloni haukuleta maendeleo ya kiuchumi kama ilivyokuwa inadhaniwa bali ulileta utegemezi wa *kiuchumi* na maendeleo duni.

Tukio muhimu sana katika mabadiliko ya uchumi wa Kiafrika katika kipindi kati ya vita lilikuwa ni mpomoko wa uchumi wa mwaka 1929 - 1933. Hali hii ilipozikumba chumi zinazotegemeana za kibepari maana yake ni kwamba ilizikumba pia chumi za Afrika zilizozitegemea chumi za kikoloni. Vilio vya kurudia rudia katika uchumi wa dunia tangu karne ya kumi na tisa viliathiri kasi ya maendeleo katika Afrika na kuleta shida kwa Waafrika ambao tayari walikuwa ndani ya uchumi wa fedha. Ukali wa mwelekeo huu ndio ulikuwa kitu kigeni katika mwaka 1930 wakati matokeo yake mabaya yalipoonekana katika kontinenti la Afrika. Mporomoko wa uchumi uliingia kwa kupitia sekta zilizoendelea sana za ubepari katika Afrika-machimbo ya madini, mashamba makubwa na maeneo ya mazao ya biashara muhimu. Hata hivyo mpomoko ulienea mpaka kwenye sekta za kati na ndogo, na kusababisha shida kwa Waafrika waliokuwa wanauza vyakula kwa wafanyakazi au kwa wakulima wengine, kadhalika kwa wafugaji walioona ni hasara kuendelea kuwa na mifugo kulingana na bei iliyokuwepo, kadhalika kwa wale waliojikita kwenye biashara tu.

Kila mshiriki kkatika uchumi wa kikoloni alichukua hatua kupambana na athari za mpomoko. Kichocheo kilitokana na makampuni ya kibepari. Mabenki na makampuni ya biashara yalipunguza shughuli zao, kiasi kwamba katika maeneo ya mazao ya biashara walibakisha vituo muhimu tu kama vile Dakar, Lagos na Nairobi, wakati matawi katika sehemu za bara na miji midogo yalifungwa. Zaidi ya hayo makampuni ya kuuza bidhaa nje yalipata faida kwa kuangamiza wakulima kwa kukata bei za wakulima wakati mazao ya 1930 yalipotolewa sokoni. Wakiwa kama waajiri, walipunguza wafanyakazi na kupunguza sana mishahara. Ukiondoa uchumi wa dhahabu ambao uliendeshwa kwa bidii upunguzaji wa wafanyakazi ulikuwa ndio ufumbuzi mkuu wa waajiri wakuu katika maeneo ya uzalishaji. Kazi na ujira ziliongezeka kiasi baada ya Vita Vikuu vya Kwanza, lakini

zilipungua kwa asilimia hamsini au zaidi kati ya mwaka 1931 na 1934. Wakati huu, ijapokuwa masetla na biashara ndogondogo zilifilisika, wanufaikaji wakuu wa mfumo wa kikoloni waliendelea kupata faida japo kidogo.

Waafrika walikabiliana na tatizo hili kubwa kwa kupinga njia za utatuzi zilizojaribiwa na Wazungu. Katika kushughulikia swala la mishahara iliyopunguzwa, wafanyakazi walitumia silaha ya mgomo wakifanya hivyo mara nyingi na kwa idadi kubwa bila kujali kkutokuwepo kwa vyama vya wafanyakazi. Mambo machache yameandikwa kuhusu mapambano ya dhati ya tabaka la wafanyakazi wa Kiafrika kabla ya kuja kwa vyama vya wafanyakazi lakini shughuli za biashara na vita vinaonekana vilikoleza mapambano. Tunasema hayo kutokana na msukosuko uliokuwepo wakati wa mpomoko wa uchumi kwa mwaka 1920 - 1921, wakati wa mpomoko mkuu wa uchumi wa mwaka 1929 - 1933, na tena wakati wa mshuko wa muda wa uchumi wa mwaka 1938. Kadhalika inawezekana sio tukio la habati tu kwamba wakulima katika Gold Coast walihodhi kakau yao na kususia maghala ya wageni katika mwaka 1920 - 1921 na pia katika mwaka 1930 na 1938.

Njia nyingine ya kujihumi kwa upande wa Waafrika ilikuwa ni kujitoa kwenye uchumi wa fedha. Maeneo ambayo ndiyo mwanzo yalikuwa yameingia katika uchumi wa fedha au ambayo yaligusiwa kidogo tu yalikuwa ya kwanza kutoka. Wakulima wengi wa Tanganyika ambao walikuwa na kiwango cha chini zaidi cha kuhusika katika biashara zafedha kuliko ndugu zao wa Gold Coast walifikiria kuacha kulima mazao ya biashara katika miaka baada ya 1930. Katika swala hili hawakufaulu sana kwa sababu nguvu za serikali ya kikoloni zilitumika kupunguza makali dhidi ya kile kilichofikiriwa kama kurejea mashenzini.

Miradi mingi iliachwa wakati wa mpomoko wa uchumi na mahali ambapo hili halikuwezekana, kitega uchumi kilikuwa tu upanuzi wa uzalishaji rahisi wa malighafi na kulifanyika kwa kutumia kazi za ushokoa, kama ilivyokuwa katika ofisi ya Kifaransa ya mradi wa umwagiliaji maji huko Niger. Kulikuwa na ufufuaji au utumiaji wa nguvu katika uhusiano wa kiuchumi, ikionyesha kuwa uchumi wa kikoloni ulibidi uimarishwe na njia zisio za kiuchumi wakati wa matatizo makubwa. Utumiaji wa Wafanyakazi wa Kiafrika na utozaji wa kodi vilidumisha reli na mapato ya kikoloni. Lakini bado Waafrika walipata shida zaidi kutokana na upunguzaji wa huduma za ijamii ambazo tayari zilikuwa chache. Katika miaka ya nafuu baada ya mwaka 1934, mishahara, bei za na huduma kwa ajili ya Waafrika zilibaki pungufu ukilinganisha na kurejea kwa faida kubwa katika mitaji ya binafsi.

Serikali za kikoloni zilitoa kiasi fulani cha nafuu kwa Waafrika walioathiriwa na mpomoko wa uchumi. Waliahirisha ukusanyaji wa kodi, na walitoa ruzuku za bei, kama Wafaransa walivyofanya katika zao la karanga. Pia walijaribu kudhibiti njia ambayo za anyonyaji za mtu wa kati. Hatua hizo zilichukuliwa pasipo lazima, kwa vile hapakuwepo na fedha iliyokuwa kwenye mzunguko na kwa vile bei ndogo katika nchi moja ziliwalazimisha wakulima kutembea ambali mrefu na kutosha mazao kwa siri hadi kwenye maeneo ambapo palipatikana faida kiasi. Kutokana na swala la mpomoko wa uchumi Waafrika waliingizwa kwenye usimamizi wa kiurasimu zaidi (uliobuniwa ili kuongeza

uzalishaji) lakini bado waliweza kughilibiwa na makampuni ya kuingiza na kutoa bidhaa nje na vibaraka wao wa ndani.

Utegemezi uliodhihirishwa na mpomoko mkuu wa uchumi ulionyesha kiasi cha mabadiliko katika maisha ya Waafrika katika kipindi cha miaka hamsini baada ya kuja kwa ukoloni. Athari katika miaka ya mwanzoni mara kwa mara ilikuwa ndogo, lakini mabadiliko makubwa yalisababishwa na ukoloni kadri ulivyoenelea. Baadaye kutokana na ukuaji wa uchumi wa fedha jamii ya Kiafrika ilitofautika sana na matabaka mapya yaliyoundwa. idadi ya wafanyakazi haikuongezeka sana bali ile ya wakulima, na hata wakawa wamegawanyika kati ya wakulima wakubwa na wadogo. Maeneo yote ya mazao ya biashara, katika miaka ya 1920 yalishuhudia kuzuka kwa wakulima wakubwa waliomiliki ardhi kibinafsi, kuajiri kwafanyakazi na mara kwa mara wenye kumudu mbinu mpya. Tabaka la pili linalojulikana lilikuwa la watu wachache waliobahatika ambao walipata elimu katika miaka ya mwanzoni mwa ukoloni wakati ujuzi fulani ulipokuwa unaanzishwa ili kufanya uchumi wa kikoloni ufanye kazi. Mwisho, ieleweke kwamba utaratibu wa usambazaji katika ngazi za chini ulikuwa umeshikwa na Waafrika ambao walipata umaarufu katika Afrika Magharibi na Kaskazini, wakulima wa mazao ya biashara waliostawi; wafanyabiashara Waafrika na wasomi kwa pamoja waliunda chimbuko la vibepari wachwara. Mara nyingi walikuwa na mizizi katika matabaka tawala ya zamani kkatika maeneo ya kimwinyimwinyi ya Afrika. Kwa hali hiyo walikuwa wanadekezwa na wazungu. Lakini jambo lililokuwa la ajabu kabisa ni kwamba, pamoja na siasa ya kikoloni, shughuli za uchumi zilinufaisha matabaka haya mapya yaliyochipaka ambayo kiuchumi na kitamaduni yalikuwa sehemu ya mfumo tegemezi wa ukoloni.

# 15

# Uchumi wa Kikoloni: Kanda Zilizokuwa Chini ya Wafaransa, Wabelgiji na Wareno

Katika sura iliyotangulia, tulijadili katika mtazamo wa kijumla na kibara zima, sifa kuu za chumi za kikoloni zilizoasisiwa na tawala mbalimbali za kikoloni ndani ya Afrika katika kipindi cha kati ya vita. Katika sura hii na sura mbili zifuatazo tutajadili kinaganaga zaidi chumi za kikoloni za kanda za kale za Wafaransa, Wabelgiji na Wareno, chumi za kanda za Waingereza na mwisho zile za Afrika ya Kaskazini.

Kanda zote hizi katika jumla ya maeneo yake na kufuatana na sera ya kikoloni, Makoloni ya Kifaransa, Kibelgiji na ya Kireno, yaani, *French Equitorial Africa* (Afrika ya Ikweta ya Kifaransa (AEF), *French West Africa* (Afrika ya Magharibi ya Kifaransa), *Belgian Congo* (Kongo ya Kibelgiji) na Rwanda na Burundi, Msumbiji na Angola, zina namna kadha ya kufanana. Zilikuwa ni makoloni au mashirikisho ya maeneo makubwa (ya) kijografia, ingawa kwa jumla idadi ya watu wake ilikua kuliko wastani wa makoloni ya (Afrika ya) Waingereza (hususa AEF - na Angola). (Taz. Mchoro 15.1). Katika upande wa uchumi kipindi hiki kilikuwa muhimu sana; mwanzo wake na mwisho wake viliambatana na mabaa makuu mawili, Vita Vikuu vya Kwanza na msukosuko wa 1931. Baa la kwanza lilisaidia kuchochea ufanisi wa kikoloni usio kifani ambao hasa ulionyesha utajiri wa nchi za kikoloni katika kipindi cha 1920 licha ya kipidi kifupi cha baa kali cha 1921 - 1922. Baa la pili lilifunga kipindi hiki kifupi cha mapanuko ya ajabu. Mambo yote haya yaliishia ufisadi mkubwa wa uchumi, jamii na itikadi. Hata kufikia mwisho wa kipindi hiki, uhusiano wa Afrika ya Wafaransa na Afrika ya Wareno wa nchi za nje ulikwishabadilishwa. Makoloni ambayo kwa jumla hayakuwa yakizitegemea nchi za wakoloni, yakaanza tangu wakati huo sehemu ya mfumo wa kibepari wa magharibi ndani ya kiunzi imara cha mfumo wa uchumi wa unyonyaji wa kikoloni.

## *Ugharimiaji wa Zana za Mtaji*

Sifa kuu ya chumi za kikoloni za wakati huo ilikuwa ni kusisitiza kuingiza zana za mtaji ambazo zilikuwa na tija kwa mataifa ya wakoloni kama zilivyokuwa mgogoro mkubwa kwa makoloni. Hakuna mtaji wa haja uliokuwa umejaribiwa kabla ya Vita Vikuu vya Kwanza, katika makoloni ya Kifaransa Weusi. Katika sehemu hiyo mtaji ulikuwa ,40 milioni na karibu hapakuwa na mtaji wowote katika Afrika ya Wareno. Lakini hali hii ilibadilika sana baada ya vita. Katika congo ya Wabelgiji, jumla ya mtaji ulioingizwa ulipanda toka faranga milioni 1215 kabla ya vita hadi faranga za dhahabu zaidi ya milioni elfu tatu katika 1935. Mtaji uliongezeka haraka kati ya 1920 na 1924, zaidi ya maradufu




**15.1** *Maliasili za makoloni ya Wafaransa, Wabelgiji na Wareno*

kati ya 1924 na 1929 na kuporomoka ghafla wakati wa mpomoko. Asilimia 65 ya vitega uchumi hivi katika 1932, ilikuwa ni ya migodi, usafirishaji, na mashamba makubwa au *shughuli za ziada za kilimo au biashara zilizohusiana na mapanuzi* ya reli au migodi. Mtaji ulioingizwa katika AOP na AEF - ambao ulikuwa kidogo uliongezeka hadi ,30.4 milioni kwa AOF na ,21.2 milioni kwa AEF mnamo 1913.

Wingi wa mtaji huu ulipatikana kutokana na mikopo, kwani makoloni yalikuwa maskini sana kuweza kumudu kugharimia yenyewe mapanuzi haya. Katika Kongo ya Wabelgiji wakati wa zahama za miaka ya mwisho ya mwongo huo, sera ya kukopa ilifikia kilele kati ya 1928 na 1932 ambapo takriban faranga 3500 milioni au karibu faranga za dhahabu za Kibelgiji milioni 600 zilikopwa. Tangu 1931 AOF nayo ikaanza juhudi zake kati za kukopa kwani matukio ya miaka ya thelathini yaliisadikishia serikali umuhimu wa kuwa na mpango wa vitega uchumi vya mtaji. Hata hivyo, ingawa AOF ilikuwa na eneo kubwa zaidi na watu wengi zaidi, ilibidi iridhike na robo ya kiwango kilichotolewa na Ubelgiji, au thuluthi tu ya kiwango kilichoidhinishwa na sheria. AEE, iliyokuwa lofa zaidi na iliyokuwa na taratibu zilizofanana zaidi na za Ubelgiji, ilikopa takriban faranga za dhahabu 300 milioni kati ya 1920 na 1936 ambazo karibu zote zilitumika katika kujenga reli ya Kongo - Atlantiki.

Matokeo yake ilikuwa ni kuongezeka kwa madeni ya nje ambayo yalikuwa tishio kubwa kwa bajeti linganifu wakati malipo ya madeni yalipozidi kkuwa mzigo katikati ya kipindi cha mpomoko, na papo hapo bei za bidhaa mahuruji kuporomoka. Katika mwaka wa 1933, fungu la malipo ya mwaka ya deni la Kongo, kiasi cha faranga za Kibelgiji 298 milioni lilikuwa karibu asilimia 88 ya mapato ya koloni hilo, au karibu nusu ya matumizi yake au karibu nusu ya thamani kya bidhaa zake za nje. Iliyokuwa afueni, yaani kiasi kilicholipwa na AOF (faranga za Kifaransa 40 milioni katika 1933) kilikuwa zaidi ya thuluthi ya bajeti yake ya jumla ya miaka migumu ya mpomoko. Malipo ya AEF ya wakati huo yalizidi asilimia 80 (asilimia 81 ya bajeti yote kwa ujumla katika 1934). Majimbo ya Kireno, ambayo yalikuwa na taarifa haba sahihi, nayo yalihemewa na madeni. Katika 1936, Angola ilikuwa inadaiwa karibu jumla ya konto 1 milioni sawasawa na ,8.7 milioni au faranga za Kifaransa za dhahabu 220 milioni. Kwa jumla, ongezeko la mizigo wa fungu la malipo wakati wa miaka ya mpomoko hakika lilikuwa haraka zaidi kuliko ilivyokuwa katika majimbo ya Kiingereza yaliyolimbikiziwa madeni.

Tukilinganisha Kongo ya Wabelgiji na AOF tutaona tofauti katika njia za unyonyaji. Madeni ya Kongo ya Wabelgiji yalikuwa mazito kupindukia ambapo shehena ya bidhaa za biashara za nje ilikuwa ndogo zaidi pamoja na umuhimu wa shughuli za migodi. Zaidi ya hayo, mapato yake ya kodi yalibanwa zaidi kutokana na ushuru mdogo wa forodha, na kodi ya kichwa ndogo kwa Waafrika. Matokeo yakawa upungufu mkubwa wa fedha wakati kwa mpomoko.

Kutopatikana huku kunaelezeka ikizingatiwa kuwa Kongo ilikuwa inafikia hatua ya unyonyaji kwa mitaji, ambapo AOF ilikuwa bado iko katika hatua ya uchumi kamuzi, yaani unaotegemea faida itokanayo na bidhaa madhuli na kuuzwa kwa bei kubwa wazalishaji wa Kiafrika, na ununuzi wa mazao yaliyoachiwa kwa bei ya chini; na pia uchumi huo ulitegemea utozaji mkubwa wa kodi bila kupata ruzuku yoyote kutoka

Ufaransa. Licha ya kuwa mpomoko ulifanya biashara isimame na kukomba kabisa fedha za Waafrika. Ufaransa ilikataa kut ruzuku kusaidia AOF. Vivyo hivyo, ruzuku ya mwisho iliyotolewa kwa AEF viza (ambayo kwa ujumla kuanzia mwaka 1910 hadi 1934 ilipata Faranga za Kifaransa 375 milioni) ilitolewa katika mwaka wa 1928 wenye makoloni wakijishughulisha tu na kuhudumia mikopo midogo tu, kiasi cha faranga 80 milioni za Kifaransa mwaka 1935 katika upepo wa mpomoko. Lakini kodi ya kichwa iliendelea kupanda wakati wote wa mpomoko, au tuseme haikutokea kupungua; kwa upande wa AOF ilikuwa faranga za Kifaransa 156 milioni katika mwaka 1929, faranga 181 milioni mwaka 1931, na ya chini kabisa faranga 153 milioni katika mwaka 1935. Ingawa Ufaransa ilikubali kufanya juhudi za kuingiza mitaji, kwa kweli hili ilikuwa jambo la muda na mitaji yenyewe ilikuwa aina ya mdhamana wa taifa wa kulipwa baada ya miaka hamsini kwa kiasi cha (riba) asilimia 4/5.5. Kwa maana nyingine kimsingi, makoloni ya Kifaransa yalikuwa bado yanatakiwa kujilipia vifaa vyao vya mitaji. AEF walikumbwa na umaskini kiasi kwamba wenye makoloni walijitwisha karibu deni lote, mwishowe. Lakini katika AOF - gharama za Ufaransa zilipunguzwa hadi asilimia 16 ya jumla ya mkopo, kati ya 1931 kna 1936 kuruhusu kuhudumia deni. Kumbe basi, ilikuwa ni jasho la wenyeji lililotumika kwanza kuendeleza jimbo.

Kwa kuwa uchumi huu mkongwe, yaani uliotegemea kikodi na uporaji badala ya nzalishi na vitegauchumi, ulikuwa dhalili, mpomoko ulipoingia ukaufanya muflisi.

Katika mwaka 1934, kongamano la uchumi la Ufaransa na makoloni yake lilifanyika kufanya jaribio la kwanza la kuandaa mpango wa ufadhili. Lakini mpango huu kwa hakika ulitekelezwa baada ya Vita Vikuu vya Pili.

Ingawa mpomoko ulikuwa wa ghafla na mkali katika Kongo ya Ubelgiji, na thamani ya bidhaa mahuruji kuanguka kwa karibu theluthi mbili, toka faranga za Kibelgiji 1511 milioni hadi 658 milioni kati ya 1930 na 1933, kwa wastani mpomoko huo haukujitokeza sana na ulizimwa haraka zaidi. Hii inadhihirishwa na kupanda tena kwa mahuruji kufikia faranga za Kibelgiji 1203 milioni katika 1935. Kwamba baada ya mpomoko, mahuruji yalikuwa mengi kuliko madhuluuli kila mahala, na inathibitisha kuwa mitaji ya awamu iliyotangulia ilisaidia tu kuendeleza zaidi sera ambayo kimsingi bado ilijengwa kwenye misingi ya unyonyaji kutoka nje dhidi ya andelezaji wa majimbo kwa manufaa yao.

*Mzigo wa Wafanyakazi*

Kipindi kati ya awamu mbili ngumu kilichoumbatana na unyonyaji zaidi na zaidi wa wafanyakazi - yaani Vita Vikuu vya Kwanza na mpomoko - kilikuwa kigumu kwa Waafrika. Wakati huo wa maendeleo ya Ukoloni, Waafrika walikuwa wa thamani tu kwa mkoloni kama walikuwa bidhaa au chombo cha uzalishaji mali. Zaidi ya hayo, ilikuwa katika kuhakikisha utenda kazi bora wao ndipo hatua ya kwanza ya kulinda wafanyakazi ikachukuliwa. Lakini hali ya wasiwasi wa maisha haikuhimili vishindo, na mpomoko ulipoingia ikatibuka.

Ufanyaji Kazi

Ingawa ushokoa ulikuwa rasmi kila mahala, upungufu wa wafanyakazi ulikaribisha kulazimishana kwa moja kwa moja au kwa njama ya kodi ambayo ilibidi ilipwe.

Huduma za Kazini na Kutoa Mazao

Kila mahala, lilikuwa jambo la kawaida kuwafanzisha watu kazi bila malipo. Mashirikisho ya Kifaransa, baada ya vita, yaliruhusu rasmi kazi zisizo na malipo kwa miradi yenye manufaa kwa nchi na kwa wakoloni. Awali ilipangwa siku saba kwa mwaka, punde ikapanda kuwa siku kumi na mbili katika AOF au siku kumi na tano kwa AEF.

Wajibu huu, licha ya mipaka yake, haukupendelewa kamwe kwa sababu ulishaji wa wafanyakazi, ambao hata haukufikiriwa hapo awali, ulibakia kuwa kazi ya wanawake kama shughuli ilikuwa mahali ambapo mfanyakazi anaweza kwenda na kurudi kijijini siku ile ile. Kazi hii ya lazima ilikuwa ni nyongeza ya ajira lazima (lakini ya malipo) kwa kazi za reli. Toka 1921 mpaka 1932 watu 127250 wakiwakilisha jumla ya miaka 138.125 ya bure waliajiriwa katika AEF kujenga reli ya Kongo - Ocean; yawezekana watu kama 20,000 walipoteza maisha yao kabla ya 1928.

Kipindi pia kilidhihirishwa na uanzishaji wa kilimo cha lazima cha mazao. Utaratibu huu ulioanzia katika Kongo ya Ubelgiji mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, ulifufuliwa tena wakati wa Vita Vikuu ya Kwanza. Katika mwaka wa 1930 Mashamba ya Taifa katika Kongo ya Ubelgiji yalikuwa na eneo la hekta zaidi ya milioni moja yakitoa tani 15,000za mchele na 30,000 za pamba. Mpango kwa hakika haukupendelewa lakini hata hivyo uliigwa katika mashirikisho ya Kifaransa mnamo 1916 ili kuchangia 'juhudi za vita' na katika makoloni yote ya Kireno. Katika AOF na makoloni ya Kireno sera hii ya kilimo cha lazima cha mazao hikufaulu. Katika AOF kushindwa kulitokana na kushindikana kwa kutatua tatizo la wingi wa watu na mazao haba ya pamba duni kambayo bei yake ilianguka toka faranga 1.25 katika 1928 hadi senti 90 katika 1929, senti 70 katika 1931 na senti 60 tu kati ya 1933 na 1936. Katika makoloni ya Kireno, ilikuwa ni kushindwa kwa mamlaka ya utawala kuhakikisha usambazaji wa mbegu au kutoa maelekezo ya kiufundi. Hata hivyo utaratibu huu uliendelea kutamba na ukongwe wake katika jimbo la Kampuni ya Msambiji, iliyoundwa katika 1891 na kuendelea kufurahia haki ya kumiliki zaidi za mraba 62,000 (km. za mraba 160,000) kwa miaka hamsini. Lakini utaratibu huu ulifanikiwa pia katika Cameroon; Ivory Coast na Rwanda-Burundi, ambako uzalishaji kabambe wa kakau na hasa saha buni ulianzishwa mwishoni mwa mpomoko.

## *Mfumo wa Kazi na Sheria*

Katika Afrika ya Wafaransa, utawala ulisimamia uajiri ambao kinadharia, baada ya 1921 katika AEF - haukuzidi theluthi moja ya wanaume waliobaleghe wenye uwezo wa kufanyakazi.

Katika Kongo ya Wabelgiji ajira ilikomea asilimia 25 ya 'wanaume baleghe wenye

uwezo'. Kiwango hiki kilipunguka hadi asilimia 10 katikati ya mwongo kwa sababu ya kuishiwa na wafanyakazi; lakini kwa jumla kiwango rasmi kilikuwa kinavukwa sana. Katika makoloni ya Wareno, muainisho mdogo uliwekwa kati ya 'kazi ya dhahabu' iliyowekwa kwa wahalifu, na ufanyaji kazi - 'tendo la wajibu katika jamii' - kwa wanaume wenye umri kati ya miaka 14 na 60 kwa akali ya miezi sita kwa mwaka.

Ufisadi wa waajiri ulijitokeza sana husa katika Kongo, ambako serikali iliyaachia mamlaka ya kuajiri makampuni kama *Bouree du Travail du Katanga* (BTK) - wakala binafsi walioajiri kwa machimbo ya migodi katika maeneo ya mashamba. Katika makoloni ya Wareno, kashfa zilitukia kila mara, mathalani kashfa ya kazi ya ushokoa na ya utumwa kwenye mashamba ya kakau ya Sao na Principe mwanzoni mwa karne ya ishirini. Walichukua kati ya 'Waajiri wa hiari' 2000 na 4000 kila mwaka. Katika mwaka wa 1903, uajiri wa wachimba madini katika Msumbiji kwa ajili ya Transvaal ulikabidhiwa *Witwatersrand Native Labour Association* (MNLA). Wastani wa ajira kati ya 1913 na 1930 ulikuwa wageni 50,000 kwa mwaka au jumla ya wafanyakazi 900,000 ambao kati yao 35,000 walifariki na 740,000 tu walirejea kwao na afya zao. Hivyo, uajiri wa wafanyakazi na usafirishaji wa bidhaa vilikuwa ndio msingi mkuu wa fedha za kikoloni (thuluthi mbili katika 1928).

Watawala wote wa kikoloni, karibu kwa wakati mmoja waliona haja ya kuwa na kanuni za kazi ambazo zilianzishwa kwa mara ya kwanza katika Kongo ya Wabelgiji 1910, 1902 katika AEF, 1928 kkatika AOF na katika makoloni ya Wareno mwaka 1911. Kanuni, zilizofanana kila mahala, zilipanga muda wa kishoria wa mkataba usiozidi miaka mitatu Kongo na miaka miwili katika makoloni ya Kifaransa na ya Kireno. Kanuni hizi hazikuwahi kutekelezwa kwa ukamilifu.

Mgogoro wa wafanyakazi, uliokuwa mkali hasa katika migodi na katika miradi ya reli, ulisababisha matumizi ya sera mashuhuri ya ubaba katika Kongo ya Wabelgiji baada ya 1926 iliyokusudiwa kubadilisha mfanyakazi wa kudumu kwa aliyeajiriwa kwa mkataba wa muda mfupi wa kati ya miezi sita na tisa kama ilivyokuwa ada katika Afrika ya Kusini. Kwa kuzingatia sera hii maeneo maalum ya kazi yalipangwa upya katika 1926; na mnamo mwaka mmoja gharama ya mfanyakazi ilipanda kwa asilimia 40, ingawa mishahara haikuwakilisha tena zaidi ya moja ya tano ya makadirio. Kila kipengee cha maisha kilipatiwa uongozi (burudani, dini, shule n.k.) Matokeo ya hatua hizi yakawa kwamba katika mwaka 1930, kwa mara ya kwanza, idadi ya waliozaliwa ikazidi ya waliokufa katika makambi ya Union Miniere, ambayo kwa wakati huo yalitoa hali za kazi afadhali kidogo katika Afrika ya Kati.

## Kodi

Licha ya maendeleo yaliyopatikana, maendeleo ya uchumi yalikuwa na athari chechefu katika hali ya maisha ya Waafrika. Kwa yakini, kufanya kazi za ajira likawa jumbo la kawaida; idadi ya wafanyakazi ikaongezeka mara kumi katika kipindi cha miaka kumi kutoka chini ya asilimia 20 ya watu walio baleghe wenye uwezo katika Kongo ambao kati yao asilimia 2 walikuwa Warundi kwa kila hali. Licha ya kupanda kwa mchirizo wa ajira,

mishahara haikuweza kupanda kiasi hicho na ilionyesha dalili za kushuka kutokana na kuanguka sana kwa thamani ya fedha huko Ulaya ukiondoa Uingereza ya mwaka 1920, kulikoachwa Afrika kutokana na bei za bidhaa maduhuli. Hadi 1926 faranga ya Kifaransa ilikwishapoteza nne ya tano ya thamani yake ya kabla ya vita na faranga ya Kibelgiji ilipoteza thamani zaidi kidogo; bila ya kutaja msererekо wa mporomoko wa thamani ya fedha ya Kireno.

Juhudi zilizoweza kuleta mafanikio ya haja zilikuwa zile za kubadilisha malipo kwa njia ya fedha na malipo kwa njia ya vitu - utaratibu uliowekwa katika Kongo ya Wabelgiji tangu 1916 na kuendelea na kutumika kidogo katika AEF. Hata hivyo, hii iliishia kulipa kodi kwa fedha taslimu jambo ambalo lilipaswa kutekelezwa na kulipa mtu mzima mwenye uwezo.

Tatizo hili la kodi liliwalemea zaidi na zaidi Waafrika kadiri ilivyoendelea kuwa ndiyo njia kuu ya kupatia fedha za kupanua shughuli kwa kipindi kati ya vita na kadiri kipato cha wakulima kilivyoendelea kuwa duni, hasa kati ya wale waliolima mazao ya lazima, ndivyo mishahara pia ilizidi kushuka. Kati ya 1928 na 1932, katika Kongo ya Wabelgiji walilima pamba 700,000 walipata wastani wa faranga 165 kila mmoja kwa mwaka; walima mpunga walikuwa afadhali kidogo (faranga 170). Matokeo yalikuwa mabaya zaidi katika AEF. Wastani wa ujira wa mwezi pia ulishuka katika Kongo ya Kati toka faranga za Kibelgiji 25.45 katika mwaka wa 1912 - mwaka wa fanaka (faranga 19.30 - katika 1913) hadi faranga 19.35 katika 1920.

Kwa jumla, mzigo wa kodi ya moja kwa moja kwa Mwafrika ulikuwa ni mzito kuliko ujira wake, na ulimtumbukiza katika madeni na uchochole-seuze kupanda kwa kodi wakati ambapo bei za vitu zilishuka chini kabisa na kuporomosha pia ujira wa mkulima. Licha ya kuongezeka kwa papo kwa mazao ya ulanguzi, dalili zote zilionyesha kuwa umaskini ulikuwa mkali.

Ingawa ulinganishaji kati kya majimbo yanayohusiku ni mgumu, baadhi ya mambo yanayofanana na yanayotafautiana katika maendeleo yake yanaweza kubainishwa. Ilikuwa katika makoloni ya Wareno ambako mzigo wa kodi ya kichwa uliendelea kuwa mzito kabisa muda wote, kwani kodi rasmi ililingana na kazi ya miezi mitatu, kodi ambayo ililipwa kwa kazi. Kufu yake kwa ujira wa siku itikadiriwa kuwa kati ya asilimia 1 na 1.5 ya jumla yake yote. Pia kodi ya kichwa, kwa wastani, ilikuwa kubwa katika AOF. Wastani wa kodi ya moja kwa moja iliyolipwa katika 1915 kwa mkazi kilikuwa faranga za Kifaransa 2 katika AOF, 1.55 katika AEF na faranga za Kibelgiji 1.35 katika Kongo ya Wabelgiji. Kadiri nchi ilivyolazimika kuishi kwa raslimali isiyokuwa yake ndivyo kodi ilivyozidi kuwa nzito.

Kwa ada, makadirio ya Kikoloni yote yaligharimiwa kwa namna moja: asilimia 25 kutoka ushuru wa forodha na asilimia 25 kutoka kodiya kichwa. Balaa likawa kwamba kutokana na kukabiliwa na mpomoko wakoloni walijaribu kuifanya kodi ya kichwa ifidie pengo la mapato ya ushuru wa forodha ambao ulikwishashuka na kuwa chini ya asilimia 20 kila mahala mwaka 2 wa 1932.

## Migogoro na Matokeo yake

Migogoro iliyojadiliwa hapo juu ilikuwa na athari kubwa kwa Waafrika. Athari ya kwanza ilikuwa ni kufakirika kwa wananchi walio wengi. Ni kweli kwamba kwa kulemewa na mzigo wa kodi ambayo hawakumudu tena kuilipa, Waafrika walitetea kuanguka kwa mapato yao kwa kuongeza uzalishaji mali. Kama tulivyokwisha kuona, ilikuwa katika kilele cha migogoro ambapo mazao ya mashamba ya kitropiki (buni, kakau, ndizi, pamba) yalipata bei kubwa kutokana shughuli za uzalishaji za wakulima wenyeji wadogo wadogo tu. Hata hivyo, kwa kuwa ongezeko la mzigo wa kodi kwa mzalishaji lilitokea wakati ule ule ambapo bei zilifikia kiwango cha chini kabisa, ujira wa wafanyakazi mashambani ulishuka pia. Zaidi ya hayo kilimo cha mazao kilisaidia kuanzisha ujenzi wa matabaka ya kijamii kwa kuzuka kikudni cha 'matajiri wapya', wenyeji wamiliki ardhi wadogo na wafanyabiashara waliojitajirisha kutokana na uchochole na madeni ya walio wengi.

Lakini kkwa upande wa umati wa wakulima wadogo maskini, ulofa kwao ulitia fora. Waafrika wakakomba akiba zao duni, wakaweka rehani ardhi zao na kuwa wazalishaji-bia katika mfumo wa thuluthi mbili na robo tatu (*Abusa* wa maeneo ya mashamba ya kakau ya Ivory Coast). Hapakawa hata na haja ya kuwabana tena kwa sheria ya kazi ya lazima. Kuanzia 1931 na kuendelea upungufu wa pesa (ambaza matumizi yake hayakuweza kuepukika tena) ukazidi mno; na ikaendelea kuwawia vigumu kurudia tena masiha yao ya asili ya kilimo cha chakula cha kujikimu, ambacho hata hakikuwa na uhakika wa kunusurika.

## Upungufu wa Chakula, Njaa na Masaibu

Pigo la pili muhimu la uchumi wa kikoloni lilikuwa ni njaa kali iliyozushwa nao. Uchumi wa Kivita wa miaka ya 1915 - 1918 ulikuwa na matukio mabaya. Haribifu zaidi ilikuwa ni hatua ya kukusanya mazao ya chakula kwa ajili ya wenye makoloni kwao wakati ambapo majeshi (askari 10,000 katika AEF, lakini zaidi kidogo ya 160,000 katika AOF) yalikuwa yakiyakamua makoloni.

Katika Gabon ni robo tu ya mazao yaliyozalishwa kwa lazima yaliyobakishwa kwa matumizi ya nchini. Hata muhogo ulisafirishwa toka Kongo ya Kati na Oubangui-Chari. Kutokana na uamuzi wa kuuza nje mazao ya chakula watawala katika AOF walikomba akiba yote ya nafaka katika maghala, akiba ambayo ilikwishaathiriwa na miaka miwili ya ukamekame (1911-1912) na mwaka mmoja wa ukame kabisa (1913). Ukame huu ulikwishaenea katika eneo lote la Sudan, toka Senegal hadi Wadai na Chad. Kutokana na upungufu wa mara kwa mara, hali ikawa mbaya hadi kufikia baa la njaa lililoangamiza kati ya watu 250,000 na 300,000.

Katika AEF ambako mauzo ya lazima yaliendelea hadi kipindi cha miaka kumi kilichofuata ili kuukimu mradi wa reli ya Congo Ocean, njaa iliyoanza katika mwaka 1918, ilienea hadi nusu ya sehemu ya kaskazini ya nchi (Woleu-Ntem) kati ya 1922 na 1925; iliangamiza karibu nusu ya Wafang, toka 140,000 hadi 65,000 katika 1933.

Kisha wenyeji dhaifu waliobaki wakaandamwa na baa la magonjwa: ndui ya mara

kwa mara na hasa kuenea kwa flu ya Kihispania toka Ulaya iliyomaliza karibu asilimia kumi ya umma wa AEF.

Hata bila ya kuambatana na matokeo maovu kama hayo mara kwa mara, tatizo la njaa kutokana na upungufu wa chakula uliosababishwa na mfumo wa kikoloni lilikuwa ni tukio lililojirudiarudia katika kipindi hicho. Lilijirudia, kwa mfano, katika Rwanda katika 1928 - 29 katika 'maghala ya Kongo ya Wabelgiji, baada ya ukame mwingine, na hasa ilikuwa dalili ya udhalilifu wa nchi zilizochoshwa na *economie de traite* licha ya kupanda kwa takwimu za mahuruji.

Kwa jumla, hata hivyo janga halikuwa la kutisha mno. Baa la njaa lilizimwa kutokana na maendeleo katika huduma za usafirishaji na baa la maradhi kuzuiwa na kampeni ya kwanza ya afya. Lakini kushuka kwa bei za kukosa kazi kulimgusa kila mtu, kila mahala, vibaya.

Haishangazi kuona kwamba katika Afrika ya Wafaransa, uhamiaji mkubwa mijini ulianza mara wakati mgogoro mkuu ulipotokea. Pamoja na huduma kwa mwongezeko wa watu (katika AOF watu 14.4 milioni katika 1931, kulinganisha na watu 14.6 milioni mwaka 1936) miji na majiji yalianza kufurika wakulima wachochole. Kati ya 1931 na 1936 idadi ya watu katika Dakar na Abidjan iliongezeka kwa asilimia 71, ambavyo ile ya Canakry iliongezeka maradufu na ile ya Oagadougou, kile kituo njaa kilicho ndani bara, iliongezeka kwa thuluthi moja wakati ule ule. Kudumaa kote huku kwa ongezeko la watu katika kipindi hiki ni ashirio dhahiri la hali ya umaskini iliyotinga.

## *Mizania ya Uchumi*

Kwa kuwa wenyeji walidhibitiwa barabara chini ya mamlaka tawala, na kutokana na kushiriki kwao kidogo katika mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi, basi mwishoni mwa kipindi walijikuta katika hali ya hatari, ambapo mfumo wenyewe ulikuwa katika mikikimikiki ya mabadiliko.

### Sekta ya Binafsi

Kwa hakika kipindi hiki kilidhihirishwa na ongezeko la viwanda vyenye nguvu ambavyo vilikuwa vimeazishwa mwanzoni tu mwa karne. Kongo ya Wabelgiji ilikuwa tangulizi katika mabadiliko haya. Kabla tu ya mpomoko nchi ilikuwa na viwanda na mashirika ya biashara 278, na wakala za makampuni ya kigeni thelathini na sita ukiachilia mbali biashara kemkem za binafsi za wenyeji. Kwa jumla, idadi ya shughuli iliongezeka kwa zaidi ya moja ya tatu katika kipindi cha miaka mitatu kutoka 4500 katika 1926 hadi 6000 katika 1929 ikiwemo usafirishaji, mabenki, madini, kilimo, viwanda biashara na misitu. Tangu 1919 hadi 1930, kiasi cha mitaji iliyoingizwa kilipanda kwa faranga za dhahabu milioni elfu moja.

Ingawa sekta zilizoshughulikiwa tayari zilikwishachepuliwa, msukumo mkubwa ulitokana na shughuli za madini na za reli. Kampuni kuu nne (Societe Generale, Empaiu, Cominiere na *Banque de Bruxelles*), zilizokuwa na vitega uchumi vya thamani ya zaidi ya

faranga 6,000 milioni, zilifanya karibu asilimia 75 ya rasilimali yote. Kampuni iliyoongoza, *Societe Generale*, yenyewe ilimiliki nusu ya raslimali hiyo, ikidhibiti karibu shughuli zote za uchimba madini (shaba, almasi, radi na hisa kubwa ya dhahabu), viwanda vyote vya saruji na vile vituo vyote muhimu zaidi vya umeme wa maji. Hii ilitofautiana na makampuni mengine ambayo yalipata miliki lakini yalikuwa yamezembea, mengi yao yakiwa hayajawa na mtaji wa kutosha kuweza kuyatumia maeneo yao makubwa. Hii ilikuwa hasa ni kweli kwa kampuni ya AEF ambayo ilikufa tangu mwaka 1900 kutokana na miaka 30 ya mpango mbaya wa miliki ambao uliuza eneo kwa bei rahisi kwa makampuni fulani makubwa arobaini ya kiukiritimba, mengi yao yakiwa tayari yalikwisha kufa ilipokaribia Vita Kuu ya Kwanza.

Ilipokaribia kipindi cha mshuko wa biashara mtaji wa pamoja wa viwanda 107 ulikuwa na jumla ya faranga za ubelgiji milioni 309 tu ambazo-kwa faranga za dhahabu-ulikuwa umeongezeka kidogo tu kufikia nusu tangu mwaka 1913, ambapo mtaji wa wenye hisa binafsi ulifikia faranga za Ubelgiji milioni 70. Dhima kuu katika uwekezaji mtaji ilikuwa bado ni ya dola-ishara ya nchi iliyokuwa ikichukuliwa kuwa ni maskini, ambapo sekta binafsi kwa muda mrefu imeiachia mamlaka ya umma mzigo wa matumizi makubwa kwa ajili ya vifaa.

Kiutendaji AOF ilibakia kuwa ndicho kiwanda cha biashara kilichokuwa na nguvu kati ya viwanda vilivyoanzishwa kwenye kilimo kwa ajili ya kuuzwa nje. Hata katika eneo hili kulikuwa na kutoendelea kukubwa ukilinganisha na Kongo.

Mnamo mwaka 1938, ushirika wa Wafaransa ulikuwa na jumla ya kampuni za biashara hamsini tu, ambazo mtaji wao uliosajiliwa haukuzidi faranga za Kifaransa milioni 600. Wakati huo, kumi kati ya kampuni hizo ziliorodhesha mtaji wa zaidi ya faranga za Kifaransa milioni 20, ambazo kati yake ni kampuni mbili tu ambazo zilikuwa na theluthi moja ya mtaji wote: Chama cha Biashara cha Afrika Mashariki (SCOA), kilichoanzishwa mwaka 1906 na mtaji wa faranga za Kifaransa milioni 125, na Kampuni ya Kifaransa ya Afrika Magharibi (CFAO), iliyoanzishwa mwaka 1887 na mtaji wa faranga za Kifaransa milioni 75.

Sababu ya uwekezaji huu mdogo ilikuwa kwamba biashara-ambayo ilikuwa ni kukusanya na kusafirisha hadi bandarini mazao ya nchi ambayo yalikuwa yapelekwe nje yakiwa ghafi au katika hali ya kuwa yametengenezwa kidogo, na badala yake kugawanya bidhaa zilizotengenezwa na kuingizwa nchini ikiwa zaidi ni bidhaa kama vile vyakula na nguo-ilihitaji mtaji mdogo. Kwa hakika miaka ya 1920 ndiyo iliyokuwa miaka ya neema kwa aina hii ya biashara, na mfumuko wa bei ndio uliokuwa chanzo cha faida kubwa; kuanzia mwaka k1913 hadi 1920 biashara ya nje ya AOF iliongezeka kutoka faranga za Kifaransa 277 milioni hadi 1143 milioni.

Athari za mshuko wa biashara zilijitokeza sana, kwani msingi wa utajiri ulikuwa hasa wa kubahatisha na haukuwa imara sana kuweza kuhimili kuanguka kwa bei za bidhaa kwani hali ya kuwa na shughuli tofauti ilikuwa bado haijaanza kikamilifu, shughuli za viwanda zilikuwa bado hazijukuwepo, uchumi wa biashara wa asili ulikuwa bado ndio uliochukua nafasi kubwa karika shughuli za AOF.

Kwa upande wa makoloni ya Wareno, bado yalikuwa hayajaweza kuchagua njia

mojawapo kati ya hizi. Msumbiji, ikiwa bado chini ya mfumo wa kumilikiwa, iliathiriwa - sana na mshuko wa biashara, kama inavyoonekana kutokana na ukweli kuwa thamani ya mauzo nje ilishuka kwa nusu kati ya mwaka 1929 na 1933. Angola napo, jaribio la kwanza la kuchimba madini lilifanywa na kikundi cha *Diamang* kwa mtaji wa Ubelgiji na Uingereza. Tangu 1920, *Diamang*, iliendelea kuwa mfadhili mkuu wa mtaji katika koloni hilo moja na uchechefu wa mchango wake wa pauni 600,000 katika 1929, au robo ya thamani ya mahuruji ya Angola.

*Vifaa na Uzalishaji*

Kwa upande wa mtaji wa vifaa na uzalishaji, mizania ya uchumi bado ilikuwa hafifu mwishoni mwa kipindi. Mafanikio makubwa yalikuwa ni ujenzi wa reli; kila mahala serikali ama ilichukua nafasi ya watu binafsi au iliendelea kuyapatia ruzuku makampuni binafsi ya awali. Mfumo wa reli ya Kongo ya Ubelgiji ulipanuka sana. Raslimali yake ilipanda toka faranga za dhahabu 480 milioni katika 1920 hadi 535 milioni katika 1935 na urefu wa reli toka km 1940 hadi 2410.

Katika AEF miradi ya fahari ya reli iliyozinduliwa katika 1913 ikiwa ni pamoja na reli ya Gaboni na kiungo cha Kongo-Chad hatimaye iliishia katika ujenzi mgumu, wa reli ya Kongo Ocean (chini ya km 500 1922-1934) kwa gharama kubwa kwa hali na mali. Reli hii iliwezesha mawasiliano nchini umbayo hapo awali yalitegemea Kongo ya Ubelgiji. Kwa upande mwingine, AOF, ambayo ilikuwa na madini haba iliendesha miradi michache tu ya mapanuzi ya reli kiasi cha km 550.

Ubunifu muhimu zaidi ulikuwa ni ujenzi, katika nchi ya Savanna, wa mfumo wa barabara ambao, kwa kukomesha mateso ya uhamali wa mwanadamu, ulibadilisha hali zilizotawala ukusanyaji na ugawaji wa mazao. Mwanzo wa ujenzi wa barabara za Ubangi (AEF) ulianzia na vita na mnamo 1926 kilometa 4200 zilikwishakamilika. Hata hivyo, magari machache tu yalikuwa yakizitumia na mengi yake yalikuwa ni ya biashara tu. Katika mwaka 1930 kulikuwa na magari chini ya 1000, 1500 katika 1931 na 2850 katika 1945, kati ya hayo 600 yalikuwa ya utalii.

AOF, hususa, ilifidia upungufu wake wa reli kwa barabara: Mnamo 1937 km 2700 zilifunguliwa kwa magari 17,229, pamoja na malori takriban 10,000. Kati ya 1926 na 1934 miradi ya barabara kuu na ya kuimarisha bandari iligharimiwa mtaji karibu sawa na ule wa reli kwa kutumia faranga 475 milioni ikilinganishwa na faranga 520 milioni (za reli).

Hata hivyo huu muundo - mbinu haukupata fursa ya kuathiri kiwango cha mahuruji kabla ya kuingia kwa mpomoko. Kwa yakini, idadi kadha ya nchi zilitoa msururu aina aina wa mazao; pamba, buni, miwa, katani na mahindi katika Angola; nazi, karanga, na mchele katika Msumbiji; mbao katika Gabon na Ivory Coast na ndizi katika Guinea. Lakini (mazao) mahuruji yaliendelea kutegemea zaidi zaidi madini na mimea ya mafuta. Ni nchi chache sana zilizobahatika kama Kongo ya Wabelgiji, ambayo maendeleo yake yalitegemea, mno mno, aina mbili tatu za mazao ambayo angalau yalikwishasindikwa kiasi. Haya yalikuwa ni mafuta ya mboga ambayo uzalishaji wake uliongezeka toka tani 2500

katika 1914 hadi 9000 katika 1921 na tani 65000 mwaka wa 1930 na shaba, iliyoongezeka mara tatu kati ya 1922 na 1931, toka tani 43000 hadi 120000.

Kwa hakika, Angola nayo ilielekea kuwa ingekuwa katika hali njema kama nchi nyingine. Hata hivyo, uzembe wa Ureno ulizifanya shughuli zake za kilimo cha kubabia zitegemee hali ya hewa na majaliwa, vitu vilivyodumaza kwa kipindi cha miaka kumi.

Kwa upande wa AEF, ndiyo kwanza ilikuwa inaibuka kutoka kuhodhi msitu wa Gabon, ambao ulitoa tani zaidi kidogo ya 400,000 za mahuruji katika 1930. Ingawa shehena ya mahuruji kutoka Cameroon iliongezeka mara tatu 1923 (toka tani 48,000 hadi 124,000), matumizi ya maliasili ya nchi yalikuwa bado yanasota mnamo 1934 ikiwa na mahuruji ya faranga za Kifaransa milioni, kati yake karibu asilimia 60 ikiwa ni mazao ya kakau na mafuta ya maweze. Mwisho, AOF licha ya kujitokeza polepole kwa mazao machache mapya, bado ilitegemea kwa zaidi ya nusu ya mahuruji yake juu ya karanga za Senegal, ambazo karibu zote zilisafirishwa bila kusindikwa.

## *Hitimisho*

Kwa kifupi, mizania ya uchumi mwishoni mwa kipindi kati ya vita ilikuwa hasi kotekote, kwa upande wa wakoloni ambapo uzalishaji ulidorora na kutochepuliwa vya kutosha, na kwa upande wa Waafrika umaskini kutinga na watu kuvurugikiwa. Hata hivyo, licha ya picha hii, vikorombwezo vilivyopo na miundo kama ya uzalishaji vilibadilisha sana muundo wa uchumi. Kwa manzili haya, mgogoro wa 1930 ulivuta nadhari ya kuwa nasera madhubuti ilikiongozwa na Taifa. Ilibashiri kuja kwa upangaji wa kikoloni, ambapo mgawano wa kazi wa kimataifa ulitumika kuhalalisha kuundwa kwa maeneo maalum ya uzalishaji shadidi.

Sifa ya ziada ya kipindi ilikuwa ni kugeuka kwa ongezeko la idadi ya watu. Katika majimbo ya wazungumza Kifaransa, inaelekea kuwa kushuka kwa idadi ya watu kulisita katikati ya miaka ya 1920. Kwa kweli, mnamo mwisho wa miaka ya 1930 mfumuko wa watu ulikuwa haujaanza. Hata hivyo kwa ongezeko la watu kulisaidia kuharakisha kufufuka kwa uchumi. Hakika, makoloni ya Kireno yalibakia na laana ya umaskini. Ubabe wa Kibelgiji uliwafanya wawe tayari kuweka vitega uchumi, lakini ubabe huu uliambatana na kukataa makusudi kuwaendeleza Waafrika nchini. Ufaransa nayo mwishowe ilikuja kuona haja ya kuingiza kwa wingi rasilimali katika uzalishaji, hata kama vitega uchumi hivyo havikuzaa matunda ya haraka. Tangu 1936 Ufaransa iliing'ang'aniza serikali ya *'Popular Front'* kuandaa mpango imara kwa makoloni ambao ni wa kisasa na wa mabadiliko. Hata hivyo ukosefu wa fedha uliizuia kupiga hatua kubwa katika welekea huu, ikaingiza katika mashirikisho yake mabadiliko ya kwanza ambayo hatimaye yalikuja kuruhusu uundaji wa vyama vya wafanyakazi na vyama vya siasa vya Waafrika.

# 16

## Uchumi wa Kikoloni: Kanda Zilizokuwa Chini ya Waingereza

Aina na tabia ya uchumi wa kikoloni uliojengwa katika maeneo ya Kiingereza haukutofautiana tu katika mambo mengi ya msingi dhidi ya ule uliosimikwa katika maeneo yaliyoelezwa katika sura iliyopita, lakini hata ndani ya maeneo ya Kiingereza yenyewe, zilikuwemo tofauti za msingi na pia kufanana kwingi kati ya maeneo ya Mashariki na Kati (Kenya, Tanganyika, Rhodesia na Nyasaland), na yale ya Magharibi (Cameroon, Nigeria, Gold Coast, Sierra Leone na Gambia).

Waingereza, kama wakoloni wengine, hawakubuni nadharia ya jumla au tabia ya ukoloni ambayo ingegubika vipengee vyote vya maisha kwa namna sawa katika makoloni yote. Mambo mengi yaliachiwa watawala kushughulikia kufuatana na hali halisi ya mahala panapohusika. Hata japokuwa hapakuwa na nadharia iliyokuwa dhahiri zilikuwepo baadhi ya imani za msingi ambazo inaelekea zilitumika kuwaongoza wapangaji na watekelezaji wa sera za uchumi wa kikoloni. Kwanza, makoloni yalitarajiwa kutoa mali-ghafi (mazao ya kilimo na madini) kwa ajili ya mashine za mataifa ya kibeberu yenye viwanda. Pili, makoloni yalilazimika kuagiza bidhaa za viwanda kutoka kwa mataifa ya kibeberu. Tatu, makoloni yalilazimika kujitegemea. Makoloni yalilazimika kukusanya fedha kwa ajili ya kuendeshea serikali na kwa kuendeleza miradi yoyote ile ya maendeleo iliyokuwa imebuniwa. Jambo la nne ambalo aghalabu lilieleweka visivyo kwa baadhi ya watawala wa kikoloni na watetezi wengine wa ukoloni ni ule ukweli kwamba Waingereza kama wakoloni wengine, kimsingi walianzisha makoloni kwa madhumuni ya kujitajirisha na kuendeleza maslahi yao, maslahi ya mashirika yao ya biashara, makampuni ya madini na mabenki. Kuendelea kwa wanaotawaliwa halikuwa jambo lililowashughulisha.

Shughuli yao kuu ilikuwa ni kujenga na kuendeleza mazingira bora ya kuendeshea shughuli za kiuchumi katika makoloni yao bila matatizo. Hii ilikuwa ni pamoja na uwekaji wa "sheria na taratibu" uliorahisisha unyonyaji madhubuti wa raslimali za makoloni, ikiwa ni pamoja na mali na watu.

### *Umilikaji wa Njia Kuu za Uzalishaji Mali*

Njia kuu na ambayo karibu ndiyo iliyokuwa njia pekee ya uzalishaji mali katika makoloni ya Kiingereza kwa kipindi hadi 1935 ilikuwa ni ardhi. Mwenendo na sera za Uingereza kuhusu ardhi vilitofutiana toka Kanda hadi Kanda, na hata ndani ya ya kila Kanda ilitofautiana toka koloni hadi koloni. Hata hivyo tunaweza kusema kwa jumla kwamba wakati Waafrika waliendelea kumiliki ardhi zao katika Afrika ya Magharibi ya

Waingereza, katika Afrika ya Mashariki na Kati ya Waingereza wengi walinyang'anywa ardhi zao. Hata hivyo, zilikuwepo baadhi ya tofauti muhimu kati ya koloni na koloni katika kila Kanda.

Katika Uganda na kwa kiasi fulani katika Tanganyika, karibu ardhi yote yenye rutuba ilimilikiwa na wenyeji, Waafrika. Wageni, wengi wao wakiwa Waingereza, walitafuta na kupata hati za kumiliki ardhi zenye madini na mbao. Karibu utajiri wote wa madini ulikuwa mali ya mamlaka ya Uingereza au wakala wake na ulitwaliwa kwa njia ambazo ziliamuliwa na mawakala rasmi na wasio rasmi wa ubeberu kama vile kampuni za madini na mabenki.


Katika Kenya na Afrika ya Kati, kama ilivyokuwa katika Tanganyika, chini ya Wajerumani, Waafrika walimiki baadhi ya ardhi, lakini maeneo makubwa ya ardhi yenye rutuba yalichukuliwa na kuuziwa masetla wa Kizungu (angalia mchoro 16.1). Katika mwaka wa 1903 ni karibu na 2,000 tu zilikwishatengewa Wazungu Kenya. Mnamo 1914 eneo lililokwishatengwa lilikwishaongezeka hadi karibu na 260,000 na kufikia karibu na 274,000 katika 1930. Hii ilikuwa sehemu kubwa sana ya ardhi yenye rutuba. Wakikuyu, ndio waliopteza sana ardhi lakini Wanandi, Wamasai, Wakipsigi na wengine pia walipoteza ardhi.

Kupatikana kwa ardhi na propaganda ya Wakoloni kuvutia kilimo cha masetla viliwavuta Wazungu wengi, wakiwemo wapita njia na masetla halisi. Katika 1903 walikuwepo Wazungu 596 tu Kenya, miaka miwili baadaye idadi ikafika 954 kati yao 700 wakiwa wa Afrika ya Kusini; mwisho mwa Machi 1914 idadi ilikwishapanda hadi 5,438 na mwishoni mwa Desemba 1929 hadi ilifikia 16,663. Wengi wa masetla wa awali, hasa hadi kufikia 1910, walipata ardhi bure au kwa bei ndogo tu. Ardhi iliyonunuliwa kati ya 1902 na 1915 ilimilikiwa kwa hati ya miaka 99. Sheria ya *Crown Lands Ordinance* (Sheria iliyohusu ardhi iliyokuwa chini ya Malkia) toka miaka 99 hadi miaka 999.


Katika Rhodesia ya Kusini (sasa Zimbabwe) kiasi kikubwa zaidi cha ardhi kilitengewa Wazungu. Kati ya 1890 na 1900 wafanyabiashara na watalii wa kizungu walimiminika nchini. Tafauti na hali ilivyokuwa katika Kenya, idadi ya Wazungu iliongezeka haraka sana, ikipanda toka 11,000 katika 1901 hadi 23,000 katika 1911 na kufikia 35,000 mnamo 1926.

Ongezeko la Wazungu liliongezea kutwaliwa kwa ardhi. Hadi 1911 Wazungu walikwishatwaa karibu hekta 7700,000, eneo pungufu kidogo ya eneo la Hifadhi za Wenyeji. Kwa upande wa Waafrika mambo yakawa kinyume; mnamo 1925 Waafrika walikuwa wamenunua ha 18,000 tu nje ya maeneo ya Hifadhi za Wenyeji. Takwimu hizi zinadhihirisha waziwazi kutoweza kwao kushindana na Wazungu katika mazingira ya wakati huo.

Katika Rhodesia ya Kaskazini (sasa Zambia) kwa wastani ni sehemu ndogo tu ya ardhi iliyochukuliwa na kuuziwa Wazungu. Katika miaka ya kati ya 1930 ardhi katika Rhodesia ya Kaskazini ilikuwa imegawiwa katika kategoria tatu hivi. Kwanza kuliwa na eneo lililohifadhiwa mahususi kwa Waafrika, ambalo lilikuwa hekta 28,740,000. Kisha kulikuwa na ardhi waliyokwishatengewa Wazungu ambayo ilikuwa zaidi ya hekta 3,430,000. Halafu hekta 60,700,000 zilizobaki zilikuwa ni misitu na hifadhi za wanyama.




16.1 *Afrika Mashariki; maendeleo ya kiuchumi katika kanda za zamani za Waingereza; mazao ya kilimo*




**16.2** *Afrika Magharibi: maendeleo ya kiuchumi katika kanda za zamani za Waingereza.*

Katika Afrika Magharibi ya Waingereza, (angalia mchoro 16.2) Waingereza walikwishajaribu mapema zaidi kuliko hata ilivyokuwa katika Afrika Mashariki, kuwa na mamlaka ya moja kwa moja juu ya ardhi, kutenga hifadhi za misitu na kutoa ardhi kwa kibali kwa wakulima wa Kizungu na wengine wenye vibali. Mapema 1894, na katika 1897 Waingereza walitunga mswada wa ardhi katika Gold Coast uliokusudiwa kuanzisha adhibiti wa moja kwa moja juu ya ardhi zilizoachwa wazi. Jibu la wananchi, kama ilivyokwishatajwa katika sura ya sita, lilikuwa ni kuundwa kwa *Aborigines Rights Protection Society* (Chama cha Kulinda Haki za Wenyeji) katika Cape Coast 1897 na wasomi wakishirikiana na watawala wa jadi ambao upinzani wao wa mswada uliilazimisha Ofisi ya Makoloni kuufutilia mbali mswada huo. Jaribio la kuingiza mswada kama huo katika Lagos nchini Nigeria katika miaka ya 1910 nalo pia lilizimwa na *Anti-Slavery Society* (Chama Dhidi ya Utumwa) na cha *Aborigines Rights Protection* kilichoanzishwa na Wasomi wakiongozwa na Herbert Macaulay na watawala wa Jadi. Kutokana na ushindi huu wa Waafrika wa Afrika Magharibi Waingereza wakaachana na sera ya kuwa na mamlaka ya moja kwa moja juu ya ardhi. Hivyo, hadi 1930 ni sehomu ndogo tu ya ardhi katika Afrika Magharibi ya Waingereza ilikuwa imetengwa kwa matumizi ya watawala wa kikoloni na Wazungu wengine na karibu ardhi yote hii ilikuwa ni kwa madhumuni ya uchimbaji wa madini.

Jambo gani lilizuia uporaji wa ardhi yote katika Afrika magharibi ya Waingereza? Jibu la kwanza ni lile ambalo Hopkins ameliita 'nusura ya kijiolojia' kwamba Afrika ya Magharibi ilikuwa haina utajiri wa madini wa kupindukia. Pili ni kushindwa kuanzisha mashamba makubwa katika Afrika Magharibi na Wazungu kama U.H. Lever, Mukki la Liverpool la sabuni na siagi na vyama kama vile Chama cha Walima Pamba cha Waingereza kati ya 1906 na 1925. Tatu na sababu muhimu kutiko zote ni mafanikio ya watu wa Afrika ya Magharibi wenyewe ya kukidhi mahitaji ya mazao mahuruji kama vile kakau, karanga, mawese wakitumia njia zao sahihi kwenye mashamba yao madogo madogo, jambo ambalo lililifanya kuanzisha mfumo wa mashamba makubwa katika maeneo haya usiwe na sababu kabisa. Jambo jingine ni upinzani ambao ungezuka kati ya Wenyeji wa Afrika Magharibi laiti jaribio la kuvamia maeneo makubwa ya ardhi lingefanywa au kuanzisha utaratibu wa manamba kwa ajili ya mashamba makubwa. Ilikuwa ni mchanganyiko wa mambo yote haya uliookoa watu wa Afrika Magharibi ya Waingereza kutokana na baa la kuporwa ardhi lililowakuta baadhi ya wenyeji katika maeneo ya Waingereza ya Afrika ya Mashariki na Kati katika Afrika ya Wareno na Wabelgiji.

## *Uzalishaji*

Taratibu za uchumi wa kikoloni zinazojadiliwa zilikuwa katika sehemu mbili - sehemu moja ikazalisha mali hasa kwa ajili ya kuwakimu wazalishaji na kwa ajili ya soko la ndani, na sehemu nyingine ikizalisha mazao ya msingi hasa hasa kwa soko la nje. Uzalishaji kwa ajili ya kujikimu ulikwishajikita hata kabla ya utawala wa kikoloni. Ndizi, viazi vikuu, muhogo, mchele na mahindi, ni mazao yaliyolimwa na wana Afrika Magharibi kwa kutumia teknolojia sahihi ambayo Waingereza waliikuta mwishoni mwa karne ya kumi na

tisa. Mambo hayakuwa tofauti katika uzalishaji wa ndizi, mahindi, muhogo, mtama na aina nyingi za mazao katika Afrika ya Mashariki na ya Kati. Sehemu hii, hata hivyo, iliachwa na utawala wa kikoloni kwani tofauti na sehemu ya bidhaa mahuruji, haikuwaletea fedha adimu za kigeni za kulipia maduhuli, wala haikutoa malighafi ya kulisha tasnia za Ulaya.

Mazao ya Biashara

Sehemu ya mahuruji kimsingi ilijishughulisha na uzalishaji wa mazao ya msingi - mazao ya kilimo na madini. Tukiondoa maeneo madogo ambako masetla wa Kizungu walimiki ardhi kubwa, sehemu ya mazao ya kilimo ya mahuruji katika makoloni ya zamani ya Waingereza ya Afrika ya kitropiki yalikuwa karibu yote, mikononi mwa mamilioni ya wakulima wadogowadogo. Mazao makuu ya biashara yaliyolimwa na wakulima hawa yalikuwa ni pamoja na kakau toka Gold Coast na Nigeria ya Magharibi, mafuta ya mawese na badamu za mawese toka Nigeria, Sierra Leone na kwa kiasi fulani, Gold Coast; pamba toka Uganda, Nigeria na Tanganyika; na buni kutoka Uganda na Tanganyika (angalia mchoro 16.1 na 16.2).

Kinyume na vile ambavyo wanahistoria wa kikoloni wangetutaka tuamini, sehemu ya mahuruji ya nchi zinazozungumziwa ilijengwa kwa msaada mdogo wa serikali. Hata viwanda vya kakau ya Gold Coast ambavyo Waingereza walijivunia sana kwa yakini viliendelezwa kwa msukumo wa wenyeji. Wakianza karibu bila kitu katika miaka ya mwanzo ya 1890, mnamo 1903 wakulima hawa walikwishalima eka zaidi ya 44,000 au ha 17,000 za kakau. Mnamo 1928 zilikuwepo hekta 364,000 au eka 900,000 za kakau na mwaka wa 1934 Gold Coast ilitoa asilimia 40 ya mavuno yote ya dunia. Bado hadi wakati huu shughuli hii ilikuwa imenufaika kidogo na (matunda ya) uchunguzi wa kisayansi uliokuwa ukifanywa nchini.

Katika Kenya na Rhodesia uzalishaji wa mazao ya biashara uliendelea kuingia mikononi mwa walowezi kadiri karne ya ishirini ilivyopiga hatua. Katika kipindi cha miaka kumi ya kwanza ya karne hii wakulima wa Kiafrika katika Kenya na Rhodesia ya Kusini walishindana barabara na masetla weupe katika kuzalisha karibu nafaka yote iliyoulisha umati wa vibarua. Ama kwa hakika hadi mwaka 1914 wakulima wa Kiafrika katika Kenya walichangia zaidi katika mazao ya biashara na ya nje kuliko masetla.

Ilikuwa ni kwa kutumia utawala wa kikoloni kupitisha hatua kadhaa ndipo nafasi na nguvu za wakulima wa Kiafrika polepole zikapunguzwa kabisa kabisa. Hatua hizi zilikuwa ni pamoja na kupora ardhi ya ziada kutoka kwa Waafrika, kuyapatia bei ya juu mazao ya masetla kuwatoza kodi Waafrika, jambo lililowalazimisha kwenda kufanya kazi kwa Wazungu, kuwalazimisha Waafrika kufanya kazi siku kadha za mwaka kwenye miradi ya serikali na mashamba na kwenye mashamba ya masetla, na mwisho kuwazuia Waafrika kupanda buni ambalo ndilo zao lililokuwa na maslahi wakati huo. Matokeo ya hatua zote hizi yakawa ni kumtoa Mwafrika katika shughuli za ukulima na kumfanya mkulima mdogo tu au kibarua. Hivyo basi, katika Kenya mnamo mwaka 1927, kati ya Waafrika 83,700 na 117,000 au zaidi ya asilimia 50 ya vibarua wote, walifanya kazi katika mashamba ya biashara wakilima hasa mahindi na buni kwa ajili ya masetla wa Kizungu ambapo katika

Rhodesia ya Kusini walilima hasa hasa mahindi au tumbaku. Hadi miaka ya mwanzo ya 1920 masetla katika Kenya walikwishawa ng'oa wakulima wa Kiafrika kwenye kilimo na biashara ya zao muhimu la mahindi. Sifa kuu ya uchumi katika koloni la Kenya ikawa imejengeka!

Madini

Nchi kadha za tropiki katika Afrika zilizokuwa makoloni ya Waingereza zilikuwa na madini mbalimbali mengi. (angalia mchoro 16.2.)1 Dhahabu ilichimbwa katika Gold Coast, Rhodesia ya Kusini, Tanganyika na Sierra Leone. Almasi ikawa mgodi mkubwa katika Sierra Leone na Gold Coast. Shaba ilipatikana Rhodesia ya Kaskazini ambapo mavi ya chuma iliendelea kuwa shughuli maalumu ya Sierra Leone.

Ni Nigeria na Rhodesia ya Kusini tu ndizo zilizochimba makaa ya mawe ambayo ni chanzo muhimu cha nishati. Karibu makoloni yote yalikuwa na aina moja au mbili za madini; ni Rhodesia ya Kusini na Sierra Leone tu ndizo zilikuwa na aina nyingi.

Isipokuwa kwa sehemu chache, madini yalichimbwa kama ilivyokuwa katika maeneo tuliyokwishaona, kwa mtaji wa nje. Hii ilisababishwa na mambo mawili. Kwanza, zilikuwepo shughuli ambazo zilidai mtaji mkubwa zaidi kuliko uwezo waliokuwa nao Waafrika. Kwa mfano uchimbaji wa shaba katika Rhodesia ya Kaskazini na chuma katika Serra Leone. Pili, kwa kiasi na hii kikubwa tawala za kikoloni kwa makusudi kabisa pole pole waliwatenga Waafrika wasinufaike na utajiri wa madini ya nchi yao. Mara tu baada ya kugunduliwa machimbo ya madini msururu wa sheria ulifuata kuwawezesha mabeberu kuyahodhi. Hata pale ambapo Waafrika walikuwa wakichimba madini kwa miaka na miaka kama vile dhahabu na bati katika Gold Coast na Nigeria, ilikuwa si halali kwao tena kukutwa na madini bila ya leseni. Hakuna Waafrika walioruhusiwa kujiingiza katika uchimbaji almasi. Shughuli hii, katika Sierra Leone na Gold Coast, ilihodhiwa na *'Consolidated African Trust'* (CAST) Kampuni zito la kimataifa lililoshughulikia uchimbaji wa madini kadhaa.

Madini yamechukuliwa kuwa msingi wa maendeleo ya uchumi karibu katika nchi zote za Kiafrika. Lakini ni wazi kwamba mchango wa madini kwa nchi hizi, katika chumi za kikoloni, ulitiliwa chumvi sana. Ni kweli kwamba madini yamechangia kiasi katika sekta ya mahuruji ya nchi chache, hasa Rhodesia, Gold Coast na Sierra Leone. Hata hivyo, madini hayakuwa muhimu kiasi hicho katika chumi za Nigeria, Kenya na Tanganyika wala hayakuchangia sana katika utajiri kwa jumla. Zaidi ya hayo, kwa kuwa uchimbaji madini ulijengwa kwa mtaji wa nje, faida iliyopatikana kutokana na shughuli hiyo ilihamishwa kwenda kusheheneza mifuko ya wenye hisa huko ng'ambo, au kuendeleza chumi nje ya Afrika. Lakini hata pale tawala za kikoloni zilipotaifisha migodi, kama ilivyokuwa katika Sierra Leone, Kenya, Tanganyika na Uganda, fedha kidogo zilipatikana na hasa zaidi kutoka katika mirabaha na kodi ya mapato. Katika Sierra Leone kodi ya moja kwa moja kutoka madini mwaka 1935 ilikuwa pauni 34,100, asilimia 5 tu ya jumla ya mapato.

Ujira ulibakia kuwa ndio njia ambayo kwayo wenyeji wangeweza kupatia sehemu maridhawa ya mapato ya madini, lakini kama ilivyokuwa katika kilimo cha masetla na cha



**16.3** *Wachumaji chai wakiwa kazini mashambani nchini Malawi (Mashamba ya Lujenda, Cholo)*

mashamba, ujira ulikuwa mdogo kiasi kwamba waajiriwa walipaswa kufidiwa na sekta ya wenyeji.

Sekta za mahuruji za nchi zinazojadiliwa zilikuwa na tabia mbili kuu. Kwanza, mahuruji ya mazao ya kilimo na ya madini yalisafirishwa yakiwa ghafi kama ilivyokuwa kawaida katika kanda nyingine, kwa jumla. Hivyo karibu mahuruji yote yalikuwa na thamani ndogo. Pili, kulikuwa na tabia ya kuwa na kilimo cha zao moja au kushughulikia zao moja tu la biashara. Jambo hili lilizifanya chumi za nchi zilizotegemea zaidi usafirishaji wa mazao ya kilimo ziwe katika mashaka makubwa. Ni Nigeria, iliyokuwa na mazao matatu hivi [kakau, (mafuta ya) mawese na karanga] na Kenya tu zilizojenga chumi chepuzi. Udhaifu wa chumi za zao moja ulijitokeza waziwazi wakati wa mpomoko mkuu wa 1929-1934 kwa wahaka na vurugu lililoonyeshwa na watawala wa kikoloni.

## *Fedha na Benki*

Waingereza kama wakoloni wengine pia walianzisha fedha za kisasa katika makoloni yao badala ya mfumo wa kale wa kubadilishana bidhaa, fedha, bidhaa na fedha kama vumbi la dhahabu, na kete. Hii ilikuwa zaidi kuhimiza uzalishaji na usafirishaji nje mazao ya biashara na kuingiza bidhaa za Ulaya. Hadi 1910, fedha za kizungu zilikwishaenea katika Afrika ya Magharibi. Zilikuwa sarafu za Kiingereza za aina mbalimbali. Katika mwaka 1912 Halmashauri ya fedha za Afrika ya Magharibi iliundwa kutoa fedha kwa ajili ya Afrika Magharibi ya Waingereza. Mnamo mwaka 1913 Halmashauri ilitoa fedha zake za kwanza zikiwemo sarafu za Sh. 2, Sh. 1 p(eni) 6 na p(eni) 3, na miaka mitatu baadaye fedha zake za noti za kwanza. Katika makoloni ya Afrika ya Mashariki, Waingereza kwanza waliingiza mfumo wa fedha uliokuwa ukitumika India ya Waingereza. Hata hivyo, katika 1920 halmashauri moja ya fedha iliundwa ili kutoa sarafu na noti kwa makoloni hayo matatu. Ni muhimu kuzingatia kwamba fedha zote hizi ziliegezwa kwenye pauni ya Kiingereza katika London.

Tukio muhimu la matumizi zaidi na zaidi ya fedha lilikuwa ni kuanzishwa kwa benki katika Makoloni ya Waingereza ya Afrika. Katika Afrika Magharibi, benki ya kwanza kufanya kazi ilikuwa *Bank of British West Africa* (Beuki ya Kiingereza ya Afrika ya Magharibi) katika 1894, ikifuatiwa na *Barclays Bank* (Benki ya Barclays) (ya Dola, Makoloni, na ng'ambo). Benki mbili hizi zilitawala kabisa kabisa shughuli zote za benki katika Afrika ya Magharibi ya Waingereza kwa muda wote wa ukoloni. Katika Afrika ya Mashariki na ya Kati ya Waingereza, *The National Bank* (Benki ya Taifa) na *Grindlay's Bank* (Benki ya Grindlay) pia zilizuka na kuwa maarufu. Shughuli za benki hizi zilizuia maendeleo ya uchumi katika makoloni kwa njia kuu tatu. Kwanza, benki ziliweka Uingereza fedha zote pamoja na akiba za Waafrika. Hii ina maana kwamba benki zilijenga mitaji ambayo ilileta maendeleo ya uchumi ya nchi tajiri za Ulaya dhidi ya makoloni maskini. Pili, na ambayo ni mbaya zaidi, uchunguzi wa karibuni unaonyesha kuwa katika sera zao za kutoa mikopo, benki zote ziliwabagua wafanyabiashara wa Kiafrika na kuwapendelea Waingereza na jamii ya Waasia. Tatu, kwa kuwa benki ilikuwa mali ya

Wazungu tu Waafrika walinyimwa fursa ya kupata mafunzo na uzoefu katika uwanja huu muhimu.

## *Soko*

Shughuli za masoko zilisahauliwa kabisa na watawala wa kikoloni. Sera ya biashara holela, au biashara huru ilitumiwa kwa viwango tofauti katika nchi zote zinazojadiliwa. Wakiwa mabingwa wa biashara huru hadi wakati huo na wakiwa wanajishughulisha zaidi na kuongeza pato kutokana na ushuru wa forodha kwa kupanua biashara mahuruji, Waingereza walielekea kumshawishi yeyote yule aliyeonekana kuchaguliwa katika pato lao. Hivyo basi, wafanyabiashara wa Kihindi hawakuruhisiwa tu, bali kwa kiasi fulani, walihimizwa kusimamia biashara katika Afrika ya Mashariki na kwa kiasi fulani katika Afrika ya Kati.

Jumuiya za ma-Levant pia ziliruhusiwa kuendesha mambo yao katika Afrika Magharibi ya Waingereza. Uingereza hata haikuzuia shughuli za kibiashara za mashirika yasiyo ya Kiingereza na za watu binafsi katika makoloni yake. Kabla ya kuzuka kwa *United Africa Company* (Kampuni Ungano ya Afrika - UCA) katika 1929 kwa mfano, mashirika mawili makuu ya Kifaransa *Compagnie Francaise de l'Afrique Occidentale* (CFAO) na *Societe Commerciale de l'Ouest-Africain* (SCOA) yaliendelea kushindana barabara na mashirika ya Kiingereza katika makoloni yake ya Afrika Magharibi.

Wala hapakuwa na namna yoyote ya kuwalinda wenyeji. Kwanza kabisa, sera ya jumla ya serikali, kama ambavyo ingetegemewa katika mazingira ya kikoloni, ilielekezwa katika kuendeleza maslahi ya mabeberu. Matokeo yake, wenyeji wakakosa kinga ya kuwakinga kutokana na makucha makwaru ya mashirika makubwa. Sana sana waliwekwa katika hali ambayo uchumi wao ungeunganishwa kwa urahisi. Baada ya miaka kumi ya kwanza ya karne ya ishirini, iliyoambatana na ujenzi wa reli, mashirika ya Wazungu yalikuwa yakiwaminya wafanyabiashara wa Kiafrika kwa njia mbili: kwa kuwung'oa katika maskani yao na kwa kupanua shughuli zao toka biashara ya jumla hadi ya rejereja. Mbaya zaidi ni mara nyingi wafanyabiashara wa Kiafrika hawakuweza kupata mikopo kwa kuwa hawakuwa na mdhamana. Kwa njama zote hizi, wafanyabiashara wakubwa wenyeji katika Afrika Magharibi walioinukia mnamo karne ya kumi na tisa waling'olewa kwenye biashara. Wala wakulima wadogo wa Kiafrika hawakutendewa vyema kwani walilipwa fedha kidogo kwa mazao yao na kuuziwa ghali bidhaa maduhuli kwa wastani.

Mara kwa mara Waafrika walitetea maslahi yao kwa pamoja kwa vizuizi (kwa kukataa kupeleka mazao sokoni) na kwa kugomea bidhaa za Ulaya. Kulikuwa na migomo mingi ya aina hii katika Gold Coast ambako wakulima wa kakau walipambana kiume na mivutano ya masoko ya kimataifa. Mgomo mkubwa kabisa kati ya hiyo ulitokea kati ya Oktoba na Desemba 1930 na mwingine wakati wa msimu wa kakau wa 1937/8. Mgomo huu wa pili uliofanywa dhidi ya makampuni mashuhuri sana ya kusafirisha kakau ambayo yalikuwa yamekula njama kununua kakau kwa bei moja tu, uliendelezwa hadi Nigeria ya Magharibi. Migomo yote ilivyotishia misingi ya uhusiano wa uchumi wa kikoloni wenyewe ilizimwa kwa nguvu na serikali ya Kiingereza.

Biashara na Waingereza iliyaletea makoloni ya Kiafrika hasara kubwa, kama ilivyokuwa wakati wa mpomoko mkuu. Katika mwaka wa 1932 Ridhaa ya Kifalme ilisimikwa katika makoloni ya Kiingereza. *Maduhuli* toka madola yaliwekewa ushuru wa forodha wa kati ya asilimia 10 na 50 chini kuliko kiwango cha kawaida. Kwa kuwa hili halikuzitenga bidhaa za Japan na nyinginezo za nje, ushuru juu ya bidhaa hizi ulipandishwa hadi asilimia 100 katika 1934 wakati huo huo kikawekwa kiwango cha kuingiza nguo kutoka Japan. Palikuwa na malalamiko ya hapa na pale kupinga hatua hizi lakini watawala ilibidi wanunue ghali, na kweli hivyo wakawa wamekuza maslahi ya mabepari dhidi yao kwa kufanya hivyo.

## *Vikorombwezo*

Kipengee muhimu kabisa katika shughuli za masoko ni Vikorombwezo. Kwa hiyo, ujenzi wa reli, barabara, njia za simu na bandari, viliushughulisha utawala wa kikoloni tangu mapema. Ingawa huduma hizi zilisaidia katika shughuli za jumla za utawala, kazi yake kuu ilikuwa ni kuhaulisha bidhaa mahuruji. Kwa hiyo, si ajabu kuona kwamba mahala na mielekeo ya reli na barabara haikujal sana matilaba ya makoloni. Karibu reli zote zilianzia pwani na kunyoosha moja kwa moja hadi ndani kwenye vyanzo vya mazao ya biashara au machimbo ya madini. Ni michepuko na viungo kati ya makoloni kidogo tu vilivyojengwa.

Karibu reli zote zilijengwa, zikamilikiwa na kuendeshwa na serikali au mawakala wake. Ujenzi wa reli ya kwanza katika Afrika Magharibi ya Waingereza ulifanyika katika miaka ya 1890 katika Sierra Leone. Treni ya kwanza ilianza kufanya kazi katika eneo la makoloni mwaka wa 1897 na kufikia 1909 reli kuu iliyopita katika ukanda tajiri wa miwese hadi Pendembu, Mashariki (km 365 au maili 227.5) ilikwishakamilika. Mara baada ya kazi kuanza katika Sierra Leone makoloni mengine nayo yakafuata mfano wake na kupata matokeo bora zaidi. Reli kubwa zote zilikwishajengwa ilipofika 1920.

Ni katika Rhodesia na Sierra Leone tu ambako watu binafsi walichangia katika ujenzi wa reli. Reli kuu inayoelekea kaskazini kupitia Rhodesia ilikuwa ni maendeleo ya mfumo wa reli za Afrika Kusini na ilijengwa na Kampuni ya Kiingereza ya Afrika ya Kusini. Ujenzi wa barabara ulifanywa na utawala wa kikoloni pamoja na tawala za kienyeji. Pale ilipowezekana, machifu wa Kiafrika waliwaandaa watu wao kuingiza uchumi wao katika uchumi ni wa dunia. Lakini barabara, kwa kawaida, zilikusudiwa kuwa viungo wala siyo badala ya reli ambazo zilikuwa kazi ya serikali. Hivyo, mlipa kodi alilazimika kuendelea na mifumo ghali tena duni.

Mchango muhimu sana wa usafiri wa kisasa ulikuwa ni kupungua ghafula kwa nauli za usafirishaji mizigo, ambako kulikuwa na matokeo mawili yenye kuhusiana. Kwanza, mashine zilitumika badala ya makuli na kuwaachia watu nafasi ya kushughulikia kazi nyingine za uzalishaji mali. Pili upunguzwaji wa gharama za usafirishaji uliowaongezea wazalishaji kiwango cha faida na kuwatia ari ya kupanua sekta ya biashara. Hata hivyo, wazalishaji wa Kiafrika walinufaika na maendeleo haya kwa nadra tu, donge nono lilikwenda kwa makampuni ya biashara na wengine waliokuwa wakijishughulisha na

upande wa mahuruji.

Katika majimbo ya masetla, nauli za bidhaa zilipangwa kuwanufaisha Wazungu, hivyo kulazimisha kilimo cha Waafrika kufidia kilimo cha masetla.

Kikorombwezo kingine kilichokuwepo kabla ya enzi za ukoloni, lakini kilichoongezeka ufanisi na umuhimu wake wakati wa ukoloni kilikuwa ni meli. Katika Afrika Magharibi ya Waingereza, kufikia 1900 uwanja huu ulikuwa umeshikiliwa na kampuni moja pekee ya Kiingereza iliyoitwa *Elder Dempster Line and Co. Ltd.*, ambayo ilikuwa ni muungano wa 1890 wa makampuni yote ya meli yaliyofanya kazi katika mwambao wa Magharibi. Katika Afrika ya Mashariki na Kusini shughuli za meli zilitawaliwa na*Union Castle Line.*

## *Afrika Kusini 1880 - 1935*

Miongoni mwa makoloni na himaya za Waingereza za Afrika, mabadiliko ya kiuchumi yaliyotokea Afrika ya Kusini yalikuwa ya aina yake na ya muhimu sana, lakini yenye kuleta athari mbaya sana kiasi kwamba yanafaa kupewa nafasi ya peke yake angalau kwa ufupi.

Mnamo 1869, Afrika ya Kusini ikiwa ni makoloni mawili ya Cape Colony na Natal na Boer au koloni la walowezi makaburu la Transvaal na Orange Free State ilikuwa masikini kama makoloni mengine ya Wazungu na makazi yao katika Afrika. Jumla ya Wazungu (waliokuwepo) ilikuwa ni watu 260,000 tu ambao asilimia 20 waliishi katika Cape Colony. Cape C ilikuwa ni mji mmoja tu yaani Cape Town ambao ulikuwa na watu zaidi ya 10,000. Kulikuwa na reli ya maili mbili tu mnamo 1860 na hapakuwa na barabara za magari. Usafiri wote ulitegemea magari ya kukokotwa na wanyama. Viwanda vilijishughulisha na kuunda mikokoteni ya kuvutwa na wanyama, samani, viatu na kutia rangi ngozi. Mahuruji ya Afrika ya Kusini katika 1860 yalikuwa ni ya mazao ya asili na zao la sufu likiongoza, likifuatiwa na chuma na ngozi yote yakiwa na thamani ya pauni 2.5 milioni kwa mwaka.

Si uchumi tu bali pia Jumuiya ya Afrika ya Kusini ilipata mabadiliko ya kimapinduzi katika kipindi cha miongo mitatu ya karne ya kumi na tisa. Haya yalitokana na hasa hasa na tukio moja tu, ugunduzi wa madini, kwanza almasi katika Griqualand katika 1867 na Kimberley katika 1870, halafu dhahabu katika Transvaal katika 1886. Katika kipindi cha miaka mitano tangu kugunduliwa katika Griqaaland almasi ya thamani zaidi ya pauni 1.6 milioni ilisafirishwa nje kila mwaka. Maendeleo ya uchimbaji dhahabu ya haraka sana baada ya kugunduliwa mwaka 1886. Mnamo 1890 dhahabu ya thamani ya pauni milioni 10 ilikuwa ikisafirishwa nje na kuifanya dhahabu bidhaa mahuruji kuu ya Afrika ya Kusini; thamani yake ilikwishafikia pauni 25 milioni mnamo 1905 na kati ya pauni 45 na 50 milioni mwaka wa 1910.

Athari za kufumuka kwa madini katika Afrika ya Kusini zilikuwa za ajabu na za mapana na marefu. Kisiasa, ugunduzi wa almasi kwanza ulileta kujitenga kwa eneo la Kimberly, halafu Transvaal yenyewe katika 1877 na mwisho kutwaliwa kwa Zululand katika 1879 baada ushindi dhalilishi wa Waingereza katika Isandhlwana. Vivyo hivyo ugunduzi wa dhahabu ulileta kujitenga kwa majimbo ya Kiafrika kusini mwa Mto

Limpopo. Uvamizi wa Jameson wa 1896, na mwisho Vita ya Pili ya Makaburu ya 1899 ambayo hatimaye ilizaa Muungano wa Afrika ya Kusini katika 1910.

Pili, ugunduzi ulisababisha mmiminiko wa mitaji na mafundi kutoka Uingereza, Ulaya na Marekani. Kwa yakini, karibu vitega uchumi vyote vilivyoingizwa katika makoloni ya Afrika kati ya 1880 na 1939 vilikwenda Afrika ya Kusini tu. Ni vitega uchumi hivi vilivyokuza viwanda vya madini na vikorombwezo vya Afrika ya Kusini kama tutakavyoona hivi punde.

Urefu wa reli uliongezeka toka km. 110 mwaka 1869 hadi 1700 km mnamo 1889, km 3300 mnamo 1899 na km 4190 mwaka 1905. Ujenzi wa barabara ulikwenda bega kwa bega na ujenzi wa reli. Mwishoni mwa Vita Kuu vya Kwanza maili 47,000 za barabara za majimbo na nyingi nyinginezo za mashamba zilikwishajengwa.

Athari ya nne ilionekana katika ulimwengu wa wafanyakazi na ardhi na pamoja na hayo uliingia upanukaji wa makazi ya mijini. Mahitaji ya wafanyakazi kwa shughuli za uchimbaji wa almasi na dhahabu hayakweza kutoshelezwa asilani. Ili kuhakikisha upatikanaji wa wafanyakazi, na hasa zaidi kulinda masilahi ya wazungu, msururu wa sheria ulipitishwa hasa katika miaka ya 1910 na 1920 kuwalazimisha Waafrika kuacha mashamba yao na mahala pao pa kuzaliwa kwenda kufanya kazi katika migodi na viwanda. Sheria hizi zilikuwa ni pamoja na *Natives' Land Act* (Sheria ya Ardhi ya Wenyeji) ya 1913. Sheria ya *Mines and Works Act* (Sheria ya Migodi na Kazi) ya 1911 na marekebisho yake katika 1926 na Sheria ya *Apprenticeship Act* (Sheria ya Uanagenzi) ya 1922. Sheria ya *Natives (Urban Act)* (Sheria ya Wenyeji) Maeneo ya Mjini) ya 1923.

Sheria ovu kabisa ya sheria hizi ilikuwa ni ile ya *Natives Land Act* ambayo kwayo asilimia 88 ya ardhi katika Afrika ya Kusini ilihifadhiwa kwa matumizi ya Wazungu tu ambao walikuwa asilimia 20 ya watu wote. Asilimia 12 iliyobaki iligawanywa katika msururu wa hifadhi za kienyeji kwa ajili ya Waafrika. Sheria ilisababisha kuhamishwa mara moja kwa maelfu ya wafugaji na wakulima mbalimbali kutoka ardhi na maskani yao ya asili na kutoka mashamba yaliyomilikiwa na Wazungu.

Sheria ya *Mines and Works Act* (Migodi na Kazi) ya 1911 na marekebisho yake ya 1926 na Sheria ya *Apprenticeship Act* Uanagenzi ya 1922 pia ziliwatoa Waafrika katika kazi nyingi na ufundi na kuweka ngazi mbalimbali za malipo kwa mafundi (wengi wao wakiwa Wazungu) na wasio na ufundi (wengi wao wakiwa Waafrika, Wahindi na Machotara). Katika mwaka 1935, mchimba madini Mzungu alikuwa akipata kwa wastani mara kumi na moja ya mshahara wa Mwafrika. Sheria ya *Natives (Urban) Act* (Wenye maeneo ya Mjini) ya 1923, Sheria ya *Native Administration Act* (Tawala za Kienyeji) ya 1927 na Sheria ya *Natives Service Contract Act* (Mkataba wa Huduma za Wenyeji) ya 1932 zote pia kwa pamoja ziliweka mipaka, na nyendo, makazi na ajira za Waafrika kwa manufaa ya wafanyakazi wa Kizungu.

Jumla ya athari za hatua zote hizi ikawa ni kuwang'oa Waafrika katika makazi na mashamba yao na kuwahamishia katika makazi mapya ya migodi na viwanda na kuwaweka katika mashamba ya Wazungu kama vibarua. Idadi ya vibarua katika machimbo ya madini iliongezeka sana katika kipindi tunachokizungumzia. Hadi 1906 migodi ilikwishaajiri watu 163,000. Wazungu 18,000, Waafrika 94,000 na Wachina 51,000; mnamo 1918

idadi hii ilikwishapanda na kufikia 291,000; kati yao hao Wazungu wakiwa 32,000.

Hapana budi kusisitiza kuwa kutokana na sheria mbalimbali zilizogusiwa, wafanyakazi wengi wa Kiafrika hawakuwa na kazi za kudumu bali za kuhamahama au za misimu. Kwa hiyo walilazimika kuishi kwa kuhamahama kati ya kazi uzunguni na maisha ya kijijini.

Athari nyingine muhimu ya neema za migodi ilikuwa juu ya miji. Kwa kuwa wafanyakazi walihamia kwenye maeneo mapya ya migodi na ya viwanda, miji mipya kabisa ilizuka na ile iliyokuwepo kukua haraka. Hivyo, Kimberly ambayo haikuwepo 1866 ilikuja kuwa mji wa watu 18,000 mwaka 1877, ambapo Johannesburg ilikuwa toka kijiji hadi mji mkuwa wa watu 166,000 mwaka 1800.

Asilimia ya Wazungu waishio mijini ilipanda toka 35.8 katika 1890 - 1891 hadi 65.2 mwaka wa 1936, na ile ya Waafrika toka asilimia 13 katika 1904 hadi 17.3 tu katika mwaka 1936.

Sekta nyingine mbili za uchumi wa Afrika ya Kusini pia zilikumbwa na maendeleo makubwa, kutokana na neema za migodi kwa kiasi fulani. Sekta hizi ni kilimo na tasnia za bidhaa. Uongezekaji mkubwa wa watu wa Afrika ya Kusini na wakazi wapya wa mijini ulileta masoko mapya kwa mazao ya kilimo na bidhaa za viwanda wakati huo huo vikorombwezo vipya kama reli na barabara vikarahisisha mazao na bidhaa hizi. Kati ya 1927 na 1935, serikali pia ilichukua hatua kadhaa kama vile kuanzishwa kwa ushuru wa kinga na kuanzishwa kwa halmashauri mbalimbali za masoko na kupanua huduma za benki kuwasaidia wakulima wa Kizungu dhidi ya wakulima wa Kiafrika. Matokeo yake yakawa kwamba wakulima wa Kizungu hawakufanikiwa kuzalisha mazao ya kutosheleza mahitaji ya ndani tu bali pia walianza kusafirisha nje mahindi tangu 1907, nyama na mayai baada ya Vita Vikuu vya Kwanza na sukari na bidhaa za maziwa tangu mwishoni mwa 1920 na kuendelea. Lakini hadi hapa Waafrika karibu walikuwa wamekwishang'olewa kwenye kilimo cha biashara na kuwa vibarua tu katika mashamba haya. Baya zaidi ni kwamba ujira wao ama ulibakia pale pale au ulipandishwa pole pole sana.

Jambo la mapinduzi zaidi lilikuwa mabadiliko yaliyotokea katika sekta ya viwanda, na haya ni ya mastaajabu zaidi kwani, kama tulivyokwisha kuona, haya hayakutokea katika sehemu nyingi za masoko katika Afrika. Kwa kujinufaisha na huduma zilizotajwa hapo juu, Wazungu walianza kukuza maendeleo ya uchumi, na kufika 1912 viwanda kadha vilikwishajengwa. Miongoni mwake vikawamo viwanda vya kuhifadhi matunda, kutengeneza jamu, kutengeneza pombe, sabuni, mishumaa, viwanda vidogo vya uhandishi vya kutengeneza mashine za upepo, pampu na kekee za kuchimbia maji, milango na nyuwa; mabuti, viatu na nguo. Kukua kwa sekta hii kulihimizwa hasa wakati wa Vita Vikuu vya kwanza kwa madhumuni ya kuchepua uchumi wa nchi, kupunguza kutegemea shughuli za madini na kutoa nafasi za kazi kwa Wazungu maskini.

Sekta ya viwanda ilikua haraka.zaidi baada ya mpomoko wa miaka ya 1920 na ya mwanzoni mwa 1930 na kufikia 1939 sekta ilikwishakuwa ya pili katika kuchangia uchumi wa taifa na madini yakiongoza.

Ni dhahiri kutokana na yote haya kwamba kati ya makoloni mengi, uchumi wa Afrika ya Kusini kwa hakika ulipata maendeleo ya kimapinduzi kwa kipindi kati ya 1880

na 1935. Kufikia 1932, pato ghafi la taifa lilifikia pauni 217 milioni na hii ilipanda hadi pauni 320 milioni katika 1937. Pia uchumi wake ukawa umecheptuka sana tofauti na chumi za nchi nyingi za Kiafrika ukitegemea kama ilivyokuwa juu ya madini, viwanda, na kilimo. Na yote haya yalitokana na ugunduzi wa dhahabu na almasi.

Hata hivyo, maendeleo yote haya muhimu sana yalipatikana kwa jasho la watu wa Afrika wasio Wazungu hususa Waafrika na Machotara. Katika maeneo ya hifadhi wingi wa watu na umaskini vilizagaa; jambo lililosababisha uhamaji usio kifani wa watu kuelekea mijini na kwenye migodi ambako Waafrika walijaa katika magenge na mabanda mabovu. Baya zaidi, watu hawa hawakuruhusiwa kuweka maskani ya kudumu sehemu hizi na aila zao lakini wengi wao wakawa wahamiaji wa muda wakizurura kati ya mjini na mashamba. Waafrika na Afrika ya Kusini waliong'olewa maskanini, wakanyang'anywa ardhi, wakalipwa ujira duni na kubaguliwa. Waliteseka kiuchumi na kijamii zaidi kuliko Waafrika wengineo popote pale katika Afrika kwa kipindi hiki tulichokipitia

# 17

## Uchumi wa Kikoloni: Afrika Kaskazini


Uchumi wa kikoloni katika nchi za Kaskazini mwa Afrika haukutofautiana sana na uchumi wa nchi za kanda zilizokwishajadiliwa kwani eneo lote hili lilitawaliwa na mataifa beberu yale yale. Tunisia, Algeria na Moroko zilitawaliwa na Wafaransa. Libya ilitawaliwa na Waitalia, na Misri na Sudani zilitawaliwa na Waingereza (mchoro 17.1). Hata hivyo inaelekea kuwa kwa ujumla, tukiacha kando ujenzi wa viwanda, uchumi wa nchi hizi ulifanana zaidi na uchumi wa kikoloni wa kanda za Wareno, Wafaransa na Wabelgiji kuliko ulivyofanana na wa kanda za Waingereza.

### *Uchumi wa Tunisia, Algeria na Moroko*

Hadi kufikia mwisho wa Vita vya Kwanza Wafaransa walikwishaanzisha taasisi za siasa, utawala, uchumi na fedha katika Tunisia, Algeria, na Moroko na walikwishaanzisha utaratibu wa kuwanyang'anya mali *fallahin* na kuchota utajiri wote na kuupeleka kwao. Shughuli zote hizi zilipunguzwa kasi na vita lakini zilianza tena mara tu vita vilipokwisha; kwanza katika kilimo kisha katika uchimbaji madini na muundo-mbinu, na hatimaye katika shughuli za fedha.

### Kilimo

Kwa upande wa kilimo utaratibu wa kuchukua rasmi ardhi kutoka kwa wananchi ikagawanywa vipande vipande na kupewa masetla wa Kizungu ulianzishwa tena na kwa kasi zaidi katika Algeria. Hadi kufikia mwaka 1930 kulikuwa na mashamba ya masetla yapatayo 25,795 yenye ukubwa wa wastani wa hekta 20 kila moja; yote kwa pamoja yakiwa na eneo la hekta 2,334,000. Katika Tunisia utaratibu wa kuwanyang'anya mali *fallahin* mara tu baada ya nchi hiyo kuwa katika hifadhi ya Wakoloni mnamo mwaka 1881. 'Ukoloni kwa njia ya Mitaji (1881 -1882), utaratibu ulioruhusu mashamba makubwa ya kibepari *(Compagnie des Batignolies, Societe Marseillaise de Credit, Societe Fonciere* de Tunisie, n.k.) kuchukua karibu hekta 430,000, ulifuatiwa na 'ukoloni rasmi' ambao kusudi lake kubwa lilikuwa ni kuongeza taratibu idadi ya Wafaransa katika Tunisia na kukuza 'ukoloni wa Wafaransa'. Mpango huu ulitengewa mafungu makubwa ya pesa. Mbali na sheria zilizotungwa zilizoelekea kuhamisha ardhi iliyomilikiwa na Watunisia na kuwapa Wafaransa mamlaka ya nchilindwa yaliwapa masetla misaada mikubwa ya fedha. Katika mwaka 1931 mashamba ya masetla katika Tunisia yalikwishafikia hekta 700,000; zaidi yakiwa katika sehemu zenye kupata maji ya kutosha na zilizo na rutuba nyingi zaidi.




17.1 *Afrika Kaskazini-Magharibi: maendeleo ya kiuchumi katika kipindi cha ukoloni*

Katika Moroko Utawala wa nchilindwa ambao ulikusudiwa kufanya makazi makubwa ya Wazungu katika dola yote ya kisharifu, nao halikadhalika upanga kwa mbinu njia za kuiweka rasmi nchi hiyo chini ya ukoloni wao. Ulitoa ardhi ya jumuiya na ile iliyomilikiwa na serikali na kuifanya mashamba ya masetla yenye maeneo ya ukubwa mbalimbali. Asilimia 60 ya masetla hao ilitoka Algeria. Ardhi hii haikutolewa bure kama ilivyokuwa katika Algeria bali iliuzwa kwa bei ndogo, kama ilivyokuwa katika Tunisia. Tofauti ya hapa na Tunisia ni kwamba katika Moroko masetla walipewa misaada mbalimbali, kama vile kusaidiwa gharama za kufyeka mashamba, kusamehewa ushuru wa forodha juu ya zana za kilimo zilizoingizwa nchini, na kadhalika. Katika kipindi hiki hiki (1922 - 1932) ukoloni binafsi ulichukua zaidi ya hekta 350,000.

*Sifa za Ukoloni wa Kilimo*

Ingawa serikali ilijitahidi kufanya jitihada kubwa za kuongeza idadi ya Wafaransa vijijini ukoloni rasmi haukuweza kuwaingiza masetla wengi wa Kifaransa katika vijiji vya Afrika Kaskazini. Tukiacha wakulima wa hapa na pale wa sabibu na matunda (Waitalia katika Tunisia na Wahispania katika Moroko) masetla wa Kizungu hawakuweza kuhesabiwa kama kundi hasa la wakulima wadogo wadogo kama ilivyokuwa katika Ufaransa wakati huo. Wao zaidi walikuwa wakulima wakubwa wenye mashamba makubwa sana; wenye zana mbali mbali za kilimo na mara nyingi wakiwa na majamba ya kuvutia sana katika mashamba yao.

Kilimo chao kilikuwa kimelenga zaidi soko la nje kuliko soko la ndani. Masetla wengi walijishughulisha na kilimo cha zao moja tu, kama vile zabibu katika eneo la Oran huko Algeria na nafaka za zaituni (katika Tunisia).

Kilimo hiki ambacho kilitumia trekta, zana za kuvutwa kwa trekta, mashine za kuvuna na mbinu nyingine za hali ya juu, mara nyingi kilizalisha mazao mengi. Mazao katika sekta zote yaliendelea kuongezeka kati ya 1919 na 1929; utengenezaji wa mvinyo katika Tunisia ukaongezeka sana kutoka *hektolitachl* 498,148 hadi kufikia *hektolitachl 918,583* kati ya mwaka 1920 na mwaka 1925; na katika Algeria, ambako wastani wa utengenezaji wa mvinyo kati ya miaka 1916 - 192o ulikuwa 6,853,000 ukaongezeka kuwa *hektolitachl* 18371,000 katika miaka ya 1931 - 1935. Fallahin wa Moroko walipata *kwintal* 1,316,000 tu kutoka kwenye eneo kubwa sana (hekta 222,815). Soko la ndani halikuweza kuhimili engezeko kubwa la mazao ya kilimo.

Je, wenyeji wa nchi hizi nao walikuwa na hali gani? Karibu na Vita vya Kwanza vya Dunia watu wengi wa Afrika Kaskazini (karibu asilimia 80) hawakuwa na ardhi huko vijijini. Mfumo wa kumiliki ardhi zaidi ulikuwa wa *mulk* (watu binafsi), *arsh* (ardhi ya jumuiya) na katika Tunisia na Moroko *habus* (ardhi inayomilikiwa na shirika fulani). Katika maeneo ya ardhi ya *mulk* kulikuwa na utaratibu msonge wa wamiliki ardhi; juu kabisa kukiwa na watu wachache wenye mashamba makubwa sana na ambao walimiliki maeneo muhimu ya ardhi ya kilimo na malisho. Wengi wa wakulima hawa walikuwa Moroko. Katika Algeria pia ingawa kulikuwa na mashamba makubwa ya masetla maeneo makubwa ya Waislamu yalichukua sehemu kubwa ya ardhi baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Hali kadhalika katika Tunisia kulikuwa na koo bora zilizoishi Tunis na ambazo

zilimiliki ardhi. Ardhi yao zaidi ilikuwa katika sehemu za kilimo cha nafaka za Tell (maeneo ya Bedja, Mateur na Kef). Ardhi hii ililima kwa ustaarabu wa kulipa 1/5 ya mazao yaliyopatikana uliojulikana kama Khammasat na ambao ulitumika pote Afrika Kaskazini. Utaratibu huu haukuruhusu maendeleo makubwa ya mbinu za kilimo.

Vijiji vidogo vidogo vingi vilizunguka miji katika maeneo tambarare yenye rutuba kama yale ya Sa'is katika Moroko na Medjerdia ya kati katika Tunisia, katika milima ambako kulikuwa na watu walioamua kukaa na kulima (Kabylia, Rif. na High Atlas ya Magharibi), na katika Oasisi.

Uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo ulibadilika badilika kutegemea kiwango cha mvua; na ingawa njaa iliendelea kupungua bado ilikuwepo mara kwa mara. Aidha utaratibu wa mikopo ya riba kubwa bado uliendelea kuleta ghasia huko bara na ni wakulima wenye mashamba makubwa tu walioruhusiwa kutumia taasisi za mikopo zilizoanzishwa na Wazungu. Lakini mapema katika Tunisia (1907) na baadaye katika Moroko (1922) *Societies indigenes de_prevoyance* (vyama vya wananchi vya kuweka akiba) vikaanzishwa hasa kwa madhumuni ya kuwapatia mikopo ya mbegu *fallahin* wadogo. Lakini misaada ya kifedha iliyotolewa na Mamlaka ya Kikoloni kwa masetla ilikuwa mikubwa zaidi.

## Uchimbaji Madini

Kukaa kwa Wazungu katika nchi tatu za Afrika Kaskazini hakukufanya tu ardhi kuwa bora ichukuliwe na masetla bali pia kulisababisha uchimbaji wa maliasili za ardhi na ambazo zilitumiwa zaidi kwa manufaa ya makampuni ya kigeni. Maliasili hizi zilipimwa mapema sana na kuchimbwa kwa haraka. Katika Algeria migodi ya kwanza ilianzishwa katika mwaka 1845; katika Tunisia mashapo ya fosfeti katika eneo la Kafsa yalikwishagunduliwa mnamo mwaka 1885 - 1886 (miaka minne tu baada ya kuanzishwa kwa Nchilindwa) na uchimbaji wake ukaanza mwaka 1889 na kuendelea. Katika Moroko, uchimbaji migodi wa kikweli kweli haukuanza hadi baada ya 1928 wakati wapimaji madini na wenye kuomba ruhusa ya kuchimba madini walipoivamia nchi kama makundi ya nzige. Hadi kufikia mwaka 1930 Moroko ilikuwa imaelekea kuwa mojawapo ya nchi za Afrika Kaskazini zenye utajiri mwingi wa rasilimali za madini ikiwa inatoa zana za chuma, mangani, kobati, plumbi na bati, pamoja na fosfeti umbayo ndiyo yalikuwa yakipatikana kwa wingi. Usafirishaji nje wa fosfeti uliongezeka toka tani za kimetriki 8,232 katika mwaka 1921 hadi kufikia tani 1,179,000 katika mwaka 1930.

Katika Algeria na Tunisia mashapo ya fosfeti (Kuwayf na Kafsa), chuma (Beni Saf, Wenza na Djarisa), plumbi, zinki n.k. yalikwishaanza kuchimbwa kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia na karibu madini yote yaliyozalishwa yalisafirishwa kwenda Ufaransa na nchi nyingine za kimagharibi. Madini haya yalichimbwa na makampuni ya kigeni tu, hasa yale ya Kifaransa ambako ndiko kulikotoka mitaji, wataalamu, wasimamizi na kadhalika.

Mawasiliano na Bandari

Ili kuunganisha mashapo mbalimbali ya madini na bandari za kusafirisha mazao reli zilijengwa mapena sana katika Algeria (kuanzia 1844) na katika miaka ya mwanzo ya nchilindwa katika Tunisia na Moroko. Hadi kufikia 1919 njia muhimu za reli za Tunisia na Algeria zilikwishajengwa; ziliunganisha miji mikubwa (mingi ikiwa karibu na pwani) na pia zikaunganisha migodi na bandari muhimu za kusafirishia bidhaa (Oran, Algeria, Tunis, Sfax, Sousse). Katika Moroko ujenzi wa reli, ambazo zilikusudiwa kuunganisha migodi na miji mikubwa, na ambazo zilijengwa na makampuni ya kigeni peke yake, ulifanyika pole pole sana kiasi kwamba reli ya kwanza kabisa, Casablanca - Rabat, ilizinduliwa Aprili, 1923. Barabara pia zilijengwa kuunganisha miji mikubwa, ambamo Wazungu wengi waliishi, na zile sehemu za bara ambako kulikuwa na mashamba ya masetla. Bandari nazo halikadhalika zilijengwa na kuendelezwa hususa kwa kuingizia bidhaa za Kifaransa na nchi nyingine za kigeni katika nchi za Afrika Kaskazini na kusafirishia nje madini na bidhaa nyingine za kilimo.

*Mfumo wa Ushuru wa Hazina*

*Mfumo wa ushuru*

Kwa kuwa Algeria ilikuwa koloni la Ufaransa bidhaa za Kialgeria ziliruhusiwa kuingia Ufaransa bila kutozwa ushuru na za Ufaransa pia zikaingia Algeria bila kutozwa ushuru. Bidhaa za kigeni zilizoingizwa ama katika Ufaransa au Algeria zilikuwa na sheria za ushuru za aina moja. Kutokana na utaratibu wa kuhodhi kwa bendera meli za Kifaransa ndizo pekee zilizokuwa na haki ya kuabiri kati ya bandari za Algeria na za Ufaransa. Kwa hivyo kulikuwa na muungano halisi wa mambo ya ushuru baina ya Ufaransa na Algeria. Lakini muungano huu uliifanya Algeria ibakie tu kuwa ya kusafirishia nje malighafi na bidhaa za kilimo na kuagiza bidhaa zilizokwishatengenezwa.

Mfumo wa ushuru katika Tunisia baada ya Vita Vikuu vya Dunia ulitawaliwa na sheria za tarehe 19 Julai 1890 na tarehe 2 Mei 1898. Sheria hii ya mwisho ilizipa upendeleo wa kwanza bidhaa zilizotengenezwa Ufaransa, hasa bidhaa za metali, mashine, nguo n.k. Bidhaa za kigeni za aina hiyo hiyo nazo pia zilikuwa hazitozwai ushuru. Kutokana na hali hiyo hiyo nazo pia zilikuwa hazitozwi ushuru. Kutokana na hali hiyo soko la Tunisia lilijaa bidhaa zilizotengenezwa Ufaransa na nchi nyingine za kigeni. Katika mwaka 1928 kulianzishwa namna fulani ya mwungano wa mambo ya ushuru. Bidhaa za kilimo za Kitunisia zilizoingizwa bila ushuru hazikuathiriwa tena na mfumo wa kwota, lakini bidhaa za Kifaransa ama zilisamehewa moja kwa moja kulipiwa ushuru au zililindwa zisiangushwe na bidhaa nyingine za kigeni za aina hiyo.

Uhusiano wa kibiashara na kiushuru baina ya Moroko na nchi nyingine za kigeni ulikuwa mbaya na usiolingana na kimaslahi. Sheria ya Algeciras (1906) iliweka msingi wa kuzingatiwa kwa usawa wa uchumi baina ya nchi zilizowekeana mikataba kuhusu soko la Moroko. Bidhaa zilizoingia Moroko zililipiwa ushuru wa asilimia 10 wa *ad valorem*

pamoja na nyongeza ya ushuru wa asilimia 2.5 kwa ajili ya *Caisses Speciale des Travaux Publics* (Mfuko Maalumu kwa ajili ya kazi za umma). Ushuru huu ulilipwa bila kujali bidhaa zilitoka mahali gani na zilikuja kwa meli gani. Utaratibu huu wa kumwacha kila mtu aje ulizifanya nchi zenye kusafirisha bidhaa kwa wingi ziijaze Moroko na bidhaa zao za kilimo na viwandani. Ili kulinda viwanda vyake vichanga visife Moroko iliamua kutumia vizuizi visivyo vya wazi kwa kuzuia kuingizwa nchini kwa baadhi ya vyakula vya kigeni kama vile ngano, shayiri na unga.

Aina ya bidhaa za Afrika Kaskazini zilizosafirishwa nje ilidhihirisha aina ya uchumi wake na mfumo wake wa ushuru wa forodha. Kutokuwepo na uwiano baina ya bidhaa zilizonunuliwa na bidhaa zilizouzwa na Afrika Kaskazini ndiko kulikosababisha kuendelea kuwepo kwa upungufu wa urari wa kibiashara; bidhaa zilizokuwa zikiingia zilikuwa na thamani kubwa zaidi kuliko zile zilizokuwa zikitoka, kwa nchi zote tatu. Mwisho, mfumo wa utozaji ushuru wa forodha kwa kiasi kikubwa ndio uliosababisha kuanguka kwa tasnia za vijijini na mijini.

*Mfumo wa hazina ya Serikali*

Mojawapo ya mambo ambayo mamlaka za Kifaransa zilifanya zilipoichukua Afrika Kaskazini ilikuwa ni kupanga upya mfumo wa hazina na fedha za serikali. Walianzisha Tawala ya Fedha (*Financial Administration*) ambayo kazi yake ya kwanza ilikuwa kutayarisha bajeti na kukagua matumizi ya fedha. Uangalifu mkubwa na nidhamu juu ya bajeti viliwawezesha kutunza vizuri mizania: na hii ilifanikiwa vizuri baina ya miaka 1919 na 1930.

Mapato ya hazina yalitokana na ushuru wa forodha na kodi zilizotozwa kwenye ardhi, mazao ya kilimo (*tartib* katika Moroko) na bidhaa nyingine za walaji (kodi siziso dhahiri). Ushuru na kodi hizi zote ziliwaangukia zaidi wenyeji ambao mara nyingi mzigo huu kwao ulikuwa mkubwa sana.

Aidha, ili kununua vifaa mbalimbali nchi zote tatu za Afrika Kaskazini zililazimika kukopa mara kwa mara. Katika mwaka 1930 Algeria ilikuwa inaiwia Ufaransa faranga 2000 milioni, na katika mwaka 1932 Moroko ilikuwa inaiwia Ufaransa faranga 1691 milioni. Vifaa na zana zilizonunuliwa kwa mikopo hii zilinufaisha zaidi kwanza sekta za kisasa za uchumi ambazo ziliwahusu zaidi Wazungu lakini sehemu kubwa ya madeni haya ililipwa na fedha za Waislam. Katika mwaka 1931 malipo ya deni la Moroko yalichukua zaidi ya theluthi moja ya bajeti ya nchi.

Msukosuko na Sekta Kubwa za Uchumi wa Afrika Kaskazini

Msukosuko mkuu wa uchumi wa 1930 - 1935 uliisonga Afrika Kaskazini kwa kuchelewa kidogo. Athari zake kubwa zilianza kuonekana kuanzia mwaka 1932 na kuendelea; lakini zilionekana mapema zaidi katika Moroko kuliko katika Tunisia au Algeria. Wakati huu Moroko ilikuwa katika awamu ya maendeleo ya uchumi wake.

Mojawapo ya sekta za uchumi zilizoathiriwa na msukosuko huu wa uchumi ilikuwa kilimo cha masetla ambacho kilitegemea sana mikopo na masoko ya nje. Bei za

bidhaa ziliposhuka ghafula na njia za usafirishaji bidhaa nje zilipofungwa au kupungua sana wale wakulima wakubwa lakini wenye kutegemea mikopo hawakuweza tena kuheshimu mikataba yao na mashirika mbalimbali yaliyowapa mikopo. Hali kadhalika hii ilijitokeza kwa upande wa migodi, ambayo nayo ilitegemea masoko ya nje kwa sababu malighafi za madini yake hazikusafirishwa wala kutumia katika nchi zalishi.

Uchumi uliotokana na bidhaa pia uliathiriwa na msukosuko huu; mchango wake kwenye bidhaa za kilimo zilizosafirishwa nje ukaathiriwa na kuanguka kwa bei. Na vivyo hivyo kwa upande wa tasnia za ufundi ambazo nazo zilikuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa miji mikubwa nchini Moroko (Fe, Mekres na Marrakesh) na Tunisia (Tunis, Kayraw na Safakus) na ambazo uuzaji wa bidhaa zake nje ulikoma kabisa. Sekta ya kwanza ya kilimo ya Kizungu ambayo iliathitika na msukosuko huu ilikuwa ni tasnia ya mvinyo, ambayo ndiyo ilitegemea zaidi masoko ya nje hasa soko la Ufaransa. Wastani wa bei ya kuuza ya hektalita 1 ya mvinyo, ambao katika mwaka 1927 ulifikia faranga 168, ulishuka na kufikia faranga 108 katika mwaka 1931 na chini zaidi hadi kufikia faranga 54 katika mwaka 1934.

Msukosuko huu pia uliiathiri tasnia ya halizeti, hasa ile ya Tunisia. Kiasi cha mafuta yaliyosafirishwa nje kutoka Tunisia kilishuka kutoka kwantili 409,800 katika mwaka 1930 na kwenda chini ya 200,000 katika mwaka 1936.

Sekta ya tatu ya kilimo ambayo iliathiriwa na msukosuko huu na ambayo ilikuwa muhimu kwa fallahin na masetla ilikuwa kilimo cha fanaka. Katika sekta hii kushuka kwa bei moja kwa moja kulisababisha kushuka kwa kiwango cha kusafirisha nje mazao: thamani ya ngano ya Tunisia iliyosafirishwa nje na Wazungu, ilishuka kutoka faranga 291,408,000 katika mwaka 1931 hadi kufikia faranga 60,845,000 katika mwaka 1934.

Tasnia ya migodi pia ikaathirika vibaya. Kusafirishwa nje kwa fosfeti ya Moroko kukashuka toka tani 1,779,000 mnamo mwaka 1930 hadi kufikia tani 900,731 katika mwaka 1931; katika Tunisia kiasi cha fosfeti iliyosafirishwa kilishuka toka tani 3,600,000 hadi kufikia tani 1,623,000 mnamo mwaka 1932. Msukosuko huu ukasababisha kufungwa kwa migodi mingi sana hasa ile iliyokuwa haileti faida kubwa sana.

*Athari za Msukosuko*

Katika hali kama hii haishangazi kuona kwamba katika nchi zote tatu za Afrika Kaskazini thamani ya jumla ya biashara ya nje ilianguka taratibu katika miaka ya 1931 na 1936. Thamani ya biashara ya nje ya Tunisia ikashuka katika mwaka 1936 karibu kwa asilimia 40 ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika mwaka 1927 - 1928. Katika Moroko jumla ya thamani yote ya biashara ya nje ilishuka kutoka faranga 3,780,606 katika mwaka 1929 hadi kufikia faranga 1,750,513 katika mwaka 1935; huko Algeria ilishuka toka faranga 9,983,000 katika mwaka 1930 hadi kufikia faranga 6,702,000 katika mwaka 1936.

Msukosuko huu ulikuwa na athari kubwa sana za kijamii. Masetla waliokuwa wameegemea sana mikopo na wakulima wa Afrika Kaskazini ambao hawakuweza kuheshimu mikataba yao walifilisiwa. Idadi kubwa ya watu ambao hawakuwa na madeni walichukua mikopo na kuweka rehani mali zao. Wakulima wa chini na wa kati ambao hawakuweza kupata mikopo ya benki kutoka taasisi za kilimo ilibidi wakakope kwa watu

binafsi huko vijijini au mijini ili kuweza kulipa madeni yao.

Msukosuko ulizidisha mgawanyiko wa kijamii kwa kuwawezesha wenye mapesa (mara nyingi wakiwa pia ni wakopeshaji fedha), wafanyabiashara wakubwa na matajiri wenye kumiliki maeneo makubwa ya ardhi mijini na mashambani kuongeza utajiri wao kwa kiwango kikubwa. Mali na kilimo zaidi vikawa katika mikono ya watu wachache sana waliomiliki mali vijijini (na mara nyingi mijini pia). Kutokana na msukosuko wa kilimo na maafa ya kimaumbile, ukame na njaa vikawa mambo ya kawaida katika sehemu nyingi za Afrika Kaskazini, hasa katika maeneo ya mapululu.

Athari nyingine iliyotokana na hali hiyo mbaya ya uchumi ilikuwa ni kuongezeka kwa uhamaji wa *fallahin* na kukimbilia mijini ili kuepuka hali duni zilizokuweko vijijini, njaa au kuwakimbia watoza kodi. Hii ilisababisha kuanzishwa kwa viunga vya miji.

Mwisho hali hii mbaya ya uchumi ilisababishwa kusimamishwa kwa kazi za ujenzi, migodo ikafungwa na karakana pia. Matokeo yake yakawa ni ukosefu mkubwa wa kazi kati ya wakazi wa miji, mafundi na wafanyakazi wengineo.

Hali ya namna hii haikuacha kuwatia wasiwasi viongozi wa serikali waliohusika. Hatua muhimu zilizochukuliwa na mamlaka za kikoloni na serikali ya Ufaransa zilihusu zaidi sekta ya kilimo. Hatua zilizochukuliwa kuisaidia tasnia ya mvinyo zilikuwa ni pamoja na ongezeko la kiasi cha mvinyo kilichoingizwa nchini bila kutozwa ushuru na kupiga marufuku kupanuliwa au kuanzishwa kwa mashamba mapya ya zabibu katika Afrika Kaskazini. Ili kukisaidia kilimo cha nafaka kulianzishwa akiba ya ngano ngumu na ngano laini na zikapangiwa kiwango cha chini kabisa cha bei. Mauzo ya nafaka iliyorundikana yakafanywa kwa nyakati mbalimbali na watu wakapewa mikopo.

Taabu zilizowapata wananchi vijijini na matokeo yake ya wananchi kuungana na kushikamana kitaifa zilizifanya mamlaka za Kifaransa zianze kuchunguza na kujaribu kuwaelewa *fallahin* wa Afrika Kaskazini. Kuanzia 1933-1935 sera ya wakulima wadogo ilianzishwa katika nchi zote tatu za Afrika Kaskazini. Katika Algeria sheria ya tarehe 9 Julai, 1933 ilianzisha *Fonds Commun des Societes Indigenes de Prevoyance* (Bohari la Vyaa vya Akiba ya Wenyeji) ambayo iliuwezesha utawala kutoa mikopo na misaada kwa Waislamu peke yao kwa kupitia *Societe in indigenes de Prevoyance*. Akiba hii pia iliwasaidia *fallahin* kujikomboa katika madeni kwa kuwapa mikopo ya kulipia madeni hayo. Idara ya 'Uchumi wa Jamii' chini ya Kurugenzi ya Mambo ya Wenyeji ilianzisha hatua fulani fulani za kuzifanya mbinu za uzalishaji za *fallahin* ziwe za kisasa. Ilitoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya upandaji miti na mikopo ya chambele kwa ajili ya kununulia mbolea, majembe ya kuvutwa na ng'ombe n.k. Lakini hatua zote hizi ingawa zilikuwa zenye manufaa makubwa hazikuweza kutosheleza.

Katika Tunisia na Moroko serikali nayo ikaamua kutoa mikopo kwa jamii ya vijijini, kusawazisha matatizo ya umitikaji ardhi na kukifanya kilimo cha *fallahin* kiwe cha michepuo mbalimbali.

Mwisho ili kuondoa kabisa mfumo wa kilimo cha aina moja, hasa miongoni mwa wakulima wa Kizungu, ambacho hatari yake ilionekana wazi wakati wa msukosuko wa uchumi Serikali iliamua kukuza kilimo cha mazao mbalimbali kwa kuwashawishi watu kupanua kilimo cha matunda na bustani za mboga. Pia waliendeleza kilimo cha

umwagiliaji maji kwa kujenga mabwawa.

Mashamba makubwa ya michungwa, miti ya klementina na milimao yalilimwa Mitidja, huko Algeria; Cape Bon, huko Tunisia; na katika Casablanca, Khenifra, Meknes, Mudja n.k. huko Moroko.

Mashirika ambayo nusu yalimilikiwa na serikali na nusu na watu binafsi kama vile *Office Tunisien de Standardisation* yalianzishwa kushughulikia ufugaji, uuzaji na usafirishaji nje wa matunda.

Hata hivyo uchumi wa Afrika Kaskazini ulibakia wa kuegemea kilimo. Kulikuwa na viwanda vichache vya kusindika bidhaa vilivyokuwa vikitumia mazao ya kilimo kama vile vinu vya unga, vinu vya mafuta na mashine za kukeneka. Kampuni, ambazo nyingi zilikuwa ndogo ndogo, zilikuwa zikimilikiwa na Wazungu na idadi ya wafanyakazi katika kiwanda haikuwa kubwa: 40,000 kwa Algeria yote. Ingawa maendeleo ya viwanda nchini yalikuwa katika kiwango cha chini sana, hata hivyo miji ya Afrika Kaskazini ilikuwa inakua kwa haraka sana kwa sababu ya wingi wa watu fukara waliokuwa wakihamia humo kutoka vijijini. Mji wa Casablanca ambao mnamo mwaka 1900 ulikuwa na wakazi 20,000 kufikia mwaka 1936 ulikwishakuwa na wakazi 257,000.


Ndiyo kusema katika kipindi kilichotangulia Vita vya Pili vya Dunia uchumi wa Afrika Kaskzini, kimsingi ulikuwa wa kikoloni. Sekta za uchumi katika Afrika Kaskazini ambazo zilikuwa na Waafrika wengi zilishindwa kuendelea kwa sababu ya ukosefu wa fedha, matumizi ya mbinu za kikale, vishamba vidogo, na kwa sababu wao walihamishiwa kwenye ardhi zisizo na rutuba. Ama kwa hakika wenyeji wa Afrika Kaskazini hawakuwemo katika sekta za kisasa za uchumi (yaani mabenki, migodi, viwanda vya kuhifadhi; mazao na mpango wa maendeleo na mipango). Lakini sekta hizi, ambazo zilitawaliwa na mitaji kutoka nje, zilitegemea sana maamuzi ya masoko na vyombo vya nje; ambavyo Waafrika wa Afrika Kaskazini hawakuwa na miliki navyo.

## *Libya, Misri na Sudani* (taz. 17.2)

### Libya

Wakati wa enzi za ukoloni uchumi wa Libya uliegemea zaidi kilimo (ikiwa ni pamoja na ufugaji wanyama) na biashara. Kazi ya kilimo ilifanywa vijijini ambapo biashara ilifanywa mijini. Kwa watu wengi shughuli hizi mbili ndizo zilizokuwa muhimu na njia ya kupatia mapato yao. Watawala wa Kituruki hawakujaribu hata kidogo kuibadilisha hali hii. Hata hivyo Waitalia walijaribu kuanzisha mabadiliko makubwa katika uchumi. Sehemu ya kwanza ya maelezo haya inashughulikia na miaka ya mwisho ya utawala wa Kituruki na sehemu ya pili inaelezea uchumi katika utawala wa Waitalia.

Katika enzi za utawala wa Kituruki (1880-1911) uchumi wa nchi ulikuwa umedumaa na shughuli za uchumi zikawa ni za kilimo, biashara na ufundi mdogomdogo tu. Aidha kilimo cha wakati huu kilibakia kuwa kile kile cha kizamani. Majembe ya kukokotwa na ng'ombe yalitumiwa kulimia. Mazao muhimu yalikuwa ngano na shayiri. Mazao mengine yalikuwa tende, mafuta ya zaituni, matunda ya jamii ya machungwa na




**17.2** *Libya, Misri na Sudan: maendeleo ya kiuchumi katika kipindi cha ukoloni*

malimao, na ufugaji. Uzalishaji wa mazao ya kilimo ulitegemea sana kiwango cha mvua ambacho kilibadilika badilika kulingana na majira ya mwaka. Makundi makubwa ya wanyama yalifungwa katika tambarare za Cyrenaica na Tripoli.

Kwa upande wa biashara, kutokana na kutokuwepo kwa barabara nzuri na njia za kisasa za usafirishaji, misafara ilitumiwa kubeba mizigo kati ya miji mikubwa katika Tripoli na nchi nyingine jirani kama vile Borno na Hausaland.

Misafara ya biashara ilipeleka bidhaa za vioo, nguo, hariri, viungo na pilipili katika Borno na Wadai na ikaleta bidhaa kama vile ngozi, pembe za ndovu, na manyoya ya mbuni. Lakini kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa biashara ya misafara ikaanza kufifia. Kutawaliwa kwa nchi nyingine za Kiafrika na Wakoloni kukaleta njia nyingine mpya zisizokuwa na gharama kubwa. Njia za kisasa na bora zaidi za usafirishaji zikachukua nafasi ya zile za zamani. Matokeo yake yakawa ni kutoweka pole pole kwa umuhimu wa biashara ya misafara. Kwa upande mwingine bandari kuu za Tripoli na Benghazi zilizanya biashara motomoto na Ulaya na nchi za jirani. Bidhaa zilizosafirishwa katika nchi hizo zilikuwa ng'ombe, kondoo, sufi, manyoya ya ngamia, tendo, shayiri, ngano na nyasi za esparto. Bidhaa zilizoingizwa nchini zilikuwa pamba, nguo za hariri, vioo, silaha (bunduki), mchele, sukari, chai na kahawa.

Viwanda vilikuwa vichache na vidogo vidogo vikishughulikia zaidi vifaa vya ufundi. Viwanda hivi vidogo vidogo vilijumuisha utengenezaji nguo, usukaji mikeka, dawa za rangi, sabuni na vitu vilivyotengenezwa kwa fedha na dhahabu.

Ingawa himaya ya pili ya Kituruki katika Tripoli ilidumu kwa zaidi ya miaka sabini hakuna jitihada kubwa zilizofanywa kuuinua uchumi wa Libya. Hapakuwa na sera ya wazi ya kuufanya bora muundo-mbinu wa uchumi kama vile barabara, bandari na mfumo wa elimu. Kulikuwa na shule chache sana za ufundi katika Libya wakati huo.

Jambo peke yake ambalo utawala wa Kituruki ulielekea kujali ni ukusanyaji wa kodi. Mfumo wa kodi uliokuwa ukitumika Tripoli wakati wa utawala wa Kituruki ulikuwa ni wa kodi ya kichwa kwa watu wazima wa kiume, 1/10 ya mazao ya kilimo na kodi ya mapato. Kodi nyingine zilikuwa ni pamoja na kodi ya kumiliki ardhi, kodi ya mirathi na kodi ya kusamehewa kwenda kutumikia jeshi ambayo ilitozwa kwa watu wazima wa kiume wasiokuwa Waislam. Kodi ya mhuri kwenye dhahabu na fedha na ushuru wa forodha zilitozwa kwa bidhaa zote zilizoingia nchini au kusafirishwa nje. Aidha serikali ilipata mapato makubwa kutokana na chumvi na tumbaku, mazao ambayo ni serikali pekee iliyamiliki. Kodi hizo ziliongezea mzigo kwenye uchumi na zikachangia katika kulegalega kwake. Kodi hizi pia zilichochea migomo kadhaa ambayo ilileta kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa na kudhoofisha utawala wa Kituruki katika nchi hii.

*Sera ya uchumi katika kipindi cha Utawala wa Waitalia*

Italia ilipoivamia Libya mnamo mwaka 1911 ilikuwa imeazimia kulifanya koloni hili mahala pa kupatia malighafi kwa ajili ya viwanda vyake, soko kwa ajili ya bidhaa zake, na njia ya kutatulia tatizo lake la wingi wa watu. Nia ya Waitalia ilikuwa ni kufanya Libya iwe sehemu ya Italia. Jitihada zao zote zilielekezwa katika lengo hili. Waitalia waliweka vitegauchumi vingi katika kilimo, viwanda na muundo-mbinu.

*Makazi ya Kilimo*

Mpango wa Waitalia wa kilimo katika Libya ulipitia katika hatua bainifu mbili, yaani mpango wa makazi ya kibinafsi, na mpango wa makazi ya kikoloni. Ili kushawishi kuendelezwa kwa makazi ya kikoloni katika Libya hatua za mwanzo za kutamalaki kwa Waitalia, serikali iliwapa mashamba makubwa Waitalia matajiri ili waweze kuyaendeleza kwa madhumuni ya kilimo. Ardhi hii aghalabu ilikuwa ardhi ya serikali au ardhi iliyonyang'anywa kwa wenye kuimiliki. Hadi kufikia mwaka 1929 takribani hekta, 58,087 zilikwishamilikiwa na hao matajiri. Mashamba hayo yalinunuliwa na wakulima wa Italia kwa mkataba wa miaka tisini na ilitegemewa kuwa wakulima wengi wa Kiitalia wangeweza kukaa katika mashamba hayo, wakisaidiwa na serikali. Hata hivyo kulikuwa na kama familia 2,031 tu zilizokaa katika mashamba kwa mpango huu; kiwango ambacho ni kidogo kuliko Waitalia walivyotarajia.

Mara tu baada ya kuuzima upinzani dhidi ya utawala wa Witalia ambao haukufanikiwa hadi ilipofika mwaka 1932 (kwa maelezo zaidi tazama sura ya 5 hapo juu), serikali ya Italia iliamua kutekeleza mpango kamambe wa maendeleo uliokuwa na lengo la kuanzisha tena makazi ya wakulima wa Kiitalia 3,000,000 katika muda wa miaka 25. Mpango huu, ambao ulikuwa chini ya dhamana za taasisi za watu binafsi na zile ambazo nusu zilikuwa na umma, ulijumuisha ufyekaji mashamba, huduma za maji, kujenga majengo ya shambani na mambo mengine yaliyohusiana nayo, na kuwapa masetla vifaa na zana zilizohitajika. Hadi kufikia mwaka 1936 mpango huu ulikwishagharimu takribani, 800 milioni, na ni Waitalia 85,000 tu waliokuwa wamekwishaanzisha makazi tena.Waitalia hawakuanzisha viwanda vikubwa katika Libya.

Hata hivyo waliendeleza baadhi ya viwanda vidogo vidogo ambavyo vilikwishakuwepo kabla ya uvamizi wa Waitalia. Kiwanda kidogo cha kusindikia aina ya samaki waitwao *'tuna'* kilianzishwa Tripoli, na uwezo wa kiwanda cha kusindika mafuta ya zeituni ukaongezeka kufikia tani 2,200 kwa mwaka. Wakati wa kipindi hiki tunachoshughulikia kulikuwa na viwanda karibu 789 vilivyokuwa vikizalisha chumvi, viatu, tumbaku, vifaa vya ujenzi, asifati, baruti, mafuta na sabuni n.k. Vingi kati ya viwanda hivi vilikuwa Tripoli. Tasnia ya kienyeji ya kazi za ufundi iliendelea kuwepo wakati wa kipindi cha Waitalia kwa sababu ya aina yake na udongo wa soko lake. Kujenga Muundo-mbinu

Kabla ya utawala wa Waitalia muundo-mbinu wa Libya ulikuwa wa hali ya nyuma sana. Kwa hiyo serikali ya Italia ikalazimika kulishughulikia sana swala hili. Zilijengwa barabara, reli na bandari; ukaanzishwa mfumo wa kisasa wa mawasiliano; zikaanzishwa kazi za umwagiliaji maji mashamba, na majamba ya jumuia. Matumizi ya vitegauchumi katika maeneo haya yalifikia lira za Kiitalia 870 milioni kwa kipindi cha kati ya mwaka 1913 na 1936. Madhumuni ya kugharamia vikubwa kiasi hiki katika muundo-mbinu ilikuwa ni kuendeleza uchumi kwa manufaa yao.

Hata hivyo kitegauchumi hiki kikubwa kilikuwa na athari yake kwa Walibya. Idadi ya watu wa Libya ilipunguzwa na vita.Watu wengi walikufa katika vita dhidi ya utawala wa Waitalia. Wengine walikufa katika makambi msongamano. Tena basi makundi

makubwa ya watu yalihamia katika nchi jirani. Wale waliopata bahati ya kuwa hai katika makambi msongamano walitumiwa, katika hali ya nusu utumwa, kujenga barabara ya pwani na kuendesha miradi mipya ya maendeleo ya kilimo. Nia ya Italia ilikuwa ni kuwaondosha wenyeji katika maeneo mazuri yenye rutuba na kuwapeleka katika sehemu zisizo na rutuba kisha waihamishie idadi ya ziada ya watu wa Italia katika sehemu zilizokuwa zimekaliwa na wenyeji.

Waitalia pia walipunguza idadi ya mifugo katika Libya. Kwa miaka mingi sana watu wa bara katika Libya walikuwa wakitegemea kondoo na ngamia kwa chakula, kama njia ya kupatia malighafi na kama njia ya usafiri. Idadi kubwa ya mifugo ama ilichinjwa au ilichukuliwa na Waitalia. Idadi ya wanyama iliyobaki pia ikapunguzwa na kufa kwa njaa walipohamishwa toka kwenye sehemu nzuri za malisho kwenda kwenye makambi msongamano ambako hapakuwa na sehemu nzuri za malisho. Kwa hiyo idadi ya kondoo ilipungua toka 810,000 katika mwaka 1926 hadi kufikia 98,000 mnamo mwaka 1933; mbuzi wakapungua toka 70,000 hadi kufikia 25,000; na idadi ya ngamia ikapungua toka 75,000 hadi kufikia 2,000. Ingawa baada ya mwaka 1932 Waitalia walijaribu kuwashawishi watu wafuge wanyama, ilipita miaka mingi kabla ya kuifikia tena hali ya utajiri wa mifugo iliyokuwepo hapo awali.

Jambo la mwisho, na ambalo lilikuwa baya zaidi, ni kwamba Waitalia hawakuwafundisha Walibya mbinu za utawala wala hawakuwapa elimu ya kutosha. Kama asemavyo Tolayan wakati Waitalia (ambao walikuwa asilimia 10 ya jumla yote ya idadi ya watu) kufikia mwaka 1939 - 1940 walikuwa na shule za msingi themanini na moja kwa ajili ya watoto wao, Walibya (ambao idadi yao ilikuwa zaidi ya asilimia 85 ya watu wote) walipewa shule tisini na saba. Pia kulikuwa na shule za sekondari saba kwa ajili ya Waitalia wakati ambapo kulikuwa na shule za aina hiyo tatu tu kwa Walibya. Hata katika kazi za polisi na jeshi hakuna mwananchi wa Libya aliyepandishwa cheo zaidi ya sajini. Kutokuwepo na watumishi waliopata mafunzo kulikuwa kikwazo katika maendeleo ya uchumi wa Libya kwa miaka mingi ya baadaye.

## *Misri*

Katika kipindi hiki tunachoshughulikia uchumi wa Misri ulijipambanua katika mieleko miwili. Kwanza alikuwa mwelekeo wa kilimo, hasa pamba kwa ajili ya kusafirisha nje. Pili, uchumi huo pia alitilia mkazo uendelezaji wa viwanda. Mabadiliko kadhaa ya kimuundo ilibidi yafanywe kulingana na mielekeo hii.

Kipindi hiki kilipata maendeleo mazuri ya muundo-mbinu katika nchi. Hata hivyo mkazo ulikuwa zaidi kwenye kazi zilizohusiana na pamba na usafirishwaji wake nje. Kukafanywa miradi mikubwa ya umwagiliaji maji. Bwawa la Aswani, ambalo lilikuwa kubwa kuliko yote ulimwenguni wakati huo, likamalizika kuchimbwa katika mwaka 1902; na likaongezwa urefu wa kwenda juu katika mwaka 1907 - 1910. Kwa hali hiyo eneo lililolimwa likaongezeka katika fedha (takriban eka 1) 4.76 milioni katika mwaka 1881 hadi kufikia fedha 5.66 milioni katima mwaka 1911. Sehemu kubwa ya ongezeko hili ilitumiwa kwa kilimo cha pamba. Hii ilikuwa kwa sababu mbali na kuwa zao hili lilikuwa

na faida kubwa kuliko mengine lakini pia Waingereza waliwashawishi watu kulilima kwani lilikuwa zao la biashara ambalo liliihitajia Misri kulipa madeni yake na pia lilihitajika sana kama malighafi huko Lancashire.

Haja ya kukiendeleza kilimo cha pamba ilihitajia kupanuliwa kwa njia za usafiri na mawasiliano; nguvu nyingi zilielekezwa kwenye mambo haya mawili (taz. ramani 17.2). Kulijengwa reli zilizounganisha miji muhimu ya Delta na moja kutoka Kairo kwenda Misri ya Juu. Reli ya kwanza ilifunguliwa mwaka 1853. Hadi kufikia mwaka 1877 kulikuwa na 1,519 km za reli ya geji ya kawaida. Reli hizi ziliongezeka zaidi ya mara mbili wakati wa utawala wa Wingereza hadi zikafikia 3,200 km katika mwaka 1909. Aidha kulikuwa na reli ndogo ndogo zenye urefu wa 1,600 km Zana za kufanyia kazi katika bandari ya Alexandria zikawa za kisasa na kuongezwa ukubwa mara kwa mara; bandari ndogo mpya zikajengwa katika Suez na Port Said kwenye mfereji wa Suez ambao ulifunguliwa kwa uabiri katika mwaka 1869. Maendoleo kama haya yaligeuza vikubwa sekta ya kilimo kutoka kwenye kilimo cha kijungu meko na kuwa kilimo cha mazao ya biashara ambayo yalilimwa kwa wingi kwa ajili ya kusafirishwa nje katika masoko ya Kimataifa.

*Awamu ya ubadilishaji bidhaa zinazoingia*

Hapana shaka kwamba utawala wa Waingereza ulifanya mabadiliko mengi ambayo yaliunufaisha uchumi wa Misri. Mambo muhimu yaliyopatikana yalikuwa katika fedha, umwagiliaji maji na utawala. Hata hivyo ni kweli kwamba utawala wa Kiingereza haukukuza shughuli za viwanda hadi ilipofika miaka ya 1920 wakati ambayo yanaashiria kipindi kipya; wakati ambapo mwelekeo ulihimili zaidi kwenye viwanda.

Baada ya Misri kupata uhuru wa kumiliki hazina yake yenyewe kutokana na kutanguka kwa mkataba wa *Anglo-Turkish* wa 1838 mnamo mwezi Februari 1930 Serikali ikaweka kodi ya asilimia 15 hadi 20 kwa bidhaa anuwai ambazo zilielekea kugombea soko na bidhaa za humo nchini. Katika miongo iliyofuata bidhaa zote za kigeni ambazo zilikuwa zinatishia soko la bidhaa za nchini zilitozwa ushuru wa forodha. Viashirio vingi vilionyesha kukua kwa viwanda. Kiashirio cha kwanza kilikuwa ni kuongezeka kwa kuajiriwa kwa watu katika viwanda. Katika mwaka 1937 karibu watu 155,000 walifanyakazi katika mashirika ya viwanda; kwa wastani watu kumi au zaidi walikuwa wakiajiriwa kila mwaka ukilinganisha na watu 30,000 katika mwaka 1916. Kiashirio kingine kilikuwa ni kuongezeka kwa bidhaa zilizozalishwa na viwanda. Kwa mfano zao la sukari liliongezeka toka tani 79,000 katika mwaka 1917 hadi kufikia tani 159,000 katika mwaka 1939: saruji iliongezeka toka tani 24,000 hadi kufikia tani 353,000 katika kipindi hicho hicho, na vitambaa vya pamba vilivyofumwa kwa mkono vikaongezeka toka mita za eneo 7.2 milioni hadi kufikia mita za eneo 159 miliomi mnamo mwaka 1939.

Jambo jingine kubwa la maendeleo lilikuwa ni kuanzishwa kwa mashirika ya biashara ya kitaifa katika miaka ya 1920. Benki ya kwanza ambayo ilikuwa mali ya Wamisri na iliyoendeshwa na Wamisri wenyewe ilianzishwa katika mwaka 1920 na ilijulikana kama *'Bank Misr'*. Ilianzisha maendoleo ya mashirika makubwa ya uzalishaji mali. Benki ikawa kivutio cha mitaji ya binafsi ambayo iliondokana na taratibu za kimapokeo za kutega uchumi; hadi kufikia mwaka 1940 kundi la Misri lilikwishapata

makampuni ishirini na moja yaliyoshirikishwa nalo. Ilikadiriwa kuwa hisa za makampuni ya viwanda ya *Bank Misr* zilikuwa asilimia 45 ya ongezeko katika mitaji iliyolipwa ya makampuni bia yote katika kipindi cha mwaka 1922 - 1938. Ndiyo kusema Bank Misr ilitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya viwanda vya Misri katika kila kipindi kati ya vita. Vitegauchumi katika kipindi hiki vilionyesha ongezeko katika matumizi ya mitaji ya nchini.

Kwa kuhitimisha basi twaweza kusema kipindi tunachokichunguza sasa kilikuwa na majaribio mengi ya kuinua maendeleo ya uchumi. Baada ya kushindwa kwa mpango wa Muhammad Ali wa kutekeleza mpango wa uanzishaji viwanda bila kuwa na muundo-mbinu wa kutosha uchumi wa nchi ulielekezwa kwenye kilimo cha zao moja tu la kusafirisha nje. Mwelekeo huu uliwashawishi watu kupanua mashamba na bidhaa za pamba za kusafirishwa nje. Matokeo yake yalikuwa ni kuwepo kwa uchumi ulioelekea zaidi katika usafirishaji bidhaa nje. Kwa upande mwingine miongo mitatu ya mwanzo katika karne ya ishirini ilipambanuliwa na kutilia mkazo zaidi katika uendelezaji viwanda.

Sudani

Katika kipindi hiki tunachokichunguza nchi ya Sudani ilipitia tawala mbili mbalimbali. Yaani dola ya Kimahdi, kuanzia mwaka 1881 hadi 1898 na utawala wa Misri ya Waingereza kuanzia mwaka 1898. Kila moja ya tawala hizi ilifuata sera yake ya uchumi.

Dola ya Kimahdi ilikuwa na muundo wake wa utawala na pia ilikuwa na mfumo wake wa mahakama. Mojawapo ya mafanikio makubwa sana ya utawala wa Kimahdi ilikuwa ni kuanzishwa kwa mfumo sahihi na wenye kutekelezeka kwa urahisi wa utozaji kodi; mfumo uliokuwa umekitwa kwenye maadili ya Kiislamu. Zakat ilichukua sehemu kubwa ya mapato. Ilitozwa kwa kiwango cha asilimia 2.5 kwenye fedha na asilima 10 kwenye mifugo na nafaka. Kutokana na usahili wa mfumo huu wa kodi na uwezo wake wa kwenda sawa na mazingira ya kijamii uliweza kuendelea hata baada ya kuanguka kwa utawala wa Kimahdi. Utawala wa Kimahdi uliwashawishi watu kulima na kufanya biashara kwa sababu shughuli zote hizi zilikuwa zimelengwa katika kulikimu jeshi na kulipatia silaha na zana nyingine za kivita.

Mchango mkubwa wa utawala wa Mwingereza katika Sudani ulikuwa ni kuendeleza muundo-mbinu na kuanzisha mfumo wa kisasa wa kilimo. Reli, bandari na mabwawa vilijengwa (taz. Ramani 17.2). Reli ya kwanza ilijengwa katika kipindi cha 1896-1898 na ilikuwa na madhumuni ya kutumiwa kama kampeni ya kivita. Baadaye iliendelezwa hadi kufikia Atbara na ilitumiwa kama njia ya usafirishaji baina ya sehemu ya kaskazini ya Sudani na Mediterani kupitia Misri. Port Sudan ilipojengwa katika mwaka 1906, reli mpya ilijengwa ili kuiunganisha bandari hiyo na Atbara. Kisha mnamo mwaka 1910 reli kuu iliendelezwa hadi kufikia Sennar. Reli nyingine katika mwaka 1924 kati ya Djazira na bahari ya Shara Huduma za meli pia zilitumiwa kuunganisha kusini na kaskazini ya nchi. Njia hizi bora na za kisasa za usafirishaji zilisaidia kusafirisha bidhaa za

kilimo na zilipunguza gharama za usafirishaji kwa kiwango kikubwa. Aidha hatua zilichukuliwa kuhakikisha kuwa ardhi na maji vinatumiwa vizuri. Mashine za maji zilijengwa na mifereji kadhaa ilichimbwa kwa ajili ya umwagiliaji maji.

Tokea mwanzo, Waingereza walimaizi utajiri mkubwa wa kilimo uliokuwako Sudani. Walianzisha majaribio ya kilimo cha pamba kwa madhumuni ya kutaka kuongezea uzalishaji wa zao hili uliokuwa ukifanyika Misri. Jaribio la kwanza katika Zaydab, mwaka 1905, ililipoonesha mafanikio mazuri iliendelezwa hadi kwenye tambarare za Djazira kati ya Blue Nile na White Nile ambazo zilikuwa na ardhi yenye rutuba nyingi zaidi katika Sudani (taz. Ramani 17.2). Mpango kamambe ulitayarishwa kwa ajili ya tambarare za Djazira ambao ulikusudia umwagiliaji maji mashamba ya eka nusu milioni ambamo pamba, mtama na nyasi za kulishia mifugo vingelimwa. Hata hivyo mpango huu haukuweza kutekelezwa kwa mafanikio hadi kwenye miaka ya 1920.

Mafanikio ya mpango wa Djazira yalichochea maendeleo ya shughuli nyingine za aina yake kama vile usafirishaji, umwagiliaji maji na vinu vya kuchambulia pamba.

Ili kuweza kugharamia mipango yote hii mfumo wa kodi uliokuwepo ulisaidiwa na mkataba baina ya Uingereza na Misri ambao kwao Sudani ilipata msaada wa kifedha na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na bajeti. Mchango wa Misri kwenye bajeti ya Sudani ulikuwa pauni za Kimisri 2.8 milioni katika kipindi kuanzia 1899 hadi kufikia 1916, na mikopo iliyotolewa na Misri kwa Sudani ilifikia jumla ya kiasi karibu pauni za Kimisri 5.4 milioni katika kipindi cha kuanzia 1900 hadi kufikia 1910.

Ili kuchochea matumizi ya ardhi robo moja ya ardhi iliyolimika ililipiwa kodi baada ya miaka miwili. Halafu ardhi yote ililipiwa kodi baada ya miaka minane mpaka kumi. Kodi nyingine zilikuwa kodi ya mifugo, ambayo ilitozwa kwa mbari kwa ujumla, kodi ya kichwa ambayo ilikuwa kati ya piasta 25 na 80 kwa kila kichwa; na katika mwaka 1912 kukaanzishwa kodi ya kumiliki mali.

*Athari ya Shughuli za uchumi wa ukoloni wa Kiingereza katika Sudan*

Tukizilinganisha shughuli za uchumi wa ukoloni wa Waingereza na zile za ukoloni wa Wafaransa katika Maghreb na ukoloni wa Waitalia katika Tripoli tunaona kwamba zile za Waingereza zastahili sifa kwa kiasi fulani. Ardhi haikuchukuliwa na wageni wala haikuwa mali ya watu wachache tu kama ilivyokuwa katika makoloni mengine. Mpango wa Djazira pia ulikuwa wa manufaa sana kwa Waingereza na Wasudani waliokuwa wakihusika nao moja kwa moja. Kuanzishwa kwa mfumo wa kisasa wa usafirishaji pamoja na ujenzi wa bandari na umwagiliaji maji mashamba pia vilisaidia kwa mfumo wa kilimo cha kisasa nchini Sudani. Hata hivyo pamoja na uzuri wote huo kulikuwepo na ila zake pia. Kwanza muundo-mbinu uliokuwapo haukutosheleza kabisa na ni wazi kuwa uliukiliwa kuchochea maslahi ya Waingereza zaidi kuliko yale ya Wasudani. Ni muhimu kabisa kutambua kwamba hakuna hata maili moja ya barabara ya matokeo iliyojengwa katika eneo lote la Sudani katika kipindi hiki na kwamba madhumuni ya mwanzo ya kujenga reli yalikuwa ni kurahisisha kampeni za kivita za Kiingereza na baadaye kusaidia katika kuendeleza miradi yao ya pamba na gundi katika Djzira katika sehemu za magharibi. Kama ilivyokuwa katika makoloni mengi maendeleo ya viwanda yalipuuzwa kabisa. Hata hivyo mashtaka au

lawama kubwa zaidi ya ukoloni wa Waingereza katika Sudani ni kule kutoijali kabisa Sudani ya kusini katika masuala ya uchumi na kijamii. Hapana shaka hii ni sababu mojawapo muhimu iliyosababisha tatizo la Sudani ya Kusini lililopo hii leo; tatizo ambalo ufumbuzi wake bado haujapatikana.

# 18

## Matokeo ya Kijamii ya Utawala wa Kikoloni: Vipengeee vya Hesabu ya Watu

Uingizaji kwa nguvu wa utawala wa kikoloni hapa Afrika haukuathiri tu miundo ya siasa na uchumi wa bara hili, bali pia ulikuwa na matokeo ya muda mrefu ya kijamii ambayo ndiyo kiini cha sura hii na sura nyingine tatu zinazofuata. Katika sura hii, tunakusudia kuongelea juu ya mada ambayo mara nyingi imeonekana kusahauliwa na wanahistoria wa ukoloni katika Afrika, nayo ni athari ya ukoloni kwenye idadi ya watu katika Afrika. Kutokana na ushahidi uliopo, inaonekana wazi kwamba kuna mabadiliko makubwa mawili yaliyotokea katika hali ya idadi ya watu katika Afrika. Mabadiliko hayo ni kiwango cha uongezekaji wa idadi ya watu na utawanyikaji wa watu.

### *Ongezeko la Idadi ya Watu*

Katika mtazamo wa ongezeko la idadi ya watu, inaonekana wazi kwamba ingawa kipindi cha kuanzia mwaka 1880 hadi kufikia mwisho wa Vita vya Kwanza vya Dunia kilikuwa na upungufu mkubwa wa kiwango cha ongezeko la idadi ya watu na hivyo kusababisha kushuka kwa idadi ya watu katika sehemu nyingi za Afrika, kipindi kilichofuatia kilishuhudia ongezeko la idadi ya watu. Ni kweli kwamba mahesabu ya sasa yanayoonyesha kwamba kwa ujumla kuliwepo ongezeko katika idadi ya watu kutoka milioni 120 katika mwaka 1880 hadi kufikia watu milioni 129 katika mwaka 1900, na milioni 142 mwaka 1920. Lakini ukiacha baadhi ya sehemu za kaskazini na Kusini mwa Afrika na pengine Ghana, ambazo zilipata ongezeko la idadi ya watu, sehemu nyingi za Afrika na hasa sehemu yote ya Afrika ya kati kulikuwa na kushuka kwa ongezeko la watu. Ama kwa hakika pamoja na ongezeko la idadi kati ya mwaka 1880 na 1920, bado kiasi cha ongezeko kilishuka hadi kufikia robo ya asilimia moja mnamo mwaka 1900 na kikapanda kwa wastani wa asilimia nusu tu mnamo mwaka 1920.

Sababu za kushuka huku kwa kiasi cha ongezeko kati ya mwaka 1880 na 1900 na kupanda kwake kwa pole pole kati ya mwaka 1900 zinaelezeka kwa urahisi. Sababu ya kwanza ilikuwa ni kupotea kwa maisha ya watu ambako hakukutokana na kuongezeka kwa utawala wa mwanzo wa kikoloni kama ambavyo wataalamu wengine hufikiria, bali kulikotokana na jitihada za kuyazima maasi ya mara kwa mara yaliyoandamana na adhabu kali; haya yote kwa pamoja yalisababisha kuleta hasara ya watu kukosa chakula kwa sababu misimu ya kilimo ilivurugwa. Mifano ya matukio haya ni pamoja na maelfu ya watu waliouawa huko Senegal mwaka 1886 walipokataa kujenga reli: vita vya Wandebele vya Rhodesia (sasa Zimbabwe) mwaka 1893, maasi ya Wabatetela katika *Congo Free State* kuanzia mwaka 1895 hadi 1907; na mfululizo wa matukio mengine katika koloni la

Wajerumani la huko Afrika ya Kusini Magharibi, (ambalo linaitwa Namibia), kati ya mwaka 1901 na 1906. Maafa makubwa yalitokea Tanganyika (sasa Tanzania), ambako Wajerumani walitumia sera ya "ardhi iliyounguzwa" katika maasi ya Maji Maji (1905-1906), sera ambayo pengine ilisababisha vifo vya mamia ya maelfu ya watu zaidi kutokana na ukosefu wa chakula. Mapambano baina ya Waingereza na Wajerumani katika Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, bila shaka navyo viliongeza kiwango cha vifo vya watu katika nchi hiyo.

Sababu kuu ya pili inahusu suala la "nguvukazi" pamoja na mipango ya makampuni iliyoruhusiwa katikati ya Afrika. Mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, watawala wa kikoloni walikuwa na imani kwamba makoloni yalipaswa kutoa faida. Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa malengo haya kulitegemea sana kuwatumia Waafrika katika kufanya kazi.Kupatikana kwa faida kulitegemea sana kusafirisha bidhaa, na mara nyingi njia iliyotumika katika sehemu nyingi za Afrika ya tropiki ni ile ya bidhaa kubebwa na watu kwa sababu mara nyingi walifanya iwe vigumu kuwatumia wanyama wavumiliao ukame; pia ukosefu wa barabara na reli vilifanya isiwezekane kutumia magari ya mashine na ya mafuta katika kusomba bidhaa. Katika Afrika ya Kati, zao ambalo kwanza lilileta faida kubwa sana lilikuwa ni katika "pembe za ndovu". Zao hili lilihitaji watu wengi wenye nguvu za kubeba. Maendeleo yaliyoletwa na baiskeli za mwanzo mwanzo mwishoni wa miaka ya 1880 Uvumbuzi wa magari ya matairi katika miaka ya 1890, yalisababisha mahitaji ya zao la mpira kuongezeka sana, mahitaji arabayo hayakuweza kutoshelezwa na mashamba ya mpira kwa muda wa kizazi kimoja (mashamba ya mpira ya huko Malay, yalianza kutoa mazao yake ya kwanza katika mwaka 1910). Wakati huo huo sehemu za tropiki za Afrika na Ametika ya Kusini, zilijitosheleza kwa mahitaji ya mpira kutokana na mipira pori, na hii ilihitaji watu wengi wa kuikusanya na kuifanyia usindikaji wa mwanzo.

Ugumu wa kazi hii ulitokana na msingi kwamba wakulima wadogo wadogo walikuwa na mahitaji yao machache, pia kazi ya kuajiriwa ilionekana kwao kama ni kazi ya kitumwa; na kwamba kazi kama hizi ziliwahusu wanawake. Wazungu walipogundua kuwa faida kubwa ilikuwa ikipotea bure waliamua kutumia njia za kishenzi na za kikatili. Kwa sababu hiyo, serikali ilianzisha kuwafanyisha watu kazi kwa kuwatumia machifu ili wawatafute watu wa kazi. Kodi ya kichwa na kodi ya nyumba zilianzishwa kwa lazima katika baadhi ya sehemu za utawala wao pamoja na kuwafanya watu wafanye kazi ili walipe kodi.

Aidha baadhi ya Waafrika walichukuliwa na kupewa mafunzo ya kijeshi na hatimaye kufanywa kuwa wanajeshi na wengine kuwa askari polisi wa kulinda usalama. Kila sehemu kulikuwa na usafirishaji wa wafanyakazi, zaidi kwa kuwapeleka ambako walihitajika. Uhamishaji huu wa wafanyakazi katika theluthi ya karne baada ya 1880 uliandamana na kiwango kikubwa cha vifo. Vibarua mara nyingi walihamishiwa katika sehemu ngeni ambazo zilikuwa na magonjwa ambayo yalikuwa mageni kwao, pamoja na yale yaliyokuwa yameletwa Afrika na wengine, kama vile homa ya matumbo. Aidha, ingawa inaeleweka kwamba Waafrika wanayo kinga ya malaria nyumbani kwao 'lakini huko ugenini sio tu kwamba walipatwa na homa na malaria kali, bali pia walipatwa na homa za matumbo.

Ni wazi kwamba hali hii ya maisha ya kazi za makambini ilisababisha kuenea kwa minyoo mwilini mwao na vijidudu vya magonjwa yapatikanayo zaidi katika Afrika ya Tropiki. Wakati mwingine walifanya kazi nyingi kuliko uwezo wao na wakaugua. Vibarua wengi walidhoofishwa na njaa. Kwa upande fulani hii ilitokana na kupewa chakula wasichokizoea kabisa na kwa upande mwingine wabeba mizigo na wafanyakazi wengine hawakupewa chakula cha kutosha ama kwa kuwa Wazungu hawakujali au waliamini kuwa Waafrika walizoea kuishi maisha ya kuokoteza chakula.

Kiwango cha vifo katika karne ya 19 hakikufahamika sana, lakini katika mwaka wa 1915, kiongozi wa serikali ya kikoloni ya Waingereza huko Sao Tome alidai kuwa watu 100 kati ya 1000 kati ya wafanyakazi vibarua walioandikishwa walikuwa wakifa. Kiasi cha idadi ya vifo cha namna hiyo pia kimekisiwa kati ya vibarua waliojenga reli kutoka Brazzaville hadi baharini mnamo mwaka 1922. Kiasi hiki kinapishana na kile cha watu 150 kwa kila 1000 waliokuwa wakifa katika ujenzi wa reli huko Cameroon kabla ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Wasomi waliitolea methali hali hii ngeni kwa kusema "Kazi ya Mtu Mweupe ni hula Watu".

Kiasi cha idadi ya vifo bado kiliendelea kuwa kikubwa sana katika machimbo ya Afrika Kusini mwanzoni mwa karne hii. Mwaka 1907, tume iliyokuwa inaripoti juu ya hali ya kiwango cha vifo katika machimbo wakati huo kilikuwa watu 71 katika kila 1000 ya Waafrika watokao Tropiki, ikilinganshwa na watu 28 ya Waafrika watokao kusini (sehemu za joto la kadiri) na 19 kwa watu weupe. Kiasi hiki cha vifo kilionekana kushuka kutoka 130,35 hadi 20 kwa kufuata mfululizo huo huo katika miaka miwili ya mwanzoni. Vilevile kulikuwa na na hali mbaya za kufanyia kazi kama inavyodhihirishwa mnamo mwaka 1902, na kupotea kwa 1/5 ya wafanyakazi katika Cameroon, katika mwaka mmoja katika mashamba yaliyokuwepo. Hali mbaya ilizuka katika *Congo Free State* (ambayo baadaye ilikuwa *Belgian Congo* na kisha Zaire), *French Congo* (baadaye ilijulikaa kama *French Equatorial Africa*) na Cameroon iliyotawaliwa na Wajerumani, karibu katika sehemu yote ya ukanda isiyo na rutuba.

Kwa hakika masuala ya magonjwa na njaa yalifuatia kuvunjika kwa taratibu za kazi katika vijiji pamoja na kuhama kama kwa wanavijiji. Hakuna mtu aliyetunza kumbukumbu za kutosha kuhusu idadi ya watu, lakini watu wengi wanakubaliana kwamba kulikuwa na kupungua kwa idadi ya watu. Ushahidi wa kushuka kwa idadi ya watu huenda ulitokana na akadiriaji uliopita kiasi ambao ulifanywa kabla ya kugawanywa kwa idadi ya watu na kule kupotea kwa idadi ya watu katika sehemu za kandokando ya mito ambako watu walikuwa wamekwishahama. Hata hivyo ni vigumu kuepuka kutoa hitimisho kwamba huenda idadi ya watu ilianza kushuka katika eneo la Katikati ya Afrika mnamo miaka ya 1890 na 1910 au hata baadaye.

Baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, hesabu ya watu wakati wa ukoloni, ilikuwa kinyume kabisa na ile ya zamani kwa sababu kulikuwa na ongezeko kubwa sana la idadi ya watu. Kutokana na mahesabu yaliyopo, idadi ya watu iliongezeka kutoka milioni 142 katika mwaka 1920 hadi kufikia milioni 165 mwaka 1935. Hili ongezeko kubwa kwa kiasi fulani lilitokana na msingi wa uchumi ambao unadhihirishwa na maendeleo mengi yaliyojadiliwa katika sura nyingi zilizotangulia. Baadhi ya maendeleo hayo yaliyokuwa

maarufu zaidi ni pamoja na usafirishaji nje bidhaa za mafuta ya chikichi kutoka Delta ya Niger; ugunduzi wa almasi na pia dhahabu katika Afrika ya Kusini mnamo miaka ya 1870 hadi 1900; ustawishaji wa tasnia ya asili ya ukuzaji wa kakao huko Ghana mnamo miaka ya 1890, na ugunduzi wa mashapo mengi ya shaba katikati ya Zaire na Zimbabwe mnamo miaka ya mwanzoni ya karne hii.

Hata hivyo, sababu zilizosaidia kuongezeka zaidi kwa idadi ya watu huenda zilitokana na kuenezwa kwa barabara na reli. Kufikia mwishoni mwa miaka ya 1920, karibu njia zote za reli zilikuwa zimekwishajengwa tayari na utengenezaji wa barabara ulikuwa ukiendelea vizuri; mwishoni mwa miaka ya 1930 malori machache ya kubebea mizigo yaliweza kufika karibu kila pembe ya bara hili. Kwa njia hii, serikali au wafanyabiashara waliweza kusafirisha chakula hadi katika sehemu zenye njaa. Huu uwezekano wa kuwa na njia za usafirishaji pamoja na kuwa na fedha zinazokubalika sehemu kubwa, vilisaidia uzalishaji wa chakula cha ziada kwa ajili ya soko. Kuanzia kama mwaka 1920, vifo vilivyotokana na njaa, ukilinganisha na upungufu wa mvua katika maeneo hayo, vilipungua kwa mlingano sawa; wingi wa vifo, uliofanya wastani wa vifo kuwa juu, sasa ulianza kupungua.

Hadi kufikia wakati huo hata nchi kama ya Uganda ilikuwa inakumbwa na vifo vya njaa. Zaidi ya watu 100,000 walikufa kwa muda wa mwaka mmoja, kama ilivyokuwa katika miaka ya 1918-1919. Pengine wamisionari walikuwa na athari ndogo lakini muhimu juu ya idadi ya vifo mbali na kuanzisha hospitali. Mtawala mmoja alidai kwamba "watoto wao walijifunza angalau kiasi fulani cha ufahamu wa kumudu tabia mpya ya maisha iliyoanzishwa na mtawala wa kikoloni".

Mwisho, nini athari za dawa za Kimagharibi katika Afrika? Ni dhahiri kwamba Waafrika walikabiliwa na magonjwa mengi. Magonjwa hayo ni kama: malaria, kaswende, buba, ukoma, homa za vipindi, kuhara damu na minyoo; pia tunaweza kuongeza magonjwa ya kuambukiza watu wengi kwa haraka kama vile homa ya majano, ndui, na ugonjwa wa malale, kifua kikuu na kipindupindu, lakini Wazungu hawakuwa na dawa za kufaa kwa magonjwa haya ya Kiafrika. Mwanzoni mwa karne ya 19, wastani wa maisha ya kuishi toka kuzaliwa katika Uingereza alikuwa chini ya miaka 40; ambapo kufikia mwishoni mwa karne hiyo, wastani huu ulipanda hadi kufikia miaka 47 kwa nchi za Uingereza, Ufaransa na Ujerumani; pia kiwango cha idadi ya vifo kilifikia karibu ya watu 20 kwa kila 1000, na kwa watoto wadogo kiwango cha vifo kilikaribia 200. Aidha, mapinduzi ya madawa yalichelewa kutilia mkazo magonjwa ya kitropiki. Ingawa uchanjaji ndui ulifahamika tangu karne ya kumi na nane (hii ni kwa sababu ugonjwa huu haakuwa hasa wa sehemu za tropiki), njia za uambukizaji wa matende, malaria na homa ya manjano zilianzishwa miaka ya 1877, 1897 na 1900 tu, kwa kufuata mfululizo huo huo. Mbali na dawa ya kwinini, na umiaji kidogo wa msombo wa aseni kutibu kaswende na buba, maendeleo ya dawa na chanjo ili kupigana na magonjwa ya tropiki yalianza mnamo miaka ya 1920 hivi tu. Hata hivyo, shule za uganga kwa ajili ya magonjwa ya nchi za tropiki zilianzishwa Ulaya mapema mwaka wa 1897 katika miji ya Liverpool na London, mwaka 1900 katika mji wa Hamburg, mwaka 1901 katika mji wa Brussels, ukifuatiwa baadaye ni mji wa Paris, Bordeaux na Marseilles, na katika Afrika mwaka 1912 katika mji wa Cape Town na

mwaka 1918 katika mji kwa Dakar.

Katika Afrika ya Tropiki, kwa muda mrefu huduma za madawa ya serikali zilitolewa zaidi kwa wanajeshi, ingawa hospitali ndogo ndogo za raia zilianza kuonekana mnamo miaka ya 1890. Kuanzia mwaka 1840, daktari wa kwanza mmisionari alipofika Siera Leone, na huko Afrika Magharibi kulikuwepo na wamisionari waganga hapa na pale wakiwemo Waafrika wachache (wengi wao wakiwa ni Wasierra Leoni). Huduma hizi zilielekezwa zaidi kwa wanajeshi, watawala na wamisionari, ingawa kwa kiasi fulani ziliwafikia pia wanajeshi wa Kiafrika, wafanyakazi wa serikali na wa misionari. Ufanisi halisi ulipatikana mwanzoni mwa karne hii tu, kama inavyodhihirishwa na kiwango cha kukadiria cha vifo vya wazungu wenye madaraka katika serikali ya Ghana jinsi kilivyoshuka kutoka watu 76 kwa elfu moja katika miongo miwili ya mwisho ya karne ya kumi na tisa hadi kufikia 31, 22 kwa mfululizo huo huo na kiasi cha watu 13 kwa miaka ya 1902, 1903 na 1904. Hata ukichukua hoja ya mpangilio wa umri, kiwango hiki kinalingana na viwango vya Uingereza vya mwaka 1912. Sababu za ufanisi huu zilikuwa ni uzingatiaji wa masharti ya afya katika kujikinga na malaria, homa za manjano, uvumbuzi wa njia bora za kutibu magonjwa ya kitropiki, na kuwa na nyumba za kuishi zilizojengwa mbalimbali. Hatua za kufuata masharti ya afya bila shaka ziliwasaidia sana Waafrika wachache walioishi katika vituo vya utawala hususani Lagos, baada ya hatua hizi kuchukuliwa katika miaka ya mwanzoni mwa karne hii na Gavana William McGregor na Dr. Ronald Ross (ambaye aligundua jinsi ambavyo malaria huenezwa).

Njia zilizotumiwa na Wazungu kuinua afya za Waafrika hazikusaidia sana kwa sababu kwa upande mmoja, baada ya Vita Vikuu vya Dunia, nchi za Ulaya zilitoa vishawishi vingi kwa madaktari kuliko ilivyokuwa katika Afrika; na sababu nyingine ni kwamba watawala wa kikoloni walipunguza matumizi ya afya kwa sababu ya mpomoko wa uchumi uliotokea katika miaka ya 1930. Mwaka wa 1924 nchi ya Nigeria ilikuwa na mpango wa matibabu wa kinadharia kwamba daktari mmoja angepaswa kuhudumia watu 200,000 lakini ukweli ni kwamba ni robo tu ya nafasi za madaktari nzido zilizojazwa. Kusema kweli, mnamo mwaka 1939 kulikuwa na uwiano wa chini wa madaktari akilinganisha na idadi ya watu nchini kuliko hata ilivyokuwa mwaka 1914. Tarakimu hizi zilitiwa chumvi kwa sababu Mwafrika hakupata huduma za afya kama ilivyokusudiwa. Mnamo miaka ya 1930, kulikuwa na hospitali 12 kwa ajili ya Wazungu wapatao 4,000, ambapo hospitali 52 tu ndizo zilizohudumia Waafrika milioni 40.

Kukosekana kwa madaktari wengi huduma mbalimbali za matibabu zilitegemea uwezekano wa kuanzishwa kwa zahanati ambazo huduma zake zingetolewa na waganga wasaidizi au na vikundi mbalimbali vya kujitolea. Huko Nigeria, zahanati ilifunguliwa Ibadan mwaka 1904 na nyingine ziliendelea kujengwa miaka iliyofuata katika miji ya Yoruba. Mnamo mwaka 1910, serikali ya Sierra Leone ilikuwa ikitoa zawadi kwa machifu wa vijiji viwili katika kila wilaya, vilivyopiga hatua ya maendeleo katika mambo ya afya na ya usafi kwa ujumla. Mnamo mwaka 1934, Uganda ilikuwa na hospitali katika vituo vyote vikubwa na ilikuwa na vituo vidogo vya zahanati vipatavyo 88 huko vijijini, ambavyo kwa pamoja vilihudumia watu wapatao 1,378,545 kwa mwaka. Penginepo si vizuri kutia chumvi kuhusu umuhimu wa mabadiliko haya: katika zahanati nyingi, dawa zilikuwa

chache na wahudumu hawakujua sawasawa wafanye nini kama ilivyokuwa katika sehemu nyingi za Afrika hadi wakati wa kujua kuandika. Andre Gide, akitembelea vituo vya afya huko Beteu karibu na mto wa Ombangui mwishoni mwa miaka ya 1920, alisema kwa uchungu kwamba madawa yaliyokuwa yakitolewa kutibu magonjwa ya watu wa eneo la katikati ya Afrika yalikuwa ni: dawa ya joto asidi boraki *(boracic acid)* na chumvi ya Glauberi tu.

Kupungua kwa kiwango cha vifo kwa Waafrika (hasa katika kipindi kilichojadiliwa katika sura hii) pengine kulifanikiwa kutokana na kuwa na mbinu zilizofaa za kujikinga na hatari za vifo vilivyotokana na njaa na magonjwa ya hatari ya kuambukiza. Juhudi za mashambulizi zilizoanza mwanzoni mwa karne dhidi ya magonjwa ya hatari ya kuambukiza, polepole zilionyesha mafanikio ya kiasi. Waigereza walishambulia ugonjwa wa malale kwa kuzuia mbung'o wasikaribie watu, kuzuia wanyama ama wasitumie maji ya visima hasa katika sehemu zenye watu wengi, au kufyeka vichaka na zaidi ya yote kuhamisha watu kama walivyofanya pwani ya Ziwa Victoria. Wafaransa walitibu idadi kubwa ya watu na kazi hii ilifanywa na Dkt. E. Janet kwa kutumia msombo wa kiaseni atokili. Sehemu mojawapo ya Cameroon yenye watu 124 elfu iliyotibiwa kwa njia hii ilirekodiwa mnamo mwaka 1924 na ilionyesha kuwa sehemu hii ilikuwa na kiwango kikubwa cha vifo cha watu 81 kwa kila elfu moja na kati ya hao 36 walikuwa wakiuawa na ugonjwa wa malale. Ilipofika mwaka 1930, ugonjwa huu wa hatari wa kuambukiza ulikuwa umekwisha. Huko Uganda, angonjwa huu wa malale ulitambuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1901, na inadhaniwa kuwa hadi kufikia mwaka 1906 ugonjwa huu ulikuwa umeua watu zaidi ya 200,000 wakati watu walipoanza kuhama kwa wingi, lakini ilipofikia mwaka 1918, kulikuwa na uhakika kwamba ugonjwa ulikuwa umekwisha na kwamba watu waliweza kurudi kwenye sehemu zao za zamani.

Uzukaji wa tauni ya mitoki ulikuwa mwingi sana mwanzoni mwa karne ya sasa, katika muongo wa kwanza nusu ya watu elfu sita waliopatwa na ugonjwa huu walikufa huko Misri; huko Uganda, karibu vifo vya watu 60,000 vilikuwa vimejulikana hadi kufikia mwaka 1932; na ugonjwa huu ulizuka pia huko Accra mwaka 1908, Lagos mwaka 1924 na zaidi katika sehemu za Yoruba katika Nigeria katika mwaka 1925. Hatua zilizochukuliwa na koloni la Waingereza la Afrika Magharibi zilionyesha kwamba ugonjwa huu ungeweza kuzuiliwa; wakati ugonjwa huu ulipozuka Accra, mji wote uliwekwa chini ya karantini na watu wapatao 35,000 walipata matibabu ya kuchanjwa dawa ya Haffkini.

Kuzuka kwa ugonjwa wa homa ya manjano kulikoanzia Senegal hadi Sudan kumetokea kwa vipindi visivyotabirika. Hadi kufikia mwaka 1927 dawa ya chanjo ilikuwa imeshagunduliwa na kufanyiwa uchunguzi katika maabara ya "Rockfeller" ya Taba, nje kidogo ya mji wa Lagos, lakini kwa vile haikutumiwa katika kiwango kikubwa hadi Vita Kuu ya Pili ya Dunia, mafanikio yoyote dhidi ya ugonjwa huu hadi mwaka 1935 yalitokana na watu wa mijini kutumia njia za kutokomeza mbu pamoja na kutumia vyandarua. Hakuna uhakika kama ugonjwa wa ukoma ulikuwa umepungua katika kipindi hiki. Mafuta ya alopeli yalikuwa yakitumika Nigeria kutibu tangu mwanzoni mwa miaka ya 1920, hata hivyo katika mwaka wa 1938, ilikadiriwa kuwa asilimia moja ya watu bado walikuwa na ugonjwa huu. Uchanjaji ndui ulikuwa bado ni wa kiwango cha chini na hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1930, ugonjwa ulipungua kwa kiasi kikubwa hasa katika sehemu

za Ghana na kusini ya Nigeria tu. Karibu sehemu nyingi za bara hili, yalikuwepo maendeleo kidogo dhidi ya adui mkubwa kuliko wote, malaria, ambao iwapo haukuua, ulidhoofisha sana na ulikuwa sababu ya vifo vingi vilivyoelezwa kuwa vilitokana na sababu nyingine.

## *Mitawanyiko ya Idadi za Watu Hadi Mwaka 1935*

Hata hivyo, sio tu kwamba kulikuwepo na ongezeko la jumla la idadi ya Waafrika kati ya miaka 1880 na 1935, bali pia kulikuwepo na ugawanyikaji tena wa watu na ukuzaji wa miji. Hii miaka 55 ilishuhudia usambazaji wa watu ambao ungesababisha tabia na muundo wa Afrika mpya. Ongezeko la watu milioni 45, lilikuwa na maana kwamba kila mtu asingeweza kupata nafasi sawa ya mahali pa kuishi kama ilivyokuwa wakati wa wahenga wao. Kwa hiyo usambazaji wa watu katika sehemu zisizokaliwa uliharakishwa. Kitu cha muhimu ni kwamba mnamo miaka ya 1890, uhamaji wa wafanyakazi kutafuta kazi za kulipwa ulikuwa umeanza huko Afrika Magharibi, mapema kidogo huko Afrika Kusini na hapo baadaye katika Afrika Mashariki. Mwanzoni, wafanyakazi walilazimika kutafuta kazi ili waweze kulipa kodi. lakini baadaye hamu ya kutaka kununua bidhaa na kutaka kwenda sehemu za mbali vilianza kuwa na mvuto mkubwa kwao pia. Mwanzo, uhamiaji ulikuwa ni wa msimu, lakini baadaye uhamiaji wa muda mrefu ulianza kuonekana kuwa ni uamuzi wa maana. Mwishoni mwa miaka ya 1920, karibu wahamiaji 200,000 kutoka Savannah waliingia Gold Coast (Ghana) na Nigeria. Serikali ziliweka vikwazo vichache kwa wale waliohama isipokuwa katika Afrika Kusini, Rhodesia (Zambia na Zimbabwe) ambako kibali cha uhamiaji cha muda kilitolewa kwa watu wazima wanaume; kwa kuhofia matatizo ya makazi ambayo yangeweza kutokea kutoka kwa vyama vya wafanyakazi weupe.

Hatimaye, uwiano mkubwa wa makundi ya uhamiaji ualianza kubadilisha mwelekeo. Badala ya kwenda kwenye mashamba na machimbo ya madini, sasa makundi hayo yalielekea mijini. Kutokana na hali hii, hatimaye kila mikoa mingi ikapata vituo vikubwa vilivyoweza kuegama huduma za kiutawala na viwanda vidogovidogo. Hapana shaka kwamba Afrika ilikuwa na miji ya kale katika bonde la chini la mto Nili, na miji ya karibuni zaidi katika Maghreb, Savannah ya Afrika Magharibi na sehemu ya Yoruba (huko Nigeria) na katikati ya Gold Coast (Ghana). Hata hivyo, kufikia mwaka kwa 1880, ni mtu mmoja tu kati ya watu mia tatu aliyeishi katika vituo vyenye idadi ya watu zaidi ya 100,000 ukilinganisha labda na mtu mmoja kati ya 50 huko Asia; na huko Ulaya, mtu mmoja kwa kati ya 15.

Mabadiliko halisi yametokea katika kipindi chetu, hususani katika Afrika Kusini mwa Sahara. Katika Afrika ya tropiki, tukiondoa mji wa Nigeria na kuorodhesha miji kumi na sita ambayo ilikuja kuwa mashuhuri katika karne ya ishirini, tunaweza kukisia idadi ya watu ya pamoja katika mwaka wa 1880 kuwa 800,000; kufikia mwaka 1930, idadi hii ilikuwa imeongezeka mara tano hadi kufikia zaidi ya nusu milioni (hivyo kuanzisha msingi wa kuongezeka zaidi ya mara kumi katika miaka arobaini ijayo). Kufikia mwaka 1931, mji wa Dakar ulikwishakuwa na idadi ya watu 54,000; mji wa Feetown" ulifikia watu 44,000,

lakini hesabu hii ilikuwa ni mara mbili ya idadi ya watu ya nusu karne iliyopita; Accra 60,000; na Addis Ababa 65,000; Nairobi 48,000, na Dar es Salaam 25,000. Katika Nigeria, kipimo kilikuwa tofauti: mji wa Ibadan ulikuwa na watu wapatao 400,000 lakini huenda ulikuwa na watu 150,000 wakati wa mwanzo wa kipindi hicho; labda mji wa Lagos ulikuwa umeongezeka mara mbili hadi kufikia watu 126,000.

Katika Sahel, idadi ya watu katika miji ya Kale ilikuwa ikishuka kwa sababu kwa upande fulani, miji hiyo haikuwa vituo muhimu vya utawala wa Wafaransa. Kufikia mwaka wa 1931, miji ya Timbuktu, Gao na Mopti kwa pamoja ilikuwa na idadi ya watu wapatao takriban 15,000 tu. Huko Afrika ya Kaskazini, miji mingi ya kale iliendelea kuwa na umaarufu wake. Katika kipindi chetu miji ya Cairo, Alexandria na Algeria, idadi ya watu iliongezeka mara tatu hadi kufikia milioni moja, mia sita na robo milioni kwa kufuata mfululizo huo huo. Kufikia mwaka 1931, miji mingine ya zamani kumi na mine ya Maghreb ilikaribia jumla ya watu milioni moja na nusu, idadi ambayo iliwakilisha walau kuongezeka mara mbili katika nusu karne, na huko Sudan mji wa Khartoum Cudurman ulikuwa na watu 159,000.

Kufikia mwaka 1931, miji mikubwa kumi na minne ya Kusini mwa Afrika (Afrika Kusini, Zimbabwe, Angola na Msumbiji) pamoja ilikuwa na jumla ya watu zaidi ya milioni moja, ongezeko ambalo pengine ni mara kumi ya idadi iliyokuwepo katika nusu karne iliyopita, na mji wa Johannesburg ulikuwa ukikaribia watu 400,000. Katika Afrika Kusini mwa Sahara watu walikuwa wakikimbilia bandarini, mijini (sehemu zenye machimbo) na kwenye tawala za miji ambako idadi yake iliongezeka mara mbili kwa kipindi cha miaka ishirini.

## *Msingi wa Baadaye*

Hadi kufikia mwaka 1935 Afrika ilikuwa imefaulu kuvihimili vishindo vya kidemografia vilivyotokana na ukoloni wa Wazungu. Sasa, idadi ya watoto waliozaliwa ilizidi ile ya waliokufa, na karibu sehemu nyingi za bara hili hasa katika miji iliyokuwa ikikua maisha hayakuwa ya shida tena. Ingawa ni kweli kwamba kwa ujumla kiwango cha idadi ya vifo katika bara hili bado kilikuwa juu (kiasi cha vifo huenda kilifikia zaidi ya watu 30 kwa elfu moja na wastani wa mategemeo ya kuishi tangu kuzaliwa mara nyingi hayakuwa zaidi ya miaka 30), lakini ni kutokana na magonjwa ya Afrika ya tropiki, kuliko sababu nyingine yoyote, kulikowafanya wavamizi kuishia kwenye ghuba na kuikinga Afrika isiwe Amerika ya Kusini ya pili. Hata hivyo kidadi ya watu weupe katika bara hili iliongezeka mara thelathini kutoka watu 25,000 katika mwaka 1800 ambao wengi wao walikuwa katika Cape Town, hadi kufikia robo tatu ya milioni katika mwaka 1880. Tano ya sita (5/6) ya jumla hii walikuwa Afrika Kusini, Algeria na Misri. Kufikia mwaka 1935 idadi iliongezeka tena mara tano hadi kufikia milioni 3.75. Nusu ya idadi hii walikuwa Afrika Kusini, robo walikuwa Algeria na wengine (moja ya tano) walikuwa katika sehemu zilizobaki za Afrika ya Kaskazini. Katika kipindi hicho hicho, Waasia (karibu wote wakiwa Wahindi isipokuwa jamii ndogo tu ya Wachina ambao wengi wao waliishi Rand) waliongezeka kutoka kama watu 50,000 hadi kufikia; zaidi ya theluthi moja ya milioni

ambao theluthi mbili kati yao wakiwa wanaishi Afrika Kusini.

## *Msingi kwa siku za Usoni*

Katika mwaka wa 1935, Afrika ilifikia kilele cha uongezekaji haraka wa idadi ya watu. Mahesabu ya kukisia yanaonyesha kwamba idadi ya watu iliongezeka toka milioni 120 katika mwaka 1880 hadi kufikia watu milioni 165 katika mwaka 1935. Kufikia mwishoni mwa miaka ya 1940, idadi ilifikia milioni 200 na kufikia katikati ya miaka ya 1960 idadi ilifika milioni 300 na hadi kufikia katikati ya miaka ya 1970 idadi ilifika milioni 400. Katika idadi ya mwisho iliyotajwa, watu milioni 50 walikuwa wakiishi katika miji yenye watu zaidi ya 100,000, hali ambayo ilikuwa ikihiliwa na wakoloni. Katika miaka ya 1880 kutokana na mahitaji ya watu wa kuwafanyia kazi.

Hatimaye, inafaa kujiuliza kama haya mabadiliko yote makubwa yalitokana na kuingiliwa na wakoloni tu au la. Bila shaka.vurugu iliyotokea katika idadi ya watu (ambao huko nyuma walikaa bila misukosuko) na kusababisha idadi kubwa ya vifo katika *Congo Free State* na kwingineko katikati ya Afrika. Upungufu wa taratibu mno wa idadi ya vifo katika sehemu nyingine za bara hili wakati wa karne ya kumi na tisa na kwa ujumla katika karne, na kuongezeka kwa haraka kwa idadi ya watu katika miji na machimbo ya madini, karibu vyote vilitokana na mapinduzi ya viwanda na kuongezeka kwa mawasiliano ya jamii zilizokuwa na viwanda. Mengi yalitokea katika mwendeleo huu, yangeweza kutokea hata bila kuwa na utawala wa kikoloni: shule za uganga za Ulaya zingekuwa tayari kusaidia tatizo la kuwahudumia wafanyabiashara wao na wengine dhidi ya magonjwa ya kitropiki; wamisionari wangeweza kuweka misingi ya hospitali pamoja na mifumo yake.

Hata hivyo, utawala wa moja kwa moja wa kikoloni uliharakisha maendeleo yote haya. Baadaye, kufikia mwishoni mwa kipindi chetu, utawala wa kikoloni ulisaidia kupunguza vifo vingi kwa kuangiza dawa kutoka nje na kutumia teknolojia ya kisasa ili kuzuia magonjwa yanayoambukiza kwa haraka. Pia kuwepo kwa njia bora za kisasa za usafirishaji kulisaidia kusambaza chakula katika sehemu zenye njaa. Haja ya kuwa na zituo vya utawala ilikuwa kiini cha kuwepo kwa miji mipya; utawala wa kikoloni, kuhakikishiwa usalama wa mtu binafsi (Wazungu) na vitega uchumi vyao kuliharakisha ukuaji wa makazi ya kibiashara, makambi ya machimbo na mashamba. Bila kuwepo kwa serikali za kikoloni, wamiliki biashara wa Kizungu wangaliweza kuwa wakatili na wauaji zaidi kuliko walivyokuwa. Kwa kawaida, Wazungu walihalalisha kuingia kwa ukoloni kwa kuonyesha mafanikio kama haya. Historia za Amerika ya Kusini na China zinaonyesha kuwa katika muda fulani haya mambo mengi ya mafanikio yangaliweza pia kupatikana ,kwa mfano, ukuaji wa viwanda usingerudi nyuma kwa sababu Afrika na nchi zinazoendelea zilikuwa na malighafi muhimu zilizotakiwa.

# 19

## *Athari Kubwa za Kijamii Zilizotokana na Utawala wa Kikoloni-Miundo Mipya ya Jamii*

Katika sura iliyopita tuliona kwamba hasa kwa sababu ya athari ya ukoloni watu wa Afrika hawakuongezeka tu katika idadi bali pia walipata migawanyiko mipya iliyosababisha maendeleo ya haraka ya miji iliyokuwepo na kuanzishwa kwa miji mingine na mipya. Lakini katika kipindi hiki tunachokichunguzia jamii za Kiafrika hazikuongezeka tu katika idadi bali pia zilipata mabadiliko mengine ya kijamii wakati huo huo.

### *Miundo Mipya ya Kijamii*

La kwanza katika mabadiliko ya kijamii yaliyotokea na ambalo moja kwa moja lilikuwa zao la kuingizwa kwa ukoloni katika bara hili lilikuwa ni kuongezea katika muundo wa kitabaka uliokuwepo, tabaka jingine zaidi la viongozi wa kigeni na watangulizi. Juu ya tabaka bora la viongozi wa zamani wa siasa na dini sasa kukawa na tabaka jipya la warasimu na wafanyabiashara wa Kizungu. Ama kwa hakika katika Afrika Mashariki, ambako Waasia walishawishiwa na ukoloni kuhamia, kuliongezeka matabaka mapya mawili. Tukiacha Afrika Mashariki ambako sehemu ndogo ya uchumi ilimilikiwa na Waasia, katika kila koloni ni Wazungu peke yao waliomiliki uchumi, siasa na elimu. Katika hali hiyo Waafrika wakawa duni na wakawa wanawategemea Wazungu, na wakati mwingine Wahindi, kwa masuala ya uongozi na mifano.

Muundo huu wa uhusiano wa kijamii ulisaidiwa na nadharia ya uwongo na ya kibaguzi ambayo ilijaribu kuyapanga matawi mbalimbali ya jamii ya mwanadamu katika mpangilio msongc wa ustaarabu: Waafrika (Wanegro) wakiwa katika sehemu ya chini kabisa ya ngazi na Wazungu (weupe) wakiwa katika sehemu ya juu kabisa. Hasa katika Afrika Kusini mwa Sahara ambako masetla weupe walijikuta wamo katika mkinzamo baina yao na Wabantu, ambao waliwazidi kwa idadi, nadharia hii ya kibaguzi ilitiliwa sana mkazo.


Katika hali halisi ya maisha kukwezwa kwa nadharia hii ya kibaguzi kulileta sera ya kuwafanya Waafrika wasipewe haki sawa na weupe. Katika serikali ya mkoloni hata kama walikuwa na elimu ya juu kiasi gani. Katika Afrika Magharibi hii ilisababisha kuachwa kwa sera za kiungwana zilizokuwepo katika miaka ya katikati katika karne ya kumi na tisa ambazo ziliruhusu Waafrika kuwa na vyeo sawa na Wazungu. Nadharia hii pia ilisababisha kuwepo kwa sera ya kuwatenga Waafrika mbali na Wazungu mijini. Hapakuwepo tu maeneo ya kuishi bali pia kulikuwepo na hospitali zao, vilabu vyao, n.k. Majengo waliyojengewa Wazungu yalikuwa tofauti kabisa na yale waliyojengewa Waafrika. Athari mojawapo ya nadharia hii ya kibaguzi ilikuwa ni kuwafanya Waafrika

wajihisi watu duni kiasi cha kutokujiamini wao wenyewe na kutokuwa na hakika na maisha yao ya baadaye; kwa ufupi, hali ambayo wakati mwingine ilimfanya Mwafrika apendelee kuwaiga Wazungu bila kusaili mambo yao. Lakini kwa bahati nzuri baadhi ya Waafrika waangaza-mambo walikerwa sana na nadharia hii ya kibaguzi wakaanza kuusaili mtazamo potofu wa ukoloni kiitikadi na kijamii wakitumia maelezo yatokanayo na historia na Ukristo. Kwa kufanya hivyo wakawa wamesaidia kutayarisha njia kwa ajili ya fikra kali na kizalendo zilizojitokeza baada ya Vita vya Pili vya Dunia.


Mbali na kuanzisha tabaka jipya la Watawala ukoloni pia ulibatilisha muundo wa kitabaka uliokuwako katika Afrika hapo awali na ukasababisha kutokea kwa makabwela wa mijini na tabaka bora jipya. Ingawa Afrika kabla ya ukoloni ilitoa nafasi nyingi za kuwawezesha wenye uwezo kupanda katika daraja za kijamii kutokana na jitihada za mtu mwenyewe muundo wake wa kitabaka ulielekea kutilia uzito zaidi swala la kuzaliwa, yaani ukoo wa mtu. Hii ilifanywa kwa kisai kwamba si vyeo va kisiasa tu bali hata vile vyenye heshima vile ukasisi na ufuaji chuma pia vilifuata ukoo. Utawala wa kigeni ulileta mabadiliko makubwa katika muundo wa jamii katika Afrika na kutilia mkazo tu uwezo na mafanikio ya mtu binafsi; kuliko kufuata ukoo, na kwa kutoa nafasi za kujiendeleza ambazo hazikuwa zikipatikana katika muundo wa jamii na taasisi za jadi katika Afrika. Aidha matumizi mabaya ya taasisi na mifumo mingi ya Kiafrika yalielekea kuvunja mamlaka na heshima ya tabaka bora la hapo awali na kuondoa hicho ambacho watu walikuwa nacho juu yao. Sheria na maadili ya kikoloni, kwa kuondoa utumwa na kutangaza usawa wa watu wote mbele ya sheria za nchi na za dini, viliwapa nafasi ya kupanda daraja hata wale waliokuwa na hali duni kabisa katika jamii za kijadi; kila mtu kulingana na uwezo na majaliwa yake.

Miji mipya na iliyokuwa inaendelea iliimarisha athari za mapinduzi ya sheria na maadili kwa kuwapa watumwa uhuru, na watu wa aina yao, nafasi ya kujishughulisha wao wenyewe pasi na kuzuiwa na mazingira ya kihistoria. Halikadhalika vituo vya miji, kutokana na sababu tulizokwishaona katika sura iliyopita viliwavutia sana watu wa matabaka mengine waliokuwa vijijini. Wahamiaji ambao walikuwa na elimu ya juu au walikuwa na ujenzi mkubwa wa ufundi walipanda daraja haraka na kuingia katika kundi la tabaka bora jipya au kulikaribiakaribia tabaka hilo. Wale wahamiaji ambao ama walikuwa na elimu kidogo au hawakuwa na elimu yoyote na ambao ama walikuwa na ujuzi kidogo wa ufundi au hawakuwa na ujuzi wowote walishuka hadhi na kuwa katika tabaka la chini kabisa la jamii ya mijini. Tabaka hili likafahamika kama "umma wa mijini" au "makabwela wa mijini", kama wanavyoitwa na baadhi ya wanazuoni. Wengi wao walijikuta chini ya fadhila za waajiri na wengine wakajifundisha mambo ya biashara, wakaanzisha biashara zao binafsi na za aina mbalimbali.

Makundi yote mawili, yaani tabaka bora jipya na makabwela wa mijini, yalichukua nafasi muhimu sana katika mabadiliko yaliyotokea katika vijiji wakati wa ukoloni. Hata hivyo ni wazi kwamba kundi la kwanza ndilo lililokuwa muhimu zaidi katika historia ya siasa, uchumi na jamii katika Afrika ya ukoloni. Faida moja kubwa waliyokuwa nayo watu wa tabaka bora jipya dhidi ya tabaka bora la kimapokeo na umma wa mijini na vijijini ilikuwa ni kisomo. Hali ilivyokuwa ni kwamba katika maeneo ya Afrika ambayo



19.1 *Wakitafuta elimu: darasa la Mengo CMS High School, Uganda (Royal Commonwealth Society)*



**19.2** *(Mchezo wa) 'Cricket' wakati wa ukoloni: Ukuzaji wa wasomi wapya*

hayakukaliwa na Waislamu pengine uvumbuzi muhimu kabisa wa utawala wa kigeni ulikuwa ni kisomo. Kujua uwezo, mamlaka na athari ambayo kizazi cha kwanza cha makarani, wakalimani, na walimu wa Kiafrika walikuwa nayo kunatoa mwanga juu ya mvuto mkubwa ambao kisomo kilileta juu ya Waafrika wengi. Kisomo kiliwawezesha watu wa tabaka hili kuyajua mawazo na fikra za Kisayansi na Kijamii za ulimwengu wa Magharibi, likawawezesha kufanya mazungumzo na watawala wa kikoloni juu ya maisha na hali ya baadaye ya Afrika, na kikawafanya waijue mitindo ya maisha ya jamii ya Ulaya. Kuijua mitindo hiyo ya maisha kulifanya mitindo yao wenyewe ya maisha iwe mifano ya kuigwa na ndugu zao ambao hawakubahatika sana kama wao.

Lakini siyo watu wote wa tabaka bora jipya la Afrika ya ukoloni walioingia katika tabaka hilo kutokana na kisomo na wala siyo kwamba wale wote walioingia katika tabaka hilo kutokana na kisomo walikuwa na hali sawa kabisa. Kama Profesa Lucy Mair na wanazuoni wengine kadhaa walivyoonyesha baadhi ya watu waliingia katika tabaka hilo kutokana na fedha walizopata ama katika mashamba yao makubwa au katika biashara na wakawafadhili ndugu zao ambao walikuwa na kisomo zaidi yao lakini ambao hawakuwa na uwezo wa kifedha kugharamia shughuli zao za upinzani wa kisiasa. Baadhi ya wakulima wa pamba na kahawa, katika Uganda, wakulima wa kakao wa Nigeria Magharibi na Gold Coast, wakulima wa kahawa wa Ivory Coast na wakulima wa karanga wa Senegal na Gambia waliweza kupata uanachama wa tabaka hilo bora kwa msingi wa mafanikio yao katika kilimo. Mafanikio katika biashara nayo halikadhalika yaliwawezesha watu kuingia katika tabaka hilo bora, hasa katika Afrika Magharibi ambako Waafrika wengi waliopata elimu tafauti tafauti waliweza kujipenyeza kama wafanyabiashara wa kati baina ya wakulima wa msingi na makampuni makubwa ya kibiashara ya Kizungu. Katika Afrika ya Mashariki na Kati; kinyume na ilivyokuwa katika Afrika Magharibi, ni Waafrika wachache sana waliweza kuingia katika kundi la tabaka bora jipya kwa sababu ya sera zilizotungwa makusudi kabisa na watawala wa kikoloni na pia kutokana na kazi za biashara uchwara za Wahindi, Wareno na Wagiriki.

Tukiacha nchi kama vile Liberia na Sierra Leone, ambako kwa muda mrefu tabaka bora jipya lilikuwa na watu ambao hawakuwa wenyeji wa nchi hizo, tunaona kwamba katika sehemu ya mwanzo ya karne hii watu wa tabaka bora jipya na tabaka bora la zamani walijenga tabia ya ushirikiano - wale wa tabaka bora jipya wakichukuliwa kama watu waliopatanisha jamii za kijadi/asili na utamaduni wa kimagharibi. Katika Gold Coast na Egbaland wale wa tabaka bora jipya walijaribu kushirikiana na wa tabaka bora la kimapokeo ili kujenga jamii mpya na kuondoa utawala wa Mzungu. Lakini jitihada hizi hazikufanikiwa.

Hata hivyo kadri utawala wa kikoloni ulivyozidi kupaya mashiko mashaka na mvutano vikaanza kujitokeza baina ya matabaka hayo mawili. Wale wa tabaka bora jipya walifikiria, kwa makosa, kwamba Ulaya ilikuwa imeazimia kuifanya Afrika iwe ya kisiasa na kwamba Wazungu wangetumia baadhi ya watu wa tabaka lao kulifikia lengo hilo. Lakini chini ya Utawala wa Mkoloni warasimu wa Kizungu ndio waliochukua nafasi ya watu wa tabaka hili bora jipya. Tena basi badala ya kuwachukua watu wa tabaka hili kama wenzi wao katika uongozi utawala wa mkoloni ulipendelea sana kuwatumia watu wa

tabaka bora la kimapokea - ambao ndio waliopewa madaraka ya serikali za mitaa. Hali hii ilijitokeza zaidi hasa katika makoloni ya Mwingereza ambako kila jitihada zilifanywa kuwalinda watu waliokuwa wakiwatawala kabla ya mkoloni. Kwa kiasi fulani hali hii pia ilijitokeza baada ya mwaka 1906 katika makoloni ya Wabelgiji. Hata katika makoloni ya Mfaransa ambako nyingi ya tawala maarufu kabisa ziliangamizwa wakati mwingine familia zilizokuwa zikitawala kabla ya mkoloni ziliachiwa kuendelea ingawa nguvu zake zilipunguzwa sana, na kutumiwa tu katika kiwango cha kijiji au wilaya.

Kwa kuwa hawakupewa nafasi katika utawala wa mkoloni watu wa tabaka bora jipya wakaanzisha upinzani wa wazi dhidi ya utawala wa mkoloni. Lakini wale watawala wa kimapokeo hawakuweza kuwaunga mkono katika upinzani huu; kwani nguvu ya watawala hawa wa jadi ilitegemea sana utawala wa mkoloni, jambo ambalo lilifanya wasiweze kufurukuta. Aidha watawala wa kimapokeo waliokuwa wengi hawakuwa na elimu ya kutosha kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kisiasa. Na kwa vyovyote vile iwapo watawala hao wa kimapokeo wangekubali kuliunga mkono tabaka bora jipya ni dhahiri kwamba wangeshuka daraja na kuchukua nafasi ya pili au pengine ya tatu. Kwa kuwa watawala hawa wa kimapokeo hawakukubali kuliunga mkono tabaka bora jipya walishutumiwa na tabaka hilo kuwa walikuwa vikaragosi vya ubeberu. Nao wakalishutumu tabaka hilo jipya kuwa walikuwa wanaleta mapinduzi ambayo yangeharibu mila zao za kale na kale na kwamba walitaka kuupindua ulimwengu.

Mambo yalikuwa mabaya zaidi makundi haya mawili yalipochonganishwa na propaganda za mabeberu kuhusu uwakilishi wa watu. Tabaka bora jipya lilidai kuwa ndilo lililokuwa mwakilishi wa watu. Watawala wa Kimapokeo walipinga madai hayo na kusema kuwa wao hasa ndio waliowakilisha watu; watawala wa kikoloni na ubishi huo ilionekana wazi katika ugomvi baina ya mfalme wa Akyem-Abuakwa katika *Gold Coast*, *Nana Sir Ofori Atta*, na viongozi wa chama cha *National Congress of British West Afrika* (Chama cha Wananchi wa Koloni la Waingereza la Afrika Magharibi) kwenye miaka ya 1920*. Halikadhalika chuki hiyo pia ilidhihirika katika ugomvi baina ya chama cha harry Thuku cha *'Young Kikuyu Association'* (Chama cha Vijana wa Kikuyu) na chama cha *Kikuyu Association*, ambacho kwa kweli kilikuwa chama cha watawala wa kimapokeo. Mwisho chuki hiyo ilijitokeza katika mapambano baina ya Blaise Diagne na watawala wa kimapokeo wa Kiislam katika Senegal.

Hata hivyo kutokana na hayo tuliyoona hapo juu hatuwezi kuhitimisha kuwa uhusiano wa kawaida uliokuwepo baina ya tabaka bora jipya na watawala wa kimapokeo katika kipindi cha 1880 hadi 1935 ulikuwa uhusiano wa ukinzani. Uhusiano uliokuwepo ulitofautiana kutegemea mahali na wakati. Katika nchi zilizotawaliwa na Wafaransa si tabaka bora jipya wala si watawala wa kimapokeo walioshamiri chini ya utawala huo wa kigeni. Na baada ya Vita vya Pili vya Dunia, wakati ambapo ukali wa nguvu ya utawala wa maguvu wa kigeni pole pole ulianza kupunguza, wale waliotokea kuwa viongozi wa utaifa wa Afrika ya Kifaransa walikuwa ni pamoja na watawala wa kimapokeo na vizazi vyao.

Katika Gold Coast chama cha *'United Gold Coast Convention'*, chama ambacho kilikuwa maarufu sana kabla ya kutokezea kwa Dkt. Kwame Nkruma, kiliwakilisha namna fulani ya mwungano wa tabaka bora la kimapokeo na tabaka bora jipya. Katika sehemu

kama Ethiopia, Misri na Buganda, ambako watawala wa kimapokeo walikuwa wamezikubali athari za kimagharibi hapakuwa na mgongano wowote wa kimantiki baina yao na tabaka bora jipya. Hali hiyo hiyo pia ilijitokeza katika jamii kama za Waigbo ambako tabaka bora la kimapokeo halikuwa na nguvu iliyoendelea hadi wakati wa ukoloni. Kwa vyovyote vile tabaka bora jipya halikuwa la watu waliong'ang'ania ndoto za ubeberu tu wala si watawala wa kimapokeo wote waliopinga jitihada za mabadiliko ya baadaye ya mawazo ya kizalengo. Makundi yote mawili yalikuwa na sifa nyingi zilizofanana kuliko ilivyokuwa ikidaiwa katika majadiliano mbalimbali yaliyotokezea.

## *Kutokea kwa Vyama Vipya*

Mbali na kuleta miundo mipya tuliyojadili hapo juu utawala wa ukoloni ulileta pia mabadiliko mengine katika muundo wa jamii ya Mwafrika. Na hapa tunazungumzia kutokea kwa vyama vipya ambavyo viliwasaidia watu wengi wa vijijini kujiweka sawa na kanuni na mahitajio ya jamii ya kikoloni. Wataalamu wa masuala ya Afrika wanakubaliana juu ya hali za kijamii zilizosababisha kuwepo kwa vyama hivi. Imeonekana kwamba vyama hivi kwa kawaida vilianzia katika vituo vya miji ingawa baadhi yake, kama vile vyenye misingi ya mbari, baada ya muda vilianzishwa matawi ya nyumbani. Kama alivyoonyesha Profesa Wallestein kwa wazi kabisa uhamaji toka vijiji vya jadi kwenda katika maeneo ya miji ya kileo "ulitegemea, ulitengua na kubadilisha mkabala wa mtu". Kwa kuwa si jamii ya kimapokeo wala utawala wa mkoloni ambao ulikuwa na hatua mathubuti za kuchukua kukabiliana na mahitaji ya wahamiaji wote hao ilibidi wahamiaji waanzishe taasisi zao wenyewe, mifumo yao wenyewe na kanuzi zao wenyewe ili kuweza kuishi katika mazingira mageni na magumu ya mjini.

Mitaala ya Godfrey Wilson katika Afrika Mashariki imeonyesha kwamba kulikuwa na uhusiano wa wazi kabisa baina ya nguvu ya jamii ya kikoloni na kuanzishwa kwa vyama hivi. Ndiyo maana Waafrika wa Kenya ambao utamaduni wao wa jadi ulikandamizwa sana na utawala wa mkoloni na uchokozi wa masetla walikuwa na vyama imara zaidi na vya kimbari zaidi kuliko walivyokuwa Waafrika wenzao katika nchi jirani kama vile Tanganyika na Uganda. Kwa hiyo katika uundaji wa vyama hivi kulikuwa na namna fulani ya kujilinda na kujiimarisha.

Aidha hali za maisha ya mijini zilitoa nafasi ambazo zilifanya iwe rahisi kuanzishwa kwa vyama kama hivyo; kama alivyosema Profesa Thomas Hodgkin hali za miji zilizota "vituo halisi ambako wenye maslahi ya aina moja waume kwa wake wangeweza kugotana".

Katika kipindi tunachokijadili kulitokezea aina tatu kuu za vyama hivi. Katika kundi la kwanza tunapata vile vyama ambavyo tungeweza kuviita vyama vya "starehe", yaani vilivyojishughulisha na ukuzaji wa starehe na burdani tu. Hivi vilisababishwa na kukosekana mijini kwa shughuli za kimapokeo kama tafrija, burdani, mafunzo ya uzalendo - kama vile michezo ya kuvaa vinyago, vyama vya marika na sikukuu za kimila. Kulikuwa pia na mvuto uliotokana na hali ya maisha ya Kizungu kama ilivyokuwa inavyojitokeza katika jamii za Kizungu katika kila koloni. Katika kategoria hii kulikuwa na vyama kama

vile vilabu vya mpira wa mguu, vyama vya Maskauti wa Kuume na wa Kike, vyama vya majadiliano (kongamano) na vyama vya vijana waliosoma pamoja zamani.

Katika kundi la pili kuna vyama vya mbali mbalimbali. Vyama hivi vilikuwa ni mwendelezo wa mshikamo wa mbari za vijijini huko mijini. Kulikuwa na vyama vya ngazi mbalimbali - vya kijiji, ukoo na vya mbari. Vyama hivi vilikuwa na kazi mbili maalumu. Kazi moja ilikuwa kumsaidia mtu ambaye ndiyo mwanzo tu alikuwa amehamia mjini ili aweze kuyakabili maisha ya mjini bila matatizo makubwa. Kutokana na vyama kama hivyo wageni walipewa malazi na kazi, na wanachama wake walipewa misaada wakati walipopata shida. Waliweza kupewa mikopo ya kuendeleza biashara zao iwapo waliendelea kupata hasara. Mazishi, ndoa na gharama nyingine zilizokubaliwa na chama viliweza kulipiwa kwa mkopo au michango kutoka kwa wanachama kulingana na hali ya mambo ilivyokuwa.

Kazi nyingine ya vyama vya mbari ilikuwa ni kuweka njia ya kujenga mwamko wa kimaendeleo nyumbani kwa kuweka uhusiano madhubuti baina ya watu wao wa mijini na watu wao wa vijijini. Mwanzoni hii ilivifanya vyaa vipate upinzani mkali kutoka kwa maofisa wa utawala wa mkoloni. Kwa mfano katika Nigeria kusini wakati mwingine shughuli zao zilifanyiwa upelelezi wa siri.

Katika kundi la tatu kulikuwa na vyama vya wafanyabiashara ambavyo vilitokana hasa na juhudi za kutaka kuleta nafuu katika mambo ya uchumi. Kwa kiasi kikubwa vituo vingi vya mijini vilitumika katika sehemu za biashara, machimbo ya madini na mawasiliano yote vikawa na nafasi za ajira kwa wafanyakazi wenye ujuzi na wasio na ujuzi. Kwa hiyo baada ya muda si mrefu kukatokea katika miji hii watu wengi ambao waliishi kwa mishahara na ujira. Kulikuwa pia na mafundi mchundo walioajiriwa wenyewe na ambao walitoa baadhi ya huduma zilizohitajika kwa watu wa mijini.

Maisha ya wakazi hawa wa mijini yalifungika katika ulimwengu wa uchumi na masoko; ulimwengu ambao hawakuelewa muundo na mwenendo wake. Ili kujilinda na ulimwengu huu wa kiuchumi ambao hawakuuzoea wale wafanyakazi kazi za kulipwa mishahara au ujira walianzisha vyama ambavyo walitumia kwa kufanyia mazungumzo na mapatano na waajiri wao ili kuweza kupata malipo mazuri zaidi na hali au mazingira mazuri zaidi ya kazi. Wale mafundi walioajiri wenyewe nao pia waliunda vyama vya mafundi ambavyo viliwasaidia katika kupanga bei, viwango, masharti ya uanagenzi katika ufundi, n.k. Wakati mwingine vyama vya wafanyabiashara na vyama vya mafundi vilishirikiana kama vyama rafiki vikiwasaidia wanachama wao kwa kuwapa misaada ya fedha na maoni wakati wa shida, vikiwapa misaada ya vifaa vya mazishi, mahitajio ya elimu, kuwalipa wanachama wao gharama za masomo na kugharimia sikukuu mbalimbali.

Miaka ya 1880-1935 ilishuhndia kiasi fulani cha mwanzo wa vyama hivi. Hivi karibuni Profesa Kilson ameonyesha kwa muhtasari kwamba hadi kufikia mwaka 1937 kulikuwa na aina mbalimbali za vyama vya wafanyabiashara na vya wafanyakazi katika Nigeria, Sierra Leone, Kenya na kwingineko. Lakini uchunguzi wake, na wa watu wengine pia, unaonyesha wazi kuwa kilele cha vyama hivi hakikufikiwa hadi baada ya Vita vya Pili vya Dunia.

Sababu za hali ya namna hii zilikuwa nyingi. Kwa kiasi fulani vyama hivi

vilitegemea kuenea kwa elimu na athari yake, kama ilivyokuwa athari ya uanamaji ilichukua muda kujitokeza. Nje ya maeneo ya pwani ya Afrika, yaani Maghrib, Misri na Kenya athari hii ilichukua zaidi ya miongo mitatu kujitokeza. Katika Afrika Kusini ambako mazingira yangekuwa mwafaka zaidi kutokana na mapinduzi ya mapema ya viwanda na mawasiliano, kuongeza kwa ukatili wa utaifa wa Makaburu na kupinga kwao Wazungu wengine kulifanya jitihada za Waafrika ziwe ngumu kidogo. Kuanzishwa kwa vyama hivi pia kwa kiasi fulani kulitegemea maendeleo ya uchumi wa kibepari lakini Afrika ya wakati wa ukoloni inasemwa kuwa haikuwa na uchumi wa kibepari uliokamaa; uchumi wake ulitegemea wafanyakazi wahamiaji - aina ya wafanyakazi ambayo yasemekana kuwa ngumu sana kuanzisha vyama vya wafanyakazi. Na hata baada ya Vita vya Pili vya Dunia katika Afrika ya ukoloni kulikuwa na wafanyakazi wa kulipwa wachache sana. Katika miaka ya 1950 idadi yao ilikadiriwa kuwa kati ya milioni nne na milioni tano. Mwisho hali ya mazingira ya unyonyaji na madaraka yasiyo mpaka vilivizuia vyama hivi au vilivifanya visitambulike kisheria hadi katika miaka ya mwisho ya 1930 au mwanzoni mwa miaka ya 1940.

Athari za kijamii za utawala wa kigeni hazikulingana kote barani Afrika. Kwa upande wa kuenea kwa elimu, ambayo ndiyo ilileta nguvu mpya za uchumi, kupanuka kwa miji ambako kulileta tabaka bora jipya, Afrika Magharibi ndiyo inayoelekea kuwa ilinufaika zaidi ikifuatiwa na Misri na Maghrib, Afrika Kusini, Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Tukichukulia migawanyiko ya makoloni mbalimbali bila kufuata maeneo ya kijografia tunaona kwamba mabadiliko makubwa zaidi yalitokea katika nchi zilizotawaliwa na Waingereza, zikifuatiwa na zile zilizotawaliwa na Wabelgiji na Wafaransa; zile zilizotawaliwa na Wareno zikiwa za mwisho. Na hata katika nchi zilizotawaliwa na Waingereza pia kulikuwa na tafauti. Katika makoloni ya Uingereza ambako mabadiliko makubwa yalionekana ni Misri, Gold Coast, Nigeria, Uganda na Sierra Leone, zikifuatiwa na Kenya na Rhodesia Kusini na Kaskazini (Zimbabwe na Zambia). Na kama tutachukua koloni moja moja tutaona kwamba kuna mabadiliko zaidi yaliyotokea katika sehemu za kusini kuliko kaskazini katika Gold Coast na Nigeria. Katika nchi za Afrika zitumiazo Kifaransa makoloni ya Afrika Magharibi yanakuwa katika mstari wa mbele yakifuatiwa na yale ya Afrika Kaskazini na yale ya French Eqnatorial. Katika sehemu za Afrika Magharibi zilizotawaliwa na Wafaransa, Senegal na Dahomey (ambayo sasa yajulikana kama Benin) zilikuwa mbele kabisa wakati makoloni mengine yalikuwa nyuma kabisa.

Sababu za kuwepo kwa tafauti hizi za nguvu za mabadiliko katika maeneo na nchi mbalimbali za Afrika ni dhahiri. Kwanza ilikuwa ni urefu wa kipindi cha mwingiliano na hali ya mwingiliano wenyewe uliokuwepo baina ya nchi fulani maalumu au eneo fulani la kijiografia na Ulaya wakati wa utawala wa mkoloni. Afrika Magharibi na Kusini zilikuwa na mawasiliano na maingiliano na Ulaya tangu karne ya kumi na sita. Kwa hiyo hadi kufikia karne ya kumi na tisa kulikwishakuwa na hali za maisha ambayo kidogo yalifanana fanana na ya kimji katika sehemu mbalimbali za pwani - huko St. Louis, Banjul, Accra, Lagos, bandari za Oil River, Luanda, na Cape (kwenye Rasi). Sehemu hizi zilikuwa ni mahali pazuri sana pa kuanzia na hatimaye kuingia ndani kwa nguvu za elimu ya kimagharibi, Ukristo wa kimagharibi na biashara ya kimagharibi. Pwani ya Mashariki ya

bara hili ilianza kuingiliana hasa na Ulaya kuanza kwenye miaka ya 1870 tu.

Sababu nyingine ilikuwa ni sera za kibaguzi zilizofuatwa na watawala wa kikoloni ambazo ziliwawekea Waafrika kila aina ya vikwazo ili wasiweze kushiriki moja kwa moja katika biashara na elimu. Kwa hivyo kiwango cha mabadiliko kikatawaliwa na nafasi za elimu na uchumi zilizotolewa kwa Waafrika Na kwa hakika hii inaonyesha kwa nini mabadiliko mengi yalitokea katika makoloni ya Waingereza, watu ambao sera yao ya ubaguzi ilikuwa nafuu kuliko wakoloni wengine wote.

Sababu ya tatu ni kuwepo kwa masetla. Hakukuwa na masetla wa Ulaya katika Afrika Magharibi. Hii, kwa namna fulani inaweza kuwa sababu ya maendeleo ya haraka ya watu wa Afrika Magharibi katika mambo ya elimu na uchumi. Lakini kulikuwa na masetla wengi Algeria, Kenya, Rhodesia Kusini na Kaskazini, na Afrika Kusini. Maslahi ya masetla hawa yaligongana na yale ya Waafrika hivyo wakatumia uwezo wao na kufahamiana kwao na watawala wa kikoloni kuwawekea vikwazo Waafrika au kuzima shughuli zao za kimaendeleo.

Mwisho, kulikuwa pia na swala la kutafautiana kwa kuathirika kwa Waafrika na athari za kigeni. Katika Nigeria Waigho waliuvaa umagharibi kwa nguvu zaidi kuliko walivyofanya Wafulani. Katika Kenya Wakikuyu walitambua mapema faida za elimu ya kimagharibi kuliko jirani zao. Upingamaendeleo wa Utamaduni wa Kiislamu na vita dhidi ya athari za kizungu, hasa katika Sudani Mashariki, viliendelea kuzuia kuenea kwa athari za Kimagharibi, hasa elimu ya Kimagharibi. Kwa upande wa Afrika Kaskazini na Misri baadhi ya watu katika tabaka bora lililokuwa likitawala walijaribu kuhakikisha kuwa utamaduni wa Kiislamu hautauawa na kuingizwa kwa sayansi na biashara ya kimagharibi. Msimamo wao ukawa ni kuoanisha utamaduni wa Kiislamu na fikra za kisayansi za kimagharibi bila kuleta mgongano. Kwa kuwa Waislamu wa Sudani Magharibi hawakuweza kuonyesha jitihada zozote juu ya jambo hili kama walivyofanya wenzao huko Misri na Afrika Kaskazini hawakuwa tayari kukabiliana na changamoto zilizoletwa na utawala wa mkoloni. Kutokana na hali hiyo Waingereza na Wafaransa wakaweza kuamua ni aina na kiasi gani cha athari za Kimagharibi viingizwe katika eneo hilo.

Kwa hiyo basi hadi kufikia mwaka 1935, hasa kutokana na athari ya ukoloni, Afrika haikuwa tu imeongeza idadi ya watu bali pia ilikuwa imepata mabadiliko ya kijamii. Miundo mipya ya kijamii, matabaka mapya na vyama vipya vilikuwa vimejitokeza. Mambo yote haya yakawa msingi ambao kwao mabadiliko makubwa na muhimu zaidi yalitokea katika miongo mitatu iliyofuata.

# 20

# Dini katika Afrika Enzi ya Ukoloni

Kipengele kingine cha maisha ya kijamii ambacho kiliathiriwa na ukoloni kilikuwa dini. Muda mfupi tu kabla ya majilio ya utawala wa kikoloni barani Afrika, dini tatu zilikwishasitawi; nazo ni Dini ya Jadi mbili ngeni za Uislamu na Ukristo. Kwa jumla inakubalika kuwa ingawa wakati huo Waafrika wengi sana walikuwa wakifuata dini ya kwanza lakini kutokana na mapinduzi ya Kiislamu na amali za Wakristo na Waislamu katika karne ya kumi na tisa, ambazo zimezungumzwa katika majuzuu yaliyotangulia, dini hizo mbili zilikwishapata wafuasi wengi. Uisilamu wakati huo ulikuwa umeshamiri katika ukanda wa Sudan na huko Afrika Kaskazini, ambapo Ukristo ulikuwa bado ungali kandokando tu ya pwani katika kanda za kusini mwa Sahara ukiacha Afrika ya Kusini na maeneo machache ya Afrika Magharibi ambako ulikwishapenya maili kadhaa barani.

## *Dini ya Jadi ya Kiafrika na Utawala wa Kikoloni*

Kati ya dini hizo tatu, hapana shaka kuwa Dini ya Jadi ilishambuliwa sana kuliko dini zote na iliathirika vibaya zaidi kuliko dini nyingine hizi mbili. Uingiliaji kati kikamilifu wa Wazungu katika kipindi cha ukoloni ulitokana na fikra kwamba, ili kuweza kuleta maendeleo ilibidi utamaduni wa Kiafrika urekebishwe kama siyo kufishwa moja kwa moja. Kwa vile utamaduni wa Kiafrika ulifungamana kwa undani kabisa na dini, inakuwa rahisi kuona namna hata sera ya kikoloni ya Wazungu ilivyokinzana vikali na baadhi ya misingi na amali ya dini ya jadi ya Kiafrika ambamo Jamii ya Kiafrika ilikitwa. Miongoni mwa misingi na amali hizo zilikuwemo imani katika mizimu, nguvu za kudura, miungu na madhehebu, uchawi, usihiri, kafara na matambiko, miiko na kutukuza mababu, sherehe za mila za utokaji nje, jando na desturi zinazohusu vifo na mazishi. Ni misingi na amali hizi ambazo wamisionari wa Kikristo walikataza na kuzishambulia vikali. Hivyo walidhoofisha taathira za viongozi wa jadi na wa kiroho wa Kiafrika kama vile wahubiri wa kiume na kike, wachawi, wagimbi na wafalme wa kiungu.

Watawala hao wa kikoloni pia walizichukia sana baadhi ya amali za jadi za kidini na walijaribu kuzibatilisha na papo hapo kukandamiza baadhi ya madhehebu na miungu. Katika Gold Coast (Ghana), utawala wa kikoloni wa Kiingereza ulipiga marufuku ya *Katawere*, mungu mlezi wa Akim Kotoku, na madhehebu ya Aberewa katika mwaka 1908. Kabla ya hapo Serikali ya Kidachi ilikwishadamiri maziara ya madhehebu ya Denteh ya Kete-Krach katika miaka ya 1880 na mhubiri wa Denteh alifungwa na kunyongwa na serikali hiyo. Wakrobo walihamishwa kwa nguvu katika makazi yao katika milima ya

Krobo na utawala wa kikoloni wa Kiingereza ambao uliyavunjilia mbali makazi yao na madhehebu ya maziara yao.

Baadhi ya madhehebu mapya ambayo yalijitokeza kwa ajili ya kuwalinda watu dhidi ya uchawi katika Afrika Magharibi yalikuwa madhehebu ya *Aberewa* (Bi Kizee) katika Chama na ambayo yaliondolewa na utawala huo wa kikoloni katika 1908. Harakati zilizoenea sana za kuondolea mbali uchawi zilikuwa za madhehebu ya Bamucapi ya Afrika ya Kusini-mashariki na Afrika ya Kati ambayo yalikuwa yameenea sana Msumbiji; Nyasaland (sasa Malawi), Rhodesia (Zambia na Zimbabwe), Kusini mwa Tanganyika (sasa Tanzania), na Belgian Congo (sasa Zaire), (Angalia mchoro 8.1). Mathalan, huko Uganda Sheria ya Uchawi ilipitishwa katika mwaka 1912 na ilirekebishwa katika mwaka 1921 ili kuongeza adhabu iwe kali zaidi kwa kuzidisha kifungo kutoka cha mwaka mmoja kuwa cha miaka mitano na vile vile kufanya umiliki wa vifaa vya uchawi ambavyo viliaminiwa kuwa vilikuwa na uwezo wa uchawi kuwa kosa la kustahili adhabu. Shambulio jingine juu ya dini ya jadi ya Kiafrika, hususa katika Afrika Mashariki, lilikuwa dhidi ya sherehe za jando na unyago.

Waafrika waliyajibu mashambulio hayo kwa njia nyingi. Mwanzoni, Waafrika wengi waliyapuuza au kukanusha shutuma hizo na walishikilia imani zao za jadi na waliendelea kuamini matambiko yao ya msingi, ama wazi wazi au kisirisiri. Kwa upande mwingine wengine walijibu kwa kutumia miungu, mababu na madhehebu kupambana na wamisionari hao wa Kikristo na tawala hizo za kikoloni. Katika miongo miwili ya kwanza ya karne hii, wapiganaji wa Kiigbo wa Nigeria ya Mashariki - Kusini walitumia njia hizo za kujilinda na wavamizi wa kigeni. Waesza wa eneo la Abakaliki Wauzuakoli na Waaro ni mfano mmojawapo. Ni dhahiri kuwa baadhi ya madhehebu yalikuwa kiini cha upinzani wa utawala wa kikoloni, kama vile Wamwari katika Rhodesia, au jumuiya za kisiri kama vile Poro katika Sierra Leone na sehemu nyinginezo za Afrika Magharibi. Harakati za kufanya uganga wa Vita pia zilitokea huko Madagascar na Bonde la Kongo. Katika Afrika Mashariki, hususa Kenya, mitume wa Kiafrika walijitokeza kutoa msaada wa kiroho na hamasa ya kupinga ukoloni kama vile mapambano yaliyotokea katika Wilaya ya Machakosi miongoni mwa watu wa Kilungu katika miezi ya awali ya mwaka 1922 (angalia sura ya 22). Mojawapo ya harakati mashuhuri zilizotumia dini na uchawi kupiugana na utawala wa kikoloni na dhuluma, kama tulivyokwishaona, ilikuwa vita vya Maji Maji katika Afrika ya Mashariki ya Kidachi mnamo mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini.

Madhehebu mengine yaliyofanana na Maji Maji yalikuwa madhehebu ya Nyabingi, ambayo yalienea katika sehemu kubwa pamoja na Ruanda (sasa Rwanda), Tanganyika ya Kaskazini - Magharibi (sasa Tanzania) na Uganda. Madhehebu hayo yalianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na yaliongezeka nguvu hadi yalipojitokeza katika uasi wa 1920 dhidi ya kutamalaki kwa Wazungu katika jimbo la Kigezi huko Uganda (angalia mchoro 7.1). Wadachi na Wabelgiji ambao walichukua Ruanda kutoka kwao baada ya Vita Kuu vya Kwanza, walishindwa kuuzima, na hata baada ya kuzimwa uasi wa 1928, madhehebu hayo yalibaki kuwapo hadi hapo mwaka 1934 yalipozimwa kabisa.

Wengine walitumia njia ya kupigana moja kwa moja na njia hiyo ilitumika hasa

katika Afrika Mashariki katika swala la jando na unyago. Katika dayosisi ya Masasi katika Tanganyika ya Kusini na katika Jimbo la Kati la Kenya, kuna mifano ya mapambano makali kati ya Wakristo na Waafrika katika suala la jando na unyago. Katika dayosisi ya Masai, ilianzishwa sera ya swala hili na matokeo yake kukawa na *jando* (kutahiri mvulana) na *malango* (kutahiri msichana) kwa kuzifanya ziwe chini ya uangalizi wa Ukristo na kuondoa mambo yoyote yaliyodhaniwa au kuamuliwa kuwa ni kinyume cha 'Ukristo'. Sera hii ilikwepa mgongano wa moja kwa moja kati ya ufundaji wa jadi na umisioni na amali za Kikristo.

Lakini katika Kenya ya Kati, maafikiano kama hayo hayakuweza kufikiwa na hivyo mapigano yalitokea katika miaka ya awali ya 1920 na 1930. Kwa mfano, shule za binafsi zilianzishwa miongoni mwa Wakikuyu ambao waliazimia kurejesha amali hiyo ya jando na kuwapatia elimu watoto wale ambao hawakuweza kuingia shule za misheni kwa sababu ya mgogoro wa suala la unyango. Katika mwaka 1929, wimbo wa ngoma, ulioitwa *muthirigu*, ambao ulidhihaki misheni na Wakristo waliopinga mila ya jando, ulienea haraka miongoni mwa Wakikuyu lakini ulipigwa marufuku na utawala wa kikoloni wa Kiingereza mwaka uliofuata. Zaidi ya hapo upinzani wa Waafrika ulionekana katika kujitenga kwa waumini wengine wa Wakikuyu, Waembu na Wameru na makanisa ya Kiprostestanti na Kianglikana. Kanisa huru, African Orthodox Church, lilianzishwa katika mwaka 1928, na katika mwaka 1930 harakati za kitume zilianza miongoni mwa Wakikuyu. Zilihubiri habari za hukumu ya Mungu ambayo ingeteremka juu ya Wazungu na Wamisheni. Lakini harakati hizo hazikuchelewa kupigwa marufuku na utawala wa kikoloni.

Upinzani wa Waafrika uliendelea kujitokeza kwa njia mbalimbali, pamoja na ghasia, mashambulizi ya shule za misheni, jitihada za kuwazuia waliubiri kuendesha sala, na hata kumwua mmisionari mmoja huko Kijabe. Pamoja na upinzani wa Waafrika dhidi ya mwelekeo wa wamisionari kuhusu unyago kulichanganyika pia na uzalendo ambao ulikuwa unaongezeka na ambao hatimaye ulisababisha mapambano ya kisiasa dhidi ya utawala wa kigeni.

Kwa kiasi fulani kutokana na mashambulio hayo na kwa kiasi fulani kwa sababu ya kasi ya Uislamu na Ukristo itakavyojadiliwa hapo baadaye, dini ya jadi ya Kiafrika ilipoteza idadi kubwa ya waumini wake. Hata hivyo, kutokana na mrejesho wa Waafrika kwa kukabili mashambulio hayo jadi kwa jumla ilipata nguvu mpya ilipofika miaka ya 1930.

## *Uislamu na Utawala wa Kikoloni*

Inaelekea kuwa Uislamu ulinusurika zaidi kuliko dini ya jadi katika kipindi cha utawala wa kikoloni. Katika maeneo ambamo utawala wa Waislamu ulikwishasitawi kabla ya majilio ya dola ya kikoloni, sheria ya Kiislamu ilikwishaleta umoja wa kieneo kuliko wa kimbari na wafuasi walitii mamlaka ya dini hiyo. Jambo hili lilisaidia ufanisi wa utawala na biashara; na Waislamu waliweza pia kuwaongoa watu na kuzidi kupata waumini wengi. Maendeleo ya mawasiliano yaliwawezesha mawakala wa Kiislamu kupenya katika maeneo ambayo

hayakuingilika kabla ya hapo, na kutokana na njia za biashara kugeuzwa kutoka jangwani kwenda pwani katika Afrika Magharibi, idadi ya Waislamu ambayo mwanzoni mwa enzi ya ukoloni ilikuwa ndogo, ilianza kuongezeka. Kwa mfano katika Sierra Leone asilimia ya watu waliokuwa Waislamu iliongezeka toka asilimia 10 katika 1891 hadi kufikia asilimia 14 katika 1911 na asilimia 26.12 katika 1931.

Idadi ya Waislamu kwenye mwambao wa Afrika Magharibi pia iliongezeka wakati Waislamu wa Kiahmadiyya walipokuja kama wamisionari wakitumia njia za bahari ya pwani. Ingawa Waahmadiyya walihesabiwa kuwa ni wazushi na Waislamu wengine lakini walisaidia katika kuwavutia baadhi ya Waislamu wajifunze elimu ya Kimagharibi. Mwelekeo wa tawala za kikoloni kuhusu Uislamu haukuwa wa aina moja. Hali baadhi walihisi kuwa Uislamu ulikuwa dini iliyoendelea zaidi kuliko dini ya jadi ya Kiafrika, wengine walichukulia sehemu mbalimbali za Uislamu kuwa ni asasi zilizoendelea za kijamii na walizitumia asasi hizo kwa maslahi ya tawala za kikoloni. Hivyo mahakama ya Kiislamu yaliruhusiwa kuanzishwa, watawala Waislamu walipewa mamlaka makubwa zaidi katika baadhi ya maeneo, na Waislamu waliajiriwa na watawala wa kikoloni katika vyeo vya chini kama vile waongoza njia, mawakala na makarani kwa njia hizo. Basi, Waislamu walipata fursa zaidi za kueneza dini yao.

Si tawala zote za kikoloni zilizoangalia Uislamu kwa jicho zuri. Hasa utawala wa kikoloni wa Kibelgiji katika Kongo ya Kibelgiji ya zamani ulichukia Uislamu na kuona Uislamu kuwa ni tishio kwa ujumbe wake wa 'Kuwatanasari' na 'kuwastaaribisha' watu. Misikiti michache tu iliruhusiwa kujengwa na skuli za Waislamu zilipigwa marufuku kabisa katika koloni hilo.

Wazungu wengine, hususan Wafaransa, walijaribu kuwalazimisha raia wao walio Waislamu na wasio Waislamu wafuate utamaduni wao kwa kuamini kuwa walikuwa na wajibu wa kuinua kiwango cha raia wao wa kikoloni kwa kuwafundisha 'faida' za utamaduni wa Kifaransa. Kinyume na Waingereza ambao siasa yao kuhusu mataifa ya Kiislamu ilitokana na msingi wa imani ya kuwa wangeweza kupata ushirikiano wa watawala wa Kiislamu, Wafaransa walifikiria vinginevyo. Mwanzoni Wafaransa walijaribu kuwekea mipaka maeneo yaliyo chini ya utawala wa Kiislamu katika jitihada zao za kutamalaki sehemu kubwa ya Sudan ya Magharibi. Ili kufanikiwa katika kupinga ueneaji wa Uislamu na Sheria ya Kiislamu, walijaribu pia kujenga dini ya jadi na kupanga kanuni za sheria za kimila za Waafrika kama upinzani kwa Uislamu.

Lakini baadaye Mataifa ya kikoloni yalikuza Uislamu badala ya kuuvumilia tu kama ilivyokuwa hapo awali. Sababu ya kufanya hivyo ilikuwa kwamba walipendelea zaidi kuwasiliana na Waafrika Waislamu kuliko na wenzi wao Wakristo. Athari za usasa wa Uislamu zilisifiwa na mataifa ya kikoloni ambayo inasemekana yaliona athari hizo kama kwamba ni 'daraja kati ya uhususa finyu wa jamii ya kijadi na ya misukumo mipana zaidi na mahitajio ya maisha ya kisasa na maslahi za kiuchumi'. Kwa hiyo, Waislamu waliokuwa viongozi watiifu walitiwa moyo mkubwa na mara kwa mara walifanyiwa fadhila rasmi kama vile kupewa heshima na tunzo za kitaifa. Walijengewa Misikiti na Vyuo vya Kurani, na vile vile walisaidiwa kwenda kuhiji na masomoni. Lakini wakati huo huo Waislamu wale ambao hawukutii amri ya wakoloni na walioasi walitiwa adabu na mara nyingi

walinyanyaswa.

Lakini Waislamu walipinga utawala wa Kikoloni kwa sababu za kidini na za kisiasa. Ingawa tawala za kikoloni, kama vile Wafaransa, kwa kiasi fulani ziliungwa mkono na Waislamu katika makoloni yao ya Afrika Magharibi, lakini Waislamu wengi waliazimia kuhifadhi utaratibu wa Uislamu na kwa hiyo hawakuweza kustahimili wawe watiifu kwa utawala wa kikafiri wa Wakristo, na walifanya juhudi za kutokomeza ukoloni wa Kifaransa katika nchi zao. Shaaku hii ilisababisha kutokeza tena kwa umahdi katika sehemu nyingi za maeneo ya Sudani ya Afrika Magharibi. Umahdi ndio uliokuwa dalili za upinzani dhidi ya Wafaransa katika Guinea ya Juu, Mauritania na Senegal, hususan tangu 1906 hadi Vita Kuu ya Kwanza.

Harakati nyingine za Kiislamu zilizoonyesha upinzani dhidi ya ukoloni wa Wafaransa zilikuwa harakati za Hamalliyya, ambazo zilianzishwa na Shaykh Hamallah na ambazo zilishamiri huko Senegal, Sudan ya Kifaransa, Mauritania na Niger. Kadhalika, ilijidhihirisha katika tarika ya Sanusiyya, ambayo iliasisiwa na Muhammad b. [c]Ali al-Sanusi huko Libya na baadaye ikageuka kuwa chama kilichowaongoza Walibya katika vita dhidi ya ukoloni wa Kiitalia tangu 1911 hadi 1932. Kati ya 1860-1901 tarika ya Sanusuyya ilienea Tunisia, Misri, Sahara ya Kati, Sudan ya Kati na Senegal.

Baadhi ya wapinzani wakubwa wa uvamizi wa Kifaransa katika Burkina Faso katika karne ya kumi na tisa walikuwa Waislamu ambao wengi wao waliwaambia Wamosi wa mahala hapo kuwa Wazungu wangeondoka nchini mwao punde tu baada ya Waafrika kusilimu. Isitoshe, kutamalakiwa kwa Wasamori katika Afrika Magharibi na Warabib katika eneo la Chad katika robo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa kuliwafanya watu wa maeneo hayo wawe na akinzani na Wazungu na kulisaidia kuuhusisha Uislamu na upinzani wa utawala wa kikoloni.

Lakini Uislamu ulistawi chini ya utawala wa kikoloni kwa sababu ya hali bora zaidi iliyokuwepo kuliko Ukristo ambao ulilazimishwa na wamisionari, na vilevile kwa sababu ya kuvurugwa kwa maisha ya kijadi kulikosababishwa na ukoloni. Watu wengi walichukulia Uislamu kuwa ni dini ya asili, iliyoenezwa na Waafrika; dini ambayo wafuasi wake hawakujitenga na jumuiya bali walichanganyika nayo. Kitendo hicho kilikuwa kinyume na cha Wakristo ambao walielekea kutenga mbali jumuiya zao na kufuata mtindo wa maisha ya Kizungu. Kwa hiyo si sadfa tu kuwa neno la Watemne (Sierra Leone) kwa Wakristo na Wazungu ni lilehile, 'poto'. Aidha, kinyume na Ukristo uliolazimishwa na wamisionari, Uislamu uliweza kustahimilia ada nyingi zaidi za kijamii na za kidini za kijadi za Kiafrika, kama vile uchawi, ukahini, kuoa wake wengi, na ujima. Kwa hiyo, mtu aliyesilimu hakutakiwa aache kabisa mila za kijadi ambazo wamisionari wa Kikristo walimlazimisha mtu aliyetanasari aziache.

## *Ukristo katika Enzi ya Ukoloni*

Ulazimishaji wa utawala wa kikoloni pia ulisaidia sana kazi ya wamisionari wa Kikristo. Mosi, watawala wa kikoloni na wamisionari walishiriki katika mkataba mmoja wa kidunia

uliotokana na utamaduni mmoja. Pili, utawala wa kikoloni ulitajamali kazi za wamisionari na mara nyingi ulizipa ruzuku skuli za kimisionari. Tatu, ulazimishaji wa udhibiti wa kikoloni juu ya kila nchi ulihakikisha kuwepo kwa amani na utulivu na kwa njia hiyo uliwahakikishia wamisionari ulinzi wa watawala wa kikoloni. Nne, uanzishaji wa njia bora za mawasiliano na uanzishaji wa uchumi wa kifedha uliendeleza biashara na ulisaidia kuleta mtindo mpya wa maisha ambao baadaye ulienea kote barani Afrika na ambao ulijiainisha kwa kusababisha ujima uvunjike na ubinafsi uendelee.

Lakini, hapana shaka, kuwa kuanzishwa kwa wamisionari wa Kikristo elimu na kisomo ndiko kulikosaidia Ukristo kuenea haraka. Kwa kupitia katika skuli nyingi zilizoanzishwa na Wamisionari Waafrika wengi walihusiana na Ukristo, na kwa hakika skuli ndiyo ilikuwa Kanisa katika sehemu nyingi za Afrika. Isitoshe, kwa kufanya lugha za Kiafrika zianze kuandikwa pamoja na kufundishwa kwa lugha za Kizungu kulileta kisomo katika sehemu nyingi za Afrika. Lugha za Kiafrika zilipoanza kuandikwa, fasihi andishi katika lugha za Kiafrika zilianza kutokea, na hayo yote yalisaidia kuenea kwa Ukristo. Kutokana na sababu hizo, pamoja na kutumia mazungumzo au mahubiri ya Injili moja kwa moja, skuli na kazi za tiba, wamisionari waliwatanasarisha watu wengi. Miaka ya mwishoni ya karne ya kumi na tisa ilijulikana sana kwa mafanikio ambayo misioni za Kikristo ziliyapata. Kwa sababu hiyo, jumuiya nyingi za Kikristo zilianza kutokeza pale ambapo hapo awali hapakuwapo hata moja.

Inafaa kusisitiza kuwa uenezaji wa Ukristo katika kipindi cha ukoloni haukutokana tu na ujasiri wa wamisionari wa Kizungu. Waongofu wa Kiafrika, walimu wa dini na wahubiri waliamini vizuri kazi zao. Miongoni mwa waamili mashuhuri walikua Kasisi Apolo, Kive Bulaya ambaye alifanya kazi Kongo ya Kibelgiji (Zaire), Samuel Adjayi Crowther katika Nigeria na Mtume William Wade Harris katika Ivory Coast na Gold Coast (Ghana).

Wamisionari pia walichangia kiasi cha kutosha katika kuanzisha uchumi wa kifedha katika Afrika Misioni zilianzisha mashamba makubwa katika sehemu nyingi za Afrika. Pamoja na kulima vyakula vya mahala pale na kuanzisha mazao mapya, walisaidia kusambaza mazao ya biashara kama vile kakao, kahawa, tumbaku, pamba na miwa.

Fatıka ya hayo yote, Ukristo ulieneza mawazo mengi. Baadhi ya mawazo hayo hayakawa mapya kabisa, na kulikuwapo hali ya kukubaliana kati ya mawazo waliyohubiri wamisionari na yale waliyoamini Waafrika, kama vile kumwamini Mungu na kutii amari yake kwa kutambua kuwa yeye ndiye Hakimu wa mwisho na Mwumba wa wanadamu.

Lakini, wamisionari hao hawakupendezwa na dini na utamaduni wa Waafrika na tangu mwanzo waliazimia kuviondolea mbali. Kama ilivyokwishaelezwa hapo awali, wamisionari hao walihubiri dhidi ya aina zote za imani na amali za kijadi pamoja na kulaani, na pia kukanusha miungu na wachawi na nguvu nyingine za kudra ambazo Waafrika waliziamini. Kwa jumla kwa kiasi kikubwa, kuwa Mkristo, kulimaanisha kuwa mtu alipaswa kuacha kuwa Mwafrika na kutumia utamaduni wa Kizungu maishani mwake. Hivyo, Ukristo ulileta athari ya kufifisha utamaduni wa Kiafrika.

Waafrika walijibu juhudi za wamisionari kwa njia tatu dhahiri: ukabalifu, ukatavu na unasibishaji. Hapana shaka kuwa Waafrika wengi walikubali upesi imani mpya na kuwa Ukristo ulipata mafanikio makubwa zaidi katika kipindi hiki kinachozungumziwa kuliko ilivyokuwa katika karne mbili au tatu zilizopita. Inaelekea kuwa kundi la kwanza la Waafrika waliotanasari lilikuwa la wale ambao walihesabiwa na Waafrika kuwa ni wakitıka miko na wale walio fakiri kama vile wenye ukoma na wengine waliokumbwa na ulemavu wa aina mbalimbali wa kijamii katika jamii za kijadi za Waafrika.

Pia kulikuwa na Waafrika, wale ambao wamekwishatajwa hapo juu, ambao walikataa katakata kupokea ujambe wa Ukristo na wanashikilia mila za kidini na za kitamaduni za jadi zao. Vitu ambavyo kwao vilikuwa na umuhimu zaidi kuliko mambo yale yaliyohubiriwa na wamisionari. Baadhi yao walishiriki katika kuwatesa na kuwatenga waliotanasari, lakini wengine pia waliendelea na kafara na matambiko kwa nia ya kuwapatanisha wanadamu na mizimu. Miongoni mwao wakatokea viongozi wa kidini na kitamaduni pamoja na waganga wa miti shamba, nao ndio ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa na jukumu la kuendeleza imani za Waafrika na kuwafahamisha watu habari kuhusu tamaduni za jadi za Kiafrika.

Makanisa Yaliyojitenga

Mwisho, kulikuwa na wale ambao walijinasibisha na dini mpya kwa kuasisi makanisa ambayo yalijulikana kuwa yalijitenga au kuwa huru, na tukio hilo linawakilisha hatua ya nne katika historia ya Ukristo katika Afrika. Makanisa hayo yalikuwa ya aina mbili kuu; yaani yale ambayo yalijitenga kutoka makanisa yaliyokuwapo na yale ambayo yalijitokeza pasi kuwa na uhusiano wowote na makundi ya kidini yaliyokuwapo. Makanisa hayo mengi yalijitahidi kuingiza kiasi kikubwa zaidi cha itikadi na amali za Kiafrika katika maisha ya Kikristo kuliko kilichokubaliwa katika makanisa yaliyokuwa yakiongozwa na wamisionari. Hayo yalikuwa yanaonyesha shauku ya Waafrika kutafuta "nafasi ya kujiona wako nyumbani" na kuingiza mawazo ya ibada ya Kiafrika katika ibada zao za Kikristo.

Kwa kiasi fulani, makanisa yaliyojitenga yaliwakalisha mrejesho au unasibishaji wao kwa ukoloni na yalikuwa na mwelekeo wa kiukombozi. Katika maeneo yaliyokaliwa na wazungu ambako ukandamizaji wa kisiasa ulikithiri, ndipo hasa makanisa hayo yalizidi kuongezeka na kuwavutia wazalendo wa Kiafrika. Mfano mmojawapo ni makanisa ya Kiethiopia katika Afrika Kusini; makanisa ambayo yalisisitiza Mwafrika kujiendeleza mwenyewe na haki za kisiasa. Ncehemiah Tele alijitenga na kanisa la Misioni la Kimethodist katika mwaka 1882 na miaka miwili baada ya hapo alianzisha kanisa la Tembu, mojawapo ya makanisa huru yaliyoanzishwa mwanzo mwanzo. La pili, ambalo lilikuwa kanisa la kwanza kuitwa la "Kiethiopia" lilianzishwa na Mhubiri wa Kiwesli, Mangena M. Mkone katika mwaka 1892, vile vile huko Afrika Kusini. Harakati hizi za Kiethiopia zilienea katika maeneo mengine ya Kusini na Masharikimwa Afrika.

Katika maeneo mengine ya kikoloni ya Afrika, makanisa yaliyojitenga mara nyingi yalionyesha uhasama dhidi ya utawala wa kikoloni. Kama tulivyokwishaona, John Chilembwe alianzisha kanisa lake la *Province Industrial Mission* katika Nyasaland



**20.1** Mchungaji John Chilembwe (1860/1870-1915) mhubiri na kiongozi wa uasi wa 1915 katika Nyasaland (Malawi), akionekana pichani na familia yake.

(Malawi) na alishambulia vikali kitendo cha kikoloni cha Waingereza cha kutoza kodi na cha kuandikisha watu "jeshini". Hatimaye katika mwaka 1915 Chilembwe aliongoza mapambano ya kisilaha dhidi ya utawala wa kikoloni wa Kiingereza ambayo yalishindwa ndipo alipokamatwa na kuuliwa. Wakati huo huo, *"Watchtower Movement"* ilianza kukua na kuenea toka Nyasaland (Malawi) hadi Southern Rhodesia (Zimbabwe) miongoni mwa Washona, na kuzifanya harakati hizi ziwe za kidini lakini zenye umuhimu wa kisiasa. Asili ya harakati hizi ni kanisa lililojitenga katika eneo hilo na ambazo zilianzishwa na Elliot Kamwana huko Kaskazini ya Nyasaland (Malawi Kaskazini) katika 1908. Kanisa hili lilijulikana kwa jina la Kitawala (Ufalme) au Kanisa la *Watch Tower* na katika Northern Rhodesia (Zambia) waluubiri wake waliozungumzia siku za furaha zijazo walitabiri kuanguka kwa ukoloni na mwisho wa dunia.

Maendeleo kama hayo yalitokea katika maeneo mengine ya Afrika pia, hususan kati ya miaka ya awali ya Vita Vikuu vya Kwanza. Simon Kimbangu alianzisha jumuiya yake ya *'Eglise de Jusus Christ sur la Terre par le Prohite Simo Kimbangu'* (EJCSK) katika mwaka 1921 huko Kongo ya Kibelgiji (Zaire). Wafuasi wake walianza kulipa kodi kwa utawala wa kikoloni wa Kibelgiji na walitangaza azma yao ya kutokubali kutumika katika ushokoa uliokuwa umewekwa na utawala huo. Kwa hiyo Simon Kimbangu alikamatwa na kufungwa jela hadi kufa kwake katika mwaka 1951. Lakini Ukimbangu uliendelea kuenea toka mahala ulipoanzia katika Mto wa Kongo ya Chini. Ukimbangumamboleo, *Mission des Noirs,* ulianzishwa na Simon-Pierre Mpadi ambao ulijulikana kama 'Khakista' ulienea toka Lower Congo hadi Kongo ya Kifaransa, na Oubangui Chari (Jamhuri ya Afrika ya Kati).

Harakati nyingine zilizofanana katika mielekeo yao na harakati iliyoanzishwa na Kimbangu na Mpadi zilikuwa zile zilizoanzishwa huko Uganda na askari mmojawapo wa zamani wa *King's African Rifles*, Ruben Sparts Mukara, ambaye alijitolea maisha yake katika juhudi ya kukomboa Afrika yote bila kujali ambalo lingempata. Jamii yake ya *African Progressive Association* na *Christian Army for the Salvation of Africa* pamoja na tawi la *African Orthodox Church)* ambalo alilianzisha yeye ilijumuisha malengo ya kisiasa na kijamii ya harakati hizo zote. Katika Nyasaland (Malawi), Kanisa la *Last Church of God and His Christ* la Jordan Nguma lilikuwa kama lile la Mukasa katika Uganda.

Makanisa mengine, yakifuata mwenendo wa Mageuzo, yalisisitiza sura fulani za itikadi za Kikristo ambazo zilipuuzwa na makanisa yaliyoanzishwa na misioni. Makanisa ya Kisayuni ya Afrika Kusini yalisisitiza umilikaji na Roho Mtakatifu, uponyaji na ubashiri na yalienea mahala pengi Kusini na Mashariki mwa Afrika. Dini ya Roho (Kanisa la Roho Mtakatifu), ambayo ilitokea miongoni mwa Abalyuya wa Kenya na ambayo ilianzishwa na Jakobo na Daniel Sande katika 1927, ilifanya ubatizo katika jina la Roho Mtakatifu, uzungumzaji wa lugha mbalimbali na uungamo wa madhambi kuwa ni masharti ya kupata uanachama kamili wa kanisa hilo. Msisitizo huo huo juu ya Roho Mtakatifu pia ulimfanya Alfayo Odongo kuanzisha kanisa lake la Joroho (Roho Mtakatifu) miongoni mwa Wajaluo wa Kenya katika mwaka 1932. Makanisa kadha ya Kiafrika na Aladura

katika Afrika Magharibi pia yalisisitiza umilikaji wa Roho Mtakatifu.

Makanisa mengine yalianzishwa kwa ajili ya wale ambao hawakuweza kutimiza masharti ya Kanisa la Kimisioni ya kuwa na mke mmoja tu na ambao walifukuzwa, pamoja na wale wasioweza kujiunga na kanisa kwa sababu walikwishaoa wake wengi. Mfano wa kanisa hilo ulikuwa *African National Church* ambalo lilisitawi katika wilaya ya Rungwe ya Tanganyika katika miaka ya 1930.

Ukristo wa Kienyeji

Mbali na makanisa haya, kundi lingine la makanisa pia lilijitokeza. Kundi hilo halikutokana na usariji wa wasiwasi au msongo katika jamii bali lilipata ilihamu kutoka itikadi iliyo chanya zaidi. Tangu siku za mwanzoni za Ukristo kuletwa kwa Waafrika baadhi ya wale walioongoka waliikubali itikadi mpya na kuivaa kwa kila hali. Kwa upande mwingine, baadhi yao waliukubali Ukristo lakini waliuelekeza katika dhana za msingi wa dini za kijadi za Kiafrika. Kwa maneno mengine, baadhi ya Wakristo wa Kiafrika walitumia baadhi ya jiha za Kikristo kuimarisha jiha za imani za kijadi zilizohitaji kuimarishwa, na papo hapo walitumia imani za jadi kuimarisha jiha za Kikristo zilizohitaji kujalizwa. Kwa hiyo, wakapata kile ambacho wao walikiamini kwa dhati kuwa ni dini halisi na Ukristo wao unaweza akaonekana kuwa ni njia ya Kiafrika ya kuwa na waumini. Hivyo ndiyo sababu tumeuita Ukristo wa Kienyeji, na tunaamini kuwa huu ni udhahirisho wa ubunifu wa kidini na upevu wa utamaduni, na wala siyo mrejeo tu, wala jibu au uhasibisho wa kichocheo kutoka nje, kama vile baadhi ya wanazuoni wanavyodai.

Katika makanisa hayo aina za ibada zinazotumika kukidhi mahitaji ya kiroho na kijaziba za wanachama, na kwa kufanya hivyo, huwezesha Ukristo, kama vile ifanyavyo dini ya jadi, kushughulikia kila eneo la maisha ya mwanadamu na kutimiza haja zote za kibinadamu. Miongoni mwa haja hizo ni uponyaji, ambao umuhimu wake katika dini ya jadi na Ukristo wa kienyeji ni mkubwa sana. Pamoja na uponyeshaji, mahitaji ya kidini ya uaguaji, ubashiri na ruya pia unatimilizwa, kwani kuna imani madhubuti ya kuwa Mungu kufunua mambo yajayo na kwa sababu za kuja kwa balaa, kwa njia ya ndoto. Wakati Makanisa yaliyoanzishwa na misioni hayaamini kuwa kuna nguvu za ubaya kama vile uchawi na usihiri, makanisa ya kienyeji yanaamini kuwapo kwa mambo haya na yanaamini kwa dhati kabisa kwamba Yesu Kristo anaweza kuwakinga dhidi ya nguvu hizo na kuwaponza pia.

Kutokea kwa makanisa haya ilikuwa ni fursa ya kuonyesha uwezo na uongozi wa Waafrika katika Ukristo, na ni katika makanisa hayo ndimo umedhihirisha Ukristo halisi wa Kiafrika. Maendeleo hayo ndiyo yaliyoanzisha theolojia ya Kiafrika ya Kikristo.

Mifano ya makanisa ya kienyeji ya Kikristo yaliyojitokeza katika kipindi cha ukoloni na ambayo bado yangali yanaendelea ni *Apostolwa Fe Dedefia Mabobo* (Jumuiya ya Ufunuo wa Kimitume) katika Gold Coast (Ghana); *Dini ya nsambwa* (Kanisa la Mababu) katika Kenya, na vile vile *Calici ca Makolo* (Kanisa la Mababu) katika Malawi, Kanisa la asili la *White Bird* (Ndege Mweupe) miongoni mwa Wazazura wa Zimbabwe; Kanisa la Kristo la Mwungano wa Wabantu na Ulinzi wa Desturi za Wabantu katika



20.2 Nabii M. Jehu-Appiah, Akaboha III Mjukuu na mrithi wa mwanzilishi wa Kanisa la Musama Dsco Christo (Ghana) akiwa amepanda machela wakati wa Sherehe za Amani za Kikanisa za kila mwaka.

Afrika Kusini;*Eglise Deo noirs* katika Kongo na Kanisa la Herero la Namibia.

*Mfano wa Kanisa la Musama Desco Christo*

Mfano mzuri wa makanisa haya ya kienyeji ya Kikristo ambao tungependa kuuzingatia kwa ufupi hapa ni kanisa la Musama Disco Christo la Gold Coast (Ghana). Mwanzilishi wa kanisa hilo, Mtume Jemesimiha Jehu-Appiah, alifanikiwa kuutumia Ukristo katika kuliunda upya kanisa kwa kufuata ruwaza ya Waakani na kuonyesha Ukristo kwa namna ambayo Waakani wanauelewa. Kanisa hili lilianza kama kundi la ibada, Chama cha Waumini, katika Kanisa la Methodisti huko Gomoa Oguan, katika Jimbo la Kati la Ghana katika mwaka 1919. Lakini kiongozi wake, Katekesta William Egyanka Appiah, na wafuasi wake walipofukuzwa toka kanisa rasmi, kundi hili likageuka kuwa kanisa kamili katika 1922.

Mwanzilishi wa kanisa hili hakuanzisha tu kanisa na kuwa kiongozi wake wa jumla wa kiroho, bali aliliunda kanisa hilo kwa kufuata mtindo wa muundo wa taifa la kijeshi la Waakani (Oman) pamoja na vyeo vyake. Kiongozi wa kanisa hilo ni Nana *Akaboha,* ambaye ana madaraka ya kiroho na kidunia na ambaye familia yake ni ya kifalme na kurithi kwa baba na wala siyo kwa mama kama ilivyo desturi hasa ya Waakani. Mke wa mwanzilishi, Nabii wa kike Natholomoa Jehu-Appiah, akawa *Akatitibi* (Mama-Malkia) wa kanisa, na hivyo Mfalme na Malkia wakawa waamuzi wa mwisho kaiika kanisa la Musama Disco Christo.

Makao makuu ya kanisa hilo, Mazano, ndiyo *ahenkro*, mji mkuu wa taifa la kijadi la Waakani. *Akaboba* (mfalme) huishi humo na maamuzi yote makuu yanayoathiri kanisa hufanyiwa humo na hapo ndipo sherehe ya kila mwaka, *Asomdwee Afe* (Sherehe ya Amani) hufanyika. Katika *Ahenkro* (mji mkuu), mna maziara na mahala patakatifu ambapo waumini husali na kupata maponyesho. Kanisa lina lugha yake yenyewe, *"Osor kasa"* (Lugha ya Mbinguni), ambayo hutumiwa katika salamu, maamkizi na kuingia majumbani, na majina yanayotumiwa kanisani pia ni ya lugha hiyo.

Kanisa hufuata mambo mengi ya kitamaduni na ya kidini ya Waakani katika kutafuta majibu ya kuridhisha ya masuala ya maisha ya wakati uliopo na kuchanganya sehemu za imani za Kimethodi na ufalme madhubuti wa Kiafrika. Kanisa hili huwakilisha upanuzi wa Ukristo katika Afrika maana limekitwa katika imani kuwa jamii ya Kikristo inaweza ikajengwa kwenye misingi ya utamaduni wa Kiafrika.

## *Hitimisho*

Kipindi cha utawala wa kikoloni katika Afrika tangu 1880 - 1935 hakikushuhudia uangamizo bali kilishuhudia uthibitisho wa wingi wa dini katika Afrika. Ukristo na Uislamu halisi pia ulienea badala ya Dini ya Jadi katika kipindi hiki kutokana na juhudi za baadhi ya watawala wa kikoloni. Hata hivyo, Dini ya Judi, ikiwa ndiyo dini mwenyeji, ilikuwa ndiyo msingi uliotegemea madhehebu mapya yaliyojitokeza. Kuwapo kwa dini nyingi kukaleta uadui, ushindani hata ukinzani katika sehemu nyingi za Afrika, lakini papo hapo kukatoa fursa ya kufanya mazungumzo kati ya dini mbalimbali.


# 21 Sanaa katika Afrika Wakati wa Utawala wa Kikoloni

Katika mtazamo wa sanaa kwa mujibu wa mabadiliko ya kijamii, kipindi tunachokichunguza kilishuhudia mabaki na hata kufufuliwa kwa amali za utamaduni mbele ya utawala wa kigeni na wa kinyonyaji katika Afrika. Mashambulio ya kivita yaliyofanywa na askari wa kikoloni na wamisionari kukosa kuelewa na kuvumilia, vilivuruga kabisa mwelekeo wa kiutamaduni uliozoewa katika bara hili. Upeo wa Uislamu ulikuwa wa aina ya pekee kwa dhati yake na uliacha athari kubwa ya utamaduni katika bara hili. Walakini ukweli tunaopata kutokana na kipindi hiki ni yale mabaki na hata uhuishwaji wa imani na amali za kweli za utamaduni wa watu wa Afrika.

## *Sanaa ya Kiafrika*

Ni vigumu kutathmini athari halisi ya biashara za kibeberu kwenye uzalishaji wa kisanaa. Aina nyingine za sanaa hazikuathirika, kwa mfano, mbinu ya "upakaji rangi wa shanga" ya wasanii wa Cameroon au sanaa ya uchongaji sanamu za kidini kati ya Wayoruba, Wabaule, Wabakota n.k. Hata hivyo, mabadiliko kidogo yalianza kuonekana katika aina nyingine za kisanaa katika fani na maudhui yake. Wakati ikiendelea kubakia na sehemu kubwa ya rangi yake, sanaa ya ukutani ya Mbari ya Waigbo (Nigeria) ilianza kuharibiwa kwa kuigwa ovyo na watu wa mijini kutokana na upatikanaji kwa wingi wa rangi za aina nyingi. Zamani, sanaa hizi za ukutani, zilitegemea usaili na uchache wa aina za rangi zilizotengenezwa na wenyeji wa mahali hapo.

Ufundi wa kienyeji haungeweza kulinganishwa na bidhaa zilizozalishwa viwandani na ambazo zilikwishaanza kujaa katika masoko ya Afrika hata mwanzoni mwa harakati za ukoloni. Hasara ya kutotangamanisha sanaa na maendeleo ya jamii ya kawaida, inaweza kuonekana katika kuanza kutoweka kwa sanaa ya *forowa* na *kuduo, tubakero* za kuwekea ugoro zilizotengenezwa kwa ufundi mkubwa, mafuta ya dawa n.k. za Waasante ambao nia yao ya urembaji kama ilivyo katika sehemu nyingi za Afrika, ilikuwa ni kuonyesha mifano kwa ajili ya mafunzo ya kijadi, methali, ushauri mwema, na matukio ya kihistoria. Uzalishaji wake, sasa ulichukuliwa na viwanda vya Uingereza ambavyo viliweza kufanya majaribio ya ziada ya kutumia aina mbalimbali za methali.



**21.1** *Vinyago vya miti kutoka ziara ya Kiyoruba ya mungu Shango*

## *Usanifu-majengo wa Kiafrika*

Ukiangalia kwa makini mpangilio wa nje na wa ndani wa baadhi ya nyumba za jadi zilizojengwa kwa pamoja katika uwanda, utaona jinsi ustadi wa usanifu-majengo wa watu wa Afrika ulivyo wa ajabu, mpangilio ulio tofauti kabisa na mpangilio wa kisasa wa kujenga nyumba katika mistari iliyopimwa ambao Waafrika kwa wakati huu walilazimishwa na Wabelgiji na Wafaransa kuiga katika mashamba ya watumwa. Usanifu majengo katika sehemu za mijini kwa wakati huo haukufuata miundo ya usanifu majengo wa jadi ila ulitokana na ujenzi uliofuata mistari na vipimo maalum. Hata hivyo, ni lazima tukiri kwamba kulikuwa na nyumba chache za kijadi zilizojengwa katikati ya miundo ya nyumba za kigeni ambazo zilikuwa ndefu kupita zote katika uwanda wote. Katika sehemu za katikati za miji mikuu ya Kongo (Zaire), Senegal, Ghana, Nigeria, Angola n.k. unaonekana nyumba ndefu katika maeneo ya jadi, yaliyozungukwa na majamba imara makubwa yaliyojengwa tangu karne ya kumi tisa iliyopita. Kwa kawaida, majengo haya huwa yamejengwa karibu na kisima cha pamoja. Mchango wa Wabrazili Waafrika waliorudi katika bara hili, ulikuwa ni mkubwa sana. Hata katika miji midogo ya bara la Afrika kuna mifano ya hapa na pale ambayo inaonyesha kusimama kwa maendeleo ya usanifu-majengo kuanzia kipindi hiki na ambavyo inaonyesha hali ya kupotea kwa ujuzi. Jiji lolote la kisasa katika Afrika, daima hutukumbusha kwamba mazingira yake ya zamani hayakubadilishwa kwa namna wenyeji walivyotaka bali kama wakoloni walivyopenda.

## *Muziki wa Kiafrika*

Muziki halisi wa Kiafrika unaendelea kutukumbusha, kwamba haukubadilika ingawa ulidhalilishwa sana. Hii haishangazi kwa sababu kwa Waafrika muziki una dhima ya kijamii. Hii ni kwa sababu ni kwa njia ya muziki, kuliko fani nyingine yoyote, ambapo utamaduni halisi wa watu hudumishwa kwa urahisi. Kwa mfano Wakikuyu wanapoimba na kucheza ngoma toka jua linapokuchwa hadi kunapokucha na kuingiza mfano wa mazishi ya mwanamke mkulima maarufu ambaye alichukuliwa kuwa ni mwanamke wa pekee katika kilimo cha mihogo, funzo tunalopata ni mwendelezo wa maisha na hata mifano ya kimatendo ya kudumisha uchumi wa wale walio hai.

Lakini muziki haukushughulikia mambo ya kisanaa ya mafumbo na umuhimu wake tu. Uhodari wa kusema, jambo ambalo linaandamana na muziki, siku zote umekuwa chombo kinachopendelewa cha mabadiliko rasmi katika jamii ikiwa ni pamoja na mipango ya kisiasa na utekelezaji wa haki. Dhima ya muziki katika mambo ya vita ni dhahiri kiasi kwamba haihitaji kusisitizwa. Hata hivyo muziki na usemaji katika mazingira rasmi ya miundo ya sheria kwa pamoja vinaweza kuchukuliwa kama ni sehemu nyingine ya utamaduni ambapo muziki haukujitenga na shughuli nyingine za kijamii, bali umetangamana nazo. Waidoma wa Kaskazini Mashariki ya Nigeria na Watusi wa Afrika ya Kati, walitumia mfumo wa kijadi wa kisheria ambazo ulitumia mtindo wa kutumia nusu ya waimbaji ya watu katika ukumbi mkubwa wa thieta.

Hoja nyingi zihusuzo muziki katika maisha ya Waafrika haziwezi kukanwa wala

kupuuzwa. Kwa mujibu wa mwimbaji wa kisasa wa Kishona:

> Kiasi kikubwa cha historia ya Mwafrika kimerithishwa kwa njia ya nyimbo. Unapopiga *mhira* na kuimba unaweza kuona picha za mandhari za siku zilizopita na maruerue ya ndoto za watu wa kale hutokeza katika wakati wa sasa. Unaweza kuwaona wahenga wakichechemea kuelekea tena ulimwengu hai .....

Yaliyoandikwa juu ya yeli katika jamii za Mali, Senegal, Gambia na Guinea, sio tu kama mtu mwenyewe kaleta mafundisho katika jamii, bali pia kama mwandishi, mwanahistoria na mwanautamaduni wa kijadi, yanaweza pia kusemwa kuhusu mwanamuziki wa Kishona ambaye ala yake, *mbira* (kipande cha mbao kilichochomekwa ndani ya kibuyu) ndiyo iliyoleta mshawasha wa maelezo yaliyonukuliwa hapo juu. Kutoka nyumbani kwa yeli huko Sndani magharibi kuelekea Kusini hadi Afrika ya Kati na Kusini, tunamkuta mwenzi wake na utenzi wa maisha yake katika kipindi cha fujo na misukosuko. Hata kwa sehemu ya Kusini ya Afrika yenye historia ya ujenzi wa himaya ulioandamana na vita, fujo na kunyanyaswa, miongo mitano ya karne iliyofuata, haikuwa ya amani kwa wakati wake na ilikuwa na matukio mengi ya utumiaji nguvu.

*Mbira*, haikuathirika vibaya na mfanyiko wa kutangua utamaduni; ama kwa hakika ilifaulu kuunda kifani cha utamaduni kati ya watu wake pamoja na uzingatiaji wa miundo yote ya kijamii ya dini na ya kidunia. Washona waliuchukulia kuwa kama zawadi kutoka kwa mzimu wao uitwao Chaminuka, ambao inaelekea alikuwa mtu hai, mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Muziki huu, akajipenyeza katika mazingira yote ya kijamiii kiasi kwamba ukawa kitu cha lazima katika shughuli mbalimbali za uponyaji, arusi, mazishi, kazi za mikono, uzazi, jando na unyago na katika matukio mengine ya kijamii.

Kinyume na aina nyingine za muziki wa kijamii katika Afrika, muziki wa *mbira* haukuwa muziki wa kifalme au wa watu bora, bali ulikuwa muziki wa jamii kwa ujumla, muziki wa umma. Kwamba wasanii wake walikuwa wakiheshimiwa sana katika jamii na kazi yao ilithaminiwa sana inaelezwa na ukweli kwamba wao walichukuliwa kuwa ni njia ya wananchi ya kuwasiliana na watu wengine wa ulimwengu. Aidha wao walifikika kwa urahisi, walikuwa wataalamu, na wakawa ishara ya umoja wa kimbari, katika kipindi cha fujo na mageuzi. Wasanii hao walikuwa wenye ujuzi wa hali ya juu kiasi kwamba ingawa ilitabiriwa tangu mwanzo kwamba wangefanyiwa ukutili, lakini hatimaye waliweza kuwavuta hata Wamisionari. Katika miaka ya 1920, ala za muziki wa *mbira* zilikwishaanza kuingia makanisani na kutumika katika uimbaji huko Rhodesia ya Kusini (Zambia). Majaribio ya nyimbo zilizokitwa kwenye sauti za *mbira* yalienea hadi kuingia katika sherehe muhimu za Wamisionari za misimu mbalimbali na watoto wa shule, sasa wakawa hawafukuzwi kwa sababu ya kukipiga chombo hiki "cha shetani" wakati wa michezo.

Hata hivyo nje na ndani ya mazingira ya kimisheni katika vituo vya dini, dhima ya muziki ya kuiunganisha jamii ilibaki kuwa ni alama muhimu ya utamaduni wa maisha katika bara hili. Kama chombo cha kiroho au cha burudani ya jamii, kama mwanahistoria au hata kama mburudisho mfalme yaani tabaka bora, mwanamuziki alikuwa na sifa muhimu ya amali za utamaduni.

## Sanaa za Maonyesho

Mara nyingi, sanaa za maonyesho zilikuwa ni mwendeleo au ufafanuzi wa sanaa za muziki; na kwa hakika ni vigumu kutenganisha hivi vitu viwili. Hata hivyo kwa kuwa sanaa za maonyesho katika pwani ya Afrika Magharibi, zilitokea katika karne ya kumi na tisa kutokana na athari za mwingiliano na mataifa ya nje, zinatoa kwa wazi zaidi, kuliko muziki, ushahidi wa mabadiliko kutokana na kuingiliwa na miundo ya Kiislamu na Uinjilisti wa Kikristo. Uinjilisti wa Kikristo ulihamasishwa na athari za watumwa huria katika Sierra Leone na Liberia ambao walileta namna mbalimbali za burudani za nchi walimokuwa, tabia za huko, amali za jamii, mavazi na mitindo ya usemaji.

Katika karne ya kumi na tisa yote, kulikuwapo vikundi vya sanaa za maonyesho katika Himaya ya Oyo ambayo ilikuwa ikilimwa na wafalme. Kuvunjika kwa himaya kulikotokana na kushambulia na Wafulani kutoka Kaskazini na uharibifu uliotokana na vita vya kiraia vya wenyewe kwa wenyewe, vilisababisha wasanii hawa hodari kutawanyika kuelekea kusini kupitia mipaka ya Dahomey na kutoweka katika sehemu yao ya asili. Waislamu, ambao walitokea kuwa wasliindi walipiga marufuku aina yoyote ya maonyesho na hasa yale yaliyohusu sherehe za wahenga. Kwa mujibu wa dini ya Kiislamu, matumizi na uabudu wa sanamu za binadamu katika sherehe hizo, ulikuwa mwiko. Wamisionari ambao walikwishaanza kuingia bara kutokea pwani walitimiliza kazi ambayo Waislamu walikwishaanza, siyo tu kwa kuwazuia wafuasi wao wasijihusishe na madhehebu mengine bali pia wasijihusishe na ala zozote zilizohusiana na sanaa za maonyesho. Kukawa na ombwe ambamo sasa utamaduni wa watumwa huria uliingia. Kadiri karne ilivyokaribia muongo wake wa tatu wa mwisho, pwani ya magharibi ilikuwa ikiathiriwa na ubunifu wa hawa watumwa huria wa Kikristo, waliokuwa na uhakika juu ya sanaa yao bora waliyoipata, wakiwa na hamu ya kutaka kuwahakikishia wakoloni weupe ambao sasa walikuwa wakitawala maisha yao kwamba mtu mweusi alikuwa na uwezo siyo tu wa kupokea bali hata wa kujifunza ile sanaa bora ya kizungu.

Fani mpya (za Kiulaya na Kimarekani) za utendaji wa sanaa za maonyesho zilizoanzishwa kwa wingi na wataalamu wageni katika Liberia, Senegal na Sierra Leone zilienea upande wa mashariki ambako zilipata kupenyezwa katika utamaduni wa ukanda huo. Burudani mchanganyiko zilizofanana na "Vaudeville" na muziki wa ukumbi zililzoetwa na "Watoka Nova Scotia", jina walilojiita watumwa huria wa Sierra Leone, zilifurahiwa na kuchezwa katika sehemu za ukanda wa pwani. Hata hivyo, fani hizi zilipoingia mashariki ya mbali ya nchi za Ghana, Dahemey na Nigeria zilileta mabadiliko katika fani na maudhui yake. Hatuongezi chumvi tunapodai kwamba ilipofika muongo wa kwanza wa karne ya ishirini, fani mpya kabisa ya sanaa za maonyesho, "maigizo", ilikuwa tayari imeshajipambanua katika Afrika Magharibi.

Vikundi vya taaluma mbalimbali viliundwa ili vifanye maonyesho ya utendaji ambayo yaliiga mtindo wa muziki wa "Victorian hall" au wa "American vaudeville". Makanisa yalitayarisha maonyesho yao, shule zilishiriki mashindano ya kupewa zawadi siku za maonyesho, siku ya kutembelewa na afisa wa wilaya, siku ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Malkia Victoria n.k. Wamisionari weusi hawakupenda kushindwa - mchungaji Ajayi

Crowther, alikuwa mfano unaojulikana, yeye alikuwa Askofu mweusi mashuhuri katika kuilea na kuitia moyo fani hii ya sanaa, ambapo mchungaji James Johnson aliligeuza kanisa maarufu la Breadruit la Lagos kuwa kichocheo cha kuonyesha sanaa za maonyesho. Watumwa huria wa Brazil waliongeza sauti za kigeni lakini bado sauti hizo zilikuwa ni za kawaida katika ladha yake, muziki wao ukiwa na mwangwi wa mahadhi ya kiasili ya Afrika Magharibi na Kongo. Siku za Krismasi na mwaka mpya katika karne iliyofuata, na katika muongo wa kwanza wa ishirini, zilishuhudia mitaa ya miji mikuu ya "Freetown" na "Lagos" kuona mwendeleo wa maadhimisho madogo ya kusherehekea kumbukumbu za mabaki ya sanaa za maonyesho zilizoonyeshwa zamani za Walatini, ambapo kati ha hizo "caretta", aina ya kejeli ficha ndiyo inaonekana kudumu kuliko zote.

Hata hivyo, utamaduni wa kitaifa ulikuwa, akiendelea kupinga uigaji wa fani zote zilizoingia. Kwa upande mwingine, sanaa za maonyesho za jadi zilihimili mashambulio siyo tu ya kuhifadhi fani yake bali pia akatazaji wa kugeuzwa kiakili kuingia katika mvutano dhidi ya utamaduni wa Kikristo. Kimsingi, msimamo huu uliweza kuathiri fani mpya ya sanaa za maonyesho iliyokwishaanza. Kwa upande mwingine, kutokana na kukubaliana na mambo yote ya utamaduni wa kibeberu wa Kikristo kama vile uzuiaji wa vifaa vya Kiafrika na uigaji wa mahadhi katika "Kanisa la Ulimwengu", kukatokea vyama vya mtawanyiko. Kuanzia mwaka 1882 hadi mwanzoni mwa miaka ya thelathini kama ilivyokwishagusiwa katika sura za mwanzo, vilitokea vikundi vingi vilivyojitenga, vingi vikiwa vimevuviwa na Roho, haja ya kumwabudu Mungu kulingana na kawaida za utamaduni wa mababu zao. Na hivyo kuanzishwa utaratibu wa kipekee wa kijadi katika Afrika Magharibi, hususani Lagos, ulioanza na nyimbo za tenzi na baadaye ulielekea kwenye uingizaji wa hadithi za biblia hadi ilipothibitika upekee wake katika hadithi za kawaida na katika maendeleo ya ufundi wa uigizaji michezo.

Wachezaji wa muziki mpya wa "vaudeville" walistawi sana. Majina ya vikundi kama vile "Bob wawili na msichana wao Carolina", huko Ghana vinatueleza jinsi mambo haya yalivyowaingia moyoni. Bwana Yalley, mwalimu wa shule, ndiye anayesemekana kuwa alianzisha mapokeo ya muziki wa aina ya "vaudeville" katika Ghana. Mwanafunzi wake Bob Johnson baadaye alimpita mwalimu wake na muziki wake "Axim Trio" na kuwa mtu maarufu katika utamaduni wa ukanda wa Ghana. Hadi kufikia katikati ya miaka ya thelathini hivi, Bob Johnson alikuwa amekwishajiimarisha kwa kiasi cha kuweza kueneza aina hii ya "Vaudeville" katika miji mingine ya Afrika Magharibi. Katika muongo huu, Afrika Magharibi iliweza kujigamba kwa kuwa na jumla ya maonyesho mengi ya aina mbalimbali za sanaa katika historia ya sanaa za maonyesho. Hata sinema, sanaa changa, ilikwishaacha alama zake katika sanaa za maonyesho za Afrika Magharibi .... Baadhi ya maigizo ya Bob Johnson yalikuwa ni matohozi ya Charlie Chaplin, yote haya yakiandamana na mavazi yake na sherehe zisizokuwa na mpangilio maalum.

Tena ipo dhihaka nyingine ya makusudi ya ukoloni. Wakati Bob Johnson alipokuwa akitayarisha safari yake ya kwanza ya kuzuru Afrika Magharibi, mwanaelimu mmoja wa Kizungu Charles Beart wa Senegal alikuwa ameanza kugeuza sera ya Kizungu ya utamadunikaji katika shule moja mashuhuri ya Senegal. Kikiwa ni Chuo kimoja maarufu cha ualimu, kilikuwa kikihudumia nchi za Kiafrika zitumiazo lugha ya Kifaransa

sawa na kilivyokuwa Chuo cha Achimota kwa nchi za magharibi zilizotuia lugha ya Kiingereza na Chuo cha Makerere katika Afrika Mashariki. Vyuo hivi vilikuwa vimekusudiwa kutoa elimu ya msingi ya kizungu kwa ajili ya watu ambao watakuwa walimu na watumishi wa serikali wa ngazi za chini. Mpango huo wa elimu ya utamadunikaji kama ulivyoingizwa katika mitaala ya Ecole William Pontry ulikuwa wa lazima kwa masomo ya Kifaransa. Michezo ya kuigiza ya Kifaransa, ushairi, muziki, sanaa, historia na sosiolojia. Hata hivyo, wakati wa uongozi wake Charles Beart, alianzisha maelekezo mapya ya wanafunzi kwa kuwashawishi kurudi kwenye jamii zao ili wapate mwelekeo wa kiutamaduni. Insha walizopewa zilitokana na ugunduzi wa wanafunzi wenyewe uliohusu fani na maudhui katika sanaa ya jadi. Vikundi kutoka kila jimbo la kikoloni vilivyowakilishwa katika William Pontry vilitazamiwa kurudi kutoka likizoni vikiwa vimejiimarisha katika utoaji wa maigizo yaliyotokana na tofauti zao, maelekezo yote yakiwa yameachwa katika mikono ya wanafunzi wenyewe.

Ingawa athari hii ya sanaa mpya ya maonyesho ilienea kwa wingi kupitia tabaka mbalimbali za kijamii za nchi za Kiafrika zitumiazo lugha ya Kifaransa na ingawa jaribio hili lilikuwa mafunzo ya sanaa hii mpya haikuonyesha maendeleo halisi ya utamaduni ulikotokea. Jumuiya iliyowakilishwa na William Pontry ilikuwa siyo halisi. Jumuia hiyo ilikuwa imejitenga mbali na ambayo utamaduni wake ilijaribu kuiga kifikra na kiutendaji. Hali hii kusema kweli haikuwa ya pekee kwa William Ponty tu bali pia katika shule na vyuo vilivyoanzishwa na wakoloni kwa madhumuni ya kutimiza malengo yao katika Afrika. Hivyo sanaa za maonyesho za William Ponty zilikuwa zikihudumia na kukidhi matakwa ya wageni wa jumuia ya koloni la Wafaransa isipokuwa ziliacha hali ya udadisi katika maisha ya jamii ingawa mwamko halisi wa watu kiutamaduni haukuguswa.

## *Mvuvumko wa maandishi katika Misri*

Katika maeneo yenye utamaduni wa kimaandishi, Misri na Magharibi ya Sudani, zinatupatia mifano kwanza ya mvuvumko wa maandishi na pili ya misaada ya pamoja iliyo dhahiri na isiyo dhahiri katika uingiaji wa utamaduni wa kigeni katika Afrika wakati wa kipindi cha ukoloni, kutokana hasa na kushindania.

Kutekwa kwa Misri na Bonaparta, mabadiliko yaliyofanywa na Muhammad 'Ali katika jeshi, nyanja za kijamii na kiuchumi na kule kupeleka tume ya elimu Ulaya, hususani Ufaransa na pia uanzishwaji wa shughuli za uchapishaji katika Bulaq mnamo mwaka 1822 vilisaidia kuleta mahusiano mapya na ya mwanzo kati ya nchi za Magharibi na nchi za Mashariki ya Kiislamu na hivyo kufungua kipindi kipya katika Misri. Huu mwanzo wa matayarisho ya mvuvumko wa maandishi katika Misri, uliharakishwa wakati wa himaya ya Khedive Ismail Pasha (1863-1879) na ulifikia kilele cha maendeleo kuanzia mwisho wa nusu ya karne ya kumi na tisa.

Mwanzo wa ustawi wa mazingira ya utamaduni wa kisasa wa Kiarabu kwa kiasi kikubwa ulileta na sababu kadha wa kadha. Sababu ya kwanza ilikuwa ni ile ya kuendelea kuhama kwa wingi kwa Wakristo wasomi wa Libano - Syria kama vile Faraha Anum (1874-1922), Yagub Sarruf (1852-1925) na Jurji Zaidan kuingia Misri kuanzia

miaka ya 1870 na kuendelea ambao walikuwa wakikimbia utawala msonge wa kidikteta wa Kituruki, huku wakiwa wamejaa mawazo waliyoiga kutoka nchi za magharibi kuhusu siasa, sayansi na fasihi. Sababu ya pili ilitokana na kuzuka kwa kikundi bora miongoni mwa Waislamu katika Misri, kilichokuwa kimejaa mawazo ya kisasa ya Kiislamu ya al-Aghani na Abduh. Sababu ya tatu, ilikuwa kurudi nyumbani Misri kwa wanazuoni waliokuwa wakisoma Ulaya wakiwa wamejifunza kozi mbalimbali za masomo zenye mwelekeo wa kijamii zilizotoa waandishi kadha wa kadha wenye hoja na nia mbalimbali. Sababu ya nne, inahusu maendeleo ya uchumi na mabadiliko ya mfumo wa nchi pamoja na uanzishwaji wa akademia mbalimbali, jamii zilizosoma, maktaba ya taifa (1870), vyuo vikuu vya kisasa, kuvifanyia marekebisho vile vilivyokuwepo (kwa mfano: al-Azhar) na uanzishaji wa mfumo wa elimu wa kisasa. Haya yote yalisababisha kuanzishwa kwa huduma za starehe kwa umma, elimu pamoja na nia ya kutaka kuunda hadhira na kisha mvuvumko halisi wa maandishi na uanazuoni. Hata hivyo, matokeo ya kazi za uandishi wa vitabu muhimu bado ulitegemea sana tafsiri za kazi za Wazungu zilizofanywa kabla ya kuanzishwa kwa nchi-lindwa ya Waingereza katika Misri na ambazo ziliendelea kustawi nchini mwao. Kazi hizi zilitoa nafasi ya kufanya mabadiliko na uigaji na hatimaye kufanya kazi za ubunifu.

Huku kuzindukana kwa kiutamaduni, kulikotolewa na mabadiliko ya hali ya kisiasa ya Misri mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, kulionyesha kwa kiasi kikubwa kukua kwa vyombo vya habari. Katika mwaka 1898, tayari kulikuwepo magazeti na majarida 169 na idadi hii iliongezeka hadi kufikia 282 katika mwaka 1913. Wakati wa utawala wa Mwiislamu mashuhuri na mrekebishaji, al-Afghani, utumiaji wa vyombo vya habari wa mara kwa mara ulionekana kama chombo cha kuelimishana kisiasa. Njia hii ya mawasiliano ilionekana kutumiwa sana na watu wa kizazi chote waliojua kusoma na kuandika wa kila hali hata na viongozi wasomi baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Hivyo, magazeti yalichukuliwa kama vyombo vya majaribio vya kupimia fani mpya za kusoma na kuandika kama vile katika hadithi fupi, michezo ya kuigiza n.k. Haja ya kutaka kujieleza na kufasiri dhana mpya za kigeni zilizoingia, ilileta mabadiliko ya "Kiarabu bora cha mapokeo".

Mabadiliko haya ya utamaduni nchini Misri chini ya utawala wa kigeni wakati wa kipindi hiki, yalileta mwamko mkubwa wa kisiasa ambao baadaye ulijitokeza katika harakati za mwanzo za utaifa.

## *Utamaduni wa maandishi katika Sudani Magharibi*

Inaonekana kwamba kimsingi wakati wa kipindi cha ukoloni kulikuwa na mkinzano wa kimaslahi katika Sudani Magharibi baina ya Wakoloni au Wazungu na Waislamu wakiwakilishwa na Wadyula. Hili kundi la pili liliingia katika nchi za Sudani Magharibi, likiwa na makusudi ya kufanya biashara; lilihamia katika miji ya Bob-Dioulasso, Kong, Bonduku, n.k. lilifuata njia ya biashara kutoka sehemu zenye dhahabu kama vile Ghana, Upper Volta na katika machimbo mengine katika ukanda wa tropiki unaoishia Sahara. Wadyula (jina linaloelezea kazi zao muhimu, biashara) walikuwa, pia wakishughulika na udumishaji na ukuzaji wa utamaduni wa Kiislamu na walisaidia kuwa kiungo cha Wamoori

na Waarabu kuingia katika ukanda wa mvua wa pwani ya magharibi.

Wakati tukikubali kwamba utamaduni wa maandishi wa Uislamu ulioingia katika sehemu za Afrika Magharibi ulikuwa kwa kiasi kikubwa haubadiliki, wenye ubalagha na wa kikasuku, wa njia ya kujifunza kwa kukariri kuliko ya utambuzi, maudhui yake yakiwa yamejikita zaidi kwenye ufafanuzi wa Uislamu na sheria (*hadithi* na *fikh*), kuendelea kwa mizunguko ya wanazuoni kati ya Pwani ya Magharibi na Afrika ya Kaskazini na Mashariki ya Kati hadi karne ya ishirini, na upatikanaji wa miswada muhimu iliyostawi bega kwa bega na mambo ya biashara ya Wadyula, vinathibitisha hali ya udadisi ya uanazuoni wa Kiarabu waliyokuwa nayo wafuasi wao wa Kiafrika. Maandishi ya kihistoria yanawiwa na wanazuoni wa Kiarabu kwa kiwango sawa na yanavyowiwa wenzao wasomi wa Kimagharibi waliohamia huku Kwa mfano uchunguzi wa maktaba za maalimu wa Pwani ya Magharibi, ambazo nyingi zilikuweko Ghana katika mwaka 1920, ulionyesha kuwepo kwa miswada ya historia, lugha (sarufi ya Kiarabu), ushairi, hisabati, mantiki, elimu ya sheria n.k.

Tumekwishaeleza juu ya mbinu zilizotumiwa na "wenyeji" dhidi ya njia zilizotumiwa na ukoloni wa kizungu wa kukashifu utamaduni wa Kiafrika; utamaduni wa Kiislamu kwa kutumia mafundisho ya imani ya Wadyula, nao ulipambana na upinzani uleule. Wakati mwingine, Wadyula, walijisilimisha katika utamaduni wa wenyeji wa mahali pale. Mifano ya kujisilimisha ya namna hii ilikuwa michache sana, lakini I. Wilks katika utafiti wake ametaja mfano mmoja wa Watagara wa Jirapa waishio kaskazini - magharibi ya Ghana. Mahali pengine ambao Waafrika walikuwa wakimiliki ardhi kwa njia zote mbili za kuonyesha mipaka na za utambikaji, Wadyula walijikuta wamesogezwa.

Sio waandishi wote wa Kimagharibi wa Afrika Magharibi wa wakati huo waliochukulia utamaduni wa Kiislamu kuwa unapingana na utamaduni halisi wa Kiafrika au kwamba utamaduni wa Kiislamu ulikuwa hauchangamani na amali za Kikristo ambazo zilikuwa zikienea kwa haraka kwa msaada wa vituo vya wamisionari vilivyoanzishwa na waumini weusi kandokando ya Niger Volta na Senegal. Kwa wanasosiolojia na wanaelimu kama vile Abbe Boillat (au mwenzi wake hodari mwanajeshi mwanazuoni, Paul Holle) lugha ya Kiarabu na utamaduni (wa Kiislamu) vilistahili vifundishwe katika vyuo vya juu vya Ufaransa ambako havingeacha athari za kuambukiza kwa Waafrika. Askofu Ajayi Crowether wa Nigeria, alikuwa tayari kutaka watu wafundishwe masomo hayo. Hii ingesaidia kutafsiri Biblia na Katekisimu katika Kiarabu ili kuendeleza masuala yote ya imani za Kiislamu katika jamii.

Mzaliwa wa Trinidad, Edward Blyden, aliyehamia na kuishi Liberia, aliamini kwa dhati kwamba utamaduni wa Kiislamu ulikuwa ndio utamaduni mkuu katika ulimwengu, ulifaa kwa tabia na kwa mazingira ya utamaduni wa Kiafrika. Kwake Uislamu ulikuwa ni kipengele kimoja tu - ingawa kipengele kikuu - katika kuleta mabadiliko ya utamaduni kwa ajili ya Waafrika, pamoja na kuzingatia mambo ya miundo na taasisi zao. Edward Blyden, aliamini sio katika mambo mengine ila katika kuleta marekebisho kamili ya elimu ya Kiafrika iliyotolewa kwa mtazamo wa Kiulaya ili ilingane na mwelekeo wa Kiafrika. Ustaarabu wa pamoja na maandishi yake ya kuvutia na kazi za kitaaluma ndivyo vilivyomvutia na kumsaidia Blyden kuweza kufanya kazi kubwa.

Lakini hayakuwa tu mambo ya historia ya kale yaliyofanya kuwa msingi wa kazi yake ya kupigania marekebisho ya utamaduni wa Kiafrika. Matukio ya sasa katika historia ya Afrika, upanuzi wa utamaduni wake na akili hata katika mazingira magumu ya "dunia mpya" yote haya yalimfanya Blyden avichunguze vitabu vya historia na kutangaza kwamba historia ya watu wa Ulaya kama vile Admiral Nelson iachiliwe mbali na badala yake ifundishwe historia ya mashujaa weusi kama vile Touissant L'Cuverture. Pia akapendekeza kianzishwe chuo kikuu katika Afrika Magharibi ambako masomo ya lugha ya Kiarabu na utamaduni yangepewa uzito wa pekee. Haikushangaza kuona kwamba chuo kikuu hicho hakikuanzishwa katika uhai wake, lakini, ushahidi tulio nao leo ni kwamba huyu mtumwa huria wa Afrika Magharibi aliyerudi akiwa amefanikiwa vema mapokeo ya Kimagharibi, aliharakisha kuvunjika uhodhi wa wamisionari wa Kikristo katika pwani ya Afrika Magharibi. Hii ni kwa sababu tarehe 2 Januari 1891, Blyden alitoa hotuba kwa umati mkubwa katika bwalo la kanisa la "Breadfruit" la Lagos na kusisitiza kwamba dini za Kizungu haziwezi kuchangamana pamoja na mapokeo ya Kiafrika katika jamii. Miezi michache iliyofuata, huko Lagos mfarakano wa kwanza ulitokea katika kanisa la "Orthodox" la "Breadfruit", na kusababisha "Kanisa la Umoja wa Wenyeji wa Kiafrika" kuanzishwa, ambalo kama tulivyokwishaeleza, lilizingatia maisha na udumishaji wa utamaduni wa Kiafrika kadri kanisa hili lilivyozidi kuenea upande wa Magharibi na Kaskazini ya Afrika Magharibi.

## *Fasihi katika Lugha za Ulaya*

Tunaweza kusema kuwa utamaduni ulioandikwa katika lugha za Ulaya huko Afrika Magharibi na Kati ndio iliyokuwa nguvu kubwa zaidi ya upinzani dhidi ya ukoloni. Fasihi simulizi iliendelea na dhima yake kama njia ya kuelezea dhihaka, michezo bubu, ngoma na mbinu mbalimbali fiche ili kuonyesha na kutoa ufafanuzi juu ya ukoloni. Lakini ni kutokana na fasihi iliyoandikwa kwa lugha za kikoloni katika fani za uandishi wa habari na katika ushairi, michezo ya kuigiza na riwaya ndipo ukapatikana mwamko wa mawazo juu ya maandishi dhidi ya ukoloni. Katika pwani ya Aftika Magharibi, kuanzia Liberia hadi Lagos, viwanda vya uchapishaji vitabu viliongeza uzalishaji wake hadi kufikia kiwango ambacho kililingana na kile cha Uingereza katika karne ya kumi na nane. Hali hiyo pia ilijitokeza Kenya ingawa kwa upande huu wa Afrika Mashariki, shughuli hizi zilikuwa zaidi katika jamii ya Wahindi. Vijitabu vidogovidogo vilivyochapishwa kwa gharama ndogo, vilisambazwa kwa urahisi na vilishambulia kwa nguvu utawala wa kigeni, unyonyaji, matendo ya udanganyifu yaliyofanywa na utawala wa kikoloni na kule kuzidi kujiingiza katika maisha ya watu na haiba zao. Koloni la Luanda la Wareno lilipata kiwanda chake cha kwanza cha uchapishaji mnamo mwaka 1841; huo ulikuwa ndio mwanzo wa uandishi wa habari wa kuchochea maendeleo ya Waafrika. Kilikuwa kipindi kilichojulikana kwa mwamko wa mtindo wake - hata kama lugha iliyotumiwa ilikuwa ya kikoloni. Lawama zinazotolewa na wabaguzi wa rangi dhidi ya ukoloni wa Kifaransa kutoka kwa Ahmadou Dugay Cledor wa Senegal zinaonyesha kwamba upo ushahidi wa maneno unaokinzana na mambo ya jadi. Rufaa zilizopelekwa katika ofisi ya mambo ya

ndani ya Uingereza, zilichukuliwa kuwa ni maandishi ya kisanaa, ambayo yalifanywa kuwa mambo ya kujifunza katika ofisi za kibalozi.

Casely-Hayford pia alichapisha riwaya yake iitwayo, *Ethiopia Unbound* mnamo mwaka 1911 ikiwa ni mojawapo ya riwaya za zamani za Afrika zilizojaribu kuchanganya mitindo ya uandishi, kuanzia ile iliyochoma hisia za wasomaji hadi ya upelelezi na mashtaka dhidi ya uchoyo na majivuno ya rangi yaliyofikia kiwango cha kuingiwa Afrika na kuleta ukoloni. Maandishi ya Casely-Hayford, wakati wote wa maisha yake yalitoa tahadhari juu ya madhara ambayo yangetokea katika bara la watu weusi, endapo wangekataa kutawaliwa. Riwaya ya *Ethiopia Unbound* haikuweza kupata wuandishi waigaji katika kipindi hiki na ilibakia kuwa ni riwaya ya pekee ya tabaka lake. Kinyume na watu kama Casley-Hayford kulikuwapo pia wanazuoni mashuhuri katika Afrika waliokuwa na mtazamo tofauti wa mwanzo, kwa mfano Askofu Ajayi Crowther wa Nigeria na Bakary Dialo wa Senegal. Wao kama Padre Boilat, waliutetea ukoloni wa kizungu kwa kudai kwamba ulikuwa mzuri na wa kusifiwa katika Afrika. Crowther, mwanatheolojia wa kiprotestanti, alichunguza kwa makini asili ya hofu zake za kipagani na zile za kijamii na kuona kwamba Ukristo umewakilisha kwa namna ya pekee mawazo ya kale, yaani ya Mungu, kwa ajili ya kuleta uzima wa milele kwa bara lisilomjua Mungu. Bakary Dialo yeye ameelemewa sana na utamaduni wa Kifaransa. Lakini kwa wapinzani wakali wa ukoloni, waliharibu waziwazi hususani utamaduni wa Kizungu kama ulivyoigwa na jamii yao na watu kuelimishwa zaidi kwa njia ya maandishi. Tanzia la mshairi mmoja maarufu, Jean-Joseph Rabearivelo wa Madagascar (?? - 1937) aliyejiua mwenyewe kulokana na kile alichokiita kushindwa kuvumilia migongano ya ndani dhidi yake na ukoloni, ni mfano dhahiri wa jambo hili. Hii ilifanya ubora wa maandishi ya Waafrika katika kipindi cha mwanzo cha ukoloni yaonekane kuwa ya kutatanisha. Kwa mfano, maandishi mengine yalisaidia kuendeleza sera ya usilimishwaji ya utamaduni, hususani ule wa Kifaransa, Kireno na Kihispania, na matokeo yake yakiwa ni kutangua na hata kukanusha chimbuko la utamaduni halisi wa Kiafrika ulioelezwa na kikundi cha watu bora.

Tofauti hizi kwa mfano zilionekana zaidi katika makazi ya walowezi ambapo sera ya "uasimilando" ilibadilishwa na kuwa ya sanaa ya kisiasa ya washairi kama vile Silverio Ferriera, Antonio Jose de Nascinento, na Francisco Castelbranco ambaye ushairi wake kuanzia mwanzoni wa karne hii ulipinga maonevu ya nguvu yaliyofanywa na walowezi. Lakini wakati huohuo, huko Angola na katika makoloni mengine ya Wareno (kama ilivyo katika makoloni yote), majibu ya kukwepa ukweli wa maisha dhidi ya udhalilishaji yalijitokeza. Mfano mmoja ni wa mshairi aitwaye Caetano da Costa Alegre (Sao Tome) ambaye mashairi yake ya mapenzi ya kusifia uzuri wa mwanamke mweusi yalichapishwa baada ya kifo chake. Ushauri wake ulifanywa kuwa msingi wa mawazo ya watu weusi ya kuanza kujithamini, mashairi ambayo yalikuwa yakisherehekewa katika harakati za ukombozi zilizoitwa*negritude* (Unegro).

Wasanii wakuu wa Negritude walikuwa: Aime Cesaire (Martinique), Leopold Senghor (Senegal), na Leon Damas (French Guyana); chanzo chake kilikuwa ni Ufaransa. *Negritude* ilitoa mashairi mengi mazuri ya kusifiwa, lakini yote hayakuwa mashairi ya "kipropaganda" kwa maana ya *da Costa Alegre* bali yalikuwa mashairi ambayo yalitokana

na mwongezeko wa mwamko wa hali halisi ya Kiafrika. Kwa kifupi, haya yalikuwa maasi dhidi ya ushindi wa utamadunishaji katika ukoloni wa Kifaransa na Kireno. Hata hivyo, mwanzo wa harakati za "negritude" zinatokana na "manifesto" katika toleo moja la jarida la *Legitime Defense*, lililochapishwa na wanachuo watatu wa kutoka Martinique. Katika manifesto hii, wanachuo walikataa kufuata utamaduni wa kizungu, pia walikataa kuamini mambo kadha wa kadha ya kizungu yaliyopotosha haiba ya mtu mweusi.

Harakati za *negritude* ambazo ndizo zinazomalizia kipindi ambacho tumekuwa tukijadili, ziliendelea kuwepo na kuimarika katika miongo iliyofuata, na hii siyo tu miongoni mwa waandishi na wanazuoni wa kikoloni wa nchi zitumiazo Kifaransa bali kwa nchi zitumiazo Kireno na hata Kiingereza. Wapinzani wakuu wa *negritude* wa sasa, ni wale wa mtazamo wa Marx ambao hushikilia hoja kwamba historia haipatani na misingi ya *negritude* na ambao baadhi yao ni viongozi wa Afrika waliosaidia kuipa *negritude* nguvu mpya katika mapambano yao dhidi ya sera za Kireno na usilimishwaji mwanzoni mwa miaka ya hamsini. Hivyo, ni sahihi kudai kwamba *negritude* ni suala la kihistoria ambalo lililetwa na hali ya mambo ya wakati huo, lakini kwa sasa *negritude* imepoteza mashiko yake kwa sababu hali iliyolazimisha kuwepo kwa *negritude*, sasa haipo, jamii sasa inakabiliwa na masuala tofauti, yanayohitaji uchanganuzi na mbinu za kimapinduzi.

# 22

# *Siasa na Utaifa wa Kiafrika: 1919 - 1935*

Kama kile kipindi cha kati ya mwaka 1880 na 1919 kilionyesha ukinzani wa Mwafrika dhidi ya kuwako kwa utawala wa kikoloni, kile cha kuanzia mwaka 1919 hadi 1935 kilidhihirisha mwamko wa utaifa wa Kiafrika. Kwanza lazima tutofautishe baina ya utaifa uliokuwako huko Ulaya kuanzia karne ya kumi na tisa na ule uliokuwako katika Afrika ya wakoloni katika kipindi baina ya Vita Vikuu vya Kwanza na vya Pili. Utaifa huko Ulaya ulidhihirishwa na shauku ya jamii zenye utamaduni uliofanana na zilizochangia historia ya namna moja na ambazo zilitaka kutambuliwa kama dola (serikali) zilizojitegemea zenyewe. Jitihada zilikuwa na kusudi la kuhakikisha kwamba taifa la kiutamaduni na dola vilikuwa kitu kimoja. Kama mifano ya Ugiriki, Italia na Ujerumani inavyoonyesha, vyama vya utaifa kwa kawaida vilisababisha kuanzishwa kwa nchi zenye serikali zake zenyewe.

Walakini, katika Afrika, makoloni mengi yaliyoanzishwa yalikuwa yamekusanya vikundi kadhaa vya watu ambao hawakuwa na utamaduni, utaifa wala historia ya namna moja, vikundi ambavyo kitu pekee kilichoviunganisha ni ile hali ya kutawaliwa na wageni. Kwa hiyo, utaifa katika Afrika ulijidhihirisha katika ile shauku ya jamii hizi mbalimbali au mataifa ya kiutamaduni kujenga utambulisho mpya ambao ungewasaidia sana katika mapambano yao dhidi ya ukatili na kasoro za tawala za kikoloni. Jamii hizi pia zilianza kuviona vile vituo vya tawala za kikoloni kama serikali za awali ambazo jamii hizo zingetumia katika kujenga moyo wa umoja. Tofauti nyingine ya kushangaza ni kwamba mielekeo ya viongozi wa Kiafrika wa tabaka bora kwa kiasi fulani iliathiriwa na muundo wa utawala wa kikoloni.

Kule ambako utawala wa kikoloni ulichukulia muundo na/au sera ya kikanda, kama ilivyokuwa katika makoloni-muungano ya Kifaransa, viongozi wa Kiafrika nao walizingatia mkabala huohuo wa kikanda. Kwa hiyo, waanzilishi wa utaifa wa Kiafrika katika kipindi kati ya Vita Kuu wameitwa Wana-Umoja wa Afrika zaidi kuliko Wana-Utaifa kama unavyoeleweka huko Ulaya. Ina maana kwamba utaifa ulikuwa unachukua sura iliyo kinyume na jinsi dhana hiyo ilivyokuwa ikichukuliwa huko Ulaya. Kinyume na jinsi mambo yalivyotokea kule Ulaya, dola iliundwa kabla ya yale mataifa kiutamaduni ambayo yangeijenga hayajaunganika kuwa jamii moja yenye siasa inayokubalika na kila mwananchi. Ya kwamba Waafrika walioishi katika makoloni haya yaliyowekewa mipaka ya bandia na watawala wa kikoloni waliweza kujiona kama taifa lenye utambulisho mmoja isitushangaze kwani tabia hiyo ilikuwa matokeo ya kule kutawaliwa kwenyewe. Awali ya yote, ukoloni uliweka mfumo wa kigeni wa amali, kanuni na fafanuzi za maendeleo ya

kisiasa na kijamii, mfumo ambao umejengwa katika hali ya kutokuwa na usawa kutokana na ubaguzi wa rangi ambao nao unatokana na ubaguzi wa jumla unaotokana na madai kwamba utamaduni wa Mwafrika mtawaliwa ulikuwa duni. Kwa hivyo, hali kama hii ilisababisha manung'uniko na ukinzani. Kwa hiyo si ajabu kuona kwamba kitu cha msingi kilichosababisha uibukaji wa utaifa wa Kiafrika ni ule utambuzi wa kubaguliwa, papohapo mojawapo ya shughuli za msingi katika utaifa na siasa ya Kiafrika katika kipindi kati ya vita vikuu viwili ilikuwa uhuishaji wa utamaduni.

Pili, ukoloni wa ujumla huhitaji msingi wa jamii ili uweze kudumu. Jambo hili hufanyika kwa kuanzisha kikundi kipya cha wasomi miongoni mwa jamii iliyotawaliwa ambao huathiriwa sana na utamaduni wa kikoloni kwa kupitia mfumo wa elimu. Lakini, mwingilio huu wa utamaduni wa kigeni siyo tu kwamba hutangamanisha tamaduni tofauti, bali hata migongano ya kitamaduni huweza kutokea na ikajibainisha kwa mikabala mikali kutoka kwa watawaliwa. Licha ya hayo, kila mara kuna tatizo la migongano ya kimaslahi kati ya mkoloni na mtawaliwa, mkoloni akikazania kuendeleza utawala wake, na mtawaliwa akikazana kujitimiliza ama kwa kujiweka sawa katika mfumo wa kikoloni uliopo au kwa kutaka kujikomboa ili ajipatie tena uhuru na mamlaka yake.

Kama vile Crowder alivyodadisi hapo juu, Vita Vikuu vya Kwanza viliamsha matumaini ya tabaka bora la wasomi waliokuwa wakiinukia popote katika bara la Afrika kwamba wadhifa mkubwa ulikuwa unawasubiri, na kwamba wangeingizwa na kupokelewa kama wenzi wa watawala wa kikoloni. Walakini matumaini haya yalikatishwa tamaa taratibu baada ya vita. Hata katika zile sehemu ambazo Waafrika waliosoma walipatiwa kazi, siyo tu kwamba walijikuta wamepatiwa kazi duni akilinganisha na Wazungu wenye mafunzo na uzoefu kama wao, na ambao walifanyakazi pamoja nao katika utawala uleule wa kikoloni, bali pia waliwekwa nyuma katika masuala ya kijamii. Mambo haya yalisababisha chuki, uchungu na kutafuta mbinu dhidi ya tawala za kikoloni. Aidha, kama Betts alivyoonyesha hapo juu, kwa sababu za kiuchumi na za kiutendaji bora wa kazi, tawala za kikoloni zilitumia taasisi za kijadi na viongozi wa tabaka bora kwa namna mbalimbali ili kurahisisha udhibiti wao kwa watawaliwa. Ama kwa hakika walipokuwa wanatafuta watumishi wa namna hii, maofisa wa kikoloni daima waliwatena watu wapya ambao wangeelewana nao na kuwatumia.

Hivi ndivyo walivyoanzishwa 'machifu wateule' huko Kusini Mashariki mwa Nigeria, mamlaka za wenyeji miongoni mwa Wamasai nchini Tanganyika na katika sehemu nyingine za Uganda nje ya Buganda, na pia wengi wa wale walioitwa *"chefs de paille"* (machifu wa mashina) chini ya utawala wa Wafaransa, Wabelgiji na Wareno. Hata hivyo, watu hawa wa tabaka bora walioajiriwa ili waendeleze utawala wa kikoloni hawakutendewa vema zaidi kuliko Waafrika wengine waliojipatia elimu yao katika mfumo wa kikoloni. Kama lilivyojikuta lile tabaka jipya bora la wasomi, watawala wa jadi nao walijikuta hawana pa kushika. Baada ya kupoteza hadhi na dhima zao za jadi machoni pa watu wao, mabwana wa kikoloni mara nyingi waliwatumia kama vyombo vya kudhibitia utawala wao na wala siyo kama washiriki halisi. Upotezaji wa uwezo kamili, hadhi na wadhifa katika jamii uliwanung'unisha wengi miongoni mwao. Isitoshe, kama

tutakavyoona baadaye, watawala hawa wa kikoloni kwa kawaida walijaribu kulipambanisha tabaka bora la jadi na tabaka bora la wasomi, na mara nyingi watawala hao walijifanya kama walinzi wa uongozi na mfumo wa serikali ya kijadi. Katika hali kama hiyo, kila moja ya makundi hayo mawili halikuridhishwa na tawala za kikoloni.

Ukoloni haukuathiri tabaka bora la wasomi na watawala wa jadi tu. Kuutazama utaifa wa Kiafrika katika kipindi kati ya vile Vita Vikuu Viwili kama jambo la watu wa tabaka bora na wakazi wa mijini tu, kama ambavyo imechukuliwa hadi sasa, ni makosa. Uchunguzi wa hivi karibuni unazidi kuonyesha kuwa chuki na uchungu mwingi dhidi ya ukoloni viliibaka miongoni mwa umma na hasa katika sehemu za vijijini kutokana na hatua mpya za kifedha na kiuchumi, mfumo mpya wa kulinda haki, na zaidi ya hayo yote, mpomoko wa kiuchumi katika miaka ya 1930. Mambo yote haya yamekwishajadiliwa tayari, na hapana shaka yalisababisha chaki nyingi na hisia za kugandamizwa siyo tu katika sehemu za mijini bali hata kule vijijini ambako vyama vya utaifa vilianzia.

Jambo jingine lililosababisha hasira nyingi na hali ya kukatishwa tamaa ni kupuuzwa kwa elimu. Kwa kuwa tawala za Kizungu zilikazania zaidi kuyafanya makoloni yalipie gharama za utawala na huduma mbalimbali, juhudi kidogo sana ilifanywa katika kueneza elimu ya kimagharibi. Katika kipindi kati ya vita vikuu viwili katika maeneo mengi ya Afrika ya mkoloni shule za msingi zilikuwa chache na za mbalimbali, na elimu ya sekondari ilikuwa haba sana. Katika Afrika ya Kati ya Waingereza, Afrika ya Ikweta ya Wafaransa, na nchi zilizotawaliwa na Mreno yaani Angola, Msumbiji na Guinea hapakuwa na uwezekano wa kwenda katika shule ya sekondari kabla ya Vita Vikuu vya Pili. Jaribio hili la kijumla la kubana aina na kiwango cha elimu lilisababishwa na woga kwamba elimu ya Kizungu pamoja na mawazo ya kisiasa na kijamii vingeubomoa ukoloni kama mfumo wa mahusiano. Woga huu ndio uliosababisha kukataliwa kwa masomo ya sayansi za jamii katika viwango vyote, na kupendelewa kwa shule za vijijini, shule za ufundi, na vyuo vya mchepuo wa ufundi baada ya elimu ya sekondari, ambavyo vingetoa watumishi wa ngazi za kati, lakini siyo vyuo vikuu. Lengo lilikuwa kuepukana na hali kama iliyotokea India ambako uenezaji wa elimu ya fani za jamii ulikuwa nyenzo kuu katika upanuaji wa siasa ya kitaifa iliyopingana na ukoloni. Hali hii ndiyo inayoelezea mwelekeo na kiwango cha masomo katika vyuo kama vile Chuo cha William Ponty katika Afrika Magharibi ya Wafaransa, Chuo cha Juu cha Yaba (Nigeria), Chuo cha Achimota (Ghana), Chuo cha Gordon (Sudani) na Chuo cha Makerere katika Afrika Mashariki ya Waingereza. Walakini, jaribio la kufinya kiasi na aina ya mabadiliko ya jamii ambayo yalitegemewa yatokee katika makoloni nalo lilikuwa chanzo cha manung'uniko dhidi ya ukoloni ambayo yalisababisha vyama vya utaifa.

Sababu ya mwisho ya ndani iliyoibusha na kukuza utaifa wa Kiafrika, hasa katika miaka ya thelathini katikati, ilikuwa vita kati ya Ethiopia na Italia vilivyoanza katika mwaka 1935, na ambavyo kwavyo Ethiopia ikatawaliwa na Italia. Matukio makuu haya ya kimataifa yalitonesha zaidi na zaidi zile hisia za mkengeuko miongoni mwa watawaliwa, hasa wale walioelimika, dhidi ya tawala za kikoloni. Kiini cha uvamizi wa Waitaliani, na ufashisti na unazi kwa ujumla kinasisitiza hali ya kibaguzi ya ukoloni katika Afrika. Wale

walioweka matumaini yao katika Umoja wa Mataifa walisikitishwa vibaya mno. Ile shauku ya kulinda fahari ya Mwafrika iliyokwisha jeruhiwa inaelezea kidogo vuvumko la mawazo na itikadi za Uafrika kama vile Unegritudi katika wakati huo. Vuvumko hilo pia lilidhihirishwa na kuanzishwa kwa mashirika ya kimataifa yaliyokuwa yanatetea uhuru wa Ethiopia, nchi iliyoashiria tumaini la Mwafrika aliyesoma kwamba siku moja angekuwa huru.

Vuguvugu la utaifa wa Kiafrika halikuanza na kusonga mbele kutokana na fedheha ya kutawaliwa na wakoloni tu. Walipokuwa wanayafuatilia matumaini yao, wafuasi wa utaifa wa Kiafrika walisaidiwa na matukio ya maendeleo vilivyokuwa vinatokea katika mataifa mengine. Matukio hayo ni kama vile athari ya Vita Vikuu vya Kwanza vilivyotajwa na kujadiliwa katika Sura ya 12 na ile nia ya Umoja wa Mataifa ya kuyaangalia maendeleo ya nchi zilizotawaliwa na wakoloni kuwa ndilo lengo kuu la ukoloni, na lengo hilo liwe ndicho kigezo cha kuamulia utendaji kazi wa mabwana wa kibeberu hasa katika zile nchi zilizodhaminiwa. Uingizaji wa dhana ya uwajibikaji kwenye jamii ya kimataifa mintarafu ya nchi zilizodhaminiwa uliwapa tumaini baadhi ya wafuasi wa utaifa. Kwa upande wa siasa, vyama vya kiitikadi vya kimataifa kama vile chama cha Lenin kilichopingana na ubeberu kilichojulikana kama *Communist International (Comintern)* na vyama vingine vya kijamaa, ukiongezea na ule mchapuko wa kuelekea kwenye uhuru katika mabara mengine ya dunia, vyote hivi viliwapa motisha wanautaifa wa Kiafrika Aidha mawazo ya Uafrika wote unaopingana na ubeberu, mawazo ambayo yalitokana na akina Sylvester Williams, Marcus Garvey, William Du Bois na Wamarekani na Wakaribeani wenye asili ya Kiafrika, nayo pia yalitoa athari ambazo zitajadiliwa baadaye.

Mkutano wa kimataifa ulioitishwa chini ya usimamizi wa Comintern kule Brussels mwezi Februari mwaka 1917 ulileteleza kuanzishwa kwa Umoja dhidi ya Ubeberu na kwa ajili ya Uhuru wa Kimataifa (ambao ulijulikana tu kwa jina la *League Against Imperialism* (Umoja dhidi ya Ubeberu). Mkutano huo ulihudhuriwa na wajumbe wapatao 180 kutoka Ulaya Magharibi, Amerika ya Kaskazini, ya Kati na ya Kusini, Visiwa vya Karibeani, Asia na Afrika. Mkutano huo uliwakutanisha Wakomunisti, makundi ya kijamaa ya mrengo wa kushoto kama vile. *Independent Labour Party (*Chama Huru cha Wafanyakazi kilichowakilishwa na katibu wake Mkuu Fenner Brockway (baadaye akawa Lord Brockway), wasomi-wajamaa wa kimapinduzi na wawakilishi wa vyama vya kitaifa katika nchi zilizotawaliwa na wakoloni. Walioshiriki kutoka Afrika miongoni mwao walikuwamo Messali Hadj na Hadjali Abdel-Kader (Magharibi); Mohamed Hafiz Bey Ramadan na Ibrahim Youssef (Misri); Lamine Senghor (Afrika Magharibi ya Wafaransa); Jomo Kenyatta (Kenya); na pia J.T. Cumede na I.A. La Guma (Afrika ya Kusini). Wanachama wa *Inter-Colonial Union* kama vile Max Bloncoux nao pia waliwakilishwa; na Carlos Deambrsis Martins kutoka Haiti pia alihudhuria.

Pia viliwakilishwa vyama vilivyoshughulika na kutetea haki za binadamu na uraia na vile vyama vilivyokuwa vinapinga utumwa ambavyo vilikuwa na matawi huko Ulaya na ndani ya makoloni mengi ya Afrika. Vyama vilivyochimbukia Amerika, kama vile

*Universal Negro Improvement Association* (Chama cha Kumwendeleza Mtu Mweusi Ulimwenguni) cha Marcus Garvey kilichoanzishwa kwa mara ya kwanza katika mwaka 1917 kilikuwa na sauti katika makoloni mengi barani Afrika.

## *Jinsi Utaifa na Siasa za Kiafrika Zilivyojieleza*

Ijapokuwa mazingira ya kikoloni na yale ya kimataifa yalifanana kwa kiasi kikubwa, utaifa na siasa ya Kiafrika vyote vikielezwa kwa ufupi na neno la Kiswahili Siasa, vilijibainisha kwa namna tofauti toka mahali hadi mahali hata katika zile nchi zilizotawaliwa na beberu yuleyule. Mambo yaliyotawala muundo na kiasi cha *pilikapilika za wafuasi* wa *utaifa* (wanasiasa) katika makoloni yalitegemea aina ya uongozi, tofauti za mweneo na kiwango cha athari za kizungu kwa njia ya mawazo na kutumia mashirika; idadi na umuhimu wa walowezi (weupe), na mwisho kabisa tabia na itikadi za kikoloni.

Karibu kila mahali, vyama vya utaifa na shughuli za kisiasa katika wakati huo wa ukoloni viliongozwa na kushikiliwa na tabaka bora jipya la wasomi wa elimu ya Kimagharibi na ambao walikuwa wamekwishaelewa barabara utamaduni wa kisiasa wa *Kizungu, na kwa hiyo waliweza kuusaili vilivyo utawala wa kikoloni. Wakati mwingine* walishirikiana bega kwa bega na tabaka bora la 'jadi' japokuwa palikuwa na suitafahamu baina yao. Ushirikiano wa namna hii ulijidhihirisha katika nchi kama vile Gold Coast (Ghana) katika Chama cha *Aborgines' Rights Protection Society* (Chama cha Kulinda Haki za Wenyeji wa Asili). Nigeria ya Kusini, Moroko, miongoni mwa Wakikuyu wa Kenya. Wakati mwingine, uongozi ulibaki mikononi mwa walio bora wa 'jadi' kama vile nchini Libya na Moroko. Lakini basi, mara nyingi, kwa vile wale waliowakilisha au walioteuliwa kuwakilisha viongozi wa tabaka bora wa jadi walipendelewa na watawala wa kikoloni kutokana na kutumiwa kwao kama vyombo vya kudhibitia, mwelekeo ukawa ni kuwasema wale wa tabaka bora la jadi kuwa ni waendelezaji wa ukoloni katika kuueleza ukoloni; na kwa hiyo wakashambuliwa sana kwa sababu hiyo, kama ilivyokwisha elezwa hapo juu.

Kuongezeka kwa tofauti za athari za Kizungu kimawazo na taasisi pia ziliathiri majibu ya Wafaransa. Waafrika walioishi katika maeneo yaliyohusishwa sana na elimu ya Kizungu walikuwa wamejiandaa kikamilifu na walikuwa tayari kukitumia kihunzi cha Kizungu cha maendeleo ya kisiasa na kijamii. Kwa hiyo, Waafrika hao walipendelea kutumia mbinu za kikatiba katika uhamasisho wa kuleta badiliko lolote lililotakiwa. Kuwapo kwa nafasi ya kufanya hivyo katika mabaraza ya kutunga sheria katika nyakati za ukoloni kulikuwa motisha.

Katika nchi kama vile Misri na Sudani iliyotawaliwa na Misri chini ya Waingereza, (*Anglo-Egyptian Sudan*), Algeria (hasa katika wilaya za Algiers, Constantine, na Oran), Moroko na Tunisia, na sehemu za mwambao wa pwani katika Afrika Magharibi ya Waingereza na Wafaransa, shughuli za Waafrika zilifuata mbinu za kikatiba, na matumizi ya nguvu za kisiasa zilizolingana na mkabala wa kisiasa utumikao Ulaya Magharibi. Sababu mojawapo ni kwamba wafuasi wa utaifa wa Kiafrika walikuwa wanatoa maoni yao siyo tu kwa watawala wa kikoloni waliokuwa karibu nao bali pia kwa

vikundi vilivyofuata siasa ya kiungwana katika nchi beberu.

Mkabala wa kikatiba uliungwa mkono zaidi na zaidi katika jamii kadiri vikundi vya Waafrika walioelimika vilivyozidi kupanuka na kadiri vikundi vipya vya kiuchumi na kijamii vilivyozidi kujitokeza kama sehemu ya mabadiliko ya uchumi na mipango ya kikoloni, hasa kuzuka kwa vyombo vya elimu ambavyo vililengwa kutoa watumishi ambao wangemudu shughuli za kiuchumi na kijamii.

Jambo jingine lililoongezea hali hiyo ni ile dhima ya itikadi rasmi tofauti zilizotangazwa na watawala wa kikoloni. Tofauti katika uelekezi mazingira na katika mtindo wa wafuasi wa utaifa wa Kiafrika zilitokana kwa kiasi fulani na ule ukweli kwamba vile vikundi mbalimbali vilikuwa na itikadi tofauti zilizokuwa zinaongoza matazamio yao na zilizotumika katika upimaji wa mafanikio yao. Kwa hiyo, miongoni mwa wafuasi wa utaifa wa Afrika waliokuwa chini ya utawala wa Wafaransa nchini Algeria na Senegal, kulikokuwa na uwezekano wa kuuondoa ukoloni kwa kutumia siasa ya 'usilimisho' iliyomwezesha mwananchi binafsi kuwa raia kamili wa Ufaransa mwenye haki kamili na madaraka kama Mfaransa, mwelekeo ulikuwa ni kuendelea kuipanua siasa hiyo ili ihusishe watu wengi zaidi na ienee mahali pengi zaidi. Kwa upande mwingine, katika makoloni ya Waingereza, Waafrika wa nchi hizo ambao walikuwa na matumaini kwamba siku moja wangekuwa nchi huru zenye mamlaka yao wenyewe ingawa zingebaki katika Jumuiya ya Madola ya Kiingereza, lengo lao muhimu katika kipindi tunachokijadili lilikuwa ni kuleta mabadiliko na ushirikishwaji ambayo yangewaandaa katika kujipatia uhuru wao. Kwa hiyo tofauti haikuwa katika lengo, yaani uhuru wenyewe, bali katika jinsi ya kulifikia.

Jambo jingine linalohusiana na itikadi ni ile hali ya kuwa na masetla. Kuwapo kwa masetla hao kulionyesha nguvu ya ukoloni kama hali ya kuendelea, kuvunjika moyo miongoni mwa watawaliwa mintarafu ya matazamio yao au upuuziaji wa madai ya Waafrika. Jambo hili ndilo linaloonyesha tofauti katika kiini na kiasi cha utaifa wa Kiafrika kati ya Algeria iliyojaa masetla wa kizungu na makoloni mengine ya Wafaransa ambako hakukuwa na tatizo la masetla wa kizungu kama lililokuwako nchini Algeria. Hali ya namna hiyo ilikuwako pia huko Kenya, Rhodesia na Afrika ya Kusini, sehemu zilizokaliwa na masetla wengi zaidi kuliko wale waliokuwako katika makoloni mengine ya Waingereza. Uzoefu tofauti ambao nchi hizi zilizuona ulitokana na nia imara ya walowezi wa Kizungu ya kuendeleza ukandamizaji wa wananchi kwa kutumia kile kilichoitwa 'ukoloni uliokithiri'

Vyama vya siasa na vyama vya vijana vilitumika kama njia za kuelezea matumaini na madai ya utaifa wa kiafrika na pia malalamiko mahsusi. Vyama vya siasa vilikuwa na maana katika zile sehemu chache ambazo zilikuwa na mabaraza ya kutunga sheria katika nyakati hizo za ukoloni. Nchini Misri, kuanzishwa kwa Bunge na Waingereza, ambao walikuwa wametangaza uhuru wa bandia katika mwaka 1922, kulitoa nafasi ya kuanzisha na kuendeleza vyama vya siasa. Kama tutakavyoona hapo nchini, hali ya kikatiba ilikiwezesha chama cha *Wafd* cha Sa'd Zaghlul na *Nationalist Party* Chama cha (cha Utaifa) kufanya kazi muhimu katika mapambano ya kurejesha uhuru kamili na mamlaka nchini Misri. Ingawa haukuwa na umuhimu sana, uingizaji wa mabadiliko ya kikatiba nchini Nigeria na Gold Coast (Ghana) katika Afrika Magharibi ya Waingereza, uliwezesha

uanzishaji na uendelezaji wa vyama vya siasa kama vile *National Democratic Party of Nigeria* (Chama cha Kidemokrasia cha Taifa Nchini Nigeria). Vyama vya siasa pia vilikuwa na dhima kubwa nchini Senegal ambako Baraza Kuu, lililoitwa Baraza la Kikoloni baada ya mwaka 1920, lilitoa nafasi kwa wananchi kutoa maoni yao.

Vyama vya vijana, vya mbari, vya wanafunzi wa zamani na vinginevyo vilivyokuwa na lengo la kuleta haki za raia na za binadamu, vilifanya kazi kubwa katika makoloni yote ingawa makoloni hayo hayakuwa na katiba ya namna moja. Vilikuwa nguvu isiyokwepeka kisiasa na kijamii hasa katika zile nchi ambazo zilikuwa haiwezekani kuendesha kiwaziwazi shughuli za kisiasa kutokana na ukandamizaji uliokuwa unaendeshwa na utawala wa kikoloni. Vyama vya vijana ambavyo vilikoleza siasa ya kitaifa ya kupingana na ukoloni, na ambavyo shughuli zake zitajadiliwa katika sura zijazo, vilikuwa kama vile: *The Gold Coast Youth Conference* (Mkutano wa Vijana wa Gold Coast) kilichoanzishwa mwaka 1929; *The Lagos* (baadaye Nigeria) *Youth Movement* (Chama cha Vijana wa Lagos (baadaye wa Nigeria); *Young Egypt* (Vijana wa Misri); *Young Kikuyu* (Chama cha Vijana wa Kikuyu) kilichoanzishwa na Harry Thuku nchini Kenya katika mwaka 1921; *The Sudan Graduates Congress* (Chama cha Wazamili wa Sudani); *The Young Gabonese* (Vijana wa Gabon); na *Young Tunisians* (Vijana wa Tunisia). Baadhi ya vyama vilikuwa na upeo wa kikanda na vingine vilibaki vya kitaifa tu. Baadhi ya vile vya kikanda ni kama vile *North African Star* (Nyota ya Afrika ya Kaskazini) kilichoongozwa na Messali Hadj; *The National Congress of British West Africa* (Chama cha Taifa cha Afrika Magharibi ya Waingereza); *The South Africa Congress* (Chama cha Afrika ya Kusini), na *West African Students Union* (Chama cha Wanafunzi wa Afrika Magharibi) kilichoongozwa na Ladipo Solanke wa Nigeria, nacho kilikuwa na wanachama kutoka eneo lote la Afrika Magharibi ya Waingereza.

Vyama vya kijamii vilivyotoa mchango wake katika kuelezea utaifa wa Kiafrika na siasa ya kupinga ukoloni miongoni mwao yalikuwa matawi kadhaa barani Afrika ya *Negro Improvement Association* (Chama cha Ulimwengu kwa ajili ya kumwendeleza Mtu Mweusi) kilichoanzishwa mwaka 1917 na Marcus Garvey kule Marekani. Ndivyo pia kilivyokuwa *Nigerian Improvement Association* (Chama cha Kumwendeleza Mnigeria) (1920). Pia vilikuwapo vyama kama vile *Ligue de Droits de l'Homme et du Citoyen* (Umoja wa Kupigania Haki za Binaadamu na Uraia nchini Gabon); *Liga Africana* (Umoja wa Kiafrika) kule Luanda na Lourenco Marques nchini Angola na Msumbiji walikotawala Wareno; *Societe Amicle des Originaires de l'afriques* (Chama cha Urafiki kcha Wananchi Asilia wa Afrika ya Ikweta ya Wafaransa) kilichoanzishwa na Andre Matswa, kilichokuwa na wanachama kutoka Libreville, Bangui na Brazzavillep *Ligue Universelle pour la Defence de la Race Negre* (Umoja wa Kiulimwengu wa Kumlinda Mtu Mweuzi) kilichoanzishwa mwaka 1925 chini ya uongozi wa Tovalou Quenum chini Dahomey (sasa Benin), Kamati (Le Comite) na Umoja wa Ulinzi wa Mtu Mweusi (*La Ligue de Defese de Race Negre)* vilivyoongozwa na Koutate Sorang (wa Sudan ya Wafaransa, sasa Mali) na Lamine Senghor (wa Senegal). Katika kiwango cha kimataifa, ilikuwapo Kamati ya

kupinga vita na ufashisti duniani (*Comite Mondial Contre la Guerre et le fascisme*) na vyama vingine vingi vya uafrika wote vilivyoanzishwa na Sylvester Williams na William Dubois. Vyama vya wafanyakazi na vyama vya watu wa tabaka la chini navyo vilikuwa nyenzo muhimu katika apambano dhidi ya mfumo wa kikoloni ingawa umuhimu wao uliongezeka hasa baada ya Vita Kuu ya Pili.

Silaha za aina nyingi zilitumika kwa kupigana na mfumo wa kikoloni katika kipindi kati ya Vita Vikuu Viwili. Machafuko na maasi ambavyo vilikuwa kitu cha kawaida sana katika kipindi kilichotangulia vilipunguzwa sana. Badala yake, magazeti, vitabu, vijarida, risala, upinzani kwa kuhama, migomo, ususaji, kisanduku cha maoni, mimbari na misikiti vilianza kutumiwa na wafuasi wa utaifa. Magazeti hasa yalikuwa chombo muhimu sana kilichotumiwa na vyama vya kisiasa na kijamii katika kueneza maoni. Magazeti haya mengine yalichapwa kila siku, mengine kila wiki, mengine kila baada ya wiki mbili na mengine mara moja kwa mwezi. Mengine yalitolewa tu ilipowezekana. Magazeti kadhaa na majarida yalikwishaanza kutolewa kabla ya Vita Vikuu vya Kwanza. Ndivyo lilivyokuwa *al-Liwa,* gazeti la Kiarabu lililoanzishwa mwaka 1900 kwa ajili ya kueneza mawazo ya kitaifa nchini Misri. *La Democratie du Senegal* (Demokrasia Senegal) na *The Lagos Weekly Record* (Habari za Wiki za Lagos) yalianzishwa mwaka 1891. Lakini, magazeti mengi yalianzishwa katika kipindi kati ya Vita Vikuu Viwili. Wakati huo ndipo yalipoanzishwa *The Times of Nigeria* (1921-1930) (Nyakati za Nigeria) na *Lagos Daily News* (1925 - 1938) za (Habari za Lagos za Kila Siku), *La Periscope Africain* (Kitazamio cha Afrika) na *La Courrier de l'Ouest-Africain* (Mjumbe wa Mwananchi wa Afrika Magharibi) (Dakar), *African Morning Post* (Posta ya Asubuhi ya Mwafrika) na *The Gold Coast Times* (Nyakati za Gold Coast) (Accra), *L'Action Tunisienne* (Juhudi ya Mtunisia) (1932) na *La Presse Port-Novienne* (Gazeti la Port Novo) likiwa na vichwa vidogo na makala mengine katika Kiyoruba. Licha ya lile gazeti *al-Liwa* lililotolewa kule Misri, baadhi ya magazeti yaliyotolewa katika Lugha za Kiafrika yalikuwa *Akede Eko,* gazeti la Kiyoruba (Lagos 1932 na kuendelea) na *La Voix du Dahomey* (Sauti ya Dahomey). Kutoka nje ya Afrika yalikuja majarida na mawazo ya kikomunisti na ki-unaafrika kama vile *Race Negre* (Jamii ya Mtu Mweusi), *Negro World* (dunia ya Mtu Mweusi), *African Times* (Nyakati za Kiafrika) na *Orient Review* (Pitio la Mashariki ya Mbali). Licha ya magazeti, michezo ya kuigiza na vijarida, insha zilichapwa, na vitabu vingi viliandikwa na baadhi ya viongozi wa wafuasi wa utaifa, na katika maandishi hayo, mfumo wa kikoloni ulilaumiwa sana na kukejeliwa.

Magazeti na majarida ya ndani na ya yale yaliyotoka nje yalitumika katika kuenezea mawazo ya utaifa uliopingana na ukoloni na uzungu. Ni katika kulishinda jambo hili ndipo hatua kadhaa za kiutawala na kisheria zilipochukuliwa dhidi ya vyombo vya habari na hata dhidi ya utangazaji kwa njia ya redio ambao ulikwishaanza kupanuka taratibu. Juhudi zilifanywa kuzuia au punguza usambazaji wa vitabu, magazeti na majarida na hata radio zenyewe ingawa zilitokea katika nchi zilezile walikotokea watawala wa kikoloni. Karibu kila mara, magazeti yaliyochapishwa nchini yalidhibitiwa na sheria za akaguzi na uchochezi. Yote haya yalifanyika ili kurahisisha utendaji kazi kwa watawala wa

kikoloni, jambo ambalo lilijibainisha katika kutoyavumilia kabisa matazamio ya wafuasi wa utaifa na katika kuwanyima haki na uhuru wa kiraia na kibinafsi. Vyombo vingine vilivyotumiwa na wafuasi wa utaifa wa Kiafrika katika kipindi chetu ni vyama vya kijadi au vya "kienyeji" na vyama vya dini za kijamii. Vyama vilivyohusika hasa kama tulivyokwishaona katika sura za mwanzoni ni vile vya utume ambavyo vilihusisha itikadi za wenyeji na zile zilizotoa picha za Uislamu au Ukristo. Hivi vilikuwa vyama ambavyo lengo lake kuu lilikuwa kujikomboa, vikidhihirisha ile kawaida ya kiulimwengu katika mazingira ambayo yalizilazimisha jumuiya zionyeshe kutoridhika kwao na hali zao za maisha na shauku yao ya kupata uhusishwaji.

Mifano inayojitokeza ya vyama vya aina hii katika kipindi chetu, ambavyo baadhi yao shughuli zake zimekwishajadiliwa katika sura ya 20, ni kama vile Uethiopia katika Afrika ya Mashariki na ya Kusini, na kile chama kilichoongozwa na wahubiri wa imani ya milenia katika Afrika ya Kati na ya Kusini mwa Afrika, hasa chama kilichoitwa kitawala (*African Watch Tower*) ambacho kilikuwa na wafuasi wengi kule Rhodesia, kikaenea hadi Kongo na Nyasaland, chama cha Kimbangui kilichokuwa na wafuasi katika Kongo iliyotawaliwa na Wabelgiji na Wafaransa, na kile chama cha Kimbangui-leo kilichoitwa *Mission des Noirs* (Misheni ya Watu Weusi) kilichoanzishwa katika sehemu za Kongo-Chini na Simon-Pierre Mpadi. Chama hicho pia kilijulikana kwa jina la Makhaki, na kilikuwa na athari miongoni mwa wenyeji wa Kongo ya Wafaransa na wa Ubangichari (sasa Jamhuri ya Afrika ya Kati). Vyama vingine nchini Uganda vilikuwa *African Progressive Association (*Chama cha Maendeleo ya Mwafrika); cha *Ruben Sparta Mukasa na Christian Army for the Salvation of Africa* (Jeshi la Kikristo kwa ajili ya Ukombozi wa Afrika). Kule Nyasaland kilikuwako chama kilichoitwa *Last Church of God and his Christ* (Kanisa la Mwisho la Mungu na Kristo Wake) kilichoanzishwa na Jordan Nsuma. Baadhi ya vyama hivi vilianza kwa kuupokea Ukristo lakini baadaye havikupendezwa na jinsi dini hiyo ilivyofafanuliwa katika kanisa mama la jamii za kikoloni. Kama ilivyokuwa vyama vya mabadiliko katika kanisa vilivyotokezea kule Ulaya na kwingineko, makanisa na vyama vilivyoanzishwa na wafuasi wa utaifa wa Kiafrika vilikuwa na lengo la kutumia itikadi za kikristo kama vile dhana za udugu wa binaadamu na umoja wa waumini ambao hauwatofautishi waumini hao kutokana na umbile au rangi yao ili kukomesha ubaguzi na ukandamizaji.

Uislamu pia uliwakilisha uzito mwingine dhidi ya itikadi ya kikoloni na pia ulitoa uwanja wa kuelezea utume. Mahdi kwa Mwislamu ni sawa na Masiha kwa Mkristo. Umahdi uliwasumbua watawala wa kikoloni huko Afrika ya Kaskazini na ya Magharibi, Sudani na Somalia. Kama tulivyokwishaona, Wasanusiyya katika Libya iliyotawaliwa na Waitalia walitoa mfano ulio wazi kabisa kuonyesha jinsi utaifa wa Kiafrika na upingaji wa ukoloni vinavyoweza kuelezeka kwa kutumia uislamu. Uislamu wote, kwa upande wa kidini wa utamaduni wa Kiarabu na dhana ya Salafiya vilikuwa na dhima kubwa katika siasa ya kitaifa na kikoloni nchini Misri, sehemu za Magharibi, na sehemu za kaskazini za Sudani ya Waingereza na Wamisri. Athari ya Wasanusiyya kama nguvu iliyopingana na ukoloni ilienea hadi sehemu za Afrika Magharibi. Watawala wa kikoloni waliviona vyama

vya kiislamu kama vile Hamalliyya, Tijaniyya, na Mouridiyya kama tishio lisilokwisha la usalama wa mfumo wa kikoloni.

Vyama hivi vya kiislamu vilitoa kiungo imara miongoni mwa waumini waliojikuta wanamilikiwa na tawala tofauti za kikoloni. Kama ambavyo Crowther ameonyesha hapo juu, tangu Vita Vikuu vya Kwanza, itikadi ya Uislamu wote iliyokuwa inaenezwa kutoka Uturuki iliwatia wasiwasi watawala wa kikoloni katika sehemu nyingi za Afrika. Lilikuwa tatizo ambalo utawala wa kikoloni ulitaka kulitatua kwa kubadilishana taarifa na kwa kuanzisha ushirikiano kati ya koloni moja na jingine.

Bila ya kujali kiasi cha kuhusishwa kwenye athari za kimagharibi ambazo Mwafrika aliyetawaliwa alijinoa, jambo la msingi katika kuuelezea utaifa wa Kiafrika lilikuwa kuanzishwa kwa vyama vya kitamaduni vilivyochukua sura tofauti. Imekwishaelezwa jinsi mnepo na umuhimu wa kudumu wa tamaduni na taasisi za Kiafrika ulivyokuwa katika Afrika yote iliyotawaliwa na wakoloni. Hata wale wasomi wa tabaka bora wa kiafrika walioelimika na kutopea kabisa katika tabia za kimagharibi bado walikumbana na uhalisia wa kwamba walikuwa wangali Waafrika ijapokuwa walikwishabeba kasumba nyingi ya utamadunikaji.

Vyama vingi vya vijana ambavyo vimekwishatajwa na ambavyo vitajadiliwa baadaye vilitambua umuhimu wa utamaduni wao katika kuulinda ujitambuo wao ingawa kasumba ya kizungu ilikuwa ikijipenyeza kwa kutumia mfumo wa elimu. Vile vyama mbalimbali vya Kikuyu vilikuwa mfano mzuri, hali kadhalika na vyama vya Uafrika wote na ile dhana isiyo imara ya Unegritudi ambayo, kama tulivyoona katika sura ya 21 hapo juu, ilijidhihirisha kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1930, na pia vile vyama vya 'kienyeji' na 'kidini' ambavyo vimekwishatajwa.

Katika kile kipindi kati ya Vita Vikuu, ukoloni na utaifa wa kiafrika na shughuli za kuupinga ukoloni havikufanikiwa kupata ushindi mkubwa katika kipindi hicho, lakini vilileta wasiwasi miongoni mwa maofisa wa kikoloni. Hatua zote za ukandamizaji ambazo zilichukuliwa dhidi ya ukoloni katika kipindi hicho zinadhihirisha wasiwasi huu. Katika kujibu changamoto zilizoletwa na utaifa wa kiafrika, wakoloni walitaka kuiwekea Afrika pazia kusudi isijue maendeleo ya ujumla yaliyokuwa yanatokea kwingineko ulimwenguni. Siyo tu kwamba hatua hii haikuwa na maana na ilijipinga yenyewe, lakini jaribio hilo lilikuwa kichocheo kilichoharakisha kukua kwa utaifa wa Kiafrika na upinzani dhidi ya ukoloni, mambo ambayo yalisababisha kupinduliwa kwa ukoloni katika muda mfupi uliofuata baada ya Vita Vikuu vya Pili.

# 23 Siasa na Utawala Kaskazini-Mashariki Mwa Afrika 1919-1935

*Utangulizi*

Aina mbili za utaifa zilishindania ukuu huko Kaskazini-Mashariki mwa Afrika katika kipindi kati ya Vita Vikuu Viwili:- Utaifa wa Kilimwengu na uzalendo uliopata msukumo kutokana na dini. Mapokeo ya Mahdi yaliyoendelea kule Sndani na yale ya Sayyid Muhammad kule Somalia yalifanikiwa kuunganisha moja kwa moja dini na fikara za kizalendo. Kwa upande mwingine, utaifa wa Kimisri uliendelea kuwa wa kilimwengu zaidi katika kipindi hicho. Kimsingi, yale malalamiko yaliyotokea kusini mwa Sudani yalikuwa ya kilimwengu tu. Ni kule kaskazini mwa Sndani na Somalia ndiko ilikokuwa vigumu kutenganisha dini na siasa katika kipindi hicho.

Licha ya upembuzi kati ya dini na mambo ya kilimwengu katika miaka hiyo, ulikuwako pia upembuzi kati ya utaifa na matatizo ya kiuchumi. Katika kipindi hicho, ilikuwemo miaka iliyokuwa na uchumi mbaya sana katika historia ya dunia ya leo. Hadi kufikia miaka ya mwisho ya 1920, hata tawala za kibeberu zenyewe zilianza kuona athari za mshuko wa uchumi uliofikia upeo wake kwenye Mpomoko Mkuu. Makoloni ya Kaskazini-Mashariki mwa Afrika yalikwishaanza kuona mpomoko wa uchumi muongo mmoja au miwili kabla Mpomoko Mkuu haujaukumba ulimwengu ulioendelea kitasnia.

Kwa upande wa Kaskazini-Mashariki ya Afrika, kitu kingine ambacho kilijibainisha katika kipindi hicho kilikuwa upanukaji zaidi wa utawala wa kibeberu na mapambano mapya dhidi ya ubeberu huo. Miaka iliyopita kati ya Vita Vikuu Viwili hivyo ilionyesha hatua za mwisho za mabeberu katika kupanua utawala wao kwa kumiliki maeneo mapya na kuimarisha utawala wa kikoloni. Lakini miaka hiyohiyo pia ilishuhudia kuanzishwa kwa mapambano dhidi ya ukoloni miongoni mwa watu waliotawaliwa, na kuanzishwa kwa chombo imara cha kisiasa kilichokuwa na lengo la kuleta uhuru na usawa, hasa nchini Misri. Walakini, katika kipindi hicho, inaelekea kuwa utaifa wa Kimisri nao ulikuwa na dalili mbaya za upanuzi wa namna yake. Viongozi wa chama kipya cha utaifa nchini Misri bado waliiona Sndani kama nchi iliyotegemea Misri, na walitaka kuimarisha mamlaka yao katika nchi hiyo.

Huo ndio ukinzani wa kimsingi ambao ulizuka huko Kaskazini-Mashariki mwa Afrika katika kipindi kilichopita kati ya Vita Vikuu Viwili:- upembuzi kati ya nguvu za kisiasa na za kiuchumi, na kati ya dini na utaifa, na pia kati ya upeo wa mwisho wa watawala wa kibeberu na upeo mpya wa kuupinga ukoloni; na vilevile kati ya uzalendo wa

kienyeji na tamaa ya wenyeji ya kutaka kupanua himaya yao, hasa katika uhusiano kati ya Misri na Sudani.

Sasa tuyaangalie mambo yote haya kinaganaga zaidi tukijadili kila nchi peke yake.

## *Misri*

### Mapinduzi ya 1919

Mojawapo ya matokeo muhimu ya Uingereza kutangaza Nchi-Lindwa kunako mwaka 1914, na kumalizika kwa Vita Vikuu vya Kwanza na mapatano yaliyofuatia, ilikuwa kuanzishwa kwa al-Wafd al-Misri au ujumbe wa Kimisri na Sa'd Zaghlul, kiongozi maarufu wa Kimisri, na wenzake wawili, katika mwezi Novemba, mwaka 1918. Madhumuni hasa ya chama hicho yalikuwa kuipatia Misri uhuru kamili na, kwa njia ya siri, kuhakikisha kuwa mamlaka Mimisri yanaendelea nchini Sudani, na kuyafutilia mbali makubaliano ya kusalimu amri.

Zaghlul na wenzake waliwakilisha sio tu tabaka bora jipya la Wamisri wenye mawazo ya kisasa - watawala, wanasheria na wataalamu wa mambo ya kilimwengu wengineo, bali pia waliwakilisha kikundi kipya cha makabaila kutoka mikoani, watu ambao walitaka kunyakua uongozi -kutoka kwenye koo bora za zamani zenye asili ya Kialbania na mchanganyiko wa Kituruki na Kimisri.

Chama cha Wafd kilirejelea matumizi ya mbinu za kimapambano ili kuimarisha uongozi wake na kuwahamasisha wananchi wote wakiunge mkono. Chama kilisambaza vikaratasi, kiliandaa mikutano ya hadhara, na kupokea maelezo yaliyotiwa saini kutoka kwa mashirika yaliyowakilisha watu mbalimbali jinsi Mradi Wafd ndicho kikawa chama rasmi kilicholiwakilisha taifa la Misri na kilichokuwa na madaraka ya kupigania hali ya baadaye ya nchi hiyo. Kilieleza kuwa uamuzi wa upande mmoja uliofanywa na Uingereza katika kuitangaza Misri kama Nchi Lindwa mwezi Desemba, 1914 haukuwa na halali na ulilidhalilisha taifa; na kilidai kuwa uamuzi huo afutiliwe mbali mara moja ili kutekeleza mafundisho na imani ya Raisi Wilson na ahadi za mataifa marafiki kwamba mataifa madogo yapatiwe uhuru wao.

Yale matatizo mengi ya kiuchumi na kijamii ambayo yaliikabili jamii ya Kimisri wakati wa Vita Vikuu yalijenga hisia ya wananchi wote kuona kuwa wamenyang'anywa mali yao; hali ambayo iliwasaidia wafuasi wa utaifa. Wakulima wengi walichakuliwa kimabavu ili wakatumikie vikosi vya kazi na vya ngamia. Nafaka na wanyama wao walichukuliwa bila ya kuipiwa fidia iliyoridhisha. Kupanda ghafla kwa gharama ya maisha kuliwadhuru hasa watumishi wa serikali na vibarua. Makabaila walishindwa kufaidika kutokana na kupanda kwa bei ya pamba kwa sababu Uingereza ilipunguza ekari zilizolimwa, ikapanga bei ya mauzo na kiasi gani kiuzwe nchi za nje. Chama cha Wafd kila mara kiliilaumu Uingereza kwa ukosefu huu wa haki na kikawashawishi Wamisri wajiunge nacho ili waweze kuliondoa baa hilo. *Kampeni hii ya nguvu ilisababisha*



**23.1** *Uzalendo katika Misri: Zaghlul Pasha (c. 1857 – 1927) akizungumza kwenye maandamano ya kutaka majeshi ya Kiingereza yaondoke, c. 1920.*

*mkengeuko wa taratibu wa matabaka yote kutoka kwa Waingereza.* Hata kufikia mwaka 1919, nchi nzima ilikwishajaa vuvumko kubwa la chuki na kutoridhika na mambo. Msisitizo wa serikali ya Uingereza kwamba Misri iendelee kuwa Nchi Lindwa na kukataa kwake katakata kuwaruhusu Husayn Rushidi, Waziri Mkuu wakati wa vita, na Zaghlul waende kuwasilisha madai ya Misri kwenye Mkutano wa Amani kule Paris kulizidi kuongezea hofu kwenye hali ambayo tayari ilikwishakuwa ya wasiwasi. Lakini kile kilichozua mapinduzi ya 1919 ni kule kukamatwa kwa Zaghlul na wenzake wawili, tarehe 8 Machi, 1919, na kupelekwa kisiwani Malta.

Maandamano makali kadhaa na migomo iliyohusisha watu wengi ilifanywa na wafanyakazi wa huduma za usafiri, majaji na wanasheria. Wanafunzi kutoka al-Azhar na shule za sekondari na vyuo vya utaalamu walishiriki kikamilifu katika mapambano ya kitaifa. Baadaye kidogo, wananchi wa majimboni nao walijiunga katika malalamiko ya umma, wakawa wanathubutu kushambulia reli na zana za mawasiliano kwa njia ya simu. Mashambulizi ya mara kwa mara pia yalifanywa dhidi ya askari wa Kiingereza, matokeo yake yakawa kuuawa kwa maofisa wanane wa Kiingereza na watu wengine pale Deyrut, waliokuwa wanasafiri kwa treni kutoka Aswani hadi Cait Cairo tarehe 18 Machi. Kwa kifupi nchi ilikwamishwa na nafasi ya Uingereza nchini Misri ilikuwa hatarini. Chama cha Wafd ndicho kikatokeza kama mwakilishi pekee wa taifa na Zaghlul alitawala siasa ya taifa hadi alipokufa katika mwaka 1927.

Mapinduzi ya 1919 kwa hakika ni tukio muhimu katika historia ya Misri ya leo. Kwa sababu, kwa mara ya kwanza, mapinduzi hayo yaliwahamasisha Wamisri wa matabaka yote (wakulima, wafanyakazi, wanafunzi, makabaila na wasomi) na vikundi vya kidini (Waislamu na Makopti) dhidi ya ukoloni kwa Kiingereza. Mapinduzi hayo pia yanaonyesha namna mpya ya utaifa wa Kimisri usiokitwa kwenye misingi ya dini.

Kutangazwa kwa Uhuru tarehe 28 Februari, mwaka 1922, kulikuwa tukio muhimu sana lililosababishwa na mapinduzi ya mwaka 1919. Baada ya kusongwa sana na wafuasi wa utaifa, Uingereza ikaamua yenyewe kuifutilia mbali Nchi Lindwa na kuutambua uhuru wa Misri, ali mradi tu ibakishe hali iliyokuwapo katika mambo yafuatayo (ambayo hiutwa Masharti Yaliyobaki) mpaka hapo mkataba utakapotiliwa saini kati yake na Misri: usalama wa njia za mawasiliano zilizomilikiwa na mabeberu, ulinzi wa Misri, usalama wa vikundi vya watu wachache na wa maslahi ya kigeni, na pia ulinzi wa Sudani. Uhuru wa Misri ulitangazwa rasmi tarehe 15 Machi 1922 na Sultani Fu'ad akapewa Cheo cha Fu'ad I, Mfalme wa Misri. Je ni kweli kwamba hatua hii iliutokomeza kabisa ukoloni? La hasha, kwa sababu uhuru uliotolewa na tangazo ulizimuliwa na yale masharti yaliyobaki, hasa lile sharti lililowawezesha Waingereza kuendeleza ukaliaji wa kijeshi nchini Misri. Pili, wageni waliendelea bado kufaidi marupurupu ya nje ya sheria ya nchi. Tatu, katiba ya mwaka 1923 haikuanzisha utawala wa kikatiba na demokrasia ya kibunge nchini Misri kwa vile uwezo mkubwa sana ulibaki mikononi mwa Ufalme, k.m. haki ya kumchagua na kumteua Waziri Mkuu, kuvunja Baraza la Mawaziri na kulivunja bunge.

Kushindwa huku katika kulipatia faida matazamio yake yote hasa kulitokana na kuvunjika polepole kwa umoja wa kitaifa uliopatikana katika mwaka 1919. Kuvunjika huku kulitokana na mfarakano uliotokea katika mwaka 1920 kati ya wananchi

wenye siasa laini walioongozwa na 'Adli Yakan, na wapambaaji walioongozwa na Zaghlul. Wale wa siasa laini walipendelea mapatano na Uingereza ambapo wale wapambanaji walisisitiza kwamba mapambano yaendelee mpaka Uingereza iwakubalie madai yao yote ya Kitaifa. Uingereza, iliyofuata diplomasia yake ya kikoloni ya 'gawanya utawala' ilitumia sana mfarakano huu kati ya wanachama wa Wafd. Huku ikiwakandamiza wale wapambanaji, Allenby alikubaliana na mawazo ya wale wenye siasa laini na kushauriana nao kuhusu kutangazwa kwa Uhuru.

Kipindi cha Mashauriano: 1924-1935

Katika kipindi kilichofuatia kutangazwa kwa Uhuru, mapambano ya kitaifa yalilenga hasa katika kujikomboa na yale masharti yaliyobaki kwa njia ya mashauriano kati ya wananchi na Uingereza. Vikao vinne vya mashauriano vilifanyika kati ya mwaka 1924 na 1935 -- mwaka 1924, 1927, 1929 na 1930. Vikao vyote hivyo vilishindwa kuleta suluhisho lolote kwa vile Uingereza ilikataa kutoa makubaliano ambayo yangelegeza ukaaji wake katika Misri au kubadilisha hali iliyokuwapo nchini Sudani.

Uingereza iliendelea kukataa hasa kwa vile ilikuwa na uhusiano mzuri na Kasri ya Misri iliyokuwa kituo chenye nguvu sana kilichopingana na wana-Wafd. Baada ya kuunga mkono umoja wa kupigania uhuru ulioongozwa na chama cha Wafd, Mfalme Fu'ad alianza kushuku kwamba Zaghlul alikuwa na njama za kuupindua ufalme na kuitangaza Misri kama jamhuri, kwa hiyo alianza mashambulizi dhidi ya chama cha Wafd. Ili kukizuia chama cha Wafd kisipate madaraka ya kutawala, Fu'ad aliiahirisha mara tatu katiba ya 1923 katika muda wa miaka isiyozidi saba - mwaka 1924, 1928 na 1930 - na kila mara alimteua waziri mkuu aliyempenda yeye mwenyewe. Serikali mbalimbali za kifalme ambazo zilitawala nchini Misri kabla ya mwaka 1935, hasa serikali ya Sidik (1930-1933), zilichukua hatua kali dhidi ya chama cha Wafd. Viongozi wa chama hicho walifungwa gerezani, magazeti yalipigwa marufuku, na wanachama walipoteza kazi zao serikalini na katika huduma za utumishi wa raia. Licha ya kuzikubalia hatua kali hizi, watawala wa kikoloni mara mojamoja walichukua hatua za kuwadhalilisha moja kwa moja wanachama wa Wafd. Kwa mfano, Zaghlul hakuruhusiwa kuwa Waziri Mkuu katika mwaka 1924 na 1926 ingawa chama chake kilikuwa na wabunge wengi kuliko vyama vingine vyote katika bunge.

Kampeni ya ukandamizaji iliyoongozwa kutoka kwenye Kasri ya mtawala polepole ilianza kupunguza ari ya wananchi katika kukipenda chama cha Wafd na umoja wake ulianza kumomonyolewa. Kutokana na kutoridhika kwao na kile walichokiita "uongozi usio wa busara" wa Zannas, aliyempokea Zaghlul, baadhi ya viongozi wa Wafd walijiondoa katika chama mnamo mwaka 1932. Kwa vile hawakuwa na uwezo wala nia ya kukabiliana ana kwa ana na ukoloni, wengi wa viongozi wa Wafd waliamua wajijenge dhidi ya ufalme kwa kukubaliana kimkataba na Uingereza kunako miaka ya 1930 katika. Uamuzi huu ulisababisha mkataba wa 1936 ambao uliihalalisha Uingereza iikalie Misri na papo hapo iwe na madaraka katika utawala wa Sudani ambao bado ulikuwa na Waingereza wengi.

## *Sudani*

Upinzani wa kisudani dhidi ya utawala wa kikoloni ulijionyesha kwa maono na harakati mbalimbali baada ya Vita Vikuu. Kundi la wasomi bora na Mamandisti, pamoja na wafuasi wa utaifa waliokuwa washikadini waliongoza upinzani huu kule Sudani ya Kaskazini, ambapo kule kusini mwa Sudani vyama vya upinzani hasa vilikuwa vya wenyeji.

### Vyama vya Upinzani vya Vijana

Kundi la walio bora lililozuka katika nyakati za karibuni na ambalo liliundwa hasa na wazamili kutoka *Gordon Memorial College (*Chuo cha Kumbukumbu ya Gordon) na *Khartoum Military College* (Chuo cha Kijeshi cha Khartoum) lilifanyakazi kubwa sana katika ukuzaji wa siasa ya Sudani katika kipindi cha kuanzia mwaka 1919 hadi 1925. Lilianzisha vyama vyao, na chama cha mwanzo kabisa kilikuwa *Graduates Club of Omdurman* (Klabu ya Wazamili wa Omdurman) kilichoanzishwa mwaka 1918, na vyama viwili vingine vilivyokuwa vya siri vilikuwa *League of Sudanese Union* - (LSU) (Ligi kya Umoja wa Kisudani) iliyoanzishwa mwaka 1919 na iliyokuwa muhimu zaidi ni *White Flag League* - WFL (ligi ya Bendera Nyeupe) ambayo ilianza katika mwezi wa Mei, mwaka 1924.

Chama cha utaifa cha Sudani kilichoanzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1920 kilipuuzwa na waandishi wengi wa Kiingereza kwamba hakikuwakilisha wananchi, na kwamba waanzilishi wake ati walikuwa mawakala na vibaraka wa Misri. Walakini uchunguzi uliofanywa hivi karibuni na wataalamu wa Kisudani umeonyesha kuwa ingawaje palikuwa na uhusiano mwingi na Misri kwa upande wa mbinu, utamaduni na itikadi, chama hiki kilianzishwa na wenyeji wenyewe, na lengo lake lilikuwa kuupindua utawala wa kikoloni wa Kiingereza. Mwito wa kuungana na Misri, uliotolewa na wafuasi wa utaifa ulikuwa zaidi maneno yenye mvuto wa siasa kuliko msingi wa imani ya wafuasi wa utaifa,na mwito huo ulilengwa katika kuifanya Misri iunge mkono na kukubaliana na madai yao, kwani walijua kwamba Misri nayo ilikuwa inaendesha mapambano ya kitaifa.

Baada ya kujifunza kutokana na mbinu zilizotumiwa na chama cha Wafd, wafuasi wa kitaifa wa kisudani waliyakuza malalamiko ya wananchi wenzao kuwa itikadi ya upinzani dhidi ya utawala wa kigeni. Walakini hawakujenga upinzani wao kwenye misingi ya kidini, ila walizingatia malalamiko ya kisiasa na kiuchumi, kila mara wakisitiza tamaa kubwa na utoka mbali wa mkoloni mwenyewe.

Mbinu kuu waliyotumia wafuasi wa utaifa mwanzoni katika kueneza mawazo na propanganda zao kwa wingi ilikuwa usambazaji wa vitini. Vikaratasi vilitumwa kwenye anwani mbalimbali nchini na wakati mwingine vilibandikwa katika sehemu za hadhara na kusambazwa mitaani. Pengine wafuasi wa utaifa walizipenyeza makala zao na kuzichapisha katika magazeti ya kimisri ambayo yalikuwa yanaunga mkono juhudi zao.

Hata hivyo kufikia mwaka 1923, wafuasi wa utawala waliacha mbinu hizi za

kisirisiri za kueneza propaganda yao na badala yake wakaamua mbinu za kimapinduzi ili kuupanua msingi wa kitaifa na kuwahamasisha wananchi wengi wakubaliane na mawazo yao. Katika mwaka 1924, waliongoza uhamasisho mkali wa kisiasa mjini Khartoum na katika baadhi ya miji mikuu ya majimbo na miji mingine. Ligi ya Bendera Nyeupe (WFL) iliongoza mfululizo wa maandamano na ghasia katika miji ya Atbara, Port Sudan, al-'Obeid na Shendi (Taz. kielelezo 4.1), hasa baada ya kukamatwa kwa raisi mwanzilishi wake, 'Abd al-Latif, na wenzake wawili katika mwezi Julai. Upande wa waumini wa mambo ya dunia wa utaifa wa kisudani ulikuwa bayana sana katika ghasia hizi.

Wanajeshi wa kisudani waliathiriwa sana na mawazo na propaganda ya Ligi ya Bendera Nyeupe. Makadeti walichochewa ili waandamane katika miji fulani ya kaskazini na ya kusini. Maofisa wa Kisudani, wengi wao wakiwa na mbari ya Wadinka, waliandaa na kutekeleza maasi muhimu ya kijeshi yaliyotokea mjini Khartoum katika mwezi Novemba, mwaka 1924. Nia hasa ya machafuko hayo ilikuwa kuonyesha huruma na umoja wao kwa majeshi ya Kimisri ambayo yaliondolewa nchini Sudani kutokana na amri ya Uingereza. Majeshi ya Kisudani yalitembea kutoka kwenye kambi yao ili yakaungane na vikosi vya kimisri kule Khartoum kaskazini. Walakini, yalipokuwa njiani majeshi hayo yalishambuliwa na askari wa Kiingereza. Matokeo yake yakawa mapigano makali yaliyoendelea jioni yote na usiku wa tarehe 27-28 Novemba, ambapo zaidi ya askari kumi na wawili wa Kisudani waliuawa. Kushindwa kabisa kwa maasi haya pamoja na ukatili wa serikali ya kikoloni iliyopania kuzuia kabisa harakati za kisiasa zilizofanyika kiwaziwazi, kulilifanya tabaka la wenye elimu liache mbinu ya mapambano katika muongo uliofuata, na badala yake tikajibana kwenye shughuli za kifasihi, kidini na kijamii. Walianzisha vikundi vya kujielimisha katika miji kadhaa na magazeti na majarida machangamfu kadhaa ingawa hayakudumu muda mrefu.

Kwa hiyo, chama cha kwanza cha utaifa kilichoanzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1920 haikufanikiwa, na sababu kubwa ya kushindwa kwake ni kwamba kwa vile hakikutafuta wala kutamani kuungana na wenyeji wala wachadini, sehemu mbili ambazo ndizo zilikuwa na umma mkubwa nchini, chama hicho hakikupendwa na wananchi wengi. Hata hivyo, chama hicho kilikuwa muhimu kwa sababu kilianza mapema zaidi kuliko vyama vingine vya utaifa vilivyokuwako katika makoloni mengine ya Afrika ya tropiki, na isitoshe, msemo wao mkuu uliovutia kisiasa, yaani Umoja wa Bonde la Naili, ulichukuliwa na vyama-muungano vya siasa katika miaka ya 1940.

## Upinzani wa Wamahdi Dhidi ya Utawala wa Kikoloni

Umahdi ulikuwa mojawapo ya silaha zilizotumiwa na Wasudani katika mapambano yao dhidi ya ukoloni katika sehemu zilizokuwa nje ya jimbo la mji mkuu wa Khartoum. Kwa wastani hakuna hata mwaka mmoja katika kizazi cha kwanza cha utawala wa Condominium (1899-1955) ambao ulipita bila ya maasi ya Kimahdi dhidi ya ukoloni. Ijapokuwa upinzani wa namna hii baadaye ulifikia taratibu katika sehemu zilizokaliwa kwa kudumu na watu nchini Sudani, Wamahdi waliendelea na vuguvugu lao huko Darfur (Taz. Kielelezo 4.1). Wengi kwao walijifanya manabii wa kitume na kutangaza vita takatifu

(djihad) dhidi ya utawala 'kafiri' wa Kiingereza. Miongoni mwa manabii hao, yule aliyekuwa maarufu sana ni *faki* 'Abdullah al-Sihayni, kiongozi wa maasi ya Nyala ya mwaka 1921.

Kama vile yale yaliyotangulia,maasi ya Nyala yalikuwa na lengo la kuupindua utawala 'kafiri' wa kikoloni na kurudisha 'utukufu' wa Umahdi nchini Sudani. Licha ya lengo hili lililokuwa na msingi wa kidini, ule uwekaji wa utawala wa kikoloni ulioongozwa kutoka katika makao makuu na kuungezeka kwa kodi ya mifugo zilikuwa baadhi ya sababu zilizowachokoza wananchi wa Darfur wajiunge na maasi hayo.

Chini ya uongozi wa al-Sihayni, kikosi cha wapiganaji elfu tano kiliishambulia ngome na soko la Nyala mnamo tarehe 26 Septemba, mwaka 1921. Waliiteka ngome na kuchoma moto jengo moja lililokuwa jirani. Al-Sihayni alifanya shambulizi la pili ambalo lingaliwafanya maadui wakimbie ovyo kama yeye mwenyewe asingalijeruhiwa vibaya. Ijapokuwa Al-Sihayni alinyongwa hadharani mnamo tarehe 4 Oktoba, wafuasi wake waliendeleza mapambano. Baada ya kuona changamoto hiyo, maofisa wa kikoloni walipeleka kikosi cha kuadhibu chenye nguvu, kikawakamata wananchi wengi, kikachoma moto nyumba zao, kikapora ng'ombe wao na kuharibu mali yao. Hata kufikia mwezi Mei, mwaka 1922, maasi hayo yakazimwa. Kwa hakika maasi ya Nyala ndiyo yaliyokuwa muhimu kuliko yote katika mapambano dhidi ya ukoloni nchini Sudani kabla ya mwaka 1924. Ingawa maasi hayo yalishindwa kuuharibu utawala wa kikoloni, mafanikio yake madogo yalichukuliwa kama ilani na Waingereza.

Umahdi-Mamboleo

Baada ya kushindwa kwa upinzani wa kimapambano wenye misingi ya kidini katika miaka ya 1920, baadhi ya wafuasi wa utaifa kama vile Sayyid 'Abd al-Rahman, mtoto wa Mahdi aliyezaliwa mara tu baada ya baba yake kufariki, waliamua kuanzisha Umahdi-mamboleo. Tangu mwaka 1914, al-Sayyid alishaona kwamba maasi ya kutumia silaha yangelileta uharibi fukamili, na kwamba maslahi ya taifa la Sudani na ya dini ya Kimahdi yangalipatikana tu kwa kushirikiana na Waingereza chini ya wito usemao Sudani iwe ya Wasudani. Al-Sayyid alikuwa mjanja pia kung'amua kwamba uhamasisho wa kisiasa na kidini ulihitaji msaada wa kifedha. Kwa hiyo alipanua miradi yake ya kilimo na biashara, hata kufikia mwaka 1936, akawa kabaila mkubwa na bepari maarufu, na alitumia mali hiyo kuimarisha shirika la Ansar. Alipoona kwamba utaifa wa kisiasa ulianza kutpita dini kama chombo muhimu cha uwezo katika sehemu za mashariki, al-Sayyid alifanya juhudi za pekee katika miaka ya 1930 ili aungwe mkono na tabaka la wenye elimu.

Hata kufikia mwaka 1935, Umahdi-mamboleo ulikwishakuwa nguvu muhimu ya kuupinga ukoloni. Umoja kati ya idadi kubwa ya wasomi na jamii za kijadi na kidini ambao ulitokana na Umahdi-mamboleo ulitumika kama kiini cha kuanzishia Chama cha Uhuru (Independence Front) ambacho kilifanya kazi muhimu na ya pekee katika kuleta uhuru wa taifa katika mwaka 1936.

Vyama vya Upinzani vya Wenyeji Kusini mwa Sudani

Waafrika wa Kusini mwa Sudani waliendeleza maasi yao wakiwa na lengo la kuutokomeza utawala wa kikoloni wa Kiingereza katika eneo hilo. Katika wimbi hili kubwa la upinzani, maasi mawili yanastahili kutajwa kwa namna ya pekee: uasi wa Waaliab Dinka (1919-1920) na uasi wa Wanueri (1927-1928). Dini ya jadi ya kiafrika iliathiri chanzo cha maasi haya. Lakini sababu ya papo kwa hapo iliyoleta uasi wa kwanza ilikuwa tabia mbaya ya *ma'mur* mtawala wa kikoloni aliyewatawala Waaliab, hasa ile tabia yake ya kughusubu ng'ombe na wanawake. Uasi huo ulianza kunako tarehe 30 Oktoba wakati kikosi cha wapiganaji 3000 walipokishambulia kituo cha polisi pale Minkamman kusini mwa Mto Sobat. Kituo chenyewe kilizidiwa nguvu na Waaliab, ingawa ma'mur aliwahi kutoroka. Kunako tarehe 2 Novemba, Waaliab walirudi tena wakashambulia nyumba ya kupumzika na kuwaua polisi wawili. Ijapokuwa mashambulizi haya ya Wadinka baadaye yalishindwa, wakoloni waliingia gharama kubwa sana kutokana na kampeni hiyo.

Wanueri walitoa changamoto nyingine kali kwa akoloni katika mkoa wa kusini. Ingawa walishambuliwa na vikosi vya doria vya kuadhibu vya Kiingereza, hawakukubali kushindwa, na upinzani wao ulifikia kilele chake katika maasi ya mwaka 1927-1928. Wakiongozwa na nabii wao Garluak mwenye nguvu na mvuto mkubwa kwa watu Wanueri wa magharibi walikataa kutii amri za utawala. Katika mwezi Desemba, mwaka 1927, kundi la maelfu ya wapiganaji wa Kinueri lilishambulia na kumwua Kamishna wa Wilaya wa eneo hilo aliyekuwa katika mtalaa wa ukaguzi pamoja na watu kumi na wanane wa upande wake.

Wakati huo uo, Wanueri waliokuwa wakiishi huko Lou, kusini mwa mto Sobat, nao waliasi dhidi ya ukoloni. Kiongozi wao mwathirifu, Nabii Gwek Ngundeng, alikataa kuonana na maofisa wa kikoloni pamoja na Gavana Jenerali mwenyewe. Wakijua kwamba Ngundeng angaliweza kushambulia wakati wowote, maofisa wa kikoloni walichukua hatua kali kukikomesha chama chake.

Utumiaji nguvu uliozidi kiasi na wa kiholela uliotumiwa dhidi ya maasi haya ulisababisha vifo na uharibifu mkubwa. Hata hivyo, upinzani wa kishujaa wa Wadinka na Wanueri uliwadhihirishia wakoloni wa Kiingereza kuwa utumiaji nguvu peke yake haukufaa. Hata kufikia miaka ya 1930 mwanzoni, wakoloni hao walilazimika kuanzisha siasa ya kuwajali na kupatana na wananchi wa Kusini mwa Sudani.

## *Somali*

Tangu zamani Wasomali walikwishajenga moyo wa umoja wa "Usomali" ambao uliambatana na utamaduni wa kitaifa wa aina moja na ambao uliimarishwa na imani yao kubwa katika Uislamu. Kama walivyokuwa watangulizi wao na wale waliofuata badaye, wafuasi wa utaifa wa kisomali walioishi katika kipindi kati ya Vita Vikuu waliutumia utambulisho huu wa kitaifa katika mapambano yao dhidi ya ubeberu wa Kiitaliani, Kiingereza na Kifaransa nchini Somalia (tazama kielelezo 4.1).

Licha ya jambo hili la msingi, kulikuwa pia na mabadiliko yaliyoletwa na ukoloni katika jamii ya kisomali. Ama kwa hakika ukoloni ulikwishaharibu taasisi za jadi za kisiasa na kijamii kwa kuingiza kila mahali nchini Somalia mfumo wa utawala ulioendeshwa kutoka kwenye makao makuu, mfumo ambao ulikabidhi mamlaka yote mikononi mwa watawala wa kikoloni na kuteua machifu, waliojulikana kama (*mawakili*) katika Nchi Lindwa na Copo (*Makaposi*) nchini Somalia, ambao walitumika kama washauri na kama vyombo vya kutekelezea maagizo ya wakoloni kwa wananchi tu. Kwa vile walikuwa wanayo hisia kali ya uhuru na chuki ya tangu jadi dhidi ya mambo yoyote ya kigeni yale, hasa dhidi ya wakristo weupe, Wasomali walilazimika kupinga badiliko hili kubwa.

Zaidi ya hayo, kabla ya enzi ya ukoloni, Wasomali walikuwa hawalipi kodi za serikali isipokuwa ada za *cadi* (kadhi) na ushuru wa uagizaji na uuzaji bidhaa nchi za nje. Walakini wakoloni waliingiza kodi dhahiri kwa mara ya kwanza waliwaandika Ushokoa watu ili wakafanye kazi kwenye miradi yao. Wafaransa waliwaandika Ushokoa Wasomali 2000 wakafanye kazi kama vibarua wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza, ambapo Mataliani mara nyingi walipeleka magenge ya watu kuwakamata mashokoa waliohitajika kufanya kazi katika mashamba yao nchini Somali. Taabu yote hii pamoja na unyonyaji uliwafanya Wasomali wengi wauchukie sana ukoloni.

Ukinzani wa Wasomali dhidi ya utawala wa kikoloni katika kipindi cha mwaka 1919 hadi 1935 julikuwa ni jibu la moja kwa moja kwa mabadiliko haya ya kijamii. somalia ilionyesha ukinzaji wake kwa njia mbili za migomo: ya wenyeji na wasomi.

## Migomo ya Wenyeji

Kwa kiasi kikubwa, ukinzani wa Wasomali katika kipindi cha baina ya vita ulikuwa wa wenyeji kimsingi na ulichukua umbo la mfululizo wa maasi ya wenyeji ambayo yalikuwa mengi sana na yaliyotawanyika mno kiasi ambacho si rahisi kutaja hapa. Lakini maasi hayo yalimaanisha nini ni jambo ambalo litaweza kuonekana kwa kuyaangalia kwa undani baadhi ya maasi hayo.

Agizo la watawala wa kikoloni kwa watemi wote na wazee wa Kisomali kuwa wasalimu amri lilikataliwa moja kwa moja na Hadj dji Hasan wa Galjal Haya. Ingawa Hadj dji Hasan alitekwa, moyo wa kupinga utawala haukuweza kufishwa, kwani wa Bantu wa Gile walianzisha mgomo mwingine karibu na Bur Acuba.

Ukinzani dhidi ya jaribio la Waitaliani kujumuisha majimbo mawili, ya Obia na Mijdurteyn, katika koloni lao ulikuwa ni mfano mwingine wa nia ya Wasomali kufinda mshikamano wa kijamii wa kitamaduni na uliohuru wa jamii yao.

Ingawa Obbia ilitekwa mnamo mwaka 1925 na Waitaliani walimlipa kiinua mgongo na kumstaafisha Yusuf akakae Mogadishu, maasi ya kishujaa yalitokea pale al-Bur. Maasi hayo yaliongozwa na 'Umar Samatar kutoka Midjuriayn aliyeteuliwa na Mataliani kama chifu wa wenyeji wa pale. Samatar aliikamata ngome ya al-Bur na majeshi yake yakalizunguka jengo lililokuwa katikati. Majeshi ya Kitaliani yaliyomzingira nayo pia yakazingirwa na wenyeji wa pale walioongozwa na Herzi Gushan, kamanda-

jeshi wa wilaya wa Sultani 'Alli Yusuf. Kunako tarehe 15 Novemba, majeshi ya kikoloni yakarudi nyuma hadi Bud Bud, huku yakiwaacha watu thelathini na wanane wamekufa, miongoni mwao akiwemo Taliani Mkazi mwenyewe. Kunako Novemba 30, Mataliani walishindwa tena walipoviziwa pale Bot.

Mataliani walipambana na ukinzani mkali zaidi katika usultani kwa Midjurtayn. Sultani wao maarufu, 'Uthman Mahmud, alikataa hadhi duni iliyotolewa na wakoloni kwake mwenyewe na kwa watu wake. Ingawa wakoloni walimkandamiza, ukinzani wake uliendelea kupata nguvu na aliwazuia wavamizi kwa karibu miaka miwili. Walakini alikamatwa karibu na mwishoni mwa mwaka 1927 na akatendewa kama alivyotendewa Yusuf mwanaukoo mwenzake. Hata hivyo, mapambano yaliendelea chini ya uongozi wa Herzi Bogor, mwanawe na mrithi wake, mpaka alipoondoka kwenda Ethiopia.

Wakati huohuo, kumbukumbu isiyokwisha ya chafuko la Sayyid Muhammad iliukomaza ukinzani katika mioyo ya Wasomali wengi waliokuwa katika Nchi Lindwa na baadhi ya wafuasi wa Sayyid Muhammad, kama vile akina A Farah 'Umar na Hadjdj Bashir Yusuf, waliyaendeleza mapambano katika sehemu za magharibi na pembeni mwa mipaka ya mashariki. Uanzishaji wa elimu ya kimagharibi katika Nchi Lindwa mnamo mwaka wa 1920 na 1935 ulifasiriwa na viongozi wa dini kama chombo cha kuendeleza shughuli za kimisionari, jambo lililochukuliwa kama tishio kwa Uislamu. Tendo hilo liliamsha uchungu na hasira nyingi iliyosababisha ghasia katika maeneo mawili: pale Burao mnamo mwaka 1922 na kule Baro katika mwaka 1936.

Maasi ya wenyeji wa Kisomali dhidi ya wakoloni wa Kifaransa nayo pia yalikuwa na umuhimu. Waafari wa Waisa, koo mbili kuu katika Somalia ya Wafaransa, walionyesha ukali mwingi dhidi ya utawala wa kikoloni. Masultani wa Kiafari waliokuwa wanatawala katika sehemu za Tadjura na Gobaad walikuwa katika mstari wa mbele. Tena basi kutokana na haki hii Wafaransa walimwondoa kighaflaghafla sultani wa Gobaad na kumfukuzia Madagascar katika mwaka 1931. Sultani Yayu wa Awsa, ambaye kwa muda mrefu alikuwa anapinga uingiaji wa Wafaransa katika eneo lake, naye aliendeleza ukinzani wake katika kipindi hiki. Alimvizia na kumkamata Lippmann, gavana mpya aliyeteuliwa pale Diknil. albert Bernard, aliyeteuliwa baada ya Lippmann, na askari kumi na sita wa Kisomali waliuawa pale Morneito mnao mwaka 1935. Uanaharakati wa Sultani wa Awsa uliongezeka zaidi baada ya ushindi wa Mataliani dhidi ya Ethiopia katika mwaka 1935.

Maasi ya wenyeji dhidi ya utawala wa kikoloni nchini Somalia yalishindwa kutokana na sababu kubwa mbili. Sababu ya kwanza ni kwamba Wasomali hawakuwa jumuia moja yenye kujitawala kisiasa bali walikuwa wamegawanyika katika koo kadhaa ambazo mara nyingi zilikuwa zinachukiana, na koo hizo nazo ziligawanyika katika vikundi vya udugu, kila kikundi kikiwa na maelfu machache tu ya watu. Kwa hiyo walishindwa kuonyesha upinzani ulioungana dhidi ya utawala wa kikoloni. Sababu ya pili ni ile siasa kali waliyoitumia wakoloni dhidi ya Wasomali. Hata hivyo, maasi haya angalau yaliendeleza vituko vilivyotokea katika enzi iliyotangulia, na yalijenga msingi wa upinzani wa wananchi dhidi ya ukoloni nchini Somalia.

### Vyama vya Upinzania vya Walio Bora

Wakati uleule ambapo maasi yalikuwa yanaendelea katika sehemu za vijijini, kule mijini nako kundi la wasomi bora wa Kisomali lilikuwa linaushambulia mfumo wa kikoloni kwa njia ya vyama vya vijana lilivyokuwa limeianzisha.

Chama cha kwanza miongoni mwao kilikuwa *Somali Islamic Association* (Chama cha Kiislamu cha Wasomali) kilichoanzishwa mjini Aden na Hadjdj Farah 'Umar, aliyekuwa ofisa wa serikali ya kikoloni na baadaye akawa mwanasiasa wa kwanza wa kisasa. Alikuwa amefukuziwa kule Aden na Waingereza kutokana na ukinzani wake dhidi ya ukatili wa utawala wa kikoloni kunako miaka ya 1920, na kwa kufanya kampeni ya kuendeleza shughuli za kiuchumi na upanuaji wa elimu. Ijapokuwa hakikuwa chama cha siasa, chama hiki kilikuza maslahi ya Wasomali. Hadjdj Farah alifanikiwa kuwafahamisha wananchi wa Uingereza juu ya matazamio ya kitaifa ya Wasomali kwa kutumia makala katika magazeti ya Aden, na kwa kuandika madai ya haki, na barua zilizolengwa ziwafikie wabunge, vyombo vya habari na serikali ya Uingereza.

Klabu za kisiasa pia zilianzishwa na wafanyibiashara na maofisa wa kikoloni kwenye miji mikubwa ya Nchi Lindwa katika miaka ya 1930 katikati , na klabu hizo zilikuwa na dhima ya kueleza manung'uniko ya wananchi na kukuza mwamko wa kisiasa mijini. Katika Somalia ya Wafaransa pia *Seamen's Union* (Umoja wa Wanamaji) ulioanzishwa mjini Djibuti katika mwaka 1931 haukushughulikia tu masuala ya mabaharia bali ulifanya kampeni ya kudai uwakilishwaji wa Wasomali katika serikali na upatiwaji wa hisa yao katika uchumi wa nchi.

Kutokana na majaribio haya ya mwanzoni *Somalia National League* -SNL (Ligi ya Kitaifa ya Somalia) kilianza kunako mwaka 1935. Hiki kilikuwa chama cha vijana kilichokuwa muhimu kuliko vyote katika kipindi kilichopita kati ya vile vikuu. Tangu kuanzishwa kwake, Ligi ya Kitaifa ya Somalia ilijiona kama chama cha Wasomali wote kilichokazania kuuvunja upinzani wa kijadi dhidi ya uzalendo wa kitaifa. Ligi hiyo iliendelea kuwapo ikichukua majina tofauti, na katika mwaka 1951 iliibuka kama chama kamili cha siasa katika Nchi Lindwa ya Kiingereza.

Kama ilivyokuwa kwa wafuasi wa utaifa waliokuwa wakiishi vijijini, vyama hivi vya walio bora havikupata ufanisi wa kuridhisha kutokana na sababu mbili kubwa. Kwanza kabisa, kundi la wasomi bora waliovianzisha walikuwa wachache mno kuweza kutoa athari kwa vile elimu.ya kimagharibi wakati wa kipindi kilichopita kati ya vile vita vikuu ilikuwa imepuuzwa katika sehemu zote za Somalia. Sababu ya pili ni kwamba watawala wa kikoloni walichukua hama za kuwanyamazisha haraka wale wanaharakati wachache katika kundi la wasomi bora, ama kwa kuwafukuza kutoka kwenye utumishi wa serikali, au kwa kuwahamishia katika sehemu zilizokuwa mbali na miji. Hata hivyo, kujitambua huku kidogo kulikoanzishwa na vyama hivi baadaye kuligeuka kuwa mwamko mkubwa wa kisiasa katika miaka iliyoifuatia Vita Vikuu vya Pili.

Katika jambo hili sharti tutaje ugunduzi wa abjadi ya wenyeji kwa ajili ya lugha ya Kisomali, *'Osmania Alphabet'* kunako mwaka 1920, iliyoitwa hivyo kufuatia jina la yule aliyeiunda, 'Uthman Yusuf Kenadid. Viongozi wa kidini wasiokubali mabadiliko na

ambao walipendelea kutumia hati za Kiarabu katika maandishi ya Kisomali na pia wakoloni wa Taliani walipinga matumizi ya abjadi hiyo. Hata hivyo, abjadi hiyo ilitumiwa na watu wachache na baadaye ilisifiwa na wafuasi wa utaifa kama 'ishara ya mafanikio ya Wasomali'.

## *Hitimisho*

Kutokana na yote tuliyoyaona hapo juu, ni dhahiri kwamba miaka iliyopita kati ya Vita Vikuu ilishuhudia kuongezeka sana kwa harakati za kitaifa kaskazini-mashariki mwa Afrika kulikoletwa siyo tu na mabadiliko yaliyoanzishwa na ukoloni bali na sababu za kidini pia. Ni wazi kwamba kinyume cha hali halisi ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Afrika, viongozi wa kitaifa hawakupigania marekebisho au mabadiliko ya ukoloni huo bali walitaka kuuondoa kabisa. Ijapokuwa ni kule Misri tu ambako harakati za kitaifa zilizaa matunda ya kuridhisha, hapana shaka kwamba mbegu za ukombozi kwa hakika zilipandwa katika Bonde la Mto Naili na kwenye Konjo la Afrika katika kile kipindi kilichovitenganisha vile vita vikuu.

# 24

## *Siasa na utaifa katika maeneo ya Maghreb na Sahara, 1919-1935*

Katika sehemu iliyobaki ya Afrika ya Kaskazini, yaani maeneo ya Libya na Maghreb, kipindi kilichopita kati ya Vita Vikuu kilikuwa na matukio makubwa matatu ya kisiasa. Takio la kwanza lilikuwa ni kule kuendelea kwa mapambano au ukinzani wa baadhi ya watu wa Afrika ya Kaskazini dhidi ya jitihada za mwisho wa ubeberu katika kutamalaki Afrika. Ukinzani huo ulikuwa na madhumuni ya kulinda mamlaka na uhuru wa wazalendo. Hii ilijidhihirisha zaidi katika shughuli za kisiasa nchini Libya na katika sehemu za Juu na za Chini za Milima ya Atlas huko Moroco. Tukio la pili lilikuwa ni kuzuka kwa ukinzani halisi dhidi ya ukoloni au kuzuka kwa harakati za kitaifa zenye madhumuni ya kuuondoa mfumo wa kikoloni au kuurekebisha, mambo ambayo yalichukua umbo la kijeshi mara tu baada ya vita. Awamu hii ilishia mnamo 1923 nchini Algeria na Tunisia baada ya kuondoka kwa al-Tha-alibi na Khalid. Lakini mambo haya hayakutokea nchini Morocco, na hasa katika eneo la Rif. Hata hivyo inaelekea kuwa utaifa katika maeneo haya ulichukua sura za kidini na kiutamaduni kama ilivyokuwa katika sehemu za Sudani na Somalia. Hali hii ilikuwa tofauti sana na Misri au Kusini mwa Sudan ambako mwamko wa utaifa ulikuwa hasa ule unaohusu utawala wa kijadi (kienyeji). Hata katika miaka ya 1930, harakati za kupinga ukoloni au kuzuka kwa fikra za kitaifa vilianza kuwepo tena, ingawa zamu hii mbinu na mikakati iliyotumiwa ilikuwa tofauti. Hii ni kwa sababu ya matokeo ya Mpomoko wa uchumi wa duniani uliotokea hasa katika nchi za Maghreb kuanzia mwaka 1932 na kuendelea. Sifa hizi tatu za siasa na utaifa katika Libya na Maghreb ndizo zinaunda mada za sura hii.

### *Vita vya Waziwazi na Ukinzani wa Kichinichini*

Watu wa Libya walijihusisha zaidi, hata kuliko watu wengine wa mataifa ya Afrika ya Kaskazini, katika kuendeleza utaifa na uhuru wao dhidi ya uvamizi wa kibeberu wa Italia katika kipindi tunachozungumzia. Mapambano haya, ambayo yaliendelea hadi miaka ya

1930, yameelezewa katika sura ya 5. Hivyo Libya haikuzungumziwa katika sura hii.

Tabia ya "Kugomagoma" au *siba* iliyokuwa kawaida ya Waberiberi ni mojawapo ya desturi za watu hao kabla ya ukoloni. Tabia hii ilivuma hasa Morocco. Kujipenyeza kwa Wafaransa katika sehemu za kati za milima ya Atlas wakati wa kipindi hiki kulifanyika kwa shida kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa kwa masultani ingawa nako kulifanywa kwa jina lilelile la "serikali halali" au *Makhzen*. Ulinzi wa taifa ulifanyika katika umbo la chuki kwa wageni na hata kujiona kama wapiganaji wa vita vitakatifu; ukinzani huu akaenea sehemu zote za juu na katikati ya milima ya Atlas. Katika utekaji wa Algeria na Morocco, eneo lililo kaskazini mwa Mauritania ya sasa na sehemu ya magharibi ya Sahara inayojulikana kama Rio de Oro, palikuwa na matukio ya mashambulio ya pamoja au *rezzous*. Wakati huohuo, kulikuwa na mipango ya kujinyakulia namna fulani ya madaraka. Mipango hiyo ilianzishwa na wafuasi wa kiongozi mashuhuri wa dini, *Ml al-Aynayn*. Kaskazini mwa ujia wa Taza, sehemu kubwa ya eneo la pwani ambayo ilipewa Hispania ilibaki bila kutekwa. Katika sehemu ya mbali zaidi ya mashariki, upande wa pili wa Sahara ya Algeria, tawala zinazojitegemea ziliendelea kuwepo katika Tripolitania. Vilevile, Wasanusi walijiimarisha katika sehemu za chemichemi. Kuifikiria hali hii, iliyokuwa imeenea namna hiyo, kama njia tu ya kulinda mambo ya desturi za kale ni kutoipa uzito unaostahili. Msukumo mkubwa wa mambo haya ulitokana na tabia ya kimapokea iliyokuwepo ya uhuru wa jamii.

## *Ukinzani Dhidi ya Ukoloni, Mapambano na Harakati za Kitaifa Katika Miaka ya 1910 na 1920*

Wakati upinzani dhidi ya kuingizwa kwa ukoloni ulikuwa ukiendelea katika maeneo yaliyotajwa hapo juu, upinzani halisi au mapambano ya kitaifa yalikuwa yakipamba moto katika maeneo ambamo mifuko ya kikoloni ilikuwa imejiimarisha tayari. Harakati hizi zilichukua sura tofauti tofauti katika Algeria, Tunisia na Morocco, na zilijidhihirisha katika miji na mashambani kati ya wasomi, wakulima na wafanyakazi.

Katika Algeria, ukinzani dhidi ya mfumo wa ukoloni ulifanyika kwa njia za mapambano wakati mfupi wa uongozi wa Jemadari Khalid. Khalid, askari aliyewahi kuwa Kapteni katika jeshi la Kifaransa, na pia mjukuu wa Abdal-Kadir, kwa muda fulani alikuwa akipendwa sana na watu. Kwa kutumia sifa zake za Uislamu, aliweza kutetea hadhi ya Algeria na kuisisitizia Ufaransa kuwa ilikuwa ni wajibu wake kutoa shukrani kwa nchi ya Algeria kuweza kuwapa askari wengi kiasi hicho. Kikundi cha Khalid kiliwashinda wapinzani wake wenye siasa laini katika uchaguzi wa halmashauri za mji wa Algeria. Ushindi huu ulionekana kuwa tishio kubwa kwa utawala wa Wafaransa kiasi kwamba matokeo ya uchaguzi yalikataliwa. Jamadari huyo aliweza tena kushinda katika uchaguzi wa pili na wa tatu. Mwishowe alilazimika kuondoka Algeria kwenda Ufaransa mwaka 1923. Ni dhahiri kuwa kuondoka kwake kulidhoofisha harakati za kitaifa katika Algeria.

Ukinzani imara wa Waberiberi katika miji ulisaidia kulanya mawazo ya watu wa

mashambani waliokuwa wengi Algeria kulenga kwenye maswala muhimu ya kijamii, hivyo kuleta umoja imara. Sheria ya tarehe 4 Februari 1919 iliwekwa ili kujaribu kuubomoa umoja huu. Sheria hii iliyojulikana kama Sheria ya Jonart ilithibitishwa na maagizo rasmi mawili. Sheria hii iliwapa baadhi ya Waalgeria haki ya kupiga kura katika baraza la pamoja au *duwar-commune*; vilevile katika mabaraza ya miji na uchaguzi wa Meya. Watu waliopewa haki hii ni wale tu waliokuwa na sifa fulani kama vile waliowahi kutumikia jeshi, waliojua kusoma au kuandika katika lugha ya Kifaransa na kadhalika. Waislamu wapatao nusu milioni walikuwa na sifa hizi, hivyo waliweza kupiga kura. Hii ni pamoja na watu wapatao laki moja waliokuwa na haki ya kuyapigia kura mabaraza ya mikoa na serikali kuu. Hata hivyo, hatua hii haikuleta usawa kamili kwani haikuzingatia haki zote ambazo watu walikuwa wakidai.

Mnamo miaka ya 1920, madai makubwa ya Waalgeria yalikuwa ni kutaka kujumuisha au kusilimishwa katika jumuia ya Kifaransa. Pia walidai kuwa baadhi yao wapewe haki ya kupiga kura katika Bunge la Ufaransa bila ya kupoteza haki zao za kupiga kura zingine ambazo wangepiga kwa mujibu wa "wadhifa" waliokuwa nao. Madai haya ya kutaka kujumuishwa, ambayo kwa kweli Waalgeria waliyaona kama ni njia ya kujitoa utumwani, yalidhihirishwa na mfululizo wa makala yaliyochapishwa na Ferhat Abbas kati ya 1922 na 1927. Makala haya yalitolewa mwaka 1932 kwa jina *Le Jeune Algerian* (Kijana wa Kialgeria). Katika makala haya, Ferhat Abbas aliushutumu sana ukoloni ambao aliuita "Nguvu bila fikra" na "ubongo bila roho". Kampeni hiyo iliongozwa na chama cha Ulama ambacho kilianzishwa mwaka 1931. Mmoja wa viongozi wake, Shaykh Abd-Hamid ben Badis alitayarisha maazimio ambayo, bila kuupinga utawala wa Kifaransa, yalisisitiza zaidi mabadiliko ya fikra na maadili, na kwa kufanya hivyo maazimio hayo yalizua masuala ya uzalendo na umoja yakawagusa watu wengi, na kuzusha fikra za namna hiyo hiyo Mashariki na Kati. Shaykh Abd alitumia utaratibu unaofanana sana na ule wa demokrasia ya Nchi ya Magharibi. Aidha, alizungumzia mambo ambayo yalionyesha ishara wazi za kutawanyika kwa jamii na kushuka kwa maadili ya watu kwa jumla.

Kitu kingine ambacho hakikujulikana sana kinahusu hali ya kijiografia. Wakiwa viongozi wa *nasab* (nasaba) viongozi wa chama hiki walitoka mikoa mbalimbali, ambayo haikuwa tu ile ya watawala wa Konstantini kama Ben Badis, ila pia ile ya *Tebessa,* Mila na *sidi Ukba.* Chama hiki hakikuishia tu katika kuunda "Duara ya Maendeleo" katika nyanda za Kati, hasa Algeria na sehemu nyingine za miji, ila kilidhamiria kuenea pote hata katika sehemu za nchi "zisizojulikana". Shaykh Bashir al-Ibrahimi aliupa msisimko mkubwa sana mji wa Tlemcen na jitihada za namna hii ziliongezeka kwa kasi zikichukua maambo ya hotuba, vyama vya kirafiki na vyama vya kusaidiana.

Kuenea kwa kasi kwa chama hicho huelezewa mara nyingi kama matokeo ya migongano ya msisi ya kidini ambayo haieleweki kwa urahisi kwa watu wa nje. Hata hivyo, mwamko huo ulikuwa ni mwanzo wa mshikamano wa umma katika maswala ya kijumla, hasa kwa jamii ambazo hadi wakati huo zilikuwa zimejitenga. Shaykh Ben Badis na rafiki zake walionyesha mfano kwa kuupa Uislamu wa Afrika ya Kaskazini mtingishiko ambao ulikuwa haujafikiriwa katika karne nyingi. Kipindi hicho kilikuwa muhimu sana

katika historia ya jamii ya Algeria.

Ingawa leo hii itaonekana kuwa kitu cha ajabu lakini sherehe za kufikia miaka mia moja tangu Wafaransa waingie Algeria hazikuzusha chuki zozote ambazo sisi, tunaoishi miaka ya sasa ya kujikwamua kutoka katika ukoloni, tumezoea kuwa nazo. Kwa Waalgeria wengi ambao walihusika sana na madai ya haki na usawa, sherehe hizi zilileta matumaini kwa mara nyingine ingawa baada ya muda mfupi iligunduliwa kuwa matumaini hayo yalikuwa kazi bure. Viongozi wa Kiislamu katika utawala hasa wakuu waliochaguliwa, makadhi na wengine, walishindana, bila aibu, wao kwa wao, katika kutaka kuwapendeza Wafaransa. Hivyo walipuuza utaratibu uliofuatwa na utawala wa jadi. Kwa bahati mbaya, sifa zisizo kifani ambazo walipewa masetla ziliwafanya Wafaransa waamini kuwa siasa zao zilikuwa bora sana Algeria. Waliishikilia imani hii kwa muda mrefu sana.

Katika Tunisia ndiko mwamko wa kitaifa ulivuma kwa nguvu karibu sawa na ule wa Misri. Katika kipindi tunachokiongelea, mawazo ya zamani ya Ottoman yalififia kati ya mabwanyenye na badala yake wakaweka matumaini yao katika kanuni za Wilson na utaifa kama ilivyokuwa katika *Wafd* ya Misri. Shaykh Abdel-Aziz al-Thaalibi (Taalbi) na rafiki zake waliamua kuelezea madai yao mbele ya umma wa Wafaransa wenyewe, hasa kwa wale waliofuata itikadi za kijamaa. Kijarida chao, *The Martyrdom of Tunisia* (Mashahidi wa Tunisia) (1920), kilielezea kwa undani kuzorota kwa utawala wa kikoloni. Waliazimia kuirudisha Tunisia katika uhuru wake kwa kuunda chama cha *Katiba* kijulikanacho kama *Desturi*, mnamo Februari 1920. Hata hivyo, kwa kufuata mapendekezo yake ya kimapinduzi ya awali, chama hiki cha *Desturi* kilichapisha manifesto iliyopendekeza mabadiliko. Hati hii ilikamatwa na watawala wa kikoloni. Mikataa aliyotoa Ben Nasir katika machapisho ya tarehe 3 Aprili, 1922, ilishambuliwa vikali na wakoloni ambao waliamua kumtishia kifungo. Hata hivyo mwaka uliofuata, maagizo na amri za Gavana Mkazi vilitolewa ili kuanzisha mabaraza ya kadhi na pia mabaraza ya Wawakilishi katika ngazi za majimbo na taifa. Wizara ya Sheria ilikuwa imeundwa tayari na ilikuwa chini ya mtoto wa mwongozi wa dini aitwaye Khayruddin. Hayo yalikuwa matokeo kidogo sana tukizingatia kuwa kampeni hii ilikuwa imeungwa mkono na utawala wa ndani na ule wa nchini Ufaransa. Shaykh al-Thaalibi alikaa kifungoni muda wa miezi kadhaa. Hata hivyo kufunguliwa kwake hakukusaidia kuleta umoja katika chama chake. Kilijigawa katika vikundi viwili ambavyo navyo havikuwa na harakati za kutosha. Katika mawazo ya kikoloni siasa laini kama uzoefu wa Maitre Guellati ilivyoonyesha, kila mara hutiliwa mashaka.

Harakati dhidi ya ukoloni katika Tunisia hazikufanywa na wasomi tu wakati wa kipindi hiki. Ziliuhusu pia umma kwa jumla, ingawa uongozi ulikuwa zaidi katika mikono ya kikundi kidogo cha wale walioelimika kwa misingi ya vyama vya Ulaya vya Wafanyakazi. Wawili kati ya viongozi hawa walikuwa Muhammad Ali na Tahar al-Haddad. Maisha ya kusafiri huku na huko ya Muhammad Ali yalikuwa yamemfanya akutane na mawazo ya ujamaa wa Kijerumani na hata kumfanya awe rafiki wa Enver Pasha ambaye pengine ndiye mtu pekee, kwa wakati huo, aliyeelewa barabara njia za kuunganisha mawazo ya kimsingi ya nchi za magharibi na yale ya kitaifa yaliyopendelewa

na umma wa kiislamu. Haddad aliyaongeza mawazo ya Muhammad Ali, ambayo yalikuwa ya uzoefu wa nchi za nje, kwa kuzingatia pia matatizo ya ndani. Alizungumzia maswala ya wafanyakazi na yale ya wanawake akionyesha wazi kuwa aliyaelewa matatizo hayo kwa undani. Makuli wa Tunis na baadaye wale wa Bicerta waliunga mkono mwito wa Haddad kwa vitendo. Wengine waliochukua hatua hiyo ni wafanyakazi wa kampuni ya saruji ya Hammam Lifu na hatimaye wengine zaidi walijiunga.

Katika mji wa Bierta mnamo tarehe 12 Oktoba, 1924, vyama vya wafanyakazi tisa vilishirikishwa. Viliungwa mkono na chama cha kikomunisti cha Ufaransa. Lakini vilipingwa vikali na sehemu ya Ufaransa ya Chama cha Wafanyakazi wa Ulimwengu (SF10), ambacho kiliona wasiwasi juu ya kuhusika kwa kikundi hicho na masuala ya kiutaifa. Chama cha Desturi hakikutaka kujihusisha na kile ilichokiita ushirikiano wa mapatano. Lakini, baada ya mabadiliko fulani, chama hicho kilikubali, mnamo Februari 1925, kujiunga katika mwungano uliojumuisha vyama vya Desturi, kikundi cha Jadi cha Baraza Kuu, Chama cha Kijamaa, na Chama Kikuu cha Kifaransa cha Wafanyakazi. Utata wa muungano huo pamoja na migongano yake ndio ulifanya matunda yake yasidhihirike, hasa kwa vile kulikuwa na migogoro mingi ambayo ilifuatwa na mapatano au mabadiliko ya msimamo. Hata hivyo, nchini Tunisia vyama hivyo vilidhoofika baada ya kufungwa kwa viongozi wa wafanyakazi na kupigwa marufuku kwa kiongozi kwao mashuhuri Muhammad Ali. Ilikuwa Septemba 1932 chama cha wafanyakazi wa Tunisia kilipoweza kukubaliwa kisheria na ni mwaka 1937 tu ndipo kiliweza kuwa huru kufanya shughuli zake chini ya utaratibu wa*Popular Front* (Chama cha Umma).

Ukinzani dhidi ya akoloni wa Hispania na Ufaransa ulianzishwa na kiongozi wa *Rif* ambaye alijulikana kama Muhammad Ben Abd al-Khattabi (Abdel Karim). Ukinzani huu ulianza kwa nguvu sana na hata uliweza kulanikiwa kwa muda fulani. Kulielezea jambo hili kama "mgomo" na kulifikiria kama ni tukio peke yake ni kutozipa uzito wa kutosha taarifa ambazo wakati huu tunaziona kama ndizo zilizokuwa mwanzo wa mambo yaliyotokea baadaye.

Chama cha Rif kilikuwa hakijakata tamaa katika harakati zake. Uwezo mkubwa wa kijeshi wa Abdel Karim ulisaidia sana katika kuipa Hispania kipigo (Anwal, Julai 1921) ambacho ni mojawapo ya maafa makubwa yaliyotokea wakati wa Vita vya Ukoloni. Wahispania walipata kipigo kingine cha namna hiyo mwezi Novemba 1924 walipolazimika kuihama Shafshawin ili kuimarisha sehemu ya jeshi lao iliyokuwa mbele. Abdel Karim alikuwa mtoto wa Kadhi wa himaya ya Hispania. Kwa hiyo alikuwa amezaliwa na kukulia katika pande zote mbili. Alipata mafunzo yake kwa kipindi fulani katika Chuo Kikuu cha Karawiyyin mjini Fez, ambako inaaminika ndiko alikoanza kujihusisha na masuala ya Kiislamu ya wakati ule. Alifahamika zaidi na watu wa wakati



**24.1** Bw. Abdel Karim )1882-1963) - wakati akiwa Kadhi wa Mellila na kiongozi wa ukinzani wa Morocco dhidi ya ubeberu wa Hispania wakati wa Vita vya Rif., 1921-1926



**24.2** Wakati wa Vita vya Rif. Majeshi ya Hispania yakionyesha vichwa vya askari wa Abdel Karim.

ule kama kiongozi wa dini ya Kiislamu kuliko kama kiongozi wa siasa. Licha ya ujasiri w kijeshi, alikuwa mtu mnyofu, mwadilifu na mwenye umahiri wa siasa. Sifa hizi zilimwezesha awe na uwezo mkubwa sana kimataifa hata kuwazidi viongozi waliofanya harakati kama yeye huko Libya kama vile Sulayman al-Baruni, Ramdan Shatiwi, na hata Umar al-Mukhtar. Mabadiliko aliyoyaleta katika ukoo wake wa Beni Warighil na jamii za jirani yalikuwa ni ya kudumu. Aliviongoza vikundi hivi, kwa kusaidiwa kwa namna fulan na migogoro ya kiukoo iliyokuwepo, hadi kuweza kurudia upya sheria za Kiislamu. Alipig marufuku viapo vya jumla na kuzuia kuwepo kwa vikundi vya udugu. Vilevile aliwakataz wanawake walioolewa wasicheze ngoma. Hata kabla ya ushindi wa Anwal, mkutano uliofanyika Al-Kamati ya Beni Warighili, Temsaman, Beni Tuzin na Rukhuya uliuimarish muundo wa serikali ya Rif. Baadhi ya wanahistoria wanaamini kuwa "taifa la Jamhuri ya Rif" lilitangazwa mnamo tarehe 18 Januari na nia yake ilikuwa ni kuubadilisha utawala w zamani bila kubomoa mambo yake mazuri, kama vile utaratibu uliokuwepo wa kushaurian na kushirikiana kati ya vikundi mbalimbali.

Wakati wa Vita vya Rif. Majeshi ya Hispania yakionyesha vichwa vya askari wa Abdel Karim.

Abd al Karim alikuwa ameanzisha uhusiano na Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa (PCF), ambacho kiliitisha mgomo wa kumuunga mkono. Wakati wa mgomo huo ambao ulitokea tarehe 12 Oktoba, 1925, wafanyakazi wengi wa Kifaransa waliandamana kupinga vita vya kikoloni nchini Morocco. Kulikuwa pia na kampeni ya umma wa Ufaransa dhidi ya vita hivyo ambavyo iliongozwa na vikundi vingi vikiwemo Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa (PCP), *The Young Communists* (Vijana wa Kikomunisti), Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi (CGTU), *Association Republicaine des Anciens Combatants.* (ARAC) (Chama cha Taifa cha Wapiganaji wa Zamani) na kadhalika. Kuanzia mwezi Aprili mwaka 1926, utawala wa serikali ya tatu nchini Ufaransa uliazimia kutumia nguvu bila kiasi ili kumwangusha Abdel Karim. Jambo hilo lilifanikiwa mwezi Mei, 1926. Lakini sehemu ya Moroco iliyobaki haikutaka kuingilia. Hata hivyo, ufumbuzi wa kivita ambao uliiwezesha Hispania kujiimarisha katika kanda iliyokuwa chini yake, haikuweza kung'oa kabisa umaarufu wa mashambulio ya Abdel Karim.

Katika Morocco yenyewe, tamko la kifalme au *Zahir* katika Kiberiberi lilifanywa tarehe 16 Mei 1930. Tamko hili lilizingatia mila za jadi za Kiberiberi katika mfumo wa sheria wa ukoloni wa kifaransa. Vilevile liliwapa vijana waliokuwa na hali nzuri kiuchumi fursa ya kuinua hali zao na akawa mwanzo wa umma mzima kuharakatika. Hii ilisababisha migogoro kutokea kwa vile ilifikiriwa kama ni shambulio kwa dini ya Kiislamu na jitihada ya kuigawa nchi kwa kudharau makubaliano ya mwaka 1912. Ingawa zilikuwa ni hatua zilizokuwa zimetarajia kusawazisha mambo yaliyohusu sehemu moja, matokeo yake yaliuhusu ulimwengu wote wa Kiislamu. Nchini Morocco hatua hizi zilizusha upinzani ambao hapo mwanzo ulikuwa hafifu na wa kisirisiri, hasa katika miji mikubwa miwili au mitatu hivi.

Katika muda wa miezi mitatu tangu tarehe za Juni hadi tarehe 30 Septemba 1930, kulikuwa na vituko zaidi ya mia moja ishirini. Sehemu kubwa ya vituko hivi ilitokea katika

misikiti ambako Waislamu walizoea kusali *Latif*, ambayo husali wakati wa dhiki. Vitendo hivi vilionekana kuwa vitisho kwa usalama wa raia kiasi kwamba utawala ulivichukulia hatua kali kama vile kuwafungulia mashtaka, kuwafunga na kuwapiga watu waliohusika. Ujumbe ulitumwa kutoka mji wa Fez kwenda mji mkuu na hatimaye tarehe 31 Agosti watatu katika ujumbe huo walifungwa. Kati yao alikuwemo Allal al-Fasi, kijana msomi kutoka Karaniyyin na Bie Hasan al-Wazzani, ambaye alikuwa amefuzu masomo yake katika Chuo cha Elimu cha Jamii na Siasa mjini Paris. Watu hao wawili walikuwa karibu kuwakilisha ishara ya umoja wa mikondo miwili katika mapambano hayo. Mkondo mmoja ulikuwa wa wale waliopenda mila na jadi, na mkondo mwingine ulikuwa wale waliopenda mambo ya kisasa. Hivyo, kitendo cha kugandamizwa na utawala kiliwasha moto mkubwa zaidi. Idadi ya watu waliowekwa kifungoni iliongezeka na kufikia 150. Kama hapo mwanzoni, maduka mengi yalifungwa kama alama ya kutokubaliana na hali hiyo. Licha ya kupigwa marufuku, sala ya *Latif* iliendelea kusikika katika misikiti. Mara kwa mara, kulikuwa na mapambano mabarabarani. Hivyo kiungo cha himaya kilionekana kulegalega na hata kuvunjika.

## *Harakati na Siasa za Kitaifa katika Mika ya 1930*

Miaka kumi kati ya miaka ishirini iliyopita kati ya Vita Vikuu, hapakuwa na maendeleo yoyote muhimu katika uhusiano kati ya Ufaransa na Maghreb. Hapana shaka kwamba hali ya kiuchumi haikuwa nzuri kwa jumla. Hata kabla ya mpomoko wa uchumi uliosababishwa na Vita Vikuu vya Kwanza kuisha, bei za bidhaa kuu duniani zilishuka. Hali hii iliifikia Maghreb mwaka 1932 ambapo hali mbaya iliyokuwepo tangu mwaka 1952 ikaongezeka zaidi. Hali hii iliendelea kwa muda wa miaka kumi zaidi. Wakati huo wote, uhusiano kati ya wenye raslimali, yaani masetla wa Kifaransa, na wafanyakazi, yaani Waalgeria ulizorota sana. Maendeleo katika utumiaji wa mashine za kulimia, upangaji wa sera, ushirika na hata uundaji wa vyama vya wafanyakazi serikalini yaliwawezesha Wafaransa kujiimarisha katika makoloni yao. Hata hivyo, utawala huo haakuweza kurekebisha mtindo wake mbaya wa uongozi. Uhusiano kati ya kuzorota kwa uchumi, ambako kulisababisha tofauti za utajiri zijitokeze, na madai ya kisiasa ulijidhihirisha. Hata hivyo uhusiano huo unahitaji kuelezwa kwa undani zaidi. Inaonekana kuwa mabadiliko ya jamii na nia ya kurudisha hadhi za jadi ndivyo vilikuwa vitu muhimu, hata zaidi ya tofauti za utajiri, katika kuleta mwamko Afrika ya Kaskazini. Kwa vyovyote vile, kulikuwa na sababu nyingi zilizosababisha msukumo wa mapambano, ambazo mara nyingi hazikuambatana na vikundi vya vyama vya siasa. "Wazalendo" wa Morocco, waliojulikana kama Wataniyyin, walikuwa hasa watu matajiri wenye kisomo. Kikundi cha "Nyota ya Afrika ya Kaskazini" ambacho kilianzishwa Paris mwaka 1924, na wahamiaji kutoka Maghreb, kilikuwa bado hakijajiimarisha nchini Algeria. Chama cha *Destur* kilikuwa bado hakijajitokeza tangu kupigwa marufuku. Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa (PCF) hakikuunga mkono kikamilifu mawazo yake ya kimapinduzi katika makoloni. Misukumo yoyote iliyohusu utendaji haikutekelezwa. Hivyo, mawazo mengi ya kisiasa yalijitokeza tu katika vilabu,

kamati, vikundi visivyo na majina na hata katika kutawanyika kwa hisia binafsi badala ya vyama vya siasa.

Ingawa utawala huo haukuweza kuzielewa njia hizi za kujieleza zisizo za wazi sana. Ulijua sana namna ya kutumia ubinafsi na migongano kati ya vikundi kwa faida yake. Vilevile ulipuuza sana malalamiko ya kisiasa. Ulikuwa na uwezo mkubwa zaidi upande wake na hata ukubalifu wa jumla. Lakini ulisahau kuwa kulikuwa na dhoruba ambayo ilikuwa inaanza kutoka kwa chini ambapo juu palionekana kuwa shwari. Ili ikiwa kulitokea mlipuko, serikali iliwalaumu "wakorofi" wa ndani na nje, au "wakomunisti". Msimamo huu uliwaachilia wale wenye siasa kali za kijadi au wahalifu.

Mbinu Mpya na Misisimko

Bourguiba na rafiki zake Bahri Kika, Tahar Safar na Dr. Matari, hawakutegemea kupata kila kitu walichonuia au kukosa kabisa. La hasha, walikuwa na makusudi ya kujipenyeza kisiasa kwa kutoyahusisha mambo ya kidini. Walimtetea raisi wa Chama cha Ushirika cha Tunisia ambaye alipatana sana na serikali. Kwa kumtetea kiongozi huyo Bourguiba na wenzake waliweza kuwavutia watu upande wao. Vilevile hawakuficha lawama na upinzani wao dhidi ya Msikiti Mkuu na Makabaila wa Tunis ambako ndiko wanachama wengi wa *Destur* walitokea. Ilikuwa imedhihirika tayari kuwa chama hicho sasa kilikuwa kimeingiliwa na kikundi kimoja cha watu wa Sahel ambacho kilikuwa kimezingatia mbinu za kijeshi na kimapinduzi. Kikundi hicho ambacho kilijulikana kwa jina la *Neo-destur* kilikuwa kimenuia kuchochea mwamko wa siasa katika wilaya zote kama mojawapo ya azma zake. Hivyo haikuwa ajabu kwamba mgawanyiko uliosababisha kuundwa kwa Chama cha *Neo-Destur* uliotokea wakati wa mkutano mkuu ambao ulifanywa katika sehemu za mashambani za Kasri Hilal tarehe 12 na 13 Mei, 1933. Wakati huo mapigano na chama cha wakazi au *Redi Residence*, yalitokea kwa nguvu zaidi, kama vile yale ya Monastir na Moknin. Kashfa za kuchukiza zilitolewa ili kuhalalisha ugandamizaji, na Bourguiba, ambaye alipinga hatua hizi, alipelekwa pamoja na wenzake kifungoni sehemu za kusini mwa Tunisia, tarehe 3 septemba 1934. Lakini, ingawa alikuwa kifungoni aliendelea kupigania haki.

Katika Algeria, utawala ulijaribu kuzuia kuenea kwa chama cha "Ulama". Utawala huo ulitumia mbinu ya kukigonganisha chama hiki na vikundi vya udugu wa kidini na viongozi wa dini. Baada ya utawala kugundua kuwa watu wengi walikusanyika kuwasikiliza wahubiri wapya, uliwazuia wasihutubie misikitini. Watu waliovutiwa na wahubiri hao waliwafikiria kama viongozi wa dini waliolet fikra mpya za Uislamu. Tarehe 16 Februari, 1933, mwongozo rasmi ulitolewa na utawala ambao ulijulikana kama "Tangazo la Michael". Jina hilo lilitokana na mtu aliyeandaa mwongozo huo. Tangazo hilo lilifuatiwa na matangazo matatu ya nyongeza. Maandamano yaliyofuata hayakufanywa na waumini wa dini tu bali pia wanachama wa vyama vya wafanyakazi na watu wenye siasa za kimapinduzi; mwungano ambao ungetegemewa kuwa na athari kubwa. Ni kweli kwamba wakati huohuo palitokea mgongano kati ya mwelekeo wa Chama cha Kikomunisti na ule

wa Chama cha Uzalendo. Tofauti hizi hazikuisha hata baada ya kuunganishwa tena kwa chama cha kikomunisti cha wafanyakazi (CGT) na Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi (CGTU) mnamo mwaka 1935. Baada ya miaka kadhaa ya mapambano ya kisirisiri, Chama cha Nyota ya Afrika ya Kaskazini kilijitokeza hadharani nchini Algeria mwezi Juni 1933. Rais wake, Mesali Hadj alikuwa akitamka neno "Uhuru" tangu mwaka 1927. Na sasa, kati ya wasiwasi uliokuwa unaanza kuonekana, palitokea mgomo dhidi ya Wayahudi mjini Constantine mwezi Agosti 1934. Haikuwa dhahiri kama mgomo huo ulikuwa ni hila, mlipuko wa hasira, kisingizio cha kukwepa masuala makubwa zaidi au matokeo ya kughadhabishwa. Lakini vyovyote vile, mgomo huo ulisababisha mapigano ya mitaani ambayo yaliwapa hofu wanasiasa wote kwa jinsi yalivyokuwa makali sana. Hata hivyo kwenye upigaji kura uliofuata mnamo mwezi Januari 1935, wagombeaji kutoka chama cha upinzani cha Dr. Bendjellul walishinda katika mji wa Constatine. Matokeo haya yalidhihirisha upande ambao watu walivutiwa zaidi. Ingawa mshindi alikuwa ni mtu aliyesilimishwa katika mawazo ya Kifaransa, aliukasirisha utawala hata kufikia hatua ya kurauondoa. Ni dhahiri; kwamba katika wakati huo wa mapambano kitu ambacho watu walijali zaidi siyo nadharia za siasa ila mapendekezo au hata matamshi yanayoweza kuwachochea watu.

Nchini Morocco, masetla walikuwa wameghadhabishwa na kushuka kwa hali ya maisha na pia kukasirishwa kwa sababu ya masharti kadhaa ambayo walikuwa wamewekewa na utawala, hivyo waliamua kutoa mkataa. Tukio hili, ambalo lina maana sana kihistoria, lilitokea siku ile ambayo kulitokea machafuko mjini Paris, tarehe 6 Februari 1934. Pia shughuli za kizalendo za uchapaji zilianzishwa Morocco wakati huo. Allal Al-Fasi alianza kujitokeza kama kiongozi wa Kamati ya utendaji wa Moroco. Kamati hiyo ilipendekeza *Mpango wa Uongozi* tarehe 1 Desemba 1934, kama ungekubalika, ungeielekeza himaya hiyo katika mkondo wa mwanzo na mawazo na msimamo wake. Katika Kanda ya Hispania, Torres na Nasiri walikuwa wameanza kuonyesha upinzani waziwazi. Walikuwa wameanza kuwashirikisha watu wa bara na hata kujaribu kumhusisha kiongozi ambaye hapo baadaye alijulikana kama Mfalme Mohammed V, katika maandamano ambayo yalifanyika mjini Fez Tarehe 10 Mei, 1934.

Kuanzishwa kwa Mpango huo kulifanyika wakati mmoja na kung'olewa kwa masalio ya upinzani sehemu za kusini. Hivyo historia sasa ilichukua mkondo mpya ambao alikuwa tofauti sana na ule wa zamani ulioendelezwa zaidi ya wakati wake na mawazo ya Lyautey na Wizara ya Mambo ya Wenyeji. Kufanyika kwa mambo haya wakati mmoja kulikuwa na maana siyo kwa Morocco tu bali pia kwa sehemu zingine. Kuzimwa kwa ukinzani huu kulikuwa pia mwisho wa vyama vya Kiarabu. Mabadiliko ya kijamii ambayo yalikuwa yamedhoofisha ushirikiano wa zamani katika Algeria na Tunisia, yaliweza pia kuunda ushirikiano wa namna nyingine. Mabarabara ya miji mikubwa na hata masoko vijijini vilibadilika kuwa sehemu za vituko vya wananchi. Vikundi vipya vilivyoundwa kufuatana na tabaka au itikadi vilijitokeza. Katika nchi hizi tatu, na hasa Algeria ambako Waziri al Regnier alikuwa amejihusisha zaidi na upelelezi, jibu pekee la serikali kwa matukio haya lilikuwa ni kuingilia shughuli za uchaguzi na kurudisha mfumo wa

ugandamizaji.

Kukataa kuchukua hatua kwa utawala hakuwezi kuelezewa tu kwa kutazama hatari ambayo ilikuwa imeanza kuonekana upande wa pili wa Mto Rhine na jinsi mambo yale yalivyoifanya Ufaransa izibe masikio. Mielekeo ambayo ilikuwa imechukuliwa na pande zote tatu, yaani Ufaransa, utawala wa kikoloni na vyama vya siasa vya kizalendo, ililingana na matakwa ya pande mbili za kwanza, yaani Ufaransa na utawala wa kikoloni. Pande hizi zilipendelea kubaki na hali ileile au Status quo. Upande wa tatu, yaani vyama vya kisiasa vya kizalendo, ulikuwa haujaweza kuipinga mielekeo hii kwa dhati. Kama masharti ya kuungwa mkono na Ufaransa, masetla waliokuwa Afrika ya Kaskazini hawakutakiwa waanzishe mambo yao wenyewe. Mathalani, masetla waliokuwa Algeria walijiita "Waalgeria" ili wanufaike kwa kulitumia jina hilo. Hata hivyo, hawakutaka kujiingiza mno katika masuala ya Algeria kama nchi yao kwa kuogopa mgongano wa Waislamu waliokuwa wengi. Kufuatana na matamshi hayo, Algeria ilikuwa ni Ufaransa, lakini Ufaransa isiyo na demokrasia. Mambo yalikuwa vivyohivyo nchini Tunisia na Morocco.

## *Hitimisho la Muda*

Kipindi tulichokizungumzia hapa hakikuweza kuyaelezea mambo yote kinaganaga. Hata hivyo, tunatumaini kuwa tumeweza kuonyesha kuwa hali iliyokuwapo Maghreb wakati huo lazima itazamwe kama kitu kilichokuwa kikifanyika kichinichini. Hivyo, mambo yaliyofichama yalikuwa na maana zaidi kuliko mambo yaliyojitokeza waziwazi. Kati ya mambo matatu, demokrasia ya kibwanyenye, ujamaa wa kimataifa na uthibiti wa watu kutambua nafsi zao, ni jambo hili la tatu ambalo lililojidhihirisha. Lakini hapo mwanzo haikuwa rahisi kujua uzito wa mambo hayo, na hasa kwa vile kulikuwa na migongano kati ya vikundi vinavyopingana kama vile wale wenye kukazia Uislamu na wale waliopendelea mawazo ya kiraia; wanaopendelea mambo ya Ulaya na wanaopendelea Umoja wa Kiarabu; wenye siasa laini na wale wenye siasa kali. Mnamo mwaka 1935, hakuna yeyote ambaye angeweza kutabiri nani angeshinda kati ya mielekeo hiyo miwili au kama mfumo wa kikoloni ungeendelea kuwepo. Tunaweza tu kuhitimisha kwa kusema kwamba historia iliyaachilia juujuu mambo ambayo yangetokea, au huenda bado yakatokea baadaye, ili kutoa mwelekeo wa hali itakavyokuwa katika awamu za hapo baadaye.

# 25

## Siasa na Utaifa katika Afrika ya Magharibi, 1919-1935

Kinyume cha hali ilivyokuwa katika Afrika ya Kaskazini utaifa na shughuli za kisiasa katika Afrika Magharibi katika kipindi kati ya Vita Vikuu vya Dunia kwa jumla vilizingatia mkondo usio wa kidini. Hiyo ni mosi; pili, malengo ya shughuli hizi katika Afrika Magharibi yalikuwa ni kuurekebisha ukoloni wala sio kuutupilia mbali kama hali ilivyoiuwa katika nchi nyingi za Afrika Kaskazini. Hata hivyo inaonekana kuwa kama hali ilivyokuwa katika Afrika Kaskazini shughuli hizo zilidhihirika zaidi katika sehemu za mijini na miongoni mwa wasomi na mabwenyenye kuliko ilivyokuwa kati ya umma na watu wa sehemu za mashambani, ingawa kama itakavyoonekana baadaye, hii haina maana kuwa umma na watu wa mashambani hawakujua wala kujihusisha na hali ya ukoloni. Mwisho kama ilivyokuwa katika Afrika Kaskazini utaifa katika Afrika ya Magharibi ulikuwa zao la hali ya ukoloni yaani utambuzi au urazini uliotokana na ukosefu wa usawa, dhuluma na ubaguzi uliokuwemo katika mfumo wa kikoloni.

Katika kipindi kinachochungumziwa, utaifa wa Kiafrika na shughuli za kisiasa katika Afrika ya Magharibi uliumbika kutokana na mambo kadhaa ambayo huonyesha asili yake ya kutohusiana na dini. Jambo la kwanza lilikuwa ni athari za Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia kwa Afrika. Jambo hili limejadiliwa kwa undani zaidi katika sura ya 12. Inatosha kusema hapa kuwa uandikwaji wa lazima wa Waafrika katika jeshi ni jambo lililochochea hasira kubwa hasa katika makoloni ya zamani ya Ufaransa ya Afrika. Pili vita hivyo vilimdhihirishia Mwafrika kuwa Mzungu hakuwa mtu mwenye uwezo zaidi kuliko wengine na kwa hiyo hivyo iliwezekana kupambana naye. Tatu, baada ya vita hivyo Waafrika waliokuwa waaminifu kwa Mzungu walitarajia kutunzwa kwa kupewa vitu kama vile ridhaa na kukubaliwa kuhusika zaidi katika uendeshaji wa mambo yao wenyewe. Bila shaka mambo haya yote yaliwafanya Waafrika wengi wa sehemu hiyo kuwa tayari zaidi, kuliko ilivyokuwa hapo nyuma, kujishughulisha na upinzani na pia kujiunga na vyama vya kuupinga ukoloni.

Jambo la pili lilikuwa ni mfumo wa kikoloni wenyewe. Mfumo huu ulipata mashiko katika kipindi hiki na namna zake za ubaguzi wa rangi zikadhihitika zaidi. Ni katika kipindi hiki ambapo zilipitishwa sheria kadhaa ambazo zilizidisha zaidi uwezo wa watawala wa kijadi na kuondolea kabisa kundi la wasomi na makundi ya wataalamu kutoka shughuli za utawala wa nchi zao wenyewe. Kitu kilicholifanya jambo hili kuleta matata zaidi ni kwamba katika kipindi hicho idadi ya kundi la wasomi na ya kundi la wataalamu

iliongezeka zaidi kutokana na kuenea zaidi kwa elimu ya kimagharibi katika sehemu hizo na pia kwa sababu ya watu wengi zaidi kupata nafasi za kusomea ng'ambo.

Lakini jambo lenye umuhimu zaidi lilikuwa ni hali za kiuchumi ya kipindi kati ya Vita Vikuu vya Dunia. Mgogoro wa kiuchumi na mabadiliko katika uchumi wa makoloni, mambo ambayo yamekwishazungumziwa hapo awali, viliathiri vibaya makundi ya waliobora kama vile wanasheria, biashara, makundi yaliyoandamia makundi ya watu bora, yaani walimu, wafanyakazi wa serikali na wafanyakazi kwa ujumla na kuwafanya watambue zaidi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma, unyanyasaji wa mfumo wa kikoloni. Katika Sierra Leone mchanganyiko wa kwa matabaka ya wasomi, wafanyabiashara wa Kiafrika na wasiokuwa na kazi walionekana hadharani katika ghasia za mwaka 1919 kuhusu ugawaji wa mchele na dhidi ya Wasyria na pia katika mgomo wa wafanyakazi uliotokea mwaka huohuo. Nchini Gambia pia upandaji wa bei ulikuwa na athari zake za kijamii na kisiasa ambazo zilizusha uporaji wa hapa na pale na wizi wa vitu vidogovidogo na pia mgomo wa mabaharia wakidai mishahara mizuri zaidi. Pia ulileta uundaji wa vyama vya wafanyakazi hasa chama cha *Gambia Native Defence Union*. Mshuko wa ghafula wa bei uliotokea mwaka 1921 ulileta upinzani zaidi kutoka kwa wafanyabiashara wa Kiafrika ambao baadhi yao walikuwa wamefilisika. Kwa hivyo, kwa ujumla matatizo haya yote ya kiuchumi yaliwafanya waandishi wa habari na magazeti wa Afrika ya Magharibi kuwa na lengo moja la kuhimiza mabadiliko ya mfumo wa Kikoloni.

Jambo la mwisho lililosababisha kuwepo kwa utaifa na shughuli za kisiasa lilikuwa ni kuanzishwa kwa *Pan-Africanist* (Umoja wa Waafrika wote) na hasa shughuli za Dubois na Garvey hasa za miaka ya baada ya 1920. Shughuli hizo zimezungumziwa zaidi katika sura ya 19. Lakini ni muhimu kutaja hapa kuwa makongamano mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Waafrika Wote yaliyoongozwa na Dubois mjini Paris mnamo mwaka wa 1919, mijini London, Brussels na Paris mnamo mwaka 1921, mijini London na Lisbon mnamo mwaka wa 1922 na mjini New York mnamo mwaka wa 1927, ambayo yalihudhuriwa na washiriki kutoka Afrika ya Magharibi yalisaidia kuzifanya shughuli za kizalendo kuwa za kimataifa na pia kuyafanya mapambano dhidi ya ukoloni barani Afrika kwa jumla na hasa katika Afrika ya Magharibi kuwa jambo la kimataifa. Pia makongamano hayo yalisaidia sana katika kuimairisha urazini wa watu weusi wote ulimwenguni kuwa wao kwa pamoja walikuwa taifa la walioonewa na kudhulumiwa. Jambo hili lilileta kupatikana kwa wafuasi zaidi wa mapambano dhidi ya ukoloni katika Afrika ya Magharibi.

Kwa kuizingatia historia hii tutavichunguza vyama na mashirika yaliyoundwa katika kipindi kati ya vita vikuu viwili kwa madhumuni ya kuyaelezea malalamiko na madai ya wazalendo katika makoloni ya Waingereza na Wafaransa.

## *Siasa na Utaifa katika Makoloni ya Waingereza ya Afrika ya Magharibi*

### Vyama na Miungano ya Vijana

Mashirika yaliyojitokeza zaidi yalikuwa ni vyama na miungano ya kimbari ya vijana. Hapana shaka kipindi kati ya vita vikuu kilishuhudia uundaji mwingi wa mashirika ya kimbari, ya kijamii, kifasihi, ya wanafunzi wa zamani, ya kujitolea na mashirika ya vijana kama vile vilabu na miungano katika nchi nyingi za Afrika ya Magharibi. Vyama vingi vya Waigbo viliundwa katika miji ya Nigeria kama vile Ibadan, Abeokuta na Lagos. Katika "*Colony*" na maeneo ya Asante nchini Gold Coast (Ghana) pekee kulikuwa na vilabu na mashirika kama hayo hamsini ambayo mengi yao yaliundwa kati ya 1925 na 1930. Ni kutokana na baadhi ya vilabu na mashirika haya ambapo Danguah aliandaa chama cha muungano wa vijana (*Youth Conference Movement)* ambao ulikutana kwa mara ya kwanza katika Accra mnamo mwaka wa 1929. Katika Gold Coast na Siera Leone Wallace Johnson alianzisha Umoja wa Vijana (*Youth League)* na pia Umoja wa Vijana wa Afrika Magharibi (*West African Youth League*). Nacho chams cha Vijana wa Nigeria (*Nigerian Youth Movement*) kilianzishwa mnamo mwaka 1934.

Vilabu na vyama hivi vyote viliongozwa ama na makundi ya watu bora waliosomeshwa na wamisheni au wanasheria vijana, madaktari na wafanyibiashara. Ingawa lengo la viongozi hawa lilikuwa ni kuuchukua uongozi wa kisiasa kutoka mikononi mwa wazee wafuasi wa utaifa wasiopendelea mabadiliko, tukiacha shirika la Vijana wa Afrika ya Magharibi, hapakuwa na kiongozi hata mmoja kati yao aliyetoa madai ya kimapinduzi hata ingawa hali ya uchumi ilikuwa inaendelea kuharibika zaidi katika miaka ya 1920 na ya 1930. Madai yao yalijikita zaidi katika nafasi na hali bora zaidi za elimu, elimu ya chuo kikuu, ujira na mishahara ya juu zaidi, usawa wa uwakilishi katika bunge na halmashauri za watendaji, kuondolewa kwa ubaguzi wa kitaifa, najiri katika kazi za serikali, kutolewa kwa nafasi za kiuchumi kwa Waafrika na uhusiano bora zaidi baina ya watawala wa kikoloni na Waafrika. Ni madai kama hayo yaliyotolewa na Mkutano Mkuu wa kwanza wa Vijana mijini Accra mnamo mwaka wa 1920, na yale yaliyotolewa na Mkutano wa Vijana wa Nigeria*Nigerian Youth Movement - NYM*).

Kati ya vyama vyote hivi kilichokuwa cha kimapinduzi ni kile tu kilichoongozwa na Wallace Johnson aliyekuwa kiongozi wa wafanyakazi kutoka Sierra Leone na ambaye alisomea Moscow katika 1941-1932. Alirejea Afrika Magharibi akiwa na lengo la kuunda chama kipya cha kisiasa kwa msingi wa ulioundwa kuzingatia maslahi ya wafanyakazi na ujira na wasiokuwa na kazi wa sehemu za mijini akiwa na lengo la kuondolea mbali mfumo wa kikoloni. Alianzisha Umoja wa Vijana (*Youth League*) katika Gold Coast kwa kuwaunganisha wafanyikazi na kuwahamasisha dhidi ya mfumo wa kikoloni kwa kuyatumia maandishi yake makali na yenye kuchochea maasi na kwa kuyatumia kwa werevu matatizo yaliyokuwemo nchini hasa ukosefu wa kazi, bei za juu za vyakula, na mtafaruku ulitootokana na kushaka kwa thamani ya kakao iliyouzwa nje kuanzia mwaka wa 1929. Kwa sababu ya shughuli zake hizi alihamishwa Sierra Leone ambapo pia alianzisha matawi ya Umoja wa Vijana mijini Free Town na Bo na pia kuanzisha gazeti lililoitwa *The Sentinal* ambalo lilishambulia hali ya wafanyakazi na sheria za elimu.

Pamoja na kampeni za maandishi ya magazeti na barua za maelezo ya malalamiko umoja huu wa vijana ulishiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na pia ukaamua kufanya migomo. Kwa hivyo walishiriki katika maandamano, ghasia na migomo ya mijini

mjini Freetown, nchini Sierra Leone (1926-1931), na pia mjini Bathurst (sasa Banjul), nchini Gambia (1929). Mjini Accra Umoja wa Vijana chini ya uongozi wa Kojo Thompson, aliyekuwa wakili Accra, na Azikiwe ulishiriki katika uchaguzi wa manispaa ya Accra chini ya Chama cha Mambii ambacho kilipingana na chama kilichokuwa kikiongozwa na wazee na wapinga mabadiliko kama vile Dkt. F.V. Nanka Bruce, na Umoja wa Vijana ukashiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa katika Cape Coast. Umoja wa Vijana wa Nigeria, ukiungwa mkono na gazeti la Azikiwe la Afrika ya Magharibi (*West African Pilot*) pia ulishiriki katika uchaguzi wa mjini Lagos katika miaka ya 1930.

Hata hivyo Umoja huu wa Vijana haukufanikiwa sana. Mafanikio yao katika uchaguzi wa miaka ya baada ya 1930 yalishindwa kuundoa uongozi wa wapinga mabadiliko. Lakini mtindo wa uongozi wa kisiasa wa vyama vya kisiasa vya baada ya mwaka wa 1945 katika makoloni ya Uingereza ya Afrika ya Magharibi ulifaidika na uzoefu ambao viongozi wao waliupata katika Umoja wa Vijana.

## Vyama vya Kisiasa

Pamoja na Umoja wa Vijana vyama vya kisiasa kadhaa viliundwa ili kupigania mabadiliko. Kati ya vyama hivyo kilichojulikana sana kilikuwa kile Chama cha Kitaifa cha Kidemokrasia cha Nigeria (*Nigerian National Democratic Party*) ambacho kiliundwa nchini Nigeria na Herbert Macaulay mnamo mwaka 1923. Katika jumla ya shughuli zake kulikuwemo na uchaguzi wa wabunge waliouwakilisha mji wa Lagos, uendelezaji wa elimu ya juu na uanzishaji wa elimu ya lazima kote nchini Nigeria, kuwapa Waafrika madaraka katika utumishi wa serikali, biashara huru na iliyo nzuri na usawa baina ya wafanyabiashara na wazalishaji mali wa Nigeria. Chama kilitumia mbinu za kawaida katika kufanikisha malengo yake yaani kushiriki katika uchaguzi wa mjini Lagos ambapo kilishinda katika uchaguzi wa miaka ya 1923, 1928 na 1933, pia kufanya mikutano ya hadhara na kutuma ujumbe kwa gavana kwa mfano, katika mwaka wa 1930. Chama hiki kilizitawala siasa za mjini Lagos hadi kiliposhindwa na Muungano wa Vijana wa Nigeria (NYM) katika uchaguzi wa mwaka wa 1938.

## Vyama vya Wafanyakazi

Chombo kingine cha kuwasilishia upinzani dhidi ya ukoloni na pia malalamiko ya wazalendo kilikuwa ni vyama vya wafanyakazi. Hata ingawa vyama vya wafanyakazi havikuruhusiwa wala kutiliwa moyo rasmi vyama kadhaa vilizuka hasa kwa sababu ya upandaji wa gharama za maisha. Baadhi ya vyama hivyo vilikuwa, Wafanyakazi wa Reli Sierra Leone (*Railway Workers Union of Sierra Leone*), Makanika wa Nigeria (*Nigeria Mechanics Union)* ambacho uliundwa mnamo mwaka wa 1919 na Ulinzi wa Wenyeji wa Gambia (*Gambia Native Defence Union*). Silaha za kawaida za vyama hivyo zilikuwa ni migomo, kukataa kununua bidhaa na ucheleweshaji wa kazi. Migomo ya kwanza ilitokea

katika vyama vya wafanyakazi wa reli na migodi. Mgomo wa wafanyakazi wa reli ulitokea nchini Sierra Leone mnamo mwaka 1919 na pia mnamo mwaka 1926. Wafanyakazi wa migodi ya dhahabu ya Ashanti katika Obuasi, nchini Gold Coast, waligoma mnamo mwaka 1924 ambapo mgomo wa wafanyakazi wa mgodi wa makaa ya mawe wa Enugu ulitokea mnamo mwaka 1925. Migomo hii yote ilikuwa kwa madhumuni ya kudai mishahara ya juu zaidi na masharti mazuri ya kazi.

Vyama vilivyounganisha nchi mbalimbali na vyama vya kimataifa - Chama cha Kitaifa cha Makoloni ya Uingereza katika Afrika ya Magharibi.

Zaidi ya mashirika, vyama na vyama vikubwa vilivyokuwa vya sehemu moja au vya kitaifa, kuliundwa chama cha makoloni ya Uingereza ya Afrika ya Magharibi na pia vyama vya kimataifa katika miji mikuu ya watawala wa kikoloni. Chama cha kwanza kilikuwa chama cha Kimataifa cha Makoloni ya Uingereza ya Afrika Magharibi (*National Congress of British West Africa* - NCBWAO) kilichoundwa Afrika Magharibi na cha pili kilikuwa Chama cha Wanafunzi wa Afrika ya Magharibi (*West Africa Students Union* - WASU) kilichoundiwa mjini London.

Bila shaka Chama cha Kitaifa cha Makoloni ya Uingereza ya Afrika Magharibi kilikuwa ndicho chama cha maana zaidi ya vyote vya kizalendo vilivyowahi kuundwa katika Afrika ya Magharibi katika kipindi kati ya Vita Vikuu. Chama hiki kiliundwa kutokana na juhudi za Casely Rayford aliyekuwa wakili na msomi kutoka Gold Coast pamoja na Dkt. Akiwanda Savage kutoka Nigeria na katika maisha yake yote chama hiki hakikuongozwa na watawala wa kijadi bali kiliongozwa zaidi na wataalamu kama vile mawakili, madaktari na wafanyibiashara.

Malengo ya NCBWA yanadhihirika kutokana na maazimio yaliyopitishwa katika mkutano wa kwanza uliofanyiwa mjini Accra kati ya tarehe 11 na 29 Machi mwaka 1929 na ambao ulihudhuriwa na wajambe kutoka Nigeria, Gold Coast, Sierra Leone na Gambia. Katika maazimio haya wajumbe hawakudai kuondolewa kwa muundo wa kikoloni bali walitaka ufanyiwe marekebisho. Mabadiliko ya kikatiba yaliyopendekezwa yalikuwa ni pamoja na kuundwa upya kwa Bunge ili nusu ya wabunge iwe inateuliwa na mfalme hali nusu ya pili iwe inachaguliwa na wenyeji. Wajumbe walilaani kutengwa kwa vyeo vya juu vya utawala kwa ajili ya Wazungu pekee. Waliomba kuwepo kwa mashirika ya manispaa na pia kuanzishwa kwa chuo kikuu cha Afrika Magharibi. Walilalamika juu ya masharti ya kifedha na kibiashara ya baada ya vita vikuu na pia uongezekaji wa uwezo wa makampuni ya kigeni. Marekebisho ya kisheria pia yalipendekezwa na hasa kuanzishwa kwa korti ya rufani ya Afrika Magharibi. Kwa sababu ya kuutambua umuhimu wa magazeti katika maendeleo ya kitaifa wajumbe waliamua kuanda Muungano wa Waandishi wa Magazeti wa Afrika Magharibi (*West African Press Union*).

Marekebisho ya mambo ya usafi na matibabu na pia kutenganishwa kwa makazi ya watu wa rangi mbalimbali na nafasi ya madaktari wa Kiafrika waliokuwa wafanyakazi serikalini ni mambo yaliyozungumziwa kwa undani zaidi. Suala muhimu la ardhi lilizungumziwa na mkutano ukaazimia kwamba "Mwafrika wa kawaida wa makoloni ya Uingereza katika Afrika ya Magharibi alikuwa na uwezo wa kuisimamia ardhi na kulinda

maslahi yake ya ardhi." Jambo la mwisho lilikuwa ni kushutumu kugawanyika kwa nchi ya Togo baina ya serikali za Uingereza na Ufaransa na pia kuwekwa kwa nchi ya Cameroon chini ya serikali ya Ufaransa bila kupata maoni wala kuyafikiria matakwa ya wananchi juu ya jambo hili. Maazimio haya yote yanaonyesha kuwa ama NCBWA kilikuwa chama kisichopenda mabadiliko au kilikuwa chama cha watu wa msimamo wa kadri.

Ujumbe ambao ulikuwa na wawakilishi kutoka Gambia, Sierra Leone, Gold Coast na Nigeria uliende London katika mwaka wa 1920 kuwasilisha malalamiko ya kudai haki kwa mfalme ili atoe kibali cha kuwepo kwa wajambe wawakilishi katika makoloni hayo manne. Kiongozi wa ujumbe huu alikuwa ni F.D. Casely Rayford kutoka Gold Coast. Hata hivyo ombi la NCBWA lilikataliwa hasa kwa sababu ya upinzani wa gavana mkuu wa Nigeria, Sir Hugh Clifford, gavana wa Gold Coast, Guggisberg na pia upinzani wa machifu wa Gold Coast waliokuwa wakiongozwa na Nana Sir Ofori Atta.

Chama kilikutana tena mjini Freetown (Januari na Februari mwaka 1923), mjini Bathurst (Desemba na Januari) mwaka 1926 na mjini Lagos mwaka 1930, ingawa siasa za uhamisho dhidi ya ukoloni ziliendeshwa na kamati za kitaifa zilizokuwa zimeundwa nchini Gambia, Sierra Leone na Nigeria. Mkutano wa mjini Freetown ambao uliungwa mkono kwa dhati na tabaka bora la kijamii la mji huo uliidhinisha katiba ya chama na pia kushughulikia ushirikiano wa kiuchumi kati ya mataifa ya Afrika Magharibi na kuorodhesha kazi za raisi, katibu mkuu, kamati ya utendaji, katibu wa fedha na pia kazi ya kamati kuu ya utendaji wa chama.

Kikao cha mjini Bathurst kiliazimia kuwa wakati ulikuwa umewadia wa Koloni la Gambia kuutumia mfumo wa kuwachagua wawakilishi kwa kuwapigia kura na kuwa sehemu mbalimbali za chama zilipaswa kulifikiria kwa dhati suala la kuwa na Jumuiya ya Makoloni ya Kiingereza ya Afrika ya Magharibi chini ya Gavana Mkuu. Pia mkutano huo ulipendekeza kuanzishwa kwa shule za kitaifa, elimu ya lazima katika sehemu zote za mijini, elimu ya ufundi na kilimo katika sehemu za mashambani, kuanzishwa kwa benki za kilimo na vyama vya ushirika, kuwepo kwa uhuru wa kibiashara na kiuchumi wa Afrika ya Magharibi, kuanzishwa kwa korti ya Rufani ya Afrika ya Magharibi pamoja na kuteuliwa kwa Waafrika katika viwango vya juu vya mahakama.

Je, chama cha Kitaifa cha Makoloni ya Uingereza cha Afrika Magharibi kilifanikiwa kupata nini? Hata ingawa NCBWA iliendelea na shughuli zake katika kipindi chote cha miaka ya baada ya mwaka 1920 fanikio lake kubwa zaidi lilikuwa ni kuanzishwa kwa katiba mpya nchini Nigeria mnamo mwaka 1923, Sierra Leone mwaka 1924 na Gold Coast katika mwaka 1925 ambapo utaratibu wa kuchaguana kwa kura ulikubaliwa. Chama kilifanikiwa pia katika kuendeleza hisia za umoja na za kuwa na lengo moja la kisiasa kati ya viongozi wote wa kisiasa katika makoloni ya Uingereza ya Afrika Magharibi. Zaidi ya mambo hayo chama hakikufanikiwa ama kuleta uhuru wa kiuchumi au kuyaunganisha makoloni manne ya Uingereza yaliyohusika na pia hakikufanikiwa kuimarisha hali ya makoloni hayo au kudhoofisha mfumo wa kikoloni. Kinyume cha mambo ni kuwa kufikia katikati ya miaka ya baada ya 1930 ukoloni ulikuwa umeshamiri zaidi kuliko ulivyokuwa katika kipindi cha miaka ya 1920.



25.1 *Ujumbe wa Chama cha National Congress cha British West Africa uliozuru London katika 1920...*

Siasa Katika Sehemu za Mashambani au Utaifa wa Umma Katika Kipindi Baina ya Vita Vikuu

Kutokana na utafiti wa hivi karibuni inaonekana kuwa shughuli za siasa za utaifa hazikujikita katika sehemu ya mijini tu bali zilidhihirika katika sehemu za mashambani ambapo wahusika walikuwa ni raia wa kawaida pamoja na wakulima, waliosoma na wasiosoma wakiwa katika kundi moja na watawala wa jadi wakiwa katika kundi jingine. Mara nyingine kundi hili la pili liliungana na watu wao dhidi ya mfumo wa kikoloni na wakati mwingine lilishambuliwa na watu hao kwa kuonekana kama maajenti wa ukoloni.

Malengo muhimu ya raia wa sehemu za mashambani yalikuwa ni kujipatia wawakilishi katika Halmashauri mpya za kitaifa zilizoanzishwa na zaidi ya yote kupinga kuongezeka kwa madaraka ya watawala wao wa kijadi na yale ya wakuu wa wilaya (DC) na pia kupunguza au kuondolewa mbali baadhi ya faini au kodi walizotozwa.

Kama utafiti wa hivi karibuni uliofanywa nchini Ghana unavyoonyesha vyombo viwili muhimu viliundwa katika sehemu za mashambani ili kusaidia kuyafikia malengo haya navyo vyombo hivyo vilikuwa ni shirika la kijadi la kampuni za *asafo* yaani shirika la kudumu la raia la huduma za kijeshi au kijamii ambalo lilikuwa halikutawaliwa ama na watawala wa kijadi au viongozi wa kisiasa na pia mashirika mapya kama vile Shirika la Wakulima wa Kakao (*Cocoa Farmers Association*) na Jumuiya ya Wakulima wa Kakao wa Gold Coast (*Gold Coast Federation of Cocoa Farmers*) ambayo yaliundwa katika miaka ya 1910 na 1928. Mbinu zilizotumiwa na mashirika haya zilikuwa ni kama vile maombi ya haki, ucheleweshaji wa kuuza kakao na kuwaondoa machifu uongozini. Baina ya miaka ya 1910 na 1944 kulikuwa na machifu 33 waliondolewa uongozini katika mkoa wa Akyem Abuakwa pekee. Mashitaka ya walioondolewa yalikuwa ni kama vile utumiaji mbaya wa mamlaka, uuzaji usio halali wa ardhi, kudai faini kubwa zaidi ya ilivyokuwa halali na kutekeleza sheria za watawala wa kikoloni zilizohusiana na kodi au kazi ya lazima. Mbinu nyingine iliyotumiwa na raia wa sehemu za mashambani ilikuwa ni kukataa kuuza kakao yao. Kwa mfano katika miaka ya 1921, 1931 na pia 1937 wakulima wa kakao chini ya uongozi wa John Kwame Ayew na Winifried Tete-Ansa walikataa kuiuza kakao yao mpaka bei bora zaidi zilipotolewa.

Kutokana na ushahidi huu wa kutoka Gold Coast inaonekana dhahiri kuwa siasa na shughuli za utaifa za kipindi cha kati ya Vita Vikuu hazikujikita katika sehemu za mijini pekee bali pia zilidhihirika katika sehemu za mashambani ambako waliohusika ni raia wa kawaida na wakulima.

Matokeo ya Shughuli za Utaifa katika Makoloni ya Uingereza ya Afrika ya Magharibi

Swala muhimu la kujiuliza ni kwa nini harakati za kitaifa katika makoloni ya Uingereza ya Afrika ya Magharibi zilifanikiwa kiasi kidogo hivi? Jibu la kwanza na lililo muhimu zaidi ni kuwa sio chama wala umoja wa Vijana uliokuwa na wafuasi wengi na pia hapakuwa na ushirikiano wowote baina ya siasa za sehemu za mijini na zile za mashambani. Kwa sababu hii viongozi wao walichukuliwa kuwa hawakuwa wawakilishi wa watu, na hivi

ndivyo Sir Hugh Clifford pamoja na afisi ya kikoloni walivyowachukulia. Jambo la pili ni kuwa hata ingawa walikuwa wasemaji, si viongozi wa chama wala wa umoja wa Vijana ambao walikuwa tayari kutumia mbinu za kimapinduzi ili kufanikisha malengo yao. Jambo la tatu ni kuwa kulikuweko na migogoro mingi kati ya viongozi wa harakati hizi na hili lilikwamisha sana shughuli zao. Katika kila koloni migogoro ilitokea baina ya wasiopenda mabadiliko na viongozi wa msimamo wa kadri na pia kati ya makundi haya mawili na kundi la viongozi wa kijadi la Wafalme. Mgogoro kama huo ndio uliotokea baina ya viongozi wa Chama na wale wa jamii ya Ulinzi wa Haki za Wazalendo (*Aborigines Rights Protection Society*), na pia baina ya viongozi wa makundi haya mawili katika upande mmoja na lile la watawala wa kijadi likiongozwa na Nana Ofori Atta ambaye alikuwa ni chifu mkuu wa Akyem Abuakwa nchini Gold Coast. Migogoro hii ilidhoofisha sana shughuli za kitaifa katika nchi hiyo. Sambamba na migogoro hii kulikuwepo na kutokukubaliana na pia migogoro ya watu binafsi katika tawi la NCBWA la mjini Lagos. Jambo la nne ni kuwa inaonekana kwamba kule kuweko kwa viti vichache sana vya wawakilishi waliopigiwa kura ambavyo vilitolewa baina ya miaka ya 1923 na 1925 kulileta athari ya kuyagawanya na kwa hivyo kuyadhoofisha kisiasa makundi ya kupigania utaifa. Jibu la mwisho la suala letu ni kifo cha Casey Hayford aliyefariki mnamo mwaka 1930, na ambaye ndiye alikuwa nguzo ya NCBWA. Kwa sababu hizi zote basi kufikia mwisho wa kipindi tunachokichunguza siasa na utaifa katika makoloni ya Uingereza ya Afrika ya Magharibi ilikuwa katika kiwango cha chini kabisa.

## *Shughuli za Kisiasa katika Makoloni ya Ufaransa ya Afrika Magharibi Kati ya 1919-1935*

Kutokana na ushahidi mchache unaopatikana kwa sasa inaonekana kuwa kulikuwa na upungufu wa shughuli za kisiasa katika makoloni ya Ufaransa ya Afrika ya Magharibi katika kipindi cha miaka ya kati ya Vita Vikuu. Hali hii ilitokana na uhasama wa Wafaransa dhidi ya mashirika na shughuli za kisiasa za Waafrika na pia kutokuwepo na magazeti ya Waafrika yenye harakati kali za kitaifa katika makoloni hayo kama hali ilivyokuwa nchini Sierra Leone, Gold Coast na Nigeria. Hata hivyo shughuli za kisiasa katika makoloni ya Ufaransa Afrika ya Magharibi, kama zilivyokuwa shughuli za makoloni ya Uingereza, zilikuwa na sura mbili, ya kitaifa na ya kimataifa. Shughuli nyingi za kisiasa za makoloni ya Ufaransa ya Afrika ya Magharibi ambazo zilifanywa kati ya miaka ya 1924 na 1936 zilifanyika hasa mjini Paris. Hata hivyo, kwa kuwa makundi mengi yaliyohusika yalikuwa ya kimapinduzi na pia kuwa yalishirikiana na vyama vya kisiasa vya Wafaransa na pia vya wafanyakazi vya kimapinduzi, shughuli zao za kuupinga ukoloni ziliuathiri utawala wa Kikoloni wa Ufaransa kwa hali ya chini sana. Kati ya makundi haya kulikuwemo lile la Muungano wa Ulimwengu wa kulinda Taifa la Weusi (*Ligue Universelle Pour la defense de la Race Noire*) ambalo lilianzishwa katika mwaka 1924 na Prince Kojo Tovalou Houenon aliyekuwa mwanasheria na mzalendo kutoka Dahomey. Kundi jingine lilikuwa Kamati ya Kulinda Taifa la Wanegro (*Comite' de la d'efense de la Race N'egre)* ambalo, liliongozwa na Tiemoho Garan-Konyat'e ambaye alikuwa mfuasi wa

Marx kutoka koloni la Ufaransa huko Sudan. Ingawa makundi haya yalikuwa ya kuvutia hayakufanyia shughuli zao Afrika ya Magharibi.

Siasa na Utaifa Nchini Senegal

Pengine makoloni mawili ya Ufaransa ya Afrika Magharibi yaliyokuwa na baadhi ya shughuli za kisiasa yalikuwa ni Senegal na Dahomey. Huko Senegal shughuli hizo zilihusiana na Blaise Diagne ambaye aliunda chama cha Kijamaa (*Republican Socialist Party*) mnamo mwaka 1914 ili kuunganisha mbari kadha zilizoishi mjini Dakar na St. Louis katika juhudi zake za kupigania kuchaguliwa kuwa mbunge wa bunge la Ufaransa katika uchaguzi wa mwaka wa 1914. Alifanikiwa kupata kuungwa mkono na mawalii wakubwa wa sehemu za mijini pamoja na mbari nyingine zilizoishi katika Dakar na St. Louis na pia kuthaminiwa kisiasa na chama cha Vijana wa Senegal (*Young Senegales*), pamoja na Wafaransa wenye fikra za mwelekeo wa mabadiliko. Katika kampeni yake yote Diagne alisisitiza umuhimu wa kuhifadhi haki ya uraia na pia haki ya Mwafrika ya kupigia kura katika mitaa minne, masuala ambayo wapinzani wake wa kizungu na machotara, ambao walikuwa wameshikilia uongozi wa kisiasa katika mitaa ile tangu mwaka 1900 na wakawa wamefikia kiasi cha kuchukua nafasi za kuchaguliwa kwa kura kama mali yao binafsi au ya familia zao, waliyapuuza na kurawona Diagne kama mgombea uchaguzi asie wa maana.

Lakini Diagne hakupigania haki za Mwafrika za kupiga kura tu bali pia alitetea kutambuliwa kwa sheria na utamaduni wa Kiislamu. Pia aliomba Mwafrika apewe nafuu zaidi ya kiuchumi, akapigania kuundwa kwa baraza la kusimamia mambo ya fedha katika kila koloni la Ufaransa, kuanzishwa kwa chuo cha utabibu mjini Dakar na haki ya Waafrika kuunda vyama vya wafanyakazi.

Hasa kwa sababu ya kampeni yake ya dhati, kutumiwa kwa kura ya siri na kwa kuungwa mkono kisiasa na makundi ya Waislamu ya sehemu za mashambani, mnamo mwezi wa July mwaka 1914 Diagne alitokea kuwa mshindi na kuwa mbunge wa kwanza wa Kiafrika katika bunge la Ufaransa. Ushindi katika kuchaguliwa kwake ulikuwa kama mapindizu katika kuhusika kwa Mwafrika katika mipango na siasa za Wasenegali. Wapiga kura wa Kiafrika wakatokea kuwa sehemu muhimu ya siasa na wala sio watu wa kutumwa ovyo na wakoloni au machotara.

Siasa na Utaifa Nchini Dahomey

Nchini Dahomey mbali na upinzani wa kawaida wa Waafrika dhidi ya ukoloni uliotokea kupitia matawi ya nchini ya Chama cha kutetea Haki za Binadamu ((*Ligue des Droit de l'Homme*), ambacho pengine ndicho kilichokuwa chombo pekee kilichoruhusiwa kutumiwa kwa shughuli za kisiasa, siasa ilihusu zaidi mgogoro kati ya vikundi vya kidini na mwingiliano wa migogoro hii na utawala wa machifu wa kijadi na ugomvi wa kurithi utawala huo. Mhusika muhimu zaidi alikuwa za kipindi tunachokijadili na aliyejumuisha siasa za utawala wa kijadi alikuwa ni Louis Hunkanrin (alikiunga mkono kikundi cha *Sognigbe*, kutoka Jamii ya Kiislamu ya Horto Novo, dhidi ya kikundi cha Waislamu wa Kiyoruba cha Jose Paraiso) pamoja na zile za kuupinga ukoloni. Hunkanria alisomea

Senegal kisha akafanya kazi kwa muda nchini Dahomey na kurejea Senegal mnamo mwaka 1913. Aliandika makala makali katika magazeti ya Ufaransa na Senegal dhidi ya maovu ya utawala wa kikoloni na pia alimsaidia Blaise Diagne katika kampeni yake ya uchaguzi wa mwaka wa 1914. Kwa msaada wa Blaise Diagne, Hunkanrin aliajiriwa mjini Paris lakini kwa kuwa alihusika na makundi ya siasa za kimapinduzi alirudishwa nchini Dahomey mnamo mwaka 1921.

Aliporejea nyumbani alilifufua tawi la Chama cha Kutetea Haki za Binadamu na pia kuunda kamati ya Wafaransa Waislamu (*Comite Franco-Musulman*). Kwa kupitia kwa wenzake katika matawi ya nchini ya makundi haya, magazeti yenye siasa kali na za kikomunisti kutoka Ufaransa na Marekani yaliwafikia wasomi wa Dahomey na pia maombi ya haki na malalamiko dhidi ya utawala nchini yalitumwa Paris.

Mnamo mwezi Februari mwaka 1923 kwa sababu ya upandaji wa kodi na pia kwa sababu ya kushuka kwa bei za mazao ya michikichi, baada ya mipomoko ya uchumi ulimwenguni katika miaka ya 1919 na 1920, 1921 na pia kwa sababu ya upandaji wa bei za bidhaa na upungufu wa sarafu za chuma, wafanyakazi wa makampuni ya kibinafsi, chini ya uongozi wa marafiki wa Hunkanrin katika kamati ya Waislamu wa Kifaransa na Chama cha Kutetea Haki za Binadamu, waligoma na kufanya mikutano ya hadhara. Majeshi yaliamriwa kuivunja mikutano hiyo nao Waafrika wakajibu kwa kuanzisha upinzani usio wa fujo ambao ulianzia Februari 13 hadi mwanzoni mwa Machi. Pia kulikuwepo na migomo mjini Whydak.. Hata baadhi ya mchifu waliwaomba machifu wenzao kuzipinga kodi mpya. Nao utawala wa kikoloni ulijihali hii kwa kuwakamata viongozi wa upinzani huo, kuomba wanajeshi zaidi kutoka Togo na Ivory Coast na pia kwa kutangaza hali ya hatari ambayo ilidumu hadi mwezi Juni mwaka 1923. Baada ya kukamatwa na kuhamishwa kwa karibu viongozi wote wa upinzani huo, ikiwa ni pamoja na Hunkanrin, siasa za utaifa ziliisha nchini Dahomey kama ilivyokuwa katika makoloni mengine ya Ufaransa katika Afrika ya Magharibi na hii ilifuatwa na kipindi cha utulivu wa kisiasa.

Zaidi za maandamo na ghasia za Prto Novo (Dahomey) za mwaka wa 1923 siasa za kitaifa zilizopangwa kama zile za NVBWS au za chama cha Herbert Macaulay cha "Chama cha Kitaifa cha Kidemokrasia cha Nigeria" zilikuwa jambo la nadra sana katika Afrika ya Magharibi katika kipindi tunachokijadili.

# 26

## *Siasa na utaifa katika Afrika ya Mashariki 1919-1935*

Tofauti na hali ilivyokuwa katika Afrika Magharibi, katika Afrika Mashariki, siasa na utaifa, dhana ambazo zaweza kufupishwa vizuri na neno moja la Kiswahili "siasa", ni jambo ambalo katika kipindi kati ya vita vikuu yalihusisha sio tu wasomi au kundi la waliosoma bali pia umma. Shughuli za kisiasa zilikuwa shughuli za umma. Pili, tofauti na hali ilivyokuwa katika Afrika Magharibi lakini sawa na hali ilivyokuwa katika Afrika Kaskazini, utaifa na shughuli za kisiasa ni mambo yaliyowahusisha watu wa dini na wasiokuwa wa dini. Ingawa hivyo, katika Afrika ya mashariki, sawa na ilivyokuwa katika Afrika Magharibi na Kaskazini, utaifa ulikua kutokana na utambuzi wa dhuluma za ukoloni na pia kulikuwepo na uhusiano baina ya siasa na hali za kiuchumi. Zaidi ya hayo malengo ya shughuli za utaifa pamoja na silaha zilizobuniwa ili kuyafanikisha malengo hayo zilikuwa sawa na zile zilizotumiwa, katika Afrika Magharibi. Katika Afrika Mashariki, sawa na ilivyokuwa katika Afrika Magharibi, malengo hayo hayakuwa ya kuutupilia mbali mfumo wa kikoloni bali kuurejesha na pia kujinufaisha nao. Baadhi ya silaha zilizotumiwa dhidi ya ukoloni zilikuwa dini, umoja wa vijana na mashirika ya vikundi vya walio bora.

### *Vyama vya Kidini vya kupinga Ukoloni*

Katika kupambana na ukoloni silaha mojawapo ambayo Waafrika wa Afrika Mashariki waliitumia tangu mwanzoni na kwa dhati kuliko Waafrika wa magharibi ilikuwa ni dini. Mapambano yalihitaji uhamasisho wa juhudi zote dhidi ya ukoloni na katika sehemu nyingi kama ilivyokwishaonekana, viongozi wa dini walijitokeza ili kuutimiza wajibu huo.

Makundi haya ya dini za kijadi ya mapambano dhidi ya ukoloni yaliendelea kuweko katika mwongo wa kwanza baada ya Vita vikuu vya Kwanza. Kwa hii njia yalidumisha kuweko kwa mwendelezo wa mambo kutoka kipindi kilichopita. Ingawa hivyo, katika mwongo wa pili uliofuata ukoloni ulizidi kuimarika na kuunda upya au kuyaharibu mashirika yaliyokuwepo ya kijamii na kisiasa na kutokana na jambo hili haja ya kuwepo kwa nguvu za kidini za kupambana na ukoloni ilijitokeza katika

Waafrika waliotawaliwa. Haja hii ilikidhiwa kwa njia mbili yaani kuweko kwa mitume wa Kiafrika na pia kuanzishwa kwa madhehebu ya Kikristo ya Kiafrika ambayo yalikuwa huru na yaliyoendeshwa sambamba na yale ya Kizungu.

Mifano ya madhehebu haya ya kuupinga ukoloni yaliyoanzia katika mwongo wa pili na yaliyodumu katika kipindi chote cha miaka ya 1920 na ya 1930 na ambayo yalipata wafuasi zaidi baada ya Vita Vikuu vya Pili yaweza kuonekana katika mbari za Wakamba na Wakisii nchini Kenya. Katika miongo miwili ya kwanza ya karne hii utaratibu wa ukoloni ulisababisha kuweko kwa hisia za kunyimwa haki na kuhangaishwa miongoni mwa umma wa Wakamba kutokana na utawala huo kuzingatia kampeni ya kunyakua mali yao kwa kudai kodi, ardhi yao na wafanyakazi wakiwatumia machifu wao wapya ambao hawakuwa na heshima kwa mujibu wa utaratibu wa utawala wa kijadi. Uajiri wa lazima wa wapagazi wa kijeshi katika miaka ya Vita Kuu vya Kwanza, kushindwa kwa watawala wa kikoloni kuyatatua matatizo mengi ya kijamii na kiuchumi yaliyoukumba umma wa Kikamba kutokana na Vita Vikuu vya Kwanza, athari mbaya zilizoletwa na shida za kiuchumi ulimwenguni za kipindi cha 1920-1921 na pia kulemewa zaidi na ulipaji wa kodi baada ya mwaka wa 1920 ni mambo yaliyozidisha idadi ya waliyokuwa tayari kuitikia mwito wa kutumia njia za dini ili kuupunguza wasiwasi katika jamii.

Mwito kama huo ulitokana na Ndonya wa Kauti aliyeanza kuuhubiri ujumbe wake wa kiutume katika Kilungu, Wilayani Machakos, kuanzia miezi ya mwanzo ya mwaka wa 1922. Alidai kuwa yeye alikuwa mtume aliyeweza kutabiri kunyesha kwa mvua na pia akawaomba akina mama kwenda kucheza ngoma ya kidini ya Kilumi nyumbani kwake. Pia alidai kuwa Mungu (Ngai) alikuwa amemteua yeye kuwaongoza watu katika Enzi Mpya iliyokuwa imewadia ulimwenguni. Katika mwanzo wa enzi mpya Wazungu wangefukuzwa nchini na baada ya jambo hili, ardhi ingerudia hali yake kabla ya ukoloni yaani yenye mvua nyingi na bila kodi. Kundi la Ndonye lilizidi kuimarika jinsi hali ya uchumi ilivyozidi kuwa mbaya zaidi. Kama ambavyo ingetarajiwa, katika mazingira ya ukoloni mtu kama Ndonye hangevumiliwa na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwani Mkuu wa Wilaya (D.C.) Ndonye, kama wengine wengi wa kabla na baada yake, hukurudi kwao kwani alifia uhamishoni.

Kikundi kingine na ambacho hakingeweza kuangamizwa kwa urahisi kilikuwa kile cha madhehebu ya Mumbo – kilichodumu wakati mmoja na utume wa Ndonye wa Kauti. Misingi ya kikundi hiki ilitokana na chuki dhidi ya ukoloni ambazo Waluo na Wakisii walikuwa nazo kwa pamoja. Chuki hizi zilianza katika vita vya ukaliaji ambavyo Waingereza walipigana na Wakisii mnamo miaka ya 1904 na 1908 na pia vita kama hivyo na Wajaluo wa Alego katika kipindi cha miaka ya 1908 hadi 1910. Chuki hizo zilizidishwa zaidi na kazi ya lazima ya ujenzi wa barabara na katika mashamba ya masetla na pia kodi ya nyumba ilikuwa inachukiwa sana. Pia tabia ya wamisheni ya kuwaamulia Waafrika yaliyowafaa iliongezea chuki hizo zaidi. Kama hali ilivyokuwa katika Ukambani, Wakisii walianza kutafuta mwokozi nao wakampata katika madhehebu ya Kiluo yaliyoitwa *Mumbo* ambayo yalikuwa ya kijadi, yaliyoamini

mizimu ya ziwani na ambayo yalikuwa mashuhuri sana katika karne ya kumi na tisa; na pia katika kiongozi wake aliyeitwa Onyango Dunde ambaye alitoka katika mbari ya Seje katika Alego. Kwa kupitia kwa Onyango Dunde, Mzimu wa Mumbo aliwashauri watu kuwa: "..... Dini ya Kikristo ni dini iliyooza Wazungu wote ni maadui wenu lakini wakati Umewadia ambapo watatoweka kutoka nchi yetu." Kwa kuwa ujumbe wake ulikuwa dhahiri na pia ulizingatia hali halisi ya kisiasa ya wakati huo madhehebu haya yalisambaa haraka, kutoka Alego wilayani Siaya hadi Nyanza ya Kusini, mpaka yalipoonekana wilayani Kisii mnamo mwaka 1914 ambapo kiongozi wake alikuwa mtume mwingine wa Kijaluo aliyeitwa Mosi Wuod Auma aliyetabiri kuondoka mapema kwa Wazungu wote kutoka Kisii, hali ambayo ingefuatwa na Wazalendo kuimiliki ardhi yao kwa amani.

Ujumbe kuwa Wazungu wangeondoka mapema ulionekana ukidhihirika mnamo mwaka 1914 wakati Wajerumani walipoishambulia ngome ya Waingereza mjini Kisii na kwa hivyo Waafrika waliasi na kuleta vituo vya wakoloni na vya wamisheni wilayani humo. Nao Waingereza waliyakomesha maasi hayo kwa ukatili ambapo Wakisii mia moja na hamsini waliuawa. Ingawa hivyo jambo hili halikuwaogofya wafuasi wa madhehebu haya kwani waliendelea na shughuli zao katika kipindi kati ya Vita Vikuu hata japokuwa kulikuwepo na kushikwa na kuhamishwa kwa mara kwa mara kwa viongozi wao. Katika nchi ya Wakisii madhehebu ya Mumbo yalichanganyika na madhehebu ya Sakawa ambayo yalikuwa ya Kiasili. Ingawa madhehebu haya yalizuiwa na utawala wa kikoloni lakini yaliendelea kudumu wakati wote na kipindi tunachokizungumzia. Pia ingawa wafuasi wa madhehebu ya mumbo waliteswa, wakahamishwa na kupigwa marufuku wilayani Kisii waliendelea kuhubiri na pia moyo wa kuupinga ukoloni haukukomeshwa bali uliendelea kwa siri mpaka ulipojitokeza tena katika miaka ya baada ya 1950 ambapo uliwasumbua watawala wa kikoloni wa Uingereza kwa mara nyingine.

Makundi mengine ya kidini yaliyokuwa na umuhimu sawa na yale tuliyoyazungumzia yalikuwa ni yale ya madhehebu ya dini huru za Kikristo. Kama tulivyoona katika Sura za 12 na 20 madhehebu mengi kama hayo yalizuka katika Afrika Mashariki kabla na yaliyotofautiana zaidi yalizuka katika wakati tunaouchunguza. Baadhi ya madhehebu hayo yalizingatia dini za Kiethiopia ambazo kama ambavyo Opoku ameonyesha, yalisisitiza kujiendeleza kwa Mwafrika na haki za kisiasa ambapo mengine yalikuwa ya Kizayoni ambayo yalisisitiza kuwepo na Roho Mtakatifu, uponyaji na utabiri wa mambo.

Madhehebu ya dini huru ya Kiafrika yaliyo ya zamani zaidi katika eneo hili, yaani madhehebu ya Nomiya Luo, ambayo yalianzishwa na Johana Owala mnamo mwaka wa 1910 yamekwishazungumziwa katika Sura ya 7 ya kitabu hiki. Mfano wa pili ni madhehebu ya 'Watch Tower' ambayo yalianzia katika Afrika ya Kati na Kusini mwa Tanganyika katika wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza na ambayo yalikuwa madhehebu ya umma yaliyotokana na juhudi za watawaliwa wa sehemu za mashambani za kujaribu kutatua matatizo yao chini ya ukoloni. Kwa kuyakataa

mamlaka ya machifu, wamisheni na watawala wa Uingereza na kwa kujenga vijiji vipya vya waumini wao, wafuasi wa madhehebu haya walijaribu kuunda jamii mpya ambapo wangejihisi kuwa wanatosheka. Kufikia mwaka wa 1919 madhehebu haya yalikuwa yameingia nchini Tanganyika na yalikuwa na wafuasi wengi katika sehemu za Kasanga, Mambwe, Ufipa na Mbozi. Mambo yalifikia kilele mnamo mwaka wa 1923 ambapo Waingereza waliwafunga jela viongozi 17 wa madhehebu haya baada ya kuwakamata na kuwashitaki kwa kosa la kuwatukana wamisheni. Jambo hili halikuwaogofya wafuasi wa madhehebu haya na yaliendelea kusambaa katika muda wote wa ukoloni.

Hata hivyo, kulikuwepo na baadhi ya madhehebu ambayo yalianzishwa kwa malengo yaliyokuwa mafinyu zaidi kuliko yale ya *Watch Tower* kwa sababu yalihusika na masuala binafsi. Kwa mfano madhehebu ya *African National Church* (Kanisa la Kitaifa la Afrika) yaliyosambaa katika wilaya ya Rungwe, nchini Tanganyika, kuanzia mwaka wa 1930 na ambayo yalikuwa madhehebu ya Kikristo yaliyoanzishwa kwa kuwashirikisha wale ambao walikuwa wamefukuzwa na ambao hawangekubaliwa katika madhehebu ya wamisheni kwa kuwa walikuwa wameoa mitara. Pia madhehebu ya *Holy Ghost Church* (Dini ya Roho Mtakatifu) yaliauzishwa miongoni mwa Abaluyia wa Kenya mnamo mwaka wa 1927 kwa kujitenga kutokana na madhehebu ya *African Friends Mission* ( Misheni ya Marafiki wa Kiafrika). Wafuasi wa madhehebu ya Dini ya Roho walisisitiza kuwa ili mtu awe Mkristo kamili ilikuwa ni lazima akubali ubatizo wa Roho Mtakatifu, aongee kwa ndimi tofauti, na atubu dhambi zake hadharani. Huku kusisitizwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu ndiko kulimfanya Alfayo Odongo Mango kuanzisha dini ya Joroho (Roho Mtakatifu) miongoni mwa Waluo mnamo mwaka wa 1932.

Ingawa watawala wengi wa kikoloni waliyachukulia makundi haya kama "misukumo ya ghafula isiyofaa kitu". Madhehebu haya ya upinzani yaonyesha dhahiri umuhimu wa mizizi ya Kiafrika na yalikuwa yanahusiana sana na utaifa. Pia misingi ya wafuasi wao ilikuwa ni umma wa sehemu za mashambani.

## *Vyama vya Vijana*

Katika historia ya hivi karibuni umuhimu mwingi umeonyeshwa wa kundi la wasomi walio bora yaani *Asomi* au *Josomi* katika maendeleo ya siasa za Arika za miaka tunayoizungumzia. Kundi hili jipya lilikuwa la wanaume wachache (karibu hapakuwepo na mwanamke ye yote) walikuwa wamesomea shule za wamisheni kama vile Maseno, Budo, Thogoto na Zanzibar ambao baadaye walikuwa waalimu, waalimu wa kidini, makarani na mafundi, wakifanya kazi kwa kuwapinga machifu walioteuliwa na wakoloni na pia kwa kuupinga utawala nchini mwao watu hawa waliunda vyama vya "vijana" kama njia za kuendeshea upinzani ambao kwazo wangeendeshea kampeni zao za kisiasa. Kwa hivyo vyama hivyo vilikuwa na wafuasi wengi. Mifano halisi kama hii ni kama Chama cha Vijana wa Buganda (Young Baganda Association), Chama

cha Vijana wa Kavirondo (Young Kavirondo Association), Chama cha Kikuyu (Central Association) (KCA).

Chama cha vijana cha Buganda kilizuka kutokana na mikinzano miongoni mwa jamii ya Baganda ambayo ilisababishwa hasa na Mkataba wa Buganda wa mwaka wa 1900 na pia tabia ya machifu wapya. Kufuatana na mkataba huo machifu wapya walipewa sehemu kubwa za ardhi zao binafsi na zao kama maafisa wa serikali na kwa hivyo wakawa maadui wa viongozi wa mbari wa kijadi (Bataka), wakulima wa mashamba madogo madogo (Bakopi), na vijana wa madhehebu ya Kikatoliki na Kiislamu ambao walikuwa hawakuridhishwa na hali hiyo. Kwa kuwa Kabaka (Mfalme wa Buganda) ndiye aliyekuwa mwenye kunufaika zaidi na mkataba huo kuliko wote, lawama kutokana na kauli na maandishi ya vijana havikumuacha kando. Pili, tabia ya machifu wapya ilikuwa ya kuudhi sana. Kwa kuwa wao walikuwa warasimu wa kikoloni wala sio viongozi wa kijadi, waliudhihaki kwa wazi uhusiano uliokuwepo katika jamii ya Buganda wa "bwana na mtumishi" ambao uliwafaidia zaidi inabwana wao wapya. Zaidi ya hayo machifu wapya, wakiwa wakala wa ukoloni, walitakiwa kuzitekeleza sheria kama zile za afya na usafi ambazo zilichukiwa sana na wakulima wa mashamba madogo madogo. Kundi la wasomi walio bora ambao hawakushirikishwa katika ngazi za madaraka waliyatumia sana malalamiko dhidi ya sheria hizi.

Viongozi wa upinzani huo walikuwa ni vijana na aliyekuwa mashuhuri zaidi kati yao alikuwa ni Z.K. Sentongo ambaye alikuwa mwandishi hodari wa kijarida na aliyeanzisha Chama cha Vijana wa Buganda mnamo mwaka wa 1919. Malengo ya chama hiki yalikuwa kuimarisha Uganda kwa njia zote, kumsaidia Mganda yoyote mwenye matatizo na kuindeleza elimu. Katika ushahidi wa maandishi yao, viongozi hawa pia walilalamika juu ya machifu wa Buganda kwa kuwashitaki kuwa waliwafunga watu bila kuhukumiwa na korti. Lalamiko lao jingine lilikuwa la kiuchumi ambapo walitaka masharti ambayo yalikuwa yamewekwa juu ya biashara ya pamba na serikali ya Uganda (Uganda Protectorate Government) yaondolewe. Kutokana na mwanzo huu wa kadri katika miaka mitatu iliyofuata Chama cha Vijana wa Buganda kilikuwa na ashirika lisilokubali mapatano. Kufikia mwaka wa 1921 chama hiki kilikuwa kimebadilika na kuwa cha wabaguzi wa wapinga Waasia.

Akiandika katika gazeti la *Uganda Herald* la mwaka huo, Z.K. Sentogo aliwalaumu Waasia kama wanyonyaji wa kwanza wa Waafrika. Kufikia mwaka wa 1922, Chama cha Vijana wa Buganda kilikuwa kimebadilika kikawa cha kuupinga ufalme, kikawashambulia machifu na Kabaka na pia kikashauri kuwa ilifaa Uganda iwe Jamhuri. Katika mwaka huo, Yowasi Paito, Joswa Naluma na Yusufu Mukasa, wote watatu wakiwa maafisa wasaidizi wa afya katika hospitali ya Namirembe na pia wakiwa wanafunzi wa zamani wa shule ya Budo, waliandika barua iliyomshutumu Kabaka Daudi Chwa kwa kuwa mtu asiye na maadili, kukosa kuiendesha ikulu (Lubiri) kwa njia nzuri na pia kwa kuwaunga mkono machifu. Bila shaka sio machifu wala Kabaka ambaye angewaacha kuiepuka adhabu. Chini ya sheria iliyopitishwa na

bunge (Lukıko) ambayo iliharamisha shutuma kwa Kabaka, waandishi wa barua hiyo wote watatu walifungwa jela mwezi Julai mwaka 1922. Kutokana na jambo hili na pia kwa kuwa baadhi ya wafuasi wa chama hiki walipewa vyeo vya ngazi za chini za uongozi, chama kilififia na kuangamia.

Chama cha Vijana wa Kavirondo (Young Kavirondo Association) kilianzishwa na wanafunzi wa zamani wa shule ya Maseno, mkoasni Nyanza, katika nusu ya pili ya mwaka wa 1921. Kuanzishwa kwa chama hiki kulitokana na kubadilishwa kwa Nchi Lindwa ya Waingereza katika Afrika ya Mashariki na kuifanya kuwa Koloni la Mfalme la Kenya na Nchi Lindwa mnamo mwaka wa 1920. Jambo hili lilitafsiriwa na viongozi wa chama hiki kuwa na maana ya hila za Waingereza za kutaka kuibadili hali ya Waafrika na pengine kuiandaa ardhi ya Kenya ya magharibi kuwa makazi ya Wazungu.

Ni katika mkutano wa hadhara ambao uliitishwa mnamo tarehe 23 Desemba mwaka 1921 ili kuyajadili malalamishi hayo ambapo chama cha YKS kilianzishwa, Jonathan Okwiri, aliyekuwa mwalimu, alichaguliwa kuwa mwenyekiti, Benjamin Owuor Gumba kuwa katibu na Simeon Nyende, mwalimu mwingine, kuwa mweka hazina. La muhimu zaidi ni kuwa baadhi ya maazimio yalipitishwa ambayo yaliomba *'kipande'* ambacho kilichukiwa sana kiondolewe, kupunguzwa kwa kodi ya nyumba na ya kichwa na hasa kuwaondolea wanawake ulipaji wa kodi, kuongezwa kwa mishahara, kuirudisha hali ya mdhamana, kutoa hati za kibinafsi za umilikaji wa ardhi kuondolewa kwa kazi ya kulazimishwa na kujengwa kwa shule ya serikali katika Nyanza ya kati. Kafuatana na jambo hili ujumbe ulienda kumuona mkuu wa kwanza wa mkoa (P.C) na baadaye ukaenda kwa Gavana ili kuwasilisha maazimio haya. Hakuna hata moja kati ya maombi haya lililokubaliwa. Hata hivyo, kwa sababu ya hofu iliyowapata watawala wa kikoloni juu ya uwezo wa kundi changa la walio bora katika kuhamasisha umma, watawala hao waliamua kulipinga kundi hilo kwa mbinu ya ulezi wa kikoloni kwa kumtumia mmisheni, Archdeacon Owen. Katika mwaka wa 1923, viongozi wa YKA walionelea kuwa Owen angekuwa daraja zuri baina yao na serikali na kwa hivyo wakampa uraisi wa chama chao. Papohapo Owen akaanzisha mbinu za kukifanya chama hiki kuwa cha heshima kwa kukihujumu. Kwa kufanya hivyo aliugeuza msingi wa chama hiki kutoka kwa umma na kufanya uwe wa wasomi na pia akazibadilisha shughuli zake kutoka kuhamasisha umma dhidi ya ukoloni hadi kuelekea kwenye mahitaji mapya kama vile nyumba nzuri, chakula kizuri, mavazi mazuri, elimu bora na usafi. Hivi ni kusema kuwa Owen aliuondoa ukali wa kiumma kutoka chama hiki ambacho kuanzia hao kilichukua jina muhimu la chama cha Kijamii cha Walipa kodi wa Kavirondo (Kavirondo Tax Payers Welfare Association - KTWA) na kuanza kutumia mbinu ya kuandika ardhi hali kama njia ya kuelezea matatizo ya kisiasa. Chama hiki kilichodhoofika zaidi mnamo mwaka wa 1931 ambapo kiligawanyika katika makundi mawili, moja la Waluo na jingine la Waluyia, ambapo lile la Waluo liliendelea kujikokota chini ya uongozi wa Owen hadi mwaka wa 1944.

Chama ambacho hakingefanyiwa hila kwa urahisi kilikuwa Chama cha Wakikuyu (Kikuyu Central Association - KCA) ambacho kuanzia mwaka 1924 kiliwapa Wakikuyu wa sehemu za mashambani nafasi ya kuelezea malalamiko yao. Makao makuu yake yalikuwa wilayani Murang'a ambapo kilianzishwa chini ya uongozi wa Joseph Kangethe na James Beauttah.

Malengo yake muhimu yalikuwa kwanza "kuipata tena ardhi iliyochukuliwa na Wazungu kutoka kwetu", kuyapinga maovu ya hali ya ukoloni na hasa kuupinga ubaguzi wa kitaifa ambao Wakikuyu walifanyiwa kutokana na sheria ya Ardhi ya Kifalme ya mwaka wa 1915 ambayo kwa mapenzi ya mfalme iliwafanya Waafrika wote kuwa wakodishaji wa ardhi na pia kupinga kukatazwa kwa Waafrika kukuza pamba na kahawa.

Umuhimu ya KCA uliimarika mnamo mwaka wa 1928 wakati Jomo Kenyatta alipokuwa katibu wake mkuu. Juhudi za Kenyatta kama katibu mkuu zilileta uhusiano wa kiutamaduni. Katika juhudi zake za kuufanya umma ukiunge mkono chama cha KCA Kenyatta, akitumia gazeti la Kikuyu la *"Muigwithania"* ambalo alilianzisha yeye, aliwaomba Wakikuyu kujivunia urithi wao wa kiutamaduni. Kurasa za *Muigwithania* zilijaa vitendawili, methali na hadithi ambazo ziliwahimiza wasomaji kujifikiria kama Wakikuyu.

Kuanzia mwaka wa 1928 Wakikuyu waliyachukulia malalamiko yao juu ya ardhi kuwa kiini cha matatizo yao. Katika mwaka huo KCA kiliutuma ujumbe uliomshirikisha Jomo Kenyatta mjini London ili kutoa malalamiko ya haki zao mbele ya Halmashauri ya Hilton Young. Kiini cha malalamiko yao kilidhihirika katika kauli iliyotolewa kama ushahidi kuwa, 'kwa miaka mingi tumeililia serikali itupe hati za umilikaji wa ardhi yetu lakini hatujazipata na bado hatujui kama ardhi ni yetu au ni ya Mfalme.' Mashaka juu ya usalama katika umilikaji wa ardhi katika 'makazi' ya Waafrika yalisisitizwa tena na Kenyatta mnamo mwaka wa 1929 alipotumwa na KCA akawasilishe mahitaji yao. Pia KCA ilizisaidia mbari za Wakikuyu katika kuutayarisha ushahidi ambao ulitolewa kwa Halmashauri ya Ardhi ya Kenya ((Kenya Land Commission) mnamo mwaka wa 1931. Ripoti ya Halmashauri ilipotolewa K.C.A iliyaongoza makundi ya kisiasa Wakikuyu katika kuiandaa ardhihali ya upinzani na pia upinzani dhidi ya ripoti hiyo. Kwa kuwa upinzani huu uliendelea bila majibu, suala la ardhi likachukua umuhimu mkubwa katika siasa za Wakikuyu na baada ya miaka ishirini ilizusha vita vya Mau Mau.

Vyama hivi "vichanga" havikufaulu ingawaje si vya kutupilia mbali kama vyama vilivyoshindwa kabisa. Ingawa havikufanikiwa kwa sababu ya kufanyiwa njama kwa kuwaingiza baadhi ya viongozi wao katika madaraka na pia kwa kutiwa kizuizini kwa wengine urithi wa kudumu unaopatikana kutokana navyo ni kuwa viliwasilisha malalamiko ya Waafrika dhidi ya mfumo wa kikoloni.

## *Vyama Vidogo vidogo*

Pamoja na vyama hivyo ambavyo vilikuwa na shughuli na madai mapana zaidi kulizuka vyama vingi vidogovidogo vilivyoundwa ili kushughulikia mambo maalumu ya mitaani. Mengi ya mambo haya yalihusiana na mipaka ya mikoa na wilaya mpya zilizoundwa na watawala wa kikoloni kwa madhumuni ya utawala wa ndani ambayo ilipitia katikati ya mbari kuu, mbari na koo. Kwa hivyo, hivi viliundwa kwa sababu za kuzitetea ardhi zilizokuwa zimeenda kwingine ama kuwaombea waliohusika waruhusiwe kujiunga na mbari zao zilizokuwa katika maeneo tofauti au kuomba wawekewe mipaka katika wilaya zao wenyewe.

Mfano mzuri wa chama kama hicho ulikuwa chama cha Waluo wa Mbari ya Kager (The Ugenya Kager Luo Clan Association) waishio kusini mwa mto Nzoia katika kata ya Ugenya, ambacho kiliundwa mnamo mwaka wa 1932 ili kuipata, "ardhi iliyopotea" kutoka kwa majirani wa Wanga. Mfano mwingine ulikuwa ni Kamati ya Wabanyoro wa Mubende (Mubende Banyoro Commitee) iliyojulikana sana na ambayo ilizingatia kwa dhati suala la kurudishwa kwa ardhi zilizopotezwa za Buyaga, Bugangaizi, Buwekula, Buruli na Rugonjo kwa ufalme wa Bunyoro nchini Uganda. Kwa ujumla wakoloni walikataa kuyatimiza maombi ya vyama hivi vidogo.

Vyama vingine na ambavyo havikuwa na umuhimu mkubwa wa kisiasa vilikuwa ni vyama vya kibiashara vilivyoundwa na wakulima na wafanyabiashara wa Kiafrika ambavyo mara nyingi vilianza na malengo maalumu lakini baadaye viligeuka na kuwa vyombo vya kuyapinga maovu yaliyotendwa na ukoloni katika sehemu zao. Mfano mmoja ulikuwa Chama cha Wazalendo Wakuzaji (wa kahawa) wa Kilimanjaro ((Kilimanjaro Native Planters (Coffee) Association) (KNPA) ambacho kiliundwa mnamo mwaka wa 1925 ili "kuyalinda na kuyaendeleza maslahi ya Wazalendo Wakuzaji wa Kahawa Mlimani", lakini ambacho kilijiona kimeingizwa katika shughuli za masetla wa Kizungu na maafisa mbalimbali wa utawala wa Kiingereza na, kwa hivyo, kikaingilia mambo kama vile usajili wa ardhi, unyang'anywaji na matumizi ya ardhi, haki za kisiasa, uwakilishi katika bunge la kikoloni, halmashauri ya maji ya Moshi na kuyapinga mamlaka ya machifu. Mfano mwingine ulikuwa ni umoja wa Wabahaya wa Bukoba (Bukoba Bahaya Union) kilichoundwa mnamo mwaka wa 1924 na makarani wa serikali na wafanyabiashara wa sehemu ya Bukoba kama vile Clemens Kiiza, Suedi Kangasheki, Ludovic Kaitasba na Herbert Rugizibwa ili "kuiendeleza nchi yetu na kutafuta njia rahisi ya kufikia ustaarabu wenye maslahi yetu sisi kwa sisi". Njia mbili za kuufikia "ustaarabu" huo zilikuwa ni elimu ya kusoma na upandaji wa kahawa. Katika kipindi chote cha miaka ya 1920 chama hiki kilizingatia malengo haya na katika juhudi hizo kiligombana, mara nyingi na uongozi wa kikoloni na wa machifu ambao kiliuona kama kikwazo kwa maendeleo yake.

Katika historia ya Afrika ya Mashariki, vyama hivi vimeelezwa kama "vyama vya kujiendeleza" vilivyoongozwa na "watu wa kisasa". Kuzuka kwa vyama hivi kulikuwa ishara ya kuwa rika jipya la walio bora – lilikuwa limetokea mbali na lile lililotokana na machifu, ambalo lilikuwa limeanzishwa na watawala wa kikoloni miaka kumi au ishirini nyuma, na ambalo lilikuwa likidai uongozi kutoka lile la

machifu. Mchango wa kundi hili la wastaarabishaji katika kisiasa katika Afrika Mashariki, unajadiliwa na wanahistoria wa Kiafrika. Baadhi ya wasomi husisitiza kuona mbali kwa kundi hili hali wengine huliona kama kundi la wajitafutia makuu wasio na mchango wo wote katika ujumla, wa kuleta siasa za kimapinduzi katika Afrika. Kwa ujumla na kwa kuwa kundi hili lilianzia hasa kwa kuyalinda maslahi yake na ya tabaka lao ni vigumu kuuona mchango wao katika uongozi wa kisiasa na uhamasishaji wa umma. Kuzingatia maslahi ya umma ni jambo ambalo kundi hili lilishughulikia tu baada ya vita Vikuu vya Pili.

Je kulikuweko na vyama vya wafanyakazi? Sawa na hali ilivyokuwa katika Afrika ya Magharibi vyama vya wafanyakazi havikuruhusiwa na utawala wa kikoloni. Vyama vilivyoruhusiwa ni vya kijamii vya wafanyakazi ambavyo havikuruhusiwa kujihusisha moja kwa moja na masuala ya wafanyakazi. Ni kutokana na sababu hii ambapo baadhi ya vyama kama hivyo viliundwa. Hata hivyo, baada ya kuundwa kwa vyama hivyo, vilitoa madai ya kisiasa. Baadhi ya vyama hivi ni kile cha Watumishi wa Serikali wa Kiafrika wa Tanganyika (Tanganyika Territory African Civil Service Association – TCSU) ambachlo kiliundwa mnamo mwaka wa 1922 na kile cha Watumishi wa Serikali wa Kiafrika wa Kenya (Kenya African Civil Service Association – KACSA) kilichoundwa kabla ya mwaka wa 1933. Chama cha TSCU kilianzishwa na Martin Kayamba ili kuendeleza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wanachama wake na kuleta ustawi wa kijamii kwa wanachama wake katika idara mbalimbali za serikali. Kwa upande mmoja, kilikuwa chama cha wafanyakazi na, kwa upande mwingine, kilabu cha kijamii ambacho shughuli zake zilikuwa ni pamoja na michezo na masomo ya jioni. Chama hiki kilizingatia hasa marupurupu ya wasomi. Hata ingawa Kayamba alikuwa ametarajia kuunda chama cha nchi nzima, chama chake kilififia katika miaka ya mwisho ya kipindi cha miaka ya mwishomwisho ya 1920 kwa sababu wafuasi wake walipewa vyeo katika utawala wa kikoloni. Kwa hivyo, hata kilipokuwa kinaendelea kuwepo mafanikio yake yalikuwa machache.

Asili hasa ya KACSA haijulikani vizuri lakini chama hicho kilitoa ardhihali muhimu kwa tume ya uchunguzi juu ya utekelezaji wa haki katika nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika iliyoundwa katika mwaka wa 1933. Kiliomba kutafsiriwa kwa sheria zote nchini kwa lugha ya Kiswahili, kuweko kwa washauri wa mahakama katika kesi zote za uhalifu na kubatilishwa kwa mfumo wa kipande. Ardhihali hiyo pia ililaumu kuwepo kwa sheria za uzururaji, sheria za adhabu ya jumla na pia kuondolewa kwa ulipaji kodi na wajane, wasio na kazi ya kuajiriwa na walio na umri wa zaidi ya miaka 50. Hakuna lo lote jingine linalojulikana kuwa lilitendwa na chama hiki. Pia ni machache sana yanayojulikana kuhusu Chama cha Waalimu wa Kiafrika wa Kenya (Kenya African Teachers Union) kilichoundwa katika mwaka wa 1934 chini ya uongozi wa Eliud Mathu na James Gichuru.

Lakini kwa jumla tu inaweza kusemwa kuwa shughuli za wasomi zililinganishwa na zile za wafanyakazi ambazo kwa kipindi chote tunachokichunguza zilizingatia migomo katika viwanda, bandari, karakana na pia katika mashamba ya



**26.1** *Harry Thuku (1895–1970), a founder and leader of the East African Association, the pioneer nationalist organization in Kenya (East African Publishing House, Nairobi)*

masetla. Kwa bahati mbaya, ni machache tu yanayojulikana juu ya migomo (mbalimbali) binafsi lakini inawezekana kusisitiza kuwa hisia za kunyimwa haki zilitokea sana miongoni mwa wafanyakazi wa Kiafrika.

## *Juhudi za Kisiasa za Upeo wa Nchi Nzima*

Hadi kufikia hapa masimulizi yetu yamekuwa yakizingatia siasa za mitaa zilizozungumziwa katika viwango mbalimbali. Tunapoliangalia suala la siasa za upeo wa nchi nzima tunaona kuwa hapa tunayo tajiriba isiyo ya kufaulu. Kwa kweli kulikuweko na juhudi mbili tu za dhati, nazo ni Chama cha Afrika ya Mashariki (East African Association EAA) na Chama cha Waafrika wa Tanganyika (Tanganyika African Association – TAA). EAA. kiliundiwa mjini Nairobi mnamo mwaka wa 1921 na mabwana Harry Thuku, Jesse Kariuki, Job Muchuchu na Abdulla Tarara. Waafrika waliotoka nchi nyingine pia walijitokeza kwa dhati ikiwa ni pamoja na Z.K. Sentongo, wa Chama cha Viajana wa Buganda, na pia bwana mmoja kutoka nchi ya Nyasaland (kwa sasa Malawi) ambaye hajatajwa kwa jina. Kwa hakika, hicho kilikuwa chama kilichojumuisha watu wa mbari tofauti tofauti na hata jina lake laonyesha misingi yake ya Kenya nzima. Hata hivyo, wanachama wake wengi walikuwa Wakikuyu. Kiliongozwa na Harry Thuku aliyekuwa karani katika Wizara ya Hazina.

Thuku alikuwa mojawapo wa vijana wa Kikuyu walioishi mjini Nairobi ambao waliona kuwa kulikuwa na haja ya kuunda shirika ambalo lingeshindana na

chama kilichotawaliwa na Wakikuyu (Kikuyu Association). La muhimu zaidi ni kuwa Thuku na vijana wengine wa Nairobi waliuona umuhimu wa kuwa na chama cha Kenya nzima cha Waafrika. Kama alivyoandika Thuku katika gazeti la *East African Standard* katika mwaka wa 1921, ilionekana kuwa, "kama vijana wa nchi hii hawakuunda chama chao mzalendo wa Kenya daima hatakuwa na sauti". Suala hili la kuunda muungano wa pamoja ndilo lililomfanya Thuku kufanya urafiki na vijana wa Kikamba, Kijaluo na Kiganda walio kuwa wanaishi mjini Nairobi. Kwa hiyo mnamo Julai Mosi mwakani 1921 walikianzisha Chama cha Afrika ya Mashariki (East African Association). Chama kilipitisha maazimio juu ya 'kipande', kazi ya lazima, ulipizwaji wa kodi ya juu na juu ya elimu. Thuku aliyatuma maazimio hayo kwa njia ya simu ya barua moja kwa moja hadi Ofisi Kuu ya Makoloni huko London.

La muhimu zaidi katika uchambuzi huu lilikuwa juhudi za Thuku kuwahusisha wasio Wakikuyu katika chama chake katika wakati huo. Alifaulu kuwapata Wakamba walioishi mjini lakini sio walioishi katika sehemu za mashambani. Katika Nyanza chama cha Thuku kilijikuta kinakwenda sambamba na chama cha Vijana wa Kikavirondo. Kufikia Desemba mwaka 1921 viongozi wa Vijana wa Kavirondo waliwasiliana na Thuku na kumhakikishia kuwa walikuwa "wakipambana" pamoja naye kwa niaba ya nchi na pia wakakichangia fedha chama chake. Thuku alipata pia kuungwa mkono na wasomi wa Kimasai waliokuwa wamepata elimu ya Kimagharibi na ambao walikuwa wamesomea Thogoto au shule za misheni ya Afrika Inland za Kijabe na Siyiapei na ambao walikuwa wamekasirikia kutwaliwa kwa ardhi yao na Waingereza.

Tena Thuku alipata kuungwa mkono na chama cha Vijana wa Buganda kilichokuwa na makao yake mjini Kampala na ambacho katibu wake, Joseph Kamulegeya, alimjulisha Thuku kwa Waamerika weusi naye Thuku akawaandikia Dkt. W.E.B., Dubois, Marcus Garvey na Taasisi ya Tuskegee ya Wamisheni Weusi ya Kutoa Misaada kwa Afrika Mashariki. Hapakutokea uhusiano wa kudumu lakini makala ya Garvey ya "Ulimwengu wa Wanegro" yalitumwa kwa Thuku.

Kama ambavyo ingalitarajiwa, utawala wa kikoloni ulikasirishwa na shughuli za Thuku na kwa hivyo alikamatwa mnamo tarehe 14 mwezi Machi mwaka 1922. Kukamatwa kwa Thuku kulizusha maandamano makubwa mjini Nairobi yaliyotokea siku mbili baadaye ambapo polisi waliwapiga Waafrika risasi na kuwaua 21.

Baada ya tukio hili Thaku alihamishiwa Kismayu, nacho chama chake kikaangamia. Kuanzia wakati huo, siasa za sehemu za mashambani na nchi ya Wakikuyu zikachukua mkondo wa Kimbari kuu. Chama kipya kilichozuka kilikuwa ni *Kikuyu Central Assoication* ((KCA.) Risasi za Waingereza zilikomesha mawazo ya Waafrika wa Nairobi juu ya mpango wo wote wa kuunda chama cha kisiasa cha kimbari katika kipindi kati ya vita vikuu vya ulimwengu.

Katika Tanganyika matazamio hayakuwa mazuri zaidi kuliko ya nchi nyingine kama mfano wa *Tanganyika African Association* (TAA) unavyoonyesha. Chama cha TAA kiliundwa mjini Dar es salaam mnamo mwaka 1927. Chini ya

uongozi wa Cecil Matolo, Kleise Skyes, Mzee Bin Sudi na Ramadhani Ali, chama kilielezea malengo yake kuwa kilikusudia "kuyalinda maslahi ya Waafrika sio tu katika nchi hii bali katika Afrika nzima". Hata hivyo, katika utendaji kwa muda wa miaka sita iliyofuata, wanachama wa TAA. hawakusambaa nje ya Dar es Salaam isipokuwa pale ambapo mwanachama wake alihamishiwa bara na kuanzisha tawi la chama kama ilivyotokea mnamo mwaka wa 1933 ambapo Mack Makeja alihamishiwa Dodoma na kuanzisha tawi huko. Hata mjini Dar es Salaam mafanikio yake yalikuwa ni kujenga nyumba ya chama tu. Pia kilitoa ombi la maandishi kwa serikali juu ya kuajiriwa kwa Mwafrika kama hakimu wa mji lakini ombi hilo halikufanikiwa. Baina ya miaka ya 1931 na 1932 mafarakano ya ndani yaliipunguza idadi ya wanachama wake na hali haikubadilika mpaka mwaka 1934 ambapo tawi la Zanzibar lilichukua jukumu la kulifufua.

Hali ya kuwa majaribio ya kuyapanga mambo ya kisiasa kitaifa haikufanikiwa si jambo la kutushangaza. Mbali na dhuluma ya kikoloni, kujitambua kisiasa kulikuwa jambo ambalo halikuwa limekua hadi kuitambna mipaka ya koloni zima kuwa ndio mipaka ya nchi. Isipokuwa watu wachache tu kama vile Jomo Kenyatta, Akiiki Nyambogo na Mbiyu Koinange ambao baada ya kusafiri na kusomea Ulaya na Marekani waliielewa hali ya kikoloni kuwa ya kibeberu, wengine wengi waliuona ukoloni kama jambo la nchini au sehemu yao tu. Kisiasa hakukuwa na Wakenya, Waganda au Watanganyika katika kipindi cha baina ya vita Vikuu.

## *Hitimisho*

Sura hii inajaribu kusimulia kiwango, hali na vikwazo vya siasa za Waafrika na utaifa katika Afrika ya mashariki katika kipindi cha baina ya miaka ya 1919, na 1935 kwa kuchunguza aina mbalimbali za matendo. Watendaji wakuu walikuwa ni umma wa watu ambapo walioyapanga mambo walikuwa ni "Vijana" waliokuwa wamenufaika kutokana na kuanzishwa kwa elimu ya wamisheni katika miaka ishirini ya kwanza ya karne hii na ambao walikuwa na ufasaha wa kuyawasilisha malalamiko ya Waafrika mbele ya watawala wa kikoloni. Kwa ujumla, walijihusisha na malalamiko ya sehemu zao kwa kuhamasisha watu dhidi ya maovu yaliyoletwa na ukoloni. Mara nyingi majaribio yao ya kuyapanga mambo kisiasa yalipigwa dafurao na wakoloni na hakuna hata chama kimoja ambacho kilifanikiwa katika malengo yake yote. Hata hivyo, vyama hivi vilipodumu vilikuwa vinawakumbusha wakoloni kuwa "sauti ya Mwafrika" ilikuwa inaweza kusikika kwa kupitia njia nyingine mbali na zile za muundo wa utawala wa ukoloni.

# 27

# *Siasa na Utaifa katika Sehemu za Kati na Kusini mwa Afrika, 1919 - 1935*

Kama ilivyoonekana katika sura za awali za juzuu hili, ukoloni wa kibepari na Kizungu ulikuwa na ukandamizaji zaidi na ulijiimarisha katika sehemu za Afrika ya Kusini na Kati kuliko katika sehemu nyingine za Afrika katika kipindi tunachozungumzia. Hali hii ilizidi kuwa mbaya zaidi baada ya masetla kuanza kujinyakulia ardhi kwa nguvu na kuliingiza ubaguzi wa rangi katika sehemu za Kusini mwa Afrika na pia baada ya kuanzisha mfumo wa mashamba makubwa ya unyonyaji na mpango wa manamba katika Afrika ya Kati. Sifa hizi za mfumo wa kikoloni, katika maeneo tunayoyazungumzia, ziliwaathiri wenyeji wa sehemu zile moja kwa moja kwa undani zaidi kuliko maeneo mengine ya Afrika. Hivyo kama ambavyo tungetegemea katika sehemu hizi, siasa za Kiafrika na mapambano dhidi ya ukoloni vilienea zaidi na vilikuwa na harakati kubwa zaidi na uhusiano mkubwa zaidi wa kimataifa kuliko kilivyokuwa katika sehemu nyingine za Afrika. sifa ya pekee kabisa katika sehemu hizi ilikuwa ile ya matumizi ya kupinga mawazo ya mkoloni na majukumu ambayo tabaka la wafanyakazi au makabwela ambalo lilitokea kuendelea zaidi Kusini mwa Afrika kuliko sehemu nyingine za Afrika. vile vile katika sehemu hizi za Kusini mwa Afrika, na hasa Afrika Kusini mwa Msumbiji, wakulima wadogowadogo pia walihusika sana na harakati hizo. Sura hii itachunguza namna mabadiliko yalivyotokea katika mikakati ya kupinga utawala katika sehemu za Kusini na Kati katika Afrika, na hasa katika nchi za Afrika Kusini, Kongo ya Wabelgiji na makoloni ya zamani ya Wareno.

## *Ukinzani wa Jumla, Utaifa na Siasa katika Afrika ya Kusini na Nchi Jirani*

Ukinzani dhidi ya utawala wa kikoloni na unyonyaji wa kibepari nchini Afrika ya Kusini ulichukua sura kuu nne: Ukinzani wa wakulima wadogowadogo, makanisa yaliyojitenga, vyama vya wasoni, na mwisho vyama vya wafanyakazi.

Katika kukabili hali ya umaskini ambayo ilikuwa ikiongezeka na pia hali ya

uchumi ambayo haikuweza kutabirika, wakulima wadogowadogo walianza kuchukua hatua nyingi ambazo zilikuwa na makusudi ya kuilinda ardhi na mifugo yao na kupinga kuongezeka kwa kodi ya kichwa na kupelekwa manamba. Hali hii ilitokea baada ya mabadiliko makubwa ya kiuchumi Afrika ya Kusini, kutoka uchumi wa wakulima wadogowadogo hadi uchumi wa kutegemea kazi za kuajiriwa. Mara nyingi hatua zilizochukuliwa zilikuwa za ghafla na zilifanywa na watu binafsi, kama vile kutoroka, kukwepa kulipa kodi, kuvunja sheria za uandikishaji wa vitu na kushambuliwa kwa machifu vibaraka wa wakoloni na askari polisi walioonyesha utiifu kwa serikali. Katika sehemu zingine hatua hizi zilikuwa za mshikamano na ushirikiano katika Ukinzani. Hivi ndivyo ilivyokuwa katika majimbo ya Transkei, Pondoland na Findoland ambako kulikuwa na kampeni iliyoenea sehemu kubwa tangu 1993, hadi 1917. Katika kampeni hii, wakulima hao walikataa kulipa kodi ya majosho ya ng'ombe wao, Walianzisha mgomo kama hatua kuyapiga baruti na kuyabomoa matenki ya kuogesha ng'ombe. Miaka minne baadaye, wanawake wa vijijini katika jimbo la Transkei walianzisha mfululizo wa migomo dhidi ya wafanya biashara wa Kizungu. Nia yao ilikuwa kupinga upangaji wa kiholela wa bei na hivyo walikataa kunza bidhaa muhimu bila kulipwa fedha taslimu. Hatimaye ilibidi serikali na machifu watiifu waingilie kati ili kuuzima mgogoro huo.

Migomo ya wakulima wadogowadogo ilitokea mara kwa mara katika Afrika ya Kusini-Magharibi ambako serikali ya Afrika ya Kusini ilikuwa imeanza tu kujiimarisha kiutawala tangu Vita Vikuu vya Kwanza. Kuanzia wakati huo, serikali ya Jan Smuts ilikikandamiza kikatili kikundi cha Bondelswart ambacho kilitokana na mbari ya Nama iliyoishi maisha ya ufugaji ng'ombe kwa wingi katika sehemu za kusini. Watu hawa walikuwa wakipinga kuongezeka kwa kodi. Mwaka 1922, jeshi lilitumwa kwenda kuwaadhibu. Jeshi lilikuwa na askari wapatao 400 wakiwa na ndege pamoja na bunduki kubwa.

Miaka mitatu baadaye, vitendo vya kikatili kama hivyo viliwakumba pia "machotara" waliokuwa wakiishi kando ya mto Rehoboth katikati ya nchi. Kijiji chote kilizungukwa ua majeshi na wakati huohuo ndege za kivita zilionekana angani. Wanakijiji waliamua "kusalimu amri": Karibu 640 kati yao waliwekwa kifungoni. Ingawa matatizo ya watu wa Bondelswart na Rehoboth yalizungumziwa kwenye Umoja wa Matifa, kwa kuwa Afrika Kusini-Magharibi ilikuwa ni himaya iliyo chini yake hapakuwa na hatua zozote zilizochukuliwa kuzuia ukatili kama huo usitokee tena hapo baadaye.

Vikundi vya ukinzani vilivyokuwa vikubwa zaidi na vilivyokuwa na mashiko zaidi na vile vilivyoongozwa na makanisa yenye kujitegemea ya aina mbalimbali za Kizioni na Kiethiopa ambayo yalikuwa yameenea sana Afrika Kusini. Idadi yake iliongezeka haraka sana kutoka 76 mwaka 1918 hadi kufikia 320 mwaka 1932, na hata kufikia 800 mnamo mwaka 1942.

Wakulima wadogowadogo walikuwa ndio msingi wa kijamii katika migogoro hii, ingawa wakazi wa mijini ndio waliokuwa katika mstari wa mbele zaidi kuendeleza harakati hizo.

Licha ya serikali kuwa macho kila wakati, vikundi hivyo vya dini vilijihusisha mara kwa mara katika mgogoro na hata mapambano. Katika mwaka 1884 Nehemiah Tile, mhubiri wa Kimethodi, aliwahimiza waumini wake wa Tembulanda wasiwatii watumishi wa serikali. Mnamo mwaka 1921, kikundi cha dini ya Kiethiopia, kilichojulikana kama *Israelitea* na kilichokuwa chini ya uongozi wa Enock Mgijima kilikataa kwa nguvu kuhama kutoka kwenye vitongoji vya mji wa Queenstown ambako walikaa bila idhini. Lakini kikundi hicho kilishambuliwa na askari waliokuwa na bunduki na watu 163 kati yao waliuawa na 129 kujeruhiwa.

Vikundi vingine vya dini viliunganisha hisia za kinabii na mtazamo wa Kigarvey, Kikundi kilichokuwa mashuhuri sana ni kile cha Wellington ambacho kilijipatia jina hilo kufuatana na mwanzilishi wake ambaye alijulikana kama Wellington Butelezi. Kikundi hiki kilivuma kuanzia mwanzo wa miaka ya 1920 hadi kufikia miaka ya katikati ya 1930. Wellington Butelezi aliwahakikishia wafuasi wake katika jimbo la Transkei kwamba Waamerika wenye asili ya Kiafrika wangekuja kwa ndege ili kuwasaidia kujikomboa. Ingawa yeye pamoja na maluteni wake walikamatwa na serikali na kuhamishiwa sehemu za mbali, mawazo yake yaliendelea kudumu. Baadaye vikundi mabalimbali vilijitokeza katika misingi ya kisiasa na kidini ili kuendeleza fikra hizo.

Hadi kufikia sehemu ya pili ya miaka ya 1930, vikundi vya dini vya Kikristo vyenye matazamo wa Kiafrika vilikwishakosa mashiko ya kufanya kazi kama vyombo vilivyotumiwa kukinzana na ukoloni. Katika kipindi tunachokijadili, katika sehemu za Kusini na hata sehemu zingine za bara la Afrika, jukumu la harakati dhidi ya ukoloni lilikuwa linachukuliwa na vikundi vya kisiasa ambavyo vilikuwa vimeundwa kwa uthabiti zaidi. Vikundi hivi vilikuwa vya tabaka bora na vya wafanyakazi na havikuhusiana na misingi ya kimbari. Kikundi cha kwanza mashuhuri na muhimu kuliko vingine vyote ni kile kilichojulikana kama *African National Congress* (ANC) ambacho kiliundwa mwaka 1912. Hapo mwanzo kilianzishwa kama chama cha Waafrika wa nchi zote zilizokuwa Kusini mwa Afrika chini ya milki ya Waingereza. Mkutano wao wa katiba ulihudhuriwa na wajumbe kutoka Rhodesia, Basutoland, Bechuanaland na Swaziland. Baadaye vyama vya siasa vya kitaifa vilianzishwa katika kila mojawapo ya nchi hizo. Kwa kawaida, vyama hivyo vilifuata mfumo na mawazo ya ANC. Vyama vingi vya kisiasa sehemu za Kusini, Kati na Kaskazini mwa Afrika zilitumia sio tu jina la ANC lakini pia, kwa namna na viwango mbalimbali, muundo, taratibu, kanuni na hata mbinu zilizokuwa zikitumiwa na chama hicho.

Hadi kufikia kipindi kati ya Vita Vikuu, chama cha ANC kilikuwa kimemaliza miaka saba ya mapambano yenye dhoruba kali. Hata hivyo, uundaji wake haukumalizika hadi mwaka 1925 ambapo kilibadilisha jina lake katika mkutano mkuu wa mwaka kutoka *South African Native National Congress,* Chama cha Kitaifa cha Wenyeji wa Afrika ya Kusini) na kuwa *African National Congress,* (Chama cha Kitaifa cha Afrika). Mwaka huohuo, chama hiki kilikuwa na wimbo na

bendera yake yenyewe. Wimbo wake uliitwa "Nkosi Sikelel' Afrika" (Mungu Ibariki Afrika). Bendera yake ilikuwa na rangi tatu: nyeusi, Kijani na dhahabu. Rangi hizo ziliashiria watu (rangi nyeusi), mbuga za Kijani na mashamba ya rutuba na utajiri mkuu wa nchi (rangi ya dhahabu). Kati ya mwaka 1919 na 1935 chama cha ANC kilifanikiwa katika mambo kadhaa ya kisiasa. Mnamo mwaka 1926, kilianzishwa kampeni kubwa dhidi ya mfululizo mpya wa mapendekezo ya sheria za ubaguzi wa rangi ambazo serikali ya Waziri Mkuu wa wakati ule, J. Hertzog, alikuwa amietaka zipitishwe. Mwezi Februari 1926, chama cha ANC kiliitisha mkutano mkuu katika jimbo la Bloemfotein ili kulaumu ubaguzi wa rangi wa namna yoyote ile. Mkutano huo pia ulitaka pawe na usawa wa watu wote unaolindwa kikatiba bila kujali rangi. Mkutano huo pia uliamua kususia mikutano ya bandia iliyojulikana kama "ya wenyeji" ambayo iliitishwa na serikali.

Mwisho wa mwaka uleule, Chama cha ANC kiliitisha Mkutano Mkuu wa Kwanza Usiokuwa wa Wazungu katika mji wa Kimberley. Vyama vingine vilivyoshirikishwa ni vyama kadhaa vya Kiafrika na Chama cha Siasa cha Afrika ambacho kilikuwa ndicho chama kikuu cha "machotara". Chama kingine kilichoshirikishwa ni *South African Indian Congress* (Chama cha Wahindi wa Afrika Kusini) ambacho kilianzishwa muda mfupi tu baada ya Vita Vikuu vya Kwanza. Mkutano huu ulilaumu vikali ubaguzi wa rangi nchini na kupinga kwa nguvu sheria mpya za Hertzog. Vilevile ulihimiza "ushirikiano wa karibu zaidi kati ya watu wa Afrika ya Kusini wasio Wazungu". Hii ilikuwa ni hatua kubwa sana na pia ulikuwa mwanzo wa ushirikiano mahimu dhidi ya ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini.

Chama cha ANC kilikuwa pia kikijishughulisha sana na mambo ya nje ya nchi. Kilichangia katika kuwashirikisha wazalendo wa Afrika Kaskazini katika *Pan-African Movement* (Umoja wa Waafrika Wote) S. "Paatje, ambaye alikuwa mmojawapo wa waanzilishi wa viongozi wa ANC, ndiye aliyehudhuria Mkutano Mkuu wa Umoja wa Waafrika Wote mwaka 1919, na mnamo mwezi Februari 1927, Rais wa ANC J.J. Gamede aliitembelea Urusi.

Hata hivyo, shughuli za ANC zilizorota sana kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1930. Hii ilisababishwa hasa na uongozi ambao ulichukuliwa na watu wenye siasa lakini waliokuwa na hofu nyingi za kuingiliwa kwa chama na itikadi za kikomunisti.

Katika nchi za jirani zilizoko kusini mwa Afrika, kuzuka kwa vyama vya kizalendo vya siasa kulichukua mwelekeo karibu sawa na wa Afrika Kusini, ingawa hakukuweza kufikia kiwango cha Kusini. Kwa kawaida, vyama hivi vilianzishwa kama "Vyama vya Wenyeji", "Mikutano ya Wenyeji" au "Vyama vya Maendeleo ya Jamii." Mwanzoni vyama hivi vilishughulikia masuala ya sehemu vilikoanzishwa, lakini baadaye vilipanua shughuli zake.

Nchini Nyasaland, "Chama cha Kwanza cha Wazalendo" kilianzishwa muda mfupi tu kabla ya Vita Vikuu vya Kwanza, na hadi kufikia mwishoni mwa 1920, vyama hivyo vilikuwa vimeenea pote nchini. Kwa mfano, mwaka 1933, vyama kumi na vitano vilikwishaanzishwa katika miji mikubwa kama vile Zomba, Blantyre

na Limo. Katika Rhodesia ya Kaskazini, chama cha Kwanza cha "maendeleo ya jamii" kiliundwa mwaka 1923 na kilichukua sura ya vyama vya namna ileile vilivyokuwa nchini Nyasaland. Baadhi ya waanzilishi wa chama hiki ni David Kaunda, baba yake Kenneth Kaunda. Kuanzia mwaka 1930 na kuendelea, vyama vya namna ile ile kilianzishwa mjini Livingstone, Makao Makuu ya utawala wa koloni hilo, na sehemu nyingine nyingi, hasa katika miji iliyokuwa katika Copper Belt (Ukanda wa Shaba) na pia kando ya reli.

Rodesia ya Kusini, vyama vya kisiasa vyenye sura mpya kabisa vilianza kuundwa katika miaka ya kwanza baada ya Vita Vikuu. Chama cha *Rhodesia Bantu Voters Association,* ambacho kilinndwa Januari 1923, kilidai haki zaidi za Waafrika katika kupiga kura na kurudishwa kwa ardhi iliyochukuliwa. Shughuli zake zilikomea katika maeneo ya Bulawayo na wilaya kadhaa katika jimbo la Matebeleland. Palikuwa pia na chama cha maendeleo ya jamii katika mji wa Gwelo na chama kimoja cha wenyeji katika jimbo la Mashonaland.

Katika nchilindwa za Kiingereza, Basutoland, Bechuanaland na Swaziland, ambazo zilikuwa zimeshikamana sana na muungano wa Afrika ya Kusini, vyama vya mapambano dhidi ya ukoloni vilishirikiana sana na ANC. Chama kilichojitokeza sana nchini Basutoland ni kile cha *Lekhotla la Bafo,* yaani chama cha Maskini, ambacho kilifanya kazi kubwa sana muda wote kati ya Vita Vikuu vya dunia. Msingi wa kijamii wa cha *cha Lekhotla la Bafo* ulitokana na wakalima wadogowadogo ambao wengi wao walikuwa wachimba migodi katika jimbo la Transvaal. Chama hicho kiliwatia wasiwasi viongozi wa ANC kwa sababu ya msimamo wake wa kimapinduzi na pia kwa sababu tangu mwaka 1928, kilianza kushirikiana zaidi na chama cha Kikomunisti cha Afrika ya Kusini. Utawala wa Kiingereza uliwaamuru machifu kuipiga marufuku mikutano ya chama hicho. Lakini mwezi Agosti, mwaka 1928, Chama cha *Lekhotla la Bafo* kilifanya maandamano makubwa katika mji wa Maseru kuipinga hatua hiyo. Haya yalikuwa maandamano ya kwanza makubwa kufanyika katika historia ya Basutoland na yalihudhuriwa na maelfu kadhaa ya watu.

Misingi ya kijamii ya vyama hivi vya awali vya kisiasa kusini mwa Afrika haikuwa mipana. Mara nyingi viliwahusu tabaka bora la wasomi peke yao, ambao wakati ule walikuwa wakifanya kazi za serikali. Vilevile, mara nyingi hapakuwa na programu zilizokuwa wazi na utekelezaji wa shughuli zake. Hata hivyo, tunaweza kusema kuwa huu ulikuwa ni mwanzo na msingi wa vyama vingine zaidi vya baadaye, vya kudumu zaidi na vyenye uwezo mkubwa zaidi.

Vyama vya wafanyakazi katika maeneo ya viwanda vilileta sura mpya ya mapambano dhidi ya ukoloni. Chama cha kwanza kikubwa katika Muungano wa Afrika ya Kusini kilianzishwa katika migodi ya kampuni ambayo ilitumiwa na wenye migodi hiyo kuzuia wafanyakazi hao vyakula na mahitaji mengine.

Mgomo uliofuata ulitokea mjini Johannesburg, na uliwahusu wazoaji wa takataka. Ingawa wagomaji hao walikuwa wachache kiidadi, walikuwa wamejiandaaa kikamilifu. Mgomo huo ulizimwa, na wote walioshiriki walifunguliwa

mashitaka. Kati yao, 152 walihukumiwa kifungo cha miezi miwili. Mnamo tarehe 1 Julai 1918 wafanyakazi Waafrika 1500 katika migodi mitatu waliamua kugoma. Polisi waliwalazimisha kurudi katika migodi hiyo baada ya mapambano makali ambayo wafanyakazi hao walitumia mashoka, sululu na mitalimbo kama silaha zao. Mwezi Februari, mwaka 1920, mgomo mpya uliikumba migodi ishirini na miwili katika Transvaal. Migomo hii iliwakusanya pamoja wafanyakazi Waafrika 71,000 ambao walitoka katika mbari mbalimbali.

Majeshi pamoja na polisi waliitwa ili kuuzima mgomo huo ambao ulikuwa mkubwa kuliko yote iliyowahi kutokea katika historia ya Afrika kabla ya 1946 mwaka ambapo mgomo mkubwa ulitokea vilevile katika jimbo la Transvaal.

Nchini Rhodesia, harakati za kwanza za wafanyakazi wa kawaida zilianza tarehe 22 Mei katika machimbo ya Mufulira yaliyoko kaskazini ya Rodesia. Harakati hizo zilienea hadi machimbo ya Nkama tarehe 26 Mei na pia katika machimbo ya Luansha tarehe 28 Mei. Wachimba migodi hao walidai mishahara mikubwa zaidi na kupunguzwa kwa kodi. Pia walilaani hali duni za maisha katika sehemu zao za kazi na ubaguzi wa rangi. Wachimba migodi ishirini na wanne waliuawa au kujeruhiwa katika mapambano ambayo yalizaka kati yao na majeshi, na wafanyakazi kadhaa waliwekwa ndani .

Katika kilele cha migomo ya wafanyakazi katika viwanda, ambayo ililikumba eneo la kusini mwa Afrika katika miaka ya kwanza baada ya Vita Vikuu, chama kikubwa kuliko vyote vya wafanyakazi Waafrika kilianzishwa mnamo Januari 1919 katika mji wa Cape Town. Chama hiki lilijulikana kama *Industrial and Commercial Worker's Union of Africa* (ICU), (yaani Umoja wa Wafanyakazi katika viwanda na sehemu za biashara, barani Afrika). Chama hiki kilianzishwa na Clemeant Kadalie, ambaye alikuwa mwalimu na mfanyakazi wa msimu kutoka Nyasaland wakati wa mgomo wa wafanyakazi wa bandarini wenye asili ya Kiafrika na machotara. Wanachama wake waliongezeka haraka toka watu chini ya 30 wakati wa uzinduzi hadi kufikia 30,000 baada ya miaka mitano na kufikia wanachama 100,000 ilipofika mwaka 1927. Pia kulikuwa na wanachama washiriki kutoka sehemu za nje ya Muungano wa Afrika ya Kusini. Chama cha ICU, ambacho kilikuwa kimetawaliwa na itikadi ya kijamaa kama utangulizi wa katiba yake ulivyoelezea waziwazi, kiliwaahidi wanachama wake kuwa kingepigania mishahara mikubwa zaidi, hali nzuri zaidi za maisha, malipo ya uzeeni, malipo ya ugonjwa na kulinda haki za wafanyakazi. Chama hicho kilitangaza kuwa kilikuwa kinahusika na bara lote la Afrika na kilifikia kilele chake cha ustawi katika miaka ya katikati ya 1920. Lakini kilidhoofika ghafla kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1920 hadi kufikia 1930. Sababu kubwa ni kwamba wakati huo kilikuwa kimegawanyika katika vikundi vitatu.

Mwelekeo wa kijamaa pia ulijitokeza katika baadhi ya vyama vya awali vya wafanyakuzi Waafrika. Mojawapo ya vyama hivyo ni kile cha *Industrial Workers of Africa*, yaani Chama cha wafanyakazi wa viwandani Barani Afrika. Uundaji na

uendelezaji wa chama hicho, vilisaidiwa sana na shirikisho la Kimataifa la Vyama vya kijamaa au *International Socialist League*. Shirikisho hilo lilianzishwa na Wazungu wa Afrika Kusini wenye mawazo ya kijamaa na pia wafanyakazi wenye fikra za kimapinduzi. Watu hao walikuwa wameanza kuelewa umuhimu wa umoja wa wafanyakazi wote bila kujali rangi. Hii ilijidhihirisha hasa katika miito iliyotolewa katika makaratasi yaliyosambazwa kwa wafanyakazi weusi na weupe. Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Kijamaa na vyama vingine vya kijamaa katika Afrika Kusini viliungana pamoja katika Mkutano Mkuu uliofanyika Cape Town mwaka 1921 na kuunda *Communist Party of South Africa* (Chama cha Kikomunisti cha Afrika Kusini). Chama hiki ndicho kilikuwa chama cha kwanza cha Kikomunisti barani Afrika. Mwanzoni, wanachama wake walikuwa ni weupe tu, lakini kufikia mwanzoni mwa miaka ya 1930, Waafrika ndio waliokuwa wengi zaidi kati ya wanachama wake na Katibu Mkuu wake alikuwa Albert Nzula (1905 - 1934) aliyetokana na kabila la Zulu. Ukombozi wa taifa ukawa ndilo lengo kubwa la shughuli za Chama hiki.

## *Kongo ya Wabelgiji*

Harakati za kijamii katika Kongo ya Wabelgiji zilipungua kwa sababu ya kuongezeka kwa madaraka ya serikali, kuanzishwa kwa sera kubwa ya ulinzi na kuzuka kwa magonjwa. Hata hivyo, upinzani wa wazalendo uliendelea ingawa kwa kiwango kidogo.

Ukinzani wa wakulima wadogo nchini Kongo ulichukua sura nyingi tofauti na ulikuwa na madhumuni ya kuzuia au kupunguza uzito wa mfumo wa kibepari ulioletwa na wakoloni ambao ungeweza kuathiri maisha yao ya kijadi. Upinzani huo ulitokea ghafla, hapa na pale, bila kuonekana kwa urahisi. Ukwepaji wa kulipa kodi uliendelea na kuongezeka zaidi katika miaka iliyofuatia kumalizika kwa Vita Vikuu vya Kwanza. Maelfu ya wakulima wadogowadogo wa Kondo Kongo walikimbia na kuvuka mipaka iliyokuwa wazi na kuingia majimbo ya mipakani nchini Angola na Kongo ya Wafaransa. Wakati uleule, wengine walijificha msituni kabla ya kufika kwa watoza kodi. Watu wengi wa vijijini walitumia mbinu ya namna hiyo ili kukwepa kufanyishwa kazi katika miradi ya serikali, migodi na mashamba makubwa ya Wazungu. Isitoshe wenyeji wengine walikataa kulima pamba na au mpunga, mazao waliokuwa wamelazimishwa kuyalima. Mara nyingine walilima maeneo nadogo zaidi kuliko walivyotakiwa au walipanda kiasi kidogo tu.

Kwa kuwa mfumo wa kikoloni ulikuwa umeenezwa katika sehemu za mbali zaidi na hata kuanzishwa umoja wa machifu waliokuwa waaminifu kwa utawala wa kikoloni, upinzani ambao ulikuwa umeanza kujitokeza mara nyingi kabla ya Vita Vikuu vya Kwanza, ulitoweka kwa kiasi kikubwa. Mara moja moja, wenyeji waliponyanyaswa waliwashambulia watu ambao waliuwakilisha udhalimu wa kikoloni, yaani ,machifu waaminifu, polisi wa Kiafrika na watoza kodi. Kilichokuwa

na madhara zaidi ilikuwa migomo ya wakulima wadogowadogo ambayo yasemekana ilitokea katika sehemu za chini za Mto Kongo kati ya 1920 na 1922. Mnamo mwaka 1931 mgomo mkubwa ulifanywa na wakulima wadogowadogo na wafanyakazi wa mbari ya Pende katika mji wa Kwilu; mgomo ambao ulisababishwa na kuongezeka kwa kodi ya kichwa, kupungua kwa bei za mazao ya wakulima kwa kiwango cha asilimia 50 na uamuzi wa kampuni ya Unilever kupunguza mishahara ya wafanyakazi wa mashamba yake. Mgomo huo ulizimwa mara moja, na zaidi ya watu 400 wa mbari ya Pende na mzungu mmoja walipoteza maisha yao katika mapambano hayo.

Kama ilivyokuwa katika Afrika ya Mashariki na Kusini, vikundi vingi vya kidini vyenye mwelekeo wa kisiasa vilizuka sana nchini Kongo vikipinga mfumo wa siasa uliokuwepo. Vikundi hivi vilikuwa ni pamoja na vile vya Muvungu, Lukusu, Mpewe na "Nyoka Azungumzaye". Vilevile kulikuwa na vikundi vilivyojulikana kama "Tume Nyeusi ya tunzi" na "Watu wa Chui". Vikundi hivi viliwavutia wenyeji wengi hasa kwa vile utawala wa kikoloni ulikuwa umevipiga marufuku vyama vya kisiasa, Kueneaza kwake pia kulionyesha kuongezeka kwa wasiwasi na kukatishwa tamaa kwa wenyeji kulikoletwa na matatizo ya uchumi ya mwaka 1921 na mpomoko wa uchumi miaka kumi iliyofuata.

Kikundi kikubwa kati ya vikundi hivi ni kile cha Ukimbangu ambacho kilijipatia jina lake kutokana na Simoni Kimbangu, mwenyeji mmoja wa mbari ya Bakongo. Kiongozi huyo alikuwa ni katekista ambaye alitangza kuwa alitokewa na Mwenyezi Mungu na kupewa uwezo wa kuponya wagonjwa, kupigana na uchawi, na kufufua wafu. Kiongozi huyo pia alitaka kwa namna fulani kuwa angewakomboa Waafrika kutoka katika uonevu wa kikoloni. Utawala wa Kibelgiji ulimkamata na kumweka ndani kwa sababu ya hotuba zake za kupinga ukoloni, kuenea kwa sifa zake na nguvu za ukakamavu na baadhi ya wafuasi wake. Baadaye alipelekwa Katanga tarehe 14 Septemba 1921 ambako alifariki kama shahidi miaka thelathini baadaye.

Ingawa Kimbangu mwenyewe hakuwa mwanamapinduzi, wafuasi wake walikifanya chama chake kiwapinge vikali Wazungu badala ya kubakia chama cha kidini peke yake; hasa baada ya kufungwa kwa kiongozi wao. Wafuasi hao waliwahimiza watu wasiwatumikie Wazungu, wasilime mazao ya kuuza nje yaliyoamuliwa na utawala wa kikoloni, wasilipe kodi, wasiwapeleke watoto wao katika shule za misheni, kutowatii Wabelgiji kwa jumla. Katika miji na vijiji wafuasi wake walishiriki kwa nguvu katika mapambano dhidi ya ukoloni, na propaganda zao zilisababisha migomo ya wafanyakazi wa ngazi za juu na chini katika reli ya Zaire kuanzia 1921 hadi 1925. Ingawa wafuasi hao wa Kimbangu walikandamizwa vikali, nguvu zao hazikuisha. Vikundi vingi vyenye sura tofauti za Ukimbangu vilienea sehemu zote za Kongo ambako wafuasi wake walianzisha uhusiano na makanisa mengine ya Kikristo yenye mwelekeo wa Kiaftika nchini Nigeria na Uganda. Pia walianzisha uhusiano na wapiuzani wa ukoloni wa Kifaransa katika Kongo ya

Kifaransa.

Kikundi kingine kikubwa cha kidini kinachojitegema, kilichoanzishwa wakati mmoja na Ukimbangu, ni *The African Watchtower*, ambacho kilijulikana nchini Kongo kama Kitawala. Misingi mikubwa ya kikundi hiki yaelekea ilikuwa ni Rhodesia ya Kaskazini, Nyasaland na Tanyanyika. Kutoka huko kikundi hiki kilienea katika jimbo la Katanga ambako hadi kufikia mwaka 1926 kilikuwa kimejiimarisha sana. Kikiwa chini ya uongozi madhubuti wa Tomo Nyirenda , chama hiki kilidhihirisha upinzani wake dhidi ya ukoloni. Pamoja na matamshi ya kizalendo kama vile "Afrika ni ya Waafrika" na "usawa kwa Watu Wote", Nyirenda na kikundi chake waliwahimiza wafuasi wao wawaue Wazungu na vibaraka wao wa Kiafrika, hasa machifu waaminifu. Watawala wa Kibelgiji walimsaka kwa kuogopa athari yake iliyoongezeka siku hadi siku. Nyirenda alikimbilia Rhodesia ya Kaskazini mnamo mwaka 1926; lakini huko watawala wa Kiingereza walimkamata na hatimaye kumnyonga. Kama ilivyokuwa wakati wa Kimbangu, kuuawa kwa nabii huyo kulikifanya kikundi cha Kitawala kipate wafuasi wengi na kuenea zaidi katika sehemu za vijijini ambako viongozi wake walilaani vikali utozwaji kodi na walionyesha chaki za waziwazi kwa machifu walioteuliwa na wakoloni.

Upinzani wa wafanyakazi wa kawaida dhidi ya ukoloni ulitokea pia Kongo ingawa ulienea polepole sana ukilinganishwa na Afrika Kusini. Tabaka la wafanyakazi wa viwandani lilianza kujitokeza tu baada ya uvumbuzi wa shaba, madini ya bati na *uranium* katika jimbo la Katanga, uvumbuzi wa almasi katika jimbo la Kasai na dhahabu katika maeneo ya Kilo Moto. Hadi kufikia miaka ya 1920, zaidi ya wafanyakazi 60,000 walikuwa wakifanya kazi ya uchimbaji wa madini.

Kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za bara la Afrika, kitendo cha kwanza cha Waafrika dhidi ya udogo wa mshahara na hali duni za maisha katika migodi, kilikuwa ni kuamua kuacha kazi na kurudi makwao. Wenyeji wengi walitoroka kutoka majimbo ya Katanga na Kasai ili kuwakimbia watu waliokuja kuwaandika kazi. Wengi waliamua kugoma au kususia kazi. Kwa mfano, mwaka 1921, idadi kubwa ya wachimba migodi wa Luishi walisusia kazi na kutembea kwa miguu hadi Elizabethvile ili kutoa malalamiko kwa serikali juu ya kuteswa kazini na kupewa chakula kidogo. Baada ya miaka miwili, mgomo wa namna ileile ulitokea katika machimbo ya Kokontwe: Isitoshe hata wakati wa Mpomoko wa uchumi duniani baada ya Vita Vikuu ya Kwanza migomo na maasi yalitokea katika machimbo ya *Union Minieres* ya Kipushi, Ruashi an Mswemu Ditu. Ghasia hizo ambazo zilitokea mwaka 1931 zilisimamisha shughuli za uchimbaji madini kwa muda fulani. Mwaka huohuo, wafanyakazi walisusia kazi mjini Elizabethville kama hatua ya kulaani bei kubwa zilizowekwa kwa bidhaa muhimu na maduka ya kampuni ya *Union Minieres* na yale ya Wazungu wenye maduka binafsi. Ghasia za namna hii ziliendelea kuenea miaka yote ya 1930 hadi kufikia kuwa mgomo mkubwa uliotokea mwaka 1941 ambapo maelfu kadhaa ya wafanyakzai wa Kiafrika walisusia kazi katika machimbo ya madini ya bati na shaba katika jimbo lote la Katanga.

Kama ilivyokuwa kwa upande wa vyama vya wafanyakazi, vyama vya kisiasa na kitaifa vilianza polepole sana katika Kongo ya Wabelgiji ukilinganisha na Afrika Kusini. Ama kwa hakika, vyama vya kitaifa vya kikwelikweli kama vile chama cha *Association de Bakongo* (ABAKO) yaani (Chama cha Wakongo), havikuanza hadi miaka ya mwishonimwishoni mwa 1950. Hata hivyo, katika kipindi hiki vilizuka vikundi vya kisirisiri vilivyojulikana kama Mbeni. Vikundi hivi vililetwa katika Kongo ya Wabelgiji na wanajeshi wa Kiafrika ambao walikuwa wamepigana Vita Vikuu vya Kwanza katika Aftika ya Mashariki ya Wajerumani. Mbeni lilikuwa jina la vikundi vya ngoma ambavyo pia vilikuwa na mfumo wa kusaidiana kati ya wanachama wake. Ingawa shabaha yao kubwa haikuwa kupinga ukoloni, nyimbo na ngoma nyingi ziliwadhihuki watawala wa Kizungu na zilionyesha chuki yao kubwa dhidi ya utawala wa kikoloni. Lakini uwezo na nguvu ya vikundi hivi vilipungua katika miaka ya 1930 kwa sababu ya kusakwa vikali na serikali, mbinu zao za mapigano ya kigaidi, migongano kati yao wenyewe, na uhamiaji wa mijini uliosababishwa na Mpomoko wa uchumi.

## *Upinzani wa Wenyeji dhidi ya Utawala wa Kikoloni Nchini Angola*

Waafrika wa Angola walikuwa ni watu wasiotakiwa kabisa katika nchi yao wenyewe. Wazungu waliwaona kama watu wasio na thamani ambao walistahili tu kuchapwa viboko au mara nyingine kufanyiwa ukatili na watawala hao wa kikoloni. Vitendo hivi vilisababishwa na matakwa ya Wazungu kuwaajiri Waafrika kazi kwa nguvu wakisaidiwa na watawala wa kikoloni na masetla wa Kireno. Hata hivyo waligundua njia nyingi za kujiepusha na uonevu wa wakoloni hao.

Namna ya kwanza ya ukinzani ilikuwa ni kuanzisha mapigano ya silaha. Njia hii haikuendelea kutumika baada ya Vita Vikuu vya Kwanza kwa kuwa haikuwa na mafanikio. Njia ya pili ilikuwa ni kwenda mafichoni katika maeneo yaliyokuwa mbali na mahali walipokuwa watawala hao wa kikoloni. Njia ya tatu ilikuwa ni changamani zaidi, nayo ilikuwa ni kuhama kwa siri kuelekea Kongo ya Wabelgiji, Rhodesia ya Kaskazini na hata Afrika ya Kusini - Magharibi. Mara nyingi watu kutoka katika vijiji walisafiri umbali mrefu wakipitia mazingira magumu wakiwa na watoto wadogo migongoni, ili kutoka katika mikono ya kidhalimu ya utawala wa kikoloni wa Kireno.

Njia ya nne ya ukinzani dhidi ya utawala wa kikoloni ilijitokeza katika vikundi vya kidini vilivyozuka wakati huo. Vikundi hivi vilianzishwa na Waafrika ili kupinga dini za kikoloni. Vikundi hivi vilikuwa tofauti na vile vilivyokuweko Kongo ya Wabelgiji; kwa kuwa vilikuwa vimeanzishwa kutoka nje ya Angola vilikuwa na wafuasi wachache na vilififia kwa urahisi sana. Mgomo wa kikundi cha Mafulu mnamo mwaka 1918 mara nyingi hutajwa kama mgogoro wa kwanza wa kidini nchini Angola ambao ulienea na kukua haraka hata kuanza kutumia silaha. Wafuasi

wa Simon Kimbangu waliweza kuwapata wafuasi wengine wengi kati ya kabila la Bakongo ambao walikuwa wakiishi katika mipaka ya Angola. Ingawa palikuwa na jitihada kubwa ya utawala wa ukoloni kukikandamiza kikundi cha Kimbangu katika miaka ya 1921 na 1922, chama hicho kiliendelea kuenea kwa njia za siri,.

Vikundi vingine pia vilijitokeza kama vile, Malaigini ambacho kilitokea hasa katika maeneo ya Canida mwaka 1930, na vile vile kikundi cha Cassongola ambacho kilijitokeza kwa muda mrefu katika kabila la Mbundu kuanzia mwaka 1924 hadi 1930. Chama cha Kitawala pia kilienea kuanzia Kongo ya Wabelgiji na Rhodesia ya Kaskazini hadi Angola mnamo mwaka 1932. Ingawa taarifa tuliyonayo ni finyu, vikundi hivi vya kidini vilionekana kutokuwa na uzito mkubwa. Kikundi cha kidini kilichowavutia wafuasi wengi kilianza katika miaka ya 1950 baada ya kuzuka kwa mawazo ya Toko.

Ingawa migogoro mingi iliwahusu wakazi wa vjijini, wasomi na waandishi wenye ustaarabu wa Kireno, mjini Luanda na Lisbon, walivilaani sana vitendo viovu vya ukoloni na hivyo walionyesha uzalendo wao kwa dhati. Baadhi ya watu wa namna hii waliofahamika sana ni Kasisi Antonio Jose de Nacimento (1838 - 1902), mwanasheria na mwandishi Jose de Fontes Pereira (1838 - 1891), mwandishi wa vitabu Joaquim Dias Cordeiro de Matta (1957 - 1894) na pengine pia wanachama wa kilichoundwa kupambana na ukoloni ambacho kilitokana na machapisho yaliyojulikana kama *Voz d'Angola Clamando no Deserto,* yaani sauti ya Angola iliyo Jangwani. Machapisho hayo yalitolewa Lisbon mwaka 1901,. Katika Angola yenyewe, chama kidogo cha watumishi wa serikali kilichojulikana kama *Linga Angolana* yaani shirikisho la Angola, kilitambuliwa rasmi na Gavana Mkuu, Narton de Matos, mnamo mwaka 1913. Punde tu pakatokea mgawanyiko katika chama hiki na chama cha *Gremio Africano* kikaundwa. Vyama vyote hivi havikuwa na wafuasi wengi na pia havikuwa na uwezo mkubwa.

Tukio lililokuwa na maana zaidi, pamoja na kuweko kwa vyama hivi vyote, ni "uhaini" wa Cuanza Norte uliozuka miaka ya 1916 na 1917. Wahusika katika tukio hilo walikuwa ni wasomi kadhaa waliochota ustaarabu wa Kireno wa wenyeji wa kabila la Mbundu ambao walikuwa wakiishi karibu na mji wa Luanda. Watu hawa waliungana kwa muda ili kutimiza azma yao. Kiongozi wao alikuwa ni Antonio de Assis Junior (1887 - 1960) ambaye alikuwa mwanasheria na mwandishi wa habari na vitabu. Alipinga vikali sana dhuluma za kikoloni na mapendeleo waliyopewa jamii ya Kisetla. Serikali ya kikoloni ilichukua hatua za haraka kwa vile iliogopa kukua kwa ushirikiano kati ya wasomi waliochota ustaarabu wa Kireno na wenyeji wa vijijini. Pia waliogopa kuwa migogoro hii ingeenea sehemu nyingine. Antonio de Assis junior alitiwa ndani na alinusurika kurudishwa kwao.

Mjini Lisboni, chama cha *Junta de Defensa do Dereitos de Africa* ambacho kiliundwa mwaka 1913 ua Waafrika waliokuwa wakiishi kule, haikuwa na uwezo mkubwa. Mfuasi mmoja wa chama hicho alijitenga na kuunda chama cha *Linga Africana,* mnamo mwaka 1919. Chama hiki kilishirikiana na Chama cha *Linga*

*Angolana de Luanda.* Mnamo mwaka 1921, chama cha *Junta de Defensa* kiliundwa upya na kujulikana kama *Partido Nacional Africano* ili kukikinga kisiingiwe na mawazo ya kijamaa.

Mwaka 1921, mwaka mmoja baada ya kurejea kwake, Balozi Narton de Matos, mpinzani mkubwa wa vyama hivyo viwili, yaani *Liga Angolana na Gremio Africano* alivivunjilia mbali vyama hivyo. Aliamuru Antonio de Assis Junior akamatwe, baadhi ya wanachama wake wakubwa warudishwe makwao, na kwamba chama cha *Linga Angolana* kivunjwe rasmi. Pia aliyapiga marufuku magazeti ya "wenyeji" na kusimamisha kupandishwa kwa vyeo kwa watumishi wa serikali wazalendo. Kufuatia pigo hili, vyama vya kitaifa Angola viliingia mafichoni.

Hali ya maisha nchini Angola ilianza kuwa ngumu sana, hasa baada ya kuanzishwa kwa utawala wa udikteta wa kijeshi wa Salazar mwaka 1926. Hivyo vyama vya Kiafrika vilionelea vianzishe sera ya ushirikiano na serikali. Chama cha *Liga Angolana* kiliruhushiwa kuanza tena shughuli zake miaka ya 1929 - 1930, baada ya "kusafishwa" kwa kuondolewa wanachama wenye siasa kali. Jina jipya la chama hicho likawa *Linga Nacional Africana.* Chama cha *Gremio Africano* ambacho kilikuwa kimefifia katika miaka ya 1920 kwa sababu ya kubanwabanwa sana, nacho kilijitokeza tena kwa jina jipya la *Associacao dos Naturais de Angola* (ANANGOLA). Vyama hivi viwili vililazimika kujihusisha na mambo ya kijamii peke yake kwa vile uwezo wake mkubwa ulikuwa umepunguzwa na pia kwa vile havikuwa tena na nguvu za kisiasa. Hivyo, upinzani wa kisiasa ambao ulionekana sana Afrika ya Kusini kati ya vyama vya watu wa tabaka bora na wafanyakazi haakutokea nchini Angola.

## *Msumbiji*

Aina ya upinzani iliyokuwako Msumbiji ilifanana sana na ile iliyokuwa Angola. Tofauti ilikuwa ni ukubwa au kuenea kwake. Palikuwa na mapambano ya silaha machache zaidi na pia uzoefu wa maandishi na uhusiano na vyama vya kisiasa vya Afrika nzima havikuwa vimeendelezwa sana. Kwa upande mwingine, idadi ya matukio ya upinzani iliyowahusu wafanyakazi na watu wa mashambani ilikuwa kubwa zaidi nchini Msumbiji kuliko Angola, na kuchipaka kwa dini mbalimbali kulikuwa kumeenea zaidi na hata kukawa na athari za kisiasa.

Upinzani wa mara kwa mara wa wakazi wa mashambani uliupa mfumo wa kikoloni na kibepari msukosuko mkubwa. Sababu kubwa ya harakati hizi ilikuwa ni kupinga kuchukuliwa manamba na kunyang'anywa utajiri wao. Kama ilivyokuwa katika miaka ya mwanzo ya ukoloni, ukwepaji na kulipa kodi ulitokea mara nyingi sana katika sehemu zote za mashambani za Msumbiji. Wenyeji hao walibuni mbinu mbalimbali za kupunguza au kuacha kulipa malipo yao ya mwaka. Wengi walitoa taarifa za uongo kuhusu umri wao au ndoa zao ili wasilipe fedha nyingi. Maelfu ya wakazi wa mashambani wa Msumbiji walijiepusha na misukosuko ya wakoloni kwa

kukimbilia nchi jirani. Misukosuko hiyo ni pamoja na kulazimika kulima pamba, kufanyishwa kazi kwenye mashamba ya kisetla na kwenye miradi ya serikali. Hadi kufikia mwaka 1919, ilikadiriwa kuwa zaidi ya watu 100, 000 wa Msumbiji ya kaskazini walikuwa wamehamia Nyasaland peke yake.

Baadhi ya wakimbizi hawa hawakutaka kutengana kabisa na jamaa au makao yao ya jadi. Hivyo, walikimbilia katika sehemu zenye madimbwi ambazo hazikuwa na watu wengi. Katika sehemu fulani,kulitokea jamii za kudumu za wakimbizi ambazo, baadhi yao, ziliweza kudumisha uhuru wao kwa muda wa miaka mingi kwa kuweza kustahimili hali mbaya za mazingira na misako ya askari wa kikoloni.

Njia ya upinzani iliyotumiwa zaidi na wakazi wa mashambani waliolima pamba na wafanyakazi katika mashamba makubwa ni kususia kazi za manamba. Haishangazi kuona kuwa upinzani wa wakazi wa mashambani haukufanyika kwa pamoja, kwa vile kulikuwa na mambo mengi yaliyowatenganisha wakazi wa mashambani na kutoridhika kwa wakazi wa mashambani kulijidhihirisha wazi zaidi. Kuanzia 1917 hadi 1921 wakazi hawa wa mashambani katika maeneo yote ya bonde la Zambezi walianzisha mgomo baada ya kukasirishwa na kazi za manamba, kuongezeka kwa kodi, kulazimishwa kulima pamba, kunajisiwa kwa wanawake na kulazimishwa kuingia jeshini. Mgomo huo uliongozwa na jamaa ya kifalme ya Barue wakisaidiwa na mizimu ya Kishona. Nia yao ilikuwa ni kuzikombea ardhi zao na kuutokomeza udhalimu wa mfumo wa kikoloni. Pia katika miaka ishirini iliyofuata, palitokea mfululizo wa migomo midogomidogo iliyosababishwa na wakazi wa mashambani katka maeneo ya Erati, Maguincal na Angoch katika sehemu za kaskazini mwa Msumbiji. Sababu kubwa ya migomo hii ilikuwa ni kulazimika kulipa kodi na kufanya kazi za manamba.

Iwapo hofu na ukandamizaji watu wasifanye upinzani wa waziwazi, mara nyingi chuki yao ilijitokeza kwa kupitia vielelezo vya utamaduni ambavyo havikueleweka kwa utawala wa kikoloni. Kwa mfano, kabila la Wachope ambalo liko kusini mwa Msumbiji, lilianzisha namna fulani ya nyimbo ambazo kwa jumla zililaani utawala wa kikoloni na hasa ziliwasuta watoza kodi ambao walikuwa wakichukiwa sana. Katika maeneo ya kaskazini, wasanii wa Kimakua na Kimakonde, waliwadhihaki watawala wa serikali, Weupe kwa Weusi, kwa kuanzisha mtindo wa kipekee wa uchongaji vinyago ambao uliwaumbua watawala hawa na kuwatolea utu wao.

Wafanyakazi wa mijini, kama ilivyokuwa kwa wale wa mashambani walianza harakati zao kwa matendo madogomadogo ya binafsi kama vile kutoroka kazini, kuhujumu vifaa na malighafi, ili kuharibu au kutokomeza mfumo mpya wa uchumi wa kibepari. Hadi kufika miaka ya 1910, wafanyakazi wa mijini walianza kubadili mikakati yao kwa kupigania hali bora zaidi kazini katika mfumo huo mpya. Oliveira, Guimares, Agostinho Jose Mathias, walijaribu kuunda chama cha *Unio Africano*, ili kuwaunganisha wafanyakazi wote wa Kiafrika mjini Louranco Marques

(sasa Maputo). Ingawa chama hicho kilikuwa na uwezo mkubwa wa mawazo na ushupavu, kilivunjika hata kabla ya kuanzishwa rasmi kwa sababu ya upinzani mkubwa kutoka katika serikali ya kikoloni yenye mfumo wa kibepari. Sababu zingine ni pamoja na kuwepo kwa vyama vingine vya wafanyakazi na kukosekana kwa umoja kati ya wafanyakazi wa Kiafrika.

Licha ya matatizo haya, kulikuwa na jitihada nyingi za kuanzisha vyama vya wafanyakazi mjini Lourenco Marques (Maputo). Migomo na ususaji wa kazi vilitokea kwa mfululizo. Mwaka 1913, wafanyakazi wa Ushirika wa Wafanyabiashara waligoma; mwaka 1917 madereva wa treni za mjini walisusia kazi; mwaka 1918 mafundi wa reli waligoma; na mwaka 1919 wafanyakazi wa kampuni moja ya uhandishi nao waligoma.

Kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Afrika, wafanyakazi wa bandari walikuwa ndio wenye msukumo mkubwa na mshikamano madhubuti. Kulitokea migomo mikubwa saba ambayo ilisababishwa na kukataa kwa kampuni za usafirishaji kuongeza mishahara ya Waafrika ili kulingana na kupanda kwa hali ya maisha. Ingawa migomo hiyo ilizuiwa kila ilipotokea na ingawa serikali ya kifashisti ilishika madaraka, migomo ya namna ile iliendelea kujitokeza hata baada ya mwaka 1926, japo kwa mara chache zaidi. Labda mgomo uliokuwa mkubwa sana bandarini ni ule mgomo wa Quiuhenta uliotokea mwaka 1933. Mgomo huo ulisababishwa na kupunguzwa kwa mishaham ya wafanyakazi wa gati ambayo hata kabla ya hapo ilikuwa ya chini sana. Mishahara hiyo ilikuwa imepunguzwa kwa asilimia 10 hadi 30.

Kuna sababu nyingi zilizowazuia wafanyakazi wa Msumbiji katika jitihada zao za kuunda umoja katika kipindi hiki. Kwanza, idadi yao ilikuwa ndogo mno. Sekta ya kibepari ya Msumbiji ilikuwa ndogo kiasi kwamba iliwaajiri watu wachache sana kwa masharti ya kudumu. Isitoshe, serikali ilipiga marufuku kuanzishwa kwa vyama vya wafanyakazi wa Kiafrika. Vile vile chama cha wafanyakazi wa Kizungu kiliwachukia wafanyakazi wa rangi na mawazo mabaya juu ya utamaduni wa Mwafrika kwa kuzingatia itikadi rasmi ya serikali yao. Hata hivyo, kulikuwa na Wazungu wachache waliowatetea Waafrika. Hivyo, tunaweza kusema kuwa wafanyakazi hawa wa Kiafrika walikuwa katika matatizo magumu, hasa kwa vile walikuwa wachahe, walikuwa mbali na vyama vikubwa vya wafanyakazi, na walipingwa vikali na vyombo vya serikali na mfumo wa kibepari.

Kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine za Kusini na Kati katika Afrika, vikundi vya kidini vilikuwa ni uwanja mwingine kwa wafanyakazi na wakazi wa mashambani kuweza kuelezea chuki yao dhidi ya mfumo mpya wa kijamii na unafiki uliotolewa na makanisa ya Kikristo. Mwaka 1918, kulikuwa na vikundi vya kidini 76 vilivyojulikana nchini Msumbiji. Miaka 20 baadaye, idadi hiyo ilikuwa imeongezeka na kufikia 380. Idadi ya wafuasi wa vikundi hivi ilitofutiana kuanzia watu kadhaa hadi kufikia zaidi ya 10,000. Kikundi kilichokuwa na wafuasi wengi ni kile cha Missao *Christa Ethiopia* ambacho kilienea katika majimbo yote manne. Karibu vikundi vyote hivi vya kidini vilianzishwa Msumbiji na wafanyakazi waliohamia nchini humo kutoka Afrika ya Kusini na Rhodesia. Sehemu kubwa ya vikundi hivi

haikuwa na msimamo madhubuti dhidi ya ukoloni. Upinzani wao ulikomea tu katika kuushambulia kwa maneno.

Kuna ushahidi pia wa kuwapo kwa chama cha Kiislamu, chenye mtazamo mpya, katika sehemu za kaskazini ya Msumbiji. Chama hiki kilikuwa kimewakusanya pamoja Waislamu ambao kihistoria walikuwa wapinzani wakubwa wa utawala wa kikoloni. Katika miaka ya 1920, viongozi wa dini ya Kiislamu walipinga vikali kazi za manamba, mishahara midogo, na kunyang'anywa kwa ardhi katika maeneo ya Quilemane. Baadhi ya machifu wa Kiislamu na raia zao pia walihusika katika mgogoro huo katika miaka ya 1930. Hata hivyo, sababu halisi ya mgogoro huo haijulikani hadi leo.

Upinzani uliofanywa na wasomi wa mijini pia ulikuwa muhimu, ingawa haukuwa umeshika mizizi kama ilivyokuwa Angola. Mwito wa kwanza kubadili mfumo wa maisha ulifanywa mwaka 1908 baada ya kuchapishwa kwa gazeti mjini Lourenco Marques (Maputo) lililojulikana kama *O Africano*. Gazeti hili lilikuwa ni chombo cha chama cha *Gremio Africano* (Umoja wa Waafrika). Chama hiki kilikuwa ni kikundi cha kijamii kazini ambacho kilianzishwa na machotara waliojulikana kama *Grades Familias* miaka miwili kabla ya hapo. Ingawa kikundi hiki kilikuwa na nafasi nzuri kimaisha na ingawa kilijiona kama ni muhimu sana, jamaa wengi wa *Gremio Africano* waliona kama ni wajibu wao kuwatetea Waafrika walioonewa. Chama kilichorithi chama hicho kiliitwa *O Brado Africano* (Sauti ya Mwafrika). Chama hiki kiliendelea na madhumuni karibu yale yale kikiwa kama ni mlinzi wa kujitolea wa Waafrika wafanyakazi na wakazi wa mashambani.

Katika hadithi na tahariri zao, magazeti haya mawili yalielezea kwa kirefu namna ya dhuluma ambazo zilifanyika mara nyingi. Dhuluma hizi zilikuwa ni *chibalo* au kazi za manamba, hali duni za maisha kwa wafanyakazi wengine wa Kiafrika, kupendelewa kwa walowezi weupe, na kutokuwepo kwa shule. Wahariri wa magazeti haya waliviona vitu hivi kama ushahidi kwamba kulikuwepo na dhuluma za kikoloni.

Ingawa lugha iliyotumika katika tahariri ya magazeti yote mawili ilikuwa yenye uangalifu mkubwa na iliyolenga kwenye mabadiliko muhimu, kwa kuwaomba wakoloni waonyeshe wema na haki, kuendelea kwa kukata tamaa kulisababisha mlipuko wa hasira na hata vitisho kwa mfumo huo wa ukoloni. Msimamo huo mpya ulianza kujitokeza zaidi mara tu serikali mpya ya Salazar ilipoanzisha utawala wa mabavu uliozima matumaini yoyote ya mabadiliko na hivyo kusababisha watu wakate tamaa. Watu waliokumbwa na hali hii walikuwa zaidi Waafrika na machotara waliokuwa na maisha bora zaidi. Hata hivyo, migongano mikubwa iliyokuwepo kati ya machotara na Waafrika wasomi ilitumiwa na watawala wa serikali kuzitenga zaidi jamii hizo mbili. Hivyo, waliwahimiza Waafrika waanzishe chama cha *Instituto Negreophilio* mnamo mwaka 1932. Miaka minne baadaye, utawala wa Salazar ulianzisha sheria za kuchuja habari za magazetini. Hii ilisababisha gazeti la *O Brado Africano* linyamazishwe kabisa.

Katika muda wote huo, idadi ndogo ya wasomi wa Msumbiji waliokuwa Ureno walisaidia kuanzishwa kwa vyama ambavyo vilishirikishwa na Umoja wa Waafrika wote. Vyama vilivyokuwa muhimu ni *Liga Africana na Pattido Nacional Africano.* Chama cha *Liga Africano* kiliendeleza uhusiano mzuri na chama cha *Pan-African Congress* cha W.E.B du Bois, na cha *Partido Nacional Africano* kiliyazingatia sana mawazo ya Garvey. Kwa bahati mbaya vyama vyote hivi viwili havikuwa na wafuasi wengi katika koloni lenyewe, yaani Msumbiji. Hivyo shughuli zake nyingi zilikomea kwenye nadharia.

## *Hitimisho*

Kwa ufupi, nchi za Afrika ya Kusini na Kati zilipinga sana ukoloni na zilikuwa zimechangia kwa kiwango kikubwa katika kuandaa harakati za uhuru katika bara la Afrika, ambazo zilifuatia katika miaka ya 1935. Upinzani dhidi ya ukoloni ambao ulikuwa umeimarika sana katika kipindi hiki ni ule uliojitokeza katika Muungano wa Afrika ya Kusini ambako kukua kwa viwanda, kukifuatiwa na kukua kwa miji, kulisababisha Waafrika waishi katika mfumo wa uchumi wa kibepari hata kabla ya nchi nyingine za Kiafrika. Vyama vya kitaifa na kisiasa vilivyoanzishwa katika Muungano wa Afrika ya Kusini vilikuwa kama mifano ya kuigwa katika nchi nyingi za Afrika Kusini, Kati na Mashariki.

# 28

## *Ethiopia na Liberia, 1914-1935: Mataifa mawili Huru ya Kiafrika katika enzi ya kikoloni.*

Katika sura ya 11 tulichunguza kunusurika kwa Ethiopia na Liberia kutokana na uvamizi wa kibeberu wa Kizungu kati ya 1880 na 1914. Karika kipindi kilichofuata cha kati ya Vita Vikuu viwili, nchi zote mbili hizo zikakumbwa tena na mashambulizi ya Wazungu. Kwa kulinganisha hali ya mambo ilivyojiri, sura hii inajadili uvamizi huo, jinsi Liberia na Ethiopia zilivyoukabili, na maendeleo mengine ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo yalitokea katika nchi hizo mbili katika kipindi hicho cha 1914 - 1935.

### *Liberia na Ethiopia: Maendeleo ya Kijamii - Kiutamaduni, 1915 - 1935*

Katika kipindi hiki, Liberia na Ethiopia zilikabiliwa na matatizo makubwa ya kuunganisha na kunusuru mataifa yao; matatizo ambayo, kwa kiasi fulani, yalisababishwa na kupanuka sana kwa maeneo yao katika karne iliyopita na vile vile kutokana na kuongezeka kwa tafauti za watu na tamaduni zao. Ni mabadiliko gani makuu ya kiutamaduni na kijamii yaliyotokea karika nchi zote mbili hizo katika kipindi hicho?

Miongoni mwa watu wa Liberia, kundi la Waliberia - Wamarekani liliendelea kumiliki uchumi na siasa. Inasemekana kuwa tangu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa idadi yao ilikuwa imepungua kwa sababu ya vifo kuwa vingi zaidi kuliko uzazi, na kusimama kwa uhamiaji wa watu weusi kutoka Marekani ijapokuwa, kama itakavyodhihirika katika sura inayofuata, zilifanyika juhudi za kuuendeleza uhamiaji huo. Hali hii ikasababisha kuongezeka kuoana na kuhusiana hasa kati ya wanaume wa Kiliberia - Kimerekani na wanawake wa Kiafrika wenyeji wa hapo ambao wengi wao walikuwa wamesoma karika shule za Kiliberia; na kutokana na hali hiyo idadi ya Waliberia wenye damu mchanganyiko wa Kiliberia-Kimarekani na kienyeji iliongezeka. Kupungua kwa idadi ya watu wa Kiliberia-Kimarekani pengine kuliendeleza desturi yao ya kuoana wenyewe kwa wenyewe, na kulingana na hayo, mfumo wa familia za kijamaa, ambao ulikuwa umeshamiri miongoni mwao, tangu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, pia uliimarika. Kwa hiyo, karika kipindi chote hicho, koo zilizositawi kama vile za akina Sherman, Barelay, Green, Bwewer, Gibson na Tubman ziliendelea kutoa viongozi wengi wa kisiasa na kichumi.

Ama kuhusu Waliberia wenyeji, upanuaji wa shule na kazi ya wamisionari wa Kikristo kotekote Liberia, kwa kiasi fulani, uliongeza elimu, usasa na usimilishaji wa baadhi ya jiha za utamaduni wa Kiliberia-Kimarekani. Kwa hiyo, Waliberia wenyeji walivyosimiliswa hivyo walihesabika kuwa 'wamestaarabishwa' (au 'wamestaarabika-nusu') na Waliberia-Wamarekani ambao waliwapa haki sawa za kisiasa na kiraia wachache tu miongoni mwa wenyeji hao, kama vile Dkt. Benjamini Payre (Bassa), Henry Too Wesley (Grebo) na Didwo Twe (Kru),

Hata hivyo, hata Waafrika ambao walielimika na ambao walikuwa wakipendelewa - achilia mbali umati wa Waliberia wenyeji wasiokuwa na haki na waliokandamizwa hawakuridhika na "utawala wa Waamerika - Waliberia" ambalo ndilo jina lililopewa serikali ya Liberia. Lakini, kwa kawaida, Waliberia wenyeji walioelimika walijaribu kurekebisha mfumo wa kijamii-kisiasa wa Liberia na kutetea kuongezwa haki za Waliberia wenyeji kuliko kujaribu kuupindua mfumo mzima.

Inafaa ielezwe kuwa usimilishaji wa utamaduni haukuwa wa upande mmoja tu. Kwa muda wa miaka mingi Waliberia-Wamarekani wenyewe walijinasibisha na jiha nyingi za utamaduni wa Kiliberia ambazo hapo awali walizilaani kuwa ni za kishirikiana au kishenzi kama vile imani katika nguvu za uchawi, usihiri, 'mitishamba' na ufundaji katika '*pori*'. Lakini katika 1935, kiasi cha Afrikanaizesheni hiyo kilikuwa kidogo mno kuweza kuondoa tafauti kuu za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kati ya kikundi cha Waamerika-Waliberia na Waliberia wenyeji.

Kama ilivyojiri huko Liberia, tokeo kubwa la upanuzi wa Ethiopia chini ya ufalme wa Menelik lilikuwa ushadidiwaji wa tofauti za watu wa Ethiopia. Miongoni mwa watu mashuhuri walioingizwa katika mipaka ya Ethiopia kufika 1914 kutokana na upanuzi huo walikuwa Waoromo ambao walikuwa wengi kama vile Waamhara-Watigre, Wagurage, Wasisama na Washanguli wa Kibeni.

Kikundi cha Waamhara-Watigre kama kilivyokuwa kikundi cha -Waliberia-Wamarekani huko Liberia kiliendelea kumiliki uchumi, siasa na jeshi katika sehemu iliyobaki ya Ethiopia katika kipindi chote. Ingawa kikundi hiki kilikuwa na fursa nyingi kuliko wengine, madaraka halisi ya kiuchumi na kisiasa na hadhi kubwa zilikuwa mikononi mwa baadhi ya familia za Kiethiopia za mamwinyi. Familia hizo ndizo zilishika vyeo vingi vya juu katika serikali na lakabu kama *ras, regus, fitawrari, dejeazmaches* na *betwoded.* Aghalabu kwa kuwatumia mamwinyi hao (na majeshi waliyoongoza) ndipo Menelik alipopanua Ethiopia kwa njia ya utamalaki. Baadaye katika majimbo aliyoyatamalaki akaweka 'makazi ya kijeshi' kama vile walivyofanya wakoloni kutoka Ulaya katika sehemu nyinginezo za Afrika. Hivyo, mamwinyi hao na vizazi vyao, pamoja na vizazi vya walowezi wa kijeshi, maafisa wa serikali na hata wahubiri wa Kikristo mara nyingi walikuwa na 'mkabala' karibi wa kikoloni au mwalekeo wa kikabaila kwa Waethiopia wengine.

Miongoni mwa Watigre wasio Waamhara (yaani Waoromo, Wasidama, Wagurne n.k.) maendeleo makuu ya kijamii na kiutamaduni katika karne ya ishirini yalikuwa ya kuendeleza 'Uamharishaji', wa watu, kama vile kutumia lugha, mavazi na kalenda ya



28.1 *Dibwo Twe, Mjumbe wa Kikru katika Baraza la Seneti, Liberia, mmojawapo wa wenyeji wachache wa kiliberia kupata cheo kikubwa cha serikali.*

Waamhara na kubadilisha imani za kidini ijapokuwa kulikuwa na pingamizi kutokana na taathira za dini za Kiislamu, za kijadi na nyinginezo. Lakini, kama ilivyotokea hako Liberia, usilimishaji wa kiutamaduni ulikuwa wa pande zote mbili. Baadhi ya walowezi wa Kiamhara-Tigre katika makazi ya kijeshi ambayo yalijitenga hatimaye walisimiliswa na wenyeji wa pale.

Vilevile, jamii ya Kiethiopia ilijigawa katika tabaka na makundi mbalimbali. Makundi hayo yalikuwa ya watumwa, wakulima, wasomi na mabepari ambao walianza kujitokeza. Makundi hayo yalimsaidia Makamu wa Mfalme, Tafari Makomen (baadaye akawa Mfalme Haile Sellassie) pamoja na yale yaliyopendelea kufanya marekebisho ili kuwa na serikali kuu madhubuti na kikundi kisichopenda mabadiliko chenye mamwinyi wakubwa na mapadre wa vyeo vya juu wa Kanisa la Ethiopia. Kikundi hiki, ambacho kilimsaidia Malkia Zauditu na kupendelea uhuru wa kimajimbo, kilikuwa ndicho nguzo ya mfumo wa Kijamii na Kiutamaduni wa Ethiopia.

Kwa hiyo, kote kuwili katika Liberia na Ethiopia, tofauti za kimbari na kiutamaduni na tofauti za kijamii zilihatarisha uimara wa utulivu wa jamii, au kama itakavyodhihirika hapo chini, zilisababisha mapambano katika kipindi hicho chetu.

## *Matukio ya Kisiasa Liberia*

Kote kuwili katika Liberia na Ethiopia katika kipindi chetu, mizozo na misongo ilitukia katika mfumo na utendakazi wa kisiasa katika nyanja kuu tatu: katika kiini, kwenye ukingo, na kati ya kiini na ukingo.

Ama kuhusu kiini cha Liberia, katika kipindi chote cha miaka ya 1910, Chama cha *True Whig Party* kilishika hatamu thabiti za madaraka pasi kutatizwa sana na chama rasmi cha upinzani. Hali hii ilibadilika kidogo katika miaka ya 1920 wakati Chama cha *People's party,* kilichoundwa katika mwaka 1922 chini ya uongozi wa rais wa zamani, Daniel B. Haward, kilipopinga vikali chama kilichotawala cha *True Whig Party.* Lakini kutokana na udhoofu wa mtawanyiko wa upinzani, ulaji rushwa mkubwa na vitendo viovu vya uchaguzi, ukosefu wa tofauti za kiitikadi au sera na ulinzi mkubwa wa serikali, hapakuwa na suala la *True Whig Party* kupinduliwa. Ama kwa hakika, katika karne ya ishirini polepole Liberia ilifikia hatua ya kuwa taifa lenye chama kimoja - mojawapo ya nchi ya kwanza katika Afrika kufanya hivyo. Wala msingi wa kisiasa wa Liberia haukupanuka ili kuwaingiza Waliberia wenyeji. Mbali na Too Wesley na wachache wengine waliokwishatajwa, hapukutokea maendeleo ya kisiasa kama hayo. Kwa hiyo, kimsingi mfumo wa siasa wa Liberia ulibaki wenye kutopenda mabadiliko na ambao ulihudumia maslahi ya mamwinyi wa Waliberia-Wamarekani na kuendeleza utawala wao wa kisiasa.

Ethiopia

Hali ya kisiasa katika Ethiopia wakati wa kipindi chetu hiki ilitofautiana na ile ya Liberia katika jiha fulani muhimu, hususa katika aina na namna ya vyombo vya kisiasa, na utendakazi na kiasi cha mtawanyiko wa madaraka na fursa za kisiasa. Lakini, kuhusiana na masuala ya kimsingi zaidi ya muundo wa mfumo wa kisiasa na kiasi cha mabadiliko ya kisiasa, muundo wa kitabaka na maslahi, Ethiopia ilifanana sana na Liberia.

Miaka ya mwisho ya utawala wa Melik ilikuwa kipindi kigumu kwa Ethiopia. Kutokana na mfalme kuugua kwa muda mrefu hadi kufikia kufa kwake katika Desemba 1913, Mfalme alimteua mjukuu wake Hij Isayu - kijana wa kiume mwenye umri wa miaka kumi na miwili - kama mrithi wake katikati ya mwaka 1908. Baadaye mwaka huohuo, alipopooza viungo na kupoteza uwezo wa kusema, alimteua jenerali wake wazamani Ras Tasamma kuwa Kaimu wake. Mnamo mwaka 1911 Tasamma alipofariki. Baraza la Taifa la Ethiopia lilitangaza kuwa Iyasu alikwishafikia umri wa kuweza kutawala mwenyewe kwa kuongozwa na Baraza hilo.

Lij Lyasu, mwanae Mikael, mtawala wa Wallo, ambaye alimrithi Menelik alikuwa mtu mweye papara nyingi. Mbali na kuwa na ujuzi mdogo wa kiutawala kuliko alivyokuwa babu yake, hukuwa na msingi wa kujiegemeza madaraka yake nje ya Wallo. Baadhi ya jiha za sera yake ya mambo ya ndani kama vile urafiki wake na Waislamu nchini na sera zake za mambo ya nje ambazo zilikitwa Hungary na Uturuki wakati Vita Vikuu vya Kwanza vilipoanza katika 1914, ziliwakengeusha mamwinyi viongozi wa kanisa na pengine ujumbe wa nchi za mataifa marafiki katika Addis Ababa. Kwa hiyo, wote hao walikula njama ya kumpindua katika Septemba 1916 na kumfunga jela tangu 1921 hadi kufa kwake mwaka 1935. Hivyo, bintiye Menelik, Zawidtu, alitangazwa kuwa Malkia, na Tafari, Mtoto wa Kiume wa binamu wa Mfalme aliyefariki, Ras Makonnen, akatangazwa kuwa Kaimu na mrithi wa Ufalme. Kutangazwa kwa Malkia Zawditu mnamo tarehe 11 Februari 1917 kulifuatiwa na serikali yenye mamlaka mawili ambamo madaraka yaligawanyika kati ya Malkia na Kaimu, kila mmoja akiwa na kasri, kikundi chake maalumu cha wafuasi na siasa zao ambazo aghalabu zilikinzana.

Ujaji wa Tafari kama Kaimu ulikuwa tukio muhimu kwani alikuwa kiongozi shupavu aliyependelea kuendeleza sera za Menelik za kuleta usasa na kudumisha uhuru wa Ethiopia. Mtindo wake wa utawala wa binafsi kwa kiasi fulani ulimwezesha polepole kueneza madaraka yake wakati bado angali Kaimu katika maeneo mahimu kadha ya serikali. Katika mwaka 1928, alitawazwa kuwa Negus na alishika madaraka yote ya kiserikali. Mnamo Machi 1930 Malkia Zawditu alipofariki Tafari akachukua enzi na kutawazwa kuwa Mfalme Haile Selassie I mnamo tarehe 2 Novemba 1930. Kama vile Liberia, mabadiliko kadhaa ya kisiasa yalitokea katika utawala wa Haile Selassie. Miongoni mwa mabadiliko hayo yalikuwa udhibiti mkubwa zaidi wa Serikali Kuu, uteuzi wa watu katika vyeo vya umma kutokana zaidi na uwezo kuliko nasaba

zao, ufyekaji wa mamwinyi wakongwe wa Kiethiopia, na uandikaji rasmi wa Katiba. Lakini mabadiliko hayo hayakuwa ya kimsingi wala ya kimuundo. Bali, ijapokuwa kulikuwa na udhibiti zaidi wa Serikali Kuu, mfarakano wa kijamii na tofauti za kiutamaduni ziliendelea kuwatenganisha watu wa Ethiopia na zikawa vizingiti vikubwa katika juhudi za kuunganisha kuwa taifa moja.

Pili, Katiba iliyothibitishwa katika 1931 ambayo ilitoa nafasi ya kuwa na bunge lenye mabaraza mawili pamoja na "Seneti" yenye wajumbe walioteuliwa na Baraza la wawakilishi, haikuwa ya kimapinduzi na haikuleta athari kubwa katika utamaduni wa kisiasa wa Ethiopia. Katiba hiyo ilibakiza madaraka makuu mikononi mwa Mfalme wa kudumisha nafasi za upendeleo kwa mamwinyi.

Bunge ambalo halikuwa na uwezo wa kuanzisha mashauri yoyote katika kutunga sheria au kuunda sera na ambalo lilikutana na kuvunjwa kwa hiari ya Mfalme, lilibaki kama chombo cha kupitishia mambo yaliyohudhurishwa na Mfalme.

Katika mambo hayo yote, Ethiopia ilitofautiana sana na Liberia kwani, ingawa Katiba ya Liberia ilimpa Rais wa Liberia madaraka makubwa ya kikatiba lakini madaraka hayo yalikuwa na mpaka. Bunge la Liberia lilikuwa na madaraka ya kisiasa ilihali Bunge la Ethiopia halikuwa nayo. Pengine hitilafu iliyojidhihirisha hasa ilikuwa ukosefu wa vyama vya kisiasa huko Ethiopia kwa sababu ya nafasi ya kihistoria ya Mfalme katika mashauri ya Kiethiopia, na ukosefu wa wasomi wenye mwelekeo wa kimagharibi ambao wangeweza kurekebisha mtindo wa Ethiopia wa kutopendelea mabadiliko.

Kwa hiyo, katika kipindi chetu hiki, Liberia na Ethiopia zilifanana zaidi kuliko kuhitilafiana katika sifa za msingi za utamaduni wa kisiasa kama vile kutopendelea mabadiliko, kanuni za jamii zilizodumisha tofauti na ukosefu wa umoja wa kitaifa, maendeleo ya kiuchumi au wa azma thabiti ya kuleta mabadiliko ya kimapinduzi katika jamii.

## *Badiliko la Kiuchumi na Kijamii*

### *Liberia*

Katika mambo mengi, miaka ya 1915 - 1935 ilikuwa miaka migumu kiuchumi kwa Waliberia wengi na kwa Serikali ya Liberia. Tangu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa biashara na kilimo cha Liberia, ambavyo vilikuwa sekta muhimu za uchumi, vilipoanza kudhoofika, vikasababisha pia kupungua sana kwa mapato ya serikali ambayo hasa yalitokana na ushuru wa forodha. Hali hii iliwakosesha Waliberia wengi njia ya kupata riziki yao.

Kwa kiasi fulani kulipa madeni yaliyokuwa yanaongezeka, likiwamo deni la mkopo kutoka Uingereza la mwaka 1870, na kwa kiasi fulani kuleta maendeleo ya ndani, serikali ya Liberia ilipata mkopo wa $ 500, 000 katika 1906 kwa asilimia 6 ya



28.2 *Haile Selassie, I, Mfalme wa Ethiopia, 1930 – 1974*

riba kutoka kwa wakopeshaji wa Kiingereza na mkopo mwingine wa $ 1, 700,000 katika mwaka 1912 kutoka mabenki fulani ya Ulaya kwa asilimia 5 ya riba.

Kwa madhumuni ya kulipia riba na kuwa na mfuko wa kulipia madeni ya mkopo huu, ukusanyaji na utunzaji wa sehemu ya mapato ya Liberia yaliyojulikana kama 'mapato yaliyotengwa' yaliyotokana na ushuru wa forodha, vilikabiliwa kwa 'Upokezi wa Kimatifa' ambamo mlikuwa Mmarekani moja kama 'Mpokezi Mkuu wa Ushuru', ambaye alisaidiwa na Wapokezi wa Kifaransa, wa Kidachi na wa Kiingereza.

Kwa hakika, faida kutokana na 'mapato yaliyotengwa' zilipungua baada ya kuzuka kwa Vita Vikuu ya Kwanza hasa kwa sababu ya kufifia kwa biashara, baada ya kuondoka kwa Wajerumani ambao walidhibiti takriban robo tatu ya biashara ya Liberia na vibaya kwa bei za mazao ya biashara ya Liberia kama vile kahawa, kakao na mafuta ya mchikichi katika soko la dunia. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 1916, riba ya kila mwaka na mfuko wa kulipia madeni ya mkopo havikuweza kulipwa kikawaida au kikamilifu. Kwa hiyo, karisaji ya malipo ililimbikana na kufikia $ 1,78,657 mnamo 30 Septemba 1918. Papohapo, mapato yaliyobaki yaliyoitwa " mapato ya ndani', hasa kutokana na ulaji rushwa wa maofisa wa Liberia, hayakutosheleza kulipia gharama za kutoa huduma za serikali ya Liberia kama vile kulipa mishahara ya waajiri wa Serikali ambayo tayari ilikwishakatwa.

Kwa hiyo, ilipokabiliwa na umufilisi, Serikali ya Liberia kwanza ikaendelea kukopa sana toka Benki ya *British West Africa* katika kipindi cha 1917 - 1918. Juhudi za kupata mkopo kutoka Serikali ya Marekani kati ya 1918 na 1921 ziliposhindikana, Serikali ya Liberia ililazimika na kuchukua hatua kadhaa za kukuza biashara na kuongeza mapato kutokana nayo. Miongoni mwa hatua hizo ilikuwa kuongeza ushuru, kuruhusu wafanya biashara wa kigeni kuingia katika mrima wa Liberia (ambao ulifungwa kwa wageni wakati Vita Vikuu vya Kwanza vilipoanza) na wakati huohuo, kuongeza ushuru wa bandari. Kama itakavyodhihirika katika sura ifuatayo, Serikali ya Liberia mwanzo ilikaribisha mipango ya *Garvery Universal Negro Improvement Association* ya kuleta mtaji wa na wahamiaji weusi katika Liberia kuendeleza rasilimali zake.

Kwa bahati nzuri kwa Liberia, ingawa mipango ya Garvey haikufana tangu mwishoni mwa 1923, kwa kiasi fulani, kwa sababu ya mabadiliko yaliyotajwa hapo awali kuuzwa kwa mali ya Wajeurmani waliyonyang'anywa wakati wa Vita Vikuu, na pia, kwa kiasi fulani, kwa sababu ya Wajerumani kuingia tena katika biashara za kigeni na Liberia katika mwaka 1922, uchumi wa Liberira ulianza kusitawi na urari wa biashara akaanza kuwa wenye faida,. Lakini, kwa vile bei za mazao makuu ya Liberia kama vile mafuta ya mchikichi, muhogo na kahawa zilianguka katika soko la dunia, ukubwa wa biashara ya Liberia pia ulipungua. Wala kuanzishwa kwa mashamba makubwa mawili na Firestone katika 1926 pamoja na mkopo wa dola milioni 5 kutoka Shirika la Fedha la Marekani (Financial Corpartion) haakuleta mabadiliko muhimu katika uchumi wa Liberia hadi baada ya 1935 ambapo kiasi cha kutosha cha mpira kilipoanza kusafirishwa nje. Kwa hiyo, katika miaka yote ya 1930,

urari wa biashara ulikuwa dhidi ya Liberia.

Katika hali hii mbaya ya kiuchumi katika kipindi chetu chote (1915 - 1935), Serikali ya Liberia daima ilibakiwa na fedha kidogo tu baada ya kuendelea kulipa madeni. Hata hivyo, juhudi zilifanyika ili kuleta maendeleo ya kijamaa na kiuchumi katika Liberia. Mpango wake wa ujenzi wa mabarabara ulioanzishwa na Rais Arthur Barclay, ulishamirishwa lakini zaidi kwa kuwafanyisha kazi za ushokoa wenyeji wa Kiliberia. Katika miaka ya 1920, Serikali ya Liberia kwa mara ya kwanza katika historia ya Liberia ilianzisha shule kadhaa za msingi katika sehemu zisizofikika kwa urahisi katika mrima wa Liberia. Mwishoni mwa 1930 pia, serikali ilianzisha Chuo cha Booker T. Washington cha Viwanda na Kilimo cha kuwafunza wanaamali wa kiufundi na Kilimo wa daraja lachini na kati. Mnamo mwaka 1934, serikali ilianzisha Chuo cha Ualimu huko Monrovia ambako kulihitajika sana kuongezea idadi ya Vyuo vilivyokuwapo kama vile Chuo cha Liberia na Chuo cha Afrika Magharibi.

Katika mwaka 1924, Serikali ilijenga hospitali huko Monrovia. Katika mwaka 1927, ilijenga kinu cha taa huko Monrovia. Vyama vya kimisionari vya Kimarekani, kama ilivyokuwa ada yao tangu nchi ya Liberia ilipoanzishwa walichangia kwa kujega shule, hospitali na makanisa. Lakini, upanuzi wa kutosha wa elimu ulikwazwa kwa sababu ya uhaba wa fedha, pia kwa sababu ya tabia ya tahadhari ya serikali ya Liberia ya kutoruhusu wamisionari, wafanyabiashara na wageni wengine kuingia katika mrima wa Liberia.

Ethiopia

Ethiopia, kama Liberia, haikupata maendeleo muhimu ya kiuchumi katika kipindi chetu. Mabadiliko ya kiuchmi na kijamii yaliyotokea yalikuwa madogo mno ya kuweza kuleta mabadiliko dhahiri katika mfumo wa uchumi wa Ethiopia ambao kimsingi ulikuwa wa kimwinyi na muundo usiopendelea mabadiliko ya kijamii-uchumi.

Mwanzilishi mkuu wa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii alikuwa Kaimu wa Mfalme, Tafari Makonnen. Mojawapo ya mabadiliko aliyoleta ilikuwa ni mfumo wa kuongeza mawaziri wa Meneliki kwa kuanzisha Wizara ya Biashara na Idara ya Ujenzi katika 1922. Katika 1923, alianzisha kiwanda cha uchapaji cha *Berhanena Salam,* au `Mwanga na Amani', ambacho kilichapa gazeti la jina hilo, pamoja na vitabu vya kidini na kielimu

Tafari, ambaye alikuwa ameshughulika sana na uhusiano wa kimataifa, aliweza kutambua haraka faida zitokanazo na umoja wa Mataifa na mfumo wake wa usalama wa pamoja. Kwa hiyo, aliomba Ethiopia ijiunge na Umoja huo wakati ulipoanzishwa katika 1919 na baada ya upinzani kidogo wa baadhi ya nchi za Ulaya kama vile Uingereza, Ethiopia iliingizwa katika Umoja huo mnamo tarehe 13 Septemba 1923, wakati Kaimu alipotia saini azimio la kufuata makubaliano makuu ya kimataifa ya kuzuia utumwa.

Baada ya ziara yake ya Ulaya ya 1924 na kutawazwa kwake katika 1930,

Haile Selassie aliendelea na mpango wake wa usasa ingawa kazi hii iliathirika vibaya na mpomoko wa dunia wa kiuchumi ambao ulisababisha kupungua kwa bizanje na yamkini kuwa vitegauchumi vya nje. Hata hivyo katika 1930 ilitungwa sheria ya upimaji na nandikishaji wa ardhi, na katika mwaka huohuo ilianzishwa wizara ya Elimu. Mwaka wa 1931 ulishuhudia maendeleo makubwa matatu, yaani, utangazaji wa katiba iliyoandikwa ambayo imekwishazungumziwa, kubadilisha Benki ya Zamani ya Abyssinia ambayo ilikuwa kampuni ya kibinafsi iliyomilikiwa na mgeni na kuifanya iwe benki ya taifa, Benki ya Ethiopia, na tatu upitishaji wa sheria ya ziada ya ufutaji polepole wa utumwa. Juhudi za kuimarisha mawasiliano pia zilifanyika. Wizara ya Ujenzi ilianzishwa katika 1932, na ujenzi wa barabara nkaanza. Kituo cha muda cha redio kilianzishwa katika 1933, na baadaye kikajengwa kituo chenye nguvu zaidi katika 1935. Shule mpya kadhaa zilianzishwa, hususa mikoani, na serikali na baadhi ya wamisionari. Ilipofika 1935, Addis Ababa ilikuwa na shule kumi na nne za kiserikali, zenye walimu 30 wa kigeni na wanafunzi elfu nne. Chuo cha jeshi kilianzishwa katika 1934 hnko Holeta, karibu na Addis Ababa. Idadi ya wanafunzi waliokuwa masomoni ng'ambo iliongezeka kufikia mia kadha. Baadhi ya wamisionari, hususa *United Presbyterian Church* ya Amerika Kaskazini, Misioni ya Wasabato ("Seventh Day Adventist"), Misioni ya Wakatoliki wa Kitaliani, ziliendesha hospitali hnko Addis Ababa, wakati chama cha *Sudan Interio Mission* kiliendesha kituo cha wakoma hnko Akaki. Maendeleo mengine yalikuwa ni pamoja na kuanzisha tume ndogo ya utumishi wa serikali, iliyoundwa kutokana na wanafunzi waliorudi kutoka ng'ambo na kwa kuendelea kuiondoa hongo ambayo ilikuwa ikitozwa na badala yake kuanzisha kodi za kulipa kwa fedha taslimu. Lakini, juhudi za kuleta usasa wakati huo zilikuwa zimegubikwa katika tishio la uvamizi wa kifashisti wa Kitaliani.

Kwa hiyo, kipindi cha 1915 - 1935 kilishuhudia mweneo mkubwa na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika Liberia na Ethiopia kuliko hapo awali. Lakini mabadiliko hayo hayakuwa makubwa na hivyo nchi zote mbili hizo zikadoda nyuma kiuchumi na hazikuendelea kijamii. Hatimaye, vitegauchumi kutoka kwa wananchi wageni na kampuni katika miradi ya biashara na kilimo vilikuwa vikubwa zaidi katika Liberia kuliko Ethiopia, na ingawa hali hii ilisaidia kuleta usasa, lakini vilevile ilisababisha wageni hao kudhibiti kiasi kikubwa zaidi cha uchumi wa Liberia kuliko ilivyokuwa hnko Ethiopia.

## *Uingiliaji kati wa Wageni katika Liberia naEthiopia 1915 - 1935*

### *Liberia*

Uingiliaji kati wa wageni katika Liberia na Ethiopia ambao umeshajadiliwa katika Sura ya Kumi na Moja uliendelea kuwapo katika kipindi cha 1915 - 1935. Kama vile vilivyo katika enzi ya Mnyang'anyiro na mgawanyo wa Afrika, sababu za kuingilia kati zilitokana na matukio na hali iliyokuwa nchini Liberia na Ethiopia na pia katika

nchi za Ulaya na Marekani.

Mosi, ufukara na madeni yasiyoisha ya serikali ya Liberia kwa kiasi fulani ulisababisha kuongezeka kwa udhibiti wa kigeni wa uendeshaji wa mashauri ya fedha ya Liberia na Upokeaji wa Kimataifa, Benki ya *Bristish West Africa,* na kampuni za Firestone zilizosaidiwa na serikali ya Marekani. Uchumi wa Liberia vilevile ulitawaliwa na kampuni za Ulaya, Marekani na Lebanon. Pili, hali mbaya ya kiuchumi, kijamii na kiutawala ya Liberia ikawa masiala makuu katika ushindani mkali wa kisiasa kati ya vyama vya *True Whig* na *People' Party* na ulivutia nadharia ya kimataifa hususa baada ya ziara ya kutembelea Ulaya na Marekani ya mkuu wa upinzani Faulkner ya kupata msaada wa kimataifa na kuudhalilisha utawala wa *True Whig* wa Rais King. Habari katika magazeti ya Marekani na Uingereza na ripoti nyingnezo kutoka kwa ubalozi na wazuru nchi wa kigeni zilishutumu serikali ya Liberia na baadhi ya Waliberia-Wamarekani wakubwa kuwa walikuwa wakiendesha utumwa, kushika shokoa, na kuwasafirisha na kuwauza wafanyakazi wahamaji kwenda kisiwa cha kikoloni cha Wahispania cha Fernando Po.

Kutokana na shutuma hizo, Umoja wa Mataifa ukapeleka tume ya kutafuta uhakika Liberia chini ya uenyekiti wa daktari wa meno wa Kiingereza, Dkt, Cuthebert Christy. Tume hiyo katika ripoti iliyotolewa tarehe 8 Septemba 1930, ilisema kuwa ingawa hapakuwa na muundo rasmi wa biashara ya watumwa, lakini wafanyakazi walilazimishwa kupoteza nguvu zao katika kufanya kazi za ujenzi za serikali, shughuli za binafsi na kusafirishwa nje kwa ushirikiano na Jeshi la Mpakani la Liberia na viongozi wa Serikali wa Vyeo vya juu. Vile vile, tume hiyo haikuridhika na mahusiano kati ya Waliberia-Wamarekani na Waliberia-Wazawa na utawala wa jumla wa serikali ya Liberia. Kwa hiyo, tume ilitoa pendekezo la kushukiwa la kuwa Liberia ikabidhiwe kwa 'utawala wenye uwezo na huruma wa watu weupe'.

Ingawa Ripoti hiyo ilisababisha kujiuzulu kwa Rais King na Makamu wa Raisi wake Allen Yancy, na ingawa utawala mpya wa Ediwn J. Barclay iliamua kutekeleza mapendekezo mengi ya Umoja wa Mataifa na ulipitisha Sheria kadhaa kati ya Desemba 1930 na Mei 1931 ambazo zilibatilisha usafirishaji nje wa wafanyakazi, uwekaji rehani na utumwa wa nchini na kazi za ushokoa, lakini Uingereza na Marekani bado zilishikilia kuwa 'Serikali ya Liberia iwekwe chini ya uangalizi wa Tume ya Kitaifa ya Utawala' kwa muda. Barclay na Baraza lake la Mawaziri pale pale, na kwa usahihi kabisa, wakalikataa pendekezo hilo kwa sababu waliona kuwa kufanya hivyo 'kungemanisha kuupoteza uhuru na madaraka yao'. Hata hivyo, waliendelea kuonyesha hamu ya kutafuta na kupokea msaada kutoka Umoja wa mataifa hususa wa wataalamu katika nyanja za uchumi na utawala wa wananchi.

Kwa hiyo, Umoja wa Mataifa ukatuma Tume nyingine ya kutafuta uhakika. Tume hii ilikuwa na wawakilishi wa mataifa manane, yaani Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Hispania, Venezuela, Poland na Liberia na ilikabidhiwa dhima ya kukomesha utumwa na kazi za Ushokoa, na kutoa msaada wa kiufundi kwa Liberia. Kamati ndogo ya watu watatu iliyoongozwa na Mwanasheria wa Kifaransa, Henry

Brunot, pia iliteuliwa kushauri tume kuhusu mabadiliko ya kifedha na utawala yaliyohitajika huko Liberia ili kufanikisha msaada wa Umoja huo.

Kama ilivyofanya tume iliyotangulia, tume hii ya pili pia ilitengeneza mipango mikubwa ya kuimarisha utawala wa ndani, fedha na afya ya jamii ya Liberia. Katika mwezi wa Januari 1932 Tume ya Brunot pia ilihudhurisha Ripoti yake kwa Umoja wa Mataifa. Miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa yalikuwa kwamba ujamaa wa kijadi wa Kiafrika uchukue nafasi ya kazi za ushokoa katika kazi za ujenzi za Serikali, Waliberia-wazawa wapewe umiliki kamili wa ardhi yao, na elimu ya Waliberia-wazawa pamoja na njia za mawasiliano na mrima wa Liberia ziimarishwe.

Tume pia ilipendekeza kuwa ili kuleta uimarishaji wa kutosha wa fedha za Liberia, ilibidi (Kampuni ya )Firestone ilegeze masharti yake ya mikopo yaliyowekwa katika makubaliano ya 1926. Ripoti ya Brunot ilipotolewa, Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Liberia ilitunga "Misingi Mikuu ya Mpango wa Msaada" kwa Liberia, na kutokana na misingi hiyo na Ripoti ya Lighthart kuhusu mazungumzo ya kifedha na Firestone, Kamati pia ilitunga "Itifaki" iliyojumuisha mpango uliopendekezwa wa msaada na mabadiliko. Itifaki hizo ziliingiza uajiri wa 'wataalamu' wa kigeni kama naibu kamishina na makamishina wa majimbo na uteuzi wa "Mshauri Mkuu" kwa serikali ya Liberia na Baraza la Umoja kwa kukubaliana na Rais wa Liberia, ambaye alikuwa kiungo kati ya Serikali ya Liberia na umoja wa Mataifa. Serikali ya Liberia iliukataa kabisa mpango huo mzima na Tume ya Umoja wa Mataifa ikaufuta.

Baada ya hapo Serikali ya Liberia ikatengeneza "Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu" wa mabadiliko ya ndani katika Liberia, pamoja na marekebisho katika Makubaliano ya mkopo ya 1926. Mpango huu uliungwa mkono na Serikali ya Marekani iliyokuwa inaongozwa na Franklin D. Roosevelt na ulikuwa ndio msingi wa mazungumzo kati ya Firestone, Marekani na Serikali ya Liberia katika 1935 wakati ambapo marekebisho yaliyohitajika katika masharti ya mkopo huo yalifanyika. Riba ya mkopo ilipunguzwa toka asilimi 7 hadi asilimia 5.

Halikuwa jambo la kushangaza kuona kuwa baada ya hapo mahusiano kati ya Firestone na Liberia yalitengemaa. Kadhalika, mahusiano kati ya Liberia na Marekani pia yalitengamaa na matokeo yake yakawa kutambuliwa kwa Serikali ya Barclay tarehe 11 Juni 1935. Uingereza pia ilifuata hatua ya kutambua Serikali hiyo tarehe 16 Desemba, 1936 na matukio hayo yakamaliza rasmi mgogoro wa uhuru wa Liberia.

## Ethiopia

Uingiliaji kati wa wageni katika mashauri ya ndani ya Ethiopia katika kipindi kinachozungumzwa ulikuwa wenye matokeo makubwa zaidi. Makubaliano ya Pandetatu ya 1906 ambayo yaliigawanya Ethiopia katika sehemu za kutawaliwa na Waingereza, Wafaransa, na Wataliaui yalikuwa ishara ya kuwa uingiliaji katiwa kibeberu wa kizungu ungetokea tena huko Ethiopia. Kifo cha Menelik katika 1913, kutawala kwa Lij Lyasu na matakio ya Vita Vikuu vya kwanza yalichochea hasa Italia

na kufufua tena mipango yake ya kibeberu dhidi ya Ethiopia tangu 1913. Hivyo, kati ya 1913 na 1919 Wizara ya Ukoloni ya Italia ilidhamiri kwa dhati utekelezaji wa mpango wa ukoloni wa Italia katika Afrika kwa madhumuni ya kuipa Italia udhibiti wa Bahari ya Sham na kuifanya Ethiopia 'iwe sehemu ya kutawaliwa na Italia peke yake'. Lakini mpango huo ulipingwa na Uingereza na Ufaransa na hivyo uliachwa katika mwaka 1919 baada ya makubaliano ya Versailles.

Ijapokuwa Waitalia walikuwa na hamu ya kuifanya Ethiopia iwe koloni na walisumbuliwa na kumbukumbu mbaya ya ushindi wa Adawa ambayo Waitalia wengi walitaka kulipizaia kisasi, lakini uhusiano kati ya Ethiopia na Italia ulikuwa mzuri sana katika kipindi cha Ukaimu wa Tafari Makomen.

Hata hivyo, katika 1930 utawala wa Mussolini ulibadilisha sera yake ya upenyezi kwa amani na kuifanya iwe ya uingiliaji kati kwa mbavu na ukaanza kufanya mipango ya siri ya kuvamia Ethiopia. Kulihitajika tu kisingizio cha kuvamia na kisingizio hicho kilipatikana wakati mapigano yalipotokea kwenye kisima cha Wal Wal mnamo Novemba 1934 kati ya jeshi la kutamalaki la Waitalia na jeshi la Ethiopia lililohusika na uainishaji wa mpaka kati ya Ethiopia na British Somaliland. Pamoja na kukataa usuluhishi baina yao, Italia ilitaka Ethiopia iiombe radhi na vile vile itambue utawala wake wa Wal Wal na itoe fidia ya Dola 200, 000 za Maria Theresa. Ingawa Uingereza na Ufaransa katika wahaka wao wa kutaka kuepusha mapigano ziliisihi Ethiopia ikubali, lakini Haile Sellassie alikataa na akafikisha jambo hilo kwenye Umoja wa Mataifa mnamo tarehe 14 Desemba. Wakati umoja wa mataifa ulipokuwa bado ukizingatia jambo hilo Italia bila ya kutangaza vita ilivamia Ethiopia tarehe 3 Oktoba 1935 chini ya uongozi wa De Bono. Ingawa uvamizi huo ulikuwa umeandaliwa kwa muda mrefu, lakini ulipotokea ulileta hofu kubwa katika dunia,. Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ulifanyika tarehe 9 Oktoba na akapitishwa uamuzi kwa kura hamsini kwa 1, ya Itali, na kura tatu ambazo hazikupigia upande wowote (Albania, Austria na Hungary), kuwa Italia ndiyo ilikuwa mvamizi na ndiyo iliyovunja mapatano ya Umoja. Ijapokuwa kitendo hicho cha uvamizi kililaaniwa takriban kwa kauli moja, lakini Umoja wa Mataifa ukitawaliwa na nchi za kikoloni za Ufaransa na Uingereza ulisita kumkasirisha Mussolini na hivyo ukawekea Italia vikwazo vidogo vya kuchumi vikiwemo uzuiaji wa kuipelekea silaha na mikopo na karadha. Kama ilivyokuwa ikitegemewa vikwazo hivyo havikuwa na athari kabisa. Kwa hiyo, jeshi la Italia lilisonga mbele na kutamalaki Adowa. Lakini Waethiopia walipambana vikali mpaka wavamizi wakalazimika kusimamisha mashambulio yao. Hivyo, De Bono alifukuzwa kazi na badala yake mnamo tarehe 16 Novemba akateuliwa askari mtaalamu, General Badaglio, ambaye alipokabiliwa na mashambulio makali ya Waethiopia pia hakuweza kusonga mbele kwa muda wa wiki nyingi. Hata hivyo, mapigano makali yalitokea kabla majeshi ya Waitalia hayajaitamalaki Addis Ababa tarehe 6 Mei 1936.

Uvamizi wa Wataliani uliwagutusha wote barani Afrika na kwingineko. Mnamo Agosti 1935, kikundi cha Waafrika na wazawa wa Waafrika waliokuwa wanaishi London walianzisha Jumuiya ya *International African Friends of Abyssinia.*

(Jumuiya ya Kimataifa ya Marafiki wa Abysinia). Miongoni mwa Wanakamati wake walikuwa C.L.R. James wa West Indies, Dkt. P.Mc. D Millard wa British Guyana, mkewe Marcus Garvey Amy Ashwood Garvey, Mohamed Said wa Somali na J.B Dangush wa Ghana. Madhumuni ya Jumuiya hiyo, kama ilivyoelezwa na katibu wake, Jomo Kenyatta, yalikuwa 'kusaidia kwa njia zote zinazowezekana kuhifadhi ardhi na uhuru wa kisiasa wa nchi ya Abyssinia.'

Mapigano yaliyotokea baada ya hapo yalifanya Ethiopia itajwe katika kichwa cha habari cha kila gazeti maana yaliathiri sana fikra za Waafrika. Kwame Nkrumah, ambaye wakati huo alikuwa mwanafunzi akipita Uingereza, alikumbuka kuwa alipoona mabango yakisema 'Mussolini avamia Ethiopia' alijawa na jaziba na alisimulia kuwa:

> Wakati huo ilionekana kana kwamba jiji zima la London lilikuwa limetangaza vita juu yangu binafsi. Katika dakika chache zilizofuata nilipigwa butaa na sikuweza kufanya kitu chochote ispokuwa kuangalia kila uso butu huku nikiwa kama watu hao waliweza kuelewa uovu wa ukoloni na kuomba kuwa nijaliwe siku ambayo miye nitashiriki katika kuangausha mfumo huo. Uzalendo wangu ukajitokeza. Nilikuwa tayari kuvumilia jambo lolote liwalo ili kufikia lengo langu.

Hisia kama hizo zilitokea kotekote Afrika. Msomi wa Kinigeria, Nnamdi Azikiwe, alitumia nafasi kubwa katika magazeti yake ya *West African Pilot na Comet* kuzungumzia mapambano ya Ethiopia.

## *Hatima ya Liberia na Ethiopia kuhusu kuingiliwa kwa Ubeberu*

Kwa nini basi, hatimaye Liberia ilinusurika na baa la kuingiliwa kati na wageni na kuhifadhi uhuru wake mwishoni mwa 1936, ilihali Ethiopia ilisalimu amri falau kwa muda mfupi? Jibu lake halimo katika hali za ndani za nchi mbili hizo kwa vile nchi zote hizo zilikuwa na hali moja kufikia 1935 kama ilivyoelezwa hapo awali. Wala sababu haimo katika nguvu za majeshi yao kwani hayo hayakuwa na nguvu zilizolingana na za majeshi ya wavamizi wa kigeni. Tofauti muhimu katika kunusurika kwa Liberia na kutonusurika kwa Ethiopia ilikuwa kwamba jirani ya Ethiopia ilikuwa beberu mwenye kuazimia kuvamia na kutamalaki ardhi ya Ethiopia na kulipiza kisasi cha Adowa na kwa hivyo, kushambulia na kutamalaki Ethiopia. Kwa upande wa pili, majirani wa Liberia, Uingereza na Ufaransa, walikwishatamalaki maeneo makubwa katika Afrika na hawakuwa na kisasi cha kulipiza na hivyo hawakuwa na sababu za kuwafanya wahambulie na kutamalaki Liberia kama vile Italia ilivyoshambulia na kutamalaki Ethiopia. Ingawa Ethiopia ilishindwa, lakini kutokana na mapambano yake makali ya kujilinda na hisia zilizotokea hasa miongoni mwa Waafrika na watu weusi wote duniani, Ethiopia ikawa mwakilishi wa shauku ya Afrika ya kujikomboa kutokana na utawala wa kikoloni.

# 29

# *Afrika na Ulimwengu Mpya*

Katika majuzuu yaliyotangulia ya mfululizo huu, tulizungumzia usafirishaji wa kulazimishwa wa mamilioni ya Waafrika hasa kutoka Afrika ya Kati na Magharibi wakati wa biashara ya karaha ya watumwa wa Bahari Kuu ya Atlantiki katika karne za kumi na saba na kumi na nane.

Katika sura hii, tutachunguza kwa makini zaidi maingiliano kati ya Waafrika na watu wenye asili ya Kiafrika walioko Marekani katika kipindi cha ukoloni cha historia ya Afrika, historia ambayo baadhi ya jiha zake zimekwishagusiwa katika sura zilizotangulia za juzuu hili.

Maingiliano kati ya Waafrika na Waamerika weusi katika kipindi kilichoanzia 1880 na kuishia 1935 yalihusika na aina tano kuu za amali: (I) kurejea kwa Waamerika weusi – wengi wao kutoka Amerika Kaskazini lakini pia kutoka Carribean na Brazil kurudi Afrika Kusini na Pembe ya Afrika; (ii) Uenezaji wa Injili wa Kimarekani uliofanyika na Wamisionari wa Marekani Waafrika/weusi kama "Waenezaji wa Injili" katika Afrika, (iii) kuanzishwa kwa Njia ya Kati ya mtiririko wa wanafunzi wa Kiafrika wakifuzu katika shule na vyuo vya Watu Weusi wa Kimarekani (iv) amali anuwai za Uafrika-wote pamoja na kuwa na mikutano, vyama, na amali za kielimu ambazo ziliwakutanisha Waafrika na ulimwengu wa watu weusi wa Amerika na ambazo zilisaidia kuathiri matukio katika Afrika ya Kikoloni; na (v) Ushikiliaji na ugeuzi wa thamani za utamaduni wa Kiafrika katika Amerika ya Kilatini na Carribean. Maudhui hayo matano yatajadiliwa moja baada ya jingine katika sehemu tano za sura hii.

## *Kurejea Afrika*

Ingawa kulikuwa na mabadiliko ya dhahiri katika hisia za Waamerika Weusi ya kutoka kwenda Liberia lakini Waamerika Weusi bado waliendelea kuonyesha raghba


ya kutaka kunamia Afrika katika miaka ya mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na ya mwanzoni mwa karne ya ishirini. Kwa mfano, katika 1878, Shirika la *South Carolina – Liberian Exodus Joint Stock Steamship Company* liliwasafirisha wahamaji wapatao 206 kwenda Liberia na katika 1889, Dkt. Edward W. Blyden, mtetezi wa Uafrika-wote, mzaliwa wa West Indies alizuru Marekani kwenda kuwashawishi Watu Weusi waunge mkono uhamaji. Vilevile, kati ya 1880 na 1900, Askofu Henry Moneal Turner alihangaika katika kujaribu kukusanya desturi mbili zilizokuwa zimetawala katika historia ya kisasa ya makingiliano kati ya Waafrika Waamerika-Weusi. Uhamaji wa Waafrika na uenezaji wa Injili ya Kikristo. Kutokana na juhudi za Turner zaidi ya Waamerika-Waafrika walihama kwenda Liberia katika Machi 1896.

Baadaye Turner aliwahi pia kuwa mshauri wa Chama cha Kimataifa cha Uhamaji (International Migration Society) ((IMS) na Alabama ambacho kiliwapeleka takriban wahamaji 500 kwenda Afrika kabla chama hicho hakijafa katika 1900. Baadhi ya watu hao 500 walibaki Liberia na baadhi yao walirejea Marekani.

Baada ya karne ya ishirini kuingia, mwito wa kurejea Afrika uliendelezwa na watu wengine. Kwa mfano, mwanzoni mwa karne ya ishirini, mtu mmoja ajulikanaye kwa jina la Captain Dean alitarajia kushawishi kufanyika makazi ya Waamerika Weusi katika Afrika Kusini ili kuwa na taifa lenye nguvu la Watu weusi. Lakini, baada ya kukaa kwa muda mfupi kabisa kwa dhamira ya kufanya mipango ya makazi hayo, Dean alifukuzwa na serikali ya Watu Weupe kwa sababu ya kile kilichoitwa `shughuli za uchokozi'. Katika 1914, Chifu Alfred C. Sam, Mwafrika kutoka Ghana, akaenda Oklahoma na akawashawishi wakulima weusi 60 hivi kuwa Afrika ilitoa fursa nzuri zaidi kwao na kisha akaabiri nao kwenda Saltpond katika Ghana. Mpango wa Sam pia ulishindwa na sababu kubwa ilikuwa vikwazo ambavyo serikali ya Ghana iliviweka kwa Waamerika waliotaka kuhamia nchini humo. Lakini hakuna aliyeathiri Waafrika na Waamerika Weusi zaidi kuliko alivyofanya mtetezi wa uhamaji Marcus Garvey.

Kwa sababu Marcus Garvey aliamsha hisia za hadhi za mtu mweusi, waangaze kwenye Afrika katika kipindi kilichofuata Vita Vikuu vya Kwanza. Katika 1914, baada ya kusafiri sana katika nchi za Carribean, Amerika ya Kati na Kusini na baada ya kuishi Uingereza kwa miaka miwili, Garvey alianzisha huko Jamaica mradi wake uliokusudia kuendeleza uhamaji wa Waafrika na mpango uliohusiana nao ambao aliuita *Universal Negro Improvement and Conservation Association and African Communities Leagues* (baadaye ukaitwa UNIA tu). Mradi huo ambao aliuhamishia Marekani, uliingiza mipango ya uanzishaji wa shule za kufunzia viwanda na kilimo kwa ajili ya watu weusi huko Jamaica, kikosi cha *Black Star* cha meli za kufanyia biashara Kati ya Watu Weusi wa Afrika na Marekani, na juu ya yote, taifa moja la mbari kuu (wa Waafrika).

Garvey, kama walivyofanya watetezi wa uhamiaji waliotangulia, alichagua nchi ya Liberia kuwa ndiyo nchi ya Afrika ya kuendeleza mpango wake na alimtuma mjumbe wake huko mnamo Mei 1920. Mjumbe huyo alieleza madhumuni ya Jumuiya




**29.1** *Wabrazili wa Kiafrika huko Afrika ya Magharibi karne ya kumi na nane na kumi na tisa*

hiyo kuwa ni uhamishaji wa makao makuu ya UNIA kwenda Liberia, msaada wa kifedha kwa Liberia wa kujenga shule na hospitali, ulipaji wa deni la Liberia, na makazi ya Waamerika Weusi nchini Liberia ili wasaidie kukuza kilimo na maliasili. Serikali ya Liberia ilikubali ombi la UNIA la kutaka kupewa ardhi nje ya Monrovia na Garvey naye akaleta kikundi cha mafundi kupima eneo la kujenga nyumba za kukaliwa na familia 20,000 hadi 30,000 ambao Marcus alitarajia kuwahamisha huko katika miaka miwili kuanzia 1924. Lakini mafundi wa Garvey walipofika Maryland mnamo Mei 1924 walikamatwa na kutiwa kizuizini na kufukuzwa mnamo Julai 1924. Punde tu baadaye serikali ya Liberia ilimpiga marufuku Garvey. Jaribio jingine la Garvey la kuanzisha mpango kama huo huko Ethiopia katika miaka ya mwisho ya 1920 pia lilishindwa.

Wabrazili-Weusi

Vilevile maelfu ya Wabrazili weusi walihama kwenda Afrika Magharibi mpaka wakati utumwa ulipokomeshwa rasmi nchini Brazil katika 1882. Vikundi hivyo vya wahamaji vilipendelea kukaa katika miji ya mwambao ya Nigeria na Dahomey (siku hizi Benin) na wachache miongoni mwao walienda Togo na Ghana. Walianzisha jumuiya katika maeneo hayo ya mwambao, ingawa wachache walienda katika miji ya mrima kama vile Abeokuta. Idadi kubwa ya wahamaji walikuwa *negro de ganho* huko Brazil, yaani watumwa walioishi mijini wakifanya kazi za uashi, useremala, ukalafati n.k. bila ya kuzuiwa na waligawana mapato yao na matajiri wao. Wajenzi wachache wenye ustadi walitumia ujuzi wao na wakajenga eneo la makazi katika Porto Novo, Whydah na hususa Lagos, ambako kulijengwa mtaa wa Brazili.

Huko Dahomey (sasa Benin) baadhi ya wanafunzi waliohudhuria skuli za Wamisionari wa Kiingereza na Kifaransa walitumiwa kama wasaidizi na watawala wa kikoloni kwa sababu walikuwa wameelimika. Ingawa kikundi hiki kilikuwa na baadhi mahususi, lakini hawakuheshimiwa na Wazungu ambao hawakuwa na uhusiano mzuri na wenyeji wa Kiafrika kwa sababu ya tabia zao na mtindo wao wa maisha.

Huko Lagos, jumuiya hiyo ilijitambulisha kwa kucheza ngoma za jadi njiani siku za sikukuu. Lakini jinsi miaka ilivyopita, vikundi hivyo huko Lagos na Benin vikapoteza sifa zao zilizowapambanua. Kireno, ambacho wakati wa nyuma kilikuwa kinahesabiwa kuwa ni lugha ya biashara, kilipitwa na Kiingereza huko Nigeria na pia Kifaransa huko Dahomey (Benin).

Huko Ghana, Wabrazili-Weusi walisitawi kama kikundi cha peke yake kutokana na tabia zao za Kimagharibi. Kutokana na hali hiyo, wakajulikana kama *Wataboni*. Lakini asteaste wakaacha mila zao mahsusi za Kibrazili wakati bado wangali wamebakiza sifa zingine za kiutamaduni kama vile upigaji ngoma nyakati za sherehe kama za maandamano ya siku-mbili ya kila mwaka katika barabara za zamani za Accra. *Wataboni* walipolowea nchini, wakawa hawana budi kufanya mkataba wa utumwa na chifu wa Wagaa wa Accra. Waliacha kutumia lugha ya Kireno mapema

sana. Maingiliano ya haraka ya *Wataboni* huko Ghana yanatofautiana na yale ya polepole ya Wabrazili-Weusi wa Lagos, Abeokuta, Porto-Novo, Wahdah na miji midogo ya mwambao ya Nigeria, Benin na Togo.

Katika Lagos jumuiya ya Wacuba-Weusi ikaanzishwa pamoja na ile ya Wabrazili. Jumuiya hiyo ilikuwa na watu wachache waliorejea kutoka Cuba.

## *Uenezaji wa Injili wa Waamerika Weusi katika Afrika*

Njia moja iliyotumika katika kukuza mahusiano kati ya Waafrika na Waamerika Weusi katika kipindi cha ukoloni, pale ambapo hapakuwa na makundi ya kuhamia Afrika, ilikuwa ya kuwaleta Wamisionari weusi Waafrika kwa kuhubiri injili ya Kikristo. Mwanzoni, sehemu kubwa ya uhubiri huo wa injili ulifanywa naWamisionari weusi ambao waliyatumikia madhehebu ya kawaida yaliyokuwa yanatawaliwa na watu weupe. Kwa mfano, Kanisa la Waprebiteri (Presbyterian) waliwadhamini wamisionari weusi katika 'French Cameroon' tangu 1896. Lakini punde tu baadaye, jumuiya za makanisa ya Watu Weusi zenyewe zikawa zinaendesha barabara shughuli za kimisionari katika Afrika.

Ama kwa hakika, Waamerika-Weusi katika karne ya kumi na tisa walihimizwa wawe na mkabala mahususi kuhusu 'ukombozi' wa jamii za Kiafrika. Kwa mfano, Askofu Turner alitetea kijasiri kuwa 'Mungu alimleta Mmarekani-mweusi kumfanya awe Mkristo ili aweze kurudi Afrika na kuikimbia nchi.

Makanisa ya *Africa Methodist Episcopal* (AME) na *African Methodist Episcopal Zion* (AMEZ) na *National Baptist Convention* (NBC) yote yalitumia wamisionari weusi katika Afrika katika kipindi chote cha ukoloni. Vituo vya mwanzo vya NBC vilianzishwa huko Liberia mnamo 1883, navyo viliimarisha kazi iliyokwishafanyika awali na Lott Carey. Kanisa la AME Zion pia lilijikita katika Liberia katika 1878 na huko Ghana katika 1896. Askofu John Bryan Small wa Carribean baadaye aliandaa mikutano miwili ya kila mwaka ya AME Zion nchini Ghana na kwa njia hiyo aliwavutia Aggrey na Franck Osama Pinauko wajiunge na makanisa ya Waamerika-Weusi na hatimaye, kutumikia kanisa la AME Zion. Katika 1930, Wamisionari wa AME Zion wakaenda Nigeria kufanya kazi, kwa kuukubali mwaliko wa makanisa ya huko ya Kiafrika yaliyofungamana na Zion. Papo hapo, Kanisa la AME, lilidhamini misioni katika maeneo kadhaa ya Afrika ikiwemo Sierra Leone 1886, Liberia 1890 na Afrika Kusini 1896.

Waamerika Weusi wengi waliouitikia mwito wa Kanisa katika miaka ya mwisho ya karne ya kumi na tisa walikwenda kusini mwa Afrika kama Wamisionari na taathira zao zilikuwa kubwa. Katika 1996 Kanisa hurn la kujitenga la "Kiafrika" au "Kiethiopia" na Kanisa la AME yaliungana. Ingawa muungano kati ya Makanisa ya AME – Ethiopia, ulivunjika baada ya mwaka mmoja wakati Dwane alipojitenga, AME liliendelea na hata kupanna amali zake za kimisioni kwa msaada wa Levi Coppin ambaye aliteuliwa kuwa Kasisi Mkazi wake wa kwanza na Charlotte Mayhe ambaye

lirejea kutoka masomoni Marekani katika 1901. Kwa muda wa miaka hamsini iliyofuata, kanisa la AME liliendelea kuwa lenye nguvu huko Afrika Kusini.

Huko Nyasaland (Malawi) *National Baptist Convention* pia lilikuwa amilifu kama AME. Chama hicho kilianzishwa na John Chilembwe, kijana wa Kiyao ambaye alikwenda Marekani mnamo 1897, akasomea katika Seminari ya Thelojia ya Virginia iliyokuwa ya Watu Weusi, akajifunza upadre na akarejea nchini kwao mnamo 1900. Kama ilivyokwishaelezwa hapo awali, Chilembwe baadaye aliongoza uasi ulioshindwa katika 1915 ambao umekwishajadiliwa, alijitahidi kuanzisha misioni ya tasnia ambamo Waafrika walifukuzwa sana na ufundi wa kufundishwa Ukristo, yaani, kufuatana na mtindo aliouona ukifuatwa na Waamerika - Weusi.

Ingawa mamlaka ya kisiasa na makanisa ya watu weupe ya Afrika Kusini yalipinga juhudi hizo, uhusiano wa AME ulioanzishwa na Turner uliiwezesha idadi kubwa ya wanafunzi wa Kiarika kuhitimu katika shule Kimarekani. Kadhalika, katika Afrika ya Kati ya Uingereza, na Afrika Magharibi, wanafunzi wa Kiafrika walishawishiwa na mara nyingi kupewa ruzuku na makanisa ya Waamerika weusi. Amali hizi za kimisheni ziliweka msingi wa awamu mpya katika mwingiliano kati ya Waafrika na Waamerika-Weusi katika kipindi cha ukoloni. Mwingiliano huo ulileta athari kubwa katika harakati zilizofuata za kizalendo za Waafrika katikati ya karne ya ishirini.

## Mwingiliano wa kidini kati ya Brazili na Mwambao wa Afrika

Katika mambo yahusuyo dini, hususa katika ufundishaji wa injili, hatuwezi kulinganisha taathira za Wamerika-Weusi na zile za Wabrazili-Weusi. Wakati Waamerika -Weusi walijishughulisha moja kwa moja au vinginevyo na uenezaji wa Biblia, Wabrazili-Weusi hawakuamania kazi za kuongea. Baada ya kufika Lagos baadhi yao walifanikiwa kurudi katika nchi zao za asili. Hati za kihistoria zimetaja kuwa Wabrazili-Weusi waliokuwa Waislamu walipitia Lagos kuelekea nchi ya Wahausa. Katika sehemu walimoishi Wabrazili hao katika Lagos msikiti mkuu ulijengwa na mafundi kutoka Brazili. Vilevile, Wakatoliki walijenga kanisa la kwanza, Kanisa la Msalaba Mtakatifu, lililoanzishwa katika 1879, na waliwapeleka watoto wao katika shule za misheni za Kiingereza na Kifaransa. Wana wa Wabrazili-Weusi waliohudhuria shule za misheni walianza kutumika kama walimu wa shule na waketikisti katika shule na misheni zilizoanzishwa na mapadri wa *African Mission Society* katika kanda hiyo. Waketikiti hao walitumikia misheni, zilizokuwa na asili ya Kizungu, na siyo vyombo vya kimisheni vilivyoanzia Brazili au vilivyotokana na juhudi za jumuiya ya Wabrazili-Weusi ya Lagos. Ama kwa hakika, lugha ya kufundishia ilikuwa Kiingereza na wakati mwingine Kifaransa.

Kinyume na vile ilivyotokea huko Marekani ambako uongofu ulikuwa wa kiwango kikubwa zaidi na kuwafanya Waamerika-Weusi wa Kaskazini kadha kuwa wahubiri wa imani ya Ukristo, Wabrazili-Weusi walishikilia imani zao za kidini za

Kiafrika. Kwa hiyo, Wabrazili-Weusi waliokuwa wanaishi katika Mtaa wa Wabrazili na ambao walikuwa ndicho kiini cha tabaka la kati ambacho kiliendelea kuwa kikundi cha kijamii kilichofungamana na kilichojitokeza, kwa kiasi fulani, kwa sababu ya dini ya Kikatoliki, waliamini madhehebu ya kaya ya *arixas* na waliomba ushauri wa *babalos ifa* (Waaguzi). Isitoshe, dini za Kiafrika bado ziliendelea kuathirki Brazili kutoka ng'ambo hii ya Atlantiki.

Vitu na vifaa vya kimadhehebu vya Kiafrika vilivyotumika katika sherehe za kidini za Wabrazili-Weusi kama vile kete na kola, daima vilikuwa vinaingizwa kutoka Brazili na asteaste vikawa vinatamaniwa sana. Kwa hiyo, thamani ya bidhaa hizo ikaongezeka kadiri idadi ya waabudu wa dini za Kibrazili ilivyoongezeka.

## *Athari za Elimu ya Kimarekani*

Wanafunzi wa Kiafrika walipokuwa wanaishi Marekani katika kipindi cha ukoloni, walianzisha misingi tofauti ya uhusiano kati ya Waafrika na Wamerika-Weusi na kati ya wanafunzi wa Kiafrika wenyewe waliotoka pembe zote za bara la Afrika. Waliporudi makwao, waliwahamasisha pia maelefu ya wananchi wenzao kujiandisha katika shule za Kimarekani kati ya 1880 na Vita Viku vya Pili. Kwa hiyo idadi ya wanafunzi wa Kiafrika nchini Marekani iliongezeka na uhusiano kati ya kikundi cha Waafrika na Waamerika-Weusi ulikuwa mrefu. Majina ya wanafunzi wa Kiafrika katika kipindi cha ukoloni walioelimishwa Marekani ni maarufu sana na miongoni mwao wako viongozi wa hivi karibuni wa nchi za Kiafrika (Azikiwe, Nkrumah na Banda) pamoja na viongozi wa awali wa vyama vya uzalendo wa jumuiya (A.B. Xuma, John Dube, Marshall na Charlotte Maxeke, J.E.K. Aggrey, Pixley Ka Izaka Seme, D.S. Malekebu - F. Osam – Pinakko, Peter Koinange, Ndabaningi Sithole, Edurdo Mondalne, na Chilembwe). Muda ulivyopita, idadi ya Waafrika waliokata nauli ya kwenda Marekani ilipita idadi ya Wamisionari weusi waliokuja Afrika kutoka Marekani. Kwa maneno mengine, jambo ambalo lilianza kama harakati za Kimarekani za kufundisha Biblia katika Afrika ili kuwakomboa watu kiroho hatimaye ilisaidia kujenga nyonyo za mapinduzi ya kielimu, kiufundi na kisiasa.

Inawezekana kukisia athari za uzoefu wa elimu ya Kimarekani kwa Waafrika katika makoloni na maendeleo ya kupinga - ukoloni kwa kuzingatia kwa ufupi wasifu wa baadhi ya wanafunzi wa Kiafrika. Kwa mfano, J.E.K. Aggrey, alikwenda Marekani kwa kuathiriwa moja kwa moja na Askofu wa AME Zion kutoka Barbados ambaye alipata elimu yake huko Marekani. Aggrey alipitia mafunzo ya 'Livingstone College; ambayo ilikuwa taasisi kuu ya elimu ya Kanisa la AME Zion huko Salisbury, North Carolina, kwa mapatano ya kuwa akimaliza masomo atarejea moja kwa moja Afrika kuhudhuria kanisa. Lakini alipokwisha kuhitimu shahada ya *baccaulaureatte* na ya dini, Aggrey alitumikia shirika la uchapishaji la AME huko Charlotte. Akawa mwandishi wa habari wa magazeti ya watu weusi, akatoa masomo ya bure kwa ajili ya walimu weusi waliokuwa wakiishi karibu, akatunukiwa uongozi wa kanisa ma

akafanywa mchungaji wa makanisa mawili ya watu weusi. Mahusiano yake na watu weusi wa Kimarekani yalikwishaongezeka alipomuona Msichana wa Kiamerika mweusi, ambaye huenda alikuwa wa kizazi cha Frederick Douglas, katika mwaka 1964. Baada ya kuishi miaka 22 miongoni mwa Waamerika-Weusi, Aggrey alirudi Afrika katika nyakati mbili tofauti akiwa mjumbe mmojawapo wa Tume ya Phelps – Stokes, lakini alifariki punde tu baada ya kakubali cheo cha "Msaidizi wa Makamu wa Mkuu" wa Shule ya Achimota ambayo ilikuwa imeanzishwa karibuni tu katika Ghana. Miongoni mwa vijana wa Kiafrika aliowaathiri ni Nnamdi Azikiwe, Kwame Nkrumah na Kamuu Banda ambazo wote baadaye walihitimu shule za watu weusi za Kimarekani.

Shughuli na taathira za John Chilembwe wa Malawi ambaye alisomea Marekani na kurudi nyumbani zimekwishazungumziwa. Mmalawi mwingine ambaye bado hajazungumziwa ni Mchungaji D.S. Malekebu. Alisomea *National Training School* katika Durham, North Carolina, kwenye 'Moody Bible Institute' hako Chicago, na baadaye mnamo 1917 alifuzu shahada ya utabibu. Aliporejea Nyasaland (Malawi) katika 1926, alianzisha tena *Providence Industrial Mission* ya Chilembwe ambayo serikali ya nchilindwa ya Nyasaland iliiangamiza baada ya uasi wake kushindwa katika 1915. Zaidi ya hayo, Malekebu alianzisha *Chidzulu Native Association* akateuliwa kuwa mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya, na akajitokeza kuwa kiongozi mkubwa wa jumuiya katika kipindi cha ukoloni.

Mfano wa mwisho unaotolewa ni ule wa Nnamdi Azikiwe ambaye kama Banda alishawishika kwenda Marekani na James Aggrey na kutokana na hisia zilizokuwapo Marekani kuhusu Marcus Garvey. Mwanzo alijiandikisha kwenye shule ya awali ya watu weusi katika West Virginia katika 1925. Baada ya miaka michache alipoingia Chuo Kikuu cha Howard, Nnamadi Azikiwe alisoma na kushirikiana na raia watano wa Kiliberia waliokuwa wanatafuta msaada wa fedha kutoka kwa Wamarekani, Washington alisisitiza kuwa "hao wako Marekani katika ziara rasmi, siyo tu kama wajumbe wa nchi zao, bali kama wawakilishi wa mbari kuu yote ya Wanegro..."

Mkutano wa Waafrika na Waamerika Weusi huko Tuskegee pamoja na miradi ya Tuskegee vilisababisha ueneaji wa "moyo wa Tuskegee barani Afrika. John Dube na D.D.T. Jabavu walikuwa watu wawili katika orodha ndefu ya Waafrika mashuhuri ambao walipitia Tuskegee. Dube alipokuwa mwanafunzi huko Oberlin na New York nchini Marekani alijihusisha na watu wawili, mwanaelimu wa Atlanta John Hope na Booker T. Wasshington wa Tuskegee. Dube alirejea Afrika Kusini katika 1899 na kuanzisha *Ohlange Institute* kwa kuiga moja kwa moja muundo wa Tuskegee. Jabavu ambaye wakati huo alikuwa mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha London, alikaa huko Tuskegee takriban muda wa miezi sita katika 1913 akizingatia mbinu za kilimo, wakati alipokuwa njiani katika ziara yake ya kutembelea taasisi nyingine za watu weusi Kusini.

Juu ya hayo, mfululizo wa mahafali za kila mwaka zilizojulikana kama *African Rhetoricals* zilifanyika huko Tuskegee pia kwa madhumuni ya kukidhi haraka haja mahususi za Waafrika. Katika mazoezi ya 1916, hotuba zenye mada kuhusu 'Maendeleo ya Tasnia ya Kakao Ghana" (The Development of the Cocoa Industry on the Gold Cost') na 'Uwezekano wa kuendeleza kilimo Afrika Kusini' ('Possibilities of the Development of Agriculture in South Africa') zilizotolewa na A.B. Xuma, na 'Dini na Maisha ya Kijamii Madagascar' (('Religion and Social Life in madagascar'). Hao ni Booker T. Washington mwanzilishi na Mkuu wa Taasisi ya Tuskegee, Dakta W.E.B. Du Bois na Aime Cessire.

Athari ya Washington na Taasisi ya Tuskegee juu ya Afrika na kwa wanafunzi wa Kiafrika waliojiandikisha na wenye hamu ya kujiendeleza ilikuwa kubwa.

Hadhi na stadi za Taasisi ya Tuskegee zililetwa Afrika na wanafunzi wake wa Kiafrika na Kimarekani, na Waafrika wengi walioizuru Taasisi au watu walioandikiana barua na Washington ambao hawakuwa wanafunzi waliofuzu mitihani na kwa njia ya mikutano mingi ya kimataifa na ujumbe wa kifundi.

Katika hotuba yake ya Msingi katika ıakutano wa Umoja wa Waafrika wote wa "Mkutano wa Kimataifa wa Mtu Mweusi" ('International Conference on the Negro') uliofanyika huko Tuskegee katika Msimu wa Mchanuo wa 1912, Washington alisisitiza maudhui ya mabadilishano ya mbinu na stadi kati ya watu weusi wa Kiafrika na wa Kimarekani. Miongoni mwa wajumbe waliohudhuria Mkutano wa 1912 walikuwa wajumbe kutoka Ghana, Afrika Mashariki ya Waingereza, Liberia, Nigeria, Ruanda, Afrika Mashariki ya Wareno na Afrika Kusini.

Miongoni mwa shughuli zilizohusiana na Afrika-wote za Tuskegee/Washington zilikuwa mikutano ya *Negro Business League* katika 1908, ambako Washington alionyesha furaha yake ya kuwepo Umoja wa Waafrika-wote kwa ajili ya mabadilishano kati ya Waamerika-Weusi. Alipokuwa anawatambulisha wajumbe wanazuoni weusi kama vile Ralph Bunche na hasa, Alain Locke na William Leo Hansberry katika masomo kama vile historia ya Waamerika-Weusi na ya Afrika kabla ya enzi ya ukoloni.

Alipohamia Chuo Kikuu cha Lincoln katika 1930, Azikiwe aliendeleza raghba yake katika historia ya watu weusi na mahusiano ya kimbari kuu. Pia alifanya kampeni ya kutaka watu weusi wateuliwe kuwa walimu badala ya watu weupe peke yao maana aliona kuwa 'ni jambo zito kuwa Chuo cha Wanegro kiwe kimeendelea miaka 86 kabla Mnegro hajawa mwalimu: Mamlaka ya Chuo Kikuu yalichukizwa na harakati za upinzani za Azikiwe kiasi ambacho yaliita kupendekeza viza yake ya uanafunzi ipunguzwe muda. Kwa hiyo, Azikiwe ilibidi aondoke zake kurudi Afrika katika 1934. Hakurejea kwao Nigeria bali alikwenda Ghana ambako alikaa kwa muda baada ya kukataliwa ualimu huko Nigeria katika King's College, Lagos na katika utumishi wa kidiplomasia huko Liberia. Huko Ghana, akawa mwandishi mmojawapo maarufu wa habari aliyepinga ukoloni mpaka aliporejea kwao ambako amekuwa na

nafasi ya uongozi katika siasa ya nchi yake tangu wakati huo na hata kuwa Gavana-Jenerali wa Nigeria.

## *Umoja wa Waafrika Wote? Vipengere vya Kisiasa na vya Kiutamaduni*

Mbali na mabadilishano hayo ya kielimu, mfulizo wa vyama na mikutano ya Umoja wa Waafrika Wote, pamoja na shughuli za kibiashara na kifasihi au kiutamaduni ziliwahusisha Waafrika na Waamerika-Weusi na kusaidia kuathiri matukio katika Afrika na Waamerika-Weusi na kusaidia kuathiri matukio katika Afrika ya Ukoloni. Amali za watu wanne zilitawala maendeleo ya Jumuiya rasmi ya Umoja wa Waafrika wote katika kipindi cha ukoloni.

Mtu wa pili ambaye alitoa nıchango mkubwa katika kuendeleza Umoja wa Waafrika-wote katika kipindi hiki alikuwa Dkt. W.E.B. Du Bois. Kimsingi Du Bois alifanya hivyo kwa njia ya kuendeshsa mikutano mitatu ya Umoja wa Waafrika-wote aliyoiitisha katika miji mikuu mbalimbali ya Ulaya.

Aliitisha mkutano wa kwanza alipokuwa Ufaransa (i) kuliandikia habari gazeti la *The Crisis* kuhusu Mkutano wa Amani wa Paris ((Paris Peace Conference); (ii) kukusanya habari kwa ajili ya kitabu kilichopendekezwa cha 'Historia ya Mnegro wa Kimarekani katika Vita Kuu' (History of the American Negro in the Great War') na (iii) kutafuta msaada kwa ajili ya haki za kisiasa za 'mbari kuu nyeusi ziishizo Marekani na kote duniani'. Miongoni mwa maazimio yaliyopitishwa kwenye Mkutano wa Paris wa 1919, azimio moja lilikuwa la kutetea uhuru wa Waafrika.

Katika Mkutano wa pili wa Umoja wa Waafrika-wote ulioitishwa 1921, Du Bois alihudhuria pamoja na Walter White, msanii Mwaamerika-Mweusi Henry O. Tanner Jessi R. Fausat, mwandishi mweusi wa Tahariri ya *The Crisis* na mwanariwaya mkubwa kati ya wnariwaya wa mvuvumko wa Harlem, Mwimbaji Mweusi wa Kimarekani Ronald Hayes na Blaise Diagne kutoka Senegal. Katika Mkutano wa 1923 wahudhuriaji walitoka Marekani, Carribean na Afrika. Pamoja na Du Bois, Rayford Lagon na Askofu Vernon wa AME wa Marekani, Chifu Amonsh III wa Ghana na Kamba Simango wa Afrika Mashariki ya Kireno walihudhuria na kusaidia kutunga maazimio muhimu kadha pamoja na mwito wa jumla wa 'kuendeleza Afrika kwa manufaa ya Waafrika'. Mkutano huo ulitamka haja ya kuwa na uwakilishi wa Afrika katika Tume ya Udhamini ya Umoja wa Mataifa (League of Nations Mandates Commission), 'taasisi ya kufanya utafiti katika tatizo la Wanegro' na kurejeshea na kuwaongezea haki watu weusi pote katika ulimwengu wa watu weusi, na ukombozi wa Abyssinia, Haiti na Liberia 'kutoka kwenye makucha ya uhodhi wa kiuchumi na riba ya wenye-fedha wa dunia'. Du Bois aliyachakua maazimio hayo binafsi kwenda kuhudhurisha mbele ya Umoja wa Mataifa huko Geneva.

Pengine ni kutokana na hisia alizoonyesha Du Bois kwa ajili ya Liberia ndio Rais Coolidge akaamua kumwomba awakilishe Marekani katika sherehe ya kumtawaza Rais wa Liberia katika 1923. Alipokuwa Liberia, katika ziara yake ya

kwanza Afrika, huenda Du Bois alipinga aina ya Umoja wa Waafrika-wote wa uhamaji uliotetewa na Garvey, maana baada ya muda mfupi tu Waliberia waliukataa mpango wa UNIA.

Mtu wa mwisho kati ya wale walioleta athari kubwa ya Umoja wa Waafrika-wote katika Afrika alikuwa Marcus Garvey. Shughuli zake hazikuishia katika uwanja wa uhamaji ambao umeshajadiliwa. Ama kwa hakika, akawa ndiye kitovu cha shauku kubwa ya Umoja wa Waafrika-wote huko Marekani, Carribean, Afrika Magharibi, Afrika Mashariki, Afrika ya Kati, fauka ya yote, Kusini mwa Afrika kati ya 1916 na miaka ya katikati ya 1930. Ujumbe wa Garvey kwa watu wote ulikuwa: panga, nunua kwa watu weusi, saidia Shirika la Meli la Black Star, (ambayo ingeweza kuwachukua wahamiaji weusi kwenda Afrika na kurudi na malighafi, na saidia kuwafukuza weupe kutoka Afrika. Wakati Du Bois alikuwa mtetezi mkuu wa Umoja wa Waafrika-wote miongoni mwa Wasomi weusi nje ya Afrika na Washington, Garvey alikuwa akijulikana vema zaidi miongoni mwa wasanii vijijini.

Athari ya Garvey iligawika sawa baina ya umma wa weusi wa kila tabaka la nje na ndani ya Afrika. Kiasi kikubwa cha ilihamu ya Garvey ya Umoja wa Waafrika wote ilitoka kwa msomi wa Kimisri, Duse Muhammad Ali, huko Uingereza katika 1912, na pia kutokana na kusoma, vilevile huko Uingereza, Tawasifu ya Washington, *Up From Slavery.*

Hapa mwanzoni chama cha UNIA cha Garvey, ambacho kiliundwa kwa dhamiri ya kuwa na shule ya aina ya Tuskegee huko Jamaica, kikawa kiungo kati ya idadi kubwa ya Wafrika na Waamerika weusi nje ya Afrika na kwa kutumia gazeti lake la kimapambano, *Ulimwengu wa Maegro* (The Negro World), Garvey alifanikiwa kuleta athari ya kutosha ya Uafrika-wote. Kati ya 1920 na 1938 ilifanyika mikutano minane ya UNIA. Mikutano mitano ya mwanzo ikiongozwa na Garvey ilifanyika Mjini New York katika mwezi wa Agosti kila mwaka toka 1920 hadi 1924, miwili iliyofuata, baada ya Garvey kufukuzwa Marekani, ilifanyika huko Jamaica katika 1929 na 1934 na wa nane na wa mwisho, ulifanyika huko Canada katika 1938.

Kuanzia mkutano wa kwanza, Garvey alitetea nanzishaji wa shule za kuwafundisha watu weusi wa Afrika na Amerika elimu ya ufundi, uendelezaji wa 'fursa za kiuchumi katika kilimo, tasnia na biashara ili kukuza biashara' kati ya watu weusi, uanzishaji wa Shirika la Meli la Black Star kusululisha biashara hiyo. Kadhalika na uanzishaji wa gazeti la kila siku ' katika miji mikuu mikubwa kadha duniani kueleza hisia za upendeleo wa mbari nzima ya Wanegro, hususa London, Paris, Berlin Cape town, New York, Washington D.C., Gold Coast (Ghana) na Carribean, Garvey aliamini kuwa utekelezaji wa mpango huo ungewaungamisha 'kila sehemu ya mbari ya Wanegro pote duniani katika chombo kimoja'. Wanarika wa Garvey walihisi kuwa ujumbe wake 'ulidhihirika katika Afrika' na uliwaathiri viongozi wa kizalendo wa Kiafrika na wasomi kama vile Casely-Hayford na Jomo Kenyatta, Kwame Nkumah, Kamuzu Banda na Nnamdi Azikiwe.

Wakati Garvey na Du Bois walikuwa wanawahamasisha kisiasa watu weusi katika miongo mitatu ya mawazo ya karne ya 20, papohapo ulitokea uhusishaji wa utamaduni wa Kiafrika ambao ulileta athari kubwa. Uthibitishaji huo wa utamaduni wa watu weusi ambao ulianza kupata mashiko katika Ulaya, Caribbean naAfrika Magharibi uliongozwa na wanafunzi wa Kiafrika na Carribean walioishi Paris na walisema lugha ya Kifaransa. Wanafunzi hao walijiunga na harakati za Umoja wa Waafrika-wote (Pan African Congress) na msisimko wa jumla wa Mvuvumko wa Harlem (Harlem Renaissance).

Kwa afupi, maingiliano kati ya watu weusi wa Caribbean wenye kutumia lugha ya Kifaransa (kama Vile Aime Cesaire wa Martinique, ambaye shairi lake maarufu *Canier d'un retour us Pays Natal* (ulichapishwa katika 1939) na wasomi wa Afrika Magharibi (kama vile mshairi-mwanasiasa wa Kisenegal Leopold Senghor) walianzisha harakati za Unegro (Negritude) ambazo zimekwishazungumziwa kwa ufupi. Harakati za Unegro (Negritude) zilikitwa katika imani ya kuwa Waafrika na watu wenye asili ya Kiafrika walikuwa na urithi mmoja wa kiutamaduni na waandishi wa Unegro (Negritude) walijaribu kurejesha uhusiano kati ya watu weusi kote duniani. Dhana ya Unegro (Negritude) iliathiriwa sana na uzoefu wa watu weusi katika nchi za ng'ambo na kwa maandishi na shauku za kisomi za Mvuvumko wa Harlem (Harlem Renaissance). Kwa upande wake, harakati za Mvuvumko (Renaissance) zilivukutwa na unasibishaji uliokuwa unajitokeza wa kiutamaduni na Afrika. Contee Gullen alijiuliza kishairi "Afrika ina maana gani kwangu"? katika shairi lake liitwalo "Urithi" ("Heritage") na Langston Hughes katika shairi lake "Mnegro Azungumzia Mito" ("The Negro speaks of Rivers") anataja jinsi alivyojenga kibanda chake karibu na mto Kongo ambao mtiririko wake ulimbembeleza mpaka akalala. Waandishi hao wawili wote waliwaathiri sana Senghor na waandishi wa Unegro ((Negritude). Lakini ni Mjamaica mwingine, Claude Mackay, ambaye ndiye shairi lake lilisaidia kuunganisha Umoja wa Waafrika-wote kiutamaduni na kisiasa, aliposhikilia katika shairi lake kuwa watu weusi wanapaswa kukiri kuwa wanateswa na kupinga mateso wanayopata na kusisitiza hadhi zao. Katika Brazili, maandishi ya Salano Trinidad (1908-19973) yaliziingiza dhana za Uafrika –Wote na Unegro (*Negritude*) katika ushairi.

## *Kudumu na kugeuka kwa thamani za Kiutamaduni na Kiafrika katika Amerika ya Kilatini na Caribbean*

Waandishi kadha wanavuta nadharia zetu kwa kutonyesha kuwa wapo Waafrika katika nchi za Kimarekani na Caribbean. Waandislu hao wanahesabu kuwapo kwa Waafrika hao kwa kuangalia asilimia ya vizazi vya Afrika katika jumla ya idadi ya watu wa kila nchi. Vikundi vitatu vikuu vyaweza kutambuliwa kutokana na vigezo hivyo.

Kikundi cha kwanza ni cha nchi ambamo walio wengi katika jumla ya idadi ya watu ni weusi. Mfano wa nchi hizo ni Haiti, Jamaica, Trinidad na Tobago na Barbados. Kikundi cha pili ni cha nchi ambamo uwiano wa watu wenye asili ya

Kiafrika ni mdogo katika jumla ya watu. Nchi hizo ni kama Argentina, Chile, Uruguay, Paraguay na Bolivia, miongoni mwa nyinginezo. Kikundi cha tatu ni chenye nchi kama Brazil na Cuba, ambako watu weusi wamekuwa na nafasi muhimu katika uchumi wao na wamekuwa na athari kubwa ya kiutamaduni na ambako mchanganyiko wa mbari mbalimbali ni matokeo ya watu wa mbari mbalimbali kuwamo.

Mwisho, vikundi viwili vingine vya nchi vinafaa vitajwe pia. Kikundi cha kwanza ni cha nchi kama Columbia, Panama, Nicaragua. n.k. ambamo mna makundi madogo yaliyofuangamana yenyc asili ya Kiafrika. Kikundi cha pili ni cha nchi zile ambamo mna vikundi vya watu wenye asili ya Kiafrika na ambazo hazijapatia mwendelezo wa · mtangamano katika Dunia Mpya kama vile Surinam ambako wanapatikana Wasoni, Wadjuka, Wasaramacasi na Waakwasi, wa Jamaica, Santo Domingo na hata Haiti na Cuba ambako ndiko maskani ya Wamaruni. Kwa vile makundi hayo yanaishi misituni huko Surinam na katika French Guiana yameweza kuhifadhi vilivyo thamani zao za msingi za kiutamaduni na muundo fulani wa kijamii.

Mfanano kati ya Amerika ya Kaskazini na Amerika ya Kusini na Carribbean katika kuwapo kwa Waafrika na hasa thamani za kitamaduni na Kiafrika si wa uhakika maana hali zilihitilafiana sana kutokana na njia mbalimbali zilizotumika na 'utangamano' wa watumwa wa zamani katika maeneo hayo, na hata kati ya nchi moja na nyingine.


Kwa upande wa utamaduni, wakati huko Marekani uongofu katika dini ya Kiprotestanti ulisababisha kuachwa kwa desturi za kiutamaduni na kutokeza kwa mkabala mpya, huko Amerika ya Kilatini na Caribbean thamani za kiutamaduni za Kiafrika zilidumu katika viwango mbalimbali au zilipata mageuzi. Kwa mfano, katika Haiti, ambako watu weusi ni wengi zaidi, dini halisi ya Kiafrika iliathirika na uhalisi wa kimuundo wa jamii ya Kihaiti na umuhimu wa machotara. Mfululizo wa mabadiliko yaliyotokea ulianzishwa na "miungu" mipya ambayo ilikidhi mahitajio ya hali mpya. Katika visiwa vya jirani, kutokana na kazi za Wamisionari wa Kiprotestanti, "utamaduni wa watu weusi" ulikwishaanza kujitokeza katika harakati mbalimbali kama vile za Warastafaria. Utamaduni ulikuwa wimbi la mrejesho wa Kimasihi dhidi ya mamwinyi weupe ambamo zilidhihirika jazanda za Kiafrika na Mfalme Haile Selassie kuonyeshwa kuwa ndiye Masihi.

Kwa upande wa pili, huko Jamaica, pamoja na madhehebu ya Sasabonsani yenye asili ya Kiasante, zilikuwapo dalili za 'utamaduni wa Kiafrika' ambazo zilidumu katika kipindi kile cha kihistoria, hatimaye madhehebu hayo yakatoweka na kupisha madhehebu yanayotokana na mizimu *Jamaica Baptist Free Church* ambayo ilikuwa fikra iliyoanzishwa na Bedward. Sifa mojawapo ya dini hii ya uunganisho ilikuwa sherehe ya sikukuu za Kikatoliki na siku za Watakatifu, pamoja na kukimbilia uaguzi na uchawi. Kwa hiyo, siku za sherehe za miungu ziliingiliana na tarehe za siku za watakatifu wa Kikatoliki.

Mifano ya dini za uunganisho zilizohusisha utamaduni wa Wahindi-Waamerika inaonekana katika West Indies, hususa huko Honduras, ambako kimetokea



**29.2** (a)-(d) Mifano ya taathira za dini ya Yoruba kwa watu wenye vizazi vya Kiafrika wa Kibahia katika Brazili.



kizazi cha machotara kwa sababu ya kuzaliana kati ya wanawake wa Wahindi-Waamerika na Waafrika wanaojulikana kama Wakaribi Weusi (Black Caribs). Waafrika hao walikuwa vizazi vya wa Waibo na Waefiki na, baadaye wa Wafante, Waasante, Wafoni na Wakongo.

Usimilishaji wa watu weusi katika jamii ya kijijini ulitofautiana kufuatana na mahitajio ya kilimo, upungufu au upatikanaji wa wafanyakazi na ukubwa wa misafara kwa madhumuni tu ya kutafuta kazi katika nchi hizo, kama vile katika Brazili katika mashamba ya mikahawa. Usimilishaji huo unaonekana katika njia mbalimbali, ukijumuisha nyimbo za vikundi vya kidini vya Waafrika katika Cuba, na Brazili, wa ala za Kisafrika ambazo ziliingizwa vizuri katika utamaduni wa kimuziki, ufundi wa mapishi ya Kiafrika, matumizi ya baadhi ya mbinu za Kiafrika, kama ilivyokuwa huko Haiti, kwa mfano, matumizi ya zana za kilimo kama vile jembe miongoni mwa zana nyinginezo, na urithishaji wa thamani za kidini na falsafa za maisha. Ingawa utumwa ulikatiza utamaduni wa Kiafrika, lakini utamaduni huo mbali na kunusirika ulianzisha pia utamaduni mpya.

## *Hitimisho*

Itadhihirika kutokana na maelezo yaliyotangulia kuwa maingiliano kati ya Afrika na Dunia Mpya katika kipindi hiki chetu yalitofautiana na yalileta taathira muhimu na yenye matokeo makubwa kwa Watu Weusi katika mabara yote mawili kwa jumla na hususa kwa wale wa bara la Afrika. Katika nyanja za dini, elimu, fasihi na siasa, hapana shaka kuwa shughuli za wahubiri weusi wa injili wa Dunia Mpya, asasi za kielimu na viongozi wa kisiasa na waamilifu kama vile Garvey na Du Bois waliwaathiri sana wazalendo waliokuwa wanajitokeza na mawazo na shughuli za Umoja wa Waafrika-wote katika Afrika. Amali hizo pia ziliandaa awamu iliyofuata na ya mwisho ya kushambulia mfumo wa kikoloni katika bara la Afrika.

# 30

## *Ukoloni katika Afrika: Taathira na Umuhimu wake*

Kama ilivyokwishadhihirika katika sura za mwanzo za juzuu hili, hadi kufikia mwaka 1935, ukoloni ulikwishaota katika Afrika na haikuelekea kwamba ungeweza kutoweka tena. Hata hivyo, ilidhihirika kwamba ukoloni, kama ilivyo asasi yoyote ile inayoanzishwa na kuendeshwa kwa mabavu isingeweza kuvumilika. Katika kipindi cha miaka arobaini na tano tu, kuanzia mwaka 1935, mfumo wa ukoloni ulikwishang'olewa katika asilimia tisini ya eneo la Afrika na ukawa umebakia tu katika sehemu ile ya bara hili iliyo kusini mwa Mto Limpopo. Hii ni kusema kwamba katika sehemu nyingi za Afrika kipindi cha ukoloni hakikudumu hata kwa miaka mia moja; na, kwa hakika, kipindi hiki kilikuwa kati ya 1880 na 1960 tu. Katika historia ya bara hili na watu wake, hiki ni kipindi kifupi sana. Katika sura ya hitimisho ya juzuu hili, tungependa kujadili masuala mawili. Kwanza ni: ukoloni uliacha urithi gani katika Afrika, au tuseme ukoloni ulikuwa na taathira gani katika Afrika? Pili, kutokana na taathira hizi tunaweza kusema nini umuhimu wa ukoloni katika Afrika?

### *Taathira za Ukoloni*

Pengine tunaweza kusema hakuna jambo ambalo limewahi kuleta majadiliano na mabishano mengi kama taathira ya ukoloni katika Afrika. Kwa baadhi ya wanahistoria kama vile Gann, Duignan, Perham na Lloyd taathira yake ama ilileta kheri au sana sana haikuidhuru Afrika. Wanahistoria wengine, wengi wakiwa wanazuoni Waafrika weusi na wanazuoni wa Kimarx, hasa wale wana nadharia za maendeleo na maendeleoduni hudai kwamba ukoloni haukuleta faida yoyote katika Afrika. Mwanahistoria mweusi wa Guyana, Walter Rodney, yeye amechukua msimamo tofatuti kabisa. Kwa mfano anadai:

> "Hoja inaashiria kwamba kwa upande mmoja kulikuwa na unyonyaji na unyanyasaji lakini kwa upande mwingine serikali zilifanya mengi kwa manufaa ya Waafrika na ziliendeleza Afrika. Maoni yetu ni kwamba hii kabisa si sahihi. Ukoloni ulikuwa na upande mmoja tu - ulikuwa ni chombo cha kuwanyonyea wananchi mali zao".

Hizo ndizo namna mbili za kutathmini ukoloni katika Afrika. Hata hivyo, kutokana na ushahidi uliopo, inaelekea kwamba kuna haja ya kutoa tathmini isiyo pendelevu; Hebu tuanze kwa kuweka urari wa mizania ya uwanja wa siasa tukianza kwanza na yale mambo chanya na kisha yale hasi.

Taathira katika upande wa Siasa

Taathira chanya ya kwanza ya kisiasa ilikuwa ni kule kuwepo, kwa kiwango kikubwa, kwa amani na utulivu wa muda mrefu baada ya kuimarishwa kwa ukoloni katika Afrika kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo. Kama tulivyokwishaona, katika Afrika, kama ilivyokuwa katika Ulaya, karne ya kumi na tisa ilikuwa ni kipindi cha mashuka na misukosuko ya kisiasa; kipindi cha *Mfacane*, cha *jihadi* za Wafulani; cha kuinukia kwa dola za Tukulor na Manden huko Sudani Magharibi; kipindi cha kuvunjika kwa dola za Oyo na Asante huko Afrika Magharibi hali iliyofanana na hali ya kipindi cha vita vya Napoleon; kipindi cha mapinduzi ya "usomi", cha vita vya muungano vya Wajerumani na vya Waitalia; kipindi cha maasi ya Wapoland na Wahungary; na kipindi cha ushindani cha kibeberu huko Ulaya ambao matokeo yake yalikuwa ni Vita vya Kwanza vya Dunia. Wakati tukikiri kwamba katika Afrika miongo miwili au mitatu ya kwanza ya enzi ya ukoloni (yaani kuanzia miaka ya 1880 hadi kwenye miaka ya 1910) ilizidisha hali ya wasiwasi, fujo, ghasia na, kama Caldwel alivyoonyesha, kuleta upungufu tukubwa wa idadi ya watu kwa kiwango kisichosameheka, hata zile shule zinazopinga ukoloni na zinazofuata siasa ya Ki-Marx zisingeweza kukana ukweli kwamba baada ya kuanzishwa kwa ukoloni na taratibu zake za utawala, vita kama vile vya kupanua maeneo na vya ukombozi vilikoma. Aidha sehemu nyingi za Afrika, hasa kuanzia mwishoni mwa Vita vya Kwanza vya Dunia zilikuwa na usalama na amani ya muda mrefu.

Taathira chanya ya pili ya kisiasa ni ile ya mgawanyo wa watu kijografia kama inavyoonekana katika nchi huru za Afrika hii leo. Kama alivyodokeza Afigbo hapo juu, kugawanya na kutamalaki bara hili kwa wakoloni kulikuwa na matokeo ya kuipa Afrika sura mpya ya mgawanyo wa kisiasa. Badala ya kuwepo mamia ya koo mbalimbali, makundi ya nasaba, miji-himaya, falme na dola zisizo na mipaka ya wazi, sasa kukawa na nchi mpya hamsini, mara nyingi zikiwa na mipaka dhahiri. Aidha ni muhimu kukumbuka kwamba mipaka ya nchi za Afrika iliyowekwa wakati wa ukoloni haijabadilika hadi hii leo.

Tatu, mfumo wa ukoloni ulileta, katika sehemu nyingi za Afrika, asasi mpya mbili ambazo nazo zimeendelea kutumiwa hata baada ya uhuru. Asasi hizo ni mfumo mpya wa mahakama na urasimu mpya. Ni dhahiri kabisa kwamba karibu kila nchi huru, tukiacha zile za Kiislamu, mfumo wa mahakama za juu ulioanzishwa na wakoloni bado unatumiwa. Utaratibu wa uongozi ulioanzishwa kwa ajili ya kuyatawala makoloni mbalimbali polepole ulianza kuzaa kundi la watumishi wa serikali, ingawa katika sehemu nyingi kundi hili lilijitokeza baadaye kabisa. Idadi ya watu wa kundi hili na athari yao vilizidi kuongezeka kadri miaka ilivyozidi kusonga mbele. Hapana shaka kwamba Waingereza waliyarithisha makoloni yao warasimu wengi zaidi, wenye uzoefu mwingi zaidi na waliopata mafunzo bora zaidi kuliko Wafaransa na hali ilikuwa mbaya zaidi katika makoloni ya Wabeligiji na Wareno.

Taathira chanya ya mwisho ya kisiasa haikuwa tu kuzaliwa kwa aina mpya ya

utaifa wa Kiafrika, kama Sithole na Oliver walivyoonyesha, bali pia kuzaliwa kwa umoja wa Waafrika wote ulimwenguni (Pan-Africanism). Utaifa wa Kiafrika, kama tulivyoona, ulikuwa na lengo la kuamsha hisia za watu wa aina mbalimbali katika mataifa mapya waweze kujitambua na kujibaini kama kundi moja au, kama ilivyo katika makoloni ya Wafaransa yaliyo Afrika Magharibi, fungu moja kubwa la makundi ya watu wamoja. Umoja wa Waafrika wote ulikuwa na lengo la kuwafanya Waafrika wote popote walipo ulimwenguni, wajihisi kuwa ni wamoja.

Lakini ni dhahiri kwamba kama kulikuwa na taathira chanya, kulikuwa pia na taathira hasi na ambazo ndizo zilizokuwa nyingi zaidi. Kwanza pamoja na kuwa maendeleo ya utaifa lilikuwa jambo zuri lakini ni jambo lililotokea kwa bahati tu na wala halikuwa matokeo ya hisia chanya za watu kujitambulisha na taifa jipya, kufungamana nalo au kujiwajibisha nalo. Kinyume na hayo wazo hili la utaifa ni matokeo hasi ya hasira, madhila na kunyanyaswa kulikotokana na baadhi ya hatua za ukandamizaji, ubaguzi, unyanyasaji na zilizotumiwa na watawala wa kikoloni. Kwa hiyo, baada ya kuondolewa kwa ukoloni, hali hiyo ilififia, na, kwa hakika, haina mashiko tena. Tatizo ambalo viongozi wa nchi huru wamekuwa wakikabiliana nalo ni jinsi ya kuzibadili hisia hizi hasi za utaifa ili ziwe chanya na za kudumu.

Pili, wakati tukikiri kwamba muundo mpya wa mgawanyo wa nchi uliotokana na kugawanywa kwa bara hili na wakoloni ulikuwa na faida kubwa, hatuna budi kukubali kuwa umeleta matatizo zaidi kuliko mema. La kwanza katika matatizo haya ni kwamba baadhi ya mipaka iliyowekwa inagawanaya makundi ya mbari, nchi na falme ambazo hapo mwanzo zilikuwa kitu kimoja. Kwa mfano, Bakongo wanajikuta wamegawanywa na mipaka ya Angola Kongo ya Wabelgiji, Kongo ya Wafaransa na Gabon. Leo hii baadhi ya Wa-Ewe wanaishi Ghana, wengine Togo na wengine Benin baadhi ya Wasomali wanaishi Ethiopia, wengine Kenya na wengine Somalia; Wasenufo wako Mali, Ivory Coast na Upper Volta. Kuna mifano mingine mingi zaidi. Hali hii haikuleta mvurugano tu bali pia imeleta migogoro mikubwa ya mipaka baina ya baadhi ya nchi huru za Kiafrika kama ile migogoro baina ya Sudani na Uganda, Somalia na Ethiopia, Kenya na Somalia na baina ya Ghana na Togo, Aidha kwa sababu mipaka hii haikufuata misingi yoyote maalumu kila moja ya nchi za Kiafrika ni mchanganyiko wa watu wenye tamaduni tofauti, mapokeo tofauti na lugha tofauti. Matatizo ya ujenzi wa taifa ambayo yanaletwa na mchanganyiko huu wa watu yameonekana kuwa magumu kutatuliwa.

Tokeo jingine la migawanyo hii ya kijuu, isiyokuwa na msingi na iliyofanywa na wakoloni, lilikuwa kwamba nchi zilizotokana na migawanyo hiyo zilikuwa na maeneo mbalimbali yenye viwango vya maliasili na uwezo wa kiuchumi visivyolingana. Wakati baadhi ya nchi hizi ni kubwa sana kama vile Sudan, Nigeria na Algeria tunakuta pia nchi nyingine ambazo ni ndogo sana kama vile Gambia, Lesotho, Togo na Burundi. Jambo la pili na ambalo ni baya zaidi ni kwamba wakati nchi nyingine zina pwani zenye urefu wa maili nyingi tu nyingine kama vile Mali, Upper Volta, Niger, Chad, Zambia, Uganda, Malawi, n.k. hazina hata maili moja ya upwa. Tatu,

wakati nchi nyingine kama Ghana, Zambia, Zaire, Ivory Coast na Nigeria zina utajiri mkubwa wa maliasili, nchi nyingine kama Chad, Niger na Upper Volta hazikupata bahati hiyo. Mwisho, wakati nchi nyingine kama Gambia zina mpaka mmoja tu wa kulinda amani nchi nyingine zina mipaka minne au zaidi, nyingine kama Zaire zina mipaka kumi, jambo ambalo linafanya iwe vigumu sana kulinda usalama na kuhakikisha kwamba mali ya nchi haitoroshwi kwenda nje. Si vigumu kuweza kufikiria matatizo yanayotokana na ukosefu wa uchache wa maliasili na kutokuwa na pwani katika nchi ambazo zilipata bahati mbaya kurithi hali hiyo.

Taathira nyingine ya ukoloni ambayo ni muhimu lakini ambayo pia ni hasi ni kule kudhoofishwa kwa mfumo wa kijadi wa serikali. Kwanza nchi nyingine za Afrika zilitwaliwa kutokna na kutamalaki na kuwanyang'anya utawala watawala wa jadi na kutokana na watawala hao kwenda ukimbizini, jambo ambalo, hapana shaka, lilileta kudharauliwa kwa utawala wa kichifu hasa katika kipindi kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Namna ambavyo watawala wa kikoloni waliwatumia watawala wa jadi kutekeleza mambo ambayo yalichukiwa na wananchi, kama vile ushokoa, ilizidi kufanya watawala hao wa jadi wazidi kudharauliwa. Aidha mfumo wa kikoloni wa mahakama ambapo watu waliweza kukata rufaa kwenye mahakama za kikoloni ulidhoofisha mamlaka na njia za watawala wa zamani za kujipatia fedha; isitoshe, kuenea kwa dini ya Kikristo kulizidi kuiangusha misingi ya imani zao za dini za jadi. Ni dhahiri kwamba mambo yote haya yalivunja mamlaka na hadhi ya mfumo wa kimapokeo wa serikali.

Taathira nyingine hasi ya ukoloni katika upande wa siasa ilikuwa ni kule kujenga katika Waafrika fikra kwamba mali ya serikali na ya umma havikuwa mali ya wananchi bali vilikuwa mali ya wakoloni watawala waliokuwepo wakati huo na kwamba inapaswa kutumiwa kwa faida ya binafsi kila nafasi inapotokea. Tabia hii ni zao la mfumo wa utawala wa kikoloni wa kuendesha mambo kisirisiri na kwa mbali; mfumo ambao uliwaondoa Waafrika, wenye elimu na wasio na elimu, katika nafasi yoyote ya kufanya maamuzi. Ni muhimu kukumbaka kwamba mwelekeo huu juu ya mali ya umma na serikali bado umo katika fikra za Waafrika wengi hata baada ya kupita miongo mingi ya uhuru; na kwa kiasi fulani hii ni sehemu ya sababu za matumizi mabaya ya mali ya serikali katika nchi nyingi za Afrika huru.

Zao la ukoloni ambalo mara nyingi halitiliwi maanani na wanahistoria wengi lakini ambalo limetokea kuwa muhimu sana - kama inavyodhihirika katika mchango wa Bett - lilikuwa ni kuanzishwa kwa jeshi la kudumu au lililowekwa tayari kwa vita. Jeshi la namna hii halikuweko katika sehemu nyingi za Afrika ambako wanaume wote, wakiwemo wale wa koo bora, walikuwa askari wakati wa vita na wakawa raia wa kawaida wakati wa amani. Mwanzo kabisa hayo yalianzishwa, mengi katika miaka ya 1880 na 1890, kwa madhumuni ya kutamalaki na kuitawala Afrika kisha wakatumiwa kwa madhumuni ya kuulinda utawala wa mkoloni na hatimaye yakatumiwa kwa kupigania vita vya dunia na kuvipiga vita vyama vya wapigania uhuru katika Afrika. Baada ya kuwaondoa wakoloni majeshi haya hayukuvunjwa bali yalichukuliwa na

watawala wa nchi hizo huru. Kama itakavyodhihirika katika juzuu linalofuata kutokana na kuingilia kwake siasa kwa mara kwa mara, na mara nyingi pasi na lazima wala misingi yoyote, majeshi haya yametokea kuwa vipingamizi vikubwa vya maendeleo ya nchi zake.

Taathira hasi ya mwisho ya ukoloni na ambayo pengine ilikuwa muhimu zaidi kuliko nyingine zote ilikuwa ni kupotea kwa utawala na uhuru wa Kiafrika ikiwa ni pamoja na kupotea kwa haki ya Waafrika kuyaumba maisha yao ya baadaye, kupanga maendeleo yao wenyewe, kuamua mikakati gani watumie na aula zao wenyewe; na mwisho kutokuwa na uhuru wa kuiga kutoka kwa watu wengine teknolojia ya kisiasa wanavyoona kuwa inawafaa. Kwa ufupi, ukoloni uliwanyima Waafrika mojawapo ya haki za msingi za binaadamu , haki ya uhuru.

Tena basi kipindi hiki cha miaka sabini ya ukoloni, kama alivyoonyesha Rodney, kilikuwa kipindi cha maendeleo makubwa na muhimu na mabadiliko katika nchi za kibepari na kisoshalisti. Kwa mfano, ilikuwa katika kipindi hiki Ulaya ilipoingia katika ulimwengu wa magari, eropleni na bomu la nuklia. Kama Afrika ingekuwa na mamlaka juu ya maisha yake ya baadaye nayo ingenufaika na hata kushiriki katika mabadiliko haya. Lakini ukoloni uliitenga kabisa Afrika na mabadiliko haya na ukaifanya ibakie katika hali ya kutegemea wengine.

## Taathira katika upande wa Uchumi

Ndiyo kusema, basi, taathira za kisiasa zilikuwa muhimu ingawa zilikuwa na namna tofautitofauti. Taathira nyingine muhimu, pengine muhimu zaidi kuliko za kisiasa, zilikuwa za kiuchumi. Taathira ya kwanza chanya ambayo ni dhahiri na muhimu kabisa, kama ilivyodhihirika katika sura nyingi zilizotangulia, ilikuwa ni kuanzishwa kwa muundombinu wa barabara, reli, simu na katika baadhi ya sehemu viwanja vya ndege. Hivi havikuweko Afrika katika kipindi kabla ya ukoloni. Kama Caldwell alivyoonyesha, hadi kufikia kipindi cha ukoloni "karibu kila usafiri wa nchi kavu ulikuwa wa uchukuzi uliofanywa na watu". Hadi kufikia miaka ya 1930 muundombinu huu wa msingi ulikwishawekwa katika Afrika; na tangu wakati huo hapajakuwapo na maendeleo makubwa, kwa mfano katika upande wa reli.

Taathira nyingine muhimu ilikuwa katika sekta ya msingi katika uchumi. Kila jitihada zilifanywa kuendeleza au kutumia baadhi ya maliasili maarufu katika bara hili; na, kwa hakika, kulikuwa na mafanikio makubwa katika suala hili. Ilikuwa katika kipindi cha ukoloni ambapo uwezekano mkubwa wa kupatikana madini katika Afrika ulipodhihirika na tasnia za migodi zikasitawi sana. Wakati huohuo kilimo cha mazao ya biashara kama kakao, kahawa, tumbaku, karanga, katani na mpira, kikaenea. Hapana shaka ni katika kipindi cha ukoloni ambapo Ghana ilitokea kuongoza ulimwengu katika uzalishaji wa kakao. Aidha, katika kipindi hichohicho hadi kufikia mwaka 1950, mazao ya shambani yalichukua asilimia hamsini ya bidhaa zote za French West Afrika.

Mapinduzi haya ya uchumi yalikuwa na athari kubwa. Kwanza, ilikuwa ni kuigeuza ardhi kuwa kitu cha biashara, hali ambayo iliifanya ardhi iwe raslimali kubwa. Pili, mapinduzi ya uchumi yaliwafanya baadhi ya Waafrika wawe na uwezo wa kununua vitu na hivyo ikasababisha kuwepo kwa mahitaji zaidi ya bidhaa za walaji na ubora wa hali za maisha. Tatu, kulima mazao ya biashara kuliwafanya baadhi ya Waafrika, hasa katika sehemu za vijijini, wapate mali bila kujali hadhi yao katika jamii.

Taathira nyingine ya kimapinduzi iliyotokana na ukombozi ilikuwa ni kuanzishwa kwa uchumi uliokitwa kwenye fedha katika sehemu nyingi za Afrika; uchumi ambao ulikuwa na athari za kuvutia. Kwanza, hata katika miaka ya 1930 kulikwishaanzishwa njia mpya ya kuthamini mali ambayo iligeuzwa si kwa kuangaliwa kiasi cha viazi vikuu alichokuwa nacho mtu au idadi ya kondoo au ng'ombe bali kwa kuangalia vitu hivyo vilikuwa na thamani gani kifedha. Pili, watu hawakujishughulisha tu na kazi za kuwapatia chakula bali pia walijishughulisha na kazi za kuwapatia fedha. Na kama itakavyodhihirika baadaye, hali hii ilisababisha kutokea kwa tabaka jipya la walipwa ujira na makundi ya walipwa mishahara. Tatu, kuanzishwa kwa uchumi wa kifedha kulileta kuauzishwa, kwa shughuli za Benki katika Afrika; shughuli ambazo, kwa hakika, ni sifa muhimu katika uchumi wa nchi huru za Afrika.

Kuanzishwa kwa malipo ya fedha na shughuli za benki zilizoandamana nayo pamoja na kupanaka sana kwa biashara baina ya Afrika ya mkoloni na Ulaya navyo hatimaye viliuingiza uchumi wa Afrika katika uchumi wa ulimwengu kwa ujumla na hasa katika uchumi wa kibepari wa serikali za kikoloni. Miaka iliyokuja baada ya 1935 ilizidisha tu huu uhusiano; na hata baada ya kupatikana uhuru uhusiano huu bado haujabadilika sana.

Je, ni kusema taathira za ukoloni katika uchumi zilikuwa za kuvutia sana? La hasha! Kinyume kabisa na fikra hizo matatizo mengi ya kimaendeleo yanayozikabili nchi za Kiafrika hii leo yametokana na taathira hizo.

Kwanza, kama alivyosema Kaniki hapo awali muundombinu uliowekwa na ukoloni haakuwa mtoshelevu wala wenye manufaa kama ilivyopaswa. Barabara nyingi na reli zilizojengwa hazikujengwa ili kufungua njia katika nchi, kuwezesha mawasiliano baina ya nchi na nchi au kukuza maendeleo ya jumla ya uchumi katika Afrika, hivi vilikuwa na lengo la kuyaunganisha na bahari maeneo yaliyokuwa na mashapo ya madini na yale yaliyokuwa na uwezekano wa kilimo cha mazao ya biashara. Pili, uchumi kama uliotokea katika makoloni ulikuwa umeegemezwa kwenye maliasili iliyokuwepo katika maeneo hayo. Hii ina maana kwamba maeneo ambayo hayakuwa na maliasili hayakushughulikiwa kabisa. Tatu, sifa kuu ya uchumi wa kikoloni ilikuwa ni kule kutojali kabisa au kukatisha tamaa, jitihada za uendelezaji wa viwanda na usindikaji nchini wa bidhaa kutoka katika malighafi na bidhaa za kilimo katika makoloni mengi. Kama alivyosema Fieldhouse, "penigne hakuna serikali ya kikoloni iliyokuwa na idara ya viwanda kabla ya 1945". Bidhaa ndogondogo lakini muhimu kama vile viberiti, mishumaa, mafuta ya kupikia, na hata maji ya machungwa na

ndimu, ambazo zingeweza kutengenezwa kwa urahisi humu humu Afrika, ziliagizwa kutoka nje. Kwa hiyo, kutokana na utaratibu wa kikoloni wa mfumo wa uchumi wa kibepari, nchi za Kiafrika zikageuka kuwa masoko tu ya bidhaa za nchi tawala na mahali pa kupatia malighafi. Nne, siyo tu kwamba uendelezaji wa viwanda haukutiliwa maanani bali pia hata zile tasnia na ufundi uliokuwepo Afrika kabla ya ukoloni karibu vyote viliangamizwa. Ni muhimu kusisitiza hapa kwamba tasnia za Afrika kabla ya ukoloni zilizalisha mahitaji yote ya Afrika kwa wakati huo. Hii ilikuwa ni pamoja na vitu kama vifaa vya ujenzi, sabuni, shanga, zana za chuma, vyombo vya ufinyanzi, na zaidi ya yote, nguo. Kama watengenezaji wa vitu hivi wangetiwa moyo na kuendelezwa kwa kufundishwa mbinu mpya za uzalishaji wa vitu hivi, kama ilivyofanywa katika India kati ya 1920 na 1945, Afrika isingekuwa imeongeza tu wingi wa bidhaa zake, bali pia ingeweza kuikuza taratibu teknolojia yake.Lakini ufundi huu pamoja na tasnia hizi karibu vyote viliangamizwa nchini kwa vitu vya bei nufuu vilivyotengenezwa kwa wingi katika nchi-tawala. Hivyo maendeleo ya teknolojia ya Afrika yakasimamishwa na hayakufufuliwa tena hadi baada ya uhuru.

Tano, ingawa baadaye katika nchi nyingi za Kiafrika mazao ya kilimo yalichukua sehemu kubwa ya njia za kupatia mapato, hakuna jitihada zozote zilizofanywa kuhakikisha kwamba uchumi wa kilimo katika makoloni hayo ulichepushwa. Kinyume na mategemeo hayo, kama lilivyokwishaonyeshwa katika baadhi ya sura zilizotangulia, hadi kufikia mwaka 1935, utaratibu uliokuwepo ulikuwa ni ule wa kulima zao moja au sana sana mawili ambayo yalikuwa na faida kubwa kibiashara - kakao katika Gold Coast, karanga katika Senegal na Gambia, pamba katika Sudan, kahawa katika Uganda, kahawa na katani katika Tanganyika, n.k. Tena basi, kutokana na kumakinika kwa mazao ya biashara wakati wa kipindi cha mkoloni, Waafrika walilazimika kutotilia mkazo uzalishaji wa mazao ya chakula chao wenyewe. Hivyo, ililazimu kwamba chakula kiagizwe kutoka nje, na ambacho watu wa hali ya chini walilazimika kununua, kwa bei kubwa. Ndiyo kusema basi, katika mfumo wa ukoloni, mara nyingi Waafrika walilazimika kuzalisha kile ambacho wao wenyewe hawakutumia na wakatumia kile ambacho wao wenyewe hawakuzalisha - hali ambayo inadhihirisha hali inayolingana na ya unyonyaji, ya uchumi wa kikoloni.

Sita, kule kugeuzwa kwa ardhi kuwa kitu cha kibiashara kulileta uuzaji haramu wa ardhi ya jumuiya uliofanywa na wakuu wa familia wenye tamaa na kukaleta kuongezeka kwa mashtaka ya madai juu ya ardhi, hali ambayo ilileta kuenea kwa ufukara, hasa katika koo za kitawala. Kama ilivyokwishadhihirika katika sura zilizotangulia katika sehemu za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika hali hiyo pia ilisababisha kutwaliwa kwa sehemu kubwa za ardhi na Wazungu - kitendo ambacho kilileta uchungu, hasira na kuwatafirisha sana wenyeji wa sehemu hizo. Hii ikawa sababu kubwa na chanzo cha mlipuko uliotokea Kenya na uliojulikana kama MauMau.

Kama tulivyokwishasema, kuwepo kwa ukoloni hapa Afrika pia kukaleta mfumo wa benki za kigeni, usafirishaji kwa njia ya meli, mashirika na makampuni ya biashara ambayo baada ya mwaka 1910 yaliungana na kufanya mashirika na makampuni ya

watu wachache tu walioyahodhi. Kwa kuwa makampuni haya ya biashara ndiyo yaliyodhibiti mali iliyoingia nchini na iliyosafirishwa nje na ndiyo yalipanga bei za bidhaa zote (zile zilizoingizwa na zile zilizosafirishwa nje na Waafrika), wenye makampuni hayo ndio waliopata faida kubwa kubwa kutokana na biashara hizi, siyo Waafrika. Ni wazi kwamba matokeo mengine ya hali hii yalikuwa ni kuwaondoa kabisa Waafrika katika sekta za uchumi zilizokuwa na faida kubwa kubwa. Kwa hiyo, matajiri wa Kiafrika wa nusu ya pili ya karne ya 19 karibu wote walitoweka katika mandhari ya ufanyibiashara katika kipindi hiki tukichunguzacho. Vikao vyao vilivyofuata vikawa vya kuajiriwa na makampuni na mashirika ya wageni ili kuweza kuishi.

Kama alivyosema Rodney, ukoloni pia karibu uliondoa kabisa biashara kati ya mataifa ya Kiafrika. Kabla ya ukoloni kulikuwa na biashara nyingi kati ya mataifa ya Kiafrika. Wakati huu kulikuwa na shughuli nyingi za biashara za masafa marefu na misafara, sifa ya kawaida sana katika uchumi wa Kiafrika kwa wakati huo. Lakini baada ya kuanzishwa kwa ukoloni biashara hizo za masafa marefu na mafupi kati ya mataifa ya Kiafrika zilipunguzwa tamaa na mara nyingi zilipigwa marufuku. Hii ilizuia kuimarisha mahusiano yaliyokuwepo hapo zamani, au kuanzishwa kwa mahusiano mapya, ambayo yangeweza kuwa yenye manufaa kwa Waafrika.

Mwisho, maendeleo yoyote ya uchumi yaliyopatikana wakati wa kipindi cha mkoloni hayakuwa ya kawaida wala hayakuwa ya haki kwani yaliandamana na watu kulazimishwa kuwafanyia kazi wakoloni, kulazimishwa kulima mazao fulani tu, kunyang'anywa ardhi, kulazimishwa kuhamia kwenye sehemu wasizopenda na matokeo yake yakawa kutanguka kwa maisha ya kifamilia, kuanzishwa utaratibu wa kuwa na pasi, vifo vingi katika migodi na mashamba, n.k. Zaidi ya hayo, sera za fedha zilizotumiwa na serikali za wakoloni katika makoloni yao kuhakikisha kuwa fedha zilizotumiwa katika makoloni ziligezwa kwenye fedha za serikali za wakoloni hao na kwamba mapato yote ya fedha za kigeni yalihifadhiwa katika miji mikuu ya nchi-mama na wakati huohuo wakihakikisha kuwa ubadilishaji wa fedha (ulikuwa Mwafrika) zilizosababisha mali zibakie katika miji mikubwa ya nchi -mama badala ya kutumiwa kama vitegauchumi katika makoloni yao. Kuhamishwa Ulaya kwa akiba za Waafrika kulikofanywa na benki na ubaguzi uliofanywa dhidi ya Waafrika katika kutoa mikopo ulizidi kuwa kipingamizi katika maendeleo ya Kiafrika.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa hapo awali tunaweza kusema pasi na kusita kuwa kipindi cha ukoloni kilikuwa kipindi cha unyonyaji wa kikatili wa uchumi kuliko kuwa kipindi cha maendeleo ya uchumi wa Afrika, ingawa watu kama Gann Duigna na Duignan wanaipinga fikra hii.

Taathira katika Masuala ya Kijamii

Mwisho, kuna rekodi gani za ukoloni katika upande wa masilahi ya kijamii? Taathira ya kwanza ya kijamii ambayo ni muhimu na yenye manufaa ilikuwa ni ongezeko la

idadi ya watu katika Afrika kipindi hiki. Kama Caldwell alivyoonyesha, ongezeko hili lilikuwa takriban 37.5%, baada ya kupungua kwake katika miongo miwili au mitatu ya kwanza ya ukoloni.

Taathira ya pili ya kijamii, ambayo inahusiana sana na hiyo ya kwanza, ilikuwa ni ujenzi wa miji. Kama alivyosisitiza Afigbo, ujenzi wa miji si jambo ambalo halikuwapo katika Afrika kabla ya ukoloni. Lakini hapana shaka kwamba kutokana na ukoloni kasi ya ujenzi wa miji iliongezeka sana,. Miji mipya kabisa kama vile Abidjan katika Ivory Coast, Takoradi katika Gold Coast, Port Harcourt na Enugu katika Nigeria, Nairobi katika Kenya, Salisbury katika Southern Rhodesia na Luluaborg katika Belgian Congo ikajengwa.

Aidha, kama ambavyo Caldwell ameonyesha, idadi ya watu katika miji iliyokuwepo na ile mipya iliongezeka kwa haraka sana katika kipindi cha ukoloni. Idadi ya watu katika Nairobi, mji ambao ulianzishwa katika 1896 kama kituo cha watu na vifaa vya kujengea reli ya Uganda, iliongezeka kutoka wachache tu hadi kufikia watu 13, 145 katika mwaka 1929 na kufikia watu zaidi ya 25,000 katika 1940. Idadi ya watu katika Casablanca iliongezeka toka 2,026 katika 1910 na kufikia 250,000 katika 1936; na ile ya Accra katika Gold Coast ikaongezeka toka 17,892 katika 1910 na kufikia 135,926 katika 1948. Miji hii ilikua haraka sana katika kipindi hiki kwa sababu ama ilikuwa miji mikuu mipya au vituo vya utawala katika utawala wa kikoloni, au ilikuwa bandari mpya na stesheni za reli.

Hapana shaka palikuwa pia na maisha bora zaidi hasa kwa wale walioishi mijini. Na hii, kama alivyoonyesha Caldwell, ndiyo iliyosababisha kuwepo kwa hospitali, zahanati, maji ya bomba na vifaa vingine vya kiafya, na ongezeko katika nafasi za ajira.

Kuenea kwa Ukristo, Uislamu na elimu ya kimagharibi vilikuwa ni athari nyingine muhimu ya ukoloni. Hakuna shaka kwamba kwa kutumia hali ya amani na utulivu iliyokuwepo, fadhila, na katika sehemu nyingine mshawasha chanya uliotolewa na ukoloni, wamisionari na wahubiri wa dini ya Kiislamu waliweza kuingiza shughuli zao ndani zaidi katika bara hili. Kama ambavyo Asare Opoku ameonyesha katika sura aliyoandika, Ukristo na Uislamu vilipata mashiko zaidi katika kipindi cha ukoloni kuliko ilivyokuwa katika karne tatu au nne zilizotangulia, kwa pamoja.

Jambo moja ambalo lilihusiana sana na kuenea kwa Ukristo ni elimu ya kimagharibi. Kama ilivyokwishaonyeshwa katika sura nyingi misioni za Kikristo ndizo hasa zilizohusika na jambo hili. Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kwamba wamisionari hawa waliweza kuendesha shughuli zao hasa kutokana na misaada waliyopata kutoka katika tawala za kikoloni . Kuenea kwa elimu ya kimagharibi kulikuwa na athari nyingi sana za kijamii. Mojawapo ya athari hizi ni kuongezeka kwa tabaka bora la Waafrika wenye elimu ya kimagharibi, tabaka ambalo leo hii ndilo linalomiiliki kazi za serikali katika nchi za Kiafrika.

Taathira nyingine muhimu ya kikoloni, ambayo kama itakavyoonyeshwa hapo baadaye ni mchanganyiko wa uzuri na ubaya, ilikuwa ni kuanzishwa kwa lugha ya

mawasiliano (*lingua franca*) katika kila koloni au katika makoloni kadhaa. Katika makoloni yote, lugha ya kwanza ya taifa linalotawala koloni hilo, iwe katika mfumo wake halisi au katika pijini, ikawa ndiyo lugha ya shughuli za kikazi na lugha rasmi. Mara nyingi lugha hiyo pia ndiyo iliyokuwa lugha muhimu ya mawasiliano kati ya watu mbalimbali wenye lugha zao katika koloni hilo. Ni muhimu kutambua kwamba tukiacha Afrika Kaskazini, Tanzania, Kenya na Madagascar, lugha hizi za kigeni zimeendelea kuwa lugha rasmi hadi hii leo.

Taathira ya mwisho ya kijamii ambayo ilikuwa na manufaa ilikuwa ni ile muundo mpya wa kijamii ambao ukoloni uliuanzisha katika baadhi ya sehemu katika Afrika au ambao maendeleo yake yaliharakishwa na ukoloni katika sehemu nyingine. Utaratibu mpya wa kikoloni pamoja na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ambayo yamekwishachambuliwa k.v. kuondolewa kwa utumwa, kuanzishwa kwa elimu ya kimagharibi, kupanuliwa kwa kilimo cha mazao ya biashara na ujenzi wa miji, vilibadili vikubwa muundo wa kijamii wa kimapokeo. Hivyo, hadi kufikia miaka ya 1930 mahali pa tabaka ya kijamii za kabla ya ukoloni (koo bora zilizotawala, watu wa kawaida, watumwa wa nyumbani na sehemu kidogo ya watu wa koo bora waliosoma) palichukuliwa na jamii mpya ambayo iligawanyika kwa wazi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali katika makundi mawili - wakazi wa mijini na wakazi wa vijijini; makundi ambayo ndani mwake mlikuwa na matabaka mbalimbali. Wakazi wa mijini waligawanyika katika makundi madogo matatu: kundi la watu bora au mabwanyenye wakiwemo wanasheria, madaktari na wafanyakazi wa serikali; kundi la watu wa kawaida wakiwemo makarani, walimu na wauguzi; kundi la makabwela wa mijini wakiwemo wafanyakazi wa ujira, madereva, makanika, mafundi cherehani, n.k. Katika sehemu za vijijini kwa mara ya kwanza, katika sehemu nyingi za Afrika, kukatokea matabaka mapya:makabwela wa vijijini au Waafrika wasiokuwa na ardhi na wukulima wadogowadogo. Kundi la kwanza lilikuwa ni la Waafrika ambao ardhi yao ilichukuliwa na Wazungu, hasa katika Afrika Mashariki na Kusini, na kwa hiyo wakalazimika kuishi maisha ya kuabiri mijini na vijijini, zaidi wakiwa ni vibaraka wahamaji. Wukulima wadogowadogo walikuwa wale walioishi katika vikundi vidogovidogo wakilima ardhi waliyomiliki, na wakitegemea zaidi wafanyakazi wa familia zao wenyewe. Yabidi tusisitize kwamba kwa kuwa katika muundo huu mpya uendaji huku na huko ulitegemea zaidi juhudi za mtu binafsi na mapato kuliko kutegemea kuzaliwa kwa mtu, hii ilikuwa hatua kubwa ya kuubadili muundo wa kijamii wa kimapokeo.

Lakini kama ukoloni ulileta athari chanya za kijamii ni dhahiri kwamba ulileta pia athari hasi, na baadhi zikiwa hasi sana. Ya kwanza katika hizo ilikuwa kuanzishwa kwa pengo kubwa baina ya vituo vya miji na vya vijiji. Ongezeko kubwa la idadi ya watu wa mijini tulililoliona halikutokana na ongezeko la kawaida la idadi ya watu mijini, bali lilitokana na kututwa kwa vijana wa kiume na kike na vituo vya miji katika jitihada zao za kutafuta elimu, kazi na huduma nyingine za kijamii; na kama Coquery-Videovitch alivyoonyesha, ongezeko hili la watu mijini pia lilitokana na watu

kuvikimbia vijiji kwa sababu ya njaa, magonjwa ya kuambukiza, ufukara, kodi na ukosefu wa mambo ya kuvutia. Ni muhimu kutambua kwamba pengo hili mpaka sasa bado halijazibwa. Wala isichukuliwe kwamba wahamaji hawa waliyakuta maisha ya mijini yakiwa yenye raha na furaha kama walivyotegemea. Wengi wao walijikuta wanaishi katika msongamano katika viunga vya miji na miji midogo ya vibandavibanda ambako kulijaa ghasia za vijana, ulevi, umalaya, uhalifu na ambako hapakuwa na kazi za kuajiriwa.

Hiba ya pili ya kijamii ambayo imekuwa na athari kubwa sana ni tatizo la ulowezi wa Wazungu na Waasia. Ingawa kulikuwa na masetla wa Kizungu katika nchi za kaskazini mwa Afrika na Afrika kabla ya kipindi cha ukoloni lakini katika kipindi cha ukoloni idadi yao iliongezeka na kukaanzishwa masetla wa Kizungu na Kiasia katika Afrika Mashariki na Kati na baadhi ya sehemu za Afrika Magharibi kama ambavyo Kaniki ameonyesha kuwa idadi ya Wazungu katika Kenya iliongezeka toka watu 596 katika 1903 na kufikia 954 katika 1911 hadi kufikia zaidi ya 35,000 katika 1926, na katika Algeria idadi ikaongezeka toka 344,000 katika 1876 hadi kufikia 946,000 mnamo 1936. Lakini katika sehemu nyingi za Afrika Mashariki, Kati na Kaskazini kilichofanya masetla kuchukiwa sana na Waafrika, ni kwamba Wazungu walichukua ile ardhi iliyokuwa na rutuba, na pia katika sehemu hizi na zile za Afrika Magharibi Waasia walihodhi biashara za jumla. Hadi kufikia 1935 tatizo hili la Wazungu na Waasia lilikwishaleta migawanyo mikubwa ya uwiano wa mali na wala halijaweza kutatuliwa kabisa hadi hii leo.

Zaidi ya hayo, ingawa kama tulivyokwishaona, ukoloni ulianzisha huduma za jamii, shurti isisitizwe kwamba huduma hizi zilikuwa hazitoshelezi kabisa na hazikuwa zimegawanywa sawa kwa makoloni yote. Tena basi, huduma hizo ziliakiliwa kuwanufaisha zaidi masetla weupe na watawala. Ndiyo maana huduma hizo zilipatikana zaidi mijini.

Kwa upande wa elimu, elimu iliyotolewa katika enzi za mkoloni kwanza ilikuwa haitoshelezi kabisa, haikutolewa kwa viwango sawa katika makoloni yote ua ilikuwa na mwelekeo mbaya. Kwa hiyo, haikuwa na manufaa kwa Afrika kama ambavyo ingepaswa kuwa. Ingawa hadi kufikia miaka ya 1930 kulikwishaanzishwa shule nyingi za msingi katika nchi nyingi za Afrika, kulikuwa na shule chache sana za sekondari, ufundi na vyuo vya ualimu, na takribani hapakuwa na vyuo vikuu vyovyote. Katika sehemu nyingi za Afrika shule za ufundi na vyuo vikuu vilianzishwa baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Tena basi, si tu kwamba asasi hizi hazikugawanywa sawa katika makoloni yote, bali pia mitaala iliyotumiwa na asasi hizi zote ilifuata modeli za nchi mama za makoloni hayo (wakati mwingine mitaala ya nchi mama ikichukuliwa moja kwa moja kama zilivyokuwa huko Ulaya) hata japokuwa asasi hizo zilitakiwa kushughulikia mahitaji ya Afrika!

Athari ya elimu ya kikoloni katika jamii za Kiafrika imekuwa kubwa na karibu ni ya kudumu. Pili, tabaka bora la wasomi lililotokana na elimu hii lilikuwa na mgeuko, tabaka ambalo liliona fahari kuiga utamaduni na ustaarabu wa Kizungu na kudharau

utamaduni wa Kiafrika. Hivyo kukawa pia na pengo jingine kati ya tabaka la wasomi hawa na umma uliobakia; pengo ambalo nalo halijaweza kuzibwa. Aidha, kuvieleza vitu kama kifo, mvua na maradhi kauka mtazamo wa kisayansi pia kuliathiri vibaya misingi ya imani za kidini za Kiafrika, miiko na taratibu za kumwadhibu mtu alipokiuka matarajio ya jamii na kwa hiyo kulisukasuka misingi ya jamii za Kiafrika na kuleta hali ya wasiwasi, tafrani na kutokuwa na hakika na amani.

Kutotilia maanani elimu ya ufundi na viwanda na kusisitiza masomo ya fani za jamii na ukarani, na kwa hiyo kupendelea kazi za ofisini, pia kuliwafanya wale waliosoma wazidharau kazi za mikono na kilimo, athari ambayo bado tunayo hii leo.

Ingawa kuwepo kwa lugha ya mawasiliano (lingua franca) kulikokuzwa na kuendeleza kupitia mfumo wa elimu lilikuwa jambo zuri, lakini nako kulikuwa na athari mbaya ya kuzuia kukua na kuendelea kwa baadhi ya lugha za kienyeji hadi kufikia kuwa lugha za taifa au lugha za mawasiliano. Kwa mfano, Twi, Hausa na Kiswahili zingeweza, kwa urahisi kabisa kuendelezwa na kufanywa lugha za taifa za Gold Coast, (Twi) Nigeria (Hausa), na Afrika Mashariki (Kiswahili). Lakini watawala wa kikoloni walizikatisha tamaa jitihada za kuendelezwa kwa lugha hizo na katika nchi nyingine kama vile Uganda zilizuiwa kabisa.

Athari nyingine ya kusikitisha iliyotokana na ukoloni ilikuwa ni kule kuendeleza kudhalilishwa kwa hali ya mwanamke katika Afrika. Ni dhahiri kwamba hii ni dhamira mpya inayohitaji utafiti zaidi, lakini haielekei kuwepo na shaka kwamba wanawake hawakuruhusiwa kujiingiza katika shughuli zilizoanzishwa au zilizoendelezwa na kuimarishwa na ukoloni, kama vile elimu ya Kimagharibi, kilimo cha mazao ya biashara katika baadhi ya sehemu za Afrika, kazi nyingi za kitaalamu kama vile uganga na sheria. Kama Iliffe alivyosema, ulimwengu wa ukoloni ulikuwa ulimwengu wa mwanamume, na wanawake hawakushawishiwa kuchukua nafasi yoyote muhimu katika ulimwengu huo.

Tena basi, kutokana na ukoloni, Mwafrika mwenyewe alidharauliwa, akanyanyaswa, na akabaguliwa waziwazi na kisirisiri. Ubaguzi huu wa rangi ambao ulivuma kwa nguvu sana katika kipindi cha ukoloni pia uliwafanya baadhi ya Waafrika wajihisi kuwa dhalili, hali ambayo haijaweza kutoweka kabisa hata baada ya kupita miongo miwili ya uhuru.

Mbaya zaidi ilikuwa ni athari ya ukoloni katika upande wa utamaduni. Wazungu waliokuja Afrika katika kipindi hiki, hasa kati ya 1900-1945 - wamisionari, wafanyabiashara, masetla, wahandisi na wachimba migodi, wote mara nyingi walijaa majivuno ya kujiona bora kuliko utamaduni na rangi ya Mwafrika. Kwa hiyo, walilaani kila kitu kilichokuwa cha Mwafrika - muziki wa Kiafrika, sanaa, dansi, majina, dini, ndoa, mifumo ya mirathi, n.k. Ili kuruhusiwa kuwa Mkristo, Mwafrika alilazimika si kubatizwa tu, bali pia kibadili jina lake na kukataa mambo mengine yote ya Kiafrika yaliyotajwa. Kwa hiyo, ukoloni ulidumaza maendeleo ya utamaduni, kama siyo kuyarudisha nyuma kabisa.

Kutokana na uchanganuzi huo, itadhihirika kuwa wale wanazuoni wanaofikiri

kuwa ukoloni ulikuwa janga baya sana kwa Afrika na kwamba haukuleta kitu kingine isipokuwa kutokuendelea na kubakia nyuma, wamekwenda mbali mno! Halikadhalika wale wenye kutetea ukoloni kama vile akina Gann, Duignan na Lilod, ambao wanauona ukoloni kama baraka kubwa sana kwa Afrika nao wamekwenda mbali mno! Kwa maoni ya mwandishi wa makala haya, uamuzi ambao ni sahihi zaidi katika suala hili siyo ule unaosema kwamba ukoloni haukuleta jambo lolote chanya kwa Afrika, bali ule unaoona kwamba kutokana na nafasi uliyokuwa nayo, amali zake, nguvu na athari ulizoleta katika Afrika ukoloni ungeweza na ulitakiwa kufanya mema zaidi kuliko ulivyofanya. Zaidi ya hayo kipengele cha unyonyaji wa uchumi katika kipindi chote cha ukoloni kilichukua sehemu kubwa zaidi kuliko kile cha maendeleo ya uchumi. Ni kutokana na sababu hizi mbili kwamba kipindi cha ukoloni huingia katika historia kama kipindi cha kukua bila maendeleo, kipindi cha nafasi za kujiendeleza zilizopotea na kipindi cha unyanyasaji wa watu wa Afrika.

## *Umuhimu wa Ukoloni katika Afrika*

Hayo tuliyokwishaona yanatufikisha kwenye swali la pili tulilojiuliza mwanzoni mwa sura hii, yaani umuhimu wa nyuma wa ukoloni katika Afrika. Je, ukoloni uliitenganisha Afrika ya nyuma na Afrika ya baada ya ukoloni au ulikuwa ni sehemu mojawapo tu katika historia ya bara hili ambayo ina umuhimu mkubwa na ambayo haikuathiri maendeleo ya baadaye ya Afrika? Hapa pia yamewahi kutolewa majibu yenye kupingana. Baadhi ya wanahistoria, ambao kwa hakika ndio kundi kubwa, ikiwa ni pamoja na wale wafuasi wa Marx na wananadharia wa nadharia za maendeleo na maendeleoduni, (kwa sababu tofauti kabisa) wanafikiri kwamba ingawa ukoloni ulichukua kipindi kifupi tu kilichongia kati, lakini ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa Afrika na uliacha alama isiyofutika. Kama wanavyodai Oliver na Atmore: "Kikipimwa katika skeli ya wakati wa kihistoria kipindi cha ukoloni kilikuwa kipindi kifupi tu kilichoingia kati (ya historia ya bara hili). Lakini kilikuwa kipindi ambacho kiliathiri vikubwa mwelekeo na nguvu mpya katika historia ya Afrika". Gann na Dunigan pia wanauona ukoloni kama kitu ambacho "kiliathiri sana hali ya baadaye ya Afrika". Jibu la wafuasi wa Marx na wananadharia wa maendeleoduni linapatikana kwa muhtasari unaojitokeza katika jina la kitabu cha Rodney kiitwacho: *How Eutope Underdeveloped Africa* (Jinsi Ulaya ilivyoleta maendeleo duni katika Afrika). Hata hivyo, kuna baadhi ya watu ambao wanaiona athari ya ukoloni kama kitu ambacho hakikuathiri sana Afrika na kwamba ukoloni haukuitenganisha Afrika ya kabla ya ukoloni na Afrika baada ya ukoloni. Katika mfululizo wa makala kadhaa, Ajayi amekuwa akidai kuwa ukoloni "huwakilisha tu tukio moja katika historia ndefu na yenye matukio mengi na wala haukuukatisha mwendeleo wa historia hiyo.

Kwa maoni ya mwandishi wa makala haya hakuna jibu rahisi la ndiyo au hapana la swali hili kwani athari ya ukoloni ilitafautiana toka sehemu moja hadi nyingine na kutoka dhamira moja hadi nyingine. Hapana shaka kwamba kwa upande

wa uchumi athari ya ukoloni ilikuwa kubwa na iliathiri sehemu za mijini na vijijini. Karibu katika kila sehemu katika Afrika kufikia mwisho wa ukoloni, uchumi wa fedha ndio uliokuwa uchumi wa kawaida na hata katika sehemu za vijijini hadhi ya mtu ilipimwa si kwa kufuata ukoo tu, bali pia kwa kuangalia kiasi cha fedha alichokuwa nacho na wingi wa mazao ya biashara ambayo mtu alikuwa akipata katika kila msimu. Aidha, kutokana na kuanzishwa kwa mazao ya biashara (fedha), ardhi ikapata thamani ambayo haikuwa nayo kabla ya ukoloni na wakati huo huo, jitihada na mapato ya mtu binafsi vikatiliwa mkazo zaidi kuliko ule utaratibu wa ujima wa kimapokeo. Uchumi wa Kiafrika nao akawa sehemu ya uchumi wa ulimwengu kwa ujumla na zaidi hasa akawa uchumi wa kibepari kuliko ulivyokuwa hapo awali. Hali hii ilileta athari ambazo pengine itakuwa vigumu kuziondoa.

Athari nyingine ya ukoloni-kubwa, ya kudumu na ambayo inawathiri watu wote wa jamii ni, athari ya upande wa siasa. Kama tulivyokwishaona nchi huru za Afrika zilizoko hii leo ni zao la ukoloni. Kutokana na kukubaliwa kwa kulheshimu mipaka ya nchi kulikofikiwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika (O.A.U.), haielekei kwamba sura hii itabadilishwa. Pili, hata japokuwa uhuru umepatikana, hapana shaka kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa na ya kudumu katika nguvu na mamlaka ya kisiasa, kutoka katika tabaka bora la kimapokeo la wafalme, malkia, familia, koo na viongozi wa kidini na kwenda katika tabaka bora jipya au watu wa matabaka ya juu na ya kati na kuanzishwa kwa mfumo wa kikoloni. Hali hii haitaweza kamwe kugeuzwa tena. Tatu, ukoloni ndio uliozaa utaifa wa Kiafrika. Nao, ni ule urithi muhimu wa ukoloni, yaani jeshi la kudumu ambalo haielekei kama litaondolewa; na kama itakavyodhihirika katika juzuu linalofuata jeshi la kudumu tayari limeishabadilisha mwelekeo wa historia ya nchi nyingine za Afrika na inaelekea kana kwamba bado halijamaliza jukumu lake la kisiasa. Mwisho inaelekea kwamba asasi za mambo ya sheria na siasa – mahakama, mabunge, wakuu wa wilaya na mikoa, n.k. zitaendelea kuwapo ingawa mabadiliko madogomadogo yamefanywa na yataendelea kufanywa. Pengine tunaweza kusema kwamba athari ya ukoloni katika upande wa siasa ilikuwa kubwa zaidi na kwa sehemu kubwa imekuwa ya kudumu zaidi kuliko ilivyokuwa katika upande wa uchumi.

Kwa upande mwingine tunaona kwamba katika mambo ya utamaduni na ya kijamii athari ya ukoloni haikuwa kubwa sana wala haikuwa ya kudumu. Mabadiliko yaliyoletwa katika utamaduni, ubaguzi uliokuwa ukifanywa na kulaani na kudharau utamaduni wa Kiafrika kulikokuwa kunafanywa katika siku za ustawi wa ukoloni, zaidi vilikuwa tu katika sehemu za mwambao na mijini, havikuingia na kupenya katika sehemu za vijijini. Dansi za Kiaftika, muziki na mifumo ya kimapokeo ya dini viliendelea kuwepo. Mambo yaliyoigwa au kuazimwa hayakuwa teuzi tu, bali pia, kama alivyosema Herak'vits,' yalikuwa ni nyongeza na wala si lazima kwamba yalikuwa vibadala. Ndiyo maana katika sehemu za vijijini, na kwa kiasi fulani mijini, imani mpya, miungu wapya, vyombo vipya, kazi mpya za usanii na vitu vipya viliongezewa kwenye vile vya zamani. Muhimu zaidi ni kwamba katika upande wa

utamaduni ule msingi uliokuwa umepotea, hata katika sehemu za miji umepatikana tena. Leo hii sanaa na kazi nyingine za Kiafrika kama vile dansi na muziki siyo tu kwamba vinafundishwa katika asasi mbalimbali za elimu, lakini pia sasa mambo haya yameenea sana katika Afrika na yanaanza kutambuliwa huko Ulaya. Ndiyo kusema, mintarafu upande wa utamaduni ni dhahiri kwamba ukoloni ulikuwa tukio mojawapo tu na athari yake haikuwa na mashiko.

Mwisho, kwa upande wa mambo ya kijamii, umuhimu wa ukoloni uko katika hali ya mchanganyiko. Kwa upande mmoja, lugha za kigeni za mawasiliano (*Lingua frncae*) zitaendelea kuwapo kwa muda mrefu sana, kama siyo daima dumu. Pili, matabaka mapya yaliyoletwa na ukoloni yataendelea kuwapo na hata yanaweza kuwa changamano zaidi. Mpaka sasa, makundi mawili mapya yamekwishaongezwa tokea kupatikana kwa uhuru. Kundi la kwanza ni lile kundi bora la wanasiasa ambalo lina wanasiasa wa daraja za juu katika vyama vya siasa ambayo vimekuwa vikijitokeza kwa wingi katika Afrika na ambao wamekuwa mawaziri wakau, marais, mawaziri, mabalozi, n.k. Kundi la pili ni lile kundi bora la wanajeshi ambalo hujumnisha maofia wa sasa na wa zamani wa kijeshi katika kila nchi huru. Kwa vyovyote vile wale waliomo katika makundi haya bora wanatofautiana sana na wengine katika mavazi, maisha, mambo wanayopendelea na katika hadhi. Ingekuwa matabaka haya bora yamechukua asilimia kubwa ya idadi ya watu katika Afrika, tungeweza kukubali kwamba kuundwa kwake kulikuwa ni badiliko jingine kubwa na muhimu lililoletwa na wakoloni. Lakini watu wa mijini au makundi mengine ya watu bora yaliyojitokeza mwishoni mwa ukoloni ni sehemu ndogo tu ya idadi ya watu katika Afrika, sana sana hawazidi asilimia 20. Kwa wakazi waliobaki wa vijijini ambaowalibakia bila elimu, wakabakia na imani zao za kimapokeo, mali zao na viwango vyao, ndio wanaochukua sehemu kubwa ya watuwote katika kila taifa la Afrika. Tunaweza kuhitimisha kwamba athari ya ukoloni katika upande huu ilikuwa kidogo sana.

Kwa kuhitimisha basi, tunaweza kusema kuwa ingawa ukoloni ulikuwa ni tukio mojawapo tu katika historia ya Afrika, ukiwa umedumu kwa muda usiozidi miaka themanini, hata hivyo, ulikuwa tukio muhimu sana kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ukoloni ulikuwa mwanzo wa mabadiliko katika historia ya Afrika na maendeleo yake ya baadaye; kwa hiyo historia ya bara hili imeathiriwa na itaendelea kuathiriwa na athari za ukoloni. Kutokana na hali hii, historia ya Afrika imelazimika kufuata mwelekeo mwingine kuliko ule ambao ingefuata kama pasingekuwepo na kuingilia kati kwa ukoloni.

# *BIBLIOGRAFIA*

**'Abd al-Rahim, M.** (1986) *Imperialism and Nationalism in the Sudan: a Study in Constitutional and Political Development, 1899-1956* (Khartoum: Khartoum University Press)

**Abraham, A.** (1978) *Mende Government and Politics under Colonial Rule: a Historical Study of Political Change in Sierra Leone 1890-1937* (Freetown: Sierra Leone University Press)

**Adam, F.** (1978) *The Kano Civil War and British Over-rule 1882-1940* (Oxford University Press)

**Adeleye, R. A.** (1971) *Power and Diplomacy in Northern Nigeria, 1804-1906: the Sokoto Caliphate and its Enemies* (London: Longman)

**Afigbo, A. E.** (1972) *The Warrant Chiefs: Indirect Rule in South eastern Nigeria, 1891-1929* (London: Longman)

**Ageron, C. R.** (1978) *Politiques coloniales au Maghreb* (Paris: Presses Universitaires Françaises)

**Ahmed, J. M.** (1960) *The Intellectual Origins of Egyptian Nationalism* (London: Oxford University Press)

**Ajayi, J. F. A.** (1965) *Christian Missions in Nigeria, 1841-1891: the Making of a New Elite* (London: Longman)

**Ajayi, J. F. A.** na **Crowder, M.** (wah.) (1974) *History of West Africa,* Juz. II (London: Longman)

**Ajayi, J. F. A.** na **Crowder, M.** (wah.) (1985) *Hisorical Atlas of Africa* (Harlow and Nigeria: Longman)

**Amin, S.** (1970) *The Maghreb in the Modern World: Algeria, Tunisia, Morocco* (Harmondsworth: Penguin)

**Arhin, K.** (mh.) (1985) *West African Colonial Civil Servants in the Nineteenth Century: African Participation in British Colonial Expansion in West Africa* (Leiden: African Studies Centre)

**Asante, S. K. B.** (1977) *Pan-African Protest: West Africa and the Italo-Ethiopian Crisis, 1939-1941* (London: Longman)

**Asiwaju, A. I.** (1976) *Western Yorubaland under European Rule, 1889-1945: a Comparative Analysis of French and British Colonialism* (London: Longman)

**Austen, R.** (`1987) *African Economic History: Internal Development and External Dependency* (London: James Curry)

**Ayache, A.** (1956) *Le Maroc: bilan d'une colonisation* (Paris: Ed. Sociales)

**Ayandele, E. A.** (1966) *The Missionary Impact on Modern Nigeria, 1842-1914: a Political and Social Analysis* (London: Longman)

**Azikiwe, B. N.** (1934) *Liberia in World Politics* (London: A. H. Stockwell)

**Baer, G.** (1962) *A History of Land ownership in modern Egypt 1800 - 1950* (London: Oxford Univesity Press)

**Baeta, C. G** (1962) *Prophetism in Ghana: a Study of some 'Spiritual' Churches* (London: SCM Press)

**Baldwin, R. E.** (1966) *Economic Development and Export Growth: a Study of Northern Rhodesia, 1920-1960* (Berkeley, Calif.: University of California Press)

**Barbour, K.M.** na **Prothero, R.M.** (wah.) *Essays on African Population* (London: Routledge na Kegan Paul)

**Bassett, T. J.** (1988) 'The development of cotton in Northern Ivory Coast', *Journal of African History*, XXIX, kur. 267-84

**Bauer, P. T.** (1954) *West African Tyrade: a Study of Competition, Oligopoly and Monopoly in a Changing Society* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Beidelman, T. O.** (1982) *Colonial Evangelism: a Socio-historical Study of an East African Mission at the Grassroots* (Bloomington, Ind.: Indiana University Press)

**Beinart, W.** (1982) *The Political Economy of Pondoland, 1860-1930* (Cambridge University Press)

**Beinart, W.** na **Bundy, C.** (1987) *Hidden Struggles in Rural South Africa" Politics and Popular Movements in the Transkei and Eastern Cape 1890-1930* (London: James Curry)

**Benenett, G.** (1963) *Kenya, a Political History: the Colonial Period* (London: Oxford University Press)

**Bennett, N. R.** (1986) *Arab versus European: Diplomacy and War in Nineteenth Century East-Central Africa* (New York: Africana)

**Benson, M.** (1966) *South Africa: the Struggle for a Birthright* (Harmondsworth: Penguin)

**Berque, J.** (1970) *Le Maghreb entre deux guerres,* Tol. 2 (Paris: Ed. Du Seuil)

**Betts, R. F.** (mh.) (1972) *The Scramble for Africa: Causes and Dimension of Empire,* Tol. 2 (London: D.C. Heath)

**Bidwell, R.** (1973) *Morocco under Colonial Rule: French Administration of Tribal Areas, 1912-1912* (London: Frank Cass)

**Bley, H.** (1971) *South West Africa under German Rule, 1894-1914* (London: Heinemann)

**Blyden, E. W.** (1997) *Christianity, Islam and the Negro Race* (London: Longman)

**Boahen, A . A.** (1985) *African Perspectives on Colonialism* (Baltimore; Md. Johns Hopkins University Press)

**Bozzoli, B.** (1981) *The Political Nature of a Ruling Class: Capital and Ideology in South Africa 1890-1933* (London: Routledge na Kegan Paul)

**Bradford, H.** (1984) 'Mass movements and the petty bourgeoisie: the social origins of ICU leadership, 1924-9', *Journal of African History*, XXV, kur. 295-310

**Bret, R. J.** (1987) *Vie du Sultan Mohàmed Bakhit, 1856-1916: la pénétration française au Dar Sila, Tchad* (Paris: Editions du Centre National de la Recherche Scientifique)

**Brett, E.A** (1973) *Colonialism and Underdevelopment in East Africa* (New York: Nok Publishers)

**Brooke-Smith, R.** (1987) *The Scramble for Africa* (London: Macmillan)

**Brunschwig, H.** (1966) *French Colonialism, 1871-1914: Myths and Realities* (New York: Praeger)

**Brunschwig, H.** (1982) *Imperialism: the Idea and Reality of British and French Colonial Expansion, 1880-1914* (New York: Oxford University Press)

**Brunschwig, H.** (1983) *Noirs et blancs dans 'Afrique noire française on comment le colonisé devient colonisateur (1870-1914)* (Paris: Flammarion)

**Caldwell, J. C.** (mh. ) (1975) *Population Growth and Socio-Economic Change in West Africa* (New York: Columbia University Press)

**Caldwell, J. C.** na **Okonjo, J.** (wah.) (1968) *The Population of Tropical Africa* (London: Longman)

**Carland, J. M.** (1985) *The Colonial Office and Nigeria, 1898-1914* (London na Basingstoke: Macmillan)

**Chimweizu** (1975) *The West and the Rest of Us: White Predators, Black Slavers and the African Elite* (new York: Vintage Books)

**Christopher, A. J.** (1988) *The British Empire at its Zenith* (London: Croom Helm)

**Clarence-Smith, W. G.** (1985) The Third Portuguese Empire (1825-1975) (Manchester: Manchester University Press)

**Clayton, A.** (1986) *The British Empire as Superpower, 1919-1939* (Basingstoke: Macmillan)

**Coleman, J.S.** (1958) *Nigeria: Background to Nationalism* (Berkeley na Los Angeles, Calif.: University of California Press)

**Coleman, J. S. na Rosberg, C. G.** (wah) (1970) *Political Parties and National Integration in Tropical Africa* (Berkeley na Los Angeles, Calif.: University of California Press)

**Collins, R. O.** (1983) *Shadows in the Grass: Britain in the Southern Sudan, 1918-1956* (New Haven, Conn.: Yale University Press)

**Colo, B. C.** na **Anignikin, S. C.** (1982) 'Pouvoir colonial et tentatives d'intégration africaines dans le système capitaliste: le cas du Dahomey entre les deux guerres', *Canadian Journal of African Studies*, XVI, uk. 2

**Cooke, D.** et al. (1985) *Teaching Development Issues, Section 2, Colonialism* (ManchesterDevelopment Education Project)

**Cooper, F.** (1980) *From Slaves to Squatters: Plantation Labour and Agriculture in Zanzibarand Coastal Kenya, 1890-1925* (New Haven, Conn. And London: Yale University Press)

**Coquery-Vidrovitch, C. na Moniot, H.** (1972) *Le Congo français au temps des grandes compagnies concessionnaires, 1898-1930* (Paris na the Hague: Mouton)

**Coquery-Vidrovitch, C.** na **Moniot, H.** (1974) *L'Afrique noire de1800 à nos jours* (Paris: Presses Universitaires Française)

**Crowder, M.** (1968) *West Africa under Colonial Rule* (London: Hutchnson)

**Crowder, M.** (mh.) (1971) *West Africa Resistance* (London: Hutchinson)

**Crowder, M.** na **Ikime, O.** (wah.) (1970) *West African Chiefs: Their Changing Status under Colonial Rule and Independence* (New York: Africana Publishing)

**Curtiu, P. D., Feierman, S., Thompson, L.** na **Vansina, J.** (1978) *African history* (London: Longman)

**Dally, M. W.** (1986) *Empire on the Nile: the Anglo-Egyptian Sudan 1898-1934* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Darby, P.** (1987) *Three Faces of Imperialism; British and American Approaches to Asia and Africa 1870-1970* (New Haven, Conn.: Yale University Press)

**Davidson, A. B.** (1972) *South Africa, the Birth of a Protest* (Moscow: African Institute)

**Davidson, B.** (1978) *Africa in Modern History* (London: Allen Lane)

**Davidsou, B.** (1983) *Modern Africa* (London: Longman)

**Deng, F. M.** (1978) *The Dinka in Afro-Arab Sudan* (New Haven, Conn. na London: Yale University Press)

**Deschamps, H.** (1960) *Histoire de Madagascar* (Paris: Berger-Levrault)

**Domergue-Cloarec, D.** (1986) *Politique coloniale francaise et réalités coloniales: la santé en Côte d'Ivoire, 1905-1958 9* Paris: Academie des Sciences d'Oytre-Mer)

**Duffy, J.** (1962) *Portugal in Africa* (Harmondsworth: Penguin)

**Ekechi, F. K.** (1987) 'The British assault on Ogbunorie Oracle in Eastern Nigeria', *Journal of African Studies*, XIV, 2 kur. 69-77

**Engel, L.** (1976) *Kolonialismus und Naiionalismus in Deutchen Protestantismus in Namibia 1907 bis 1945* (Frankfurt-on-Main: Peter Lang)

**Erlich, H.** (1982) *Ethiopia and Eritrea during the Scramble for Africa: a Political Biography of Ras Alula, 1875-1897* (East Lansing, Mich.: African Studies Centre, Michigan State University)

**Esoavelomandroso, M.** (1979) *La Province maritime orientale du Royaume de Madagascar à la fin du XIXe siécle (1992-1895)* (Antananarivo: FT)

**Fabb, J.** (1987) *The British Empire from Photographs: Africa* (London: Fatsford)

**Fabian, J.** (1986) *Language and Colonial Power: The Appropriation of Swahili in the Former Belgian Congo, 1880-1938* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Fanon, F.** (1967) *The Wretched of the Earth* (Harmondsworth: Penguin)

**Fashole-Luke, E., Gray, R., Hastings, A.** na **Tasie, G.** (wah.) (1978) *Christianity in Independent Africa* (London: Rex Collings)

**Feltz, G.** (1985) 'Histoire des mentalitès et histoire des missions au Burundi, ca. 1880-1960', *History in Africa,* XII, kur. 51-63

**Fetter, B.** (1983) *Colonial Rule and Regional Imbalance in Central Africa* (Boulder, Colo.: Westview Press)

**Fieldhouse, D. K.** (1981) *Colonialism 1870-1945: an Introduction* (London: Weidenfield na Nicolson)

**Finer, S. F.** (1962) *The Man on Horseback* (London: Pall Mall)

**First, R.** (1963) *South West Africa* (Harmondsworth: Penguin)

**Gahama, J.** (1984) *Le Burundi sous administration Belge* (Paris: Karthala)

**Gailey, H.A.** (1982) *Lugard and the Abeokuta Uprising: the Demise of Egba Independence* (London: Frank Cass)

**Gallaway, H.** (1987) *Gender, Culture and Empire: European Women in Colonial Nigeria* (Basingstoke: Macmillan)

**Gann, L. H.** na **Duignan, P.** (1967) *Burden of Empire* (London: Pall Mall)

**Gann, L. H.** na **Duignan, P.** (wah.) (1969) *Colonialism in Africa, 1870-1960,* Juz. I, *The History and Politics of Colonialism 1870-1914* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Gann, L. H.** na **Duignan, P.** (wah) (1970) *Colonialism in Africa 1870-1960,* Vol. II, *The History and Politics of Colonialism 1914-1960* (Cambridge University Press)

**Garvey, A. J.** (mh. (1923-5) Philosophy and Opinions of Marcus Garvey (London: Frank Cass, Tol. 1967

**Garvey, A. J.** (1963) *Garvey and Garveyism* (Kingston: United Printers)

**Geiss, I.** (1974) *The Pan-African Movement* (London: Methuen)

**Gershoni, I.** na **Jankowski, J. P.** (1987) *Egypt, Islam and the Arabs: the Search for Egyptian Nationahood 1900-1930* (New York: Oxford University Press)

**Gifford, P.** na **Louis, W. R.** (wah.) (1967) *Britain and Germany in Africa: Imperial Rivalry and Colonial Rule* (New Haven, Conn. na London: Yale University Press)

**Gifford, P.** na **Lous, W. R.** (wah. (1971) *France and Britain in Africa* (New Haven, Conn. na London: Yale University Press)

**Gilkes, P.** (1975) *The Dying Lion: Feudalism and Modernization in Ethiopia* (London: Julian Friedmann)

**Goglia, L.** (1985) *Storia fotografica dell 'imperofacista 1935-41* (Bari: Editori Laterza)

**Grassi, F.** na **Goglia, L.** (wah.) (1981) *Il colonialismo italiano da Adua all 'impero* (Rome na Bari)

**Greenhalgh, P.** (1985) *West African Diamonds 1919-1983; an Economic History* (Manchester: Machester University Press)

**Gulgelberger, G. M.** (1984) *Nama/Namibia: Diary and Letters of Nama Chief Hendrik Witbooi, 1884-1894* (Boston, Mass.: Boston University African Studies Centre)

**Hallett, R.** (1970) *Africa to 1875: a Modern History* (Ann Arbor, Mich.: Michigan University Press)

**Hansen, H. B.** (1984) *Mission, Church and State in a Colonial Setting: Uganda 1890-1925* (London: Heinemann)

**Hargreaves, J. D.** (1963) *Prelude to the Partition of West Africa* (London: Macmillan)

**Herskovits, M.** (1941) *The Myth of the Negro Past* (New York: Harper)

**Hess, R. L.** (1966) *Italian Colonialism in Somalia* (Chicago: Chicago University Press)

**Hill, A. C.** na **Kilson, M.** (wah.) (1971) *Apropos of Africa: Sentiments of Negro American Leaders on Africa from the 1800s to the 1950s.* (New York: Anchor)

**Hodges, G.** (1987) *The Carrier Corps: Military Labor in the East African Campaign, 1914-1918* (Westport, Conn.: Greenwood Press Inc.)

**Hodgkin, T.** (1956) *Nationalism in Colonial Africa* (London: F. Muller)

**Holt, P. M.** (mh.) (1968) *Political and Social Change in Modern Egypt* (London: Oxford University Press)

**Home, R.** (1982) *City of Blood Revisited: a New Look at the Benin Expedition of 1897* (London: Rex Collings)

**Hopkins, A. G.** (1973) *An Economic History of West Africa* (London: Longman)

**Hull, R. W.** (1980) *Modern Africa Change and Continuity* (Englewood Cliffs, Nj: Prentice Hall)

**Ikime, O.** (mh.) (1980) *Groundwork of Nigerian History* (Ibadan: Heinemann)

**Iliffe, J.** (1969) *Tanganyika under German Rule, 1905-1912* (Cambridge: Cambridge Universty Press)

**Iliffe, J.** (1979) *A Modern History of Tanganyika* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Isaacman, A.** (1972) *Mozambique: the Africanization of a European Institution: the Zambesi Prozos, 1750-1902* (Madison Wis.: University of Wisconsin Press)

**Isaacman, A.** (1976) *The Tradition of Resistance in Mozambique: Anti-Colonial Activity in the Zambesi Valley, 1850-1921* (Berkeley, Calif. University of California Press)

**Isaacman, A.** na **Isaacman, B.** (1983) *Mozambique: from Colonialism to Revolution* (Boulder, Colo. Westview Press)

**Issawi, C. P.**(1963) *Egypt in Revolution: an Economic Analysis* (London: Oxford University Press)

**Joseph, R. A.** (1978) *Radical Nationalism in Cameroun: Social Origins of the UPC Rebellion* (Oxford: Oxford Universtiy Press)

**July, R. W.** (1968) *The Origins of Modern African Thought* (London: Faber)

**Kabwegyere, T. B** (1974) *The Politics of State Formation* (Nairobi: East African Publishing House)

**Kadalie, C.** (1970) *My Life and the ICU: the Autobiography of a Black Trade Unionist in South Africa* (London: Frank Cass)

**Kaddache, M.** (1970) La Viepolitique à Alger de 1919 à 1939 (Algiers: Société national d'édition et de diffusion [SND]

**Al-Kaddal, M. S.** (1973) *Al-Mahdiyya wal Habasha* (Khartoum)

**Kaniki, M. H. Y.** (mh.) (1980) *Tanzania under Colonial Rule* (London: Longman)

**Kay, G. B.** (mh.) (1972) *The Political Economy of Colonialism in Ghana: Documents 1900-1960* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Kelly, R. C.** (1985) *The Nuer Conquest: the Strucrure and Development of an Expansionist System* (Ann Arbor, Mich. University of Michigan Press)

**Kent, R. K.** (mh.) (1979) *Madagascar in History: Essays from the 1970s* (Berkeley, Calif. Foundation for Malagasy Studies)

**Keppel-Jones, A.** (1983) *Rhodes and Rhodesia: the White Conquest of Zimbabwe, 1884-1902* (Kingston na Montreal: McGill-Queen's University Press)

**Kilingray, D.** (1984) 'A swift agent of government: airpower in British colonial Africa, 1916-1939', *Journal of African History*, XXV, kur. 429-44

**Kimble, D.** (1963) *A Political History of Ghana: the Rise of Gold Coast Nationalism 1850-1928* (Oxford: Clarendon Press)

**Kopytoff, J. H.** (1965) *A Preface to Modern Nigeria: the 'Sierra-Leoneans' in Yoruba 1830-1890* (Madison, Wis. University of Wisconsion Press)

**Lancheraf, M.** (1965) L'Algérie: nation et société (Paris: Maspero)

**Langley, J. A.** 91973) *Pan-Africanism and Nationalism in West Africa 1900-1945: A Study in Ideology and Social Classes* (Oxford: Clarendon Press)

**Last, M.** (1967) *The Sokoto Caliphate* (London: Longman)

**Lee, E.** (1985) *To the Bitter End: a Photographic History of the Boer War 1899-1902* (New York: Viking)

**Leith-Ross, S.** (1983) *Stepping-stones: Memoirs of Colonial Nigeria 1907-1960*, mh. M.Crowder (London na Boston: Peter Owen)

**Levy, N.** (1982) *The Foundations of the South African Cheap Labour System* (London: Routledge na Kegan Paul)

**Lewis, I. M.** (1965) *The Modern History of Somaliland: from Nation to State* (London: Longman)

**Leys, C.** (1975) *Underdevelopment in Kenya: the Political Economy of Neo-colonialism, 1964-1971* (London: James Currey)

**Liebenow, J. G.** (1969) *Liberia: the Evolution of Privilege* (Ithaca, NY: Cornell University Press)

**Liesegany, G., Pasch, H.** na **Jones, A** (1986) *Figuring African Trade: Proceedings of the Symposium on the Quantification and Structure of the Import and Export and Long Distance Trade in Africa, 1800-1913* (Berlin: Dietrich Reimer Verlag)

**Lloyd, P. C.** (1972) *Africa in Social Change*, tol. rud. (Harmondsworth: Penguin)

**Louis, W. R.** (1963) *Ruanda-Urundi*, 1884-1919 (Oxford: Clarendon Press)

**Lous, W. R.** (mh.) (1976) *Imperialism: the Robinson and Gallagher Controversy* (New York: Franklin Watts)

**Lovejoy, P. E.** (1988) 'Concubinage and the status of women slaves in early colonial Northern Nigeria', *Journal of African History*, XXIX, kur. 245-66

**Lubeck, P. M.** (mh.) (1987) *The African Bourgeoisie: Capitalist Development in Nigeria, Kenya and the Ivory Coast* (Boulder, Colo. Lynn Reinner Publisher)

**Lynch, H. R.** (1967) *Edward Wilmot Blyden: Pan-Negro Patriot* (London: Oxoford University Press)

**McCracken, J.** (1978) *Politics and Christianity in Malawi 1875-1940: the Impact of the Livingstonia Mission in the Northern Province* (Cambridge: Cambridge Commonwealth Series)

**Macknzie, J. M.** (1984) *Propaganda and Empire: the Manipulation of British Public Opinion, 1880-1960* (Manchester: Manchester University Press)

**Macpherson, F.** (1981) *Anotomy of a Conquest: the Occupation of Zambia, 1884-1924* (Harlow: Longman)

**Makonnen, R.** (1973) *Pan-Africanism from Within* (Nairobi: Oxford University Press)

**Manning, P.** (1982) *Slavery, Colonialism and Economic Growth in Dahomey, 1640-1960* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Marcum, J.** (1969) *The Angolan Revolution* (Cambridge, Mass.: Massachusetts Institute of Technology Press)

**Marcus, H. G.** (1975) *The Life and Times of Menelik II: Ethiopia 1844-1913* (Oxford: Clarendon Press)

**Marks, S.** (1970) *Reluctant Rebellion: the 1906-1908 Disturbances in Natal* (Oxford: Clarendon Press)

**Marks, S.** na **Rathbone, R.** (wah.) (1982) *Industrialization and Social Change in South Africa: African Class Formation, Culture and Consciousness 1870-1930* (Harlow: Longman)

**Maunier, R.** (1949) *The Sociology of Colonies,* Juz. 2 (London: Routledge na Kegan Paul)

**Mazrui, A. A.** (1980) *The African Condition* (London: Heinemann)

**Mba, N. E.** (1982) *Nigerian Women Mobilized: Women's Political Activity in Southern Nigeria 1900-1965* (Berkeley, Calif. Institute of International Studies)

**Mbiti, J. S.** (1969) *Affrican Religions and philosophy* (London: Heinemann)

**Meebelo, H.** S. (1969) *Reaction to Colonialism: a Prelude to the Politics of Independence in Northern Zambia, 1893-1939* (Manchester: Manchester University Press)

**Meredith, D.** (1984) 'Government and the decline of the Nigerian oil-palm export industry, 1919-1939', *Journal of African History*, XXV, kur. 311-29

**Monti, N.** (mh.) (1987) *Africa Then: Photographs 1840-1918* (New York: Knopf)

**Morikawa, J.** (1985) 'The myth and reality of Japan's relations with colonial Africa - 1885-1960', *Journal of African Studies*, XII, 1, kur. 39-46

**Mosley, L.** (1964) *Haile Selassie: the Conquering Lion* (London: Weidenfeld na Nicolson)

**Mosley, P. C.** (1983) *The Settler Economies: Studies in the Economic history of Kenya and Southern Rhodesia* (1900-1963) (Cambridge: Cambridge University Press)

**Mourao, F. A. A.** (1977) *La Présence de la culture Africaine et la dynamique du processus socal brésilien* (Lagos: Colloquium)

**Mugomba, A. na Nyaggah, M.** (wah.) (1980) *Independence without Freedom: the Political Economy of Colonial Education in Southern Africa* (Santa Barbara na Oxford: ABC-Clio Press)

**Munro, J. F.** (1975) *Colonial Rule and the Kamba* (Oxford: Clarendon Press)

**Munro, J.** F. (1976) *Africa and the International Economy, 1800-1960* (London: Dent)

**Muriuki, G.** (1974) *A history of the Kikuyu, 1500-1900* (Nairobi: Oxford University Press)

**Mutibwa,** . M. (1974) *The Malagasy and the Europeans: Madagascar's Foreign Relations 1861-1895* (London: Macmillan)

**Newitt, M. D. D.** (1981) *Portugal in Africa: the Last Hundred Years* (London: C. Hurst)

**Nkrumah, K.** (1975) *Ghana: the Autobiography of Kwame Nkurumah* (London: Nelson)

**Nzemeke,** A. D. (1982) *British Imperialism and African Response: the Niger Valley, 1851-1905* (Paderborn: Schonimgh)

**Nzula, A. T., Potekhin, I. I.** na **Zusmanovich, A. Z.** (1979) *Forced Labour in Colonial Africa* (London: Zed Press)

**Obichere, B.** I. (1971) *West African States and European Expansion: the Dahomey - Niger hinterland, 1885-*1898 (New Haven, Conn. Yale University Press)

**Ofcansky, T. P.** (1986) 'The East African campaign in the *Rhodesian Herald'*, *Journal of African Studies,* XIII, kur. 283-94

**Ogot, B.** A. (mh.) (1972) *War and Society in Africa* (London: Frank Cass)

**Ogot, B.** A. (mh.) (1974) *Zamani: a Survey of East African History* (Nairobi: East African Publishing House, Tol. 2)

**Oliver, R.** na **Crowder, M.** (1981) *The Cambridge Encyclopaedia of Africa* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Oliver, R.** na **Sanderson, G. N.** (1985) *The Cambridge History of Africa: from 1870 to 1905*, Juz VI (Cambridge: Cambridge University Press)

**Oliver de Sardan, J. P.** (1984) Les Sociétés Songhay-Zarma (Niger-Mali): chefs, guerriers, esclaves, paysans (Paris: Editions Karthala)

**Olorunfemi, A.** (1984) 'The contest for Salaga: Anglo-German conflict in the Gold Coast hinterland', *Journal of African Studies*, XI, 1, kur. 15-24

**Omu, F. I. A.** (1978) *Press and Politics in Nigeria, 1880-1957* (London: Longman)

**Opoku, K. A.** (1978) *West African Traditional Religion* (Singapore: FEP)

**Osuntokun, J.** (1978) *Nigeria in the First World War* (London: Longman)

**O'Toole, T.** (1984) 'The 1928-1931 Gbaya insurrection in Ubangui-Shari: messianic movement or village self-defence?' *Canadian Jornal of African Studies*, XVIII, uk.2

**Owen, R.** na **Sutcliffe, B.** (wah.) (1972) *Studies in the Theory of Imperialism* (London: Longman)

**Pachai, B.** (mh.) (1972) *The Early History of Malawi* (London: Longman)

**Packard, R. M.**(1984) 'Maize, cattle and mosquitoes: the political economy of malaria epidemics in colonial Swaziland,' *Journal of African History*, XXV, kur. 189-212

**Padmore, G.** (1956) *Pan-Africanism or Communism*? (London: Dobson)

**Page, M. E.** (mh.) (1987) *Africa and the first World War* (Basingstoke: Macmillan)

**Pankhurst, R.** (1968) *Economic History of Ethiopia, 1800-1935* (Addis Ababa: Haile Sellassie I University Press)

**Parson, J.** (1984) *Botswana: Liberal Democracy and the Labour Reserve in Southern Africa* (Boulder, Colo.1 Westview Press)

**Peel, J. D. Y.** (1983) *Ijeshas and Nigerians: the Incorporation of a Yoruba Kingdom. 1890s-1970s* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Pélissier, R.** (1977) *Les Guerres grises: résistance et révoltes en Angola* (1945-1941) Juz. 2 (Orgeval: Pélissier)

**Pélissier, R.** (1984) *Naissance du Mozambique: rèsistance et rèvoltes anticoloniales* (1854-1918) Juz. 2 (Oegeval: Pèlissier)

**Perham, M.** (1960) *Lugard: the Years of Authority, 1898-1945* (London: Collins)

**Perkins, K. J.** (1981) *Qadis, Captains and Colons: French Military Administration in the Colonial Maghrib, 1844-1934* (New York: Africana Publishing Co.)

**Perrings, C.** (1979) *Black Mineworkers in Central Africa: Industrial Strategies and the Evolution of an African Proletariat in the Copperbelt, 1911-1941* (London: Heinemann)

**Person, Y.** (1968-75) *Samori: une rèvolution Dyula*, Juz. 3 (Paris: Mem. De l'Institut Fondamental de l'Afrique Noire)

**Phimister, I. R.** na **Van Onselen, C.** (1978) *Studies in the History of African Mine Labour in Colonial Zimbabwe* (Gwelo: Mambo Press)

**Phimister, I. R.** (1984) 'Accommodating imperialism: the compromise of the settler state in Southern Rhodesia, 1923-1929', *Journal of African history*, XXV, kur. 279-94

**Porter, B.** (1986) *Imperialism and Popular Culture* (Manchester: Manchester University Press)

**Prouty, C.** (1986) *Empress Taytu and Menelik II: Ethiopia 1883-1910* (London: Ravens Educational and Development Services)

**Ragsdale, J. P.** (1986) *Protestant Mission Education in Zambia, 1880-1954* (Selinsgrove: Susquehann University Press)

**Ranger, T. O.** (1967) *Revolt in Southern Rhodesia, 1896-1897* (London: Heinemann)

**Ranger, T. O.** (mh.) (1968) *Aspects of Central African history* (London: Heinemann)

**Ranger, T. O.** (mh.) (1968) *Emerging Themes of African History* (Nairobi: East African Publishing House)

**Ratcliffe, B. M.** (1981) 'The economics of the partition of Africa: methods and recent research trends', *Canadian Journal of African Studies*, XV, 1, kur. 3-32

**Reyntjens, F.** (1985) *Pouvoir et droit au Rwanda: droit public et évolution politique 1916-1973* (Tervuren: Musée royal de l'Afrique centrale, Belgium)

**Rich, P. B.** (1986) *Race and Empire in British Politics* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Robinson, R.** na **Gallagher, J.** (1961) *Africa and the Victorians: the Official Mind of Imperialism* (London: Macmillan)

**Rodney, W.** (1972) *How Europe Underdeveloped African* (Dar es Salaam: Tanzania Publishing House)

**Rodrigues, J. H.** (1964) *Brasil e Africa outro Horizonte* (Rio de Janeiro: Civilizacao Brasileira)

**Rosberg, C. G.** na **Nottingham, J.** (1966) The myth of Mau Mau: Nationalism in Kenya (Nairobi: East African Publishing House)

**Ross, R.** (mh.) (1982) *Racism and Colonialism: Essays on Ideological and Social Structure* (The Hague: Martiunus Nijhoff)

**Rotberg, R. I.** (1966) *The Rise of Nationalism in Central Africa: the Making of Malawi and Zambia, 1873-1964* (Cambridge, Mass: Harvard University Press)

**Rotberg, R. I.** na **Mazuri, A. A.** (wah.) (1970) *Protest and Power in Black Africa* (New York; Oxford University Press)

**Rout, L. B.** (1976) *The African Experience in Spanish America, 1502 - Present Day* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Rubenson, S.** (1964) *Wichale XVII: the Attempt to Establish a Protectorate over Ethiopia* (Addis Ababa: Haile Sellassie 1 University Press)

**Rweyemamu, J.** (1974) *Underdevelopment and Industralization in Tanzania: a Study in Perverse Capitalist Industrial Development* (London na Nairobi: Oxford University Press)

**Saint-Martin, Y.** (1972) *L'Empire toucouleur et la France: un demi-siécle de relations diplomatiques (1846-1893)* (Dakar: Publications de la Faculté des lettres et sciences humaines, Université de Dakar)

**Sanderson, L. P.** na **Sanderson, N.** (1981) *Education, Religion and Politics in Southern Sudan, 1899-1964* (London na Khartoum: Ithaca Press na Kharotum Univesity Press)

**Schreuder, D. M.** (1980) *The Scramble for Southern Africa, 1877-1895: the Politics of Partition Reappraised* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Schneider, W. H.** (1982) *An Empire for the Masses: the French Popular image of Africa, 1870-1900* (Westport, Conn. Greenwood Press)

**Segal, R.** na **First, R.**(1967) *South West Africa: Travesty of Trust* (London: André Deutsch)

**Serman, W.** (1982) *Les Officiers français dans la nation, 1848-1914* (Paris: Aubier Montaigne)

**Shenton, R. W.** (1986) *The Development of Capitalism in Northern Nigeria* (Toronto: University of Toronto Press)

**Shepperson, G.** na **Price, T.** (1958) *Independent African: John Chilembwe and the Origins, Setting and Significance of the Nyasaland Native Uprising of 1915* (Edinburgh: Edinburgh University Press)

**Shibayka, M.** (1978) *Al-Sudan wal Thawra al-Mahdiyya*, Juz. 1 (Khartoum)

**Shibeika, M.** (1952) *British Policy in the Sudan, 1882-1902* (London: Oxford Univesity Press)

**Shipley, D.** (1980) *Black Africa and de Gaulle: from the French Empire to Independence* (London: Pennsylvania State Universirty Press)

**Sik, E.** (1964) The history of Black Africa, Juz. II (Budapest: Akadémiai Kiadó)

**Silberman, L.** (n.d) *The Mad Mullah: Hero of Somali Nationalism* (London)

**Simons, H. J.** na **Simons. R. E.** (1969) *Class and Clourin South Africa,1850-1950* (Harmondsworth: Penguin)

**Spacensky, A.** (1970) *Madagascar, cinquante ans de vie politique: de Ralaimongo à Tsiranana* (Paris: Nouvelles Editions Latines)

**Spittler, G.** (1981) *Verwaltung in einem afrikischen Bauernstaat: das Koloniale Franzosisch - Westafrika* (1919-1939) (Wiesbaden: Steiner)

**Steinhart, E. I.** (1978) *The kingdoms of Western Uganda, 1890-1907* (Princeton: Princeton University Press)

**Stevens, R. P.** (1967) *Lesotho, Botswana and Swaziland* (New York:Praeger)

**Stokes, E.** na **Brown, R.** (wah.) (1966) *The Zambezian Past: Studies in Central African history* (Manchester: Manchester Univesity Press)

**Sundkler, B.G. M.** (1961) *Bantu Prophets in South Africa, Tol.. 2* (London: Oxford University Press)

**Sure-Canale, J.** (1964) *L'Afrique noire, l'ére coloniale, 1900-1945* (Paris: Éd. Sociales)

**Suret-Canale, J.** (1971) *French Colonialism in Tropical Africa, 1900-1945* (London: C. Hurst)

**Symonds, R.** (1986) *Oxford and Empire: the Last Lost Cause?* (Basingstoke: Macmillan)

**Thompson, V.** na **Adloff, R.** (1960) *The Emerging States of Equatorial Africa* (Stanford, Calf. Stanford University Press)

**Thompson, V.** na **Adlff, R.** (1968) *Djibouti and the Horn of Africa* (Stanford, Calif. Stanford University Press)

**Tosh, J.** (1978) *Clan Leaders and Colonial Chiefs in Lango: the Political History of an East African Stateless Society, c. 1800-1939* (Oxford: Clarendon Press)

**Touval,s S.** (1963) *Somali Nationalism* (Cambridge, Mass. Harvard University Press)

**Torner, V.** (mh.) (1971) *Colonialism in Africa 1870-1960* Juz. III, *Profiles of Change: African Society and Colonial Rule* (Cambridge: Cambridge University Press)

**Turrell, R. V.** (1987) Capital and Labour and the Kimberley Diamond Fields 1871-1890 (Cambridge: Cambridge University Press)

**Ukpabi, S. C.** (1987) *Mercantile Soldiers in Nigerian history: a history of the Royal Niger Company Army, 1886-1990* (Zaria: Gaskiya Corporation)

**Uzoigwe, G. N.** (1974) *Britain and the Conquest of Africa: the Age of Salisbury* (Ann Arbor, Mich. Michigan University Press)

**Vail, L.** na **White, L.** (1980) *Capitalism and Colonialism in Mozambique: a Study of Quelimane District* (London: Heinemann)

**Van der Ross, R. E.** (1986) *The Rise and Decline of Apartheid: a Study of Political Movements among the Coloured People of South Africa, 1880-1985* (Cape Town: Tafelberg)

**Van Onselen, C.** (1982) *Studies in the Social and Economic History of the Witwatersrand, 1886-1914,* Juz.2 (Harlow: Longman)

**Vansina, J.** (1966) *Kingdoms of the Savanna* (Madison, Wis. University of Wisconsin Press)

**Vatikiotis, P. J.** (1969) *The Modern History of Egypt* (London: Weidenfeld na Nicolson)

**Verrier, A.** (1986) *The Road to Zimbabwe* (London: Jonathan Cape)

**Vickery, K. P.** (1986) *Black and White in Southern Zambia: the Tonga Plateau Economy and British Imperialism,* 1890-1939 (New York: Greenwood Press)

**Webster, J. B.** (1964) *The African Churchers among the Yoruba, 1888-1922* (Oxford: Clarendon Press)

**Webster, J. B.** na **Boahen, A. A.** (1967) *The Revolutionary Years: West Africa since* 1800 (London: Longman)

**Weiskel, T. C.** (1980) *French Colonial Rule and the Baule Peoples, 1889-1911* (Oxford: Clarendon Pres)

**Weiss, H.** (1967) *Political Protest in the Congo* (Princeton, NJ: Princeton University Press)

**Welch, C. E.** (1966) *Dream of Unity: Pan-Africanism and Political Unification in West Africa* (Ithaca, NY: Cornell University Press)

**Wickins, P.** (1986) *Africa 1880-1920: an Economic History* (Cape Town: Oxford University Press)

**Williams, W. L.** (1982) *Black Americans and the Evangelization of Africa, 1877-1900* (Madison, Wis. University of Wisconsin Press)

**Wilson, H. S.** (1978) The Imperial Experience in Sub-Saharan Africa since 1870 (Oxford: Oxford University Press)

**Wolff, R. D.** (1974) *The Economics of Colonialism: Britain and Kenya, 1870-1930* (New Haven, Conn. na London: Yale University Press)

**Worger, W. H.** (1987) *South Africa's City of Diamonds: Mine Workers and Monopoly Capitalism in Kimberley, 1867-1895* (New Haven, Conn. na London: Yale University Press)

**Yoshida, M.** (1984) *Agricultural Marketing Intervention in East Africa: a Study in the Colonial Origins of Marketing Policies, 1900-1965* (Tokyo: Institute of Developing Economics)

**Young, C.** (1965) *Politics in the Congo: Decolonization and Independence* (Princeton, NJ: Princeton University Press)

**Yudelman, D.** (1983) *The Emergence of Modern South Africa: State, Capital and the Incorporation of Organized Labour in the South African Gold Fields, 1902-1939* (Westport, Conn. Greenwood Press)

**Zayid, M. Y.** (1965) *Egypt's Struggle for Independence* (Beirut: Khayats)

**Zulfu, I. H.** (1976) *Shikan Ta'rikh Askari Lihamlat Al-Ganaral Hicks* (Abu Dhabi)

# FARAHASA


'Abd al-Latif - 297
'Abd al-Rahman - 298
Appiah – 266
'Abdullah al-'Alli Yusuf - 301
A.B. Xuma – 375
A.I. Asiwaju - 165
Abbas Hilmi - 43
Abbas wa II - 43
Abbe Boillat - 277
Abd al-Azizi - 56
Abd al-Kadir Muhammad Imam - 49
Abdalkadir - 167
Abdal-Kadir – 305
Abdel Karim – 308, 311
Abd-Hamid ben Abdille Hassan - 51
Abdu al-Rahman al-Nudjumi - 48
Abdulla Tarara – 336
Abdullah ibn al-Sayyid Muhammad - 47
*Aberewa* - 256, 255
Abraham Razafy - 140
*Abusa* - 199
Abushiri - 89
Achimota - 275
Adli Yakan - 295
Admiral Nelson - 278
Adrar - 62
Aggrey – 373, 376
Agostinho Jose Mathias – 351
*ahenkro* – 266
Ahmad al-Numan Mek - 49
Ahmad al-Sharif - 58, 60
Ahmad Lufti al-Sayyid - 44
Ahmad Urabi - 38, 40
Ahmadou Dugay Cledor - 278
Ahmadu - 69, 70, 72
Aime Cesaire - 279
Ajayi Crowether - 277, 279
*Akede Eko* – 288
Akiiki Nyambogo – 338
Akini Kotoku, - 255
Akiwanda Savage – 320
Akyem Abuakwa – 323, 250
al Regnier – 314
Aladura - 263
Alan Burns - 6
Alaphetite - 167
al-Azhar - 276
Albert Bernad - 301
Albert Nzula – 345
Albertini - 141
al-Bur - 300
Alexis - 150
Alfayo Odongo - 263
Alfayo Odongo Mango – 330
Alfred C. Sam – 370
al-hadj Umar - 69
allal al-Fasi – 312, 314
Allen Isaacman - 31
Allen Yancy – 365
Allenby - 295
*al-Liwa* – 44, 288
al-Radjma - 163
al-Rida - 60
al-Sayyid - 52, 298
al-Sihayni - 298
al-Tha-alibi - 304
Ameziya - 57

Amiri Idris al-Sanusi - 60
Amy Ashwood Garvey – 368
Andre Gide - 241
Andre Matswa – 287
*Ansar* - 45, 47, 48
Antonio Jose de Nacimento – 279, 349
Antun - 275
Anwal – 311
Anwar Pasha - 58
Archinard - 70
*arixas* – 375
Arthur Barclay – 363
*asafo* – 323
Asantehene - 76, 77
*Asomi* – 330
*Asondwee Afe* – 266
Ataturk - 58
Azikiwe – 319, 375

B.O. Oloruentimehin - 9
Babiyanea - 118
Badis – 306
Badaglio – 367
Badoglio - 61
Bahri Kika – 313
Bai Burch - 81, 82
Bakary Dialo - 279
Bakopi – 331
Banda – 375
Barelay – 355
"Baraza la Wenyeji" - 177
Bartle Frere - 115
Barue - 32
Basil Davidson - 4
Bataka – 331
Batha Hagos - 149
Behanzin - 5, 74, 75
Ben Nasir – 307
Bendjellul – 314
Beni Warighil – 311
Benito Sylvain - 149
Benjamin Owuor Gumba – 332
Benjamini Payre 356
Betts – 282
Bey - 168
Beya - 54
Bie Hasan al-Wazzani – 312
*bilad al-siba* - 56
Bismarck - 17
Blaise Diagne - 162, 167, 250, 325, 326
Blyden - 278
Bob - 274
Bob Johnson - 274
Boilat, - 279
Bonaparta, 275
Booker T. Washington - 113, 114, 363, 376
Borgnis - Desbordes - 69, 72
Botha - 168
Bourguiba – 313
Brunot – 366
Brunschwig - 35
Bwewer – 355
*Cadi* - 175
Caetano da Costa Alegre - 279
Captain Dean – 370
Carlos Deambrsis Martins – 284
Carlton Hayes - 14
Carnet Wolseley - 42
Carolina - 274
Casely hayford - 150
Casely Rayford – 279, 320, 324
Casey Hayford – 324
Casolis - 121
Catshwayo - 115
Caudrelier - 74
Cecil John Rhodes - 116
Cecil Matolo – 338
Cecil Rhodes - 20
Cetshwayo - 5, 116, 118, 120
*Ceuta* - 54
Chakosi - 20
Chaminuka – 271
Changanure - 122
Charles Beart - 274, 275
Charles Darwin - 12
Charles Gordon - 47
Charles Mac Carthy - 76
Charles Temple -178
Charles Von Onselen - 37
Charlie Chaplin, - 274
Charlotte Maxeke – 375

Charlotte Maythe – 373
Chilembwe - 110, 375
*Chimurenga* - 125, 126
Chioko - 109
Chota - 125
Clemeant Kadalie – 344
Clemens Kiiza – 334
Colliad - 121
Combes - 72
Conchon - 139
Condominium - 297
Constantine – 314
Court Teleki - 87
Coutchilli - 75
Cromer - 43, 44
Crowder – 67, 83, 282
Crowther - 274, 290
Cuanza Norte – 349
Cuthebert Christy – 365
Cynthia Brantley Smith - 32
Cyrenaica - 163

D.S. Malekebu – 375
Dali'dephu - 32
Damel - 19, 67
Danguash – 318, 368
Dangush – 368
Daniel B. Haward – 358
Daniel Sande - 263
Darwin - 13
David Beach - 33
David Kaunda – 343
Davidson - 28, 29
De Bono – 367
Degkur - 50
Delavignette - 176
Dengkur - 50
Denteh - 255
Denton - 77
Destenava: - 1
*Destur* – 313
*Diamang* - 202
Didwo Twe – 356
Dike - 15
Dinizulu - 116
Dinshaway - 44
Diu - 50
Djabal Saghuru - 58
Dodds - 74, 75
Dorgere - 74
Dowl Diu - 50
Dubois – 317
Duchesne - 132
Duke - 16
Dussac - 141
Dussao - 141
*Duwar-commune* – 306
Dwane – 373

E.S. Atieno-Othiambo - 9
Ediwn J. Barclay – 365
Eduado Mondalne – 375
Edward Blyden, - 277, 370
Edward Wilmot Blyden - 4
Eillie Mokalapa - 107
Eldon Gorst - 44
Elija - 164
Eliot - 92
Eliud Mathu – 335
Elleck Mashingaidze - 33
Elliot Kamwana - 263
Emin Khalid - 167
Emir - 172
Emir Mahmud *Ansar* - 48
Emmanueli Razafindrakoto - 140
Enock Mgijima – 341
Enver - 58
Enver Pasha – 307
Eric Hobsbawn - 106
Ernest Lyon - 156

F. Osam – Pinakko – 375
F.D. Casely Rayford – 321
F.H. Hinsley - 14
F.V. Nanka Bruce – 319
Fada N'Gouma - 81
*faki* - 298
Faki Ali - 49
*Fallahim* - 166, 226
*Fandroana* - 133
*Fanompoana*
Farah 'Umar - 301

Faulkner - 153, 365
Fenner Brockway – 284
Ferhat Abbas – 306
Fernando Po. – 365
Firestone – 366
Fode Kabba - 81
Fode Silla - 81
*Fonompoana Forowa* – 268
Francis Scott - 77
Francisco Castelbranco - 279
Franck Osama Pinanko – 373
Franklin D. Roosevelt – 366
Frederick - 173
Frederick Cumngton - 125
Frederick Douglas – 376
Frederick Lugard - 87
Fu'ad - 295
Fu-ad I, - 294

G.N. Uzoigwe - 16
Gabra Sellase - 154
Galjal haya - 300
Gallagher - 17
Gallieni - 69, 135, 136, 137
Gamede – 342
Gandhi - 141
Gardew - 82
Garluak - 299
Garnet Wolseley - 76
Garric Braide - 164
Garvey – 317, 354, 362, 372
Gazuangonongo - 109
George - 168
George Goldie - 19
George Ledebour - 11
Gerald Portal - 146
Gibson – 355
Gilbert Gwassa - 32
Godfrey Wilson - 251
Gordon – 283, 296
Gouraud - 57
Graziani - 60
Green – 355
*Gremio Africano* – 353
*Guerras Pretas* - 104
Guggisberg – 321
Guiseppe Sapeto - 146
Gungunyama - 101
Gungunyane - 102, 108
Gwek Ngundeng - 299

H.H. Johnston - 6
H.M. Stanley - 16
Habar Awal - 51
Habar Gerhajis - 51
Haddad – 308
Hadj dji Hasan - 300
Hadjali Abdel-Kader 284
Hadjdj Bashir Yusuf - 301
Hadjdj Farah 'Umar - 302
Haile Selassie – 358, 364
Hailé Selassie I – 359
Hamallah - 259
Hammam Lifu – 308
Hamu Catshwayo - 116
Hans Dominik - 20
Harris - 164
Harry Johnston - 103
Harry Thuku – 287, 336
Hassan bin Omari - 89
Hayes - 15
Heln - 118
Henderson - 74
Hendrik Witbooi - 127
Hendrik Witthoi - 3
Henri - 34
Henry Bulwer - 115
Henry Meebelo - 31
Henry Moneal Turner – 370
Henry Too Wesley – 356
Hentry – 365
Herbert Macaulay - 208, 319, 326
Herbert Rugizibwa - 334
Hercules Robinson - 116
Herman Ven Wissman - 89
Hertzog – 342
Herzi Bogor - 301
Herzi Gushan - 300

Hewett - 79
Hicks Pasha - 47
Hidjra - 47
Hij Isayu – 359
Hilaire Belloo - 5
Hilal – 313
Hilton Young – 333
Hobson - 11, 12
Holland Rose - 21
Hopkins - 15, 208
Hugh Clifford – 321, 324
Humbert - 73
Husayn Rushidi - 294

I.A. La Guma – 284
Ibrahim Youssef – 284
Idris al-Sanusi - 163
Illing - 52
Immmunuel Wallerstein - 35
*Induma* Lotshe - 118
Isa - 51
Isaacman - 25, 32, 35

J.E.K. Aggrey – 375
J.T. Cumede – 284
Jabavu - 128, 376
Jacob Ajayi - 30
Jaja - 79
Jakobo - 263
James – 368
James Aggrey – 376
James Beauttah – 333
James Gichuru – 335
James Johnson - 274
Jameson - 118, 120
Jan Smuts – 340
Janet - 241
Jardan Nguma - 263
Jean-Joseph Rabearivelo - 279
Jemesimiha Jehu-Jesse Kariuki – 336
*Jiha* - 7, 8
*Jihadi* - 163
*jihadi* - 47, 48, 51, 52
*Jirika* - 134
Joaquim Dias Antonio de Assis Junior – 349, 350
Job Muchuchu – 336
Johana Owala – 329
John Atkinson
John Bryan Small – 373
John Chilembwe - 109, 163, 164, 261, 374, 376
John D. Hagreaves - 6
John Dube – 375, 376
John Dunn - 116
John Gallagher - 14
John Hope – 376
John Iliffe - 96
John Kumalo - 118
John Kwame Ayew – 323
John Langalibabele Debe - 113
John Makunga - 118
John Owalo - 93
John Smith Moffat - 117
John Ţengo Jabavu - 113
Johnson - 79
Jomo Kenyatta – 284, 333, 338, 368
Jonathan Okwiri – 332
Jonnart - 180
Jose de Fontes Pereira – 349
Jose Fontes Pereira - 107
Joseph Anene - 25
Joseph Kamulegeya – 337
Joseph Kangethe – 333
Joseph Schumpeter - 13
*Josomi* – 330
Joswa Naluma – 331
Jules Ranaivo - 140
Julian Cobbina - 33
Jurji Zaidan - 275

Kabaka – 331, 332
Kabaka Daudi Chwa – 331
Kabarega - 7, 20, 89, 91
Kadhi - 175
Kagama - 120, 121
Kagubi - 126
Kakunguru - 91

Kamala - 58
Kamil - 44
Kamilo - 44
Kamuu Banda – 376
Kamwana - 109
Kaossen - 163
Karl Peters - 101
Kasisi Apolo, - 260
*Katawere,* - 255
Katekesta William Egyanka Appiah – 266
Kayamba – 335
Kenadid - 302
Keme-Brema - 72
Kenneth Kaunda – 343
Kgama - 125
Kgamane - 120
Khalid - 304, 305
Khalifa - 47
Khalifa Abdallah - 20
Khalifa Abdullah - 48
Khama - 120
Khayruddin – 307
Khedive - 40, 42, 43
Khedive Ismail - 38
Khedive Ismail Pasha - 275
Khedive Tawfik - 38, 47
Khomo - 125
Kiamba - 94
*Kiandriana* - 133
Kibanga - 89
Kilson - 252
*Kimainty* - 133
Kimbangu - 263
King – 365
Kinjekitile - 32
Kinjekitile Ngwale - 94
Kinueri - 50
Kitchezer - 48
Kive Bulaya - 260
Kleise Sykes – 338
Kojo Thompson – 319
Kojo Tovalou Houenon – 324
Konde - 74
Kondolo - 109
Kotavy - 137
Kotokoli - 20
Koutate Sorang – 287
Krobo - 256
*Kuduo* – 268
Kwame Nkruma - 250
Kwame Nkrumah – 368, 376
Kwanza - 65

La Myre de Vilers - 132
Ladipo Solanke – 287
Lamine Senghor – 284, 287
Laroui - 25
Lat Dior - 5, 19
Lat Dior Damel -3
Lat Dior Diop - 67
*Latif* - 312
Le Myre de Vilere - 131
Lenana - 88
Lenin - 12
Leon Dams - 279
Leopard - 16, 185
Leopold Senghor - 279
Lever - 208
Levi Coppin – 373
Lewamika - 120, 121
Lewis Gaun - 6
*Liga Africano* – 354
*Liga Angolana* – 350
Lighthart – 366
Lij Lyasu – 366
Limo – 343
*Linga Angolana* – 349
Lippmann - 301
Livingstone - 4
Lobengula - 20, 115, 116, 117, 118, 120
Lord Brockway – 284
Lord Chelmsford - 116
Lord Cromer - 180
Lott Carey – 373
Louis - Hubert Lyautey - 175
Louis Archinard - 19
Louis Hunkanrin – 325
Lubiri – 331
Lucy Mair - 249
Ludovic Kaitasba – 334
Lugard - 20, 88, 89, 172, 173, 175, 176, 177, 178
Lukiko – 332
Lyautey – 314

Ma'Aynayn - 57
Mabona - 33
Machemba - 3
Mack Makeja – 338
Mackenzie - 121
*Madhiyya* - 45
Mage - 69
Maguiguana - 109
Maguire - 117
Magwende - 125
Mahdi - 45, 47, 48, 49, 52, 53, 146, 298
Mahmudi Sami al-Barudi - 40
*Mainduma* - 118, 125
Mainduna *Motshede* - 118
Maitre Guellati – 307
Maji Maji - 32, 33, 96
Majoe Gerad
Makana - 33
Makhaki - 289
Makhezen - 56
*Makhzen* – 305
Makoko - 17
Makoni - 125
*malango* - 257
Malekebu – 376
Malkia Victoria - 118
Mamadou Lamine - 19, 73, 81
Mangena M. Mkone - 261
Mangwenda - 126
Mangwende - 114
Mapondere - 106
*marabout* - 57
Marcus – 372
Marcus Garvey – 285, 287, 337, 368, 370, 376,
Marealle - 89
Margery Perham - 6
Maria Teresa - 146, 367
Marry Thuku - 250
Marshall – 375
Marx - 12, 325
Maserkasi - 42
Mashayamombe - 125, 126
Massimy - 57
Matari – 313
Max - 280
Max Bloncoux – 284
Mazrui - 88, 93, 94
Mbaruk bin Rashid - 88
*Mbira – 271*
Mbiyu Koinange – 338
Mbuya - 32
mek - 49
Melik – 359
Melilla - 54
*Menalamba* - 133
Menelik - 3, 5, 148, 149, 153, 155, 356, 359, 366
Menelik Il - 154
Meneliki – 363
Mesali Hadj – 314, 284, 287
Mgana - 121
Mhiripiri - 126
Mhugulu - 125
Michael – 313
Midjurtayn - 301
Mikael – 359
Millard – 368
Mkwawa - 89
Mohamed Hafiz Bey Ramadan – 284
Mohamed Said – 368
Mohammad Ali - 183
Mohammed V, – 314
Mongameli Mabena - 32
Monteil - 73
Mosheshe - 120
Moshoeshoe - 121
Mosi Wuod Auma – 329
Moutaga - 70
Mpandi - 263
Msiba Mwea - 88
Msvikiro - 126
Mtakatifu Louis - 82
Mtetwa - 122
Muchemwa - 126
Muhamad Farid - 44
Muhamad Ahmad Ibn 'Abdallah - 45
Muhamad al-Madhi - 45
Muhammad - 301
Muhammad ' Ali - 233, 275, 307, 308
Muhammad b. Ali al-Sanusi - 259
Muhammad Ben Abd al-Khattabi

- 308
Muhammad Salih - 52
Mukasa - 263
Mulay Idris - 57
Mulaya Abd-Aziz - 57
Mumbo - 94
Mumia - 86, 88
Murcus Garvey - 284
Mushidi - 109
Mussolini - 367, 368
Mustafa - 58
Mustafa Kamil - 43
*Muthirigu* - 257
Mwanga - 7, 18, 20, 86, 91
Mwase Kasungu - 99, 108
*Mwasi* - 126
Mwene Mutapa - 109, 122
Mzee Bin Sudi - 338
Mzilikazi - 117
Mzimu wa Mumbo - 329
maasi ya Ikaya - 109
maasi ya Massingire - 109
maasi ya Shangaani - 109

Nabii Muhamad - 45
Nana - 35, 79
Nana *Akaboha* - 266
Nana Ofori Atta - 324
Nana Olomu - 36
Nana Prempeh - 19
Nana Sir Ofori Atta - 321
Nancy Hafkin - 36
*Napoleon* - 183
Narton de Matos - 349, 350
Nasiri - 314
Natholomoa Jehu-Appiah - 266
Ncehemiah Tele - 261
Ndabaningi Sithole - 375
Ndonye - 328
Ndwande - 122
Negus - 359
Nehanda - 126
Nehemiah Tile - 341
Nelson - 88
ngai - 328
Ngwane - 120
Njonjo - 85
Nkosi Sikelel' Afrika - 342
Nkrumah - 375
Nnamdi Azikiwe - 368, 376
Ntsikana - 33
Nyamand - 125
Nyandoro - 125
Nyindo - 164

*Ofori Atta* - 250
Ogot - 34
Oliveira Guimares - 351
Olorumtimehin - 83
Omdurman - 296
Onyango Dunde - 329
Opoku - 329
Ottoman - 307
Ovambo - 110
Ovimbudu - 34
Owen - 332

Panasha - 126
Paul Holle - 277
Paul Reynaud - 141
H. Peter Duignan - 6
Peter Koinange - 375
Peter Rigby - 32
Phelps - Stokes - 376
Pili- 132
Pixley Ka Izaka Seme - 375
Planque - 141
Prempeh - 5, 76, 77
Prempeh I - 1, 7
Paatje - 342

Rabih - 19
Radama I - 129
Rainiariwony - 19
Rainitavy - 134
Ralaimongo - 141
Ramadhani Ali - 338
Ramdan Shatiwi - 311
Ranavalona III - 19
Ranavolana - 129
Ranavolana wa Ranger - 33

Ranger - 34
Ras Alula - 146
Ras Makonnen – 359
Ras Mangasha - 148, 149
Ras Tasamma – 359
*ratib* - 49
Ravoahangy - 141
*rezzous* - 305
Rhodes - 117, 118, 121, 125
Richard Hathbone - 160
Robinson - 17
Ronald Robinson - 14
Ronald Ross - 240
Ruben Sparts Mukara, - 263
Rudd - 117
Rumaliza - 35
Sa'd Zaghlul - 167, 286, 292
Sadivahe - 139
Sakawa – 329
Salazar – 350
Salsa - 58
Samatar – 300
Samir Amin - 35
Samori - 73, 74
Samori Ture - 19
Samori Toure - 7, 31
Samuel Adjayi Crowther - 260
Samweli Maherero - 127
Sanusi - 163
Saraukenyi Mori - 74
Savorgnan - 17
Sayyid - 52
Sayyid Muhammad - 51, 53, 291
Sebele - 121
Seke - 125
Sekgoma - 120
*Sepais* - 104
Servatius - 67
*Sharia* - 175
Shaykh Abdel-Aziz al-Thaalibi – 307
Shaykh Bashir al-Ibrahimi – 306
Shehe Ahmadu Bamba - 83
Shehe Hamollah - 83
Shehu Ahmadu - 31
Sherman – 355
Shippard - 117
Sidi Abdallah - 58
*sidi Ukba* – 306
Sidik - 295
Sidney - 116
Sikombo - 125
Silverio Ferriera, - 279
Sihayni, - 298
Simeon Nyende – 332
Simon Kimbangu - 263, 346, 349
Simon-Pierre - 263
Siotume - 94
Smuts - 168
Societa Rubattino - 146
Somari Ture - 72
Sowabulana - 125
Stanley - 4
Steinhart - 35
Suedi Kangasheki – 334
Sulayman al-Baruni – 311
Sylvester Williams – 284, 288
Saadia Touval - 25
Tafari – 359
Tafari Makonnen – 358, 363, 367
Tahar al-Haddad – 307
Tahar Safar – 313
Talila Akafuna - 120
*tartib* - 224
Tawfik - 40, 42
Tayta - 153
*Tebessa* – 306
Theodor Leutwein - 127
Theophilus Shepatone - 115, 127
Thomas Hodgkin - 251
Thompson - 117
Thuku – 337
Tieba - 73
Tiemoho Garan-Konyat'e – 324
Tipp Tip - 103
Tiyo Soga - 113
Toera - 135
Tofa - 7
Tomo Nyirenda – 347
Too Wesley – 358
Torres – 314
Touba-Kouta - 19

Touissant L'Cuverture. - 278
Tovalou Quenum – 287
*Tranzozoro* - 141
*Tubakero* – 268
Tubman – 355
Tukulor - 69
Turner – 373, 374
Tuwat - 56
Twarik - 62
Taalbi – 307
Umar al-Mukhtar – 60, 61, 311
Undi - 97
Union Jack - 118
Urabi - 42, 53
Uthman Rifki - 40
'Umar Samatar - 300
'Uthman Mahmud - 301
'Uthman Yusuf Vansina - 25

*Vato Sakelika*
Victoria - 146
Vita baina ya Waingereza na Makaburu - 184
vita dhidi ya Ahmadu - 70
Vita kati ya Wataliana na Yohannes - 146
Vita Kuu – 45, 281, 312
Vita Kuu vya Kwanza - 9, 83, 216, 256, 328
Vita Kuu vya Pili - 9
Vita Kuu ya Kwanza - 201, 259, 288
Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia - 238
Vita Kuu ya Pili – 288
Vita Kuu ya Pili ya Dunia - 241
Vita Vikuu - 290, 292, 296, 299, 303, 304, 320, 323, 324, 329, 338, 341, 343, 344, 345, 355
Vita Vikuu Viwili – 283, 288, 291, 317
Vita Vikuu vya Dunia - 92, 223, 240, 316, 317,
Vita Vikuu vya Kwanza - 7 80, 81 189, 192, 195, 217, 263, 281, 282, 284, 288, 290, 292, 300, 312, 316, 327, 329, 340, 342, 348, 359, 366, 370
Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia -60, 64, 237, 276
Vita Vikuu vya Pili - 177, 195, 283, 290, 302, 328, 335, 375
Vita Vikuu ya Kwanza – 347, 362
vita vya "gonga - kimbia" - 88
vita vya 1904 - 102
vita vya Adowa - 154, 155, 163
vita vya al-Karadabiyya - 163
vita vya askari wa msituni - 94
vita vya Bailundi - 36
vita vya *Chimurenga* - 125
vita vya *Jihadi* - 42
vita vya jihadi vya Fulani - 25
vita vya jihadi: - 45
vita vya Karari - 48
vita vya Kusseri - 19
Vita vya Kwanza - 219
Vita vya Kwanza - 36
Vita vya Kwanza vya Dunia - 50, 93, 94, 96 139, 140, 158, 161, 168, 169, 184, 187, 221, 222, 236,
Vita vya Maji Maji - 94, 256,
Vita vya Makaburu - 168
Vita vya Mau Mau - 333
vita vya msituni - 52, 74, 82,125
vita vya mwishomwisho - 25
Vita vya Pili - 179

Vita vya Pili vya Dunia - 169, 182, 227, 246, 250, 252, 253
Vita vya Rif – 311
vita vya Shaykan - 47
vita vya Tushki - 48
Vita vya Uhuru wa Somalia - 51
Vita vya Ukoloni – 308
Vita vya Wadachi - 20
vita vya wenyewe kwa wenyewe - 60, 120
vita ya Atbara - 48
vita ya kujikomboa - 45
Vita ya Pili ya Makaburu - 216
Vittori - 141
Von Lettow Vorbeck - 160, 163
Von Trotha - 127

W.E.B. du Bois – 9, 337, 354
Wad Habuba - 49
Wadyula - 277
Waiyaki - 85, 87
Wakabre -20
Wakila Amhouch - 58
Wakonkomba - 20
Wallace Johnson – 318
Wallestein - 251
Walter Rodney - 30, 34
Walter Rubusana - 114
*Wamenalamba*
Wami - 164
Wanga - 89
Wasamari Ture - 3
*Wataboni* – 372
Wellington Butelezi – 341
Whata - 125
William Du Bois – 284, 288
William H. Ellis - 150
William McGregor - 240
William Pontry - 180, 275, 283
William Wade Harris - 260
Willoughby - 121
Wilson - 292, 307
Winifried Tete-Ansa – 323
Winston Chrchill - 92
Woermann - 152
Woodrow Wilson - 167, 169
Waalib Dinka - 299

Xavier Copplani - 62
Xavier Coppolam -

Yagub Sarruf - 275
Yalley - 274
Yambio - 50
Yayu - 301
Yohannes - 146,
Yowasi Paito – 331
Yule Marks - 29
Yusuf - 300
Yusuf Abu Rahil - 61
Yusufu Mukasa – 331
Yves Peron - 73
Yaa Asantewa - 81

Z.K. Sentongo – 331, 336
Zaghlul - 294, 295
*Zahir* - 311
Zannas – 295
Zauditu – 358
Zawidtu – 359

## Historia Kuu ya Afrika

*Historia* hii inatoa mwanga juu ya umoja wa kihistoria wa Afrika pamoja na uhusiano wake na mabara mengine, hasa Amerika na Karibian. Kwa muda mrefu aina zote za taarifa za kubuni na hisia pendelevu zimeficha historia ya kweli ya Afrika kwa ulimwengu kwa jumla.

Kwa kujumuisha maarifa yetu juu ya Afrika, tukiweka bayana maoni mbalimbali kuhusu tamaduni za Afrika na kwa kupitia upya historia, *Historia* hii ina manufaa ya kutoa mwanga na uvulivuli na kueleza bayana tofauti za mawazo ambazo zinaweza kuwepo baina ya wasomi.

## Mapitio ya Majuzuu yote

"Mazao ya mwanzo ya UNESCO ni lazima yasifiwe kuwa ni mchango mkubwa wa kitaaluma."
**Roland Oliver**, *Times Literary Supplement*

"Ni mojawapo wa miradi mikubwa ya kitaaluma iliofanyika katika karne hii."
*West Africa*

"Majuzuu haya yametolewa kwa unadhifu mkubwa lakini yana bei nafuu sana ... Yanawakilisha matumizi mazuri kabisa ya pesa ambayo mnunuzi yeyote wa vitabu anaweza kuyapata ..."
**Basil Davidson**, *Third World Quarterly*

# VII Afrika chini ya Utawala wa Wakoloni 1880 - 1935

Juzuu la VII linachunguza kipindi cha mgawanyo, utamalaki na ukaliaji kuanzia mwanzoni mwa 'ugombeanaji wa Wazungu kwa Afrika' hadi uvamizi wa kifashisti wa Waitaliano huko Uhabeshi mwaka 1935. Kwenye juzuu lote, lengo limeelekezwa kwenye majibu ya Waafrika kuhusu changamoto la ukoloni.

Sura mbili za mwanzo zinaangalia mitazamo ya Waafrika na kujitayarisha kwao muda mfupi kabla ya enzi ya ukoloni, na usuli wa tamaa za Wazungu za kitawala. Sura saba zinazofuatia zinajadili jitihada za Waafrika na majibizo yao wakati wa ugawanyaji na ushinde hadi vita ya Kwanza ya Dunia.

Uangaliaji wa jumla unafuatiwa na uchambuzi wa kina zaidi na kimaeneo. Sura za 13 hadi 21 zinahusu athari za kiuchumi na kijamii za mfumo wa ukoloni Afrika kuanzia mwaka 1919 hadi 1935, utekelezaji wa uchumi wa kikoloni kwenye maeneo ya zamani ya Wafaransa, Wabelgiji, Wareno na Waingereza na Afrika ya Kaskazini; kutokea kwa miundo mipya ya kijamii na ruwaza za idadi ya watu na dhima ya dini na sanaa Afrika wakati wa ukoloni.

Sehemu ya mwisho inafuatilia ukuaji wa matapo dhidi ya ukoloni, uimarishaji wa uzalendo wa kisiasa Afrika na maingiliano baina ya Afrika ya watu weusi wa Dunia Mpya. Liberia na Uhabeshi zinajadiliwa katika sura maalumu.

**TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO**

**S.L.P 35110, Dar es Salaam**

ISBN 9976 911 24 6